



Kuripoti kuhusu
Wahamiaji
na **Wakimbizi**

MWONGOZO WA WALIMU WA UANAHABARI

MFULULIZO WA UNESCO WA ELIMU YA UANAHABARI

Kuripoti kuhusu
Wahamiaji
na **Wakimbizi**

MWONGOZO WA WALIMU WA UANAHABARI

MFULULIZO WA UNESCO KUHUSU ELIMU YA UANDISHI WA HABARI

Chapa ya kwanza 2022

© UNESCO, Erich Brost Institute for International Journalism, 2022

ISBN: 978-92-3-000184-1



Mwongozo huu unapatikana katika mfumo wa huru wa ufikiaji kwa leseni ya Attribution ShareAlike 3.0 IGO (CC-BY-SA 3.0 IGO) (<http://creativecommons.org/licenses/by-sa/3.0/igo/>).

Kwa kuyatumia yaliyomo katika mwongozo huu, watumiaji wanakubali kuzingatia kanuni za utumiaji za hifadhi huru (<http://www.unesco.org/open-access/terms-use-ccbysa-en>).

Jina Halisi ya Ripoti: Reporting on Migrants and Refugees. Handbook for Journalism Educators Imechapishwa mwaka wa 2021 na United Nations Educational, Scientific and Cultural Organization, 7, place de Fontenoy, 75352 Paris 07 SP, France.

Maelezo na mambo yote yaliyowasilishwa katika mwongozo huu hayalengi kwa njia yoyote kuwakilisha maoni yoyote ya UNESCO kuhusu hali ya kisheria ya nchi yoyote, himaya, jiji au eneo wala uongozi wake au kuhusu mipaka yake.

Mawazo na maoni yaliyotolewa katika mwongozo huu ni ya waandishi; haina maana kwamba ni ya UNESCO na hayalipatii shirika wajibu wala kuliwekea masharti yoyote.

Wahariri: Susanne Fengler, Monika Lengauer, Anna-Carina Zappe

Waandishi wanaostahili kutajwa: Fengler, S., Lengauer, M., & Zappe, A.-C. (eds.). (2021). *Kuripoti kuhusu wahamiaji na wakimbizi. Mwongozo wa walimu wa uanahabari*. Nais: UNESCO.
muundo wa picha

Waliochangia picha za kurasa za kwanza za kila moduli: J. Bävman (UNHCR) (uk. 11); A. Sen (UNHCR) (uk. 29); H. Caux (UNHCR) (uk. 53); M. O'Shea (uk. 97); S. Korovainyi (uk. 113); C. ten Brink (uk. 135); C. K. Arnaud (uk. 155); S. Dinges (uk. 175); C. Tijerina (UNHCR) (uk. 197); A. Tzortzinis (uk. 223); M. Hofer (UNHCR) (uk. 243); J. McIntosh (flickr) (uk. 263); W. Vassilo poulos (uk. 277)

Asili za picha za waandishi waliochangia: Binafsi (uk. 299-302)

Picha ya jalada: Fishman64/www.shutterstock.com

Maelezo kuhusu picha yanapatikana katika uk. 296-297.

Upambaji wa kurasa: thinkandact-mainz.de

Upambaji wa jalada: thinkandact-mainz.de

Mpangaji wa chapa: thinkandact-mainz.de

Mchapishaji: Erich Brost Institute for International Journalism

Kimechapishiwa Ujerumani

Chapa halisi kwa Kingereza, kimetafsiriwa na Wainainah Kiganya

Tafsiri imefadhiliwa na Code for Africa

Msahihishaji : Kiprotich Koros

Upambaji wa kurasa kwa chapisho la Kiswahili : Jeremy Mwangi

Kuripoti uhamiaji: Changamoto kwa walimu wa uanahabari duniani kote

Mwongozo huu unawawezesha walimu wa uanahabari kote duniani kushughulikia changamoto mojawapo za karne ya 21 — masuala ya uhamiaji na wakimbizi. Mkusanyiko huu wa moduli 13 unawapa walimu wa uanahabari mtaala mpana wenye maarifa na mambo mengi yanayohitajika kufundishia, kuchanganua, kutafiti, kuwasilisha, kuuza na kuangazia itikeli katika kuripoti kuhusu uhamiaji.

Mwongozo huu ni wa kipekee kwani unashirikisha matokeo ya utafiti wa fani ya mawasiliano pamoja na sayansi za siasa na jamii. Umestawishwa na kundi la kimataifa na lililoleta pamoja tamaduni mbali mbali la watafiti wa masuala ya vyombo vya habari, waelimishaji wa uanahabari na wanahabari wazoefu.

Wakiutumia mwongozo huu, waelimishaji wa uanahabari wataasisi mtaala mpya. Wanafunzi wa uanahabari watajifunza kwamba masuala ya uhamiaji na uhamaji wa kulazimishwa yanahusu binadamu na ndiposa yanahitaji ufahamu wa kanuni na taarifa sahihi za kweli, vyanzo vya kuaminika na kutegemewa, kuripoti wakizingatia itikeli na utendaji kazi bora. Wanahabari wenye tajiriba watafaidika kwa kutumia mwongozo huu kama kifaa cha kujifundisha wenyewe, nayo mashirika ya maendeleo ya vyombo vya habari yanaweza kuushirikisha mtaala huu katika mipango yao ya mafundisho.

Mazao ya huu yatakuwa ripoti pana za habari kuhusu masuala ya uhamiaji na wakimbizi kuanzia nchi wanakotoka, wanakopitia na wanakoenda, na mjadala unaoangalia pande zote ukizingatia ufahamu kamili katika nchi na tamaduni mbali mbali.



“Kwa kuwa vita huanzia ndani ya akili za wanaume na wanawake, ni ndani ya akili za wanaume na wanawake ambamo lazima kinga za amani zijengwe”

YALIYOMO

x	Orodha ya akronimu na vifupisho
xi	Dibaji

1 UTANGULIZI

4	Malengo na Muundo
8	Mawazo ya Uvumbuzi, Ubunifu na Ubukuzi Yasiyo na Mipaka!
9	Hitimisho
10	Marejeleo

12 MODULI 1 : MASUALA YA UHAMIAJI NA WAKIMBIZI – CHANGAMOTO ZA KARNE YA 21

na Susanne Fengler na Monika Lengauer

13	Malengo ya Moduli
13	Matokeo ya Mafunzo
13	Muhtasari
17	Mkataba wa Ulimwengu kuhusu Wakimbizi na Mkataba wa Ulimwengu kwa Uhamiaji Salama, kwa Mpango na Kanuni
21	Mataifa Tofauti, Mitazamo Tofauti
25	Muundo wa Mwongozo
27	Kazi ya Ziada
27	Usomaji wa Ziada
28	Marejeleo

31 MODULI 2 : VYANZO MUHIMU, MAMBO MUHIMU, ISTILAHU MUHIMU NA TAKWIMU

na Monika Lengauer

32	Malengo ya Moduli
32	Matokeo ya Mafunzo
32	Muhtasari
33	Vyanzo vya Data Vilivyochaguliwa
38	Istilahi Muhimu - Kutofautisha Wahamiaji na Wakimbizi
46	Wahusika Wakuu Teule
49	Kazi ya Ziada
51	Usomaji wa Ziada
51	Marejeleo

58 MODULI 3 : VIPENGELE VYA MUKTADHA WA UHAMIAJI NA UHAMISHWAJI WA KULAZIMISHWA

na Monika Lengauer na Susanne Fengler

59	Malengo ya Moduli
59	Matokeo ya Mafunzo
59	Muhtasari
60	Utaalamu
62	Uhamiaji na Maendeleo
63	Uhamiaji — “Habari Njema”, “Habari Mbaya”?
66	Kuangazia Yanayowasukuma na Kuwavutia Wahamiaji na Wakimbizi
68	Ongezeko la Idadi ya Watu
71	Migogoro
74	Masuala ya Kiuchumi
75	Pesa Zinazotumwa Nyumbani na Wahamiaji
79	Taasisi
80	Elimu
84	Mabadiliko ya Hali ya Hewa
86	Mitandao ya Kikabila (Diaspora)
87	Kazi ya Ziada
88	Uso maji wa Ziada
89	Jinsia
93	Uso maji wa Ziada : Jinsia
93	Marejeleo : Jinsia
95	Marejeleo

105 MODULI 4 : VYOMBO VYA HABARI NA HADITHI ZA UHAMIAJI – UCHANGANUZI WA NCHI TOFAUTI

na Susanne Fengler

106	Malengo ya Moduli
106	Matokeo ya Mafunzo
106	Muhtasari
108	Utafiti Kuhusu Kuripoti Uhamiaji: Mapitio ya Maandishi
111	Uchunguzi wa Jinsi Habari za Uhamiaji Huripotiwa Katika Nchi Tofauti za Afrika na Ulaya
114	Uhamiaji na Mtiririko wa Habari za Kimataifa
115	Utafiti wa Jinsi Habari za Uhamiaji Zinaripotiwa Katika Nchi Tofauti: Ulaya, USA, Russia
118	Kazi ya Ziada
119	Uso maji wa Ziada
119	Marejeleo

**123 MODULI 5 : KURIPOTI KUHUSU UHAMIAJI – TAATHIRA ZA VYOMBO VYA HABARI
NA CHANGAMOTO ZA KITAALAMU**

na Anna-Carina Zappe

- 124 Malengo ya Moduli
- 124 Matokeo ya Mafunzo
- 124 Muhtasari
- 125 Maoni ya Umma Kuhusu Uhamiaji
- 128 Kampeni za Uchaguzi na Uhamiaji
- 129 Kuripoti Uhamiaji na Watumiaji wa Vyombo vya Habari: Taathira Zinazoweza
Kujitokeza
- 133 Taathira ya CNN na Kisa cha “Aylan Kurdi”
- 135 Changamoto za Kitaalamu
- 136 Uhaba wa Vitendea Kazi
- 138 Upendeleo na Mawazo Potovu Yasiyo na Uasili
- 138 Uhuru wa Uanahabari na Vyanzo Vilivyo na Ushawishi wa Hoja kwa Umma
- 140 Kazi ya Ziada
- 141 Usomaji wa Ziada
- 141 Marejeleo

147 MODULI 6 : UCHANGANUZI KIFANI WA GUINEA-BISSAU (AFRIKA MAGHARIBI)

na Monika Lengauer

- 148 Malengo ya Moduli
- 148 Matokeo ya Mafunzo
- 148 Muhtasari
- 149 Wasifu wa Nchi
- 150 Sifa ya Uhamiaji
- 157 Sababu Teule za Kimuktadha 1: Umaskini
- 160 Sababu Teule za Kimuktadha 2: Ongezeko la Watu na Vijana
- 162 Sababu Teule za Kimuktadha 3: Kuvutwa Hadi Bissau
- 163 Kazi ya Ziada
- 164 Usomaji wa Ziada
- 164 Marejeleo

169 MODULI 7 : UCHANGANUZI WA KIFANI WA CAMEROON (AFRIKA YA KATI)*na Monika Lengauer na Johanna Mack*

170	Malengo ya Moduli
170	Matokeo ya Mafunzo
170	Muhtasari
171	Maelezo Mafupi Kuhusu Cameroon
173	Maelezo Mafupi Kuhusu Uhamiaji
176	Masuala Teule ya Kimuktadha
181	Jinsia
184	Kazi ya Ziada
185	Usomaji wa Ziada
185	Marejeleo

192 MODULI 8 : UCHANGANUZI WA KIFANI WA UJERUMANI (ULAYA MAGHARIBI)*na Monika Lengauer na Johanna Mack*

193	Malengo ya Moduli
193	Matokeo ya Mafunzo
193	Muhtasari
194	Wasifu wa Nchi
197	Jamii Inayozeeka
198	Sura ya Uhamiaji
205	Watoto Wasioandamana na Watu Mzima Katika EU: Wasioonekana
206	Kigezo cha Mvuto: Sumaku ya Ustawi
208	Kigezo cha Mvuto: Kimbilio la Salama
209	Kazi ya Ziada
209	Usomaji wa Ziada
210	Marejeleo

217 MODULI 9 : UHAMIAJI NA UHAMAJI KATIKA AFRIKA: KUTOKA BARANI, NDANI YA BARA, NDANI YA NCHI*na Monika Lengauer*

218	Malengo ya Moduli
218	Matokeo ya Mafunzo
218	Muhtasari
219	Uhamiaji wa Kimataifa wa Waafrika Kutoka Barani
225	Uhamiaji wa Kimataifa wa Waafrika Ndani ya Bara
232	Uhamishwaji Wa Lazima Kutokana Na Migogoro: Wakimbizi Na Wahamiaji Wa Ndani (IDPs)
233	Wakimbizi wa Ndani (IDPs)
239	Usomaji wa Ziada
239	Marejeleo

**245 MODULI 10 : KURIPOTI KUHUSU UHAMIAJI KITAALAMU: UTENDAJI KAZI BORA
NA MKABALA WA KIITIKELI**

na Anna-Carina Zappe

- 246 Malengo ya Moduli
- 246 Matokeo ya Mafunzo
- 246 Muhtasari
- 247 Uhamiaji kama Habari
- 250 Kuripoti Kitaalamu: Vigezo vya Utendaji Kazi Bora
- 251 Chaguo la Vyanzo na Wahojiwa Wanaofaa
- 253 Habari za Kuaminika na Utafiti wa Kutegemewa
- 257 Maneno Sahihi na Mitazamo
- 260 Kuripoti Kuhusu Wahamiaji na Wakimbizi: Mifano ya Utendaji
- 261 Kazi ya Ziada
- 261 Usomaji wa Ziada
- 262 Marejeleo

**266 MODULI 11 : KURIPOTI KUHUSU WAHAMIAJI NA WAKIMBIZI: KUKABILIANA NA
MAJERAHA YA MAWAZO**

na Anna-Carina Zappe

- 267 Malengo ya Moduli
- 267 Matokeo ya Mafunzo
- 267 Muhtasari
- 268 Majeraha ya Mawazo
- 269 Majeraha ya Mawazo, Wahamiaji na Wakimbizi
- 273 Kuwahoji Wahamiaji na Wakimbizi na Kuchunga Usiwajeruhi Mawazo
- 275 Mahojiano Bora na Wahamiaji Yanayojali Majeraha ya Mawazo (TIIM)
- 279 Afya ya Akili ya Wanahabari Wanaoripoti Kuhusu Wahamiaji na Wakimbizi
- 281 Kazi ya Ziada
- 281 Usomaji wa Ziada
- 282 Marejeleo

286 MODULI 12 : MIPANGO YA USHIRIKIANO KATIKA KURIPOTI KUHUSU UHAMIAJI*na Tina Bettels-Schwabbauer na Nadia Leihls*

- 287 Malengo ya Moduli
- 287 Matokeo ya Mafunzo
- 287 Muhtasari
- 288 Ushirikiano wa Wanahabari Wataalamu
- 292 Kushirikiana na Umma
- 293 Ushirikiano na Wahamiaji na Wakimbizi katika Kuripoti
- 295 Ushirikiano Baina ya Nchi
- 296 Kazi ya Ziada
- 297 Usomaji wa Ziada
- 298 Marejeleo

301 MODULI 13 : KUBORESHA TAATHIRA: MIKAKATI YA UANAHABARI NA MASOKO YA HABARI*na Anna-Carina Zappe na Gordon Wüllner-Adomako*

- 302 Malengo ya Moduli
- 302 Matokeo ya Mafunzo
- 302 Muhtasari
- 304 Matumizi ya Vyombo Vya Habari Katika Afrika na Ulaya
- 305 Jinsi Wahamiaji na Wakimbizi Hutumia Vyombo vya Habari
- 306 Hadhira na maslahi ya vyombo vya habari
- 309 Habari za kuvutia
- 311 Hadithi za mfano za uhamaji na uhamishaji wa kulazimishwa: Muhtasari wa mazoea mazuri
- 314 “Kuuza” Habari Kuhusu Uhamiaji na Uhamishwaji wa Kulazimishwa
- 315 Kazi ya Ziada
- 316 Usomaji wa Ziada
- 316 Marejeleo

321 KIAMBATISHO

- 321 Picha
- 323 Anwani
- 326 Wahariri
- 327 Waandishi Waliochangia
- 332 Shukrani

ORODHA YA AKRONIMU NA VIFUPISHO

ORODHA YA AKRONIMU NA VIFUPISHO

4Mi	Mixed Migration Monitoring Mechanism Initiative	JIGC	Journalism in a Global Context
ADB	Asian Development Bank	LDC	Least Developed Countries
AfDB	African Development Bank	LGBTI	Lesbian, Gay, Bisexual, Transgender, Intersex
AFP	Agence France Presse	LIC	Low-Income Countries
AMI	African Media Initiative	LMIC	Low- and Middle-Income Countries
AP	Africa Positive	MENA	Middle East and North Africa
AU	African Union	MSF	Médecins Sans Frontières
BBC	British Broadcasting Corporation	NGO	Non-Governmental Organisation
C-Africa	African Regional Organisation of the International Trade Union Confederation	ODA	Official Development Assistance
CEDAW	Convention on the Elimination of all Forms of Discrimination Against Women	OECD	Organisation for Economic Cooperation and Development
CEE	Central and Eastern Europe	OHCHR	Office of the United Nations High Commissioner for Human Rights
CNN	Cable News Network	PTSD	Post-Traumatic Stress Disorder
CPI	Consumer Price Index	SBTF	Standby Task Force
CPJ	Committee to Protect Journalists	SDG	Sustainable Development Goals
CPLP	Community of Portuguese Language Countries	SIDS	Small Island Developing States
CSO	Civil Society Institutions	UNDESA	United Nations Department for Economic and Social Affairs
DTM	Displacement Tracking Matrix	UNDP	United Nations Development Programme
DW	Deutsche Welle	UNESCO	United Nations Educational, Scientific and Cultural Organization
EASO	European Asylum Support Office	UNGA	United Nations General Assembly
EJN	Ethical Journalism Network	UNHCR	United Nations High Commissioner for Refugees
EJO	European Journalism Observatory	UNICEF	United Nations Children's Fund
EMN	European Migration Network	UNPD	United Nations Population Division
EU	European Union	UNRWA	United Nations Relief and Works Agency for Palestine Refugees
EUROSTAT	European Statistical Office	UNSD	United Nations Statistics Division
FDI	Foreign Direct Investments	WDI	World Development Indicators
FOIA	Freedom of Information Act	WFP	World Food Programme
GO	Government Organisation		
HDI	Human Development Index		
HDR	Human Development Report		
ICIJ	International Consortium of Investigative Journalists		
IDMC	Internal Displacement Monitoring Center		
IDP	Internally Displaced Person		
ILO	International Labour Organisation		
INGO	International Non-Governmental Organisation		
IOM	International Organization for Migration		
IRC	International Rescue Committee		
ISIL	Islamic State of Iraq and the Levant		
ITU	International Telecommunication Union		

Ikumbukwe: Katika toleo la Kiingereza la mwongozo huu, nchi zimetajwa kwa majina yake ya Kiingereza na pia vifupisho vinavyofuatia. Kwa majina rasmi ya nchi, tazama <https://www.un.int/protocol/sites/www.un.int/files/Protocol%20and%20Liason%20Service/officialnamesofcountries.pdf>.

DIBAJI

Nilihusika kwa mara ya kwanza katika mradi huu mnamo 2016 nilipoalikwa kuchangia mtazamo wa Uganda kwa kile ambacho kingeishia kuwa uchanganuzi wa taarifa za habari kutoka mataifa 11 kuhusu uhamiaji na uhamisho wa kulazimishwa ndani na kati ya Afrika na Ulaya. Baada ya kubadilishana baruapepe nyingi na kufanya mikutano ya ana kwa ana, makala yenye anwani “Kuripoti kuhusu Uhamiaji — katika Afrika na Ulaya: Matokeo ya Uchanganuzi Linganishi wa Mataifa” yaliyochapishwa na Journalism Practice mnamo 2020. Mojawapo ya matokeo ya uchanganuzi huo ni kwamba vyombo vya habari katika Afrika na Ulaya havitilii maanani ipasavyo sababu za uhamiaji na uhamisho wa kulazimishwa. Matokeo hayo yalizaa wazo kubwa zaidi: Haja ya kuleta pamoja tunu ya maarifa na ujuzi wa timu hiyo na kuunda rasilimali ya pamoja ambayo itachangia katika kuimarisha na kuzidisha kina cha kueleza habari za uhamiaji na uhamisho wa kulazimishwa kote duniani. Tukiongozwa na Prof. Susanne Fengler, Monika Lengauer na Anna-Carina Zappe wa Erich Brost Institute for International Journalism, wazo hilo lilipata uhai kwa fadhila za wenzetu kutoka katika karibu kila bara. Ilichukua juhudi za waandishi na wataalamu zaidi ya 30 waliojitolea kwa dhati wa masuala ya vyombo vya habari, uhamiaji na uhamisho wa kulazimishwa kutoka kwa karibu nchi 20 kuandaa chapisho hili, “Kuripoti kuhusu Uhamiaji na Wakimbizi: Mwongozo wa Walimu wa Uanahabari”.

Bila shaka kuripoti kuhusu uhamiaji na uhamisho wa kulazimishwa ni suala tatanishi na hatari wakati mwingine. Kitabu chochote cha kiada ambacho kinakusudia kupasha masomo na ustadi kuhusu utoaji wa habari za uhamiaji na uhamishwaji wa lazima kinaweza kuwa na faida kiki-zingatia mfumo wa mkusanyiko wa masomo mengi tofauti na tamaduni mbali mbali. Ni nadra sana kupata katika sehemu moja habari pana, rasilimali, vidokezi na masimulizi kuhusu suala hili. Mwongozo huu umetolewa kwa wakati ufaao, na kina chake na mabadiliko ambayo utaleta ni za manufaa makubwa kwa hadhira za kimataifa. Ni mwongozo ambao una tunu ya rasilimali zinazopatikana kwa urahisi ambazo zinaafikiana na mahitaji ya watumiaji wanaokumbwa na uhaba wa nyenzo. Pana ushirikiano wa kimataifa wa kushangaza na chaguo kibao la uchanganuzi kifani muafaka. Uchanganuzi huo umefanyika katika kila sehemu ya dunia (isipokuwa eneo la Pacific). Kadhalika, mwongozo huu una marejeleo maridhawa — nyongeza ambayo ni muhimu kwa mwalimu yeyote wa uanahabari na awezayo kuutumia kwa kufundishia au kutafiti. Kadhalika umeangazia nadharia nyingi za uhamiaji na uhamisho wa kulazimishwa na hivyo basi kuweka msingi wa kuchambua ripoti za habari kuhusu wahamiaji na wakimbizi.

Moduli 1 inaweka ratiba na muundo wa mwongozo huu. Moduli zinazofuata zinashughulikia wahuusika wakuu, hali zinazochangia, istilahi, takwimu na miktadha ya hali zinazochangia uhamiaji na uhamisho wa kulazimishwa. Moduli 4 inashughulikia asili ya habari za uhamiaji na uhamisho kulazimishwa ikitilia maanani utafiti mwingi uliofanyika na wakati huo huo kuwapatia changamoto walimu wa uanahabari kuangazia tamaduni tofauti. Moduli 5 inajihusisha na taathira za vyombo vya habari kwa utambulisho wa wahamiaji na wakimbizi na pia muktadha wa kisiasa wa mitazamo hiyo, na kusisitiza changamoto za kitaalamu. Moduli 6 na 7 zinamulika nafasi ya umaskini, mapigano na jinsia pamoja na umuhimu wa changamoto za uhuru wa uanahabari

kwa kueleza habari kuhusu suala hili tatanishi. Moduli hizo zinasisitiza umuhimu wa muktadha katika uandishi na uchanganuzi wa habari za uhamiaji na uhamisho wa kulazimishwa. Moduli 8 inaangazia uhamiaji ikilenga Ujerumani ambapo Chansela Angela Merkel alitawala vichwa vya habari mnamo 2015 wakati aliwakaribisha nchini mamia ya maelfu ya wakimbizi kwa tamshi “Tunaweza kufanya hivyo.” Moduli 9 inatueleza kuhusu uhamiaji ndani ya bara ikilenga uhamiaji katika Afrika. Suala muhimu la maadili ya kitaalamu linashughulikiwa katika Moduli 10. Mwandishi hapa anawasilisha wajibu wa kuhakikisha ukweli, kuthibitisha na uteuzi wa maneno akitumia mifano ya kiutendaji. Mara nyingi suala la majeraha ya akili hupewa kisogo katika kueleza habari za wahamiaji na wakimbizi na limeshughulikiwa kwa mapana katika Moduli 11. Ni muhimu kwa kila mmoja kufahamu kwamba majeraha ya akili kinashughulikiwa hapa kuhusiana na wahamiaji na wakimbizi na pia athari zake kwa wanahabari wanaokusanya na kutoa habari za wahamiaji na wakimbizi. Moduli 12 inafichua kwamba suala la wahamiaji wengi kuvuka mipaka ya nchi na watu kulazimishwa kuhama makwao linahitaji ushirikiano kati ya wataalamu wa vyombo vya habari na pia wahamiaji na wakimbizi. Jambo la msingi ambalo mara nyingi husahaulika la kutetea kuripoti kuhusu wahamiaji na wakimbizi limejadiliwa katika Moduli 13.

Kazi hii bora na iliyopitiliza muda mrefu inaweza kubadili jinsi habari za uhamiaji na uhamisho wa kulazimishwa huelezwa kote katika dunia. Ni vigumu kukisia nyenzo nyingine pana na iliyofanyiwa utafiti wa kina kuhusu suala hili katika masoko yetu leo. Kila taasisi ya mafunzo ya uanahabari kote duniani inapaswa kuwa na mwongozo huu.

Professeur Monica B. Chibita

Mkuu wa Kitivo cha Uanahabari, Vyombo vya Habari na Mawasiliano

Uganda Christian University

DIBAJI

Ni mazoea ya watu kuhamahama kwa makundi makubwa kwa sababu tofauti, jambo linalofanya suala hilo kuwa ngumu kufahamika na ngumu zaidi kwa wanahabari kulieleza. Vyombo vya habari huripoti kuhusu uhamiaji panapokuwa na tukio la kipekee au wakati tukio hilo linashika mwelekeo wa kisiasa. Ili kuimarisha uelewa wa umma, wanahabari na walimu wao wanapaswa kutia bidii zaidi. Kusoma mwongozo huu kutakuwezesha kufahamu jinsi kuna mengi ya kujifunza. Ni kutambua haja ya utaalamu halisi unaohitajika iwapo maripota watautendea haki uanahabari wa wahamiaji na wakimbizi. Kwa mfano, pana umuhimu gani kwa wanahabari kuyachukulia kuwa visawe majina mhamiaji, mkimbizi na mkimbizi wa ndani kwa ndani (IDP)? Kwa nini linakuwa ni tatizo tukituma maelezo kama vile “mhamiaji haramu” au “mhamiaji asiye na hati halali”? Kuna walimu wa uanahabari ambao huenda wakatumia baadhi ya sura za mwongozo huu kwa kuzishirikisha katika masomo yao mapana. Huenda wengine nao wakatumia nyenzo hii kikamilifu kutoa kozi maalumu. Katika hali yoyote ile, Maisha ya wanahabari yataimarika kwa sababu kurasa hizi ni tunu ya hazina ya kuongeza ustadi iliyo na mazoezi ya kivumbuzi ya kujifunzia.

Mwongozo huu ni kitabu chenye mafundisho mazito kinachohitaji muda wa siku mbili mfululizo kukisoma kwa makini. Juhudi hii, bila shaka, ina manufaa mengi. Mkiwa walimu wa uanahabari, mtajifunza mengi kuhusu tukio muhimu la nyakati zetu na pia mtapata mazoezi ya mara kwa mara kwa wanafunzi. Isitoshe, wahariri wamefanya kazi murua ya kutafuta nukuu za baadhi ya wanahabari wazoefu na kuwasilisha pia maelezo kuthibitisha ukweli kutoka katika nchi tofauti yaliyoandaliwa na walimu wa uanahabari. Ili kurahisisha ufuatilizaji wa masomo, kuna anwani nyingi za tovuti zenye mifano maridhawa ya uchunguzi kifani na utafiti wa kina. Miongoni mwa mafunzo yanayojitokeza katika mwongozo huu ni umuhimu wa kuripoti kuhusu wahamiaji tukitilia maanani watokapo, wapitiapo na kikomo cha safari zao. Hakuna awezaye kuifahamu hadithi yote kwa kushughulikia tu hatua moja ya utaratibu huo. Mwongozo unaonyesha pia jinsi ya kuchanganua hadithi katika kiwango cha mtu binafsi na pia kundi, huku ukitilia maanani mambo muhimu kama jinsia, umri, sababu tofauti na majeraha ya akili yanayowapata wahusika wote. Mara nyingi suala hilo hushughulikiwa kama mzozo wa wakimbizi au mzozo wa uhamiaji, ilhali wanahabari wanaweza kufanya vyema kwa kuuliza “ni mzozo, wasiwasi na tatizo kwa nani?”, au hata “ni nani anayefaidika?” Maswali hayo yanatambua kwamba kuna wanaofaidika na “tatizo” hilo, ikiwa ni pamoja na wahamiaji, wanaowasaidia kusafiri kutoka nchi moja had nyingine na wenyeji wao hatimaye. Mwongozo unatukumbusha kwamba tatizo la maelezo muafaka ya mzozo/wasiwasi/tatizo ni la sera. Ndiposa inakuwa muhimu kwa wanahabari kuchanganua iwapo pana sera inayosimamia kikamilifu jinsi watu wanavyohama — kuanzia katika asili yao hadi hatima ya safari yao, na pia wanapopitia.

Uanahabari hutekeleza wajibu muhimu katika kusawazisha mahusiano kati ya wenye haki na walio na majukumu. Kama ilivyobainika wazi katika mwongozo huu, wakimbizi na wahamiaji wana haki, na kwa upande mwingine kila mmoja ana jukumu la kuheshimu haki hizo. Na hasa wanaotunga sera wenye jukumu la kusimamia uhamiaji kama huo wa wanadamu, wanahitaji habari za kiwango cha juu na pia kuangaziwa na vyombo vya habari ili kuhakikisha wanawajibika. Vyombo

vya habari navyo vina wajibu pia kwa wahamiaji ambao vinaripoti kuhusu ikiwa ni mojawapo ya majukumu yake kwa haki za binadamu kwa upana zaidi. Kuna masuala ya kisheria na kiitikeli yanayohusiana na uhamiaji wa wanadamu na wanahabari wanapaswa kufahamu jinsi ya kuendesha shughuli zao kuambatana na kanuni na mambo hayo ya kimsingi. Wakati huo huo, mwongozo huu unamulika uwezekano wa uanahabari wa kuleta manufaa – lakini sio kwa kupuuza jukumu la kuhakikisha wahusika wenye mamlaka na uwezo mkubwa wanawajibika ipasavyo, ila kwa sababu ya manufaa ya kuchukua hatua zaidi kufichua tatizo kwa kutafuta ufumbuzi wake. Yote haya, kama mwongozo utakavyodhihirisha, yanaakisia umuhimu wa ushirikiano katika nchi zote na pia katika kuripoti kuhusu wakimbizi wa ndani (IDPs). Kurasa za mwongozo huu zinatoa vidokezi kuhusu vile itikeli za habari za kidenturi na wazo la “habari za kuvutia” zinaweza kutumiwa kuhakikisha habari za suala hili zinaelezwa kupitia kwa vyombo vya habari.

Mojawapo ya majukumu ya UNESCO ni kuimarisha uanahabari kama shughuli maalumu ya uhuru wa kujieleza na kutoa maoni — lengo ambalo linahakikisha washiriki hawana budi kuahidi kueleza habari zilizothibitishwa kwa manufaa ya umma. Elimu kwa wanahabari inalenga kuinua kiwango cha uanahabari. Mwongozo huu ni chapisho la ziada kwenye mfululizo wa UNESCO unaoakisia elimu ya uanahabari kusudi kuchangia kuleta mabadiliko katika fani ya elimu ya uanahabari kote ulimwenguni — ikitiliwa maanani ukubwa wa eneo kijiografia wa maelezo ya sura na umbo la tukio la watu wanaohama. Wahariri wanastahili pongezi kwa kuhakikisha kwamba ingawa waliangazia zaidi Afrika na Ulaya na uhusiano uliopo katika mabara hayo mawili, ustadi wao unaweza kuwafaa wengine wengi na kuleta thamani katika mabara mengine. Mwongozo huu unavutia kwa kutambua athari za ugonjwa wa virusi vya korona-19 (Uviko-19) kwa masuala ya uhamiaji na wakimbizi. Kuimarisha elimu ya uanahabari ni mojawapo ya matokeo manne muhimu yanayotafutwa na International Programme for the Development of Communication (IPDC) wa UNESCO. Kila baada ya miaka kadha, mataifa mwanachama wa UNESCO huchagua wanachama 39 miongoni mwao kusimamia IPDC, mradi wa kipekee unaoshirikisha serikali mbali mbali kwenye mfumo wa Umoja wa Mataifa unaozingatia ustawi wa masuala ya vyombo vya habari pekee. IPDC iliadhimisha miaka 40 tangu kuanzishwa na tayari imesaidia uandalizi wa miongozo mingine kuhusu masuala mengine. Mengi ya machapisho hayo yamepokelewa kwa hamu kiasi kwamba baadhi ya wasomaji wamejitolea kuyatafsiri. Moyo huo wa kujitolea unakaribishwa kwa sababu unawezesha usambazwaji wa elimu na maarifa kwa lugha nyingi. Kwa kuanzia, mwongozo huu utachapishwa kwa Kiingereza, Kifaransa, Kiarabu, Kihispania na Kiswahili. Lakini iwapo msomaji yeyote yuko tayari kujitolea kusaidia kuwezesha mwongozo huu kupatikana kwa lugha nyingine, anaalikwa kuwasiliana nasi.

Haja ya kuwepo na wanahabari waliofunzwa vyema wakiandaa ripoti za kiwango cha juu kuhusu wahamiaji na wakimbizi katika muktadha wa kisasa inapata umuhimu zaidi kutokana na mtiiririko wa kipekee na usio na kifani wa usambazaji makusudi wa habari za uongo na madai ya njama yasiyo na msingi. Uanahabari wa kiwango cha juu kuhusu wahamiaji na wakimbizi ni muhimu katika mazingira ambapo mazoea ya kujitafutia sifa kuendeleza hisia za chuki bila sababu yamekuwa ni kawaida kwa jamii nyingi za wanadamu, hali ambayo imezaa kutoelewana, woga na chuki.

Mwongozo huu na uwe mchango wenye manufaa kwa ulimwengu ambapo usimamizi wa watu wanaohama unatekelezwa kwa kueleza habari za kujenga na kuleta manufaa zaidi iwezekanavyo kwa kutilia maanani haki za binadamu, wala sio kuongozwa na habari zisizo na kina na zilizotiwa chumvi zinazoweza kuchochea tu ndoto na kupandisha hasira na hamu kubwa.

Guy Berger

Katibu: International Programme for the Development of Communication (IPDC)

UTANGULIZI

Idadi kubwa ya watu na ambayo haijawahi kushuhudiwa hapo awali imekuwa ikihama katika nyakati zetu. Mnamo 2019, watu milioni 272 kote ulimwenguni walikuwa wahamiaji na wakimbizi, ongezeko la watu karibu milioni 120 tangu 1990 (Migration Data Portal, 2020). Idadi na kiwango cha uhamiaji huo zimezidi makadirio ya takwimu zilizotarajiwa kufikia mwaka 2050 za takribani milioni 230 (IOM, 2019b, uk. 2). Kwa sasa, idadi ya wahamiaji wa kitaifa ni asilimia 3.5 ya watu wote duniani ikilinganishwa na asilimia 2.8 mnamo 2000. Kwa sababu idadi ya wahamiaji kimataifa “inaongezeka kwa kasi kuliko jumla ya watu, fungu lao kati ya watu walio duniani limekuwa likiongezeka” (UNDESA, 2019, uk. 1). Uhamiaji na uhamaji mkubwa wa wahamiaji na wakimbizi una utata wa kisiasa, kiuchumi, kijamii, kimaendeleo, kiufadhili na kibinadamu, na haki za binadamu. Wanaoondoka huenda wakakumbana na hatari nyingi; huenda wakaingizwa katika biashara haramu ya ulanguzi wa wanadamu na safari za dhiki na shida; huwa hawana uhakika wa makaribisho yanayowasubiri katika mwisho wa safari zao; wana haki. Uwezo wa mataifa na jamii mwenyeji, mshikamano wao¹ kijamii na kiuchumi huathirika. Wakati huo huo, mataifa yao ya asili huenda yakaathirika kwa kupoteza wataalamu mbali mbali au kunufaika na maarifa na ujuzi wa wahamiaji wanaorudi nyumbani.

Uhamiaji na uhamisho wa kulazimishwa ni masuala ambayo yanapenya kutoka upande mmoja mpaka wa pili, yenye sura nyingi, yameenea kimataifa kwa kiwango kikubwa, yenye mpishano wa imani na mila, na kuingiliana kitaaluma. Yanahitaji elimu na maarifa katika masuala tatanishi na yanayohusiana ikiwa ni pamoja na haki za binadamu, maendeleo endelevu, vyombo vya habari, mawasiliano, maoni ya raia nchini na ng'ambo pamoja na uelewa wa kisiasa, kiuchumi, kimila, kisaikolojia, kinadharia na masuala ya kiutendaji, maajenti wa uandalizi wa sera za ndani, kanda na kimataifa na mashirika husika (mashirika ya serikali, mashirika yasiyo ya serikali na mashirika ya kimataifa yasiyo ya serikali). Hayo ni masuala machache tu, mbali na hali za kimuktadha zijulikanazo lakini bado hazijajadiliwa.² Uhamiaji na watu kulazimishwa kuhama makwao ni masuala yanayovuka mipaka yote ya nyanja za maisha ya binadamu.

Jambo hilo lilibainika zaidi wakati wa janga la Uviko-19 ambalo limeuletea ulimwengu changamoto ambayo haijawahi kushuhudiwa ya “tisho nambari moja la usalama duniani katika ulimwengu wetu wa leo” kama alivyosimulia Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa António Guterres kwa maneno makali alipowahutubia wanahabari Septemba 2020. Aliomboleza “vifo vya watu milioni moja kutokana na virusi hivyo. Na kwa sasa, mlipuko wa ugonjwa huo hauwezi kuzuilika wala kudhibitiwa” (UN, 2020c). Mawanda ya janga hili na vikwazo vilivyoandamana nalo kwa usafiri na uhamiaji ni vya kihistoria. Madhara yake yalikuwa makali zaidi kwa waliokuwa safarini,

1 Kiini cha mshikamano wa jamii ni ufungamano, mada muhimu ambayo itaandaliwa na kuwa jukwaa la mafunzo ya mtandao kwa udamini wa serikali ya Ujerumani.

2 Vipengele vya maudhui kuhusu uhamiaji na uhamisho wa kulazimishwa vinajulikana kama vipengele vya “msukumo” na “mvuto” – tazama Moduli 3 kwa maelezo na/au faharasa zilizopendekezwa katika Moduli 2: EMN (2018); IOM (2019a); UNHCR (n. d.).

kama vile wahamiaji katika hali zisizo za kawaida, wafanya kazi wahamiaji wanaotegemea njia hatari za kujipatia riziki na watu wanaokimbia mateso na adhabu, vita, mapigano, ukiukwaji wa haki za binadamu au majanga — iwe ni ndani ya nchi zao (wanaofurushwa makwao - IDPs) — au nje ya mipaka ya nchi zao wakimbizi na wanaotafuta hifadhi za amani.³ Athari zisizo kifani za janga la Uviko-19 zimejitokeza kwa matatizo matatu yaliyofungamana:

Tatizo la kiafya, tatizo la kijamii na kiuchumi, na tatizo la kujikinga. Mara nyingi watu huishi katika hali duni au zenye msongamano na huwa hazina huduma muhimu za kimsingi kama vile lishe, maji, na vyoo na vifaa vya kuondoa takataka na maji chafu; wanawake na wasichana hukabiliwa na hatari za dhuluma za kijinsia; wakimbizi huenda wakakwama na kushindwa kukimbilia usalama katika nchi nyingine. Uviko-19 huathiri pakubwa haki za watu wengi wakiwa safarini (UN, 2020a; UN, 2020b). “Tunapokabiliana na ugonjwa hatari”, akasema Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa Antonio Guterres, “ni lazima tufanye kila tuwezalo kuzuia kuenezwa makusudi kwa habari hatari za kupotosha” (UN, 2020c).

Wanahabari wanalo jukumu muhimu kuhusiana na suala hili — kuupasha umma habari kitaalamu (UNESCO, 2020). Hata hivyo, kazi yao inakwamishwa na janga hilo — sio tu kwa sababu taarifa muhimu za habari za tatizo la wakimbizi (tazama Moduli 4), lililojadiliwa pakubwa na vyombo vya habari, lilipitwa na tatizo kubwa zaidi lililofuatia, Uviko-19 — lakini pia kwa sababu ya kubadilika kwa hali za kazi za wanahabari. Maripota Wasio na Mipaka (Reporters Without Borders) walionyesha kwenye matokeo ya utafiti uliofanyika kote duniani kwamba athari za Uviko-19 kwa hali yao ya kazi na kwa uhuru wa vyombo vya habari zilizidisha “matatizo yanayotishia uhuru wa kueleza habari huru, za namna mbali mbali na za kutegemewa.” (Reporters Without Borders, 2020). Uanahabari wa kiwango cha juu ni muhimu katika hali ambapo serikali za kiimla “huzingatia imani zenye sifa mbaya – ... [na] na kuweka masharti magumu ya kuzingatiwa katika nyakati za kawaida” (Reporters Without Borders, 2020). Utafiti wa UNESCO wa habari za kupotosha kuhusu Uviko-19 (Posetti & Bontcheva, 2020a; Posetti & Bontcheva, 2020b) unatilia mkazo muktadha wa haki za binadamu (Posetti & Bontcheva, 2020a, uk. 4). Baadhi ya hatua ambazo vyombo vya habari vinapaswa kutilia maanani ni ushirikiano wa kimataifa kuhusu Uviko-19 na athari zake kwa uhamiaji na kuhakikisha kwamba yale ambayo nchi zilizostawi zilipitia hayo nyeshwi kisogo (Posetti & Bontcheva, 2020b, uk. 13).

Elimu ya uanahabari inapaswa kushughulikia masuala hayo muhimu ya kimataifa ya nyakati zetu ambayo yote ni taaluma nyingi zinazolingiliana na zinazohitaji utafiti. Suala la uhamiaji na watu kufurushwa makwao limeshughulikiwa katika juhudi za mwanzo zilizofungulia mlango mwongozo huu (Posetti, 2015; Turpin, 2018; UNHCR & NUJ, 2015). Elimu ya uanahabari imeangaziwa katika Mkataba wa Kimataifa kwa Uhamiaji (Global Compact for Migration) wataalamu wa habari kuhusu masuala ya uhamiaji na istilahi kwa lengo la kuimarisha “utoaji wa ripoti huru,

3 Kwa maelezo kuhusu wahamiaji wasio wa kawaida na makundi mengine yote, tazama faharasa zilizopendekezwa katika Moduli 2: EMN (2018); IOM (2019a); UNHCR (n. d.).

zisizopendelea na za kiwango cha juu” ambazo zinazingatia “kanuni za maadili za kuripoti [...] na kuheshimu kikamilifu uhuru wa vyombo vya habari” (UN General Assembly, 2018, uk. 26, para 33(c)). Ingawa hakuna nchi yoyote *moja* iwezayo kukabiliana peke yake na changamoto za kisiasa za uhamiaji na uhamisho wa kulazimishwa, *hakuna* chuo chochote cha elimu ya uanahabari, chumba cha habari, mwandishi habari *wala* mfumo wowote wa vyombo vya uanahabari kukabiliana na changamoto hizo kivyake. Uhamiaji na uhamisho wa kulazimishwa ni masuala ya kimataifa kadiri yalivyo pia masuala ya kibinafsi na elimu ya uanahabari inahitaji mikakati ya kukabiliana na changamoto hizo.

Ni hapo ambapo “Kuripoti kuhusu wahamiaji na wakimbizi: Mwongozo wa walimu wa uanahabari” unanuia kuongeza thamani wakati unapofikia walengwa na yaliyomo kufundishwa kwenye mitandao ya kimataifa ya walimu wa uanahabari. Mwongozo huu unakusudiwa kuhimiza ubadilishanaji wa mawazo, ushirikiano katika utayarishaji wa taarifa za habari na kukuzwa hatua kwa hatua kwa lengo la kuhakikisha unapata umilikaji kamili katika mabara yote na desturi za vyombo vya habari kuanzia Afrika na Ulaya, na kufika nchi za Mashariki ya Kati na Afrika Kas-kazini (MENA), Asia, Marekani na Shirikisho la Russia. Mwongozo huu umebuniwa na kutayarishwa na kundi maalumu lenye mwingiliano wa tamaduni tofauti la walimu wa uanahabari na wanahabari kutoka Afrika na Ulaya. Unashirikisha maoni ya wanahabari zaidi ya 100 kutoka Afrika na Ulaya ambao walishiriki tangu 2018 katika warsha za mafunzo ya majaribio ya awali ya kutumia yaliyomo. Ingawa mengi yaliyomo yanahusu Afrika na Ulaya, yanafaa pia kwingineko (kwa taswira za kanda ya MENA, Asia, Marekani na Shirikisho la Russia, tazama tovuti ya mradi www.mediaandmigration.com).

Utafiti wa ripoti za vyombo vya habari katika Afrika na Ulaya kuhusu uhamiaji na watu kufurushwa makwao umeonyesha kwamba habari zinazotolewa kuhusu suala lote hilo huwa pungufu au hukumbwa na tatizo la kupendelea au taswira za waandishi kujifikiria wenyewe tu. Uchunguzi linganishi katika Afrika na Ulaya unaonyesha kwamba vyombo vya habari kwenye mabara yote mawili huangazia zaidi habari za kusisimua za meli za wahamiaji zinazozama katika Bahari ya Mediterranean, huku vikipuuza uchambuzi wa sababu za kutatanisha za uhamiaji huo. Kwa mujibu wa uchanganuzi wa African Media Initiative (AMI), utoaji wa habari za uhamiaji katika nchi nyingi za Afrika hukosa kutilia maanani msukumo halisi wa kiuchumi, kijamii na kisiasa unaowapelekea watu kuhamia Ulaya kutoka Afrika, ilhali vyombo vya habari vya Ulaya mara nyingi huakisia suala la usalama mipakani (Fengler na wengine, 2020). Hiyo ni ishara kwamba wanahabari wa Ulaya wanahitaji pia mafunzo sawa na wenzao katika Afrika – jukumu ambalo ni mojawapo ya mawazo kiini cha mwongozo huu, tunapotafuta kuwafikia walimu wa uanahabari na wanafunzi wao katika mabara yote, tukitumaini kuwaunganisha kupitia kwa mtandao wetu www.mediaandmigration.com.

Ni jambo la muhimu kwa habari za uhamiaji na watu kufurushwa kuangaziwa katika muktadha halisi wa desturi za kitaifa na mfumo wa kiuchumi na kisiasa. Ripoti za habari kuhusu mataifa wanakotoka wahamiaji na wakimbizi zimeendelea kutilia mkazo athari za wahamiaji na wanaofurushwa kwa mataifa yanayowakaribisha. Hata hivyo, uhamiaji unapaswa na unaweza kutumika

kama kioo cha jamii asili za wahamiaji. Habari hizo zinapaswa kusimuliwa, kwa njia isiyopen-delea wala kuathiriwa na jazba, inayovutia sana na kuridhisha, na inayoelezea kauli za washika dau wote, ndani ya nchi na kitaifa. Ripoti za vyombo vya habari ni mswada jaribio wa kwanza wa historia ya watu. Je, wanahabari wanasimulia nini kuhusu enzi yao iliyojaa safari hatari na kubwa za raia wakitafuta mahala bora zaidi pa kuishi na kujipatia riziki na wanajipata wapi hatimaye?

Mwongozo huu unashughulikia uhamiaji na kufurushwa kwa njia ambazo zinahitaji maarifa ya-nayoegemea utafiti na utathmini makinifu wa asili za yaliyomo. Mwongozo huu kwa kutilia mkazo msingi wa kisomi wa uanahabari unanuia kutosheleza hitaji hilo. Kadhalika, utafiti umeonyesha kwamba ni nadra sana habari zinazotolewa kuangazia wahamiaji na wakimbizi binafsi; mwon-gozi huu unawageukia *watu* na kuwapatia haki ya kutangulia katika ripoti za habari na vidokezi vyake muhimu vitahusishwa na maeneo yote ya dunia.

Kwa mtazamo wa uchanganuzi, watu wote hao wamo katika makundi tofauti na hapo ndipo mambo yanakuwa magumu kiasi, hali inayowapasa wanahabari wawe makini kwa maelezo kami-lifu; wanahitaji kuchunguza kuhusu wahamiaji na wakimbizi ili kuipasha hadhira yao habari sahihi na kufanikisha mjadala wa umma kuhusu suala hilo, na mwongozo huu wa walimu wa uanahabari unanuia kusaidia katika jambo hilo. Wanahabari wanahitaji kufahamu kwamba *waki-kiwa safarini* huenda *wanalazimika* kuhama kutoka nchi zao asili wakiwa wakimbizi na kutafuta hifadhi salama kwingineko, huku wengine *wakilazimika* kuhama makwao lakini bado wanaende-lea kuishi katika nchi zao asili wakiwa IDPs — idadi ya IDPs ni kubwa zaidi kuliko ya wakimbizi lakini ripoti zake huwa pungufu kupindukia. Hawa wote na makundi mengine (kwa mfano watu wasio na uraia wa nchi yoyote) huitwa watu waliofurushwa na wengi wao wako chini ya ulinzi wa shirika United Nations Refugee Agency UNHCR.⁴ Mnamo 2019, UNHCR iliripoti kwamba *watu milioni 74 walifurushwa* na kulindwa na shirika hilo, ukiongezea milioni 5.6 ya Wapalestina wa-kimbizi⁵, jumla ya takribani milioni 80 (UNHCR, 2020, uk. 1). Wapalestina ni kundi maalumu la wakimbizi walio chini ya mamlaka ya United Nations Relief and Works Agency (UNRWA). Watu wengine wakiwa katika safari huenda wakaamua kuhama kutoka nyumbani kwa hiari. Hao ni *wahamiaji*. Watu karibu milioni 180 kati ya milioni 272 (thuluthi mbili) ya *wahamiaji wa kima-taifa* huwa *wanatafuta kazi* na wengi wao hutoka katika nchi zinazoendelea wakilenga kuingia katika mataifa tajiri (IOM, 2019b, uk. 2, uk. 25).

Malengo na muundo

Mwongozo huu unalenga kuwapatia walimu wa uanahabari mkusanyiko wenye maarifa mengi wa vitengo vya kuwawezesha kufundisha wanafunzi wa uanahabari jinsi ya kuelewa vyema vipengee

4 United Nations High Commissioner for Refugees (UNHCR).

5 Fahamu kwamba UNRWA inahusu wakimbizi wa "Palestine", si wakimbizi Wapalestina, kueleza kundi hilo kuwa la "watu ambao makazi yao ya kawaida yalikuwa Palestine kati ya Juni 1, 1946 na Mei 15, 1948, na walipoteza makao na riziki kufuatia mapigano ya 1948" (UNRWA, n. d.). Mwongozo huu unatumia wakimbizi Wapalestina kulingana na msemu wa kawaida.

tatanishi vya ukweli kuhusu utoaji wa habari za uhamiaji na watu kufurushwa, na kufasiri maarifa hayo kuwa mbinu thabiti na inayojali hisia za wote lakini muhimu na ya kulisimua kuripoti.

Mwongozo huu ni matokeo ya utafiti wa miaka mitano na uchanganuzi katika muktadha wa mradi wa Journalism in a Global Context (JiGC) ulioanzishwa 2015 kuimarisha wajibu wa vyombo vya habari kwa uhamiaji na watu kufurushwa katika Afrika na Ulaya. Walimu wa uanahabari na wanahabari kutoka Afrika na Ulaya wameungana kuandaa mtazamo unaoshirikisha tamaduni tofauti wa kuripoti kuhusu uhamiaji na watu kufurushwa. Washirika wakuu katika mradi huo ni Erich Brost Institute for International Journalism (EBI) katika Chuo Kikuu cha TU Dortmund cha Ujerumani, shirika lisilo la kiserikali la Africa Positive (lililoko Ujerumani), na AMI (yenye makao yake makuu Kenya) inayoleta pamoja mashirika huru 2,000 ya habari kutoka kote katika Afrika. Washirika wetu kimasomo katika bara Afrika ni pamoja na Chuo Kikuu cha Makerere, Kampala, Uganda; Ghana Institute of Journalism, Accra, Ghana; Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Dar es Salaam, Tanzania; Uganda Christian University, Mukono, Uganda; Chuo Kikuu cha Daystar, Nairobi, Kenya; Chuo Kikuu cha Addis Ababa, Addis Ababa, Ethiopia; Chuo Kikuu cha Nnamdi Azikiwe, Awka, Nigeria; Chuo Kikuu cha Witwatersrand, Johannesburg, Afrika Kusini; na Chuo Kikuu cha Yaoundé I, Yaoundé, Cameroon. Tumeshirikiana pia na Institut Supérieur de l'Information et de la Communication (ISIC), Morocco; Chuo Kikuu cha Kiamerika kilichoko Cairo (Idara ya Uanahabari na Mawasiliano ya Umma); Chuo Kikuu cha St. Petersburg State (Shirikisho la Russia); na Universidade Estadual Paulista (UNESP) Sao Paulo. Wakishirikiana na watafiti kutoka Bangladesh, Nepal, Myanmar na Pakistan, wanazuoni kutoka vyuo hivyo vikuu pamoja na wanahabari wamechangia katika mwongozo huu, ikiwa ni pamoja na nyenzo zilizoandamana na utayarishaji wa mwongozo huu. Afisi ya mashauri ya kigeni ya Ujerumani pamoja na wakfu wa Robert Bosch Stiftung wametoa pesa za kuanzisha mtandao wa JiGC na kuandaa mikutano, mafunzo na miradi ya utafiti katika nchi tofauti. Msaada wa wakfu uliwezesha kuandaliwa kwa vifaa vya kuandikiana na taarifa zilizotumiwa hapa, huku mashauriano baina ya kanda yakipata kipaumbele kati ya Afrika na Ulaya.

Kundi la JiGC katika safu ya mikutano ya kimataifa na warsha mijini Addis Ababa, Dakar, Dortmund, Nairobi na Rabat, limetambulisha changamoto zinazowakabili wanahabari na mashirika hasa katika Afrika, lakini pia katika nchi za Ulaya ambayo mwongozo huu utashughulikia. Wanahabari na wanazuoni zaidi ya 200 walioalikwa kusimulia waliyokumbana nayo kazini walisitiza kwamba pana uhaba wa maarifa kuhusu mtazamo na vipengele vya mtagusano wa tamaduni tofauti katika habari za uhamiaji. Walitilia mkazo haja ya kuwepo kwa rasilimali zaidi ili kuwezesha utafiti changanuzi na ushirikiano wa wahariri kwa lengo la kufuatilia habari muhimu. Wanahabari Waafrika hunufaika sio tu kwa mafunzo ya kueleza habari za wahamiaji na wakimbizi kwa mtazano wa Kiafrika; huwa pia wanajenga mitandao ya wanahabari wa jamii mbali mbali za Afrika — wakikiri kwamba hili ni suala tatanishi (Berger, 2011), wanaweza pia kukabiliana na kushindana ipasavyo na taarifa za mashirika ya kimataifa ya habari zinazotawala vyombo vyao. Pana haja pia ya kushughulikia vyombo huru vya habari vya kusambazia habari za kina na zinazoakisi vipengele vingi, na ujuzi wa kibiashara wa kutafuta masoko ya habari za kiutafiti. Mchango wa wanahabari

wa Ulaya na mkusanyiko wa matokeo ya utafiti kuhusu uhamiaji katika Ulaya unavyoshughulikiwa unabaini ongezeko la manufaa kwa maripota wa huko waliopata mafunzo ya suala hili.

Yaliyomo katika mwongozo huu yalifanyiwa majaribio ya awali kwenye vikao vya mafunzo barani Afrika mnamo 2018 na 2019, na wanahabari Waafrika walioshiriki katika mafunzo hayo wamehibitisha dosari zilizotajwa awali za uhalisia wa kueleza habari. Kadhalika, mwongozo huu umejaribiwa awali kwa kufundishia wanafunzi wa uanahabari katika Chuo Kikuu cha TU Dortmund kwa mihula mitatu. Kutoka kwa washiriki 100 wa warsha zetu za majaribio katika Ghana, Guinea, Ivory Coast na Nigeria, wengi hawakuwa na ujuzi wowote wa awali kuhusu uhamiaji na watu kufurushwa kama maudhui ya habari wala hawakuwa wamehusisha tukio hilo na masuala ya maendeleo. Washirika walikiri kutokuwa na habari kuhusu matatizo ambayo wahamiaji hukumbana nayo katika nchi mwenyeji wa za Ulaya. Walihukumu pia kwamba ingawa huenda raia wengi wa Afrika wanafahamu hatari za uhamiaji usiofuata kanuni zifaazo, matokeo ya kunufaisha wanayoyatarajia kwa kuhamia Ulaya — malipo na manufaa ya kifedha kwa familia pamoja na sifa wanazojizolea — ni mengi kuliko hatari hizo. Wanahabari wa Ulaya walioshiriki katika mikutano yetu ya kuufanyia mwongozo huu majaribio awali walisisitiza haja ya safari za kutangamana kita-maduni ili kuufahamu uhamiaji.

Mwongozo huu unakusudia kuwapa wanahabari wa siku zijazo ujuzi na maarifa yaliyosimuliwa hapo awali. Unawashughulikia hasa walimu wa uanahabari na wanafunzi katika vyuo vya elimu ya kitaalamu barani Afrika na Ulaya, pamoja na walio katika vitivo vya uanahabari kote ulimwenguni ambao wanaalikwa kuutumia mwongozo huu katika miktadha yao. Yaliyomo katika mwongozo huu yametungwa katika daraja tatu:

- **Daraja I:** Utoaji wa elimu inayozingatia utafiti kuhusu uhamiaji na watu kufurushwa ikitilia maanani vipengele vya kimuktadha katika Afrika na Ulaya, pamoja na kuripoti masuala hayo.
- **Daraja la II:** Uchanganuzi kifani wa vipengele vya kimuktadha katika Afrika na Ulaya.
- **Daraja la III:** Utendaji kazi ya uanahabari ya kuripoti kuhusu uhamiaji na watu kufurushwa na kuunda mitandao ya kuripoti katika tamaduni tofauti.

Mitazamo kuhusu uhamiaji na watu kufurushwa katika MENA, Asia, Marekani na Shirikisho la Russia imesimuliwa kwenye mtandao. Mbali na mitazamo hii ya nchi hizo, tovuti ya mradi www.mediaandmigration.com inatoa nyenzo nyingi pia.

Vifaa vyenye mbinu mbali mbali za kupata au kutoa habari na kutangamana vinapatikana kwenye tovuti ya mradi www.mediaandmigration.com. Kozi 13 zimepangwa kutekelezwa katika muhula mmoja kwa vikao visivyozidi 13. Mpangilio huo wa moduli unatoa nafasi ya kupunguza au kuongeza idadi ya vikao kulingana na muundo wa kila mpango wa masomo na kanuni zifaazo. Vikao visivyopungua 12 vimependekezwa katika hali iliyo bora. Kila kikao ni cha dakika 90. Moduli

zinazotoa muhtasari wa utafiti muhimu kuhusu uhamiaji na watu kufurushwa zimeshughulikiwa kwa kiasi kikubwa kuliko zile zinatilia mkazo uanahabari. Hii ni kwa sababu lengo la mwongozo huu ni kutoa huduma kubwa iwezekanavyo kwa walimu wa uanahabari ili kuwezesha kufundishwa pakubwa kwa mada hii.

Mwongozo umejaribu kurahisisha jinsi unavyotumiwa na kutekelezwa katika mifumo tofauti ya elimu ya vyombo vya habari. Mwongozo unatambua hali halisi za maisha zilizoenea kote (uhaba wa fedha, desturi za ufundishaji, kuzimiwa stima, uhaba wa maktaba na vifaa vya maabara, tofauti zilizopo kati ya walimu wa uanahabari na wanahabari wazoefu na mengineyo), na ndiposa unawaachia nafasi watumiaji wake kuamua kuandaa mihadhara, kupendekeza kuwaalika mara moja moja wahadhiri wageni, ama kutoa nafasi kwa wanafunzi kushiriki kikamilifu. Moduli zina-
pendekeza utaratibu tangamani wa kufundisha, kuhimiza moyo wa ushirikiano na uhusishwaji kikamilifu wa washirika. Kila moduli inaanzia kwa maelezo ya jumla ya malengo ya somo yata-
kayoshughulikiwa na walimu.

Baada ya hapo, matokeo ya somo yanaelezwa kwa usahihi ili kueleweka, jambo ambalo kulingana na nadharia ya uainishaji ya Anderson na Krathwohl (2001) huakisi malengo ya mafunzo ambayo wanafunzi wanafuatilia, na ni nini wahusika wanaweza kufanya baada ya kukamilisha somo. Nadharia inatambulikana kwa kuainisha malengo ya elimu katika ngazi sita tofauti za uzingativu (tazama Kielelezo 1).⁶

Ndiposa maelezo ya malengo ya somo yanatekeleza wajibu muhimu katika uandalizi wa mitihani na ufundishaji. Malengo ya somo hutoa maagizo bayana ya kufundishia na, wakati huo huo, ya mitihani. Ndiposa matokeo ya kujifunza yanaakisiwa kwa utendaji darasani na mazoezi ya baada ya darasa. Matokeo ya kujifunza hushughulikia sio tu stadi za utambuzi za somo lakini pia stadi za mitazamo binafsi na maadili, na nyanja nyingine za elimu.⁷


Matokeo ya kusoma yanafuatwa na muhtasari wa kila moduli ambao ni mkusanyiko wa muhtasari wa maudhui ya somo na utangulizi wake; moduli hatimaye inawasilisha maudhui, inainisha muktadha, mambo ya kutenda darasani na orodha kubwa ya marejeleo. Walimu na wanafunzi watapata orodha teule ya video fupi, vifaa vya kusikiza na kujisomea kwenye tovuti ya mradi www.mediaandmigration.com. Vingi kati ya vifaa hivyo vilitayarishwa kipekee kwa mwongozo huu na kutumika kwa mazoezi ya darasani. Kila moduli ina mahojiano na wataalamu, wahamiaji na wakimbizi, na makala bora teule za wanahabari. La muhimu zaidi ni kwamba walimu wanaalikwa kupakua kutoka kwa tovuti ya mradi www.mediaandmigration.com mkusanyiko wa slaidi

6 Nadharia ya uainishaji ya Anderson & Krathwohl (2001) ni masahihisho ya uainishaji wa Bloom (1956) ambao una madaraja sita ya utambuzi.

7 Daraja kuu za miliki ya stadi za mitazamo ya kibinafsi na maadili ni kupokea na kujibu. Ni vigumu kuthibitisha katika kozi hii viwango vya juu vya kuifanya mitazamo na mienendo kuwa sehemu ya maisha (kukubali na kuzingatia maadili, kujitolea, utaratibu na ubainishaji wa tabia). Miliki ya stadi za utendaji ni pamoja na kusogeza sehemu tofauti za mwili, uratibu na utumiaji wa msuli wowote wa mwendo kama vile kuandika, kupiga picha na stadi zingine husika. Kwa maelezo zaidi, tazama – miongoni mwa wengine: Krathwohl, Bloom, & Masia (1973), Simpson (1972), na Harrow (1972).

zilizotayarishwa kikamilifu kwa matumizi ya uhadhiri, na ni matumaini yetu kwamba watazitohoa slaidi hizo ili kuwafaa kwa matumizi mahususi, mahitaji ya maeneo yao na matilaba.

Kielelezo cha 1 : Nadharia ya Bloom ya uainishaji wa taratibu za utambuzi ambayo wanafunzi katika mandhari ya ualimu wanahitaji kufahamu



Chanzo: Armstrong (2010). Kielelezo chetu

Mawazo ya uvumbuzi, ubunifu na ubukuzi yasiyo na mipaka!

Msukumo wa kuutayarisha mwongozo huu ulitokana na miradi ya kitamaduni na sanaa. Wana-zuoni wa uanahabari kutoka kote katika dunia watatambua mifano yao ya kutia moyo. Mwongozo huu ukiangazia wahamiaji na wakimbizi umetoa mifano kadhaa ya utendaji kazi bora: Wasanii ambao wanaamini kwamba ujumbe unaowasilishwa kwa nyimbo ni bora zaidi kuliko maneno yaliyotamkwa (kwa mfano tazama Moduli 7, Cameroon (Prolific Dream Revolution 237)), au watunzi wa mashairi ambayo mrindimo wake una nguvu kuliko riwaya (Mansour, 2018). Sisi, katika EBI, tumeanza kushughulikia usanii na utaalumu wa masomo: Msanii wa kimataifa Yoko Ono alionyesha “Add Color (Refugee Boat)” katika Dortmund. Kazi zake za sanaa yake shirikishi zilizinduliwa wakati wa mkutano wa kila mwaka wa European Journalism Training Association (EJTA) uliofanyika Oktoba 2019, ulioandaliwa na EBI. Kwa miongo mingi, Yoko Ono amekuwa akijishughulisha na watu wanaokabiliwa na mateso wakitoroka vita na dhuluma na amebuni kazi kadha za sanaa kuonyesha dhiki ya watu hao, ikiwa ni pamoja na “Add Color (Refugee Boat)”. Wanafunzi wetu walishiriki kikamilifu kuongoza na kuwasiliana na maelfu ya wageni kwa miezi

mitatu. Walijifunza sura za uandishi habari ambazo huwa hazijitokezi madarasani. Mwanafunzi wa uanahabari Roman Winkelhahn anasimulia baadhi ya mafunzo aliyoyapata: “Waliofika katika onyesho hili la sana walikuwa waaminifu kabisa. Wanaposimama mbele ya sanduku la meli ya wakimbizi, wakialikwa kuandika mawazo yao, wanafanya hivyo papo hapo na wazi wazi. Kwetu sisi wanahabari, uaminifu na uhalisi ni muhimu sana. Ndiposa utunzaji wa onyesho hili ume-kuwa wa kunufaisha na kutupatia fursa ya kujumuika na wageni wake. Kuyasikiliza masimulizi ya wahamiaji na wakimbizi kulitupatia vidokezi muhimu vya mojawapo ya mada kuu ya nyakati zetu.” Onyesho hilo lilifana, hasa kwa sababu wanafunzi wetu wa uanahabari walijumuika kila siku na wageni wengi kutoka kote katika dunia, wakajifunza kutokana na masimulizi yao wakiwa wahamiaji na wakimbizi, na kujadili jinsi hadithi ya uhamiaji na kufurushwa inasimuliwa katika tamaduni tofauti za uanahabari.

Hitimisho

Kwa kuimarisha kiwango cha juu cha kuripoti kuhusu uhamiaji na watu kufurushwa katika nchi zao za asili, njia wanazopitia na kufika katika nchi wanazokusudia, ni matumaini yetu kwamba mradi huu utachangia katika kuboresha majadiliano ya umma. Mwongozo huu unanua kuimarisha uhuru wa wanahabari na mashirika na kukuza utaalamu wa fani ya uanahabari katika nchi zinazokumbwa na vikwazo vya kiuchumi na kisiasa. Utaendeleza mjadala wenye vipengele vingi katika vyombo vya habari kuhusu suala muhimu la uhamiaji na watu kufurushwa, na hivyo basi kuchangia katika taratibu za maamuzi za ngazi tofauti za jamii. Mwongozo utakuza ujuzi wa kufanya utafiti na kuripoti wa wanahabari walioshiriki na kupanua pakubwa maarifa yao na uelewa wa masuala haya katika muktadha wa kimataifa. Kwa kubuni mitandao inayoshirikisha wanahabari kutoka mataifa tofauti ya Afrika na kuimarisha uelewa wa tamaduni kutangamana katika Afrika yote, wanahabari watapanua uelewa wao wa maendeleo katika nchi majirani na kuweza kutumia ujuzi wa wataalamu wenzao walio nchini nyingine za Afrika katika kueleza habari zao. Hali ni hiyo hiyo katika Ulaya ambapo mpango wa kubadilishana ujuzi na maarifa kati ya wanahabari wa Ulaya na Afrika utaimarishwa. Kwa maeneo yote ya ulimwengu, mwongozo unaweza kusaidia kutoa mafunzo ya ujasiriamali kwa washiriki ili kuwawezesha kupata masoko ya habari zao na kuwafikia wahariri ili waunge mkono juhudi zao. Washiriki wanahimizwa kuwapasha wenzao na wakuu wao maarifa waliyopata, nao walimu wa uanahabari wanahimizwa kutoa mafunzo zaidi huria, halisi na ya kufaa katika fani ya kuripoti ulimwenguni. Ni matumaini yetu kwamba mwongozo huu utawaongezea nguvu walimu wa uanahabari, wanafunzi na wanahabari katika shughuli zao za kuripoti. Tunatarajia kwamba mfumo mpya wa kutoa habari utajenga imani kwani utashirikishwa katika mitaala ya masomo vyuoni, kwa kuongozwa na maamuzi thabiti kuhusu nyenzo ipi ya data inafaa kutumiwa na uakisi tunduizi wa rasilimali za chuo. Watu watakuwa kiini cha habari na hivyo basi kuwainua kuwa wahusika na kuwawezesha kuchukua maamuzi yanayolingana na ujuzi na stadi zao za hali ya sasa na za baadaye za jamii wanamoishi.

Susanne Fengler, Monika Lengauer, Anna-Carina Zappe na waandishi wote waliochangia

Marejeleo

Anderson, L. W., & Krathwohl, D. R. (2001). *A taxonomy for learning, teaching and assessing: Revision of Bloom's taxonomy of educational objectives*. New York: Longman.

Armstrong, P. (2010). *Bloom's Taxonomy*. Vanderbilt University Center for Teaching. Retrieved March 8, 2021, from <https://cft.vanderbilt.edu/guides-sub-pages/blooms-taxonomy/>

Berger, G. (2011). Networking African journalism educators: Bonding, bridging, and linking. *Global Media Journal*, 5(1), 1-23. <https://doi.org/10.5789/5-1-55>

Bloom, B. S. (1956). *Taxonomy of educational objectives: Handbook I: Cognitive domain. Handbook II: Affective domain*. New York: David McKay.

EMN (2018). *Asylum and migration. Glossary 6.0: A tool for better comparability produced by the European Migration Network*. Retrieved December 15, 2020, from https://www.emn.at/wp-content/uploads/2018/06/emn-glossary-6-0_en.pdf

Fengler, S., Bastian, M., Brinkmann, J., Zappe, A.-C., Tatah, V., Andindilile, M., Assefa, E., Chibita, M., Mbaine, A., Obonyo, L., Quashigah, T., Skleparis, D., Splendore, S., Tadesse, M., & Lengauer, M. (2020). *Covering Migration – in Africa and Europe: Results from a comparative analysis of 11 countries*. *Journalism Practice*, 1-21. Retrieved <https://doi.org/10.1080/17512786.2020.1792333>

Harrow, A. (1972). *A taxonomy of psychomotor domain: A guide for developing behavioral objectives*. New York: David McKay.

IOM (2019a). *Glossary on Migration*. Geneva. Retrieved December 15, 2020, from https://publications.iom.int/system/files/pdf/iml_34_glossary.pdf

IOM (2019b). *World migration report 2020*. Geneva. Retrieved December 15, 2020, from https://publications.iom.int/system/files/pdf/wmr_2020.pdf

Krathwohl, D. R., Bloom, B. S., & Masia, B. B. (1973). *Taxonomy of educational objectives. Handbook II: Affective domain*. New York: David McKay.

Mansour, I. (2018). *I am a refugee*. Retrieved March 5, 2020, from <https://www.pbs.org/video/i-am-a-refugee-hrq5gb/>

Migration Data Portal (2020). *Migration Data Portal: The bigger picture*. Retrieved September 20, 2020, from https://migrationdataportal.org/?i=stock_abs_&t=2019

Posetti, J. (2015). *Reporting migration, with a focus on refugees*. In Bonda, F. (Ed.), *Teaching journalism for sustainable development: New Syllabi* (pp. 79-98). Paris: UNESCO.

Posetti, J., & Bontcheva, K. (2020a). *Deciphering Covid-19 disinformation* (Policy Brief No. 1). Paris. Retrieved December 19, 2020, from https://en.unesco.org/sites/default/files/disinfodemic_deciphering_covid19_disinformation.pdf

Posetti, J., & Bontcheva, K. (2020b). *Disinfodemic: Dissecting responses to Covid-19 disinformation* (Policy Brief No. 2). Retrieved December 19, 2020, from https://en.unesco.org/sites/default/files/disinfodemic_dissecting_responses_covid19_disinformation.pdf

Reporters Without Borders (2020). *2020 World Press Freedom Index: Entering a decisive decade for journalism, exacerbated by coronavirus*. Retrieved September 22, 2020, from <https://rsf.org/en/2020-world-press-freedom-index-entering-decisive-decade-journalism-exacerbated-coronavirus>

Simpson, E. J. (1972). The classification of educational objectives in the psychomotor domain. Washington, D.C.: Gryphon House.

Turpin, S. (2018). Media coverage on migration: A practical guide for journalists. Retrieved December 18, 2020, from <https://rodakar.iom.int/sites/default/files/document/publications/Media%20Toolkit%202018%20-%20EN%20RO%20Dakar%20%281%29.pdf>

UN (2020a). Policy Brief: Covid-19 and people on the move. Retrieved September 29, 2020, from <https://unsdg.un.org/resources/policy-brief-covid-19-and-people-move>UN (2020b). UN Response to Covid-19. Retrieved September 29, 2020, from <https://www.un.org/en/coronavirus/UN-response>

UN (2020c). Press Conference by Secretary-General António Guterres at United Nations Headquarters. New York. Retrieved September 29, 2020, from United Nations website: <https://www.un.org/press/en/2020/sgsm20258.doc.htm>

UN General Assembly (2018). Global Compact for Safe, Orderly and Regular Migration: Resolution adopted by the General Assembly on 19 December 2018. Retrieved December 20, 2020, from https://www.un.org/en/ga/search/view_doc.asp?symbol=A/RES/73/195

UNDESA (2019). Population facts 2019: International migrants numbered 272 million in 2019, continuing an upward trend in all major world regions. New York. Retrieved November 16, 2020, from https://www.un.org/development/desa/en/news/population/international-migrant-stock-2019.html_PopFacts_2019-04.pdf

UNESCO (2020, March 27). UNESCO stresses importance of safety of journalists amid COVID-19 pandemic [Press release]. Paris. Retrieved September 29, 2020, from <https://en.unesco.org/news/unesco-stresses-importance-safety-journalists-amid-covid-19-pandemic>

UNHCR (n. d.). Glossary. Retrieved December 20, 2020, from <http://www.issm.cnr.it/progetti/emigrazione/METADATA%20E%20GLOSSARI/UNHCR/GLOSSARY%20UNHCR.pdf>

UNHCR (2020). Global Trends: Forced displacement in 2019. Copenhagen. Retrieved December 20, 2020, from <https://www.unhcr.org/5ee200e37.pdf>

UNHCR, & NUJ (2015). Reporting on refugees: Guidance by and for journalists. Retrieved December 19, 2020, from <https://www.unhcr.org/en-ie/58e1ed994.pdf>

UNRWA (n. d.). Palestine refugees. Retrieved December 19, 2020, from <https://www.unrwa.org/palestine-refugees>



MODULI 1

Masuala ya Uhamiaji na wakimbizi – Changamoto za Karne ya 21

na Susanne Fengler
na Monika Lengauer



MALENGO YA MODULI

- Kuwafahamisha washirika kuhusu mitazamo ya kimataifa ya masuala ya wahamiaji na wakimbizi.
- Kuwatahadharisha washirika kuhusu athari kwa mataifa asili, njiani na katika kikomo cha safari.
- Kuwahimiza washirika kujenga umakinifu wa kimtazamo kutathmini mjadala uliopo.



MATOKEO YA MAFUNZO¹

Kufikia mwisho wa moduli hii, washiriki wanapaswa kuwa na uwezo wa:

- Kutambua umuhimu wa masuala ya nchi asili, njiani na katika kikomo cha safari
→ **Matokeo ya mafunzo kwa mitazamo binafsi na maadili: Kupokea**
- Kutambua changamoto za kueleza habari za mada zinazoweza kuibua hisia kali kama vile uhamiaji na kuhamishwa kwa lazima. → **Matokeo ya mafunzo kwa mitazamo binafsi na maadili: Kuitikia/kushawishika**
- Kufafanua wazo la kuhusu mtazamo wa sasa wa suala hilo katika mabara tofauti.
→ **Matokeo ya mafunzo kwa utambuzi: Kutekeleza**
- Kuchunguza vifaa na taarifa tofauti kuhusu wahamiaji na wakimbizi. → **Matokeo ya mafunzo kwa utambuzi: Kutekeleza**

Muhtasari

Masuala ya wahamiaji, wakimbizi na waliofurushwa makwao lakini wangali ndani ya nchi zao (IDPs) ni changamoto ya karne hii. Kufikia katikati ya 2020, idadi ya wahamiaji na wakimbizi kote duniani ilifika kiwango cha juu kabisa kwa mara ya kwanza tangu Vita Kuu vya Pili (IOM, 2019b, uk. 2; UNHCR, 2020a, uk. 2) kwani inakadiriwa kwamba watu zaidi ya milioni 272 walihama kwa hiari au wakafurushwa² (Migration Data Portal, 2020b). Idadi inayozidi kuongezeka kwa kasi ya wahamiaji na wakimbizi imekuwa hali halisi ya nyakati zetu katika mabara yote, kama inavyoonyeshwa bayana katika Kielelezo 2 kutoka kwa Asian Development Bank (ADB, 2018, uk. 80, Figure 5.2) Wahamiaji wengi wa kimataifa huondoka makwao kwenda kutafuta nafasi bora zaidi za maisha — karibu thuluthi mbili za wahamiaji huwa wakitafuta kazi³ (IOM,

1 Tazama utangulizi, tanbihichini 6-7.

2 Kumbuka kwamba UNHCR hutumia istilahi “uhamisho wa kulazimishwa”. Wanaohamishwa kwa lazima ni pamoja na watu wote walio chini ya mamlaka ya UNHCR ikiwa ni pamoja na wakimbizi, waliofurushwa kutoka makwao, waombaji hifadhi, watu wasio na uraia wa taifa lolote na wengineo. Wakimbizi Wapalestina pia ni watu waliohamishwa kwa lazima na ambao masuala yao yanashughulikiwa na United Nations Relief and Works Agency (UNRWA). Tazama Moduli 2 kwa maelezo zaidi na uangalie pia faharasa ya UNHCR kwa maelezo kuhusu watu wanaoshughulikiwa na shirika hilo (UNHCR, n. d.).

3 Tazama faharasa iliyopendekezwa katika Moduli 2 kwa maelezo kuhusu wafanyakazi wahamiaji: EMN (2018); IOM (2019a); UNHCR (n. d.).

2019b, uk. 2). Kuhusu wakimbizi na watu waliofurushwa, kufikia mwisho wa 2019 shirika la United Nations High Commissioner for Refugees (UNHCR) lilikuwa limehesabu watu milioni 74 waliofurushwa kwa sababu za mateso, mapigano, dhuluma au ukiukaji wa haki za binadamu (ukiongezea wakimbizi milioni 5.6 Wapalestina⁴). Hii ndiyo idadi kubwa zaidi ya waliofurushwa iliyowahi kurekodiwa na iko juu katika mabara yote⁵ (UNHCR, 2020a, uk. 3, uk. 30, uk. 71-82).

- Watu milioni nane katika Colombia wamefurushwa kutokana na vita ambavyo vimeendelea kwa miongo mingi.
- Watu milioni saba kutoka Syria wamesajiliwa kuwa wakimbizi na milioni sita wamefurushwa kutokana na vita.
- Watu milioni tano katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) wamefurushwa na wengine karibu milioni moja wameandikishwa kuwa wakimbizi.
- Watu milioni nne kutoka Venezuela wamefurushwa wakiwa ng'ambo.
- Watu milioni tatu kutoka Afghanistan wamesajiliwa kuwa wakimbizi.
- Watu milioni mbili kutoka Sudan Kusini wamekuwa wakikimbia vita vya wenyewe kwa wenyewe vilivyotokea baada ya nchi hiyo kupata uhuru⁶.
- Watu milioni moja wasio na uraia wa taifa lolote⁷ wametoroka kutoka Myanmar.

Mataifa mengine ambapo watu wamefurushwa ni pamoja na Ukraine, Iraq, Libya, Somalia, Jamhuri ya Afrika ya Kati (CAR), Ethiopia na Yemen (UNHCR, 2020a, uk. 6). Wengi wa wakimbizi (68%) wanatoka nchi tano (Syria, Venezuela, Afghanistan, Sudan Kusini na Myanmar), kadhalika, IDPs wengi ni wa Colombia, Syria, DRC, Yemen, Somalia na Afghanistan. Ni muhimu kutambua kwamba IDPs ndio wengi miongoni mwa waliofurushwa (takribani milioni 46) na kubaki katika nchi zao, na takribani milioni 20 ni wakimbizi wanaovuka mipaka ya kimataifa (UNHCR, 2020a, uk. 2-3).


4 Kumbuka kwamba UNRWA inawataja kuwa Wakimbizi wa Palestine, wala sio Wapalestina wakimbizi, wakilieleza kundi hili kuwa “mtu ambaye makao yake ya kawaida yalikuwa Palestine kati ya Juni 1, 1946 na Mei 15, 1948, na ambaye alipoteza makao na njia za kujipatia riziki kufuatia mzozo wa 1948” (UNRWA, n. d.). Kulingana na matumizi ya lugha ya kawaida, mwongozo huu unatumia istilahi wakimbizi Wapalestina.

5 Nambari na desimali zimefanywa herufi kamili katika maandishi haya katika juhudi za kuweka uwiano mzuri kati ya usahihi na usomaji.

6 Sudan Kusini ilipata uhuru 2011, vita vya wenyewe kwa wenyewe vilianza 2013.

7 Tazama faharasa zilizopendekezwa katika Moduli 2 kwa ufafanuzi, hasa wa UNHCR (n. d.), wa ulinzi wa watu wasio na uraia wa taifa lolote.

Kielelezo 2: Wahamiaji wa kimataifa kulingana na maeneo wanakotoka (milioni)



Asia ingali asili kubwa ya wahamiaji wa kimataifa. Mataifa ambayo idadi yake ya watu imeendelea kukua na jumla ya nguvukazi kuzidi kupanuka yanaongoza kwa idadi ya wahamiaji kulingana na Asian Development Bank (ADB, 2018, uk. 80).


Chanzo: Hesabu iliyofanywa na ADB, wakitumia data kutoka UNDESA (ADB, 2018, uk. 80, Figure 5.2). Mchoro ni wetu.

Masuala ya uhamiaji na watu kufurushwa makwao huathiri pakubwa nchi zinazowapatia makao. Tutatoa mifano michache kuthibitisha kauli hii. Ni mataifa matano pekee ambayo ni mwenyeji wa wengi wa wakimbizi: Mnamo 2019, Turkey ilikuwa na wakimbizi milioni 3.6, Colombia milioni 1.8, Pakistan milioni 1.4, Uganda milioni 1.4 na Ujerumani milioni 1.1 (UNHCR, 2020a, uk. 3), ilhali kwa upande mwingine, thuluthi mbili za wahamaji wote wa kimataifa huishi katika mataifa 20 pekee, hasa Marekani (milioni 51), Ujerumani na Saudi Arabia (takribani milioni 13 kila mmoja), Shirikisho la Russia (milioni 12) na Uingereza (milioni 10; UNDESA, 2019a, uk. 11; tazama Kielelezo 3).

Hata hivyo, utaratibu wa uhamiaji na watu kulazimishwa kuhama makwao umebadilika pakubwa katika ulimwengu ambapo kiasi cha habari, udijitishaji na uhamiaji na uhamaji wa watu zimezidi kuongezeka. Ingawa uhamiaji ni tukio la kimataifa, safari nyingi zinahusu kundi ndogo la mataifa. Ni tukio ambalo limeenea na kuvuka mipaka ya kanda na mabara na kusababisha changamoto kwa wahamiaji na wakimbizi, jamii mwenyeji, waandalizi wa sera na wanahabari wataalamu wanaotekeleza wajibu mkuu katika kushawishi maoni ya umma.

Mifano iliyotolewa awali haionyeshi bayana umuhimu wa mada hii tu, lakini inatukumbusha haja ya kuwa waangalifu kwa maneno tunayoamua kutumia. Mara nyingi vyombo vya habari hutumia istilahi zenye maana tofauti kabisa na zilizokusudiwa, huku vikichanganya wahamiaji, wakimbizi,

Kielelezo 3: Mataifa 20 yenye wahamiaji wengi zaidi wa kimataifa (kushoto) na mataifa asili (kushoto) mnamo 2019 (kwa mamilioni)



Zaidi ya asilimia 40 ya wahamiaji wote wa kimataifa duniani (milioni 112) walizaliwa katika bara la Asia, hasa India na China. Mexico ilikuwa nchi ya pili kubwa ya asili, ikifuatwa na Shirikisho la Russia katika nafasi ya nne. Mbali na Marekani, nchi kadha za Ulaya zina idadi kubwa ya wahamiaji, hasa Ujerumani. Tukiangalia jinsi walivyotawanyika kulingana na mapato ya jumla ya taifa,⁸ karibu thuluthi mbili ya wahamiaji wa kimataifa walikuwa wanaishi katika mataifa yenye pato la juu mnamo 2019 – takribani milioni 176. Idadi hiyo inaweza kulinganishwa na watu milioni 82 waliozaliwa ugenini na ambao walikuwa wakiishi katika mataifa yenye pato la wastani (karibi thuluthi moja ya wahamiaji wanaojulikana) na milioni 13 katika nchi zenye kipato cha chini mwaka huo huo. (IOM, 2019b, uk. 26). Chanzo: IOM World Migration Report 2020 (2019b, uk. 26, Figure 2).

wahamiaji wasio wa kawaida,⁹ waliofukuzwa makwao, safari mchanganyiko za wakimbizi na wahamiaji na mengineyo. Wahamiaji mara nyingi huondoka nchini zao wakienda kutafuta nafasi za kujijenga kimaisha, kinyume na wakimbizi ambao hulazimika kukimbia vita, vurugu, mapambano au dhuluma na huvuka mipaka ya kimataifa wakitafuta usalama katika nchi nyingine. Kutofautisha kati ya wahamiaji na wakimbizi ni suala lenye utata wa kisiasa kwa upande mmoja, na kwa upande mwingine tofauti kati ya makundi hayo mawili zimeainishwa bayana na sheria za kimataifa. Wakimbizi wameelezwa chini ya sheria za kimataifa na za kanda za wakimbizi, na jamii ya kimataifa ina jukumu la kisheria kwao (Mkataba wa Wakimbizi wa 1951 na mwingine wa 1967 imeweka majukumu ya mataifa yaliyoitia sahihi; 2016). Hata hivyo, wote wawili,

8 Tazama Moduli ya 2 kwa maelezo. Tofauti ya nchi katika vikundi vya mapato inarejelea Benki ya Dunia inayojumusha uchumi wa kipato cha chini, uchumi wa chini wa kipato cha kati, uchumi wa kipato cha kati ya juu na uchumi wa kipato cha juu (UNDESA, n. d.; Benki ya Dunia, n. d.).

9 Kuna istalahi nyingi zitumiwazo kuwaeleza wahamiaji wasio na hati halali (kwa mfano viza) za kuingia na/au kukaa katika nchi ya kigeni, tazama Moduli 2.

wahamiaji na wakimbizi, wana haki zao za binadamu (tazama Moduli 2). Tofauti kati ya wahamiaji na wakimbizi zinaelezea kwamba mikataba miwili tofauti ya kimataifa ilifikiwa kufuatia mashauriano (UN, 2020). Mikataba yote miwili ilitokana na Azimio la 2016 la New York kuhusu Wakimbizi na Wahamiaji (UN General Assembly, 2016).



ZOEZI LILILOPENDEKEZWA KUSHUGHULIKIA STADI ZA UTAMBUZI ZA UTEKELEZAJI NA STADI ZA MITAZAMO YA KIBINAFSI NA MAADILI ZA KUPOKEA:

NHCR na EarthTime wanatoa taswira ya safari za wakimbizi katika hali teule kati ya 2000 na 2015 (Earthtime & UNHCR, 2019). Kumbuka kwamba kila kitone kinawakilisha wakimbizi 17. Washiriki wanapaswa kuchagua hali tofauti — Nigeria, Colombia, Syria au nchi yoyote waliyoichagua — na waandike ripoti fupi za habari (angalau herufi 600) kuhusu hali hiyo, wakitumia kurasa za nchi katika tovuti ya data ya uhamiaji kwa marejeleo ya data na maelezo ya awali. Wawasilishe taarifa hiyo ya habari, maarifa yao na utathmini kuhusu uhamiaji na safari za wakimbizi.

Mkataba wa Ulimwengu kuhusu Wakimbizi na Mkataba wa Ulimwengu kwa Uhamiaji Salama, kwa Mpango na Kanuni

Mikataba hiyo miwili — Mkataba wa Ulimwengu kuhusu Wakimbizi na Mkataba wa Ulimwengu kwa Uhamiaji Salama, kwa Mpango na Kanuni — hushughulikia usimamizi wa watu walio safarini za uhamiaji na uhamaji na jinsi ya kuwalinda katika mataifa yao asili, wakiwa safarini na katika nchi mwenyeji. Mikataba hiyo inatoa muundo sanifu wa kwanza unaokubalika na wengi kuhusu safari za watu tangu 1951.¹⁰ “Msukumo wa kuandaa mikataba hiyo ulitokana na kuwasili Ulaya kwa wahamiaji na wakimbizi zaidi ya milioni moja mnamo 2015. Kwenye mashauriano kuhusu mikataba hiyo, masuala mengine ya awali ambayo hayakuwa yameshughulikiwa kikaamilifu kwa muda mrefu yalishirikishwa, kama vile suala la waliofukuzwa makwao na kushindwa kurudi kwa muda mrefu na hatua za kulinda haki za wahamiaji” (Ferris & Martin, 2019, uk. 5).¹¹

Mkataba wa Kimataifa wa Uhamiaji (UN General Assembly, 2018a) unaegemea maafikiano ya kimataifa yanayoainisha haki za wahamiaji na pia wakimbizi: haki za binadamu ni nguzo kuu na

¹⁰ Utatanishi wa Mapatano kuhusu Wakimbizi ya 1951, yakifuatiwa na mkataba wake wa 1967 (tazama Moduli 2).

¹¹ UNHCR inaeleza hali ya wakimbizi walio uhamishoni kwa muda mrefu ambao idadi yao ni 25,000 au zaidi wakitoka taifa moja na ambao wamekuwa uhamishoni kwa angalau miaka mitano mfulululizo katika nchi yoyote ya kigeni mwenyeji wao (Wakimbizi Wapalestina hawamo katika kundi hili kwani wako chini ya mamlaka ya UNRWA). Wakimbizi walio uhamishoni kwa muda mrefu huhitaji kushughulikiwa kwa mtazamo wa uangalizi maalumu na suluhu. Inakadiriwa kwamba wakimbizi milioni 15.7 (77 %) waliokuwa katika hali hiyo ya kukaa kwenye hifadhi kwa muda mrefu kufika mwisho wa 2019, na milioni 15.9 mwaka 2018. Wakimbizi hawa milioni 15.7 walikuwa wakiishi katika mataifa mwenyeji, wakijumuisha hali 51 za wakimbizi walio uhamishoni kwa muda mrefu. Takwimu zinajumuisha pia hali zinazokumba wakimbizi Wa-afghan katika Pakistan na Iran pamoja na hali za wakimbizi wa Sudan Kusini walio Kenya, Sudan na Uganda (UNHCR, 2020a, uk. 24).

maafikiano yanayokataza uhalifu wa magenge (ikiwa ni pamoja na mkataba wa kuzuia ulanguzi wa binadamu na unaopiga marufuku usafirishaji kimagendo wa wahamiaji); mkataba wa kupinga utumwa; mkataba kuhusu badiliko la hali ya anga; mikataba inayohimiza kazi za heshima na uhamiaji wa nguvukazi; Ajenda ya 2030 ya Maendeleo Endelevu na mingineyo. (UN General Assembly, 2018a, uk. 1, Preamble, para 2). Mkataba huo unakusudia kuimarisha ushirikiano wa kimataifa kwa kusisitiza “mshikamano”, “ushirikiano katika majukumu”, “uwiano wa maku-sudio” na “uelewa wa wote” kuhusu uhamiaji wa kimataifa “ambao inakubalika unaathiri nchi zetu, jamii, wahamiaji na familia zao” (UN General Assembly, 2018a, uk. 1, Preamble, para 8) kuanzia mataifa wanakotoka, wanakopitia na nchi mpya mwenyeji. Mkataba unakusudia:

“kuwezesha uhamiaji salama, unaofanyika kwa mpango na kufuata kanuni, huku ukijaribu kupunguza visa na athari za uhamiaji usiozingatia kanuni [...] Uhamiaji salama, kwa mpango na kanuni ni wa manufaa kwa wote unapofanyika kwa weledi, uliopangwa na kukubaliwa na pande zote. Uhamiaji haufai kamwe kuwa tendo linalotokana na hali mbaya maishani na ya kukatiza watu tamaa. Na endapo mambo yanageuka kuwa hivyo, hatuna budi kushirikiana kushughulikia mahitaji ya wahamiaji wahusika kwa kutafuta ufumbuzi wa changamoto zinazowakabili. Ni lazima tufanye kazi pamoja ili kujenga hali zinazoweza jamii na watu binafsi kuishi kwa usalama na hadhi katika mataifa yao” (UN General Assembly, 2018a, uk. 4, para 11, 13).

Ibara ya 12 inaeleza kwamba mkataba unanua “kuweka mikakati kukabiliana na matatizo na mambo ya kimuundo ambayo huzuia watu kujenga na kudumisha mbinu endelevu za kujipatia riziki katika nchi zao za asili, na hivyo basi kuwalazimisha kuangalia kwingineko kwa mategemeo ya siku zijazo”.

Mkataba huo ambao umelenga kutimiza mengi, umefungua milango ya uthibiti wa kimataifa wa uhamiaji kwa mpango, kuzingatia kanuni na kujali usalama, mambo ambayo tukiangalia historia, miundo iliyopo ya sheria na sera, imeshindwa kutimiza (Gest na wengine, 2019). Utekelezwaji wake unaongozwa na shabaha 23 zilizoainishwa, tukianza na ukusanyaji wa data (Shabaha 1; tazama Moduli 2). Shabaha 17 ambayo inalenga kumaliza “aina zote za ubaguzi na kuimarisha mjadala wa umma unaozingatia ushahidi thabiti katika kujenga taswira za uhamiaji” inahusika kimuktadha na vyombo vya habari na uhamiaji.

Msingi wa Mkataba wa Kimataifa wa Uhamiaji (UN General Assembly, 2018b) ni sheria za kimataifa na viwango vya matarajio ya jamii ya kimataifa, ikiwa ni pamoja na Mkataba wa Wakimbizi wa 1951 na maafikiano kuhusu haki za binadamu. Unawahimiza washika dau kuimarisha juhudi zao na kuzuia au kusuluhisha mizozo na kutafuta ufumbuzi wa kiini cha hali zinazowafanya wengi kuwa wakimbizi (ibara 9). Mataifa yote wanachama wa Umoja wa Mataifa pamoja na washika dau wengine na vyombo vya habari watagawana sawa na kwa nia iwezayo kutabirika wajibu na mzigo wa mkataba huo (UN General Assembly, 2018b, para 3).

Kwenye shabaha zake nne, Mkataba wa Kimataifa kuhusu Wakimbizi unanuia: (i) kupunguza shinikizo kwa mataifa mwenyeji wa wakimbizi, hasa nchi majirani wa maeneo ya vita; (ii) kuimarisha uwezo wa wakimbizi kujitosheleza (mathalani kwa chakula na lishe); (iii) kupanua mbinu za kupatikana ufumbuzi katika mataifa mwenyeji wa wakimbizi (hizi ni pamoja na njia salama na zinazosimamiwa ipasavyo za kuwezesha wakimbizi kuishi kihalali katika nchi mwenyeji, kwa mfano kwa visa za ufadhili, kuwawezesha kuungana na familia zao, nafasi za elimu au ajira, mbali na kuwapatia makao¹²); na (iv) kusaidia kuimarisha hali katika mataifa asili ili kuwawezesha wakimbizi kurudi salama na kwa hadhi (UN General Assembly, 2018b, uk. 2, para 7).

Wadadisi wa kimataifa wanajiuliza iwapo hali ya wahamiaji na wakimbizi itakuwa bora zaidi kutokana na makubaliano hayo. McAdam (2018) anatabiri kwamba 2018, mwaka ambao mikataba hiyo miwili iliidhinishwa, “umeweka historia kwa kuwa mwaka muhimu kwa kuwalinda wakimbizi na wahamiaji” lakini anaongezea “angalau katika maandishi” (McAdam, 2018, uk. 571). Pana matumaini, hata hivyo, kwa sababu mikataba yote miwili inaahidi kuheshimu haki za wahamiaji na wakimbizi na inaungwa mkono na idadi kubwa ya wanachama wa Umoja wa Mataifa.¹³ Inawakilisha mifumo mipya ya kusanifisha jinsi ya kushughulikia safari za wahamiaji na wakimbizi kwa kuweka viwango vipya na taratibu za kuimarisha ushirikiano wa kimataifa kuhusu wahamiaji na wakimbizi. (Ferris & Martin, 2019). Mkataba wa Ulimwengu wa Uhamiaji ni mwanzo wa uwekaji sheria ulimwenguni kusimamia uhamiaji (McAdam, 2018). Mkataba huo unaharakisha harakati za “kuwafanya wakimbizi kuwa wahusika katika kupanga hali zao za baadaye” kwani unalenga kubadilisha mipango ya kuwakaribisha wakimbizi kwa kuwaweka katika kambi na badala yake kuzingatia “muundo ambao unaimarisha ushirikishwaji wa wakimbizi kwenye harakati za kijamii na kiuchumi, ikiwa ni pamoja na nafasi za kupata elimu katika mfumo wa kitaifa, huduma za afya na nyinginezo, pamoja na nafasi za kazi” (Grandi, 2019, uk. 24).

Mikataba hiyo miwili ambayo inalenga kushughulikia maslahi mbalimbali na matarajio, imeelezwa bayana kwamba makubaliano hayo sio ya kubana kwa wanachama, na kwamba inatambua wajibu wa kimsingi na uhuru wa kila taifa mwanachama. Ingawa mikataba ina malengo inayonua kufikia, shabaha yake ni kutafuta ufumbuzi wa matatizo. Utekelezaji wa Mkataba wa Wakimbizi utachunguzwa kila baada ya miaka minne kwenye kikao cha Baraza la Kimataifa la Wakimbizi (kikao cha kwanza kilifanyika Geneva mnamo Desemba 2019), na hatua zilizopigwa kuhusiana na Mkataba wa Uhamiaji zitajadiliwa kwenye Baraza la Uchunguzi wa Uhamiaji lita-kalokusanyika kila baada ya miaka minne kuanzia 2022 (UN General Assembly, 2018a; UN General Assembly, 2018b).

12 Tazama faharasa zilizopendekezwa katika Moduli 2 kwa maeleza kuhusu kupewa upya makao: EMN (2018); IOM (2019a).

13 Mikataba hii miwili ilitokana na Azimio la New York kuhusu Wakimbizi na Wahamiaji ambalo Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa (UNGA) liliidhinishwa kwa kauli moja mnamo Septemba 19, 2016. Mkataba wa Ulimwengu kuhusu Wakimbizi uliidhinishwa na UNGA Desemba 17, 2018, kwa kura 181 za waliounga mkono; nchi mbili zilipinga (Hungary na Marekani) na tatu hazikupiga kura (Dominican Republic, Eritrea na Libya). Mkataba wa Ulimwengu kuhusu Uhamiaji Salama, wenye Utaratibu na Kuzingatia Kanuni uliidhinishwa na serikali 164 katika mkutano wa ngazi za serikali uliofanyika Marrakech, Morocco, mnamo Desemba 10, 2018. Uliidhinishwa rasmi na UNGA mnamo Desemba 19, 2018, baada ya kupigiwa kura 152 za kuunga mkono, tano za kupinga (Jamhuri ya Czech, Hungary, Israel, Poland na Marekani) na mataifa 12 hayakupiga kura (Algeria, Australia, Austria, Bulgaria, Chile, Italia, Latvia, Libya, Liechtenstein, Romania, Singapore na Uswizi; UN News, 2018).

Janga la Uviko-19 huenda likawa changamoto kuu ya kwanza kwa Mkataba wa Ulimwengu kuhusu Wakimbizi na Mkataba wa Ulimwengu kwa Uhamiaji Salama, kwa Mpango na Kanuni. Janga hilo limewaweka wasio na makwao katika hatari ya “kuzuiwa kufikia huduma za afya, kinga za kiuchumi na juhudi za kuanza upya maisha ya kawaida” (Lambert na wengine, 2020, uk. e313). Kama ilivyoielezwa hapo awali, mikataba yote miwili imelenga kutimiza mengi kwa kufungua milango ya usimamizi wa kimataifa wa safari za watu kuzingatia viwango vipya na taratibu za kumimarisha ushirikiano wa kimataifa. Janga la Uviko-19 lilituletea mambo tofauti mapya maishani, maelfu ya vikwazo vya usafiri vikawekwa, mipaka ikafungwa na sheria zikabadilika haraka. Watu wamekwama mipakani, wakawekwa vizuizini, wakafukuzwa baada ya kutangazwa kuwa watu wasiotakikana katika nchi mwenyeji ama wakashindwa kurudi nyumbani; wengine “wamebaguliwa na kunyimwa nafasi za kupata haki [...] ikiwa ni pamoja na habari, uchunguzi wa kimatibabu” na mengineyo. (UN Network on Migration, n. d., uk. 3). Katika hali kama hiyo, wahamiaji na wakimbizi hujipata hatarini ya kuaibishwa na kuchukiwa kwa kuwa wageni (UN Network on Migration, n. d., uk. 3; UNHCR, 2020b). Hali hizo za kimuktadha zinatishia kupunguza kasi ya kushirikisha wahamiaji na wakimbizi katika taratibu za matibabu na mikakati ya jamii ya kuwakinga wanyonge na masuala ya kiuchumi kama ilivyonuiwa na mikataba hiyo miwili. Desturi njema (UN Network on Migration, n. d., uk. 8-22) zaonyesha kuwa serikali kote ulimwenguni zimetoa muda wa msamaha kwa wahamiaji wasio na vyeti hitajika kurudi nyumbani (Kuwait), zimewapatia tena wafanyakazi wahamiaji vibali vya kazi na pia viza mara tu baada ya muda wa hati za awali kumalizika (United Arab Emirates), zimeachilia watu waliozuiliwa (Uholanzi; Zambia) ama kusimamia huduma za afya kwa wahamiaji (Colombia). Ureno imeamua kwamba wahamiaji na wakimbizi wote ambao wamewasilisha maombi ya vyeti vya makazi watapata vyeti vya muda na kuwa na haki sawa na raia, ikiwa ni pamoja na huduma za jamii. Ujerumani imeanzisha jukwaa linalodhibitiwa na kompiuta la kuandikisha vibarua, ikiwa ni pamoja na wanaotafuta kimbilio la hifadhi ya kisiasa, ili kufanya kazi ya kujinufaisha kutokana na uhaba wa nguvukazi uliosababishwa na Uviko-19 (Lambert na wengine, 2020; UN Network on Migration, n. d.; UNHCR, 2020b).



ZOEZI LILILOPENDEKEZWA KUSHUGHULIKIA STADI ZA UTAMBUZI ZA UCHANGANUZI NA STADI ZA MITAZAMO NA MAADILI ZA KUPOKEA;

Washirika waunde makundi mawili: Kundi 1 litafiti Mkataba wa Kimataifa wa Wakimbizi nalo kundi la pili lichunguze Mkataba wa Kimataifa wa Wahamiaji (UN, 2020).

Kila kundi katika uchunguzi wake litafute masuala yanayohusiana na uanahabari na kutayarisha muhtasari wa ukurasa mmoja kujibu swali lifuatalo: Vyombo vya habari vinaweza kujitolea kutoa mchango gani unaotangamana na shabaha za mikataba hiyo miwili? (UNHCR, 2020b).

Mataifa tofauti, mitazamo tofauti

Mijadala katika mataifa mengi ya Mkataba wa Ulimwengu kuhusu Wakimbizi na Mkataba wa Ulimwengu kwa Uhamiaji Salama, kwa Mpango na Kanuni imeonyesha tofauti kubwa za kimtazamo katika masuala ya wahamiaji na wakimbizi. Ingawa sehemu kubwa ya mwongozo huu inaangazia Afrika na Ulaya, tunahimiza walimu wenzetu katika kanda nyingine za ulimwengu kushamirisha mifano na maelezo tunayoitumia kuanzia Moduli 1 hadi 13. Waandishi wenzetu wasifika kutoka MENA, Asia, Marekani na Shirikisho la Russia huchangia uchanganuzi wa elimu na uanahabari na kutoa ujuzi wa kipekee kuhusu uhamiaji na watu kuhamishwa kwa lazima kote katika maeneo ya ulimwengu. Rasilimali hizi za thamani isiyoweza kukadiriwa zimechapishwa kama miswada kamili katika www.mediaandmigration.com.

Kusema kweli, watu wengi hushangaa wakijifunza kuhusu mtazamo wa wakimbizi na waliofuruishwa makwao kwingineko. Barani Afrika, wengi hufurahia uhamiaji ingawa kuna visa vichache vya chuki ya wageni na wanahabari huwa hawaoni haja ya kuliangazia suala hilo katika taarifa zao kwa sababu ni jambo lililomea mizizi kwenye jamii za Afrika. Uhamiaji mdura¹⁴ — safari za uhamiaji na uhamiaji wa watu zinazobadilika kila mara kati ya mataifa — ni tukio la kawaida kote katika Afrika ambapo miungano kadhaa inatoa uhuru wa kuingia na kutoka nchi moja hadi nyingine.¹⁵ Ni kawaida ya watu kuvuka mipaka ya nchi kwa sababu, kwa mfano, ya mahusiano ya karibu ya kabila, tamaduni na lugha fauka ya kutawanyika katika mataifa huru tofauti yaliyobuniwa na wakoloni (Robinson, 2016). Ingawa ni suala ambalo hupewa kisogo na wadadisi wengi wa kimataifa, nchi nyingi za Afrika ni mwenyeji wa idadi kubwa ya wakimbizi na wafanyakazi wahamiaji kutoka kwa mataifa jirani. Ramani ya utangamano ya EarthTime na UNHCR (2019) inasawiri kiwango cha uhamiaji huo barani Afrika, nayo Idara ya Mashauri ya Uchumi na Jamii ya Umoja wa Mataifa (UNDESA) hutengeneza upya data hiyo kila mara. Mnamo 2019, asilimia 65 ya wahamiaji wote wa nchi za Afrika kusini ya Jangwa Sahara walikuwa wakiishi katika mataifa mengine ya eneo hilo¹⁶ (UNDESA, 2019b, uk. 3). Kuna baadhi ya visa ambapo uhamiaji huashiria maendeleo (tazama kielelezo kuhusu Nigeria). Mtu yeyote aliyeenda ng'ambo — hasa Ulaya — hupata heshima kubwa na taadhima akirejea nyumbani (Marfaing, 2016). Waafrika wengi bado wanajihisi kuwa na uhusiano mkubwa na waliokuwa watawala wao wa kikoloni na huamini Ufaransa, Ureno na Uingereza ni watu wao wa karibu (tazama Moduli 3). Mtindo huu umechochewa na picha za kuvutia za Ulaya ambazo hubuniwa sio tu na vyombo vya habari na burudani lakini pia — na pengine kwa kiwango kikubwa — na picha na risala ambazo wahamiaji husambaza kupitia kwa mitandao ya jamii na pesa ambazo Waafrika waliotawanyika ng'ambo hutuma nyumbani.

14 Tazama faharasa zilizopendekezwa katika Moduli 2 kwa ufafanuzi (IOM, 2019a; EMN, 2018).

15 Katika kiwango kidogo, usafiri huru husimamiwa kwa mfano na Jumuiya ya Nchi za Afrika ya Kati (ECCAS) na Jumuiya ya Kiuchumi ya Mataifa ya Afrika Magharibi (ECOWAS; ILO, n. d.). Muungano wa Afrika huhimiza usafiri huru katika Afrika.

16 Hili linafungamana na kanuni za kimataifa za safari za kawaida na uhamiaji: Wahamiaji wengi wa kimataifa huhamia nchi nyingine katika kanda ya walikozaliwa, kwa mfano zaidi ya thuluthi mbili ya wahamiaji wa kimataifa waliozaliwa Ulaya huishi Ulaya. Mnamo 2019, wahamiaji milioni 42 kati ya milioni 61 wa kimataifa waliozaliwa Ulaya walikuwa wanaishi katika nchi za Ulaya (69%). Wengi wa wahamiaji kutoka nchi za Afrika za kusini ya Jangwa Sahara walikuwa wakiishi katika nchi nyingine za Afrika kusini ya jangwa hilo (65%; UNDESA, 2019b, uk. 3).

Mara nyingi wahamiaji hujipata wakishinikizwa na jamii za nyumbani kuthibitishia ufanisi wao kwa jamii hizo ambazo huenda zilijikaza kushirikiana kugharamia uhamiaji wa mmoja wao na huwa zinatarajia kuona faida ya juhudi zao kupitia kwa pesa ambazo mhamiaji huwatumia (Sanchez na wengine, 2018). Pesa zinazotumwa nyumbani na wahamiaji zimekuwa njia mojawapo ya mapato kwa mataifa mengi ya Afrika (African Development Bank Group, 2011; Plaza & Ratha, 2011). Hali hiyo imewapatia changamoto viongozi wengi wa kisiasa hasa wanapohitajika kuangazia masuala ya uhamiaji, na pia kuhusiana na tatizo sugu la kazi katika nchi wanakotoka wahamiaji (Koch na wengine, 2018). Tukiangalia Nigeria, tayari Muungano wa Ulaya (EU) ume-tangaza masharti makali ya taratibu za kutoa viza ya Schengen kwa Wanigeria ukihoji kwamba taifa hilo “linashindwa kutekeleza wajibu wake kuhusiana na kurudi nyumbani na kuwakaribisha raia wake wote wanaoishi Ulaya kiharamu” (Schengen Visa News, 2020). Kwa sababu ya uhamiaji katika Afrika kupewa kisogo na wanahabari barani, vyombo vya habari vya Afrika hutoa taarifa chache na kuwa na vichwa haba vya habari kuhusu Waafrika wanaohama kutoka barani wakielekea Kaskazini.


Kinyume kabisa na hali hiyo, tatizo la uhamiaji na wakimbizi lililoanza 2015 limetawala ajenda za kisiasa na majadiliano ya umma katika Ulaya, hasa tangu Chansela Angela Merkel wa Ujerumani alipoamua kukubali waathiriwa wa vita vya wenyewe kwa wenyewe vya Syria vya 2015 kuingia katika nchi yake bila pingamizi yo yote (European Commission, 2018). Tangu wakati huo, mjadala kuhusu uwezo wa Ulaya kukubali wahamiaji wengine na kuwapatia wakimbizi makao limeathiri kwa kiwango fulani matokeo ya uchaguzi, kama vile katika Uingereza, Ujerumani, Ufaransa na Italia. Vyama vya kisiasa vinavyozingatia mfumo wa kujitafutia umaarufu kwa kuonyesha kujali fikra za umma, vilitilia mkazo tishio la wahamiaji. Hili limesababisha mgawanyiko mkubwa uliopo kati ya mataifa ya Ulaya ya Mashariki ya Kati (CEE) na yale ya Ulaya Magharibi kuhusiana na masharti ya sera ya uhamiaji (Lehne, 2016; tazama Moduli 5). Mtazamo wa karibuni ni kwamba idadi ya wahamiaji kutoka nchi za Afrika kwenda EU imeendelea kuongezeka — kutokana hasa na kutokuwepo na ustawi wa kiuchumi na ongezeko la juu la idadi ya watu katika bara Afrika linalotazamiwa kuendelea hadi 2050 (Kebede na wengine, 2019) — umepata nafasi kubwa katika mjadala ya umma Ulaya na kusababisha harakati nyingi za kisiasa. Picha za meli za wakimbizi katika Bahari ya Mediterranean zilizopakiwa wahamiaji Waafrika zimekuwa sura kuu katika vyombo vya habari vya Ulaya, sawa na picha kutoka Amerika ya Kati za wahamiaji katika mpaka wa Marekani na Mexico. Hata hivyo, maeneo mengine yanayoguswa na masuala ya uhamiaji na watu kufukuzwa kutoka makwao hutajwa mara moja moja na vyombo vya habari ulimwenguni, au hata kupuuziliwa mbali kabisa.

Wazungu wengi wamewahi kukumbana na tatizo la kulazimishwa kuhama makwao. Katika karne ya 20, Vita Vikuu vya Pili vilifurusha watu milioni 40 kutoka makwao na wakawa wakimbizi. Hata hivyo, leo hii masuala ya wahamiaji na wakimbizi yamekuwa yakizusha mabishano ya kimtazamo. Kipengele kikuu ni kwamba mataifa ya EU hayako tayari kufungulia watu wasio raia wa EU nafasi za kufanya kazi. Pamoja na kuimarishwa kwa vikwazo vya utoaji viza, maombi ya uhifadhi wa kisiasa ndiyo kwa muda mrefu imekuwa njia ya pekee ya kupata nafasi ya kazi katika nchi za EU kwa watu wasio na paspoti za Ulaya. Jambo hilo limezua utata na mjadala kuhusu sababu halisi

na hali ya wahamiaji na wakimbizi. Kufuatia tatizo la uhamiaji na wakimbizi la 2015, mataifa mengi ya Ulaya yamekumbwa na shida ya kuongezeka kwa kiwango cha raia wake kutoridhishwa na wahamiaji na wakimbizi, hali iliyozidishwa na ongezeko la waombaji wa hifadhi za kisiasa.

Chinyere Stella Okunna, Profesa katika Idara ya Mawasiliano ya Habari, Chuo Kikuu cha Nnamdi Azikiwe, Awka, Jimbo la Anambra, Nigeria:

“Kauli ya umma katika Nigeria kuhusu uhamiaji ni kwamba shughuli hiyo ni ya kujenga kwani uhamiaji huvutia wengi. Kusema kweli, Wanigeria huwaonea fahari (na hata kuwahusudu) na kuwapongeza watu wanaoondoka nchini. Wanigeria wanaweza kufanya juu chini kufadhili jamaa na marafiki waondoke nchini. Vivutio vyake ni mchanganyiko wa mambo tofauti, ikiwa ni pamoja hali ya kiuchumi, hadhi kubwa na fahari na mengineyo. Mbali na manufaa ya kiuchumi yaletwayo na kuhamia ‘malisho mabichi’, kuishi ama kusomea ng’ambo ni ishara ya hadhi ambayo hutafutwa na Wanigeria wengi. Wanigeria huhamia kote katika Afrika, hasa Afrika Kusini, Libya, Ghana na Togo. Ukweli ni kwamba Wanigeria huhamia kila nchi ulimwenguni, ikiwa ni pamoja na maeneo ya mbali na yasiyokalika ya dunia. Mtawanyiko huu wa kushangaza unaelezwa kikamilifu katika tamshi maarufu la kiutani kwamba ukienda katika nchi yoyote duniani na usimpate Mnigeria yeyote (hasa Wa-Igbo) toroka kutoka nchi hiyo haraka iwezekanavyo. Msukumo wa kuhama Nigeria kwenda kwingineko Afrika na katika mataifa mengine hauepukiki. Maendeleo katika Nigeria hayajafikia kiwango cha matarajio ya wengi.”¹⁷



Chanzo : Binafsi

Historia huathiri pia mitazamo ya wahamiaji na wakimbizi katika Ulaya (tazama Moduli 8). Uamuzi wa Ujerumani wa 2015 wa kufungua mipaka yake unahitaji kufasiriwa katika muktadha wa Vita Vikuu vya Pili wakati wa utawala wa Nazi ambapo mamilioni ya Wazungu waliuawa, wakalazimika kutoroka na kutafuta hifadhi mbali na kwao, na mamilioni ya Wajerumani wenyewe wakafukuzwa baada ya taifa hilo kupoteza Poland na Czechoslovakia zilizokuwa chini ya himaya yake. Kwa upande mwingine, kiini cha wasiwasi miongoni mwa nchi nyingi za CEE ni changamano ya vita na mapambano, historia, maendeleo ya kisiasa na utambulisho wa kitamaduni; nchi za CEE zilipoteza mamlaka ya kujitawala na kulazimishwa kujiunga na muungano wa Urusi baada ya 1945. Mitazamo tofauti kuhusu jinsi ya kukabiliana na changamoto ya uhamiaji na hifadhi ya kisiasa imeendelea kuzua taharuki miongoni mwa wanachama wa EU, hivyo basi kuakisi tofauti katika historia, utamaduni, mahitaji ya nguvukazi na takwimu za idadi ya watu kama vile kima cha umri, miongoni mwa masuala mengine. Suala la kurudisha wahamiaji na wakimbizi kwao¹⁸ ni mfano mwingine wa jinsi mitazamo ya umma na waandalizi wa sera katika Afrika na Ulaya inaweza kutofautiana (de Haas, 2009). Kwa upande mmoja, viongozi wengi wa

17 Kwa maelezo ya jumla kuhusu uhamiaji na uhamishwaji wa lazima kutoka au kuingia Nigeria, tazama ukurasa wa nchi katika tovuti ya data ya uhamiaji (Migration Data Portal, 2020c).

18 Tazama faharasa zilizopendekezwa katika Moduli 2 kwa ufafanuzi (IOM, 2019a; EMN, 2018): EMN (2018); IOM (2019a).

Afrika hujaribu kukwepa suala la raia wake kurudishwa nyumbani baada ya kunyimwa hifadhi na makao katika Ulaya; kwa mfano, hatua ya kuwataka wahamiaji na wakimbizi kurudi nyumbani inaweza kudhuru sifa ya kimataifa ya nchi husika na kuonekana kama jambo la fedheha kwa familia za Kiafrika ilhali uhamiaji ni wa faida kwao kutokana na pesa wanazotumiwa kutoka nje. Kwa upande mwingine, viongozi wa Ulaya wanashinikizwa na raia wao kuthibitisha uwezo wao kudhibiti uhamiaji ipasavyo (kurudi na kukubaliwa nyumbani ni kipengee muhimu cha Mapatano Mapya ya Tume ya Ulaya kuhusu Uhamiaji na Kimbilio za Salama, 2020, ya EU). Mifano ifuatayo huenda ikaeleza mtanziko huo: Mwaka 2018, afisi za mabalozi na wawakilishi wa kibalozzi wa Schengen katika Nigeria walishughulikia maombi karibu 90,000 ya viza na karibu 45,000 kati yake yakakataliwa na hivyo kuwa kima kikubwa zaidi cha takribani asilimia 50 cha maombi ya viza hiyo yaliyotupwa miongoni mwa mataifa yote ya yanayostawi (Schengen Visa Info, 2019; Schengen Visa News, 2020).



ZOEZI LILILOPENDEKEZWA KUSHUGHULIKIA STADI ZA MITAZAMO YA KIBINAFSI NA MAADILI ZA KUPOKEA:

Watu katika nchi yako wana mtazamo gani kuhusu wahamiaji na wakimbizi?

Lijadili swali hili darasani na ukusanye istilahi na maneno; unda wingu la maneno ya nchi yako au eneo – na upakie kwenye mtandao wetu www.mediaandmigration.com.

Mawingu mawili ya maneno (tazama Kielelezo 4 na 5) – Asili ya wingu la kwanza ni anwani 538 za makala za kielimu zilizochapishwa katika majarida saba ya kielimu kati ya 2015 na 2016, nalo la pili liliundwa kufuatia warsha yetu kwa wanahabari kutoka Ivory Coast – yanaweza kuwasaidia katika uandalizi wa mawingu yenu.

Kielelezo 4 : Wingu la neno ‘Uhamiaji’ kutoka kwa makala za kielimu

Kielelezo 5: Wingu la maneno lililoundwa na wanahabari kutoka Ivory Coast



Chanzo: McAuliffe et al. (2017, p. 106); Mack, J. (2018): Word Cloud: Migration.Ivory Coast.Kielelezo chetu

Muundo wa mwongozo

Licha ya masuala shinikizi kama vile mabadiliko ya hali ya anga na changamoto mpya kama mkurupuko wa ugonjwa wa Ebola ulioanza 2014 au janga la Uviko-19, huenda uhamiaji na watu kufukuzwa makwao zikatawala ushawishi wa kujenga hoja kwa ulimwengu katika karne hii. Tuki-tilia maanani sababu za kauli hiyo – zilizoelezwa katika Moduli 3 na kujadiliwa kwa kina katika uchanganuzi kifani (Moduli 6-8) – wataalamu wanatarajia idadi ya wahamiaji wa kimataifa na wakimbizi kubaki juu.¹⁹ Wanahabari na vyumba vya habari kote duniani watakabiliwa na changamoto ya kutafuta na kueleza habari za suala hili tatanishi na nyeti. Mkataba wa Ulimwengu wa Wahamiaji unanuia:

“Kuimarisha utoaji habari huru, usiopendelea na bora wa vyombo vya habari, ikiwa ni pamoja na habari inayoenezwa kwa Intaneti, kwa kuwahamasisha na kuwaelimisha wataalamu wa uanahabari kuhusu masuala ya uhamiaji na istilahi, kuwekeza kwa utoaji habari na matangazo ya biashara zinazozingatia viwango vya kimaadili [...], kwa heshima kamili ya uhuru wa vyombo vya habari” (UN, 2018, uk. 24, Objective 17, para 31(c)).

Mwongozo huu unanuia kuwasaidia walimu wa uanahabari kutayarisha kizazi kijacho cha wanahabari kwa kazi hii. Una thamani pia kwa wanahabari ambao tayari wanafanya kazi na juhudi za mafunzo kwa walio katika ngazi za katikati. Ingawa mwongozo unaakisi wahamiaji, wakimbizi na IDPs walio ndani na kati ya Afrika na Ulaya, una data na mifano kutoka maeneo mengine na muundo na nyenzo zake zinawaruhusu walimu wa uanahabari kuufanyia marekebisho ila kuzifaa changanuzi zao za kifani. Mwongozo unaangazia uhamiaji na watu kufukuzwa makwao katika vipengee vyake vyote. Ni lengo letu kuwahimiza walimu kuwatahadharisha wanafunzi wa uanahabari wakiwa majenti wa mabadiliko katika jamii zao — kuhusu ukweli kwamba sote ni lazima kwanza tuchunguze na kujaribu kuyaelewa kikamilifu masuala haya tatanishi kuhusu uhamiaji na uhamishwaji wa lazima. Ni kwa kufanya hivyo tu ambapo habari tunazotoa zinaweza kuwatendea haki wahamiaji, wakimbizi na IDPs, na pia watu katika mataifa asili na mwenyeji kwa utoaji wa habari zenye msingi wa maarifa, sahihi na dhahiri, za huruma, kitaalamu na haki.

Usimamizi kwa busara na kwa pamoja miongoni mwa washika dau wote wa safari za uhamiaji na uhamaji wa watu ni mbinu iwezayo kufanikisha kupunguzwa kwa hatari za maisha ya umasikini na matatizo kwa familia ya karibu na ya mbali; safari hizo zinaweza kunufaisha taifa asili pamoja na taifa mwenyeji. Uhamiaji sio mbinu ya pekee, na kwa wengi waliokufa, wakaoptea ama wahamiaji wasiotimiza kanuni²⁰, ulikuwa ni uamuzi mbaya ulioshia kwa majonzi.²¹ Uhamiaji

19 Ni vigumu kubashiri mieleleko ya siku zjazo kwa sababu ya uhaba wa data za uhamiaji na mara nyingi huwa si kamili, na mambo mengi yasiyotabirika huenda yakawasukuma watu kuvuka mipaka ya kimataifa ya nchi — mara nyingi kutokana na mabadiliko ya kasi ya ustawi wa kiuchumi, kijamii, kisiasa na kimazingira. Ubashiri wa Vollset na wengine (2020) kwa mwaka 2100 unaonyesha idadi kubwa zaidi ya wahamiaji inayotarajiwa katika Marekani, India, China, Somalia, Ufilipino na Afghanistan. Tovuti ya data za uhamiaji (Migration Data Portal (2020a) inahimiza “uandalizi mkubwa na uweza wa watu kufanya mabadiliko kwa kuweka mipango ya dharura kwa hali tofauti zinazoweza kutokea.”

20 Tazama faharasa zilizopendekewa katika Moduli 2 kwa ufafanuzi wa wahamiaji wasio wa kawaida: EMN (2018); IOM (2019a).

21 Kuokoa maisha na kuanzisha juhudi za kimataifa zinazosimamiwa ipasavyo kuhusu wahamiaji wasiojulikana walipo ni mojawapo ya shabaha 23 za Mkataba wa Ulimwengu kwa Wahamiaji.

usiozingatia kanuni hauwezi kufidia uksefu wa nafasi za kujiimarisha nyumbani. Maafikiano ya Uhamiaji Salama, kwa Mpango na Kanuni Ulimwenguni yanasisitiza hayo na malengo mengine. Miradi ya serikali na ya mashirika yasiyo ya serikali, ikiungwa mkono mara nyingine na mashirika ya ushirikiano wa maendeleo ya kimataifa, huenda ikawasaidia walimu, wavumbuzi, waumbaji na wajasiriamali katika nchi asili za wahamiaji.

Kwa mujibu wa Eric Chinje aliyekuwa rais wa African Media Initiative (AMI), ni nadra sana kwa vyombo vya habari katika Afrika kutoa taarifa za mafanikio ya Waafrika na badala yake hukariri habari za sura mbaya zisizo na usuli za mashirika ya habari ya kigeni. Ni wajibu wa kijamii wa vyombo vya habari kusawazisha habari zinazohitajika pakubwa zenye mifano ya kutia moyo, ambazo huenda zikawahimiza vijana kuepuka safari hatari za kwenda ng'ambo. Katika nchi mwenyeji, vyombo vya habari vinaweza kufanya mengi kueleza kuhusu watu wanaoingia humo, ikiwa ni pamoja na kukabiliana na dhana zinazokaririwa zisizo na msingi kwa lengo la kusisitiza utu wa wageni hao na kuonyesha manufaa ya jumla kwa uchumi wa nchi zinazokaribisha wageni hao, hasa ikitiliwa maanani kwamba idadi kubwa ya wenyeji ni wazee na hivyo basi kuna tatizo la kupata wafanya kazi. Tukishikilia uzi huo huo, mataifa mwenyeji yanaweza pia kuamua kuzingatia uanahabari unaosadia kujenga na kuleta ufumbuzi wa changamoto zinazohusishwa na wahamiaji na wakimbizi. Masuala hayo yanahusu wanadamu, wala sio mambo tu ya kuota, kama ilivyothibitishwa na mifano ya ripoti bora tulizokusanya kuhusu taarifa zilizotolewa.

- Moduli 2-5 zinachanganua ufafanuzi muhimu na taarifa kuu za kweli pamoja na athari za hali zinazosababisha mvuto na msukumo wa uhamiaji na watu kufukuzwa makwao kwa kutumia mifano kutoka Afrika na Ulaya. Uhaba wa nafasi za kujiendeleza, maendeleo ya kiuchumi, badiliko la hali ya anga, dhuluma za kisiasa na ufiisadi ni baadhi ya mambo ambayo yanasukuma watu kuhama nchi zao, ilhali usalama, nafasi za kazi, elimu, uwezo wa kupata mapato ya kupeleka nyumbani hatimaye, na miradi ya maslahi ya jamii ndivyo vivutio vikuu katika mataifa yanayokaribisha wahamiaji na wakimbizi. Moduli zinaakisi pia wajibu wa vyombo vya habari katika kutoa taarifa za wahamiaji na wakimbizi.
- Moduli 6-9 zinatumia changanuzi kifani na mitazamo kutoka Afrika na Ulaya kufafanua nadharia na mifano modeli.
- Moduli 10-13 zinatumia maarifa ya kimsingi yaliyopatikana kufikia sasa ili kuelimisha washirika umuhimu wa kuhakikisha masuala ya uhamiaji na wakimbizi yanasimuliwa kwa taarifa za habari kamili na pana, zinazovutia na kuzingatia maadili. Moduli hizo zinatoa mifano ya utendaji kazi bora wa kukusanya na kutoa habari kutoka kote ulimwenguni, kuwafahamisha washirika kuhusu asili na mbinu za kuripoti, na kutoa maelekezo kuhusu maadili. Itakiandaa pia kizazi kipya cha vijana wanahabari ambao watashirikiana na timu zingine katika mataifa mbali mbali



**ZOEZI LILIOPENDEKEZWA KUSHUGHULIKIA STADI ZA UTAMBUZI ZA KU-
CHAMBUA NA STADI ZA MITAZAMO YA KIBINAFSI NA MAADILI ZA KUJIBU:**

Usikize wimbo “Emigrason Clandestino” wa mwanarap Abdul Embalo kutoka Guinea-Bissau, ambaye alifanya safari ya kutamausha kisha akarudi nyumbani. Utaupata wimbo huo katika www.mediaandmigration.com.

Tambulisha vifaa kuhusu uhamiaji na uhamishwaji wa lazima vilivyotayarishwa na wasanii wa eneo lako na mjadili mkiangazia maswali kutokana na ujumbe wake mkuu kuhusu wahamiaji na wakimbizi na athari zake kwa hadhara za wasanii hao.



**ILIYOPENDEKEZWA KUSHUGHULIKIA STADI ZA UTAMBUZI ZA
KUTEKELEZA NA STADI ZA MITAZAMO NA MAADILI ZA KUJIBU:**

Mtaalamu wa masuala ya kisiasa Ivan Krastev (2018) amechanganua safari za uhamiaji na uhamaji na kuitaja kuwa mapinduzi ya karne ya 21: “Haiongozwi na itikadi lakini na ramani za Google. Ukitaka kubadilisha maisha yako, si uamuzi wa busara kubadilisha serikali. Badala yake unabadilisha nchi unamoishi.”

Andika ripoti na taarifa ya maoni (kwa angalau herufi 5,000) kuhusu dai hili ambayo huenda ikachapishwa na gazeti la kitaifa: Je, kuna ushahidi wa mapinduzi haya kufanyika katika nchi yako au la? Safari za uhamiaji na uhamaji wa watu zina athari gani kwa nchi yako na nchi nyingine husika? Unaonaje kuhusu taarifa hiyo na kwa nini? Inawezekana kuwa hatari wakati mwingine kujitahidi kuleta mabadiliko nyumbani au ni jambo la busara kuhama? Je, watu huwa na hiari ya kuamua wakati wote?



USOMAJI WA ZIADA:

Kiakademia:

McAdam, J. (2018). The Global Compacts on Refugees and Migration: A new era for international protection? *International Journal of Refugee Law*, 30(4), 571-574.

Kiuanahabari:

Anyadike, O. (2015). Since you’ve been gone. The families migrants leave behind: IRIN Special Feature: Nigeria to Morocco and Gambia to Italy. Retrieved November 26, 2020, from <http://newirin.irinnews.org/special-feature-since-youve-been-gone>

Krastev, I. (2018). Flüchtlinge und Migranten sind die wahren Revolutionäre unserer Zeit. Retrieved November 26, 2020, from <https://www.nzz.ch/meinung/revolution-ist-nicht-laenger-ein-sprung-in-der-zeit-sondern-eine-bewegung-im-raum-ld.1351218>

Kitaasisi:

UNDESA (2019a). International Migration 2019: Report. New York. Retrieved November 16, 2020, from https://www.un.org/en/development/desa/population/migration/publications/migrationreport/docs/InternationalMigration2019_Report.Pdf

Marejeleo

ADB (2018). Asian economic integration Report 2018: Toward optimal provision of regional public goods in Asia and the Pacific. Manila. Retrieved December 15, 2020, from <https://www.adb.org/sites/default/files/publication/456491/aeir-2018.pdf>

African Development Bank Group (2011). Leveraging migration for Africa remittances, skills, and investments. Washington, D.C. Retrieved December 19, 2020, from <https://www.afdb.org/fileadmin/uploads/afdb/Documents/Generic-Documents/Leveraging%20Migration-P4-rev-3.31.2011.pdf>

African Union (2018). Protocol to the treaty establishing the African Economic Community relating to free movement of persons, right of residence and right of establishment. Retrieved January 5, 2021, from https://au.int/sites/default/files/treaties/36403-treaty-protocol_on_free_movement_of_persons_in_africa_e.pdf

Anyadike, O. (2015). Since you've been gone. The families migrants leave behind: IRIN Special Feature: Nigeria to Morocco and Gambia to Italy. Retrieved from <http://newirin.irinnews.org/special-feature-since-youve-been-gone>

De Haas, H. (2009). The Myth of Invasion: The inconvenient realities of African migration to Europe. *Third World Quarterly*, 29(7), 1305-1322.

Earthtime, & UNHCR (2019): Global Refugee Crisis: The big picture. Retrieved January 25, 2021, from https://earthtime.org/stories/global_refugee_crisis_the_big_picture

EMN (2018). Asylum and migration: Glossary 6.0. European Migration Network. Retrieved December 15, 2020, from https://www.emn.at/wp-content/uploads/2018/06/emn-glossary-6-0_en.pdf

European Commission (2018). Special Eurobarometer 469: Integration of immigrants in the European Union. Brussels. Retrieved September 23, 2020, from https://ec.europa.eu/home-affairs/news/results-special-eurobarometer-integration-immigrants-european-union_en

European Commission (2020). New Pact on migration and asylum: Communication from the Commission to the European Parliament, the Council, the European Economic and Social Committee and the Committee of the Regions. Brussels. Retrieved December 19, 2020, from European Commission website: https://ec.europa.eu/info/sites/info/files/1_en_act_part1_v7_1.pdf

Ferris, E. E., & Martin, F. S. (2019). Introduction to the Special Issue “The Global Compact for safe, orderly and regular migration and The Global Compact on refugees. *International Migration*, 57(6), 5-18.

Gest, J., Kysel, I. M., & Wong, T. K. (2019). Protecting and Benchmarking Migrants' Rights: An Analysis of the Global Compact for Safe, Orderly and Regular Migration. *International Migration*, 57(6), 60-79.

- Grandi, F. (2019). The Global Compact on Refugees: A historic achievement. *International Migration*, 57(6), 23-26. <https://doi.org/10.1111/imig.12671>
- ILO (n. d.). Regional Economic Communities (RECs) – Work on the free movement of persons and labour migration (Africa). Retrieved September 23, 2020, from <https://www.ilo.org/africa/areas-of-work/labour-migration/economic-communities/lang--en/index.htm>
- IOM (2019a). Glossary on Migration. Geneva. Retrieved December 15, 2020, from https://publications.iom.int/system/files/pdf/iml_34_glossary.pdf
- IOM (2019b). World Migration Report 2020. Retrieved November 30, 2019, from https://publications.iom.int/system/files/pdf/wmr_2020.pdf
- Kebede, E., Goujon, A., & Lutz, W. (2019). Stalls in Africa's fertility decline partly result from disruptions in female education. *Proceedings of the National Academy of Sciences of the United States of America*, 116(8), 2891-2896. <https://doi.org/10.1073/pnas.1717288116>
- Koch, A., Weber, A., & Werenfels, I. (2018). Profiteers of Migration? – Authoritarian States in Africa and European Migration Management. Berlin. Retrieved December 19, 2020, from https://www.swp-berlin.org/fileadmin/contents/products/research_papers/2018RP04_koh_et_al.pdf
- Krastev, I. (2018). Flüchtlinge und Migranten sind die wahren Revolutionäre unserer Zeit. Retrieved November 26, 2020, from <https://www.nzz.ch/meinung/revolution-ist-nicht-laenger-ein-sprung-in-der-zeit-sondern-eine-bewegung-im-raum Id.1351218>
- Lambert, H., Gupte, J., Fletcher, H., Hammond, L., Lowe, N., Pelling, M., Raina, N., Shahid, T., & Shanks, K. (2020). COVID-19 as a global challenge: Towards an inclusive and sustainable future. *The Lancet Planetary Health*, 4(8), e312-e314. [https://doi.org/10.1016/S2542-5196\(20\)30168-6](https://doi.org/10.1016/S2542-5196(20)30168-6)
- Lehne, S. (2016). How the refugee crisis will reshape the EU. Retrieved September 29, 2020, from <https://carnegieeurope.eu/2016/02/04/how-refugee-crisis-will-reshape-eu-pub-62650>
- Mack, J. (2018). Word Cloud: Migration. Ivory Coast. Internal document.
- Marfaing, L. (2016). Nicht nur "Armutsflüchtlinge"! Mobilität von Migrant/inn/en in Westafrika und von afrikanischen Unternehmern als Entwicklungspotenzial. *Journalism in a Global Context (JIGC)*. Dortmund. Retrieved December 18, 2020, from <https://en.ejo.ch/?s=Nicht+nur+%22Armutsf%C3%BCchtlinge%22%21+Mobilit%C3%A4t+von+Migrant%2Finn+%2Fen+in+Westafrika+und+von+afrikanischen+>
- McAdam, J. (2018). The Global Compacts on Refugees and Migration: A new era for international protection? *International Journal of Refugee Law*, 30(4), 571-574.
- McAuliffe, M., Pedrotti, M., & Weerasinghe, S. (2017). Migration research and analysis: Growth, reach and recent contributions. In *World Migration Report 2018* (pp. 95-121). Geneva: IOM.
- Migration Data Portal (2020a). Future migration trends. Retrieved September 24, 2020, from <https://migrationdataportal.org/themes/future-migration-trends>
- Migration Data Portal (2020b). Migration Data Portal: The bigger picture. Retrieved August 20, 2020, from https://migrationdataportal.org/?i=stock_abs_&t=2019
- Migration Data Portal (2020c). Nigeria. Retrieved September 25, 2020, from https://migrationdataportal.org/?i=stock_abs_&t=2019&cm49=566
- Plaza, S., & Ratha, D. (2011). Diaspora for development in Africa. Washington, D.C. Retrieved December 19, 2020, from World Bank website: <https://www.knomad.org/publication/diaspora-development-africa>
- Robinson, A. L. (2016). Nationalism and ethnic-based trust: Evidence from an African border region. *Comparative Political Studies*, 49(14), 1819-1854.

Sanchez, G., Hoxhaj, R., Nardin, S., Geddes, A., & na wengine (2018). A study of the communication channels used by migrants and asylum seekers in Italy, with a particular focus on online and social media. Retrieved December 29, 2020, from <https://op.europa.eu/en/publication-detail/-/publication/2af2973d-48fc-11e8-be1d-01aa75ed71a1/language-en>

Schengen Visa Info (2019). Country-specific Schengen visa statistics. Retrieved September 24, 2020, from <https://statistics.schengenvisainfo.com/>

Schengen Visa News (2020). EU plans to impose visa restrictions on Nigerians. Retrieved September 24, 2020, from <https://www.schengenvisainfo.com/news/eu-plans-to-impose-visa-restrictions-on-nigerians/>

UN (2018). Global Compact for Safe, Orderly and Regular Migration: Intergovernmentally negotiated and agreed outcome. Retrieved July 6, 2020, from https://refugeesmigrants.un.org/sites/default/files/180713_agreed_outcome_global_compact_for_migration.pdf

UN (2020). Refugees and Migrants: Global Compact for Migration / Global Compact on Refugees. Retrieved April 11, 2020, from <https://refugeesmigrants.un.org/>

UN General Assembly (2016). New York Declaration for Refugees and Migrants: Resolution adopted by the General Assembly on 19 September 2016. Retrieved December 20, 2020, from http://www.un.org/en/development/desa/population/migration/generalassembly/docs/globalcompact/A_RES_71_1.pdf

UN General Assembly (2018a). Global Compact for Safe, Orderly and Regular Migration: Resolution adopted by the General Assembly on 19 December 2018. Retrieved December 20, 2020, from https://www.un.org/en/ga/search/view_doc.asp?symbol=A/RES/73/195

UN General Assembly (2018b). Global Compact on Refugees: Report of the United Nations High Commissioner for Refugees. Retrieved December 20, 2020, from https://www.unhcr.org/gcr/GCR_English.pdf

UN Network on Migration (n. d.). The Global Compact for Migration: Well governed migration as an essential element of effective Covid19 response. Retrieved December 20, 2020, from https://migrationnetwork.un.org/sites/default/files/docs/policy_brief_-_gcm_and_well_governed_migration_as_an_essential_element_of_effective_covid-19_response.pdf

UN News (2018): General Assembly endorses landmark global Compact on Refugees. Retrieved January 25, 2021, from <https://www.un.org/press/en/2018/ga12107.doc.htm>

UNDESA (n. d.). Definition of regions. Retrieved September 5, 2020, from <https://population.un.org/wpp/DefinitionOfRegions/>

UNDESA (2019a). International Migration 2019: Report. New York. Retrieved December 20, 2020, from https://www.un.org/en/development/desa/population/migration/publications/migrationreport/docs/International-Migration2019_Report.pdf

UNDESA (2019b). Population Facts 2019: International migrants numbered 272 million in 2019, continuing an upward trend in all major world regions. New York. Retrieved November 17, 2020, from https://www.un.org/en/development/desa/population/migration/publications/populationfacts/docs/MigrationStock2019_Pop-Facts_2019-04.pdf

UNHCR (n. d.). Glossary. Retrieved December 19, 2020, from <http://www.issm.cnr.it/progetti/emigrazione/METADATA%20E%20GLOSSARI/UNHCR/GLOSSARY%20UNHCR.pdf>

UNHCR (2016). Refugee or Migrant? Word choice matters: UNHCR viewpoint: 'Refugee' or 'migrant' – Which is right? The two terms have distinct and different meanings, and confusing them leads to problems for both populations. Retrieved November 26, 2020, from <http://www.unhcr.org/news/latest/2016/7/55df0e556/unhcr-viewpoint-refugee-migrant-right.html>

UNHCR (2020a). Global Trends: Forced displacement in 2019. Copenhagen. Retrieved December 19, 2020, from UNHCR website: <https://www.unhcr.org/5ee200e37.pdf>

UNHCR (2020b). The role of the Global Compact on Refugees in the international response to the COVID-19 pan-demic. Retrieved September 29, 2020, from <https://globalcompactrefugees.org/article/role-global-compact-refugees-international-response-covid-19-pandemic>

UNRWA (n. d.). Palestine refugees. Retrieved December 20, 2020, from <https://www.unrwa.org/palestine-refugees>

Vollset, S. E., Goren, E., Yuan, C.-W., Cao, J., Smith, A. E., Hsiao, T., Bisignano, C., Azhar, G., Castro, E., Chalek, J., Dolgert, A., Frank, T., Fukutaki, K., Hay, S., Lozano, R., Mokdad, A., Nandakumar, V., Pierce, M., Pletcher, M., Robalik, T., Steuben, K., Wunrow, H., Zlavog, B., & Murray, C. J. L. (2020). Fertility, mortality, migration, and population scenarios for 195 countries and territories from 2017 to 2100: A forecasting analysis for the Global Burden of Disease Study. *The Lancet*. Advance online publication. [https://doi.org/10.1016/S0140-6736\(20\)30677-2](https://doi.org/10.1016/S0140-6736(20)30677-2)

World Bank (n. d.). Country and lending groups: World Bank Data, Help Desk. Retrieved July 6, 2020, from <https://datahelpdesk.worldbank.org/knowledgebase/articles/906519>



MODULI 2

Vyanzo muhimu, mambo muhimu, istilahi muhimu na takwimu

na Monika Lengauer



MALENGO YA MODULI

- Kuamua ni ufafanuzi gani wa maneno muhimu ya kutumia na kwa nini.
- Kuainisha wahusika wakuu katika uhamiaji na uhamishwaji wa kulazimishwa.
- Kuthibitisha vyanzo vya kuaminika vya data na kufanya mazoezi ya jinsi ya kuvitumia.



MATOKEO YA MAFUNZO

Kufikia mwisho wa moduli hii, washiriki wanapaswa kuwa na uwezo wa:

- Kuelezea umuhimu wa kutumia vyanzo vya kuaminika kwa data na ufafanuzi → **Matokeo ya mafunzo kwa mitazamo binafsi na maadili: Kupokea**
- Kujadili maana ya matumizi tofauti ya istilahi muhimu. → **Matokeo ya mafunzo kwa mitazamo binafsi na maadili: Kujibu**
- Kueleza ni nani huathiri uhamiaji na uhamishwaji wa kulazimishwa. → **Matokeo ya mafunzo kwa utambuzi: Kuelewa**
- Kuchagua na kutumia ipasavyo ufafanuzi na data muhimu. → **Matokeo ya mafunzo kwa utambuzi: Kutumia**
- Kuchunguza watendaji wakuu na mashirika katika bidhaa za vyombo vya habari. → **Matokeo ya mafunzo kwa utambuzi: Kuchanganua**

Muhtasari

Maneno lazima yaeleweke, data ziaminike, vyanzo vya uwazi na watendaji wanaojitambua na wanaofahamu mitazamo, itikeli na upendelevu wao — hii ni sehemu ya ruwaza ya mwongozo huu kwa mijadala ya umma kuhusu uhamiaji na uhamaji wa watu. Wanahabari, wanahabari watara-jiwa, walimu wa uanahabari na wakuzaji mitaala wana jukumu la kuchukua maamuzi ya kielimu juu ya ufafanuzi, data na vyanzo wanavyotumia na hivyo kuvieneza.

Lengo la moduli hii ni kuwasaidia kuelekeza ubora wa mjadala wa umma. Tunatambulisha wahu-sika wanaoathiri uhamaji wa kulazimishwa; kujadili fasili na kufichua jinsi fasili hizi zinavyohu-siana na data; kusesitiza vyanzo vinavyokusanya na kusambaza data; kusambaza data ambazo zilikusanywa na kuwasilishwa kwa mbinu za uwazi na zinazokubalika kufanyiwa uchanganuzi wa kitaaluma na kukaguliwa kwa makini na umma; na zielekezwe kwenye programu-tumizi na vifaa vinavyoonyesha utafiti. Matumaini ya moduli hii ni kuwawezesha watumiaji kufanya maamuzi sahihi kuhusu vyanzo, data na ufafanuzi wanaotumia. Hili pia litawezesha ukuzaji wa mtaala na kuchochea muundo wa moduli mahususi za nchi za kuripoti masuala ya wahamiaji na wakimbizi kwa kuwa vyanzo vinavyopendekezwa hapa vinaruhusu utangamano unaofaa na tafiti maalumu.

Vyanzo vya data vilivyochaguliwa

Wanahabari wanaoripoti masuala ya uhamiaji na uhamaji wa kulazimishwa mara kwa mara wanakabiliwa na ukosefu wa data kwa upande mmoja na msururu wa watoa data kwa upande mwingine. Ni vigumu kukadiria thamani ya vyanzo vya data na kutumia data hizo kwa tathmini huru. Hadi sasa, licha ya mipango mingi ya kimataifa ya kuboresha ukusanyaji na ulinganifu wa data, mifumo mingi ya kitaifa ya kukusanya data bado haijatarishwa vizuri kukusanya taarifa za kina (UN, 2020). Vyanzo mbalimbali hukusanya na kusambaza data katika ngazi za kitaifa na kimataifa (ofisi za kitaifa za takwimu kwa mfano kupitia sensa au sajili za idadi ya watu). Sababu za ukosefu mkubwa wa data ya thamani ni nyingi. Kuna changamoto za baadhi ya malengo, kwa mfano maswali yote yanayohusiana na ufafanuzi: Mhamiaji na mhamaji ni nani? Mkimbizi ni nani? Je, wanatofautiana, au la? Uhamiaji, kama alivyoangazia Zlotnick (1987), bila shaka ni jambo gumu zaidi la kidemografia kupima kwa sababu — tofauti na vifo na uzazi — halihusiani na tukio linaloonekana la kibaiolojia. Mtoto anazaliwa mara moja, na bila shaka ni mtoto mchanga, ambaye ni mhamiaji, na ni mara ngapi anahama, na je, yeye huhama kila mara au yeye ni mkimbizi kwa wakati fulani? Kuna mifano mingi kutoka katika kanda na nchi kote ulimwenguni ambayo inakuza changamoto. Tuchukue mfano wa Afrika. Kinyume na matukio ya mara moja katika maisha kama vile kuzaliwa na kifo — na hata hapa, takwimu muhimu katika nchi kadhaa barani Afrika zinatia wasiwasi mkubwa (Sankoh na wengine, 2020) — uhamiaji ni suala tata zaidi, labda hufanyika mara kwa mara, na hata lisiloleweka sana. Oucho (1998, uk. 89) anaeleza kuwa nchi za “Afrika za kusini ya Jangwa la Sahara zinadhihirisha mfano mwema wa kuchunguza [...] tatizo la upungufu wa data” kuhusu uhamiaji na uhamaji wa watu wa ndani kwa ndani, katika kanda na kimataifa. Kwa sasa, Mkataba wa Dunia wa Uhamiaji umepewa jukumu la kutoa data linganifu kwa njia za kina na unaangazia haja ya kukusanya na kuwasilisha data za kuaminika, zinazoweza kulinganishwa na kwa wakati unaofaa (UN, 2020).

Walimu wa uanahabari mara nyingi hujitolea kuwaongoza wanafunzi wao kupata data mwanzo kabisa kutoka kwa vyanzo vya kuaminika na vyenye mamlaka — hali ambayo ni ngumu katika uhamiaji na uhamaji wa kulazimishwa kwa sababu ukusanyaji wa data sio tu suala tatanishi na liwezalo kubadilika wakati wowote, bali pia la gharama kubwa sana, hasa wakati data inayohitajika ni radidi, inayotokezea mara kwa mara na iliyo na ulinganisho wa kimataifa. Inapowezezana, mwongozo huu unarejelea vyanzo rasmi vya data, vinavyoaminika na vya kitaaluma (IMI, 2020) au vyanzo mseto (Our World in Data, 2020).¹

Kwa sababu wanafunzi wa uanahabari na wanahabari wazoefu wanahitaji ufikiaji wa haraka wa data ya kuaminika na kwa wakati unaofaa, mwongozo huu unapendekeza kutumia data kutoka kwa vyanzo ambavyo:

1 Our World in Data ni juhudi shirikishi kati ya watafiti katika Chuo Kikuu cha Oxford, ambao ni wahariri wa kisayansi wa machapisho ya tovuti; na shirika lisilo la faida la Global Change Data Lab, ambalo huchapisha na kudumisha tovuti na zana za data. Tazama Oxford Martin Programme on Global Development (Our World in Data, 2020).

(1) vinaaminika ipasavyo kulingana na majukumu yao ya kukusanya na kusambaza data, na kwa kuzingatia mbinu zao ambazo ni wazi na zinazoweza kuchunguzwa kitaaluma na hata na umma;

(2) vilivyo na wajibu wa kutoa data ambayo ni muhimu, sahihi, ya sasa na inayojirudia mara kwa mara, radidi, inayoweza kulinganishwa kimataifa na inayolingana kimataifa, iliyoainishwa kwa jinsia na umri, iliyothibitishwa, na ambayo hupatikana katika chanzo huria, kwa urahisi na kueleweka wazi wazi;

(3) ikiwezekana pia ionyeshe jinsi ya kupiga taswira ya data ili kuwezesha utafiti linganishi wa uanahabari wa kimataifa katika viashirio vya viwango vilivyotanuka.

Hazinadata zilizoratibiwa ambazo hazifikii viwango hivi hazipendekezwi (Buneman na wengine, 2009). Mwongozo huu unapendekeza tovuti ya Data Migration Portal (2020a; 2020d) kama sehemu ya kwanza ya kufikia utafiti wa data. Katika lugha nne (Kiingereza, Kihispania, Kifaransa na Kijerumani) tovuti hii inaangazia wanahabari na umma kwa jumla, inasimamiwa na International Organisation for Migration (IOM) na kuungwa mkono na serikali mbali mbali (kwa mfano Marekani, Ujerumani, Uswizi). Ni kituo cha jumla cha data kutoka kwa vyanzo vya kuaminika na vilivyo na mamlaka vya kimataifa vilivyoidhinishwa na kutambuliwa rasmi (UN Statistical Commission, 2020; UNSD, 2020a).²Vyanzo vingine ni pamoja na:

- Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia takwimu (United Nations Statistics Division - UNSD) hukusanya na kusambaza data rasmi ya kitaifa kuhusu mtiririko na hifadhi za wahamiaji wa kimataifa.³Mkusanyiko wa data wa Kitabu cha Kila Mwaka cha Demografia cha UNSD na Kitabu chake cha Kila Mwaka cha Takwimu ni vyanzo maridhawa vya data mbalimbali kwa nchi na maeneo yote (UNSD, 2020b; UNSD, 2020c)
- Shirika linaloshughulikia masuala ya idadi ya watu la Umoja wa Mataifa (United Nations Population Division - UNPD) hutayarisha makadirio ya idadi za wahamiaji kwa kila nchi kwa kutumia data iliyotolewa na UNSD, na takwimu zake za kila mwaka husaidia sana kulinganisha nyakati, katika mabara na nchi zote (UNDESA, 2019a; UNDESA 2019b) .
- Shirika la Wafanyakazi Duniani (ILO) hukusanya na kuweka pamoja takwimu za uhamiaji wa kimataifa wa wafanyakazi (ILO, 2020).
- Shirika la Umoja wa Mataifa la kuhudumia wakimbizi (UNHCR) linakusanya na kuweka pamoja data kuhusu wakimbizi, wanaotafuta hifadhi, wakimbizi wa ndani kwa ndani (IDPs), watu wasio na utaifa na “watu wengine wanaohusiana na makundi haya” (UNHCR, 2020b ; tazama Kielelezo 6).

2 Tume ya Takwimu ya Umoja wa Mataifa ndiyo chombo cha juu zaidi cha mfumo wa takwimu wa kimataifa kinacholeta pamoja wakuu wa takwimu kutoka nchi wanachama wa Umoja wa Mataifa kutoka kote duniani. Ni kiungo cha juu zaidi cha kufanya maamuzi kwa shughuli za kimataifa za takwimu, na husimamia kazi ya UNSD.

3 Ufafanuzi wa makundi ya wahamiaji na mtiririko wa wahamiaji: Tazama faharasa zinazopendekezwa na mwongozo huu: IOM (2019a); EMN (2018).

- IOM hukusanya, kutumia, kuchanganua na kuchapisha data za mada mbalimbali za uhamiaji (Migration Data Portal, 2019a).
- Shirika la Umoja wa Mataifa linalotoa misaada kwa wakimbizi wa Palestina (UNRWA) hutoa takwimu kuhusu wakimbizi Wapalestina (UNRWA, 2019)
- Hazinadata ya Viashiria vya Maendeleo ya Dunia (WDI) ya Benki ya Dunia ni mkusanyo wa takwimu zinazoweza kulinganishwa baina ya mataifa mbalimbali kuhusu maendeleo ya kima-taifa na mapambano dhidi ya umaskini. Hupatikana katika lugha kadhaa zikiwemo Kiarabu, Kirusi na Kireno (Benki ya Dunia, 2019).


Mifano ya mwelekeo wa kikanda ni Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) yenye takwimu zake za Afrika katika vitabu vya kila mwaka (AfDB na wengine, 2019; AfDB, 2020). Ofisi ya Takwimu ya EU (Eurostat) ina jukumu la kukusanya na kusambaza data (Eurostat, 2019).

Ukusanyaji wa data unajumuisha vyanzo vyote vinavyopatikana, ikijumuisha wachunguzi maalumu nyanjani na ripoti za vyombo vya habari, zinazotumwa kwa mfano na kituo kinachojihusi-sha na uhamiaji wa ndani wa kulazimishwa — Internal Displacement Monitoring Centre (IDMC, 2019, uk. 9, 13, 19).

Data imekusanywa kwa hali ngumu sana wakati wa Uviko-19, zikiwemo sheria za watu kutokaribiana, wakati wahamiaji na wengine wamekwama kwenye mipaka iliyofungwa au kufungiwa kwenye vituo vya mapokezi, haki zao mara nyingi zimeathiriwa kwa njia isiyo sawa. Data sahihi na kwa wakati ufaao ni muhimu zaidi katika hali hizi, ili kuelewa athari za janga hili, kupanga afua na kuhifadhi maisha (UN Network on Immigration, n. d.; UNHCR, 2020c).

Kwa kuzingatia utofauti wa mashirika ya kukusanya data na makundi lengwa, haishangazi kwamba data si lazima zifanane. Taasisi mara nyingi hukusanya data ili kuafikia malengo yao wenyewe. Wao hutumia maelezo tofauti, mitindo na vigezo tofauti hivyo basi inakuwa vigumu kusambaza, kulinganisha na kuchanganua data kwa pamoja (UNHCR, 2016a, uk. 40). Kwa mfano, IOM hufuatilia “watu waliohamishwa”, na UNHCR hukusanya data kuhusu “watu waliohamishwa kwa lazima” — hatua hizi mbili zina maana tofauti na haziwezi kutumika kama njia mbadala. Kwa UNHCR, watu waliohamishwa kwa lazima kimsingi wanajumuisha wakimbizi, wanaotafuta hifadhi na kundi fulani la wakimbizi wa ndani (UNHCR, 2019, uk. 63). Wakimbizi wa Kipalestina mara nyingi hujumuishwa, ingawa si kila mara, miongoni mwa wahamiaji wa kulazimishwa (UNHCR, 2020d, uk. 2; Benki ya Dunia, 2017, uk. 15-16, Annex A, uk. 34-35).

Kielelezo 6: Watu milioni 79.5 walilazimishwa kuhama makwao kote duniani mwishoni mwa 2019



*Wakimbizi milioni 20.4 walio chini ya mamlaka ya UNHCR; Wapalestina wakimbizi milioni 5.6 wanaoshughulikiwa na UNRWA

**Chanzo: IDMC

Makundi kadhaa ya watu waliohamishwa kwa lazima yako chini ya utunzaji wa UNHCR na wao ni pamoja na wakimbizi, wakimbizi wa ndani (IDPs), waombaji hifadhi na watu wasio na uraia (data iliyo hapa juu ni ya Juni 2020, 18). UNHCR hukusanya data kuhusu watu hao wanaohitaji kushughulikiwa. Wakimbizi Wapalestina wako chini ya mamlaka ya UNRWA. Chanzo: UNHCR (2020d, p. 2). Kielelezo chetu.



ZOEZI LILIOPENDEKEZWA LA KUSHUGHULIKIA STADI ZA UTAMBUZI ZA UELEWA, STADI ZA MITAZAMO YA KIBINAFSI NA MAADILI ZA KUPOKEA NA STADI ZA UTENDAJI ZA KUSTAWISHA USAHIHI:

Kwa nini takwimu hazifanani?

Wagawe washiriki katika vikundi viwili.

Kundi 1 litajishughulisha na watu waliohamishwa na kufuatiliwa na DTM ya IOM. Kwa mfano: Kufikia Oktoba 2020, DTM ikinukuu IDMC ilionyesha kuwa watu milioni 25,064,734 waliohamishwa. DTM pia inaonyesha watu milioni 37,564,555 waliohamishwa kutokana na migogoro na vurugu kufikia Desemba 2019 (IOM DTM, 2020).

Kundi 2 litajishughulisha na watu waliohamishwa kwa lazima na kuchunguza data iliyotolewa na UNHCR: Watu milioni 79.5 walilazimika kutoroka makazi yao duniani kote mwishoni mwa 2019 (UNHCR, 2020b).

Vikundi vyote viwili vitasahihisha kwanza takwimu zilizotajwa hapo juu ili ziifikiane na za hivi karibuni. Kisha watatafiti kile takwimu hutuambia, kwa kutumia vyanzo vilivyotolewa hapo juu:

- Nini madhumuni na upeo wa zoezi la kukusanya data?
- Ni muda gani wa matukio ulioangaziwa?
- Je, data ilikusanywa vipi (kwa mfano, watafiti nyanjani walijumuishwa au ripoti za vyombo vya habari)?

Taarifa kuhusu watu waliowakilishwa katika takwimu hizo inaweza kujumuisha:

- Tabia za wahamiaji na wahamaji, kwa mfano wasifu wao kidemografia kama umri, jinsia, hali ya kiuchumi, mafanikio ya elimu na mengineyo.
- Iwapo walikuwa wakisafiri peke yao au na familia.
- Vikundi vya watu waliohesabiwa, kwa mfano wakimbizi, wafanyakazi wahamiaji, watoto wasioandamana na watu wazima na waliotenganishwa, wanawake, wahanga wa ulanguzi wa binadamu au watu kutoka nchi fulani ya asili au watu wanaoelekea sehemu fulani au kutumia njia fulani za uhamiaji na mengineyo.
- Hatari kwa usalama wao.

Wawasilishe ripoti fupi wakitumia Powerpoint ili kutoa mwanga juu ya hadithi ambazo takwimu hizi husimulia. Wakijadili mawasilisho hayo mawili, washiriki watachunguza kwa nini idadi ya watu waliohamishwa inayotolewa na IOM hailingani na ile ya watu waliohamishwa kwa lazima ambayo shirika jingine la kimataifa (UNHCR) limechapisha.

Wakati wa kujadili ufafanuzi katika sehemu inayofuata, itadhihirika kwamba fani bado haina ufafanuzi unaokubalika na wote wa neno muhimu - wahamiaji - ambalo baadaye linazuia ulinganisho na uchanganuzi wa data.

Wakati wa kutayarisha changanuzi za kifani za nchi, vyanzo vilivyoidhinishwa vinapatikana pia kwa data husika inayofungamana na wakati mahususi wa nchi na inayolingana kimataifa. Mbali na vyanzo vilivyotajwa hapo juu, mashirika yafuatayo yanaweza kuwa muhimu: UNdata (2020), ripoti za maendeleo ya watu ya UNDP (HDR; UNDP, n. d.; UNDP, 2019), UNESCO yenye data ya elimu (UNESCO & UIS, 2020), kutaja tu machache. Baadhi hutoa uchanganuzi wa data, kwa mfano kuhusu mabadiliko ya idadi ya watu na maendeleo endelevu (Berlin Institute for Population and Development, 2020), mwegemeo wa kidini (Pew Research Center & John Templeton Foundation, 2016) na wengineo. Tukikumbuka kwamba ramani “kama vile hotuba na michoro, ni mkusanyo wa habari ulioandikwa, unaoweza kupotoshwa” (Monmonier, 2018), mwongozo huu unapendekeza kushauriana na kitengo cha habari cha UN Geospatial Information Section (2019) kila inapowezekana.

Istilahi muhimu - kutofautisha wahamiaji na wakimbizi

Istilahi mbili muhimu katika mjadala huu ni wahamiaji na wakimbizi pamoja na suala maalumu la wakimbizi wa Kipalestina ambalo halitafafanuliwa zaidi katika hatua hii kwa masuala ya uwazi wa istilahi mbili muhimu. Tafakari zifuatazo zinalenga kuelewa istilahi hizo mbili kwa kuangazia tofauti kati ya wahamiaji na wakimbizi. Kumbuka kwamba tunapoangalia tofauti, haki za makundi yote hukubaliwa daima. Ingawa wakimbizi wanalindwa na sheria za kimataifa, wahamiaji pia wana haki ingawa sio nyingi (tazama maelezo yanayofuatia).

Wakimbizi hukubaliwa na mateso katika nchi zao na hivyo wanalazimika kukimbia. Ingawa kwa kawaida serikali inahakikisha haki za kimsingi za binadamu na usalama wa raia wake, wakimbizi hawalindwi na serikali zao; jumuiya ya kimataifa huingilia kati katika hatua ya kuhakikisha haki za binafsi na usalama. Kwa vile wakimbizi hawawezi kulindwa katika nchi zao, wanalindwa na sheria za kimataifa. Wahamiaji, kwa upande mwingine, wanaweza kulindwa katika nchi zao za asili (Cherem, 2016, uk. 190). Kiini cha kimataifa cha ulinzi wa wakimbizi ni Mapatano ya Umoja wa Mataifa (UN) ya Hadhi ya Wakimbizi, yanayoitwa pia “Makubaliano ya Wakimbizi” na pia “Mapatano ya Geneva”⁴; yaliyoidhinishwa 1951, na kurekebishwa na Mkataba wa 1967 unaohusiana na Hadhi ya Wakimbizi, unaoitwa “Mkataba wa Wakimbizi” (UNHCR, 2010; kwa hali mahususi za Kiafrika⁵ tazama Moduli 9). Mkimbizi, kwa mujibu wa Kifungu 1 A. (2) cha Mkataba wa Wakimbizi ni mtu ambaye:

“kwa kuhofia kuteswa kwa sababu za rangi, dini, utaifa, uanachama wa kundi fulani la kijamii au maoni ya kisiasa, yuko nje ya nchi ya utaifa wake na hawezi au, kwa sababu ya hofu hiyo, hayuko tayari kupewa ulinzi wa nchi hiyo; au ambaye, bila kuwa na utaifa na kuwa nje ya nchi ya makazi yake ya awali kutokana na matukio yaliyotajwa, hawezi au, kutokana na hofu hiyo, hataki kurejea” (UNHCR, 2010, uk. 14).

Watu wanaokimbia vita na migogoro ya kivita wanashughulikiwa kwa uwazi na kanuni hii, kama UNHCR ilivyofafanua (UNHCR, 2016c). Mkataba wa Wakimbizi haufafanui tu neno “mkimbizi” lakini pia unaweka haki za wakimbizi chini ya sheria za kimataifa. Haki muhimu zaidi iliyotolewa kwa wakimbizi chini ya mkataba huo ni haki ya kutorudishwa katika nchi ambako maisha au uhuru wao zinatishiwa: “Nchi haziwezi, kwa hali yoyote, kumrudisha mtu ambaye ni mkimbizi au anayedai kuwa mkimbizi katika nchi ambayo anaikimbia” (Grech, 2014, uk. 41). Mbali na mkimbizi kutorudishwa alikotoka, anapewa kinga katika nchi yake mpya. Wakimbizi wanastahili kupokea angalau haki na usaidizi wa kimsingi sawa na mgeni mwingine yeyote ambaye ni mkazi halali — ikiwa ni pamoja na uhuru wa kujieleza na uhuru wa kutodunishwa au kudhalilishwa — na haki sawa za kiuchumi na kijamii ikiwa ni pamoja na kupata matibabu, shule na haki ya

4 Mapatano ya Wakimbizi yalipitishwa na Mkutano wa Umoja wa Mataifa wa Mashirika ya Umma juu ya Hadhi ya Wakimbizi na Watu Wasio na Uraia, uliofanyika Geneva Julai 1951.

5 Mkataba unaosimamia masuala maalumu ya matatizo ya wakimbizi barani Afrika, uliopitishwa Septemba 10, 1969 na mkutano wa wakuu wa nchi na serikali; ulianza kutumika Juni 20, 1974 (OAU, 1969)

kufanya kazi. Kwa sababu za kibinadamu, mataifa yanapaswa kuruhusu mke au mume na watoto wanaowategemea kujiunga na watu wao waliokubaliwa kuwa wakimbizi au kupata hifadhi ya muda (Cherem, 2016, uk. 184-187; Grech, 2014, uk. 191).

Mataifa yana wajibu wa kushirikiana na UNHCR, ambayo imepewa mamlaka ya kutoa ulinzi huu kwa wakimbizi katika kambi, katika mipango yoyote ya makazi ya kibinafsi, katika usafiri na kurudi nyumbani (“kurejeshwa”⁶). Mbali na wakimbizi, UNHCR inawajibika kwa wengine wanaokabiliwa na hatari kubwa na wanahitaji ulinzi wa shirika hilo la kuhudumia wakimbizi (UNHCR, n. d.a; UNHCR, 2019, uk. 63):

- Wanaotafuta hifadhi: Watu ambao wametafuta ulinzi wa kimataifa na ambao maombi yao ya kutaka kutambuliwa kuwa wakimbizi bado hayajaidhinishwa.
- Wakimbizi wa ndani (IDPs): Watu ambao wamelazimishwa kuhama makwao lakini hawajavuka mpaka wa kimataifa; sababu zao za kuhama kwao zinaweza kuwa migogoro ya vita, vurugu za jumla, ukiukaji wa haki za binadamu, majanga (kwa mfano mafuriko) na mengineyo.
- Watu wasio na uraia: Watu ambao hawachukuliwi kama raia na serikali yoyote.
- Makundi ya ziada yanajumuisha wakimbizi waliorudishwa katika nchi zao za asili, IDPs waliorudishwa makwao, na vikundi vingine vinavyolindwa na UNHCR.

Wahamiaji hawajabainishwa wazi, na haki zao si nyingi. UNDESA imeweka juhudi kubwa katika kujaribu kuoanisha taratibu nyingi tofauti za kuainisha wahamiaji, na matokeo yake ni ufafanuzi huu ulioanza kutumika 1998, unaoeleza kuwa mhamiaji wa muda mrefu wa kimataifa ni:

“ [a] mtu anayehamia nchi isiyo ya makazi yake ya kawaida kwa muda wa angalau mwaka mmoja (miezi 12) ili nchi anakoenda iwe nchi yake mpya ya makazi ya kawaida”⁷ (UNDESA, 1998, Box 1, uk. 10).”

Ufafanuzi huu wa wahamiaji wa kimataifa unatokana na dhana ya nchi ya makazi ya kawaida ambayo si lazima iwe nchi ya kuzaliwa kwa mhamiaji au ambapo ana uraia. Hii ni tofauti muhimu ili kuelewa kwamba kwa mfano mhamiaji kutoka Cameroon ambaye aliishi Ufaransa kwa zaidi ya miezi 12, na kisha kuhamia Morocco kutoka Ufaransa sasa atahesabiwa kama mhamiaji kutoka Ufaransa, na uhamiaji wake wa awali kutoka nchi ya asili ya Cameroon hauhesabiwa katika hatua hii, ingawa bado inaweza kuwa muhimu kwa hadhi ya mtu huyo katika nchi ya pili. Wahamiaji wa kimataifa wanajumuisha makundi yote mawili, wale wanaoondoka kwenye nchi yao ili waende wakaishi katika nchi ya ugenini — wahamaji — na wale wanaovuka mpaka na kuingia katika nchi nyingine — wahamiaji (EMN, 2018; IOM, 2019a). Kinyume na hekima iliyozoeleka, labda tofauti hii inaelezewa kwa lengo la ufafanuzi wa Umoja wa Mataifa kuwezesha uwekaji wa

6 Kwa ufafanuzi wa kurudishwa nyumbani, tazama faharasa zinazopendekezwa na mwongozo huu: EMN (2018); IOM (2019a).

7 Wale wanaokaa miezi mitatu hadi chini ya 12 huchukuliwa kuwa wahamiaji wa kimataifa wa muda mfupi (UNDESA, 1998, uk. 10, Box 1).

takwimu za kimataifa za uhamiaji. Matatizo zaidi yanahusishwa hapa, kwa mfano mabadiliko ya hadhi ya kisheria ya mhamiaji anapopita kutoka mamlaka na ulinzi wa nchi moja hadi nyingine. “Uraia ni dhana muhimu sana katika uhamiaji wa kimataifa” (Bilsborrow, 2016, uk. 114) kwani unabainisha ni nani yuko chini ya udhibiti wa uhamiaji na ambaye yuko chini ya ulinzi wa serikali — wafadhili wanaweza kuwa na haki chache za kisheria kuliko wananchi. Wanahabari hutatanika zaidi kutokana na ufafanuzi wa UNDESA wa mhamiaji wa kimataifa kwamba wanajumuisha sio tu wahamiaji halali lakini pia wanaotafuta hifadhi na wale wanaojaribu kuvuka mipaka bila hati halali. (pasi, viza) — wahamiaji wasio wa kawaida — au ambao hubakia baada ya muda wa viza kuisha, yaani waliozidisha muda wao⁸ (Bilsborrow, 2016).

Majaribio ya kufanya ufafanuzi wa takwimu za wahamiaji wa kimataifa “ufanye kazi zaidi” (UNDESA, 2006, uk. 4, para A.2) yanaakisiwa katika Mkataba wa Kimataifa wa Uhamiaji unaotambua hitaji la kuendeleza zaidi ufafanuzi wa takwimu wa mhamiaji wa kimataifa ikiwa ni pamoja na “seti ya viwango vya kupima hifadhi na mtiririko wa wahamiaji, na kuweka kumbukumbu za mwelekeo na safari za uhamaji, sifa za wahamiaji, pamoja na misukumo na taathira za uhamiaji” (UNGA, 2018, uk. 7-8, para 17).

Katika muktadha wa haki, tofauti kati ya wahamiaji na wakimbizi inadhibitiwa kwa uwazi na sheria za kimataifa: Wakimbizi wanafafanuliwa chini ya sheria ya kimataifa na ya kikanda ya wakimbizi, na jumuiya ya kimataifa ina wajibu wa kisheria kwao — Mapatano ya Wakimbizi ya 1951 na mkataba wake wa 1967 huamua wajibu wa mataifa yaliyotia sahihi. Hati hii na nyingine za kisheria, kama vile Mapatano ya Wakimbizi Afrika ya 1969 (OAU, 1969; tazama Moduli 9) “yamepenya katika sheria na desturi nyingine nyingi za kimataifa, kikanda, na kitaifa” (UNHCR, 2016b). “Ingawa kuna mkataba mmoja, unaoshurutishwa kisheria kudhibiti wanayotendewa wakimbizi, [...] hakuna hati yoyote ya msingi inayoshurutisha serikali kuzingatia haki za wahamiaji wote” (Ferris & Martin, 2019). Hata hivyo, wahamiaji na wakimbizi wote wana haki kwani hata wao ni binadamu. Wana haki za binadamu kwa wote na uhuru wa kimsingi, unaowalinda dhidi ya unyanyasaji wa ubaguzi wa rangi na chuki kwa wageni, kutumiwa vibaya, kufanyizwa kazi ya kulazimishwa na mengineyo (Amnesty International, n. d.; Migration Data Portal, 2020c). Haki za wahamiaji hutolewa hasa na sheria za haki za binadamu, na pia kupitia mikataba kutoka matawi mengine ya sheria ya kimataifa ya umma, kwa mfano sheria ya kazi, sheria ya kibinadamu, sheria za kimataifa kuhusiana na uhalifu, hasa mikataba inayohusiana na biashara haramu ya binadamu na magendo (Migration Data Portal, 2020c). Wahamiaji ni kundi lisilo la kikabila linalokabiliwa na udhaifu mwingi unaowakumba wanawake, wasichana, wanaume na wavulana, pia

8 Ufafanuzi wa waliokaa zaidi: tazama faharasa zinazopendekezwa humu EMN (2018); IOM (2019a). Kwa wahamiaji ambao hawana hati za kisheria zinazohitajika (kwa mfano viza) ili kuingia na/au kukaa katika nchi ya kigeni, masharti kama vile siri, haramu, yasiyoidhinishwa, yasiyo na hati na yasiyo ya kawaida ni ya kawaida. Tume ya Ulaya imetumia katika sheria yake maneno raia wa nchi ya tatu aliyepatikana kuwapo kinyume cha sheria au anakaa kinyume cha sheria. Baraza la Ulaya linatofautisha kati ya uhamiaji haramu na uhamiaji usio wa kawaida – haramu linapendelewa wakati wa kurejelea hali au mchakato, nalo usio wa kawaida linaangazia mtu. Umoja wa Mataifa ulitambua kuwa neno haramu halipaswi kutumiwa kufafanua wahamiaji katika hali isiyo ya kawaida. Neno lisilo la kawaida ni afadhali kuliko haramu kwa sababu neno hili la pili lina maana ya jinai, ni kinyume cha utu wa wahamiaji na linadhooifisha heshima ya haki za binadamu za wahamiaji (EMN, 2018; IOM, 2019a).

watu wenye mahitaji maalumu, wazee na wanajumuiya ya LGBTI⁹; sababu mbalimbali zinaweza kuwasukuma mbali na nyumbani na kuingia katika maeneo mapya ndani ya nchi yao ya asili (IDPs) au nje ya mipaka (tazama Moduli 3). Wahamiaji na wakimbizi wanapofika kwenye mpaka wa nchi wanayopitia au kikomo cha safari zao, lazima wakabiliane na haki ya mamlaka ya dola ya taifa hilo kuamua sera yake ya uhamiaji kwa mujibu wa sheria za kimataifa. Hili limethibitishwa tena katika Mkataba wa Wahamiaji na Mkataba wa Wakimbizi. Ni haki ya kila nchi kubainisha sera yake ya kitaifa ya uhamiaji, sera za usimamizi wa mpaka, na kudhibiti uhamiaji chini ya mamlaka yake. Mataifa yanaweza kutofautisha kati ya hali ya uhamiaji wa kawaida na usio wa kawaida, kwa kuzingatia tofauti za hali halisi za kitaifa, sera, vipaumbele na mahitaji ya kuingia, makazi na kazi. Ushirikiano wa ndani wa wakimbizi pia umethibitishwa kama uamuzi huru wa serikali. Uamuzi wa nchi lazima uongozwe na kanuni za haki za binadamu, sheria za kimataifa na wajibu wa mkataba. Hii ina maana kwa wahamiaji na wakimbizi kwamba watakutana na hali tofauti za uhamiaji katika nchi mbalimbali (UNHCR, 2018b, uk. 1, para 2; uk. 7, para 33; uk. 17, para 86; uk. 19, para 97; UNGA, 2018, uk. 5, para 15(c); uk. 20, para 27).

Kando na mtazamo wa kitakwimu wa ufafanuzi wa wahamiaji wa kimataifa (tazama ufafanuzi wa Umoja wa Mataifa wa 1998) na ufafanuzi wa kisheria wa wakimbizi (tazama Mkataba wa Wakimbizi), swali la mhamiaji ni nani bado liko kwenye mjadala (Anderson & Blinder, 2017; Crawley & Skleparis, 2017; Long, 2013; Zetter, 2007). Taasisi hutofautiana kwa kiasi kikubwa na yule wanayemchukulia kama mhamiaji. Njia tatu zitaakisiwa, zile zilizopendekezwa na UNHCR, IOM na Shirika la Utangazaji la Uingereza (BBC). Ikikumbuka kwamba UNHCR ina jukumu la kushughulikia mahitaji ya ulinzi ya “watu wanaowajali” - ikiwa ni pamoja na wakimbizi, wanaotafuta hifadhi na IDPs — shirika hili la wakimbizi la Umoja wa Mataifa linaelezea:

“ Kuna tofauti muhimu kati ya maneno ‘mhamiaji’ na ‘mkimbizi’, ambayo hayawezi kutumika kwa kubadilishana. Wakimbizi wako nje ya nchi yao kwa sababu ya tishio kwa maisha au uhuru wao. Zinafafanuliwa na kulindwa na mfumo maalumu wa kisheria wa kimataifa. Neno ‘mhamiaji’, kwa upande mwingine, halifafanuliwi chini ya sheria za kimataifa, na wakati mwingine hutumiwa tofauti na washikadau tofauti. Kijadi, neno ‘mhamiaji’ limekuwa likitumiwa kuteua watu wanaohama kwa hiari badala ya kukwepa migogoro au mateso, kwa kawaida kuvuka mpaka wa kimataifa, kwa mfano kujiunga na wanafamilia ambao tayari wako ng’ambo, kutafuta riziki, au kwa madhumuni mbalimbali” (UNHCR, 2018a).”

9 Mahusiano ya jinsia moja yanayojumuisha wasagaji, mabasha, wenye viungo vya siri vya kiume na kike pamoja, wenye jinsia tofauti, waliobadili jinsia (LGBTI).

Vilevile, kundi la wataalamu la Umoja wa Mataifa kuhusu takwimu za wakimbizi na IDP linabainisha:

“haja ya kutofautisha kwa ufanisi zaidi, kimawazo, kati ya wahamiaji wa kima-taifa na wakimbizi. [... Mkimbizi] kisheria, kiulinzi, na vile vile kitakwimu, [...] ha-jashughulikiwa ipasavyo chini ya neno “wahamiaji” na katika hali zingine, ni wazi kuwa wakimbizi sio wahamiaji kabisa (kwa mfano, wakimbizi wengi wa Palestina.)” (UN Statistical Commission, 2018, uk. 7, para 25).”



ZOEZI LILILOPENDEKEZWA KUSHUGHULIKIA STADI ZA UTAMBUZI ZA KUTEKELEZA:

Kila kundi lijaribu kuhisi maono ya watu wanaohama, likichunguza kama na jinsi gani wahamiaji na wakimbizi wanaweza kuwa na sifa mahususi, changamoto na fursa, kwa mfano:

- Jukumu la Kundi la 1 la kuigiza wahamiaji,
- Jukumu la Kundi la 2 la kuigiza wakimbizi.

Kila kundi lijaribu kuhisi maono ya watu wanaohama, likichunguza kama na jinsi gani wahamiaji na wakimbizi wanaweza kuwa na sifa mahususi, changamoto na fursa, kwa mfano:

Wahamiaji wanaweza:	Wakimbizi lazima:
Kuchagua kuondoka nyumbani ("kwa hiari").	Waondoke nyumbani kwa sababu "wanateswa". Kwa hivyo, "wanahamishwa kwa nguvu".
Kudhani watalindwa na serikali zao ambazo zinahakikisha haki msingi za binadamu na usalama wa raia wao.	Wafikiri kwamba serikali zao hazitalinda tena.
Kabla ya kuondoka nyumbani, wahamiaji wanaweza kukusanya hati muhimu (pasipoti, vitambulisho), vyeti vya elimu na historia ya kuajiriwa, na mengineyo.	Wanyakue haraka kile kinachopatikana wakati wa kukimbia kutoka nyumbani.
Kutuma pesa nyumbani (masurufu), wakiwa ndio tegemeo kutoka mbali, na mengineyo.	Wajitahidi kuwasiliana na familia zao ili wasihatarishe usalama na ustawi wa wale walio nyumbani, na mengineyo.

Ongeza muda mfupi ili kuyapatia makundi hayo nafasi ya kujadiliana kuhusu waliyokumbana nayo; wanapofanya hivyo wajaribu kufuata mpangilio wa muda wa maandalizi ya mtu binafsi, uamuzi, kuondoka, usafiri, kuwasili katika nchi lengwa, maisha katika sehemu mpya, na kujumuisha haki za mtu binafsi.

IOM sasa inafanya kazi na ufafanuzi-jumla wa wahamiaji unaojumuisha wakimbizi pamoja na watu wengine wote wanaohama kutoka katika makazi yao ya kawaida, “iwe ndani ya nchi au kuvuka mpaka wa mataifa mengine, kwa muda au kwa kudumu, na kwa sababu mbalimbali”. IOM inajumuisha kwa uwazi watu wanaokimbia vita au mateso, kwa mfano wakimbizi (IOM, 2019a, uk.132-133). Kwa hivyo, shirika limefanya mabadiliko kutoka kwa ufafanuzi wake wa 2011 ambao ulisema kwamba istilahi:

“mhamiaji kwa kawaida ilieleweka kushughulikia kesi zote ambapo uamuzi wa kuhama ulichukuliwa kwa uhuru na mtu husika kwa sababu za “hali ya kibinafsi inayofaa” na bila ya ushawishi kutoka nje; kwa hiyo mhamiaji lilitumika kwa watu, na wanafamilia, waliohamia nchi au eneo jingine ili kuboresha hali zao za kwa hali na mali ama kijamii na kujiinua wenyewe au ya familia zao” (IOM, 2011, uk. 61).

Mbali na ufafanuzi wa takwimu na/au wa kisheria wa wahamiaji na wakimbizi wa kimataifa, baadhi ya vyombo vya habari vimebuni ufafanuzi wao. BBC iliamua kutumia ufafanuzi tofauti kwa kuongeza kipengele cha utafutaji wa hifadhi, na kuchukulia wahamiaji kuwa:

“watu wote walio safarini ya kuhama lakini bado hawajakamilisha mchakato wa kisheria wa kuomba hifadhi. Kundi hili linajumuisha watu wanaokimbia nchi zilizokumbwa na vita kama vile Syria ambao wana uwezekano wa kutambuliwa kuwa wakimbizi, pamoja na watu wanaotafuta kazi na maisha bora, ambao huenda serikali ikawataja kuwa wahamiaji wa kiuchumi” (The BBC News , 2016).

Gazeti la *The Guardian* liliwaalika wasomaji kujadili iwapo istilahi “mhamiaji haramu” inafaa kubadilishwa na kuwa “mhamiaji ambaye anashutumiwa kwa kuingia nchi kinyume cha sheria” na likahitimisha kwamba istilahi hiyo inaweza kuwa chaguo bora zaidi, “japo maelezo hayo si ya kistadi” (Elliott, 2014).



ZOEZI LILILOPENDEKEZWA LA KUSHUGHULIKIA STADI ZA UTAMBUZI ZA KUTEKELEZA NA STADI ZA MITAZAMO YA KIBINAFSI NA MAADILI ZA KUJIBU:

Waalike washiriki kuandaa makala fupi (kurasa mbili) kuhusu jinsi ya kufafanua istilahi mbili muhimu, wahamiaji na wakimbizi. Wanapaswa kushughulikia maswali yafuatayo na kuhitimisha kwa mapendekezo:

1. Je, unawafafanua je wahamiaji? Je, unafafanua je wakimbizi? Kwa nini?
2. Ni istilahi ipi au zipi unazopendekeza kwa kazi yako ya uanahabari na unapendekeza kufafanua je?

Istilahi katika lugha rasmi ya nchi yako na hasa katika lugha za kienyeji na za kikabila zinaweza kuongeza kipengele cha kuvutia kwenye mjadala wetu. Sambaza makala yako na uichapishe kwenye tovuti ya mradi www.mediaandmigration.com.

Istilahi nyingine nyingi hutumika katika mjadala wa uhamiaji na uhamiaji wa kulazimishwa — shughuli ya siri, kinyume cha sheria / isiyo ya kawaida / wasio na vibali zikilinganishwa wahamiaji halali, uhamiaji mduara, kuwarudisha makwao, wahamiaji waliorejeshwa, wakimbizi waliorejeshwa au IDPs waliorejeshwa, wanaotafuta hifadhi na IDPs. Dhana ya safari mchanganyiko za wahamiaji na wakimbizi zinaashiria ukweli kwamba wahamiaji na wakimbizi mara nyingi hutumia njia sawa za usafiri, katika kundi moja, wote wakikabiliwa na shida na dhiki sawa, wakilenga shabaha moja — mara nyingi hata kwa sababu sawa lakini kutumia lebo tofauti (Crawley & Skleparis, 2017).

Mwongozo huu unawashauri watumiaji kurejelea kazi za kitaaluma kabla ya kutumia istilahi. Kuna ensaiklopedia, ingawa hizi mara nyingi hutegemea ada (Oxford Research Encyclopedias, 2019) na zinahitaji fedha, na hazipatikani kwa urahisi kwa madarasa mengi na vyumba vya habari kote ulimwenguni. Kwa hivyo, faharasa tatu za kitaasisi — zote zinafikiwa kwa urahisi bila malipo — ambazo hutoa ufafanuzi hitajika. Kwanza, faharasa “ukimbizi na uhamiaji”, iliyochapishwa na Euro-pean Migration Network (EMN), hufanya juhudi kuwasilisha miktadha tofauti, na kutafsiri maneno katika lugha 22. Kichwa cha faharasa kinadokeza lengo la mchapishaji katika maelezo yake kuhusu hifadhi na uhamiaji (EMN, 2018) — mtazamo ambao BBC pia inaupendelea (tazama hapo juu). Pili, faharasa ya UNHCR inarejelea watu wa shirika hilo (UNHCR, n. d.a). Tatu, tunapendekeza faharasa ya IOM kuhusu uhamiaji (IOM, 2019a). Faharasa hizi hutumiwa vyema sambamba ili kutambua mambo muhimu ya taasisi. Faharasa za kitaaluma au za kitaasisi kutoka Afrika au Asia hazipatikani kwa urahisi, lakini faharasa ya uandishi wa habari wa Afrika Kusini ipo na hurejelea IOM (Chiumia, 2016).

Katika utaratibu wa ufafanuzi, uamuzi juu ya neno au istilahi sahihi ya kutumia ni mgumu. Wanazuoni wanafichua undani wa suala la taaluma mbalimbali. Vyombo vya habari vinahitaji ma-

neni mafupi ambayo ni sahihi, yanayounganishwa na wapokeaji, yanayoeleweka kwa urahisi, na kuvutia uangalifu. Takwimu za kimataifa zinahitaji kutoa ushahidi kwa uundaji wa sera. Taasisi zinafuata majukumu yao. Mwongozo huu unawaangazia wahamiaji na wakimbizi kama makundi tofauti ya watu wanaohama au kukimbia. Makundi yote mawili yana haki kama ilivyoainishwa hapo awali. Mtazamo unategemea hali katika nchi wanakotoka, ambapo wakimbizi hawalindwi na serikali yao: Wanahitaji sana ulinzi nje ya nchi. Wahamiaji wanasalia chini ya ulinzi wa serikali zao. Wale walio na mamlaka ya kuwalinda na kuwasaidia — ikiwa ni pamoja na serikali zao, mawakala wa ushirikiano wa kimaendeleo wa kimataifa, mashirika yasiyo ya serikali na wengineo — wanaweza kuwafikia wahamiaji watarajiwa katika nchi zao kwa mipango na miradi maalumu. Ikiangaziwa kwa mtazamo wa nchi wanakoenda, inapendekeza kwamba nchi ambazo zimetia saini Mkataba wa 1951 zinalazimika kuwalinda wakimbizi katika eneo lao na kuwashughulikia kulingana na viwango vinavyotambulika kimataifa. Kwa ujumla, mataifa wanachama yana mamlaka ya kuamua sera zao za uhamiaji kuzingatia sheria za kimataifa, na yanaweza kutofautisha kati ya wanaotafuta hifadhi, hali ya uhamiaji ya mara kwa mara na isiyo ya kawaida (kama inavyothibitishwa tena na Mapatano ya Kimataifa ya Uhamiaji na Mapatano ya Kimataifa ya Wakimbizi, tazama usimulizi wa awali).

Mwongozo huu kwa jumla unarejelea wahamiaji na wakimbizi na masuala ya uhamiaji na uhamishwaji wa kulazimishwa. Unatambua pia makundi mengine kama vile watu wasio na utaifa au IDPs na inarejelea uhamiaji na uhamaji mchanganyiko wa wahamiaji na wakimbizi iwapo muktadha unapendekeza hili kwa kulenga uwazi. Tunasisitiza kwamba watu wote wanaohama au kukimbia wana haki, ingawa ni tofauti. Tunasisitiza zaidi kwamba uanahabari unapaswa kufichua makundi ya watu wanaohusika katika mfumo wowote wa takwimu unaotajwa, ili kuepusha michanganyiko na dhana zisizotarajiwa.

Istilahi nchi za Kaskazini na nchi za Kusini za ulimwengu zinatumiwa sana katika taaluma (Kloß, 2017). Vyombo vya habari katika pembe zote mbili za dunia vinapenda istilahi hizo pia, (Glennie, 2016; Kelegama, 2014; The New Humanitarian, 2012). Istilahi hizo zinakumbusha kuhusu tume ya maendeleo ya kimataifa, North-South Commission, iliyoongozwa na Willy Brandt ambayo ilivumisha istilahi ya nchi za Kaskazini na za Kusini, ikitoa wito wa ushirikiano wa nchi zinazostawi na zilizostawi kwa ajili ya amani na maendeleo, kupigana na “ufisadi, ukandamizaji na vurugu, milipuko [...] ya ushabiki, masaibu ya mamilioni ya wakimbizi, au ukiukwaji mwingine wa haki za binadamu ambao unadhuru haki na mshikamano, ndani na nje ya nchi” (Schmidt, 2018, uk. 7). Baada ya muda, changamoto zilibadilika na suluhu zikarekebishwa, na Shabaha za Maendeleo Endelevu (SDGs; UN, n. d.a) sasa zinajaribu kushughulikia masuala haya moto-moto. Kwa baadhi ya wadadisi, kuugawanya ulimwengu katika sehemu ya Kusini na Kaskazini si njia mwafaka ya kutatua matatizo kwa pamoja. Katika ushauri wa Toshkov (2018): “Nchi za Kusini’ ni neno la kutisha. Usilitumie!”. Mwongozo huu unaelewa maneno Nchi za Kusini na Nchi za Kaskazini kama urithi wa uanahabari. Hata hivyo, kwa uainishaji wa maana, tunachagua zile zinazotumiwa katika ripoti za kila mwaka za Maendeleo ya Binadamu (HDRs) zinazobainisha maendeleo ya binadamu kwa nyanja tatu (1) kuishi maisha marefu, yenye afya na ubunifu, (2) kuwa na ujuzi na (3) kupata rasilimali hitajika kwa maisha bora. Ratiba ya HDR inaainisha

maendeleo ya binadamu ya nchi kuwa ya juu sana, juu, kati na chini (UNDP, 2019). Jumuiya ya kimataifa imeendelea na inafanya kazi kwa uainishaji zaidi, ambao mwongozo huu unaunga mkono, na kila uainishaji unatumika vyema katika muktadha wake ufaao (UNDESA, n. d.):

- Maeneo ya kijiografia: nchi ziliwekwa katika makundi kijiografia katika maeneo sita makuu yaliyoteuliwa kama Afrika, Asia, Ulaya, Amerika ya Kusini na Caribbean, Amerika ya Kaskazini, na Oceania.
- Uainishaji wa maendeleo wa Umoja wa Mataifa (maelezo “yaliyostawi zaidii” na “yaliyostawi kidogo” ni kwa madhumuni ya takwimu na hayawakilishi maamuzi kuhusu mchakato wa maendeleo):
 - ▶ Maeneo yaliyoendelea zaidi ni pamoja na Ulaya, Amerika Kaskazini, Australia/New Zealand na Japan.
 - ▶ Maeneo ambayo hayajaendelea sana yanajumuisha maeneo yote ya Afrika, Asia (isipokuwa Japan), Amerika Kusini na Caribbean pamoja na Melanesia, Micronesia na Polynesia.
 - ▶ Nchi zenye maendeleo duni zaidi sasa ni pamoja na nchi 47, nyingi (32) za Afrika za kusini ya Jangwa la Sahara.
 - ▶ Nchi 32 zinazoendelea na hazina bahari (LLDCs).
 - ▶ Nchi zinazoendelea za visiwa vidogo (SIDS) zinajumuisha mataifa 58.
- Benki ya Dunia inagawanya uchumi wa kipato kama: kipato cha chini, kipato cha chini-kati, kipato cha juu-kati, kipato cha juu (Benki ya Dunia, 2020).
- Kanda za SDG: nchi na maeneo yamejumuishwa katika kanda nane za SDG: (1) Nchi za Afrika za kusini ya Jangwa la Sahara, (2) Afrika Kaskazini na Asia Magharibi, (3) Asia ya Kati na Kusini (4) Mashariki na Kusini-Mashariki mwa Asia, (5) Amerika ya Kusini na Caribbean, (6) Oceania, (7) Ulaya, (8) Amerika Kaskazini.

Wahusika wakuu teule

Wahusika ni akina nani? Imetafsiriwa kutoka lugha ya darasani hadi lugha ya chumba cha habari: Je, Wahusika ni watu? Frey (1985) anaeleza kuwa katika hali ya jumla, wahusika ni washiriki katika maisha ya kisiasa, katika nafasi zao nyingi tofauti.

Kijadi, mataifa wanachama yametazamwa kama wahusika wakuu kuhusiana na sera za uhamiaji na uhamishwaji wa lazima. Wanahifadhi haki muhimu licha ya uanachama wao katika mashirika makubwa ya kimataifa kama vile EU au Umoja wa Afrika (AU). Nchi wanachama wa EU, kwa mfano, zina haki ya kukubali au kuwatenga watu wanaoingia kutoka nchi zisizo za EU kutafuta kazi, na sera ya pamoja kuhusu hifadhi bado ni “lengo” tu la kuendelezwa (Ong’ayo, 2013; Schmid-Drüner, 2019; Sokolska, 2020).

Kimataifa, utawala wa usimamizi wa uhamiaji unaongozwa na SDGs: Katika SDG 10, lengo 10.7, nchi wanachama wa Umoja wa Mataifa zinajitolea kuwezesha “utaratibu, usalama na uwajibikaji katika uhamiaji na usafiri wa watu, ikiwa ni pamoja na sera za utekelezaji wa uhamiaji uliopangwa na unaosimamiwa vizuri.” (UN, n. d.b). Ni wahusika gani hasa wanaoongoza katika utungaji sera ni swali moja linaloongoza Viashiria vya Utawala wa Uhamiaji vya IOM (MGI), vinavyopatikana kwa sasa katika takriban nchi 50 (Migration Data Portal, 2020b). IOM, sawa na wadau wengine wa kimataifa kama vile UNHCR au UNRWA, pia ni mhusika mkuu (BpB, 2016), na wahusika wasio wa serikali huchukua jukumu muhimu zaidi.

Jinsi masuala ya uhamiaji na uhamishwaji wa kulazimishwa yamekuwa ya kisiasa na muhimu, vivyo hivyo mitandao ya kimataifa ya watendaji imekuwa mingi, tatanishi na iliyounganishwa sana. UNHCR, kwa mfano, huwa na mashauriano ya kila mwaka na mashirika yasiyo ya serikali (UNHCR, 2020a), na kuripoti ushirikiano na zaidi ya washirika 900, na kulipa takriban 40% ya matumizi yake ya kila mwaka ndani ya kundi hili (UNHCR, n. d.b). Wanaopokea fedha ni, kwa mfano, mashirika makubwa ya kimataifa yasiyo ya serikali yenye rekodi ndefu na zenye mafanikio katika utekelezaji wa miradi kama vile Médecins Sans Frontières (MSF), CARE, Caritas, Save the Children na International Rescue Committee (IRC), pamoja na mashirika ya ndani yasiyo ya serikali kama Kamati za Taifa za Msalaba Mwekundu na Red Crescent. Mashirika hao hutoa huduma za afya, chakula, wanatafuta haki ya kupata hifadhi, wanaweka watoto shuleni, wanaunganisha wahamiaji na wakimbizi, wanafundisha wanahabari, wanakuza uwezo wa jumuiya za mitaa katika miradi ya jamii ya vyombo vya habari, na mengineyo. Jukumu kuu la mashirika haya yasiyo ya serikali sio tu kutekeleza miradi lakini pia kutekeleza sera. Kwa mfano mashirika 200 yasiyo ya serikali na mashirika ya kutetea haki za raia (CSOs) yalihudhuria mkutano wa ngazi ya juu wa Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa kuhusu kushughulikia harakati kubwa za wahamiaji na wakimbizi Septemba 2016, ambapo asilimia 10 yalikuwa ya Waafrika¹⁰ (UNGA, n. d.). CSOs za kila aina zimeibuka, zikiwemo kutoka mijini, jumuiya za mitaa na maeneo (Caponio, 2019; Lau-sevic, 2018), diaspora, sekta binafsi, na makundi ya watu binafsi (wanawake, vijana). Köngeter & Smith (2015) wanahoji:

“Uhamiaji hauwezi tena kuwa dhana tu katika suala la sera za taifa, kama vile ushirikiano, au utangamano wa tamaduni nyingi. Kwa hakika, wahamiaji hudumisha uhusiano, hujenga mitandao, na kujenga nyanja za kijamii za kimataifa kuvuka mipaka ya kitaifa [...] Wahamiaji hawafikiriwi tena kama waathirika wa utandawazi wa kiuchumi au serikali za uliberali mamboleo, lakini badala yake wanachukuliwa kuwa wahusika wa kimataifa katika ulimwengu wenye sifa ya kukosekana kwa usawa wa kijamii na mahusiano ya mamlaka” (Köngeter & Smith, 2015, uk. 1-2).

10 Baada ya 2015 na halaiki kubwa ya wahamiaji kuingia Ulaya, mashirika mapya yasiyo ya serikali yalianza kuunga mkono wahamiaji. Jong and Ataç (2017) walichanganua mashirika ya wakimbizi ambayo yaliibuka punde nchini Austria baada ya 2015, na kupendekeza kuwa «aina mpya» ilijitokeza: iliyokosoa sana mfumo ulioanzishwa, uliochochewa na uhusiano wa kibinafsi na wakimbizi, unaochanganya utoaji wa huduma na mahitaji ya kisiasa. Kwa wote, imara au mpya, ufadhili ni suala tata, na majina makubwa na rekodi yao ya kuthibitishwa huchukua sehemu kubwa. Mashirika yasiyo ya serikali yanalalamikia ubaguzi (Redvers, 2017).



ZOEZI LILILOPENDEKEZWA LA KUSHUGHULIKIA STADI ZA UTAMBUZI ZA UCHANGANUZI:

Waalike washiriki kutazama ripoti ya habari ya Deutsche Welle (DW) ya dakika 05:20 Ceuta fence: Africa's Spanish enclave lures desperate migrants (DW, 2018), na kupata orodha ya watu na taasisi zinazochukuliwa kuwa wahusika wakuu katika uhamiaji na uhamishwaji wa lazima, kimataifa na hasa katika nchi yako. Utapata kiunga kwenye

<https://www.youtube.com/watch?v=w6h5X86KhCo>

Wanahabari, pamoja na majukumu yao tofauti ya kitaaluma, yaliyoundwa na mifumo yao ya vyombo vya habari (Hallin & Mancini, 2004; Hallin & Mancini, 2012; Hanitzsch na wengine, 2019) na kuongozwa na dhamira na maadili ya vyombo vyao vya habari, ni kundi jingine muhimu katika mjadala huo. Vyombo vya habari huathiri jinsi watu wanavyofikiri na wanavyotenda, jinsi sera zinavyoundwa na kurekebishwa, na jinsi wahamiaji na wanaotafuta hifadhi wanavyofanya maamuzi yao. Kiasi kikubwa cha tafiti kimeangazia taathira za vyombo vya habari (kwa mfano Allen na wengine, 2017; Allen & Blinder, 2013), kama inavyofafanuliwa zaidi katika moduli zinazofuata za mwongozo huu (tazama Moduli 5). Wakati mwingine, watendaji wawili muhimu huungana, kwa mfano wakati wahamiaji au wakimbizi wanakuwa wanahabari (Womack & Meier, 2018; Wüllner & Spies, 2019).

Kundi jingine la wahusika wakuu wanaochangia mjadala ni watafiti, walioandaliwa katika mitandao, vituo vya utafiti, vituo vya uchapishaji, programu za kitaaluma na kwingineko; nyanja za utafiti wa taaluma mbalimbali zimeimarishwa, na IOM inaelekeza kwenye “matokeo makubwa zaidi ya kitaaluma yaliyowahi kutolewa” (IOM, 2019b, uk. 4, uk. 125-126). Kuna vyuo vikuu vichache visivyo na utambuzi wa kitaasisi wa masomo ya uhamiaji na wakimbizi (Yalaz & Zapata-Barrero, 2018).¹¹

Tusipuuze, msukumo wa watu kuhamia maeneo mengine umezua tasnia ya uhamiaji inayofanana na biashara kubwa ya kimataifa, na biashara inayokuwa; wengine ni halali, wengine wahalifu na hata wasio na utu, wengine wanaleta senti, wengine bahati. Wanaofaidika ni madereva wa teksi wa ndani ambao huwabana wahamiaji wengi sana kwa malipo ya juu kwenye magari yao, polisi wakidai rushwa, mashirika ya uhamiaji ambayo hupokea ada za udalali (wakati fulani kwa kazi

11 Majarida ya kitaaluma katika nyanja hizi yamejikita, katika uhamiaji kwa mfano majarida kama: International Migration (tangu 1961), International Migration Review (1964), Journal of Ethnic and Migration Studies (JEMS, tangu 1998), Migration Studies (tangu 2013) .. Ingawa majarida haya yana neno 'uhamiaji', yanachapisha aina zote za uhamiaji, kinyume na Journal of Refugee Studies (tangu 1988) ambalo linazingatia uhamishwaji wa kulazimishwa (Vargas-Silva, 2015). Miongozo ya utafiti ya maktaba ya Umoja wa Mataifa katika Geneva inaongoza kwa vituo mbalimbali vya kimataifa vya utafiti kuhusu wakimbizi (United Nations Library and Archives, 2019). EU inasaidia utafiti kuhusu uhamiaji kupitia Mpango wake wa Mfumo wa Utafiti, na programu ya Horizon 2020 (2014-2020) ilitoa «uhamasishaji ambao haujawahi kushuhudiwa wa rasilimali za umma ili kukabiliana na changamoto ya uhamiaji» (King & Lulle, 2016). Katika nchi za Afrika za kusini ya Jangwa la Sahara, utafiti

zenye kutia shaka na wakati fulani kupigwa marufuku na serikali kama ilivyo Uganda), kampuni za kimataifa zinazosimamia vizuizi au kulinda usalama mipakani. Biashara kubwa ni pamoja na mitandao ya uhalifu iliyopangwa kujinufaisha kutokana na ulanguzi na usafirishaji haramu wa binadamu (Gammeltoft-Hansen & Nyberg Sorensen, 2012). Ingawa inaweza kushangaza kwa wengine: Kuwaona wahamiaji na wakimbizi kama wahusika wakuu inaonekana kuwa wazo geni, ambalo Fengler na wenzake (2020) wamechanganua katika utafiti wao wa jinsi mambo yalivyo-ripotiwa katika pande zote za Mediterranean (tazama Moduli 4).



ZOEZI LILILOPENDEKEZWA LA KUSHUGHULIKIA STADI ZA UTAMBUZI ZA KUTEKELEZA, STADI ZA MITAZAMO YA KIBINAFSI NA MAADILI ZA KUJIBU NA STADI ZA UTENDAJI ZA KUENDELEZA UHAKIKA:

Ili kujumlisha wazo la moduli hii na vyanzo vyake vya data, istilahi muhimu na wahusika wakuu, waalike washiriki kuandaa ripoti fupi ambayo inaweza kuchapishwa katika gazeti la kitaifa (angalau herufi 2,000), inayoonyesha wasifu wa nchi na wasifu wa uhamiaji wa nchi ya chaguo, kwa kutumia tovuti ya data ya uhamiaji (Portal ya Data ya Uhamiaji, 2020d), kwa mfano kujibu maswali haya:

1. Wasifu wa nchi

Kwa wasifu wa nchi (kwa mfano Cameroon), tumia data kutoka Tovuti ya Data ya Uhamiaji na kutoka UNData, Ripoti za Maendeleo ya Binadamu, UNHCR, UN Geospatial Information Section, majumuiya ya washauri kama vile Berlin Institute for Population and Development, Pew Research Center, au vyanzo vingine vilivyowasilishwa katika moduli hii au vinavyozingatia mapendekezo yaliyotolewa humu.

2. Wasifu wa uhamiaji

Kwa wasifu wa uhamiaji, wanafunzi wanaweza kutafiti:

- Uhamaji na uhamiaji (chagua mwaka wa hivi karibuni):
 - ▶ Ni wahamiaji wangapi wa kimataifa waliohama kwa mfano kwenda Cameroon?
 - ▶ Ni makundi yapi matatu makubwa yaliyohama kwa mfano kwenda Cameroon?
 - ▶ Ni watu wangapi walihama kwa mfano kutoka Cameroon?
 - ▶ Ni nchi gani tatu zilizopendelewa na wahamiaji kwa mfano kutoka Cameroon?

- Hatari ya wahamiaji (chagua mwaka wa hivi majuzi zaidi):
 - ▶ Ni wanawake wangapi walisafirishwa?
 - ▶ Ni watoto wangapi walisafirishwa?
 - ▶ Ni wahamiaji wangapi waliopotea?
 - ▶ Nchi asilia imeridhia vyombo vingapi vya haki za binadamu (sema ni vipi ikiwezekana)?

- Uhamishwaji wa kulazimishwa:
 - ▶ Nchi inahifadhi wakimbizi wangapi?
 - ▶ Ni wakimbizi wangapi waliokimbia kutoka nchini?
 - ▶ Je, ni watu wangapi waliokimbia makazi yao kwa sababu ya migogoro nchini?
 - ▶ Je, ni watu wangapi waliokimbia makazi yao kutokana na maafa nchini?
 - ▶ Je, nchi ilikuwa mwenyeji wa IDPs wangapi mwaka wa 2019?

Kurasa za nchi za tovuti ya Migration Data Portal — baadhi yake hutoa ripoti za hivi majuzi za wasifu wa uhamiaji (kwa mfano kwa Cameroon kutoka 2009) — na hivyo kutoa muktadha.



ILIYOPENDEKEZWA YA KUSHUGHULIKIA STADI ZA UTAMBUZI ZA KUTEKELEZA NA KUCHANGANUA, STADI ZA MITAZAMO YA KIBINAFSI NA MAADILI ZA KUJIBU NA STADI ZA UTENDAJI ZA KUENDELEZA UHAKIKA:

Waalike washiriki kutazama somo la mtandao kuhusu jinsi ya kutumia Tovuti ya Data ya Uhamiaji (Migration Data Portal, 2019b). Mhadhara huu wa dakika 45 husaidia kuonyesha jinsi ya kutumia zana kwa ubora zaidi. Chagua swali moja au zaidi kati ya yafuatayo:

(A) Wape washiriki jukumu la kutafiti takwimu zilizochaguliwa kutoka kwa ripoti za vyombo vya habari vya ndani na kuhakiki data kwa kutumia Tovuti ya Data ya Uhamiaji.

(B) Wape fursa washiriki kuandika ripoti kwa gazeti la kitaifa (angalau herufi 5,000), kufafanua Mapatano ya Wakimbizi na maana yake kwa wakimbizi katika nchi yako, Mapatano ya Uhamiaji na maana yake kwa wahamiaji wanaoondoka nchini mwako; washiriki wajumuishe takwimu kwa kutumia Tovuti ya Data ya Uhamiaji.

(C) Unaweza kutaka kualika mtaalamu (kwa mfano mshiriki wa ofisi ya karibu ya IOM) kwa awamu ya maswali na majibu na kipindi cha mazoezi ili kujadili maana ya matumizi tofauti ya istilahi muhimu.



USOMAJI WA ZIADA:

Kiakademia:

Bilsborrow, R. E. (2016). Concepts, definitions and data collection approaches. In M. J. White (Ed.). *International Handbook of Migration and Population Distribution* (6th ed., uk. 109-156). Dordrecht, Heidelberg, New York, London: Springer.

Kiuanahabari:

Raymond, N. A., Scarneccia, D. P., & Campo, S. R. (2017). Humanitarian data breaches: The real scandal is our collective inaction. Retrieved November 27, 2020, from <https://www.thenewhumanitarian.org/opinion/2017/12/08/humanitarian-data-breaches-real-scandal-our-collective-inaction>

Kitaasisi:

Migration Data Portal (2020d). The bigger picture. Retrieved December 20, 2020, from https://migrationdataportal.org/?i=stock_abs_&t=2019

Marejeleo

AfDB, AU Commission, & UNECA (2019). *African Statistical Yearbook*. Retrieved December 13, 2020, from <https://www.afdb.org/en/knowledge/publications/african-statistical-yearbook>

AfDB (2020). *Statistics*. Retrieved December 13, 2020, from <https://www.afdb.org/en/knowledge/statistics>

Allen, W., & Blinder, S. (2013). *Migration in the News: Portrayals of immigrants, migrants, asylum seekers and refugees in national British newspapers, 2010 to 2012*. Migration Observatory report, COMPAS, University of Oxford. Retrieved December 14, 2020, from https://migrationobservatory.ox.ac.uk/wp-content/uploads/2016/04/Report-Migration_News.pdf

Allen, W., Blinder, S., & McNeil, R. (2017). Media reporting of migrants and migration. In *World Migration Report 2018* (pp. 191-208). Geneva: IOM. Retrieved December 14, 2020 from https://www.iom.int/sites/default/files/country/docs/china/r5_world_migration_report_2018_en.pdf

American University of Cairo (n. d.). AUC, Center for Migration and Refugee Studies. Retrieved November 11, 2020, from <https://www4.aucegypt.edu/CMRS/>

Amnesty International (n. d.). Key facts about refugees and asylum seekers' rights. Retrieved September 25, 2020, from <https://www.amnesty.org/en/what-we-do/refugees-asylum-seekers-and-migrants/>

Anderson, B., & Blinder, S. (2017). Who counts as a migrant? Definitions and their consequences (Briefing). Oxford. Retrieved September 11, 2020, from http://www.migrationobservatory.ox.ac.uk/wp-content/uploads/2016/04/Briefing-Who_Counts_as_a_Migrant.pdf

Berlin Institute for Population and Development (2020). *Shaping demographic change*. Retrieved December 13, 2020, from <https://www.berlin-institut.org/en>

Bilsborrow, R. E. (2016). Concepts, definitions and data collection approaches. In White, M. J. (Ed.). *International handbook of migration and population distribution* (6th ed., pp. 109-156). Dordrecht, Heidelberg, New York, London: Springer.

- BpB (2016). Actors in national and international (flight) migration regimes. Retrieved May 8, 2020, from <https://www.bpb.de/gesellschaft/migration/kurzdoessiers/229618/actors-in-national-and-international-flightmigration-regimes>
- Buneman, P., Müller, H., & Rusbridge, C. (2009). Curating the CIA world factbook. *International Journal of Digital Curation (IJDC)*, 4(3), 29-43. <https://doi.org/10.2218/ijdc.v4i3.126>
- Caponio, T. (2019). City networks and the multilevel governance of migration: Policy discourses and actions. Euro-pean University Institute (EUI, Robert Schuman Centre for Advanced Studies (RSCAS) No. 8). Retrieved April 20, 2019, from http://cadmus.eui.eu/bitstream/handle/1814/60666/RSCAS_2019_08.pdf?sequence=1&isAllowed=y
- Cherem, M. (2016). Refugee rights: Against expanding the definition of a “refugee” and unilateral protection else-where. *Journal of Political Philosophy*, 24(2), 183-205. <https://doi.org/10.1111/jopp.12071>
- Chiumia, S. (2016). Guide: Defining migration, migrants, and refugees (and why it matters). Retrieved November 27, 2020, from <https://africacheck.org/factsheets/guide-defining-migration-migrants-refugees-matters/>
- Crawley, H., & Skleparis, D. (2017). Refugees, migrants, neither, both: Categorical fetishism and the politics of bounding in Europe’s ‘migration crisis’. *Journal of Ethnic and Migration Studies*, 44(1), 48-64. <https://doi.org/10.1080/1369183X.2017.1348224>
- DW (2018). Ceuta fence: Africa’s Spanish enclave lures desperate migrants. Retrieved November 27, 2020, from <https://www.youtube.com/watch?v=w6h5X86KhCo>
- Elliott, C. (2014, August 14). The readers’ editor on ... whether we should use the term ‘illegal immigrant’: A person can’t be illegal – but is there a concise alternative to describe someone who is in a country unlawfully? *The Guardian*. Retrieved May 6, 2020, from <https://www.theguardian.com/commentisfree/2014/aug/24/open-door-should-we-use-term-illegal-immigrant>
- EMN (2018). Asylum and migration. Glossary 6.0. European Migration Network. Retrieved November 27, 2020, from https://www.emn.at/wp-content/uploads/2018/06/emn-glossary-6-0_en.pdf
- Eurostat (2019). Eurostat co-ordination role of statistical activities. Brussels. Retrieved November 27, 2020, from <https://ec.europa.eu/eurostat/about/overview/co-ordination-role>
- Fengler, S., Bastian, M., Brinkmann, J., Zappe, A.-C., Tatab, V., Andindilile, M., Assefa, E., Chibita, M., Mbaine, A., Obonyo, L., Quashigah, T., Skleparis, D., Splendore, S., Tadesse, M. & Lengauer, M. (2020). Covering Migration – in Africa and Europe: Results from a comparative analysis of 11 countries. *Journalism Practice*. <https://doi.org/10.1080/17512786.2020.1792333>
- Ferris, E. E., & Martin, F. S. (2019). Introduction to the special issue “The Global Compact for safe, orderly and regular migration and The Global Compact on refugees”. *International Migration*, 57(6), 5-18. <https://doi.org/10.1111/imig.12668>
- Frey, F. W. (1985). The problem of actor designation in political analysis. *Comparative Politics*, 17(2), 127-152. Retrieved December 14, 2020, from <https://www.jstor.org/stable/pdf/421726.pdf?refreqid=excelsior%3Ac00137ba7c12a3ee27ed5d0f9663511e>
- Gammeltoft-Hansen, T., & Nyberg Sorensen, N. (Eds.) (2012). *The migration industry and the commercialization of international migration*. London: Routledge.
- Glennie, J. (2016, January 18). Who lives in the real world: global south pessimists or northern optimists? *The Guardian*. Retrieved May 9, 2020, from <https://www.theguardian.com/global-development/2016/jan/18/who-lives-in-the-real-world-global-south-pessimists-or-northern-optimists>
- Grech, O. (2014). Migrants’and refugees’ rights: A brief international law perspective. In O. Grech & M. Wohlfeld (Eds.). *Migration in the Mediterranean: Human rights, security and development perspectives* (pp. 40-49). Malta: MEDAC, University of Malta.

- Hallin, D. C., & Mancini, P. (2004). *Comparing Media Systems: Three models of media and politics*. Oxford: Cambridge University Press.
- Hallin, D. C., & Mancini, P. (2012). *Comparing media systems beyond the Western world*. Oxford: Cambridge University Press.
- Hanitzsch, T., Hanusch, F., Ramaprasad, J., & de Beer, A. S. (Eds.) (2019). *Worlds of Journalism: Journalistic cultures around the globe*. New York: Columbia University Press.
- IDMC (2019). *Global Report on Internal Displacement (GRID): Methodological Annex*. Retrieved December 13, 2020, from <https://www.internal-displacement.org/sites/default/files/2019-GRID-methodology.pdf>
- ILO (2020). *Key ILO databases and sources*. Retrieved December 13, 2020, from https://www.ilo.org/pardev/public-private-partnerships/WCMS_418560/lang--en/index.htm
- IMI (2020). *Migration databases*. Oxford. Retrieved December 13, 2020, from <https://www.migrationinstitute.org/data/demig-data>
- IOM (2011). *Glossary on migration*. Retrieved August 22, 2018, from https://publications.iom.int/system/files/pdf/iml25_1.pdf
- IOM (2019a). *Glossary on Migration*. Geneva. Retrieved August 5, 2019, from https://publications.iom.int/system/files/pdf/iml_34_glossary.pdf
- IOM (2019b). *World migration report 2020*. Geneva. Retrieved from https://publications.iom.int/system/files/pdf/wmr_2020.pdf
- IOM DTM (2020). *Displacement Tracking Matrix: Displacement*. Retrieved November 27, 2020, from <https://displacement.iom.int/>
- Jong, S. de, & Ataç, I. (2017). Demand and deliver: Refugee support organisations in Austria. *Social Inclusion*, 5(3), 28. <https://doi.org/10.17645/si.v5i3.1003>
- Kelegama, S. (2014, July 23). Will the BRICS bank and fund boost Global South? *The Daily Star*. Retrieved May 9, 2020, from <https://www.thedailystar.net/will-the-brics-bank-and-fund-boost-global-south-34443>
- King, R., & Lulle, A. (2016). *Research on migration: Facing realities and maximising opportunities: A policy review*. Brussels. Retrieved February 15, 2019, from https://ec.europa.eu/research/social-sciences/pdf/policy_reviews/ki-04-15-841_en_n.pdf
- Kloß, S. T. (2017). The Global South as subversive practice: Challenges and potentials of a heuristic concept. *The Global South*, 11(2), 1-17. <https://doi.org/10.2979/globalsouth.11.2.01>
- Köngeter, S., & Smith, W. (2015). Transnational agency: Migrants, movements and social support crossing borders. In Köngeter, S. & Smith, W. (Eds.). *Transnational Agency and Migration: Actors, movements and social support* (pp. 1-22). Abingdon: Routledge.
- Lausevic, V. (2018). Increased role and sovereignty for urban areas – A key to handle migration crisis. Retrieved November 27, 2020, from <https://www.vocaleurope.eu/increased-role-and-sovereignty-for-urban-areas/>
- Long, K. (2013). When refugees stopped being migrants: Movement, labour and humanitarian protection. *Migration Studies*, 1(1), 4-26. <https://doi.org/10.1093/migration/mns001>
- Migration Data Portal (2019a). *IOM data overview*. Retrieved September 30, 2020, from <https://migrationdata-portal.org/themes/iom-data-overview>
- Migration Data Portal (2019b). *Webinar: 5 best uses of the Migration Data Portal*. Retrieved November 28, 2019, from <https://migrationdataportal.com/blog/5-best-uses-migration-data-portal>

Migration Data Portal (2020a). About. Retrieved September 25, 2020, from <https://migrationdataportal.org/about>

Migration Data Portal (2020b). About the migration governance indicators. Retrieved October 4, 2020, from <https://migrationdataportal.org/overviews/mgi#0>

Migration Data Portal (2020c). Migrant rights. Retrieved November 17, 2020, from <https://migrationdataportal.org/themes/migrant-rights>

Migration Data Portal (2020d). Migration Data Portal: The bigger picture. Retrieved September 20, 2020, from https://migrationdataportal.org/?i=stock_abs_&t=2019

Monmonier, M. (2018). *How to lie with maps* (3rd ed.). Chicago, London: University of Chicago Press.

OUA (1969). Convention governing the specific aspects of refugee problems in Africa: Adopted on 10 September 1969 by the Assembly of Heads of State and Government CAB/LEG/24.3. Retrieved November 27, 2020, from <https://www.unhcr.org/about-us/background/45dc1a682/oua-convention-governing-specific-aspects-refugee-problems-africa-adopted.html>

Ong'ayo, A. O. (2013). Linking local actors in migration and development: Strengthening strategic cooperation between diaspora and civil society institutions in Africa. Retrieved April 20, 2019, from <https://www.diaspora-centre.org/DOCS/2013/2013researchreportOtieno.pdf>

Oucho, J. O. (1998). Recent internal migration processes in Sub-Saharan Africa: determinants, consequences, and data adequacy issues. In R. E. Bilsborrow (Ed.), *Migration, urbanization, and development: New directions and issues* (pp. 89-120). New York: UNFPA and Kluwer Academic Publishers.

Our World in Data (n. d.). About. Retrieved September 30, 2020, from <https://ourworldindata.org/about>

Oxford Research Encyclopedias (2019). Oxford Research Encyclopedias. Oxford. Retrieved November 27, 2020, from <http://oxfordre.com/page/subjects/>

Pew Research Center, & John Templeton Foundation (2016). Global Religious Futures Project. Retrieved April 25, 2020, from <http://www.globalreligiousfutures.org/explorer/about>

Raymond, N. A., Scarneccia, D. P., & Campo, S. R. (2017). Humanitarian data breaches: The real scandal is our collective inaction. Retrieved November 27, 2020, from <https://www.thenewhumanitarian.org/opinion/2017/12/08/humanitarian-data-breaches-real-scandal-our-collective-inaction>

Redvers, L. (2017). Local aid agencies: still waiting for a bigger share of the funding cake. Retrieved November 27, 2020, from <https://www.thenewhumanitarian.org/analysis/2017/03/27/local-aid-agencies-still-waiting-bigger-share-funding-cake>

Sankoh, O., Dickson, K. E., Faniran, S., Lahai, J. I., Forna, F., Liyosi, E., Kamara, M., Jabbi, S.-M., Johnny, A., Conteh-Khali, N., Bangali, A., Kangbai, J., Bockarie, T., Massaquoi, M., Smart, F., Jambai, A., Clarke, M., Dlamini, A., & Weston, M. (2020). Births and deaths must be registered in Africa. *The Lancet Global Health*, 8(1), e33-e34. [https://doi.org/10.1016/S2214-109X\(19\)30442-5](https://doi.org/10.1016/S2214-109X(19)30442-5)

Schmid-Drüner, M. (2019). Immigration policy (Fact Sheets on the European Union). Retrieved May 8, 2020, from https://www.europarl.europa.eu/RegData/etudes/fiches_techniques/2017/N54569/doc_en.pdf

Schmidt, W. (2018). Willy Brandt: Online Biography. "One world" – Engagement in the North-South conflict 1969–1992. Retrieved May 9, 2020, from <https://www.willy-brandt-biography.com/politics/north-south-conflict/>

Sokolska, I. (2020). Asylum Policy (Fact Sheets on the European Union). Brussels. Retrieved May 8, 2020, from https://www.europarl.europa.eu/ftu/pdf/en/FTU_4.2.2.pdf

The BBC News (2016). Migrant crisis: Migration to Europe explained in seven charts. Retrieved November 27, 2020, from <https://www.bbc.com/news/world-europe-34131911>

The New Humanitarian (2012, September 11). Global South leads the way towards universal healthcare coverage. Retrieved May 9, 2020, from <http://www.thenewhumanitarian.org/report/96280/health-global-south-leads-way-towards-universal-healthcare-coverage>

Toshkov, D. (2018). The 'Global South' is a terrible term. Don't use it! Retrieved May 9, 2020, from <http://re-design.dimiter.eu/?p=969>

UN (n. d.a). Sustainable development goals. Retrieved November 27, 2020, from <https://sustainabledevelopment.un.org/?menu=1300>

UN (n. d.b). Sustainable Development Goals: SDG 10: Reduce inequality within and among countries. Retrieved November 24, 2020, from <https://sdgs.un.org/goals/goal10>

UN (2020). Global Compact for Migration / Global Compact on Refugees. Retrieved December 20, 2020, from <https://refugeesmigrants.un.org/>

UN Geospatial Information Section, & GGIM (2019). General Maps. New York. Retrieved November 27, 2020, from <https://www.un.org/Depts/Cartographic/english/htmain.htm>

UN Network on Migration (n. d.). The Global Compact for Migration: Well governed migration as an essential element of effective Covid-19 response. Retrieved September 29, 2020, from https://migrationnetwork.un.org/sites/default/files/docs/policy_brief_-_gcm_and_well_governed_migration_as_an_essential_element_of_effective_covid-19_response.pdf

UN Statistical Commission (2018). Report of the expert group on refugee and internally displaced persons statistics. Retrieved October 4, 2020, from <https://unstats.un.org/unsd/statcom/49th-session/documents/2018-16-Refugee-E.pdf>

UN Statistical Commission (2020). Overview. Retrieved December 13, 2020, from <https://unstats.un.org/unsd/statcom/>

UNdata (2020). About: Country profiles. Retrieved October 1, 2020, from <https://data.un.org/>

UNDESA (n. d.). Definition of regions. Retrieved May 9, 2020, from <https://population.un.org/wpp/DefinitionOfRegions/>

UNDESA (1998). Recommendations on statistics of international migration. Revision 1. New York. Retrieved December 8, 2020 from https://unstats.un.org/unsd/publication/seriesm/seriesm_58rev1e.pdf

UNDESA (2006). Migration statistics: Report of the Secretary-General. New York. Retrieved October 3, 2020, from <https://unstats.un.org/unsd/statcom/38th-session/documents/2007-16-migration-E.pdf>

UNDESA (2019a). World Population Prospects. Retrieved December 14, 2020 from <https://population.un.org/wpp/>

UNDESA (2019b). World Population Prospects 2019, Volume I: Comprehensive Tables. New York. Retrieved December 14, 2020, from https://population.un.org/wpp/Publications/Files/WPP2019_Volume-I_Comprehensive-Tables.pdf

UNDP (n.d.). Human Development Reports. Retrieved December 13, 2020 from <http://www.hdr.undp.org/>

UNDP (2019). Human Development Report 2019: Beyond income, beyond averages, beyond today: Inequalities in human development in the 21st century (Human Development Reports). New York. Retrieved March 10, 2020, from United Nations Development Programme website: <http://hdr.undp.org/sites/default/files/hdr2019.pdf>

UNESCO, & UIS (2020). Data for sustainable development goals. Retrieved November 27, 2020, from http://uis.unesco.org/en/home#tabs-0-uis_home_top_menus-3

UNGA (n.d.). NGOs and CSOs attend high-level plenary of the General assembly on 19 September 2016 on addressing large movements of refugees and migrants. Retrieved April 19, 2019, from <https://refugeesmigrants.un.org/list-approved-ngos-and-csos>

UNGA (2018). Global Compact for Safe, Orderly and Regular Migration: Resolution adopted by the General Assembly on 19 December 2018. Retrieved September 25, 2020, from UN General Assembly website: https://www.un.org/en/ga/search/view_doc.asp?symbol=A/RES/73/195

UNHCR (n. d.a). Glossary. Retrieved November 25, 2020, from <http://www.issm.cnr.it/progetti/emigrazione/META%20DATA%20E%20GLOSSARI/UNHCR/GLOSSARY%20UNHCR.pdf>

UNHCR (n. d.b). Non-governmental organizations. Retrieved November 27, 2020, from <https://www.unhcr.org/non-governmental-organizations.html>

UNHCR (2010). Convention and protocol relating to the status of refugees. Geneva. Retrieved July 1, 2018, from <https://www.unhcr.org/protection/basic/3b66c2aa10/convention-protocol-relating-status-refugees.html>

UNHCR (2016a). The 10-Point Plan in Action: Chapter 2: Data collection and analysis. Retrieved October 1, 2020, from <https://www.unhcr.org/the-10-point-plan-in-action.html>

UNHCR (2016b). Refugee or Migrant? Word choice matters: UNHCR viewpoint: 'Refugee' or 'migrant' – Which is right? The two terms have distinct and different meanings, and confusing them leads to problems for both populations. Retrieved November 27, 2020, from <http://www.unhcr.org/news/latest/2016/7/55df0e556/unhcr-viewpoint-refugee-migrant-right.html>

UNHCR (2016c). Guidelines on international protection No. 12 (No. HCR/GIP16/12). Geneva. Retrieved May 6, 2020, from <https://www.unhcr.org/publications/legal/58359afe7/unhcr-guidelines-international-protection-12-claims-refugee-status-related.html>

UNHCR (2018a). Migrant definition: Emergency handbook. Retrieved March 6, 2020, from <https://emergency.unhcr.org/entry/250459/migrant-definition>

UNHCR (2018b). Report of the United Nations High Commissioner for Refugees. Part II. Global compact on refugees. Retrieved February 2, 2019, from https://www.unhcr.org/gcr/GCR_English.pdf

UNHCR (2019). Global trends: Forced displacement in 2018. Geneva. Retrieved March 10, 2020, from <https://www.unhcr.org/5d08d7ee7.pdf>

UNHCR (2020a). Annual consultations with NGOs. Retrieved November 27, 2020, from <https://www.unhcr.org/annual-consultations-ngos.html>

UNHCR (2020b). Data. Retrieved September 30, 2020, from <https://www.unhcr.org/data.html>

UNHCR (2020c). Data collection in times of physical distancing. Retrieved September 30, 2020, from <https://www.unhcr.org/blogs/data-collection-in-times-of-physical-distancing/>

UNHCR (2020d). Global Trends: Forced displacement in 2019. Copenhagen. Retrieved August, 2020, from <https://www.unhcr.org/5ee200e37.pdf>

United Nations Library and Archives (2019). Research guides: Refugees and asylum seekers: Websites. Geneva. Retrieved November 27, 2020, from <https://libraryresources.unog.ch/c.php?g=462675&p=3162952>

UNRWA (2019). In figures 2018-2019. Retrieved May 9, 2020, from <https://www.unrwa.org/?id=253>

UNSD (2020a). Demographic and social statistics: International Migration. Retrieved December 13, 2020, from <https://unstats.un.org/unsd/demographic-social/sconcerns/migration/index.cshtml>

UNSD (2020b). Statistical Yearbook 2020. New York. Retrieved December, 13, 2020 from <https://unstats.un.org/unsd/publications/statistical-yearbook/>

UNSD (2020c). Demographic and social statistics: Demographic Yearbook System. New York. Retrieved December 13, 2020, from <https://unstats.un.org/unsd/demographic-social/products/dyb/index.cshtml>

Vargas-Silva, C. (2015, September 30). Which migration journal has the highest Impact Factor? COMPAS Blog, Retrieved November 27, 2020, from <https://www.compas.ox.ac.uk/2015/which-migration-journal-has-the-highest-impact-factor/>

Wits University (2019). African Centre for Migration and Society. Retrieved November 27, 2020, from <https://www.wits.ac.za/acms/>

Womack, H., & Meier, J. (2018). Magazine's media studies course is good news for refugees. Retrieved October 5, 2020, from <https://www.unhcr.org/news/stories/2018/6/5b3502004/magazines-media-studies-course-good-news-refugees.html>

World Bank (2017). Forcibly Displaced: Toward a development approach supporting refugees, the internally displaced, and their hosts. Washington, D.C. Retrieved December 13, 2020, from <https://openknowledge.worldbank.org/bitstream/handle/10986/25016/9781464809385.pdf?sequence=11&isAllowed=y>

World Bank (2019). World Development Indicators. Retrieved November 27, 2020, from <http://datatopics.worldbank.org/world-development-indicators/>

World Bank (2020). The world by income and region. Retrieved May 9, 2020, from <https://datatopics.worldbank.org/world-development-indicators/the-world-by-income-and-region.html>

Wüllner, G., & Spies, M.-C. (2019, January 2). Newspaper gives refugees a voice. Deutsche Welle. Retrieved May 9, 2020, from <https://www.dw.com/en/newspaper-gives-refugees-a-voice/a-46877218>

Yalaz, E., & Zapata-Barrero, R. (2018). Mapping the qualitative migration research in Europe. An explanatory analysis. In Zapata-Barrero, R. & Yalaz, E. (Eds.). IMISCOE Research Series. Qualitative Research in European Migration Studies. Cham: Springer International Publishing. Retrieved December 14, 2020, from https://link.springer.com/chapter/10.1007/978-3-319-76861-8_2

Zetter, R. (2007). More labels, fewer refugees: Remaking the refugee label in an era of globalization. *Journal of Refugee Studies*, 20(2), 172-192. <https://doi.org/10.1093/jrs/fem011>

Zlotnick, H. (1987). Introduction: Measuring international migration: Theory and practice. *The International Migration Review*, 21(4), v-xii. <https://doi.org/10.2307/2546497>



MODULI 3

Vipengele vya muktadha wa uhamiaji na uhamishwaji wa kulazimishwa

na Monika Lengauer
na Susanne Fengler



MALENGO YA MODULI

- Kuwasilisha dhana teule za masuala ya taaluma ya jamii ya uhamiaji kwa uchanganuzi wa harakati za uhamiaji.
- Kuanzisha mjadala kuhusu misukumo na vivutio vinavyowapelekea watu kuhama au kukimbia.
- Kuwezesha uelewa wa kina wa vipengele teule vya muktadha.



MALENGO YA MAFUNZO

Kufikia mwisho wa moduli hii, washiriki wanapaswa kuwa na uwezo wa:

- Kutambua umuhimu wa vipengele vya muktadha wa kuripoti masuala ya uhamiaji na uhamishwaji wa lazima. → **Matokeo ya mafunzo kwa stadi za kibinafsi: Kupokea**
- Kuelezea nadharia na msingi wa utafiti wao uwe fasihi ya kitaaluma. → **Matokeo ya mafunzo kwa stadi za utambuzi: Kuelewa**
- Kutambua vipengele vya muktadha kwa wahamiaji na wakimbizi na kueleza → **Matokeo ya mafunzo kwa stadi za utambuzi: Kuelewa**
- Kuweka muktadha wa mambo ya kusukuma na kuvuta ipasavyo kwa kuyawasilisha katika uanahabari. → **Matokeo ya mafunzo kwa stadi za utambuzi: Kutekeleza.**

Muhtasari

Sababu nyingi zinaweza kuwasukuma wahamiaji na wakimbizi kuondoka nyumbani, zikiwemo za kisiasa, kijamii, kijinsia, kiuchumi, kikabila, kitamaduni, kidini na nyinginezo. Wataalamu wa masuala ya jamii ya uhamiaji na uhamishwaji wa lazima¹ wanatofautisha kati ya msukumo na mvuto, ambayo yote kwa pamoja yanajulikana kama sababu za kimuktadha za kusukuma au kuvuta watu kutoka nyumbani. Wahamiaji wanalazimika kuondoka nyumbani na/au kuamua kwa hiari kuondoka ilhali wakimbizi wanalazimishwa kukimbia vita au mateso katika nchi zao (tazama Moduli 2). Mambo yanayovuta ni motisha kwa wahamiaji kufika katika nchi wanazonuia. Msingi wa moduli hii ni dhana teule za masuala ya kijamii ya uhamiaji. Inatoa muhtasari wa mambo muhimu ya kusukuma na kuvutia ambayo huwang'oa makwao wahamiaji au wakimbizi, na hapa tunaangazia wakati wahamiaji na wakimbizi haswa wanapohusiana. Baadhi ya mambo haya yatafafanuliwa zaidi katika changanuzi kifani za nchi (Moduli 6-8), mitazamo kutoka Afrika (Moduli 9) na mitazamo ya kimataifa (eneo la MENA, Asia, Marekani na Shirikisho la Urusi — tazama tovuti ya mradi www.mediaandmigration.com).

1 Kwa ufafanuzi wa uhamiaji wa kulazimishwa, wahamiaji na wakimbizi angalia Moduli 2 na faharasa zinazopendekezwa: (UNHCR, n.d.; EMN, 2018; IOM 2019a).

Utaalamu

Uhamiaji ni kipengele muhimu cha maisha ya binadamu, na watu wamehama tangu wanadamu wa kwanza walipotoka Afrika ya Kati hadi mabara mengine. Katika historia ya wanadamu, watu daima wamekuwa wakihama, kwa hiari au kwa kulazimishwa (Bellwood, 2013). Hata hivyo, mara nyingi walichukuliwa kuwa tu wageni (IOM, 2019a, uk. 6).² Hadi kufikia karne ya 20, wakimbizi hawakuwa suala muhimu kwenye ajenda ya kimataifa; kabla ya Vita vya Kwanza vya Dunia, walitendewa kama wageni kulingana na sheria za kila taifa, na hapakuwa na sera ya kimataifa iliyoshughulikia hali maalumu ya wakimbizi. Vita vya Kwanza vya Dunia (1914-1918) vilifurusha mamilioni ya Wazungu, ambao wengi wao walilazimika kutafuta makao katika nchi za kigeni. Mkataba wa 1933 Kuhusiana na Hali ya Kimataifa ya Wakimbizi ulikuwa wa kwanza uliohitaji mataifa ya ulimwengu kuuzingatia kisheria (Kugelmann, 2010, uk. 18-19). Yakiwa makubaliano ya kwanza, yalishughulikia pia hati za usafiri, hadhi ya kibinafsi, ajira, haki za kijamii, elimu, kufukuzwa na mengineyo. Uhamaji wa kulazimishwa, ulanguzi wa binadamu na utumwa barani Afrika, hata hivyo, yalibakia kuwa mambo yasiyo ya kawaida katika jukwaa la kimataifa hadi miaka ya 1960. Ujio wa wakoloni na tamaa ya upanuzi wa milki za kifalme kutoka nje ziliandamana na safari za masetla walowezi waliokalia ardhi za wengine, bila kujali maisha za wenyeji wao za hapo awali, tamaduni, lugha na umiliki wa mali na kutojali kabisa kuhusu athari za tendo hilo.

Uwanazuoni fadhili kuhusu uhamiaji ulianza mwishoni mwa karne ya 19 na mwanzoni mwa karne ya 20 (Aigner, 2017). Kulingana na uchanganuzi wa awali wa mtiririko wa uhamiaji uliofanywa na mwanasayansi Mjerumani-Mwingereza Ravenstein (1876; 1885; 1889), wahamiaji huwa wanatafuta kuboresha hali zao za maisha, haswa mali. Katika muktadha wa kihistoria wa uhamiaji mkubwa kutoka Ulaya hadi Marekani mwishoni mwa karne ya 19, zaidi ya Wajerumani milioni 60, raia wa Uswizi, Ireland, Italia, Poland na Wazungu wengine wengi walihamia Amerika Kaskazini na Kusini kukitafuta maisha bora. Nadharia za uhamiaji za mwanzoni mwa karne ya 20 zililenga ujumuishaji wa wahamiaji, wanaochukuliwa kuwa wageni, katika tamaduni tofauti tofauti za jamii mwenyeji (kwa mfano Park, 1928). Wakati mhamiaji huyo akielezwa kuomba kukubalika, jamii zilizompokea zilielezwa kuwa zinatafuta uaminifu wa mhamiaji huyo. Mchakato wa uhamiaji uliundwa kama seti ya hatua ambazo wahamiaji walikuwa wakipitia, ambazo pia ni pamoja na awamu za ushindani kati ya wahamiaji na jamii zinazowapokea, na migogoro. Wasomi wa awali walisisitiza lengo la wahamiaji kujihusisha kikamilifu na jamii lengwa, huku tafiti zilizofuata pia zikizingatia athari za utamaduni wa wahamiaji kwenye utamaduni wa jamii mwenyeji, zikisisitiza umoja katika wingi wa watu tofauti na tamaduni mbali mbali. Pia, makabila tofauti yalipatikana kuwa na njia na uwezo tofauti wa kukabiliana na usimilishaji (kwa mfano Eisenstadt, 1953).

Ni katika katikati ya karne ya 20 tu ambapo mwelekeo wa kitaaluma uliwageukia wahamiaji na nia zao halisi. Kuzorota kwa usalama na upungufu unaonekana katika nchi za asili husukuma watu kuhama, kwa matumaini ya kuondokana na upungufu huu; lakini matatizo mapya ya usa-

2 Kwa ufafanuzi wa wageni, angalia faharasa zinazopendekezwa katika Moduli 2: (EMN, 2018; IOM, 2019a).

lama huibuka baada ya kuwasili ugenini. Nia tofauti huathiri maamuzi ya wahamiaji. Mchango muhimu katika mjadala ulitolewa na mfano wa Lee wa mambo yanayosukuma na kuvutia (1966). Kama jaribio la kwanza la kitaratibu la kuchanganua mambo yanayoathiri maamuzi ya uhamiaji, Lee alitofautisha kati ya misukumo ya kiuchumi, kijamii, kisiasa, kidini, kibinafsi/familia na mazingira: Ukosefu wa kazi, mizozo ya kivita, kutovumiliana kidini, njaa, na ukame ni baadhi tu ya sababu zinazowasukuma watu kuamua kuondoka nyumbani. Mambo yanayomsukuma mtu kuhama yanaweza kutokana na hiari yake, kutegemea mambo mengine au kuchanganyana na vivutio: Watu huhamia nchi wanazokusudia wakitafuta usalama, uhuru wa kisiasa na wengine, elimu na ajira katika soko za kazi ambazo zinahitaji wafanyakazi (wenye ujuzi wa juu na wa chini). Utafiti umejumuisha hatua kwa hatua vipengele vya kitamaduni na kijamii vya uhamiaji. Utafiti umeendelea kuuweka uhamiaji katika muktadha wa kimataifa, ukisisitiza muingiliano na wingi wa makabila na tamaduni (kwa mfano Glazer & Moynihan, 1963) na kuangazia mvutano uletwao na kukosekana kwa usawa wa jamii, na kuchochea hamu ya kuhama kati ya wanajamii wanaochukuliwa kama nguvu kidogo na isiyo na fahari kubwa (kwa mfano Hoffmann-Nowotny, 1970). Kimataifa, uhamiaji unaweza kunufaisha masoko ya kazi yaliyojaa katika nchi za asili kwa upande mmoja, na nchi wanazonuia kuhamia na ambazo zinahitaji nguvukazi kwa upande mwingine (Sassen, 2007). Ingawa uhamiaji wa watu wenye maarifa na stadi mbali mbali za kazi unaweza kudhoofisha jamii wanakotoka na kufaidi nchi zinazowapokea, uhamiaji mduara³ unaweza kufaidi pia nchi asili ambapo wahamiaji hurudi nyumbani (Constant, 2020, uk. 5). Nchi asili na nchi mwenyeji mara nyingi huunganishwa na mifumo ya kihistoria (ya kikoloni), mahusiano ya kitamaduni na kikabila, mahusiano ya desturi za kibiashara, lugha, dini na mengineyo ambayo pamoja, huunda mfumo wa uhamiaji, unaounganishwa na miamala ya kifedha (fedha zinazotumwa nyumbani na wahamiaji) na mawasiliano (tazama maelezo yanayofuatia). Mawasiliano kati ya watu wa jamii zinazotuma watu nje ya nchi zao na wenzao wanaoishi nje ya nchi yanaweza kuchochea uhamiaji zaidi, hali inayowezeshwa zaidi na kupungua kwa umbali kutokana na mafanikio ya kiteknolojia (Douglas na wengine, 1994). Intaneti na mitandao ya jamii huwawezesha wahamiaji wa kimataifa kuendeleza uhusiano wa karibu katika nchi wanakotoka, hivyo basi kuongeza idadi ya walio na utambulisho mseto (Dekker & Engbersen, 2014).



ZOEZI LILILOPENDEKEZWA ZA KUSHUGHULIKIA STADI ZA UTAMBUZI WA KUTEKELEZA NA STADI ZA MITAZAMO YA KIBINAFSI KATIKA KUPOKEA:

Washiriki wanapaswa kuangazia nchi yao ya asili na kuandika hadithi ya maneno 4,000 kwa vyombo vya habari vya vyuo vyao wakijibu swali la utafiti: “Ni nini historia ya uhamiaji na uhamiaji katika nchi yetu?!”

- Chunguza angalau makala au vitabu viwili vya kitaaluma kuhusu historia ya uhamiaji ya nchi yako.
- Eleza nchi yako kama mahali pa wahamiaji wa nje na ndani ya nchi. Ili kukusanya data muhimu, tumia ukurasa wa nchi yako katika Tovuti ya Data

3 Kwa ufafanuzi wa “uhamiaji mduara”, angalia faharasa zinazopendekezwa katika Moduli 2: IOM (2019a); EMN (2018).

ya Uhamiaji (2020d). Hakikisha umefafanua kuwa wahamiaji wa kimataifa ni watu kutoka nje wanaoingia katika nchi na wananchi wanaohamia nchi nyingine.

- Hoji mhamiaji mzoefu ndani ya nchi na upime uzoefu wake kulingana na maandishi ya kitaaluma na data ulizokusanya.

Kumbuka: Ikiwa hadi sasa wanafunzi hawajasoma kuhusu itikeli za kuripoti, wanaweza kuwa hawajajiandaa vyema kuwahoji wahamiaji. Katika hali hii, badala ya kufanya mahojiano wabadilisha na badala yake wafanya utafiti wa ushuhuda na ithibati katika vyombo vya habari vya ndani au mashirika yasiyo ya serikali ama wahoji mwakilishi wa NGO ambayo inashughulikia wahamiaji ndani ya nchi (kwa mfano IOM).

Uhamiaji na maendeleo

Mtazamo mwingine unaofaa kwa mjadala kuhusu uhamiaji ni jukumu la maendeleo. Watunga sera mara nyingi hujikuta kwa shinikizo linaloongezeka la umma kupigana na sababu kuu za uhamiaji. Dhana ya wazi ni kwamba — pamoja na mikataba ya kibiashara yenye manufaa zaidi na ushirikiano wa kiuchumi — kuongezeka kwa ushirikiano wa maendeleo na misaada ya kigeni kuna athari kwa uhamiaji: Uboreshaji wa hali ya maisha unaweza kupunguza misukumo ya kuhama, na hivyo kupunguza uhamiaji (Lanati & Thiele, 2017). Hata hivyo, uchanganuzi unaoonyesha kuwa ushirikiano wa kimaendeleo una taathira za kutatanisha katika uhamiaji, hata mtu asipozingatia ushahidi unaoonyesha kuwa sehemu husika ya misaada rasmi ya maendeleo (ODA) haiwafikii wananchi bali inamezwa kifisadi na wenye mamlaka (Alesina & Weder, 2002; Asongu, 2012). Kulingana na baadhi ya tafiti, idadi ya wahamiaji wanaoondoka huenda sambamba na kukua kwa mapato na elimu bora, na inapungua mara tu nchi inapofikia kiwango cha juu kila mwaka cha matumizi ya bidhaa na huduma kwenye uchumi wa taifa (GDP). Kwa hivyo, kulingana na utafiti kama huo, maendeleo — angalau mwanzoni — yanasadifiana na kuongezeka kwa kasi kwa viwango vya uhamiaji kwa sababu maendeleo ya kijamii na kiuchumi yanawezesha na kuwahamasisha watu kuhama (de Haas, 2007). Kwa kuchukua nadharia ya mpito ya uhamaji ya Zelinsky (1971) na kazi ya Martin & Tayler (1996) kama sehemu za kuanzia, athari za maendeleo katika uhamiaji na uhamaji katika maendeleo (kwa mfano, kupitia utumaji pesa nyumbani) zimejadiliwa kwa karibu miaka 50. Tamshi muhimu la kuvumisha ni “nadharia ya panda-shuka za uhamiaji” (Martin & Taylor, 1996).

Sambamba na wazo hili, ushirikiano wa kimaendeleo na nchi za kipato cha chini unaweza kusaababisha uhamiaji zaidi. Belloc (2011) anaonyesha katika utafiti wa nchi 48 za Afrika za kusini ya Jangwa la Sahara kwamba kile ambacho mara nyingi huitwa ‘misaada ya kigeni ya maendeleo’ au ODA, “ina matokeo mazuri na ya kitakwimu kwa uhamiaji” (Belloc, 2011, uk. 187). ODA inaweza kuchochea uhamiaji kwani fedha mara nyingi husaidia taasisi zinazoruhusu watu

kujenga uwezo wao na hivyo kupata fursa mpya za ajira (elimu, sekta za biashara, mawasiliano, miundombinu na mengineyo). Lakini kudhibiti mtiririko wa uhamaji na sera za maendeleo inahitaji kuchochea ukuaji wa uchumi usio na kifani katika nchi nyingi zinazoendelea” (Dao na wengine., 2018, uk. 32).



ZOEZI LILILOPENDEKEZWA LA KUSHUGHULIKIA STADI ZA UTAMBUZI ZA UELEWA NA STADI ZA MITAZAMO YA KIBINAFSI NA MAADILI ZA KUPOKEA:

Alika darasa lisikilize kauli ya video ya Eric Chinje, rais wa zamani wa AMI (tazama tovuti ya mradi www.mediaandmigration.com)

Waagize wanafunzi waeleze uhusiano kati ya uhamiaji na maendeleo.

Afrika Kaskazini inaweza kuwa mfano kwa sababu wengi wa watu wanaohamia Ulaya wana asili ya kutoka nchi za kipato cha chini za Afrika Kaskazini,⁴ hasa Morocco, Algeria na Tunisia. Kwa jumla, wahamiaji si miongoni mwa maskini zaidi katika jamii zao lakini wanawakilisha wale ambao wamepata njia ya kufikia uamuzi wa uhamiaji au wameweza kukusanya fedha zinazohitajika katika jumuiya zao (de Haas, 2010a, uk. 239). Wahamiaji wa Kiafrika wanaoenda Ulaya wana baadhi ya hali na mali zinazowawezesha kufanya safari ngumu na ya hatari: ujana, nguvu, fedha na uwezo wa kujitafutia pesa safirini, wana marafiki ughaibuni wa kuwaonyesha njia, kubadilishana namba za simu na kusambaziana habari, na familia kubwa nyumbani ambazo huendelea kuwatumia pesa (tazama sehemu ya mitandao/ughaibuni hapa chini). Simu smati ni mshirika hodari wa kila mtu.

Uhamiaji — “habari njema”, “habari mbaya”?


Vyombo vya habari huwa vinazingatia matukio makubwa katika mchakato wa uhamiaji. Kulingana na moja ya tafiti zetu linganishi (kwa maelezo zaidi juu ya utafiti na jinsi vyombo vya habari vinaripoti, tazama Moduli 4), majanga ya ajabu ya mashua na meli katika Bahari ya Mediteranean yanayohusisha wahamiaji kutoka Afrika yametawala habari za uhamiaji katika vyombo vya habari vya Afrika na pia Ulaya (tazama Kielelezo 7).

Raia wengi na watunga sera barani Afrika kwa muda mrefu wamekuwa hawafahamu kuhusu hali ngumu mara nyingi, na katika nyakati nyingi hali ya kinyama ambayo wahamiaji hukabiliana nayo safirini. Ilikuwa ni ripoti ya televisheni ya CNN kuhusu Waafrika kuingizwa utumwani katika kambi za Libya ambayo ilisababisha viongozi wa Afrika kuzungumzia suala hilo hadharani wakati

4 Tazama Moduli 2 kwa usuli juu ya uainishaji huu wa nchi ambao umefafanuliwa katika UNDESA (n. d.). Kufikia 2020, nchi zote za Afrika Kaskazini ni nchi za kipato cha chini isipokuwa Libya ambayo ni ya juu-kati (Serajuddinnada & Hamadeh, 2020).


wa mkutano wa Umoja wa Afrika (tazama Moduli 5). Vyombo vya habari katika nchi nyingi za Afrika pia vilipokea habari kuhusu mashambulizi ya chuki katika Afrika Kusini yaliyofanyiwa wahamiaji kutoka nchi nyingine za Afrika (Bornman & Cronjé, 2020). Ukiukaji wa haki za bina-damu na uhalifu dhidi ya wahamiaji Waafrika katika Ghuba ni baadhi ya visa ambavyo haviripo-tiwi inavyofaa. (Best, 2019; Thorogood, 2019).

Vyombo vya habari vinahitaji kuripoti matukio makubwa kama yale yaliyoelezwa hapo awali lakini sio lazima yaishie hapo, kwa sababu zaidi ya janga hilo, kuna hadithi ambazo zinawapa umma



mtazamo mpana: Ni nini kimewafukuza waathiriwa kutoka nchi yao? Je, wahamiaji wanakumba-na na hali na uhalisia gani katika nchi wanakoenda? Nini kinatokea katika usafiri? Moduli zina-zofuata zinatoa msukumo wa jinsi ya kupata vipengele bora zaidi vya habari ili kuuleza umma ukweli unaofaa wanaohitaji kuujuua, jinsi ya kukabiliana na matatizo ya kiitikeli (tazama Moduli 10 na 11), na jinsi ya kuuza hadithi za uhamiaji kwa wahariri (tazama Moduli 13). Vipengele vya kusukuma na kuvutia huathiri maamuzi ya mtu binafsi ya uhamaji na safari kubwa za uhamaji. Hata hivyo, ingawa vipengele hivi vya kusukuma na kuvutia ni maarifa muhimu ya usuli, vinao-nekana sio tosha kwa habari zenyewe. Mwongozo huu unalenga kufichua hadithi nyingi muhimu za habari zilizofichwa katika maarifa ya usuli ambazo zinangoja tu kuibuliwa.

Chinyere Stella Okunna, Profesa katika Idara ya Mawasiliano ya Umma, Chuo Kikuu cha Nnamdi Azikiwe, Awka, Jimbo la Anambra, Nigeria:



Chanzo : Binafsi

“Vyombo vya habari kwa kiasi kikubwa viko kimya kuhusiana na masuala ya uhamiaji, au vinatoa ripoti chanya kuhusu uhamiaji, kulingana na maoni ya umma na sera ya serikali juu ya uhamiaji, isipokuwa katika mazingira ya kutishia maisha kama vile mashambulizi ya hivi karibuni ya chuki kwa wageni nchini Afrika Kusini au kashfa ya biashara ya utumwa Libya iliyotajwa awali. Kuhusu kuripoti, kesi bora zaidi inajitokeza kwenye ripoti ya kurejeshwa kwa wahamiaji wa Nigeria kutoka Afrika Kusini kufuatia mashambulizi ya hivi karibuni yaliyochochewa na chuki kwa wageni. Ripoti ya maslahi ya kibinadamu kuhusu suala hili ilionyesha warejea wa Nigeria wakionyesha uzalendo wa hali ya juu katika kujituma kuimba wimbo wa taifa wa Nigeria wakati mmiliki wa Shirika la Ndege la Peace (Bw. Allen Onyema) alipofika kuwakaribisha waliorejea na kuingia ndani ya ndege yake iliyowarudisha nyumbani bila malipo — tukio lililosababisha wengi wa waliorejea na pia Bw. Onyema mwenyewe kumwaga machozi ya furaha na uzalendo. Ripoti kama hizo za kihemko na za kizalendo zinaweza kuzuia wimbi la uhamiaji kutoka Nigeria.”



ZOEZI LILIOPENDEKEZWA LA KUSHUGHULIKIA STADI ZA UTAMBUZI WA KUTEKELEZA:

Watambulishe wanafunzi wako kwa baadhi ya ushuhuda, kwa mfano kutoka kwa tovuti I am a migrant (IOM, 2017). Eleza ni misukumo na/au mambo gani ya kuvutia yanayoweza kusababisha uamuzi wa wahamiaji kuondoka kutoka nchi zao. Baada ya kuonyesha jinsi ya kutumia ushuhuda kuelezea vipengele hivi vya kusukuma/kuvutia, lialike darasa kutafsiri mambo ambayo huenda yalichochea uamuzi wa wahamiaji kuondoka kutoka nchi zao.

Timu ndogo zina jukumu la:

- Kuchagua ushuhuda mmoja kutoka kwa tovuti “*I am a migrant*” (IOM, 2017);
- Kutafuta ushuhuda mwingine wa wahamiaji (kwenye tovuti za taasisi, vyombo vya habari vya kitaifa au kutoka kwa mikutano ya kibinafsi).

ZOEZI LILILOPENDEKEZWA KWA DARASA LA KUSHUGHULIKIA STADI ZA UTAMBUZI ZA KUTATHMINI NA STADI ZA MITAZAMO YA KIBINAFSI NA MAA-DILI ZA KUJIBU:

Liambie darasa likusanye orodha ya vipengele vya kusukuma na kuvutia vilivyotajwa katika ushuhuda huu. Kila mshiriki anaweza kuandika tathmini fupi juu ya nguvu ya uthibitisho, akizingatia majibu ya maswali yafuatayo:

1. Je, ushuhuda huwasaidia wengine — kwa mfano wewe mwenyewe — kukuza uelewa bora wa wahamiaji?
2. Je, ushuhuda huwasaidia wahamiaji kujieleza wenyewe kwa maoni yako?
3. Hatimaye, aya watakayotayarisha itatoa mawazo ya kina juu ya mada “Mimi ni mhamiaji”: Je, mada hii inaunga mkono ujumuishaji wa wahamiaji katika jamii inayowapokea au inawatenga na kuwasukumizia dhana potovu zisizo na msingi — ama swali elekezi liwe bora zaidi kwa kuuliza “Mimi si mhamiaji! Basi mimi ni nani”?

Kuangazia yanayowasukuma na kuwavutia wahamiaji na wakimbizi

Huenda likawa ni jambo la kuwazindua wanafunzi katika Afrika na Ulaya ili kuangazia kwa makini misukumo na mambo ya kuvutia, kwani dhana potofu na kupuuzwa na vyombo vya habari huenda zikaendelea kuathiri mtazamo. Kwa mfano, ripoti zinazotolewa Ulaya za uhamiaji kwa muda mrefu zimekuwa zikidokeza kwamba watu huondoka kutoka nchi zao kwa sababu ya vita au migogoro (Berry na wengine, 2015), kauli ambayo ni kweli kwa kiasi kidogo tu kuhusu uhamiaji wa sasa wa kutoka bara moja hadi jingine (angalia Moduli 1 na 9 na sehemu za migogoro, uchumi, fedha kutoka nje na mabadiliko ya hali ya hewa katika maelezo yanayofuata). Kwa upande mwingine, Waafrika wengi hawajui mitazamo halisi ya kisiasa, kiuchumi, kijamii na kibinafsi ambayo wahamiaji wanakumbana nayo Ulaya (Zappe na wengine, 2019).

Vipengele vichache vilivyochaguliwa vya misukumo vinaweza kutumika kama chanzo cha mjadala: Ingawa uchumi wa nchi nyingi za Kiafrika umepata viwango vya juu vya ukuaji tangu 2000, na licha ya utajiri wa maliasili (Devarajan & Fengler, 2013; UNDESA, 2005, uk. 90-93; UNDESA, 2010, uk. 125-127; Benki ya Dunia, 2020a), umaskini bado ni hali halisi katika jumuiya nyingi za Kiafrika, hata katika nchi zenye ukuaji wa uchumi (Wilhelm, 2020). Mabadiliko ya hali ya hewa huongeza viwango vya hatari kupitia ukame, kupanda kwa kina cha bahari, mafuriko, misimu ya mvua isiyotegemewa na mambo mengine (Adenle na wengine, 2017). Wakati nchi nyingi za Kiafrika zimepata uzoefu mkubwa wa mageuzi ya kisiasa (Decalo, 1992; Lynch, 2011), mivutano mbalimbali inatawala, na nchi kama Cameroon, Chad, Mali, Nigeria, Rwanda, Sudan, Sudan Kusini, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (tazama Moduli 7) na nyinginezo zimekumbwa na machafuko au vita vya wenyewe kwa wenyewe (Alcorta na wengine, 2020; Moscona na

wengine, 2018; Ottoh, 2018). Miundombinu duni ya umma ni sababu nyingine inayosukuma wananchi wengi wa Afrika kutoridhishwa na kiwango cha elimu, huduma za afya na huduma nyingine za umma (nishati, mtandao, usafiri n.k.; Benki ya Dunia, 2017). Pesa zinazotumwa kutoka nje zimechangia pakubwa kimaendeleo na ni “njia iliyothibitishwa ya kugawana ustawi” (Benki ya Dunia, 2019, uk. 15).

Katika siku za usoni, maendeleo ya kidemografia katika Afrika na Ulaya yataathiri pakubwa mambo ya kusukuma na kuvutia na kuzidisha tofauti kati ya mabara. Idadi ya watu duniani inaendelea kukua na inakadiriwa kuongezeka kwa watu bilioni mbili⁵ kati ya 2020 (bilioni 7.7) na 2050 (bilioni 9.7); zaidi ya nusu ya ukuaji huo utatokea katika nchi za Afrika za kusini ya Jangwa la Sahara, eneo linalotarajiwa kuwa na watu wengi zaidi duniani ifikapo 2062 (UNDESA, 2019a, uk. 6). Ongezeko la idadi ya watu ni “nguvu isiyoweza kukomeshwa” (Dao na wengine, 2018, uk. 11), na ni kiashiria kikuu cha uhamaji. Inatabiriwa kwamba kutakuwa na “shinikizo kubwa la uhamiaji” (Dao na wengine, 2018, uk. 31), na hasa kwenda Ulaya, kutokana na mabadiliko ya kidemografia katika nchi za Afrika za kusini ya Jangwa la Sahara na hasa katika baadhi ya nchi za MENA (Dao na wengine, 2018, uk. 31-32). De Haas, hata hivyo, anakumbusha kuhusu ukweli kwamba watu hawahami “kwa sababu ya” ongezeko la watu bali kwa sababu ya mambo mengine (kwa mfano uchumi uliodorora, ukosefu mkubwa wa ajira) ambayo yanazidisha athari za msongamano mkubwa wa watu (2010b). , uk. 12). Kwa mfano, ongezeko kubwa la watu katika mataifa ya Ghuba yenye utajiri wa mafuta pamoja na kasi ya ukuaji wa uchumi halihusiani na ongezeko la viwango vya wahamaji — lakini, kinyume chake, ni viwango vya chini vya nguvu za uzazi katika Ulaya Mashariki ambapo uchumi umedumaa ambavyo vinalingana na viwango vya uhamaji (de Haas, 2010b, uk. 12).

Kutafiti uhamiaji na uhamishwaji wa lazima kutoka Afrika kwenda Ulaya chini ya dhana ya usalama wa binadamu, Giménez-Gómez na wengine (2019, uk. 1797) wanarejelea mchanganyiko wa misukumo na mambo ya kuvutia yanayoshawishi safari za watu binafsi; “hasa, kuongezeka kwa mateso ya kisiasa, [...], ukiukaji wa haki za binadamu, ukosefu wa utulivu wa kisiasa na migogoro ya wenyewe kwa wenyewe” pamoja na migogoro ya kikabila (Giménez-Gómez na wengine, 2019, uk. 1797). Imekubaliwa kote kwamba sababu za jumla za kusukuma/kuvutia hazielezei vya kutosha uhamiaji na kwamba ni nadra sana watu kushawishiwa na sababu moja. Viwango viwili vya kusukuma na kuvutia hufanya kazi kwa mshikamano, na vivyo hivyo vipengele husika, vinavyoshawishi watu kuamka-na-kwenda. Uhusiano kati ya vipengele mbalimbali vinavyowashawishi watu kuhama nchi zao za asili, kuamua watapitia wapi na safari zao zitaishia wapi usafiri hufanya iwe vigumu kutenga jukumu la viendeshaji huru. Hili wakati mwingine husababisha ugumu kwa mara ya kwanza kubainisha kati ya mhamiaji na mkimbizi — kwa mfano, wakimbizi ambao wamekimbia mateso kwa kuvuka mipaka ya nchi wanaweza kulazimika kuhamana tena kufuatia majanga kama vile dhoruba, mafuriko au mengineyo. Uwiano kati ya vipengele vya kusukuma na kuvutia umelezewa vyema, kwa mfano fursa za kiuchumi zikilinganishwa na changamoto, amani dhidi ya migogoro, ulinzi dhidi ya mateso (Docquier na wengine, 2014; Hooghe na wengine, 2008). Dhana ya mitazamo mingi inatumika pia wakati mkazo unapotiliwa

5 Nambari na desimali zimefanywa herufi kamili katika maandishi haya katika juhudi za kuweka uwiano mzuri kati ya usahihi na usomaji.

kwenye mambo ya kusukuma pekee: Watu ambao maisha yao yako hatari kutokana na mateso ya kisiasa mara nyingi pia huathiriwa na ukosefu wa usalama wa kiuchumi ambao unahatarisha maisha yao (Braithwaite na wengine, 2014; Chuo Kikuu cha Maastricht, & GMDAC, 2016; Giménez -Gómez na wengine, 2017). Hanlon & Christie (2016) wanaona viwango vya migogoro na ukosefu wa utulivu, pamoja na viwango vya juu vya wasio na ajira na viwango vya chini vya ujira, hasa miongoni mwa vijana, kama mchanganyiko wa mambo yanayosukuma uhamiaji.

Kuongezeka kwa madhara ya mazingira yanayopunguza rasilimali za watu kunaweza pia kusababisha migogoro na vurugu (Raleigh, 2011). Freeman (2017) ametafiti uwiano huu kwa Afrika, wakati Gleick (2014) alitanguliza katika kuelezea chanzo cha vita nchini Syria kuwa:

“matokeo ya mambo changamani yanayohusiana. Lengo la mzozo huo ni kuleta mabadiliko ya serikali, lakini vichochezi ni pamoja na mambo mengi ya kidini na kijamii, kuzorota kwa hali ya kiuchumi, wimbi la mageuzi ya kisiasa linalokumba Mashariki ya Kati, changamoto za [mabadiliko ya] hali ya anga [...] na upatikanaji na matumizi ya maji safi” (Gleick, 2014, uk. 331).

Afifi (2011) anaonyesha kuwa masuala ya mazingira (kwa mfano ukame, uharibifu wa udongo, ukataji miti) yanazidisha kwa kiasi kikubwa ukosefu wa usalama wa kiuchumi na uhamiaji nchini Niger. Akichanganua data kutoka nchi 45 za Afrika za kusini ya Jangwa la Sahara kati ya 1965 na 2005, Naudé (2008) anaonyesha ongezeko la idadi ya watu na athari zake kwa mazingira, hali inayoathiri shughuli za watu kwa kusababisha migogoro na ukosefu wa ajira. Ongezeko la idadi ya watu na uhaba wa rasilimali vinaweza kusababisha migogoro kuhusu usalama wa rasilimali, na kuzidisha shinikizo la kutoroka (Borderon na wengine, 2019).

Baadhi ya vipengele vya muktadha vinajitokeza — hivi hasa ni viashirio vya kiuchumi na migogoro kama sababu za kusukuma; na amani, heshima kwa haki za binadamu na ulinzi na utambuzi wao pamoja na viwango bora vya maisha kama mambo ya kuvutia. Ongezeko la idadi ya watu na mawasiliano (uanahabari, mitandao ya jamii, mawasiliano ya kibinafsi kati ya wahamiaji na pia jumuiya za makabila yao na wenzao wanaohama na mengineyo) ni mambo mtambuka ya muktadha yenye umuhimu mkubwa. Vipengele vilivyochaguliwa vya misukumo na mambo ya kuvutia havikusudiwi kujumlisha lakini vinajumuisha baadhi ya masuala muhimu ya muktadha wa uhamiaji na uhamishwaji wa lazima.

Ongezeko la idadi ya watu

Tukikumbuka kwamba de Haas (2010b, uk. 12) anaonya dhidi ya kuangalia ongezeko la watu kama msukumo pekee wa watu kuhama kwani watu hawahami “kwa sababu ya” ongezeko la watu bali kwa sababu ya mambo mengine (tazama simulizi la awali). Sehemu hii inaangazia baadhi ya takwimu na muktadha. Idadi ya watu duniani inakadiriwa kuongezeka kwa watu bilioni

mbili kati ya 2020 (bilioni 7.7) na 2050 (bilioni 9.7)⁶. Kati ya watu hawa bilioni mbili, bilioni 1.5 watatoka nchi 22 duniani kote ambapo 12 ni za Afrika za kusini ya Jangwa la Sahara (UNDESA, 2019a, uk. 13, Kielelezo 6). Nchi 10 kati ya hizi 12 za Afrika ni miongoni mwa nchi zilizo nyuma kimaendeleo (UNDP, 2019b, uk. 2-5)⁷. Kwa mfano, katika muda huo huo (2020-2050), idadi ya watu wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo inatarajiwa kuongezeka kutoka milioni 87 hadi karibu milioni 200, idadi ya watu wa Nigeria inatarajiwa kuongezeka mara mbili kutoka milioni 200 hadi milioni 400, na idadi ya watu Tanzania pia itaongezeka maradufu — kutoka milioni 58 hadi milioni 129; idadi ya watu Ethiopia itaongezeka kutoka milioni 112 hadi 205, na idadi ya watu wa Misri itaongezeka kutoka milioni 100 hadi milioni 160. Kama eneo linalokua kwa kasi zaidi duniani, Afrika inatarajiwa kuwa na watu zaidi ya bilioni mbili ifikapo 2050, kumaanisha kwamba idadi ya watu katika nchi za Afrika za kusini ya Jangwa la Sahara inakadiriwa kuongezeka maradufu kufikia wakati huo (UNDESA, 2019a, uk. 6, Jedwali 1). Mnamo 2019, kiwango cha uzazi cha nchi 36 ulimwenguni kilikuwa zaidi ya jumla ya watoto wanne kwa kila mwanamke, huku nchi 33 za Afrika zikiwa katika kundi hili. Kiwango cha uzazi cha 4.6 kwa kila mwanamke, kinazidi wastani wa kimataifa wa watoto 2.5 kwa kila mwanamke (UNDESA, 2019a, uk. 23). Baada ya 2050, inatarajiwa kuwa Afrika itakuwa eneo pekee ambalo bado linakabiliwa na ongezeko kubwa la idadi ya watu huku idadi ya watoto wanaozaliwa ikiongezeka licha ya kushuka kwa viwango vya uwezo wa kuzaa (UNDESA, 2019a, uk. 24).

Ingawa watoto wengi huzaliwa Asia, tukiangazia idadi kamili, wanawake katika nchi za Afrika za kusini ya Jangwa la Sahara wana wastani wa idadi kubwa zaidi ya watoto. Wakati huo huo, wamo hatarini kubwa ya kiafya wakati wa ujauzito na kuzaa kwa sababu vifo vya uzazi na watoto wachanga ni vingi kuliko mahali pengine popote ulimwenguni. Tofauti na Afrika, idadi ya watu inapungua katika baadhi ya nchi za Ulaya na Asia kwa sababu watoto wachache huzaliwa kuliko wanaohitajika kuchukua nafasi ya kizazi cha wazazi (Sippel na wengine, 2011, uk. 13).

Idadi ya vijana ikilinganishwa na jumla ya watu katika nchi wanakotoka wahamiaji ni kigezo muhimu cha kupimia kiwango cha uhamaji na uhamiaji. UNDESA inakadiriwa kuwa idadi ya wahamiaji wa kimataifa walio na umri wa chini ya miaka 19 ilipanda kutoka milioni 29 mwaka 1990 hadi milioni 38 mwaka 2017 (Migration Data Portal, 2020a). Afrika ina idadi kubwa ya vijana duniani kote, ambayo mara nyingi huadhimishwa kama “mgawo wa faida”, na wakati mwingine inahofiwa kuwa “janga” (Canning na wengine, 2015). Ongezeko la kasi la idadi ya watu barani Afrika linachanganya serikali nyingi za Kiafrika. Chukua elimu nchini Nigeria kwa mfano: Watu

6 Hii ni kulingana na makadirio ya thamanikati kigeu. Kumbuka kwamba wanademografia kwa kawaida husisitiza kwamba makadirio si utabiri, ingawa thamanikati kigeu ya Umoja wa Mataifa hutumiwa kwa madhumuni hayo. Kwa vile mwelekeo wa idadi ya watu duniani kote unasukumwa kwa kiasi kikubwa na uzazi, makadirio haya pia yanatokana na dhana kwamba viwango vya uzazi vitaendelea kupungua. Wastani wa uzazi wa maisha ya watoto 2.1 wanaozaliwa hai kwa kila mwanamke ni takriban kiwango kinachohitajika kwa idadi ya watu walio na vifo vya chini kuwa na kiwango cha ukuaji cha sifuri katika muda mrefu (UNDESA, 2019a). Kiwango cha uingizwaji kinaweza kutofautiana na wastani wa watoto 2.1 wanaozaliwa hai kwa kila mwanamke (kwa mfano nchini Niger ni zaidi ya watoto watatu wanaozaliwa hai kwa kila mwanamke).

7 Nigeria, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Ethiopia, Tanzania, Uganda, Niger, Sudan, Msumbiji, Madagascar, Ivory Coast ni “maendeleo ya chini ya binadamu”, mbili (Angola, Kenya) ni “maendeleo ya kati ya binadamu”. Misri, si nchi ya Afrika katika kusini ya Jangwa la Sahara bali ni nchi ya Kiafrika, imeorodheshwa katika suala la maendeleo ya juu ya binadamu (UNDP, 2019a, uk. 301). Nchi zisizo za Kiafrika ambazo zitachangia ukuaji wa idadi ya watu kufikia 2050 ni za Asia (India, Pakistan, IndonAsia, Ufilipino, Bangladesh, Afghanistan) na USA (UNDESA, 2019a, uk. 13, Kielelezo 6).

milioni 16 wako katika kundi linalopaswa kuwa vyuoni ya wa elimu ya juu (miaka 18 hadi 22) lakini ni jumla ya asilimia 10 pekee waliojiunga na elimu ya juu mwaka 2011 (Benki ya Dunia & UIS, 2011). Mahabub (2014) anaeleza kuwa mahitaji ya elimu ya vyuo vikuu hukua sambamba na ongezeko la watu lakini mfumo wa elimu haustawi kwa kasi sawa. Manufaa ya ustawi wa kiuchumi kutokana na badiliko la muundo wa demografia, hasa kupunguka kwa vifo na kushuka kwa uwezo wa kuzaa, yatadhihirika pakiwa na mabadiliko ya sera za umma kwa kuzingatia udhibiti wa uzazi ili kusimamisha au kubadilisha ongezeko la idadi ya watu na kuimarisha hali ya wanawake, na hivyo kupunguza ukubwa wa familia na kuruhusu uwekezaji zaidi katika afya na elimu kwa kila mtoto na kundi la vijana walioelimika vilivyo tayari kwa kazi zinazolipa vizuri ambazo zimeundwa katika mazingira wezeshi (Canning na wengine, 2015; Sippel na wengine, 2011). Baadhi ya wanazuoni wanaonya kuhusu pingamizi muhimu zilizopo, ikiwa ni pamoja na wanasisia kujitolea shingo upande kuweka mikakati ya kupunguza haraka uwezo wa kuzaa, uhaba wa nafasi za kazi, kubaguliwa kwa wanawake na vijana, mishahara ya chini na huduma duni za kukinga jamii (Groth na wengine, 2019). Iwapo vijana wanaozidi kuongezeka watanufaika na ustawi wa kiuchumi kutokana na kupunguka kwa kasi ya ongezeko la watu na kushuka kwa idadi ya wanaokufa, hatua za haraka na zinazoonekana zinapaswa kuchukuliwa kuondoa pingamizi hizo. Hatua za kupata ustawi wa kiuchumi kutokana na mabadiliko ya muundo wa kidemografia, Sippel na wengine (2011) wanatumaini patakuwa na uwezeshaji wa wanawake, upangaji uzazi, elimu, huduma za afya, usalama wa kijamii, na kwamba hakutakuwa na “ustawi wa kiuchumi kutokana na kushuka kwa kasi ya uzazi na idadi ya vifo bila ajira” (Sippel na wengine, 2011, uk. 71). Kwa vijana wa leo katika nchi nyingi za Afrika, ushindani wa idadi ya watu unapunguza sana fursa. Matarajio ya juu, yasiposhughulikiwa ipasavyo, yanaweza kuongeza taabu na dhiki na kusababisha mambo mawili: “ondoka au toa sauti”, yaani, uhamiaji au maandamano (Baudassé na wengine, 2016).



ZOEZI LILILOPENDEKEZWA LA KUSHUGHULIKIA STADI ZA UTAMBUZI ZA UTEKELEZAJI:

Lialike darasa kutazama mahojiano ya dakika 4:48 na Dkt. Reiner, mkurugenzi wa zamani wa taasisi ya Berlin ya masuala ya idadi ya watu na maendeleo (Berlin Institute for Population and Development) inayoweza kupatikana katika tovuti ya mradi www.mediaandmigration.com.

Zitumie dhana zake na data kwa nchi yako au nchi yoyote unayoichagua na utafiti swali lifuatalo: Je, mabadiliko katika demografia yataathiri uhamiaji kwa njia gani katika nchi hiyo? Jenga hoja zako kwa kutumia tovuti ya Migration Data Portal kukusanya data mahususi ya nchi uliyoichagua.

Mbali na uhamiaji wa kimataifa, ongezeko la idadi ya watu pia huathiri uhamiaji wa kutoka vijijini hadi mijini. Kufikia 2050, inakadiriwa kwamba theluthi mbili za watu duniani wataishi katika miji. Kadiri idadi ya watu inavyoongezeka, sehemu ya rasilimali kwa wakazi wa vijijini ina-

pungua. Nguvu za umeme, chakula, maji, na nyumba zinaelekezwa vituoni vilivyo na watu wengi. Ukuaji wa mataifa yanayoendelea ni tofauti na ule wa mataifa mengi yaliyoendelea kwa kuwa katika nchi zinazostawi, hali hiyo haihusiani kabisa na nafasi za kazi zinazoundwa (Beauchemin & Bocquier, 2004; Liddle, 2017; Mount-ford & Rapoport, 2014; Oucho & Gould, 1993)

Migogoro

Migogoro imetambulika kama sababu kuu ya msingi kwa watu ambao walilazimika au kulazimishwa kuondoka nyumbani⁸ (Davenport na wengine, 2010; Chuo Kikuu cha Maastricht, & GDMAC, 2016; Giménez- Gómez na wengine, 2017; Hayes na wengine, 2016). Migogoro na fujo hujitokeza kama namna yoyote ya vitisho vya kweli au vinavyodhaniwa, kukosekana kwa utulivu, vita, kuzorota kwa usalama kwa jumla, mateso ya kisiasa, migogoro ya wenyewe kwa wenyewe na ya kikabila, ukiukwaji wa haki za binadamu, mapigano kati ya jumuiya au mashambulizi ya kiholela dhidi ya raia, na mara nyingi huzuka wakati wa mabadiliko ya mfumo wa kisiasa ya kidemokrasia (Adebayo, 2012). Mifano ni pamoja na Jamhuri ya Afrika ya Kati, Afrika Kusini na Kenya (Amodio & Chiovelli, 2017; André na wengine, 2019; Klopp & Zuern, 2007; Vlavonou, 2016), na mifano miwili ya Kiafrika katika mwongozo huu ni Cameroon (Mbuagbo & Akoko, 2004) na Guinea-Bissau (Ferreira, 2004). Katika mwauo wa maandishi kuhusu mambo muhimu ya kuvutia na kusukuma uhamaji unaohusiana na hifadhi (Chuo Kikuu cha Maastricht, & GDMAC, 2016), maandishi pia wanarejelea kazi za Naudé (2010), Schmeidl (1997), na Moore & Shellman (2004; ambazo zote zimetajwa katika Chuo Kikuu cha Maastricht, & GDMAC, 2016, uk. 21-22). Naudé aligundua kuwa katika Afrika mwaka wa ziada wa migogoro uliongeza uhamaji na uhamiaji kwa watu 1.7 kwa kila wakazi 1,000. Schmeidl anapendekeza kuwa aina tofauti za vurugu au ukosefu wa utulivu husababisha viwango tofauti vya uhamiaji wa uhamaji wa kulazimishwa (kwa mfano vurugu za jumla kama vile mauaji ya halaiki, vita vya wenyewe kwa wenyewe husababisha watu wengi kulazimika kuhama makazi yao). Moore & Shellman hutumia sampuli ya kimataifa ya nchi zilizo na data kutoka 1952 hadi 1995 kuhitimisha kwamba kadiri tishio lilivyo kubwa, ndivyo idadi ya watu wanaotoroka inavyoongezeka. Aina hizi mbalimbali za hatari nyumbani zinaweza pia kuwiana na dhiki ambazo watu wako tayari kukubali ili kutoroka (Malakooti, 2015). Uhamiaji na uhamaji wa watu hupungua wakati wa uthabiti wa kisiasa na mifumo ya kidemokrasia inapoanzishwa, na haki za kisiasa na za kiraia huboreka kwa kiasi kikubwa (Giménez-Gómez na wengine, 2019, uk. 1816).

Idadi ya watu waliolazimika kuyahama makazi yao kwa sababu ya vita, migogoro, mateso, ukiukwaji wa haki za binadamu na matukio yanayosumbua sana utulivu wa umma iliongezeka hadi milioni 79.5 kufikia mwisho wa 2019. Ndiyo idadi kubwa zaidi katika rekodi na karibu mara mbili ya idadi ya 2010 ya milioni 41, na ongezeko kubwa kutoka idadi ya 2018 ya milioni 70.8. Idadi ya wakimbizi duniani chini ya mamlaka ya UNHCR ilifikia watu milioni 20.4 mwisho wa 2019 — na ukiongeza wakimbizi wa Kipalestina milioni 5.5 chini ya mamlaka ya UNRWA,

8 Kwa ufafanuzi wa kuhama kwa hiari na kuhamishwa kwa lazima, angalia faharasa zinazopendekezwa katika Moduli ya 2 (UNHCR, n.d.; EMN, 2018; IOM, 2019a).

jumla ya wakimbizi duniani inafika karibu milioni 26. Mbali na wakimbizi hawa — ambao kwa ufafanuzi wanavuka mipaka ya kimataifa — watu wengi zaidi wanahamishwa katika nchi zao. Wakimbizi wa ndani kwa ndani (IDPs) wailikadiriwa kuwa milioni 45.7 kufika mwisho wa 2019⁹ (UNHCR, 2020b, uk. 2-3, uk. 8).

Makundi mawili makuu ya watu waliohamishwa kwa lazima kutokana na migogoro chini ya mamlaka ya (UNHCR) ni wakimbizi na IDPs (bila kujumuisha Wapalestina katika muundo huu mahususi). Migogoro kadhaa mikuu ilichangia kuhama kwa watu wengi katika muongo mmoja uliopita, ikiwa ni pamoja na nchi za MENA (Iraq, Libya, Syria, Yemen), Asia (Afghanistan, Myanmar), Ulaya (Ukraine), Amerika ya Kusini (Venezuela, Colombia) na Afrika (Jamhuri ya Afrika ya Kati, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Ethiopia, eneo la Sahel, Sudan Kusini; UNHCR, 2020b, uk. 6).

Hadi kufika mwisho wa 2019, zaidi ya thuluthi mbili (68%) za wakimbizi duniani walikuwa wametoka katika nchi tano tu: Syria, Afghanistan, Sudan Kusini, Myanmar na Somalia, na wengi wao walikuwa wenyeji wa nchi tano tu: Uturuki, Colombia. Pakistan, Uganda na Ujerumani. Tukipitia muongo uliopita (2000-2019), ni Pakistani, Ujerumani na Iran pekee zilizoshikilia nafasi katika nchi 10 bora zinazowahifadhi wakimbizi mwanzoni na mwishoni mwa muongo huo (UNHCR, 2020b, uk. 22); Ujerumani pekee ndiyo inawakilisha kimbilio la mbali kwa wakimbizi wengi ambapo, kwa kawaida, ukaribu wa kijiografia ni jambo muhimu kwa watu wanaokimbia migogoro na mateso: Wasyria wengi hukimbilia Uturuki, Lebanoni au Jordan; katika Afrika, idadi ya wakimbizi katika kanda hiyo iliongezeka karibu mara tatu katika muongo huo. Katika mwaka wowote wa miaka 10 iliyopita, robo tatu ya wakimbizi au zaidi walikaribishwa na taifa jirani wa nchi yao. Kipengele cha ukaribu katika harakati za wakimbizi kinazibebesha mzigo nchi zilizoendelea kimaendeleo kwa kiasi kikubwa, zikiwemo Bangladesh, Chad, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Ethiopia, Rwanda, Sudan Kusini, Sudan, Tanzania na Uganda. Wakiwa na pato la taifa (GDP) la asilimia 1.2 tu walikuwa na rasilimali chache zaidi za kukidhi mahitaji ya watu wanaotafuta hifadhi (UNHCR, 2020b, uk. 22). Wakati nchi jirani zinahifadhi wakimbizi wengi, madai ya kutafuta hifadhi yanawasilishwa hasa Marekani na Ulaya (UNHCR, 2020b, uk. 38; ramani 4, uk. 45).

Kikundi kisichoripotiwa sana na kinachoongezeka kwa kasi ni cha IDPs. Ingawa wakimbizi kwa ufafanuzi huvuka mipaka ya kimataifa ili kukimbia mateso na/au migogoro nyumbani, IDPs wanahamishwa katika nchi zao na kubaki chini ya ulinzi wa serikali zao, hata kama serikali haina uwezo au iko tayari kuwalinda (UNHCR, 2020d).

Idadi yao pia imeongezeka pakubwa, na ni wengi kuliko wakimbizi. Idadi ya IDPs chini ya ulinzi wa UNHCR iliongezeka kutoka milioni 6.6 mwaka 2005 hadi milioni 15 mwaka 2010 na zaidi

9 Kwa data, angalia Moduli ya 2. Dokezo kuhusu data iliyotumika hapa: UNHCR inanukuu data ya IDMC ya idadi ya IDPs (UNHCR, 2020b, uk. 2-3, tanbihichini 1).

ya milioni 43.5 mwishoni mwa 2019. Katika mwongo uliopita, UNHCR iliripoti idadi ya IDP milioni 59 chini ya mamlaka yake. UNHCR inaonya kuwa “Idadi hii haijumuishi idadi ya kima-taifa” (UNHCR, 2020b, uk. 30), huku shirika hilo likiangazia watu milioni 79 waliohama makazi yao kati ya 2010 na 2019 waliorekodiwa na IDMC. Idadi kubwa ya IDP walioshughulikiwa na UNHCR kufikia mwisho wa 2019 walikuwa Colombia, Yemen, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Somalia, Afghanistan, Nigeria, Sudan, Ethiopia na Sudan Kusini (UNHCR, 2020b, uk. 3; ramani 3, uk. 31). “Ingawa kulazimishwa kuhama ni tukio la kimataifa”, Kamishna wa AU wa Masuala ya Kisiasa anaandika, “linajitokeza zaidi katika Afrika” (André na wengine, 2019, uk. 7). Migogoro na vurugu zinaibuka au kuongezeka katika nchi nyingi za Kiafrika kama vile Cameroon, Burkina Faso, Mali, Niger na Libya. Mingi ya migogoro hii si mipya bali imekuwepo kwa muda mrefu na ni ya kudumu (UNHCR, 2020b).

Suala jingine la maendeleo linahusu wale waliopewa mamlaka ya kulinda na kusaidia IDPs: Uhamiaji wa ndani kwenda vijijini ulikuwa umeenea hapo awali lakini IDPs wanahamia maeneo ya mijini. Wahamiaji wawili kati ya watatu sasa wako mijini au katika mazingira ya mijini kulingana na data ya UNHCR. Hili limeleta changamoto kubwa kwa ulinzi katika nchi zenye migogoro inayoendelea mijini kwa mfano Aleppo nchini Syria, Bangui katika Jamhuri ya Afrika ya Kati, Tripoli nchini Libya, au Jijiga nchini Ethiopia. IDPs wanaishi katika vitongoji vilivyotengwa na hawana huduma nzuri au makazi rasmi, hawawezi kupata maji safi, vyoo, nafasi za elimu na kazi na huduma nyinginezo, na kuwaacha hatarini (André na wengine, 2019; UNHCR, 2020b).

Takwimu za watu waliohamishwa zinazohusishwa na migogoro na vurugu zinaomba kwa sauti kubwa hatua za haraka zichukuliwe kukomesha na kubadili mwelekeo huo. Kando na mipango ya kisiasa ya kuunga mkono au kudumisha amani, UNHCR inatafuta “suluhisho za kudumu” tatu kwa kuwarejesha nyumbani kwa hiari, ushirikiano wa ndani, na makazi mapya. Makazi mapya ni uhamishwaji wa wakimbizi hadi katika nchi ambayo imekubali kuwapokea na hatimaye kuwapatia makazi ya kudumu. UNHCR inalaumu “idadi ndogo tu ya mataifa ambayo hushiriki katika mpango wa makazi mapya wa UNHCR”, hasa Amerika ya Kaskazini, Australia na Ulaya (UNHCR, 2020b, uk. 2, uk. 48 ff; UNHCR, 2020c).



ZOEZI LILILOPENDEKEZWA LA KUSHUGHULIKIA STADI ZA UTAMBUZI ZA UTEKELEZAJI:

Pakua video fupi “*Who is an IDP?*” ambayo inawatambulisha IDP walio chini ya mamlaka ya UNHCR (2020d).

Liambie darasa litumie vyanzo vya data vilivyoelezwa hapo awali (na UNHCR, na IDMC) kuandaa wasilisho la dakika 10 ambalo linaelezea harakati za IDP katika nchi yako ya asili (au, ikiwa haitumiki, katika nchi unayochagua).

Maswali yanayoongoza kwa uwasilishaji ni:


1. Ni idadi gani ya IDPs inaweza kupatikana katika nchi hii?
2. Kwa nini walilazimishwa kuondoka nyumbani?
3. Je, unaweza kupata data iliyogawanywa kulingana na jinsia na umri (wanawake, watoto, vijana)?

Masuala ya kiuchumi

Masuala ya kiuchumi yameangaziwa mara kwa mara kama kichocheo cha uhamiaji. Wasomi wanaozingatia nadharia tofauti wanakubali kwa mapana kwamba maamuzi ya uhamiaji pia yana-changiwa na mapato yanayotarajiwa (ya maisha) kwenye uwekezaji (Borjas, 1994; Bryceson, 2019; Sjaastad, 1962). Masuala ya uchumi mkuu kama vile utandawazi na hitaji la wafanyakazi nafuu katika shughuli za utengenezaji bidhaa na wataalamu wenye ujuzi wa hali ya juu katika jamii za maarifa yana jukumu muhimu (Adepoju, 2007). Wahamiaji kwa kawaida hutarajia kupata faida bora kutokana na ujuzi wao katika nchi kikomo cha safari zao kuliko katika nchi zao za asili. Kwa kutilia maanani masuala ya kiuchumi, dhana moja ya msingi ni kwamba watu wanahama wakati manufaa ya kifedha kutokana na uhamiaji ni ya juu kuliko yale ya kukaa nyumbani, na mapato ya kazi zao nje yanazidi jumla ya michango ya mhamiaji binafsi, familia na jumuiya ya “wawekezaji” nyumbani iliyofanikisha uhamiaji wao. Ndiposa fursa za ajira na tofauti za mishahara ni muhimu katika kuchochea maamuzi ya uhamiaji. Umuhimu wa tofauti za mishahara na viwango vya maisha kati ya nchi asili za wahamiaji na wanakohamia mara kwa mara hujitokeza kama vipengele muhimu katika kuelezea uhamiaji wa kimataifa. Uwezo wa kipengele hiki katika kuchochea uhamaji, hata hivyo, hubadilika kulingana na wasifu wa wahamiaji, kwa mfano kati ya watu wenye ujuzi wa juu na wa chini (Kuschminder na wengine, 2012; Neto & Mullet, 1998; Vogler & Rotte, 2000). Mpango wa Mixed Migration Monitoring Mechanism au 4M-Initiative unaonyesha kuwa idadi kubwa ya wahamiaji husukumwa na sababu za kiuchumi: asilimia 73 ya wanawake na 96% ya wahamiaji wanaume kutoka Afrika Magharibi waliohojiwa Mali na Niger mnamo Aprili 2018 (jumla ya mahojiano 311 ya kina) walisema walihama kwa sababu za kiuchumi, zikifuatwa na sababu za kibinafsi au za familia, vurugu, ukosefu wa huduma na mateso (4Mi, 2018; tazama Kielelezo 8).

Matokeo sawa yameripotiwa na tafiti zingine. Afrobarometer iligundua kuwa 75% ya wahamiaji wanaotarajiwa wanafikiria kuondoka ili kutafuta kazi (44%) au kuepuka umaskini au matatizo ya kiuchumi (29%; Appiah-Nyamekye Sanny na wengine, 2019, uk. 14). Kirwin na Anderson (2018) wanaonyesha katika utafiti wao wa nchi sita za Afrika Magharibi (Burkina Faso, Ivory Coast, Mali, Niger, Nigeria na Senegal) kwamba sababu za kiuchumi zinaongoza orodha ya nia kwa kiasi kikubwa. Wachapishaji wa ripoti ya kwanza ya Uhamiaji wa Kiafrika, AU na IOM, wana-pinga ufafanuzi wa nambari hizi (Adepoju na wengine, 2020; tazama Moduli 9).

Kielelezo 8: Misukumo ya kuhama



Sababu za kiuchumi ndizo msukumo na kivutio kikuu cha wahamiaji wanawake na wanaume lakini ni muhimu zaidi kwa wanaume (asilimia 96 ya waliohojiwa) kuliko wanawake (asilimia 73). Kwa wanawake, sababu za kibinafsi au familia zilikuwa sababu ya pili ikiungwa mkono na asilimia 28. Kwa wanaume, ni uhaba wa huduma za jamii na uongozi mbaya nchini. Dhuluma na kuzorota kwa usalama ilikuwa sababu muhimu kwa wanawake (asilimia 19 ya waliohojiwa) lakini sio sana kwa wanaume (asilimia nne). Chanzo: 4Mi (2018, uk. 2). Kielelezo chetu

Pesa zinazotumwa nyumbani na wahamiaji

Pesa kutoka nje zinazotumwa nyumbani na wahamiaji¹⁰ — “kauli mbiu mpya ya maendeleo” (Kapur, 2004) — ni kiungo cha moja kwa moja na kinachojulikana kati ya uhamiaji na maendeleo. Kwa kawaida hujulikana kama pesa ambazo wahamiaji hutuma nyumbani kwa faragha. Zinazidi mtiririko wa mtaji wa kibinafsi¹¹ na misaada ya maendeleo kutoka nje, zinachukua zaidi ya mara tatu ya ukubwa wa misaada ya maendeleo inayotolewa na nchi za kigeni (ODA), na (bila kujumuisha Uchina) ni kubwa zaidi kuliko uwekezaji wa moja kwa moja wa kigeni (FDI) katika nchi zinazoendelea (tazama Kielelezo 9). Takwimu hizi zinaonyesha tu data iliyorekodiwa rasmi

10 Istitlahi kutuma pesa nyumbani pia inaweza kujumuisha bidhaa, mawazo, maarifa na mengineyo lakini katika mwongozo huu, tunarejelea tu usafirishaji wa fedha (Fackler na wengine, 2018).

11 Mtiririko wa mtaji wa kibinafsi unajumuisha uwekezaji wa moja kwa moja wa kigeni (FDI) na uwekezaji kwa hisa. Uwekezaji wa kigeni wa moja kwa moja ni mapato halisi ya uwekezaji ili kupata maslahi ya kudumu ya usimamizi [...] katika biashara inayofanya kazi katika uchumi tofauti na ule wa mwekezaji. Ni jumla ya mtaji wa hisa, uwekaji upya wa mapato, mtaji mwingine wa muda mrefu, na mtaji wa muda mfupi kama inavyoonyeshwa katika salio la malipo. Uwekezaji wa kwingineko unajumuisha miamala katika dhamana za hisa na dhamana za madeni” (Benki ya Dunia, 2020e).

- “Kiasi halisi cha fedha zinazotumwa kutoka nje, ikijumuisha mtiririko kupitia njia zisizo rasmi, ni kubwa zaidi” (Benki ya Dunia, 2018b, uk. 4).

Fedha zinazotumwa kutoka nchi za nje zinaweza kuelezewa kama mkakati wa uwekezaji sio tu kwa mtu binafsi ila kwa jamaa nzima au jumuiya na kama dhahirisho la makubaliano ya kimkataba isiyo rasmi kati ya mhamiaji na familia yake kubwa na/au jumuiya. Wanawekeza katika safari ya wahamiaji inayolenga kutafuta ajira na kutuma pesa nyumbani. “Makubaliano haya ya kimkataba yasiyo rasmi yanahakikisha kwamba wote wanashiriki kwa gharama na manufaa ya uhamiaji” (Chuo Kikuu cha Maastricht, & GMDAC, 2016, uk. 15). Jambo ambalo mara nyingi huripotwa kama kujitolea kwa wahamiaji kwa ajili ya wapendwa wao (Jordan, 2020) ni kweli lakini ubinafsi kama nia ya kutuma pesa nyumbani sio simulizi kamili (Chuo Kikuu cha Maastricht, & GDMAC, 2016, uk. 15). Pesa zinazotumwa kutoka nje pia husambaza tena faida kutokana na uhamiaji uliofaulu na ni mkakati wa kukinga boma na jamii zinazowekeza (Chuo Kikuu cha Maastricht, & GDMAC, 2016). Kirwin & Anderson (2018) wanaonyesha kwa data za hivi majuzi kwamba ajira na fedha zinazotumwa ni sababu kuu za uhamiaji kutoka nchi nne za Afrika Magharibi (Ivory Coast, Mali, Nigeria, Senegal), na Tiemoko (2004) wameangazia jukumu muhimu la familia katika nyanja zote za upatikanaji wa mitaji ya kibinadamu, kijamii na kifedha na uwekezaji kupitia uhamiaji, pia kuchunguza hali katika Afrika Magharibi (Ghana, Ivory Coast).

Pesa zinazotumwa kutoka nje na wahamiaji, kwa ujumla, zinaendelea kuongezeka: Nchi za kipato cha chini na cha kati (LMICs)¹² zilipokea dola bilioni 501 za malipo kutoka nje mwaka 2019, kutoka dola bilioni 272 mwaka 2009 (+84% katika miaka kumi); Pesa zilizopokelewa katika nchi za kipato cha chini (LICs) ziliongezeka zaidi ya mara mbili kutoka dola bilioni 10 mwaka 2009 hadi zaidi ya dola bilioni 21 kufikia 2019 na ziliruka katika nchi za kipato cha kati (MICs) kutoka dola bilioni 263 (2009) hadi karibu dola bilioni 480 mwaka 2019 (+82% katika miaka 10; Benki ya Dunia, 2020d). Katika asilimia ya pato la taifa, fedha zinazotumwa kutoka nje ni muhimu sana kwa LICs ambapo ziliwakilisha karibu 4.3% ya pato la taifa mwaka 2019, ikilinganishwa na 1.6% katika LMICs na 1.5% katika MICs (Benki ya Dunia, 2020c). Nchini Sudan Kusini, kwa mfano, fedha zinazotumwa kutoka nje na wahamiaji zilijumuisha zaidi ya 35% ya pato la taifa, nchini Lesotho 21% na katika Gambia, Comoro, Senegal, Liberia kati ya 10% na 15% ya pato la taifa. Nchini Nigeria, nchi yenye uchumi mkubwa zaidi barani Afrika, pesa zinazotumwa kutoka nje zilikuwa zaidi ya 5% ya pato la taifa (data ya Oktoba 2020; Benki ya Dunia, 2020f). Mtiririko wa kutuma pesa kwa ujumla huonyesha picha mchanganyiko (tazama Kielelezo 10).


Wakati janga la Uviko-19 lilipokumba ulimwengu mnamo 2019/2020, mipaka ya nchi ikafungwa na bei ya mafuta ikashuka, wimbi la mshtuko liliwagonga wahamiaji wanaotuma pesa, jamii zinazopokea na nchi. Mnamo Aprili 2020, Benki ya Dunia ilitahadharisha kuwa pesa zinazotumwa kutoka nje na wahamiaji zingepungua hadi 20%, “kupungua kwa kasi zaidi katika historia ya

12 Tazama Moduli 2 kwa usuli wa uainishaji huu wa nchi ambao umefafanuliwa katika UNDESA (n. d.).

hivi karibuni” (Benki ya Dunia, 2020b, uk. 7). Huku fedha zinazotumwa kutoka nje zikichangia kupunguza umaskini, ilitarajiwa kupotea kwa usaidizi wa kifedha kungesababisha umaskini zaidi na uhaba (Benki ya Dunia, 2020b).

Noxolo (2016, uk. 53) anaona kuwa taathira kwa umaskini za fedha zinazotumwa ni ndogo sana barani Afrika kuliko katika miktadha mingine: “Ongezeko la asilimia 10 la mgao wa fedha kutoka nje katika pato la taifa husababisha kupungua kwa takriban asilimia moja katika uwiano wa idadi ya watu maskini [katika Afrika wakati utafiti kuhusu] taathira za fedha zinazotumwa katika nchi zinazoendelea za Asia-Pacific uligundua kuwa ongezeko la 10% la fedha zinazotumwa hupelekea kupungua kwa umaskini kwa 2.8%” (Noxolo, 2016, uk. 53). “Athari ndogo zaidi kwa umaskini barani Afrika [...] inatokana [kimsingi] na gharama kubwa ya kutuma pesa barani Afrika” (Noxolo, 2016, uk. 53). Gharama za utumaji pesa zinatia wasiwasi mkubwa katika uhusiano wa uhamiaji na maendeleo: Mpango wa Social Development Goals (SDGs) unashughulikia utumaji fedha katika lengo la 10, lengo la 10c, ambalo shabaha yake ni kupunguza hadi chini ya 3% gharama za shughuli za utumaji fedha za wahamiaji kutoka kwa viwango vya sasa vya zaidi ya 5% (Umoja wa Mataifa, n. d.). Mkataba wa Kimataifa wa Uhamiaji unatoa wito wa “uweza wa haraka zaidi, salama na nafuu wa usafirishaji wa fedha na kukuza ushirikishwaji wa wahamiaji katika shughuli za hazina” (UN, 2020b, uk. 6, uk. 27-29, lengo la 20). Gharama za kutuma pesa ni kubwa katika nchi zinazoendelea na kwa 7.1% mwaka 2018 “juu kabisa”

Kielelezo 9: Pesa kutoka nje zinazotumwa na wahamiaji nyumbani katika mataifa yenye kipato cha chini na cha wastani ikilinganishwa na misaada ya maendeleo kutoka nje (ODA) na uwekezaji wa moja kwa moja wa mashirika ya kigeni katika mataifa hayo (FDI)




Pesa ambazo wahamiaji hutuma nyumbani kutoka nje ni kiungo muhimu cha maendeleo na uhamiaji kwani zinanufaisha moja kwa moja familia na jamii zinazozipokea. Pesa hizo husaidia kukabiliana na umaskini na/au kusaidia uwekezaji mashinani. Pesa zilizotumwa kwa mataifa yenye kipato cha chini na cha wastani (LMICs) zilikuwa nyingi kuliko za misaada ya maendeleo kutoka nje (ODA) na uwekezaji wa moja kwa moja wa mashirika ya kigeni (FDI)

Chanzo: Banki ya Dunia (2018b, uk. 3, Figure 1.1). Kielelezo chetu.

ya lengo la SDG la 3% (Benki ya Dunia, 2018b, uk. 6). Gharama katika Asia Kusini ilikuwa ya chini zaidi mwaka 2018, kwa 5.2%, wakati Afrika “ilikuwa na gharama ya juu zaidi” (Benki ya Dunia, 2018b, uk. 6) kwa 9.4 %, pamoja na kuongezeka kwa gharama katika mbinu nyingi za mawasiliano Afrika (sababu ni kwa mfano viwango vya chini vya mtiririko rasmi, kiwango cha chini ya upenyezaji wa teknolojia mpya). Shughuli na njia za kuunganisha nchi katika kanda ni za gharama kubwa zaidi: “Ukanda unaunganisha Angola na Namibia ulikuwa wa gharama ya juu zaidi [...] [21.4 % katika 2016-2017, na ya bei nafuu zaidi ikiwa 2.9 %] katika Ivory Coast hadi Mali” (Benki ya Dunia, 2018b, uk. 34).

Kielelezo 10: Picha mchanganyiko inayoonyesha mtiririko wa pesa za kutoka nje (jumla ya kiasi cha cha miezi, Desemba 100=2019)



Ingawa Benki ya Dunia ilikadiria kwamba mlipuko wa janga la Uviko-19 mnamo Aprili 2020 ungesababisha kushuka kwa asilimia 20 kiasi cha pesa ambazo wahamiaji hutuma nyumbani katika mataifa yenye kipato cha chini na cha wastani, la kushangaza ni kwamba ubashiri huo haukutimia. Mnamo Septemba 2020, Shirika la Fedha Ulimwenguni (IMF) liliripoti kwamba mara nyingi kiasi cha mapato kutoka nje hujimudu misukosuko katika nchi mpokeaji. Mtiririko unaonyesha kwamba kiasi cha pesa kutoka nje kililingana na sera za kukabiliana na janga hilo katika mataifa yenye kipato cha juu zilizowekwa Machi 2020 na kusababisha kushuka kwa pesa ambazo wahamiaji walituma nyumbani. Masharti yalipolegezwa Mei, kiasi hicho kiliongezeka hata kupita viwango vya kabla ya janga katika baadhi ya nchi (Kenya, Mexico, Bangladesh, Pakistan). Chanzo: Quayyum & Kpodar (2020). Kielelezo chetu.

Taasisi

Athari za taasisi katika maamuzi ya uhamiaji zimetafitiwa, na kuwasilisha taasisi za kidemokrasia kama sababu muhimu katika kuvutia wahamiaji. Baudasse na wengine (2016, uk. 25) wanasema kuwa taasisi ni za “msingi” na “katika kiwango sawa na mambo ya kiuchumi” wa kueleza ni kwa nini watu huacha nchi yao ya asili ili nchi nchi nyingine. Bertocchi & Strozzi (2008, uk. 97), ambao walichanganua uhamiaji kutoka Ulaya hadi Amerika kati ya 1870 na 1910 kwa nia ya maendeleo ya sasa, walipata ushahidi kwamba nchi za kidemokrasia zilizo na taasisi zinazohusiana zilikusishwa na viwango vya juu vya uhamiaji. Katika mfumo huu wa mawazo, taasisi zinazohusika na uhamiaji zinajumuisha kisiasa (kwa mfano katiba, haki za kiraia, ushiriki), kijamii (ulinzi, ugawaji wa mapato, mshikamano usio rasmi na mengineyo) na kiuchumi (kwa mfano haki za kumiliki mali, ujasiriamali dhidi ya ufisadi kama ishara za udhaifu wa taasisi) (Baudasse na wengine, 2016, uk. 6). Bertocchi & Strozzi (2008, uk. 83) wanatofautisha athari za taasisi zinazoweza kuvutia wahamiaji, kama vile sera za uraia, ardhi na elimu na athari za taasisi za kisiasa.

Ufisadi, uliokithiri katika nchi kadhaa za Afrika, ni ishara ya taasisi dhaifu. Kwa hamu na matarajio makubwa, Umoja wa Afrika uliteua 2018 kuwa mwaka wa “Ushindi wa Mapambano Dhidi ya Ufisadi: Njia Endelevu ya Mabadiliko ya Afrika” (Tankou, 2018). “Rushwa inaendelea kudhuru Afrika, ikikwamisha demokrasia, maendeleo na uwezo wa kuwatoa watu kutoka kwenye umaskini”, Transparency International inaonya na kusisitiza kuwa “athari za rushwa haziwezi kupuuzwa. Takriban asilimia 43 ya Waafrika wanaishi katika umaskini huku mali za wizi zenye thamani ya zaidi ya dola bilioni 50 zikisafirishwa nje ya Afrika kila mwaka”. Linaona kwamba “ukosefu mkubwa wa maendeleo [...] unaimarishwa na mipango mingi ya rushwa, ambayo inawaogopesha wawekezaji na kukatisha tamaa ya maendeleo zaidi.” Shirika hilo linakadiria kuwa “fedha zisizotumika ipasavyo zinachangia kupotea kwa asilimia 25 ya rasilimali za maendeleo katika Afrika” (Transparency International, 2018).



ZOEZI LILILOPENDEKEZWA LA KUSHUGHULIKIA STADI ZA UTAMBUZI ZA ULEWA NA KUTEKELEZA PAMOJA NA STADI ZA MITAZAMO YA KIBINAFSI NA MAADILI ZA KUPOKEA:

Waalike washiriki kuangazia “mitazamo ya hali njema” kulingana na viashirio vilivyoonyeshwa katika faharasa ya maendeleo ya binadamu (UNDP, 2019b, uk. 30-33) na faharasa ya mtazamo wa ufidiaji (Transparency International, 2019) na kutumia vyanzo hivi:

- Kukusanya data kwa ajili ya nchi yako au nchi unayochagua: Kagua viashiria vya maendeleo ya binadamu kama vile “uhuru wa kuchagua”, na mitazamo kuhusu serikali kama vile “imani katika mfumo wa mahakama”, “hatua za kuhifadhi mazingira” na “imani katika serikali ya kitaifa”.
- Tambua ripoti za vyombo vya habari kwa ajili ya nchi uliyochagua vinavyojadili masuala ya rushwa na “hali njema” ya watu kwa kuzingatia viashiria vya maendeleo ya binadamu.

Tafiti nyingi ziligundua kuwa raia wenye ujuzi wa juu huhama kadiri ufidiaji unavyoongezeka na ubora wa taasisi za kidemokrasia ukipungua (Cooray & Schneider, 2016; Kirwin & Anderson, 2018).

Elimu

Elimu hubadilisha maisha ya mtu binafsi na ni muhimu kwa ustawi wa jamii. Ni kichocheo kikuu cha mabadiliko ya kijamii na kiuchumi na muhimu sana katika kufikia SDGs. Elimu ni thamani kuu katika uhusiano wa maendeleo ya uhamiaji, na, kulingana na UNESCO, “kichocheo kikuu katika uamuzi wa kuhama” (UNESCO, 2019, uk. xvii, uk. 2-4).

Kati ya kanda zote za dunia,¹³ UNESCO inasema, nchi za Afrika za kusini ya Jangwa la Sahara zina viwango vya juu zaidi vya raia wanaoachwa nje ya mfumo wa elimu: Katika eneo lote, wasichana milioni tisa¹⁴ na wavulana milioni sita wa umri wa kati ya miaka sita na 11 hawatawahi kwenda shule kamwe (UIS, 2020). Ikithibitisha ukweli kwamba zaidi ya 20% ya watoto katika kundi hili hawaendi shule barani Afrika, na karibu 60% ya vijana kati ya miaka 15 na 17, UNESCO inatahadharisha kwamba “hali inaweza kuwa mbaya zaidi wakati eneo linakabiliwa na mahitaji yanayoongezeka ya elimu kutokana na idadi ya watu wenye umri wa kwenda shule wanaoendelea kuongezeka” (UIS, 2020). Onyo hilo lilitumwa kabla ya Uviko-19, janga ambalo lilizorotesha hali hiyo. Katika Afrika, kufungwa kwa shule katika nchi zote kutokana na janga hili kulitokea wakati ambapo idadi kubwa ya shule zilikuwa tayari zimefungwa kwa sababu ya kuzorota kabisa usalama, migomo au hatari za hali ya hewa (AfricaNews, 2019; UN, 2020a; Yameogo & Tidey, 2019). Kuwepo kwa wanafunzi nyumbani kunahitaji familia sio tu kuwatafutia

13 Kwa uainishaji wa kanda na nchi, angalia Moduli ya 2 na UNDESA (n. d.).

14 Kaps na wengine (2019) inaangazia dhima muhimu ya kipekee ya elimu ya wanawake ikiyeme kushuka kwa viwango vya uzazi: “Wataalamu wengi wanaamini kwamba elimu ndiyo njia bora ya udhibiti wa uzazi” (Kaps ., na wengine 2019, uk. 12).

mlo sawa na walivyokuwa wakilishwa shuleni, na kuwawezesha kuendelea kujifunza, kinachotia wasiwasi zaidi ni tishio kwamba, bila usaidizi, hawawezi kurudi shuleni.

Ingawa Afrika imepiga hatua kubwa katika kuziba pengo la usajili wa wanafunzi wa shule za msingi, idadi katika eneo hilo inapungua ghafla kutoka 99% katika shule za msingi hadi 43% wanaojiunga na shule za sekondari na 9% tu katika elimu ya juu (Benki ya Dunia & UIS, 2020a; Benki ya Dunia & UIS, 2020b; Benki ya Dunia & UIS, 2020c). Ni 4% tu ya watoto barani Afrika wanatarajiwa kuingia katika taasisi ya kuhitimu na ya uzamili, ikilinganishwa na 14% katika Kusini na Magharibi mwa Asia na 36% katika Amerika ya Kusini (Musau, 2017-2018). Kote kote, ubora wa ufundishaji na ujifunzaji ni suala la kutiliwa maanani sana (Sifuna & Sawamura, 2009). Mfano kutoka moja ya nchi zilizoendelea zaidi katika nchi za Afrika za kusini ya Jangwa la Sahara ni Afrika Kusini, ambapo pia pana changamoto kubwa: Takriban 80% ya walimu wa hisabati wa darasa la 6 “hawawezi kupata 60% kwenye mtihani wa hesabu wa darasa la 6/7” (Spaull, 2019, uk. 3); “walimu wengi kwa sasa hawana ujuzi wa maudhui au ujuzi wa ufundishaji unaohitajika ili kufanikisha mtaala” (Spaull, 2019, uk. 8). Katika Guinea-Bissau (UNDP, 2019a, uk. 302), “hali ni mbaya” (Boone na wengine, 2013) ambapo 27% ya karibu watoto 10,000 waliofanyiwa utafiti walio na umri wa kati ya miaka saba na 17 waliweza kujumlisha tarakimu mbili, na takriban 20% waliweza kusoma na kuelewa maneno rahisi (Boone na wengine, 2013).¹⁵

Changamoto hizi zinashughulikiwa katika utafiti wa masuala yote ya elimu barani Afrika, na wakati fulani vyombo vya habari vinaripoti masuala hayo (AU, 2020; News24, 2011; UN, 2020b; UN, 2020c).¹⁶ Ripoti ya UNESCO kuhusu “Uhamiaji, uhamishwaji wa lazima na elimu” (2019) hutoa maelezo ya kina kuhusu elimu kwa kuzingatia wahamiaji, wakimbizi na jumuiya zinazowapokea. Ripoti hiyo inaangazia suala hilo kuanzia utotoni hadi elimu ya watu wazima, kutoka mafunzo ya ufundi stadi hadi elimu ya chuo kikuu na programu za kubadilishana kitaaluma, kushughulikia wanafunzi, wanafunzi, waelimishaji na kujumuisha wahamiaji wa ndani na nje ya nchi pamoja na wakimbizi. Inaonyesha kuwa uhamiaji na uhamishwaji wa kulazimishwa huathiri elimu katika maeneo ya asili na wanakohamia. Kwa mfano, katika maeneo walikohamia, mfumo wa elimu unahitaji kudhibiti uanuwei mpya katika madarasa na kuoanisha viwango tofauti vya elimu vya wanafunzi wazawa na wahamiaji au wakimbizi. Unahitaji pia waelimishaji walioji-tayarisha vyema. Katika maeneo wanayotoka, kuhama kwa vijana wenye umri wa kwenda shule kunaweza kuzuia uwekezaji katika elimu na hivyo kupunguza fursa kwa wale wanaobaki nyuma;

15 Tazama cheo cha Afrika Kusini na Guinea-Bissau kwenye Kielelezo cha Maendeleo ya Kibinadamu: UNDP (2019a, uk. 300-303). Afrika Kusini, walimu kushindwa kupata 100% ya mtihani wa hesabu wa Daraja la 6/7 una maana - kulingana na tafiti za kitaifa - zaidi ya 60% ya wanafunzi wa Darasa la 5 hawawezi kuongeza na kupunguza namba nzima, na hawaelewi kuzidisha namba kwa nyingine moja, kwa mfano hawawezi kufanya hesabu za kimsingi (Spaull, 2019).


16 Angalia, kwa mfano: Elimu ni mojawapo ya kanuni sita elekezi za Mkakati wa Elimu ya Bara la Afrika wa Umoja wa Afrika (CESA) 2016-2025 (AU, 2020) pamoja na mawazo yake yenye matarajio kama vile “mfumo wa elimu na mafunzo wa Afrika ... [utatimiza] ujuzi, umahiri, stadi, uvumbuzi na ubunifu unaohitajika [...] katika ngazi ya kitaifa, kanda na bara”. Elimu ni mada mtambuka katika Mkataba wa Kimataifa wa Uhamiaji, na Mkataba wa Kimataifa wa Wakimbizi (aya ya 68 na 69) unazungumzia elimu hasa kwa kuzingatia ubora, kupunguza muda wa pengo kwa watoto wakimbizi kati ya kuwasili na kuanza shule na kutambuliwa - utoaji wa usawa wa sifa za kitaaluma na kitaaluma (UN, 2020b). Tazama pia SDGs, hasa SDG 4 (UN, 2020c).

uhamaji wa wasomi kutoka nchi moja hadi nyingine wakitafuta maslahi huwaondoa wataalamu kutoka nchi zao asili, hali ambayo inaleta faida kwa upande mwingine wakati wahamiaji hutuma pesa nyumbani (tazama sehemu ya awali kuhusu utumaji pesa kutoka nje). Huwa kuna uwezekano mkubwa wa watu hao wenye elimu ya juu — ambao hunyima nchi za nyumbani ujuzi na maarifa waliyo nayo — kuhama (tazama Kielelezo 11): Katika nchi 53, uwezekano wa kuhama uliongezeka maradufu kati ya wale walio na elimu ya msingi, mara tatu kati ya wale walio na ya sekondari na mara nne kati ya wale walio na elimu ya juu, ikilinganishwa na wale wasio na elimu (UNESCO, 2019, uk. 15). Hii ilionyesha kuwa wakimbizi pia mara nyingi hawajui kusoma na kuandika (15% ya wakimbizi nchini Ujerumani hawajui kusoma na kuandika lakini pana uwezekano mdogo wa kuhudhuria kozi ya kusoma na kuandika; UNESCO, 2019, uk. 183, Mchoro 13.3), na “miongoni mwa wanaotafuta hifadhi na elimu ya msingi, ni asilimia 50 tu ya waliohojiwa nchini Ugiriki na 41% nchini Italia walikuwa wamefikia kiwango cha chini cha ujuzi wa kusoma na kuandika” (UNESCO, 2019, uk. 117, Kielelezo 7.2).

Wakati baadhi ya wataalamu wanaona elimu kuwa kichocheo kikuu cha uamuzi wa kuhama, wengine wanaelezea elimu kuwa moja tu kati ya mambo mengi ya kijamii na kiuchumi ambayo yanalenga maisha bora (Browne, 2017). Ikichunguza sababu za kuzingatia uhamaji, Afrobarometer (Appiah-Nyamekye Sanny na wengine, 2019, uk. 16, Jedwali la 1) inaripoti kuwa ni sehemu ndogo tu ya watu waliojibu swali hili wanaonyesha kuwa wanataka kuendelea na elimu (6%), idadi ambayo ni chini sana kuliko wale wanaotaka kuepuka umaskini au matatizo ya kiuchumi (29%) na wanaotaka kupata kazi (44%; Appiah-Nyamekye Sanny na wengine, 2019, uk. 14, Kielelezo 12). Aina hizi, hata hivyo, zinahusiana kwa karibu kwani matarajio ya kiuchumi na elimu yanalingana, kama Browne (2017, uk. 2) anavyoeleza. Mwandishi anapendekeza kwamba elimu huwa sababu ya uhamiaji wa kimataifa katika ngazi ya chuo kikuu. Elimu ya chuo kikuu, kwa ulinganisho wa kimataifa, ni nafuu zaidi katika nchi za Afrika za kusini ya Jangwa la Sahara na nafuu zaidi barani Ulaya (UNESCO, 2019, uk. 148-149).

Kwa nchi za Afrika za kusini ya Jangwa la Sahara, Klingholz na wengine (2017) wanaelezea ukosefu wa elimu (bora) kama chanzo kikuu cha changamoto nyingi: Vijana mara nyingi watalazimika kujikimu kimaisha kwa urahisi kama vibarua katika shughuli za kilimo au kazi zisizo hitaji ujuzi maalumu. Kaps na wengine (2019) wanaeleza kwamba “upungufu wa elimu na ukosefu wa fursa za mapato huzuia maendeleo ya kiuchumi na hivyo kufanya iwe vigumu kwa watu kuepuka mtego wa umaskini” (Kaps na wengine 2019, uk. 6). Dresen na wengine (2020) wanaonyesha katika utafiti wa UNICEF kwamba majibu yanayofaa yanahitajika. Utafiti wao wa kufungwa kwa shule katika zaidi ya nchi 120 unahitimisha kuwa hakuna mbinu au mtindo mmoja zinazofaa wote za kutoa mafunzo kwa mbali kupitia kwa mtandao. Mbali na tofauti kubwa za kimataifa katika upatikanaji wa mtandao, TV na redio (takriban 3% tu ya maeneo katika nchi kama Guinea-Bissau yana umeme), UNICEF inapendekeza kutumia njia nyingi za kuwasilisha mafunzo. Nchini Jordan, kwa mfano, watoto wakimbizi walipokea vifurushi vya kujifunza; kwingineko, kampuni za mawasiliano ya simu hazikutoza gharama za data kwa maudhui ya elimu na kadi za SD kwa simu smati zilizopakiwa awali masomo zenye vifaa vya kusikiliza ziliwasilishwa kwa

Kielelezo 11: Pana uwezekano mkubwa wa walio na elimu ya juu kuhama (kima cha wahamiaji kulingana na kiwango cha elimu, nchi zilizochaguliwa, vipindi vya miaka mitano mitano 2010-1999)



Ulimwenguni, walio na elimu ya juu huwa na uwezekano mkubwa wa kuhama kutoka nchi zao na kiwango cha wahamiaji hao katika nchi za Afrika Magharibi, Kati, Mashariki na Kusini ni cha juu zaidi ikilinganishwa na maeneo mengine. Chanzo: UNESCO (2019, uk. 16). Kielelezo chetu.

familia katika maeneo ambayo ni magumu kufikiwa nchini Burundi; TV hutumiwa na nchi nyingi kutoa elimu.

Wanafunzi walio katika mazingira magumu zaidi pia ni miongoni mwa wale ambao hawana uwezo wa kufikia vyombo vya habari vya kidijitali na kujifunza kwa mbali, na wengi hawajui lugha ya kufundishia kwa ufasaha (UN, 2020a, uk. 7). Kwa hiyo Umoja wa Mataifa unaonya vikali: “Kuzuia shida ya kujifunza kutokea kuwa janga la kizazi kunahitaji hatua za haraka kutoka kwa wote” (UN, 2020a, uk. 3).

Mabadiliko ya hali ya hewa

Athari zinazozidi kuwa mbaya za mabadiliko ya hali ya hewa zinatarajiwa kuhamisha mamilioni ya watu ndani (kuongeza idadi ya IDPs) katika kanda tatu za dunia — nchi za Afrika za kusini ya Jangwa la Sahara, Asia Kusini na Amerika Kusini. Katika hali inayobashiri mabaya zaidi kati ya hali tatu (uzalishaji mkubwa wa gesi chafu na njia zisizo sawa za maendeleo), kufikia 2050 karibu watu milioni 143 (asilimia tatu ya jumla ya watu katika maeneo hayo mitatu), huenda wakalazimishwa kuhama kutoka makwao hadi pengine mahali salama. Makadirio haya ya mabadiliko ya hali ya hewa, uhamiaji, uhamishwaji wa kulazimishwa na maendeleo, iliyochapishwa na Benki ya Dunia katika utafiti wa kihistoria unaoitwa “Groundswell” (Rigaud na wengine, 2018; Benki ya Dunia, 2018a), inatoa mitazamo ya kutisha hata katika pendekezo kwamba kuimarisha hali ya hewa kuzingatia njia za maendeleo huenda kukaboresha mambo. Kwa Afrika, uhamaji wa ndani kutokana na mabadiliko ya hali ya hewa utaongezeka katika hali zote tatu kutokana na kupunguka kwa kiasi cha maji uzalishaji wa mazao sambamba na kupanda kwa kina cha bahari na mawimbi ya dhoruba (Benki ya Dunia, 2018a, uk. 1; ona Mchoro 12). Kufikia 2050, jumla ya idadi ya IDPs kutokana na mabadiliko ya hali ya hewa “inaweza kuwa juu kama milioni 85.7 au asilimia nne ya jumla ya wakazi wa eneo hilo” tukizingatia ubashiri wa hali ya kukata tamaa, kiwango cha juu kuliko Asia Kusini na Amerika ya Kusini; hali bora zaidi (“inayofaa kwa hali ya hewa”) inabashiri kwamba watu milioni 28.3 watahamishwa (Benki ya Dunia, 2018a, uk. 2).


Pana utafiti mwingi wa kinadharia na kitaalamu kuhusu mabadiliko ya hali ya hewa yanayosababisha uhamiaji na uhamishwaji wa lazima na (utafiti) umeongezeka katika miongo mitatu iliyopita (Migration Data Portal, 2020c). Wakati wa kuandika mwongozo huu 2020, mwauo wa maandishi ulichapishwa na kutoa muhtasari wa hivi majuzi wa mada (Flavell na wengine, 2020). Kama ilivyoainishwa katika sehemu ya migogoro (tazama maelezo ya awali), idadi ya IDPs ni kubwa kuliko wale waliovuka mipaka ya nchi (wakimbizi), na haiangaziwi kikamilifu kimataifa. Hii inatumika pia kwa watu ambao wanahamishwa kwa sababu ya mabadiliko ya hali ya hewa. IDMC inalalama kwamba IDPs “wanafukuzwa ndani lakini wanapuuzwa kimataifa” (Bilak, 2020). Hata baadhi ya hati za kawaida za marejeleo za kimataifa kama vile SDGs hazishughulikii kundi hili kwa uwazi (Zeender, 2018). Vyanzo vichache barani Afrika vinaweka masuala haya hadharani — kwa mfano, mfululizo wa “Mabadiliko ya Tabianchi na Uhamiaji Barani Afrika” wa Tovuti ya

Afrika (2020) na muhtasari wa mara kwa mara wa wanahabari (Fagan, 2019), kutaja mifano miwili tu.

Kuna makubaliano, “Groundswell” inahakikisha, kwamba uhamishwaji unaosababishwa na mabadiliko ya hali ya hewa ndani ya nchi — badala ya kuhamia kwenye mipaka ya kimataifa — utaendelea kuwa “jambo kubwa zaidi” (Benki ya Dunia, 2018a, uk. 2). Changamoto kubwa za maendeleo zinadokezwa, na ripoti inatoa hoja thabiti ya “hatua za pamoja za kukabiliana na mabadiliko ya hali ya hewa, pamoja na sera za maendeleo jumuishi na kushirikisha uhamiaji kutokana na hali ya hewa katika mipango ya sera” (Benki ya Dunia, 2018a, uk. 1). Kuzingatia tu mawazo hayo, Klingholz na wengine (2020) wanatetea mwelekeo mpya wa sekta ya kilimo endelevu Afrika na tija zaidi ili kulisha watu ambao idadi yao inazidi kuongezeka; misingi ya “mkurupuko huu mkubwa ni utafiti, maendeleo na usambazaji wa uvumbuzi wa kiufundi na kijamii, pamoja na uhamishaji wa maarifa na ujasiriamali” (Klingholz na wengine, 2020, uk. 67).

Ripoti ya “Groundswell” inahusu wahamiaji kutokana na hali ya hewa, sio wakimbizi wa hali ya hewa. Uamuzi huu wa uhariri unalingana na sheria za kimataifa na msimamo wa UNHCR wa kushikilia ufafanuzi wa mkimbizi.¹⁷ Katika mjadala wa hadhara na hata katika faharasa zilizo-pendekezwa na mwongozo huu, matumizi na ufafanuzi wa istilahi hutofautiana — katika matu-

Kielelezo 12: Makadirio ya hali tatu zinazobashiriwa kufikia 2050 za idadi na wahamiajiwa ndani kutokana na athari za hali ya anga katika nchi za Afrika Magharibi, Kati, Mashariki na Kusini



Chanzo: Banki ya Dunia (2018a, p. 2, figure 1). Kielelezo chetu

17 Kumbuka fasili zilizojadiliwa katika Moduli ya 2. “Mkimbizi” anafafanuliwa kama mtu ambaye amevuka mpaka wa nchi wa kimataifa “kwa sababu ya kuhofia kuteswa kwa sababu za rangi, dini, utaifa, uanachama wa kikundi fulani cha kijamii au kisiasa.” kulingana na Mkataba wa 1951 unaohusiana na Hadhi ya Wakimbizi.

mizi, kwa mfano, mazingira, wahamiaji, wakimbizi wa hali ya hewa — na wakati fulani ufafanuzi hujumuisha watu waliohamishwa baada ya ajali za viwandani (EMN, 2018; IOM, 2019a; Ionesco na wengine, 2017; UNHCR, 2020a). Mwongozo huu unarejelea uhamishwaji unaosababishwa na hali ya hewa, ukiunganisha na ukweli kwamba watu wengi wamehamishiwa ndani. Maneno yoyote ambayo waandishi na taasisi huchagua — wote wanakubali kwamba IDPs wana mahitaji makubwa ya kibinadamu, wanakumbwa na udhaifu na wanahitaji ulinzi. Upungufu wa data ulioainishwa katika Moduli 2 kuhusu uhamiaji na uhamishwaji wa lazima unadhihirika zaidi kuhusu IDPs na hasa kwa kuzingatia watu waliohamishwa kutokana na mabadiliko ya hali ya hewa. IDMC inaripoti kwa mfano kwamba uhamishwaji wa watu kutokana na ukame haujakadiriwa kwa kuwa data imekuwa ikipatikana kwa nchi chache tu tangu 2017 (André na wengine, 2019, uk. 19). Kulingana na chanzo hiki, majanga — majanga ya asili, ukiondoa ajali za viwandani — yalisababisha watu milioni 2.6 kuhamishwa 2018 na zaidi ya milioni 21.2 kati ya 2009 na 2018. Jumla ya 85% ya watu wote waliorekodiwa barani Afrika tangu 2009 wamehamishwa na janga la mafuriko. Vimbunga vya Idai na Kenneth vilisababisha maafa makubwa zaidi mwaka 2019, huku watu milioni 2.2 wakiathiriwa, na 617,000 waliokimbilia makazi mapya nchini Msumbiji, Malawi, Zimbabwe na Madagaska (André na wengine, 2019, uk. 19, uk. 24). Shirika la habari za maendeleo The New Humanitarian limeeleza hisia kuhusu Praia Nova, mtaa wa mabanda katika mji wa bandari wa Beira, Msumbiji, ambao ulikuwa wa kwanza kukumbwa na kimbunga Idai. Kitongoji cha karibu watu 500,000 kiliharibiwa pakubwa. Familia bado zimevurugika zisijue zikae nyumbani katika makazi ya dharura, huku zikitarajia kujengewa upya, ama kuhamia katika makazi mapya yanayoungwa mkono na serikali na vikundi vya misaada katika vijiji vilivyo mbali na maeneo ya mabondeni yanayokumbwa na mafuriko (Kleinfeld, 2019).

Ripoti ya “Groundswell” inahitimisha kuwa uhamiaji wa ndani kutokana na hali ya hewa “huenda ukaongezeka hadi mwaka 2050 na kisha kuharakishwa isipokuwa kuwe na upungufu mkubwa wa uzalishaji wa gesi chafu na hatua thabiti za maendeleo zichukuliwe” (Rigaud na wengine, 2018, uk. xix).

Mitandao ya kikabila (diaspora)

Utafiti kuhusu mitandao na uhamiaji mara nyingi huchukulia kuwa watu binafsi wana uwezekano mkubwa wa kuhamia mahali ambapo wana uhusiano mwingi. Hii ni kweli lakini sio simulizi kamili. Mitandao mikubwa inaweza kuzuia uhamaji, kwa mfano ikiwa wahamiaji watahindania fursa na rasilimali na kuhisi ushindani fulani kuhusu kusambaziana habari (Blumenstock na wengine, 2019, uk. 2-3), au wakati wamekatishwa tamaa kwa kukosa ulinzi na kinga za wenzao (Kuschminder, 2016).

Mitandao ya wanajamii waliotawanyika katika nchi za nje (diaspora) pamoja na familia na marafiki nyumbani na nje ya nchi, hata hivyo, imetambuliwa kama msukumo muhimu wa uhamiaji. Pana uwezekano mkubwa wa watu kwenda mahali ambapo wanawafahamu wahamiaji wengine ambao wamehamia huko hivi karibuni, na mitandao hii ina jukumu la kipekee katika kutoa

msaada (nyenzo, kijamii) na kama chanzo cha habari kuanzia katika hatua ya kupanga, wakati wa safari hadi kufika kikomo kwa kuwezesha, na hata kushawishi maamuzi ya nchi lengwa (Chuo Kikuu cha Maastricht, & GDMAC, 2016, uk. 21-22). Kama Blumenstock na wengine, (2019) alivyotoa mfano wa Rwanda, mtandao wa kijamii wa mhamiaji mmoja ni mpana.

Pamoja na umuhimu wa kulenga mtandao wa jamii zilizotawanyika nje ya nchi, familia na jamaa nyumbani ndio chombo kinachofanya maamuzi, kinachowatuma washiriki wao kupitia njia za kawaida au zisizo za kawaida za uhamiaji, mara nyingi huwezesha na matumizi ya mitandao ya jamii (Cummings na wengine, 2015; Fleischer, 2006; Tovuti ya Data ya Uhamiaji, 2020b; Simpson, 2017). Kwao, kumwezesha mwanajamii anayeamnika na fedha na kumtuma nje ya nchi, mara nyingi huonekana kama mkakati mseto wa kupanua uwezekano wa familia kujiendeleza na kuzikinga kutokana na hatari.

Kama ilivyoonyeshwa hapo awali, uteuzi huu wa vipengele vya muktadha ni wasilisho lisiloku-muisha yote yanayohitajika. Waelimishaji wa uanahabari wanaotumia mwongozo huu watapata msukumo wa kualika madarasa yao kutafakari kwa kina juu ya haya na mambo mengine ya muktadha; inatarajiwa kuwa watachangia kukamilisha picha kwa kufichua mitazamo ya nchi zao.



ILIYOPENDEKEZWA KUSHUGHULIKIA STADI ZA UTAMBUZI ZA UELEWA NA KUTEKELEZA NA STADI ZA MITAZAMO YA KIBINAFSI NA MAADILI ZA KUPOKEA KWA KUIWASILISHA KATIKA UANAHABARI:

Waalike washiriki kuandaa muhtasari wa kurasa mbili wa somo kuhusu vipengele vya muktadha, wakitumia nchi yao ya asili au nchi wanayochagua kufanyia uchanganuzi wa kifani. Ruhusu wanafunzi kuchagua kati ya mada mbili na kuwauliza waeleze nadharia na msingi wa utafiti wao kwa kutumia maandisho ya kitaaluma.

Mada ya 1: Vigezo vya ziada vya muktadha wa uhamiaji

Eleza nadharia iliyoainishwa katika moduli hii na ueleze ni sababu zipi za muktadha kuhusu uhamiaji zinafaa kwa nchi yako — au nchi unayochagua — na kwa nini. Kwa kuongeza, fikiria mambo yote ya kuvutia au misukumo ambayo haijawasilishwa katika moduli hii na ueleze umuhimu wake.

- Tambua umuhimu wa vipengele vya muktadha wa kuripoti masuala ya uhamiaji na uhamishwaji wa lazima kwa kuchunguza jinsi chombo kimoja cha habari katika nchi uliyochagua kinavyoripoti kuhusu uhamiaji kwa wiki moja (chagua wiki moja yenye habari nyingi zaidi za uhamiaji): Tambua ni vipengele vipi vya msukumo/mvuto vilivyoshughulikiwa.
- Tambua mambo ya muktadha ambayo huleta pamoja wahamiaji na wakimbizi katika mtiririko mchanganyiko.
- Viweke vipengele vya maudhui katika muktadha na kuviwasilisha katika kurasa mbili.

Mada ya 2: Wakimbizi katika hali ya hatari nyingi

Wakimbizi wanateswa nyumbani na kulazimika kuvuka mipaka ya nchi wakitafuta hifadhi. Kwa sababu wanateswa, wanakabiliwa na changamoto za ziada ambazo, mwanzoni, zinaweza kuonekana kama sababu za kuwasukuma kuhama, kwa mfano ukosefu wa fursa za ajira. Chukua mwanahabari mwanamke kama mfano na ueleze hatari na changamoto zake nyingi katika nchi yako au nchi unayochagua. Chagua kutoka kwa simulizi za maisha zilizokusanywa na Kamati ya Kulinda Wanahabari (CPJ, 2020).

- Eleza nadharia na uegemeze utafiti kwa maandishi ya kitaaluma.
- Tambua umuhimu wa vipengele vya muktadha wa kuripoti kuhusu wakimbizi wanawake: Je, hatari zao mahususi ni zipi?
- Weka muktadha wa mambo ya msukumo/mvuto kwa kuchunguza jinsi wakimbizi wanawake wanavyowasilishwa kwenye vyombo vya habari. Kwa kuchunguza utangazaji wa vyombo vya habari kuhusu wanawake katika chombo cha habari unachokipenda kwa muda wa mwezi mmoja (chagua mwezi wenye habari nyingi): Je, wanawake kama wakimbizi wanawasilishwaje, na je, wanasikilizwa?
- Tambua vipengele vya muktadha kwa wakimbizi wanawake na ueleze jinsi walivyo wakati mwingine katika mtiririko mchanganyiko pamoja na wahamiaji.



USOMAJI WA ZIADA:

Kiakademia:

Piché, V. (2013). Contemporary migration theories as reflected in their founding texts. *Population*, 68(1), 141-164. <https://doi.org/10.3917/popu.1301.0153>

Kiuanahabari:

News Deeply (n. d.). Articles. Retrieved January 5, 2021, from <https://deeply.thenewhumanitarian.org/>

Kitaasisi:

IOM (2019b). World migration report 2020. Geneva. Retrieved December 15, 2020, from https://publications.iom.int/system/files/pdf/wmr_2020.pdf

UNDESA (2019b). International Migration 2019: Report. New York. Retrieved December 15, 2020, from https://www.un.org/en/development/desa/population/migration/publications/migrationreport/docs/InternationalMigration2019_Report.pdf

UNHCR (2020b). Global Trends: Forced displacement in 2019. Copenhagen. Retrieved December 15, 2020, from <https://www.unhcr.org/5ee200e37.pdf>

JINSIA

na *Monika Lengauer*

Maneno jinsia na uana hayapaswi — lakini yanatumiwa — kutumiwa kwa kubadilishana. Jinsia inaelezea sifa za wanawake, wanaume au utambulisho mwingine wowote, ambao umeundwa kijamii, wakati uana ni hali za maumbile ambazo zimeamuliwa kibaiolojia (“uainishaji kulingana na mwonekano wa sehemu ya siri wakati wa kuzaliwa” (LGBT Resource Center, n. d.). Utambulisho wa kijinsia na majukumu ya kijinsia pia huamua mambo wanayokumbana nayo wanawake, wasichana, wanaume, wavulana na walio katika kikundi cha LGBTI wakiwa wahamiaji na wakimbizi. Katika ukusanyaji wa data, hata hivyo, jinsia na uana hutumiwa mara kwa mara kumaanisha kitu kimoja na jinsia mara nyingi huangazia wanawake pekee; kwa kuongeza, data huwa haiainishwi kamwe kwa utambulisho wa LGBTI (Migration Data Portal, 2020). Data iliyoainishwa kijinsia ni muhimu kwa utungaji sera na mipango inayotegemea ushahidi, na Mkataba wa Kimataifa wa Uhamiaji na Mkataba wa Kimataifa wa Wakimbizi imejitolea kuboresha upungufu huu (Hennebry & Petrozziello, 2019; UN, 2018; UNGA, 2018). Kwa kuhitimisha kutokana na data iliyoainishwa inayopatikana, wanawake wanachangia karibu 50% ya watu wote waliohamishwa kwa lazima — wakimbizi, wakimbizi wa ndani (IDPs) au watu wasio na utaiifa (UNHCR, 2020)¹. Sehemu ya wanawake katika uhamiaji wa kimataifa haijabadilika sana katika miongo ya hivi majuzi lakini wahamiaji zaidi wanawake wanahama kivyao kwa ajili ya kazi, elimu na kama wakuu wa boma zao (Migration Data Portal, 2020).

Uga wa utafiti wa jinsia na uhamiaji ni fani thabiti ya utafiti wa jinsia na uhamishwaji wa kulazimishwa². Kuhusu tafiti za uhamiaji, “wasomi sasa wanasisitiza kuwa uhamiaji wenyewe ni suala la kijinsia na unahitaji zana za kinadharia na uchanganuzi kuliko masomo ya majukumu ya kiuana.” (Donato na wengine ., 2018, uk. 6-7). Tafiti za wakimbizi zimechunguza masuala ya kijinsia kutoka kwa wigo mpana, ikijumuisha uchunguzi wa misingi ya kisheria na kimaadili kwa watu binafsi kupata hifadhi na ulinzi dhidi ya unyanyasaji unaohusiana na jinsia (Gerver & Millar, 2013). Katika mkusanyiko wao uliohaririwa wa jinsia, unyanyasaji na wakimbizi, Buckley-Zistel na Krause (2019) wanafafanua kuhusu sio tu dhana hizi na zingine bali pia unaruhusu maarifa katika wigo mpana wa uchanganuzi kifani — ikiwa ni pamoja na masuala ya LGBTI — kutoka Angola kusini mwa Afrika hadi Uswizi katika Ulaya ya Kaskazini. Katika uhamiaji na uhamaji wa binadamu, jinsia ina “athari kubwa zaidi” kwa yale ambayo wanawake, wasichana, wanaume, wavulana na watu wanaojitambulisha kama LGBTI hukumbana nayo (Migration Data Portal, 2020). Jinsia huathiri nia, njia na mitandao ambayo watu hutumia, wanayokumbana nayo, mapokezi, fursa za kujiendeleza, vikwazo na hatari zinazowakabili nyumbani, katika usafiri na katika nchi

1 Wanawake wanachangia karibu 48% ya hifadhi ya kimataifa ya wahamiaji. Kumbuka kwamba “[Stocks] anawajumuisha wakazi wote waliozaliwa nje ya nchi bila kujali waliingia nchini lini”. Kwa hivyo data hizi haziwezi kulinganishwa na data ya UNHCR kuhusu watu waliohamishwa kwa lazima. Tazama ukurasa wa mandhari ya Tovuti ya Data ya Uhamiaji “Jinsia na Uhamiaji” kwa vyanzo vya data (Portal Data ya Uhamiaji, 2020).

2 Mwauo wa maandishi unaonyesha upeo wa nyanja zote mbili, kwa mfano Fleury (n. d.) au Kituo cha Pamoja cha Data kuhusu Uhamishwaji wa Kulazimishwa (2020).


kikomo cha safari zao huwezesha kutunga mijadala katika vyombo vya habari na sera (Schrover & Moloney, 2013). Ni wazi kuna mengi tofauti katika makundi haya lakini pia kuna hatari ambazo wote wanaweza kukumbana nazo na zikawaathiri wawe wanawake, wanaume ama LGBTI kama vile unyanyasaji na dhuluma za kijinsia. Utafiti — kwa mfano, mkusanyiko uliohaririwa hapo awali na Buckley-Zistel & Krause (2019), taasisi na vyombo vya habari zimeweka hadharani uhalifu wa kutisha wa unyanyasaji wa kingono na dhuluma. “Wanawake wakimbizi” ni utafiti uliofanywa na UNHCR huko El Salvador, Guatemala, Honduras na Mexico ukifichua “viwango vya janga la mlipuko wa unyanyasaji” ambavyo “vimevuka uwezo wa serikali kulinda waathiriwa” (UNHCR, 2015, uk. 2) katika sehemu kubwa za nchi, na ambapo wanawake hukimbia mauaji, unyang’anyi na ubakaji. Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo imekumbwa na uhamishwaji wa lazima kufuatia ubakaji kutokanana migogoro, ingawa gazeti la The Washington Post limechaphisha ukanusho wa waasi kuhusu ukiukaji wao wa haki za binadamu (Wilén & Ingelaere, 2017).

Wanawake wanakabiliwa na ubaguzi maalumu na hukumbwa na hatari mahsusi za wazi wakiwa wahamiaji na wakimbizi, hasa katika ulanguzi wa binadamu (tazama Kielelezo 13). Ulanguzi wa binadamu ni uhalifu.³ Unafuata kwa upana njia na mifumo ya uhamiaji na uhamishwaji wa kulazimishwa. Kulingana na ripoti ya kimataifa ya UNODC ya 2018 kuhusu ulanguzi wa binadamu, “wanawake wanawakilisha idadi kubwa ya wahasiriwa wa biashara hiyo kwa unyanyaswaji wa kingono, na wanawake na wasichana ni 35% ya wahasiriwa wanaosafirishwa kwa kazi ya kulazimishwa” (UNODC, 2018, uk. 10). Ripoti inaelekeza kwenye “tofauti kubwa za kikanda katika jinsia na wasifu wa umri wa waathiriwa wa ulanguzi wa binadamu. [...] Katika Afrika Magharibi, wengi wa waathiriwa waliogunduliwa ni watoto, wavulana na wasichana, katika Asia Kusini, waathiriwa kwa usawa wanaripotiwa kuwa wanaume, wanawake na watoto” (UNODC, 2018, uk. 10). Katika Asia ya Kati, idadi kubwa ya wanaume watu wazima husafirishwa kuliko sehemu nyingine za dunia; katika Amerika ya Kati na Caribbean, wasichana zaidi wamerekodiwa (UNODC, 2018, uk. 10).

Wanawake wanaotoroka migogoro huwa hatarini kubwa sana. Haja ya kuchukua hatua za haraka imetambuliwa na Tuzo ya Amani ya Nobel la 2018, ambalo lilitolewa kwa Denis Mukwege na Nadia Murad, ambao walitunukiwa “kwa juhudi zao za kukomesha unyanyasaji wa kijinsia kama silaha ya vita na migogoro ya silaha” (Nobel Prize Committee, 2018). Denis Mukwege, daktari wa upasuaji kutoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, “amewatibu maelfu ya waathiriwa wa unyanyasaji wa kijinsia katika migogoro ya silaha, na amekosoa serikali kwa kutofanya vya kutosha kukomesha unyanyasaji wa kijinsia dhidi ya wanawake kama mkakati wa maisha na silaha ya vita” (Nobel Prize Committee, 2018). Nadia Murad alianzisha Nadia’s Initiative (Nadia’s

3 “Kuajiri, kusafirisha, kuhamisha, kuhifadhi au kupokea watu, kwa njia ya tishio au matumizi ya nguvu au aina zingine za kulazimishwa, utekaji nyara, udanganyifu, kulaghaiwa, matumizi mabaya ya madaraka, au ya kutoa au kupokea malipo au manufaa ili kumshurutisha mtu kukubali kudhibitiwa na mtu mwingine, kwa madhumuni ya ukandamizaji. Ukandamizaji utajumuisha, kwa uchache, utumiaji mabaya wa ukahaba wa wengine au aina nyingine za unyanyasaji kingono, kazi au huduma za kulazimishwa, utumwa au mazoea sawa na utumwa, utumwa au kuondolewa kwa viungo.” Chanzo: mkataba unaoangazia wa kuzuia na kuadhibu ulanguzi wa binadamu, hasa wanawake na watoto (Protocol to Prevent, Suppress and Punish Trafficking in Persons, Especially Women and Children) pamoja na Mkataba wa Umoja wa Mataifa Kupambana na Uhalifu wa Magenge wa Kimataifa —, United Nations Convention against Transnational Organized Crime (IOM, 2019, uk. 213).

Kielelezo 13: Takwimu za waathiriwa wa ulanguzi wa binadamu katika kanda za ulimwengu za 2016 (au za karibuni zaidi) ambazo zinaonyesha mikondo mbalimbali



Uchunguzi wa UNODC unaonyesha kwamba wanawake na wasichana hutekwa nyara na kuingizwa utumwani wa ngono na ndoa za lazima katika nchi zinazokumbwa na machafuko za Afrika ya Kati na Magharibi, na Mashariki ya Kati. (UNODC, 2018, uk. 12). Chanzo: UNODC, 2018, uk. 10. Kielelezo chetu

Initiative, 2020), shirika lisilo la faida linalojitolea kujenga upya jamii zilizo katika shida na kutetea kimataifa waathiriwa wa unyanyasaji wa kijinsia. Shirika hilo kwa sasa linalenga kujenga upya maeneo ya Wayazidi katika Sinjar (Iraq), ambako Nadia Murad alikulua. Magaidi wa ISIS waliharibu kijiji chake, wakawaua na kuwafanya watumwa na kuwabaka wanajamii (Arraf, 2019; Marczak, 2018; Nobel Prize Committee, 2018). “Utawala wa ulinzi wa kimataifa unawaangusha wakimbizi wanawake na wasichana”, liliandika shirika la ttafiti wa uhamiaji wa kulazimishwa, Forced Migration Research Network, Chuo Kikuu cha New South Wales, kwenye mchango wao katika mchakato shirikishi wa UNHCR hadi kufikia Mkataba wa Kimataifa wa Wakimbizi (Bartolomeina na wengine, 2017). Waandishi pia walidokeza mwanamke akijipata hatarini au katika mazingira magumu haina maana kwamba hiyo ndiyo hali yake “asili ya mazingira magumu” au kuwa mwathirika asiyejitahidi kujikinga au mnufaika wa misaada asiye na namna. Krause (2020) anaonyesha hili katika utafiti wake kuhusu Uganda, akiwatambua wanawake kama “wahusika wakuu wa kijamii”, na pia “wahusika wakuu katika harakati za wakimbizi”. Katika maelezo ya mkusanyiko wa picha, UN Women inawaonyesha wanawake wakimbizi kama watu waliowezes-hwa licha ya maisha yao katika kambi za wakimbizi (UN Women, 2016).

Wanahabari wanawake kama wakimbizi na wahamiaji hawaripotwi kutoka kila pembe, labda isipokuwa chache, kama vile Chuo cha Uanahabari cha Missouri ambacho huchapisha Global Journalist kuwaonyesha wanahabari walio uhamishoni (Global Journalist, 2020) na Maripota Wasio

na Mipaka (2019) pamoja na Kamati ya Kulinda Wanahabari (CPJ, 2020), tukitaja wachache tu. Tovuti ya Refugees Deeply, iliyoandaliwa katika mtandao wa The New Humanitarian, ina hadithi maalumu kuhusu wanawake wanahabari wakimbizi kutoka Libya (Nallu, 2016).

Fleury (n. d.) anafichua katika mwauo wa maandishi kuhusu wanawake na uhamiaji jinsi nyanja ilivyo pana na ni tafiti jarabati ngapi tofauti zimetoa mwanga katika vipengele tofauti. “Hali ya masomo ya jinsia na uhamiaji ni thabiti kimsingi [...] [pamoja na] wimbi la kweli tangu mwishoni mwa miaka ya 1980 la utafiti”, wakasema Donato na wengine (2018, uk. 6-7).

Katika nyanja ndogo ya uhamiaji na maendeleo, fedha zinazotumwa na wanawake nyumbani husimulia habari zifaazo lakini zilizofichwa katika data za kiuana zilizoainishwa ... Azam na wengine (2020) huhitimisha kutokana na utafiti mdogo unaohusu nchi 11⁴ kwamba wanawake wahamiaji wanatuma nyumbani sehemu kubwa ya mapato yao, na kutuma kiasi au hata zaidi kuliko wanaume. Utafiti huu unaonekana kuthibitisha utafiti wa awali ambao unaonyesha wanawake wahamiaji nchini Uhispania walituma 38.5% ya mapato yao ikilinganishwa na wanaume walio-tuma 14.5% (Fleury, n. d., uk. 14). Mifumo hii ya utumaji pesa za wanawake hutokea licha ya pengo la malipo ya kijinsia duniani ambapo wanalipwa kwa wastani wa 20% chini ya wanaume na licha ya mapendekezo mahususi ya wanawake katika njia za uhawilishaji fedha: Inasemekana kwamba wanawake wanapendelea kutumia biashara za kutuma pesa huku wanaume wakitumia teknolojia za kutuma pesa kupitia kwa simu mara nyingi. Mwenendo huu umefafanuliwa na mgawanyiko unaoendelea wa jinsia wa kidijitali na kiwango cha chini cha elimu ya kidijitali kwa wanawake. Wanawake wanaripotiwa kutuma kiasi kidogo lakini mara nyingi, jambo ambalo husababisha gharama kubwa kwao (Azam na wengine, 2020, uk. 4; Fleury, n. d., uk. 15). Katika hatua ya kupokea, tafiti kadhaa zimeonyesha kuwa wanawake hutumia pesa kuboresha ustawi wa familia zao; wanawekeza katika afya na elimu ilhali wanaume wanaopokea fedha hununua mali (Fleury, n. d., uk. 15). Wanawake ndio kiini cha mchakato wa maendeleo, na uwekezaji katika sekta ya elimu unahitajika haraka kwa sababu elimu “ni jambo kuu katika kupunguza viwango vya uzazi, ambapo elimu ya wanawake ina taathira kubwa” (Kaps na wengine, 2019, uk. 12).

Tofauti nyingine kati ya wanawake wahamiaji na wanaume ni kutengwa katika uhamiaji wa wafanyikazi. Wanaume huwa na kazi katika uzalishaji bidhaa au ujenzi. Wanawake wahamiaji kwa ujumla hufanya kazi za nyumbani au huwa walezi. Wafanyakazi wanawake wenye ujuzi wa chini ni wasaidizi na walezi wa nyumbani, wanawake wenye ujuzi wa juu, kwa mfano ni wale walio katika nafasi za uuguzi (Fleury, n. d., uk. 10-11). Wafanyakazi wahamiaji wanawake mara nyingi hukabiliwa na unyanyasaji, kazini na pia majumbani mwao, kama Hiralal (2017) alivyoandika kuhusu wanawake wahamiaji nchini Afrika Kusini. “Ni muhimu kukomesha uhamiaji usiozingatia jinsia”, linasihi UN Women, ambalo pia linakumbuka mashirika muhimu ya Umoja wa

4 Utafiti hauwakilishi ipasavyo na una upeo mdogo kwa kuwa unarejelea tafiti za kitaifa za maboma kutoka nchi 11 ambapo jinsia ya watumaji pesa imejumuishwa kama kigezo katika hazinadata pamoja na thamani ya fedha zinazotumwa kutoka kwa mtumaji. Kati ya nchi hizo 11 ni sita za Afrika (Burkina Faso, Kenya, Nigeria, Senegal, Uganda, Tanzania), tatu za Asia ya Kusini (Bangladesh, India, Nepal) na mbili kutoka Ulaya Mashariki/Asia ya Kati (Albania na Tajikistan; Azam na wengine, 2020, uk. 4).

Mataifa ya haki za binadamu yanayoshughulikia uhusiano kati ya jinsia na uhamiaji, ikiwa ni pamoja na Kamati ya Wafanyakazi wa Uhamiaji (CMW), Kamati ya Kutokomeza Ubaguzi dhidi ya Wanawake (CEDAW), Kamati ya Kutokomeza Ubaguzi wa Rangi (CERD), na Kamati ya Haki za Kiuchumi, Kijamii na Kiutamaduni (CESCR; von Hase, 2017).



USOMAJI WA ZIADA:

Kiakademia:

Buckley-Zistel, S., & Krause, U. (Eds.) (2019). Gender, Violence, Refugees. Forced Migration. New York: Berghahn.

Kiakademia/kiuanahabari:

Global Journalist (2020). Project Exile. Retrieved January 22, 2020, from Global Journalist website: <https://globaljournalist.org/2018/01/8964/>

Kitaasisi:

Migration Data Portal (2020). Gender and migration. Retrieved December 20, 2020, from <https://migrationdataportal.org/themes/gender>

Marejeleo: Jinsia

Arraf, J. (2019). 'We Pray For The Caliphate To Return': ISIS Families Crowd Into Syrian Camps. KUNC, Community Radio for Northern Colorado. Retrieved May 11, 2020, from <https://www.kunc.org/post/we-pray-caliphate-return-isis-families-crowd-syrian-camps#stream/0>

Azam, M., Rodgers, Y., Stewart-Evans, M., & von Hase, I. (2020). Migrant women & remittances: Exploring the data from selected countries (Policy Brief). New York. Retrieved October 15, 2020, from <https://www.unwomen.org/-/media/headquarters/attachments/sections/library/publications/2020/policy-brief-migrant-women-and-remittances-exploring-the-data-from-selected-countries-en.pdf?la=en&vs=2913>

Bartolomei, L., Dixon, T., Sheikh-Eldin, M., Zahau, C., & Pittaway, E. (2017). Gender audit report on the second and third thematic discussion on the Global Compact on Refugees: Recommendations from the Gender Audit Team, University of New South Wales Forced Migration Research Network. Geneva. Retrieved October 16, 2020, from <https://www.unhcr.org/events/conferences/5a251b537/gender-audit-report-second-third-thematic-discussions-global-compact-refugees.html>

Buckley-Zistel, S., & Krause, U. (Eds.). (2019). Gender, Violence, Refugees. Forced Migration. New York: Berghahn.

CPJ (2020). Defending journalists worldwide. Retrieved December 13, 2020, from <https://cpj.org/>

Donato, K. M., Gabaccia, D., Holdaway, J., Manalansan, M., & Pessar, P. R. (Eds.) (2018). A Glass Half Full? Gender in Migration Studies [Special issue]. International Migration Review, 40(1), 3-26. <https://doi.org/10.1111/j.1747-7379.2006.00001.x>

- Fleury, A. (n. d.). Understanding women and migration: A literature review. Retrieved October 17, 2020, from <https://www.knomad.org/publication/understanding-women-and-migration-literature-review-annex-annotated-bibliography>
- Gerver, M., & Millar, K. (2013). The Gendered Refugee Experience. *St Antony's International Review*, 9(1), 2-10.
- Global Journalist (2020). Project Exile. Retrieved January 22, 2020, from Global Journalist website: <https://globaljournalist.org/2018/01/8964/>
- Hennebry, J. L., & Petrozziello, A. J. (2019). Closing the Gap? Gender and the Global Compacts for Migration and Refugees. *International Migration*, 57(6), 115-138. <https://doi.org/10.1111/imig.12640>
- Hiralal, K. (2017). Women and Migration-Challenges and Constraints – A South African Perspective, 26(2), 158-175.
- IOM (2019). Glossary on Migration. Geneva. Retrieved August 5, 2019, from https://publications.iom.int/system/files/pdf/iml_34_glossary.pdf
- Joint Data Center on Forced Displacement (2020). Forced displacement Literature Review 2019-2020. Washington, D.C. Retrieved December 19, 2020, from <http://documents1.worldbank.org/curated/en/940291575434038147/pdf/Forced-Displacement-Literature-Review-2019-2020.pdf>
- Kaps, A., Schewe, A.-K., & Klingholz, R. (2019). Africa's demographic trailblazers: How falling fertility rates are accelerating development. Berlin. Retrieved August 14, 2020, from https://www.berlin-institut.org/fileadmin/Redaktion/Englisch/Studien/Africa_s_Demographic_Trailblazers/Pressemitteilung_Afrikas_demografische_Vorreiter_en_final.pdf
- Krause, U. (2020). Rethinking Refuge: Rethinking refugee women's power and vulnerability. Retrieved October 16, 2020, from <https://www.rethinkingrefuge.org/articles/rethinking-refugee-women>
- LGBT Resource Center (n. d.). General definitions. University of California, San Francisco. Retrieved October 17, 2020, from <https://lgbt.ucsf.edu/glossary-terms>
- Marczak, N. (2018). A Century Apart: The Genocidal Enslavement of Armenian and Yazidi Women. In Connellan, M. M. & Fröhlich, C. J. (Eds.), *Rethinking political violence. A Gendered Lens for Genocide Prevention* (pp. 133-162). London: Palgrave Macmillan.
- Migration Data Portal (2020). Gender and migration. Retrieved December 1, 2020, from <https://migrationdata-portal.org/themes/gender>
- Nadia's Initiative (2020). Nadia's Initiative. Retrieved November 10, 2020, from <https://www.nadiasinitiative.org/>
- Nallu, P. (2016, May 3). High profile to exile. Part 1: Libyan female journalists. *News Deeply*. Retrieved October 17, 2020, from <https://deeply.thenewhumanitarian.org/refugees/articles/2016/05/04/high-profile-to-exile-libyan-female-journalists>
- Nobel Price Committee (2018). The Nobel Peace Prize 2018: Nadia Murad and Denis Mukwege. Retrieved January 1, 2020, from <https://www.nobelprize.org/prizes/peace/2018/murad/facts/>
- Reporters Without Borders (2019). Support for exile journalists. Retrieved December 1, 2020, from <https://rsf.org/en/news/rsf-helps-free-and-independent-voices-resist-country-origin-and-exile>
- Schrover, M., & Moloney, D. M. (2013). Introduction: Making a difference. In Schrover, M. & Moloney, D. M. (Eds.), *Gender, migration and categorisation: Making distinctions between migrants in Western countries, 1945-2010* (pp. 7-53). Amsterdam: Amsterdam University Press.
- UN (2018). Report of the United Nations High Commissioner for Refugees: Global compact on refugees. Retrieved February 4, 2019, from https://www.unhcr.org/gcr/GCR_English.pdf

UN Women (2016). Photo essay: Stories of hope from a Cameroon refugee camp. Retrieved October 15, 2020, from <https://www.unwomen.org/en/digital-library/multimedia/2016/5/photo-refugee-camps-in-cameroon>

UNGA (2018). Global Compact for Safe, Orderly and Regular Migration: Resolution adopted by the General Assembly on 19 December 2018. Retrieved September 25, 2020, from https://www.un.org/en/ga/search/view_doc.asp?symbol=A/RES/73/195

UNHCR (2015). Women on the run: First-hand accounts of refugees fleeing El Salvador, Guatemala, Honduras and Mexico. Washington, D.C. Retrieved October 15, 2020, from <https://www.refworld.org/docid/56307e2a4.html>

UNHCR (2020). Women. Retrieved November 27, 2020, from <https://www.unhcr.org/women.html>

UNODC (2018). Global report on trafficking in persons 2018. New York. Retrieved October 17, 2020, from https://www.unodc.org/documents/data-and-analysis/glotip/2018/GLOTIP_2018_BOOK_web_small.pdf

Von Hase, I. (2017, May 19). Protecting women migrant workers' rights: View from UN Women. Retrieved from <https://europa.eu/capacity4dev/articles/view-un-women-protecting-women-migrant-workers-rights>

Wilén, N., & Ingelaere, B. (2017, August 31). War-torn Congo has been called the 'rape capital of the world.' Here is how fighters think about sexual violence. The Washington Post. Retrieved October 16, 2020, from <https://www.washingtonpost.com/news/monkey-cage/wp/2017/08/28/what-do-rebels-think-about-sexual-violence-in-congo-we-asked-them/>

Marejeleo

4Mi (2018). West Africa: Monthly 4Mi update: Mali and Niger. Retrieved December 16, 2020, from https://www.humanitarianresponse.info/sites/www.humanitarianresponse.info/files/documents/files/4miwestafricaapril2018_0.pdf

Adebayo, A. G. (Ed.) (2012). Managing conflicts in Africa's democratic transitions. Lanham: Lexington Books.

Adenle, A. A., Ford, J. D., Morton, J., Twomlow, S., Alverson, K., Cattaneo, A., Cervigni, R., Kurukulasuriya, P., Huq, S., Helfgott, A., & Ebinger, J. O. (2017). Managing climate change risks in Africa: A global perspective. *Ecological Economics*, 190-201. <https://doi.org/10.1016/j.ecolecon.2017.06.004>

Adepoju, A. (2007). Highly skilled migration: balancing interests and responsibilities and tackling brain drain. Brussels. Retrieved January 5, 2021, from <http://www.sussex.ac.uk/Units/SCMR/drc/research/typesofmigration/RT+1+1+Background+paper+en.pdf>

Afifi, T. (2011). Economic or environmental migration? The push factors in Niger. *International Migration*, 49(D4), e95-e124. <https://doi.org/10.1111/j.1468-2435.2010.00644.x>

Africa Portal (2020). The climate change and migration in Africa: Series. Retrieved October 11, 2020, from <https://www.africaportal.org/features/climate-change-migration-africa-series/>

AfricaNews (2019). Guinea-Bissau: Students protest over threat by teachers to strike: AfricaNews. Retrieved August 19, 2020, from <https://www.africanews.com/2019/02/09/guinea-bissau-students-protest-over-threat-by-teachers-to-strike/>

Aigner, P. (2017). *Migrationssoziologie: Eine Einführung*. Studienskripten zur Soziologie. Wiesbaden: Springer VS.

Alcorta, L., Swedlund, H. J., & Smits, J. (2020). Discrimination and ethnic conflict: A dyadic analysis of politically- excluded groups in sub-Saharan Africa. *International Interactions*, 46(2), 251-273. <https://doi.org/10.1080/03050629.2020.1716748>

- Alesina, A., & Weder, B. (2002). Do corrupt governments receive less foreign aid? *American Economic Review*, 92(4), 1126-1137. <https://doi.org/10.1257/00028280260344669>
- Amodio, F., & Chiovelli, G. (2017). Ethnicity and violence during democratic transitions: Evidence from South Africa. *Journal of the European Economic Association*, 16(4), 1234-1280. <https://doi.org/10.1093/jeea/jvx034>
- André, C., Anzellini, V., Hajžmanová, I., & Leduc, C. (2019). Africa Report on internal displacement. Retrieved December 16, 2020, from <https://www.internal-displacement.org/sites/default/files/publications/documents/201912-Africa-report.pdf>
- Appiah-Nyamekye Sanny, J., Logan, C., & Gyimah-Boadi, E. (2019). In search of opportunity: Young and educated Africans most likely to consider moving abroad. *AfroBarometer*. (288). Retrieved December 16, 2020, from http://afrobarometer.org/sites/default/files/publications/Dispatches/ab_r7_dispatchno288_looking_for_opportunity_africans_views_on_emigration1.pdf
- Asongu, S. (2012). On the effect of foreign aid on corruption. *Economics Bulletin*, 32(3), 2174-2180. <http://dx.doi.org/10.2139/ssrn.2493289>
- AU (2020). Continental Education Strategy for Africa 2016-2025 (CESA 16-25). Retrieved August 18, 2020, from <https://edu-au.org/strategies/185-cesa16-25>
- Baudassé, T., Bazillier, R., & Issifoua, I. (2016). Migration and institutions: Exit and voice (from abroad)? (No. 20). Orléans. Retrieved December 14, 2020, from <https://hal.archives-ouvertes.fr/hal-02484265/document>
- Beauchemin, C., & Bocquier, P. (2004). Migration and urbanisation in francophone West Africa: An overview of the recent empirical evidence. *Urban Studies*, 41(11), 2245-2272. <https://doi.org/10.1080/0042098042000268447>
- Belloc, F. (2011). International economic assistance and migration: The case of sub-Saharan countries. *International Migration*, 543(1), 187-201. <https://doi.org/10.1111/j.1468-2435.2011.00686.x>
- Bellwood, P. S. (2013). *First migrants: Ancient migration in global perspective*. Chichester, West Sussex, UK, Malden, MA: Wiley Blackwell.
- Berry, M., Garcia-Blanco, I., & Moore, K. (2015). A Press coverage of the refugee and migrant crisis in the EU: A content analysis of five european countries. Retrieved January 29, 2021, from <https://www.unhcr.org/protection/operations/56bb369c9/press-coverage-refugee-migrant-crisis-eu-content-analysis-five-european.html>
- Bertocchi, G., & Strozzi, C. (2008). International migration and the role of institutions. *Public Choice*, 137(1/2), 81-102. <https://doi.org/10.1007/s11127-008-9314-x>
- Best, B. (2019). WDR Sport Inside: Trapped in Qatar [YouTube]. Benjamin Best Productions GmbH: WDR; Benjamin Best Productions GmbH. Retrieved October 8, 2020, from <https://www.youtube.com/watch?v=BjgYVHdU0Zo&t=11s>
- Bilak, A. (2020). Internally displaced, internationally disregarded. Retrieved October 12, 2020, from <https://www.internal-displacement.org/media-centres/internally-displaced-internationally-disregarded>
- Blumenstock, J., Chiz, G., & Tanx, X. (2019). Migration and the value of Social Networks. Retrieved January 29, 2021, from http://www.jblumenstock.com/files/papers/migration_networks.pdf
- Boone, P., Fazzio, I., Jandhyala, K., Jayanty, C., Jayanty, G., Johnson, S., Ramachandrin, F., Zhan, Z. (2013). The surprisingly dire situation of children's education in rural West Africa: Results from the CREO study in Guinea-Bissau. Retrieved November 30, 2020, from: <https://www.nber.org/papers/w18971>
- Borderon, M., Sakdapolrak, P., Muttarak, R., Kebede, E., Pagogna, R., & Sporer, E. (2019). A systematical review of empirical evidence on migration influenced by environmental change in Africa. Vienna. Retrieved January 29, 2021, from <http://pure.iiasa.ac.at/id/eprint/15382/1/WP-18-003.pdf>

- Borjas, G. J. (1994). The economics of immigration. *Journal of Economic Literature*, 32(4), 1667-1717. <https://www.jstor.org/stable/2728791>
- Bornman, J., & Cronjé, M. (2020, September 23). South Africa: Xenophobia turns migrants into scapegoats. *allAfrica*. Retrieved October 8, 2020, from <https://allafrica.com/stories/202009230734.html>
- Braithwaite, A., Dasandi, N., & Hudson, D. (2014). Does poverty cause conflict? Isolating the causal origins of the conflict trap. *Conflict Management and Peace Science*, 33(1), 45-66. <https://doi.org/10.1177/0738894214559673>
- Browne, E. (2017). Evidence on education as a driver for migration: K4D Helpdesk Report. Retrieved January 29, 2021, from https://assets.publishing.service.gov.uk/media/598086a0ed915d022b00003c/K4D_HDR_Migration_and_Education.pdf
- Bryceson, D. F. (2019). Transnational families negotiating migration and care life cycles across nation-state borders. *Journal of Ethnic and Migration Studies*, 1-23. <https://doi.org/10.1080/1369183X.2018.1547017>
- Canning, Raja, & Yazbeck (2015). Africa's demographic transition: Dividend or disaster? Washington, D.C. Retrieved January 29, 2021, from <https://openknowledge.worldbank.org/bitstream/handle/10986/22036/AfrDemographicTransitionOVERVIEW.pdf>
- Constant, A. F. (2020): Time-space dynamics of return and circular migration: Theories and evidence. Es-sen: Global Labor Organization (GLO). Retrieved December 15, 2020, from <https://www.econstor.eu/bitstream/10419/210984/1/GLO-DP-0446.pdf>
- Cooray, A., & Schneider, F. (2016). Does corruption promote emigration? An empirical examination. *Journal of Population Economics*, 29(1), 293-310. <https://doi.org/10.1007/s00148-015-0563-y>
- Cummings, C., Pacitto, J., Lauro, D., & Foresti, M. (2015). Why people move: understanding the drivers and trends of migration to Europe. Retrieved December 15, 2020, from <https://www.odi.org/publications/10217-why-people-move-understanding-drivers-and-trends-migration-europe>
- CPJ (2020). Defending journalists worldwide. Retrieved October 13, 2020, from <https://cpj.org/>
- Dao, T., Docquier, F., Maurel, M., & Schaus, P. (2018). Global migration in the 20th and 21st Centuries: The unstoppable force of demography. Retrieved December 6, 2020, from <https://ferdi.fr/publications/global-migration-in-the-20th-and-21st-centuries-the-unstoppable-force-of-demography>
- Davenport, C., Moore, W., & Poe, S. (2010). Sometimes you just have to leave: Domestic threats and forced migration, 1964-1989. *International Interactions*, 29(1), 27-55. <https://doi.org/10.1080/03050620304597>
- Decalo, S. (1992). The process, prospects and constraints of democratization in Africa. *African Affairs*, 91(362), 7-35.
- de Haas, H. (2007). Turning the tide? Why development will not stop migration. *Development and Change*, 38(5), 819-841. <https://doi.org/10.1111/j.1467-7660.2007.00435.x>
- de Haas, H. (2010a). Migration and development: A theoretical perspective. *The International Migration Review*, 44(1), 227-264. <https://doi.org/10.1111/j.1747-7379.2009.00804.x>
- de Haas, H. (2010b). Migration transitions: A theoretical and empirical inquiry into the developmental drivers of international migration (Working Papers No. 24). Retrieved December 15, 2020, from <https://www.migrationinstitute.org/publications/wp-24-10>
- Dekker, R., & Engbersen, G. (2014). How social media transform migrant networks and facilitate migration. *Global Networks*, 14(4), 401-418. <https://onlinelibrary.wiley.com/doi/epdf/10.1111/glob.12040>
- Devarajan, S., & Fengler, W. (2013). Africa's economic boom: Why the pessimists and the optimists are both right. *Foreign Affairs*, 92(3), 68-81.

- Docquier, F., Peri, G., & Ruysen, I. (2014). The Cross-country determinants of potential and actual migration. *International Migration Review*, 48(1), 37-99. <https://doi.org/10.1111/imre.12137>
- Douglas, S. M., Arango, J., Graeme, H., Kouaouci, A., Pellegrino, A., & Taylor, J. E. (1994). An evaluation of inter-national migration theory: The North American case. *Population and Development Review*, 20(4). <https://doi.org/10.2307/2137660>
- Dreesen, T., Akseer, S., Brossard, M., & na wengine (2020). Promising practices for equitable remote learning: Emerging lessons from Covid-19 education responses in 127 countries (Innocenti Research Brief). Florence. Retrieved Decem-ber 16, 2020, from <https://www.unicef-irc.org/publications/pdf/IRB%202020-10%20CL.pdf>
- Eisenstadt, S. N. (1953). Analysis of patterns of immigration and absorption of immigrants. *Population Studies*, 7(2). <https://doi.org/10.2307/2172030>
- EMN (2018). Asylum and migration. Glossary 6.0: A tool for better comparability produced by the European Migration Network. Retrieved January 29, 2021, from https://www.emn.at/wp-content/uploads/2018/06/emn-glossary-6-0_en.pdf
- Fackler, T., Giesing, Y., & Laurentyeva, N. (2018). Knowledge remittances: Does emigration foster innovation? Working Paper No. 7420. Retrieved January 5, 2020, from http://ideas.repec.org/p/ces/ceswps/_7420.html/
- Fagan, L. (2019, December 24). Africa's 'climate refugees' are already here – and there. *Africa Times*. Retrieved October 11, 2020, from <https://africatimes.com/2019/12/24/africas-climate-refugees-are-already-here-and-there/>
- Fengler, S., Bastian, M., Brinkmann, J., Zappe, A. C., Tatah, V., Andindilile, M., Assefa, E., Chibita, M., Mbaine, A., Obonyo, L., Quashigah, T., Skleparis, D., Splendore, S., Tadesse, M., & Lengauer, M. (2020). Covering Migration – in Africa and Europe (Internal Document). Dortmund.
- Ferreira, P. M. (2004). Guinea-Bissau between conflict and democracy. *African Security Review*, 13(4), 45-57. <https://doi.org/10.1080/10246029.2004.9627317>
- Flavell, A., Milan, A., & Melde, S. (2020). Migration, environment and climate change: Literature review. First report in the "Migration, environment and climate change" series. Berlin: Bundesumweltamt (German Environment Agency), (Migration, environment and climate change No. 1). Retrieved December 15, 2020, from https://www.umweltbundesamt.de/sites/default/files/medien/1410/publikationen/2020-03-04_texte_42-2020_migration-literature-review_1.pdf
- Fleischer, A. (2006). Family, obligations, and migration: The role of kinship in Cameroon (MPIDR Working Paper No. 2006-047). Rostock. Retrieved December 16, 2020, from <https://www.demogr.mpg.de/papers/working/wp-2006-047.pdf>
- Freeman, L. (2017). Environmental change, migration, and conflict in Africa. *Journal of Environment and Development*, 26(4). <https://doi.org/10.1177/1070496517727325>
- Giménez-Gómez, J. M., Walle, Y. M., & Zewdu, Y. (2019). Trends in African migration to Europe: Drivers beyond eco-nomic motivations. *Journal of Conflict Resolution* 63(8), 1797-1831. <https://doi.org/10.1177/0022002718823907>
- Glazer, N., & Moynihan, D. P. (1963). Behind the melting pot: The Negroes, Puerto Ricans, Jews, Italians, and Irish of New York City. New York City: Massachusetts Institute of Technology.
- Gleick, P. H. (2014). Water, drought, climate change, and conflict in Syria. *Weather, Climate, and Society*, 6(3), 331-340. <https://doi.org/10.1175/WCAS-D-13-00059.1>
- Groth, H., May, J. F., & Turbat, V. (2019). Policies needed to capture a demographic dividend in sub-Saharan Africa. *Canadian Studies in Population*, 46(1), 61-72. <https://doi.org/10.1007/s42650-019-00005-8>

- Hanlon, R. J., & Christie, K. (Eds.) (2016). *Freedom from fear, freedom from want: An introduction to human security*. Toronto: University of Toronto Press. Retrieved December 16, 2020, from <https://utorontopress.com/us/freedom-from-fear-freedom-from-want-4>
- Hayes, S., Lundy, B. D., & Hallward, M. C. (2016). Conflict-induced migration and the refugee crisis: Global and local perspectives from peacebuilding and development. *Journal of Peacebuilding & Development*, 11(3), 1-7. <https://doi.org/10.1080/15423166.2016.1239404>
- Hoffmann-Nowotny, H.-J. (1970). *Migration: Ein Beitrag zu einer soziologischen Erklärung*. Stuttgart: Enke.
- Hooghe, M., Trappers, A., Meuleman, B., & Reeskens, T. (2008). Migration to European countries: A structural explanation of patterns, 1980-2004. *International Migration Review*, 42(2), 476-504.
- IOM (2017). I am a migrant. Retrieved May 3, 2020, from <https://iamamigrant.org/stories>
- IOM (2019a). Glossary on Migration. Geneva. Retrieved December 16, 2020, from https://publications.iom.int/system/files/pdf/iml_34_glossary.pdf
- IOM (2019b). World Migration Report 2020. Retrieved May 17, 2021, from https://publications.iom.int/system/files/pdf/wmr_2020.pdf
- Ionesco, D., Mokhnacheva, D., & Gemenne, F. (2017). *The Atlas of Environmental Migration*. London, New York: Routledge.
- Jordan, M. (2020, October 6). Even when they lost their jobs, immigrants sent money home. *The New York Times*. Retrieved October 6, 2020, from <https://www.nytimes.com/2020/09/24/us/coronavirus-immigrants-remittances.html>
- Kaps, A., Schewe, A.-K., & Klingholz, R. (2019). *Africa's demographic trailblazers: How falling fertility rates are accelerating development*. Berlin. Retrieved November 24, 2020, from https://www.berlin-institut.org/fileadmin/Redaktion/Englisch/Studien/Africa_s_Demographic_Trailblazers/Afrika_online_e.pdf
- Kapur, D. (2004). *Remittances: The new development mantra?* New York, Geneva. Retrieved from UNCTAD website: https://unctad.org/en/Docs/gdsmdpbg2420045_en.pdf
- Kirwin, M., & Anderson, J. (2018). Identifying the factors driving West African migration: West African Papers No.17 (West African Papers No. 17). Paris. Retrieved December 20, 2020, from <http://www.oecd.org/swac/publications/2018-wap-17-identifying-the-factors-driving-west-african-migration.pdf>
- Kleinfeld, P. (2019, December 16). In post-cyclone Mozambique, lots of aid but little reconstruction. *The New Humanitarian*. Retrieved October 12, 2020, from <https://www.thenewhumanitarian.org/photo-feature/2019/12/16/Mozambique-cyclone-Idai-Kenneth-reconstruction-aid>
- Klingholz, R., Sütterlin, S., Kaps, A., & Hinz, C. (2020). *Leapfrogging Africa: Sustainable innovation in health, education and agriculture*. Berlin. Retrieved December 20, 2020, from https://www.berlin-institut.org/fileadmin/Redaktion/Englisch/Studien/Leapfrogging/BI_Leapfrogging_Africa_2020_online.pdf
- Klopp, J. M., & Zuern, E. (2007). The politics of violence in democratization: Lessons from Kenya and South Africa. *Comparative Politics*, 39(2), 127-146. <https://doi.org/10.2307/20434030>
- Kugelmann, D. (2010). Refugees. *Oxford Public International Law*, 1-15. Retrieved January 29, 2021, from <http://opil.ouplaw.com/view/10.1093/law:epil/9780199231690/law-9780199231690-e866>
- Kuschminder, K., Andersson, L., & Siegel, M. (2012). Profiling Ethiopian migration: A comparison of characteristics of Ethiopian migrants to Africa, the Middle East and the North. In Udelsmann Rodrigues, C. & Tomàs, J. (Eds.), *Crossing African Borders: Migration and Mobility* (ISBN: 978-972-8335-22-9, pp. 39-43). Lisbon: Center of African Studies (CEA) ISCTE-IUL, University Institute of Lisbon. Retrieved December 16, 2020 from https://repositorio.iscte-iul.pt/bitstream/10071/4366/3/crossing_african_borders_2012_v2-1.p

- Kuschminder, K. (2016). Strong ties, weak ties: Exploring the role of networks in domestic worker migration from Ethiopia to the Middle East. *Asian and Pacific Migration Journal*, 25(4), 401-421. <https://doi.org/10.1177/0117196816673641>
- Lanati, M., & Thiele, R. (2017). The impact of foreign aid on migration revisited (EUI Working Papers (MWP) No. 2017-05). Retrieved December 20, 2020, from <https://doi.org/10.1016/j.worlddev.2018.06.021>
- Lee, E. S. (1966). A theory of migration. *Demography*, 3(1), 45-57. <https://link.springer.com/article/10.2307/2060063>
- Liddle, B. (2017). Urbanization and inequality/poverty. *Urban Science*, 35(4), 1-7. <https://doi.org/10.3390/urbansci1040035>
- Lynch, G. (2011). Democratization in Africa 1990-2010: An assessment. *Democratization* (18), 275-310. <https://doi.org/10.1080/13510347.2011.554175>
- Maastricht University, & GMDAC (2016). The push and pull factors of asylum-related migration: A literature review. Retrieved January 29, 2021, from <https://www.easo.europa.eu/sites/default/files/publications/The%20Push%20and%20Pull%20Factors%20of%20Asylum%20-%20Related%20Migration.pdf>
- Mahabub, M. G. (Ed.) (2014). The challenges of access to university education in Nigeria: International Centre of Economics, Humanities and Management. Retrieved December 20, 2020, from <https://icehm.org/upload/5708ED1214104.pdf>
- Malakooti, A. (2015). Migration trends across the Mediterranean: Connecting the dots. Retrieved January 29, 2021, from https://publications.iom.int/system/files/altai_migration_trends_accross_the_mediterranean.pdf
- Martin, P. L., & Taylor, J. E. (1996). The anatomy of the migration hump. In Taylor, J. E. (Ed.), *Development strategy, employment and migration: Insights from models* (pp. 43-62). Paris: OECD.
- Mbuagbo, O. T., & Akoko, R. M. (2004). Roll-Back: Democratization and social fragmentation in Cameroon. *Nordic Journal of African Studies*, 13(1), 1-12. Retrieved December 14, 2020, from <https://citeseerx.ist.psu.edu/viewdoc/download?doi=10.1.1.583.3293&rep=rep1&type=pdf>
- Migration Data Portal (2020a). Child and young migrants. Retrieved November 24, 2020, from <https://migrationdataportal.org/themes/child-and-young-migrants>
- Migration Data Portal (2020b). Diasporas. Retrieved November 24, 2020, from <https://migrationdataportal.org/themes/diasporas>
- Migration Data Portal (2020c). Types of migration: Environmental migration. Retrieved November 24, 2020, from https://migrationdataportal.org/themes/environmental_migration
- Migration Data Portal (2020d). Migration Data Portal: The bigger picture. Retrieved October 27, 2020, from https://migrationdataportal.org/?i=stock_abs_&t=2019
- Moscona, J., Nunn, N., & Robinson, J. A. (2018). Kinship and conflict: Evidence from segmentary lineage societies in sub-Saharan Africa. Cambridge: National Bureau of Economic Research. <https://doi.org/10.3386/w24209>
- Mountford, A., & Rapoport, H. (2014). Migration policy, African population growth and global inequality (DP No. 8329). Bonn: Institute for the Study of Labor (IZA). Retrieved December 14, 2020, from <http://ftp.iza.org/dp8329.pdf>
- Musau, Z. (2017-2018). Africa grapples with huge disparities in education: Reducing inequalities: Higher enrolment numbers mask exclusion and inefficiencies. *Africa Renewal*. Retrieved August 19, 2020, from <https://www.un.org/africarenewal/magazine/december-2017-march-2018/africa-grapples-huge-disparities-education>

- Naudé, W. (2008). Conflict, disasters and no jobs: Reasons for international migration from sub-Saharan Africa (Research Paper No. 8). Helsinki. Retrieved December 18, 2020, from <https://www.wider.unu.edu/publication/conflict-disasters-and-no-jobs>
- Neto, F., & Mullet, E. (1998). Decision-making as regards migration: Wage differential, job opportunity, and the network effect. *Acta Psychologica*, 98(1), 57-66. [https://doi.org/10.1016/S0001-6918\(97\)00035-8](https://doi.org/10.1016/S0001-6918(97)00035-8)
- News24 (2011, April 4). Teachers battling with simple maths. News24. Retrieved October 11, 2020, from <https://www.news24.com/News24/Teachers-battling-with-simple-maths-20110404>
- Noxolo, M. (2016). The impact of remittances on poverty in Africa: A cross-Country empirical analysis. (Unpublished doctoral dissertation). University of Cape Town, South Africa.
- Ottoh, F. O. (2018). Ethnic identity and conflicts in Africa. In Oloruntoba, S. O. & Falola, T. (Eds.), *The Palgrave Handbook of African politics, governance and development*. (335-351). New York: Palgrave Macmillan.
- Oucho, J. O., & Gould, W. T.S. (1993). Internal migration, urbanization, and population distribution. In Foote, K., Hill, K. & Martin, L. (Eds.), *Demographic Change in Sub-Saharan Africa*. Washington, D.C.: National Academies Press (pp. 256-296).
- Park, R. E. (1928). Human migration and the marginal man. *American Journal of Sociology*, 33(6), 881-893.
- Piché, V. (2013). Contemporary migration theories as reflected in their founding texts. *Population*, 68(1), 141-164. <https://doi.org/10.3917/popu.1301.0153>
- Quayyum, S. N., & Kpodar, R. K. (2020, September 11). Supporting migrants and remittances as COVID-19 rages on. Retrieved October 6, 2020, from <https://blogs.imf.org/2020/09/11/supporting-migrants-and-remittances-as-covid-19-rages-on/>
- Raleigh, C. (2011). The search for safety: The effects of conflict, poverty and ecological influences on migration in the developing world. *Global Environmental Change*, 21, S82-S93. <https://doi.org/10.1016/j.gloenvcha.2011.08.008>
- Ravenstein, E. G. (1876). Census of the British Isles, 1871: Birthplaces of the people and laws of migration. *Geo-graphical Magazine*, 3, 173-7, 201-6, 229-33.
- Ravenstein, E. G. (1885). The laws of migration. *Journal of the Statistical Society of London*, 48(2), 167-235. <https://doi.org/10.2307/2979181>
- Ravenstein, E. G. (1889). The laws of migration. *Journal of the Royal Statistical Society*, 52(2), 241. <https://doi.org/10.2307/2979333>
- Rigaud, K. K., de Sherbinin, A., Jones, B., & Bergmann, J. (2018). *Groundswell: Preparing for internal climate migration*. Washington, D.C. Retrieved December 19, 2020, from <http://hdl.handle.net/10986/29461>
- Sassen, S. (2007). *A sociology of globalization. Contemporary societies*. New York: Norton.
- Serajuddinada, U., & Hamadeh, N. (2020). New World Bank country classifications by income level: 2020-2021. Retrieved October 7, 2020, from <https://blogs.worldbank.org/opendata/new-world-bank-country-classifications-income-level-2020-2021>
- Sifuna, D. N., & Sawamura, N. (2010). *Challenges of quality education in sub-Saharan African countries*. Hap-pauge: Nova Science.
- Simpson, N. (2017). Demographic and economic determinants of migration. *IZA World of Labor*. <https://doi.org/10.15185/izawol.373>
- Sippel, L., Kiziak, T., Woellert, F., & Klingholz, R. (2011). *Africa's demographic challenges: How a young population can make development possible*. Berlin: Institute for Population and Development in cooperation with Deutsche Stiftung Weltbevölkerung (DSW).

Sjaastad, L. A. (1962). The costs and returns of human migration. *Journal of Political Economy*, 70(5), 80-93. <https://www.jstor.org/stable/1829105>

Spaull, N. (2019). The education problem: Priorities for education in SA: Input document for Treasury's Economic Colloquium. Stellenbosch. Retrieved December 16, 2020, from <https://nicspaull.files.wordpress.com/2019/01/spaull-priorities-for-educ-reform-treasury-19-jan-2019.pdf>

Tankou, E. A. (2018). President Buhari of Nigeria launches the AU theme of the year 2018 on fighting corruption in the continent. Retrieved November 24, 2020, from African Union website: <https://au.int/en/pressreleases/20180129/president-buhari-nigeria-launches-au-theme-year-2018-fighting-corruption>

Thorogood, J. (2019, June 6). Qatar 2022: FIFA admits violation of workers' standards. Deutsche Welle. Retrieved October 8, 2020, from <https://www.dw.com/en/qatar-2022-fifa-admits-violation-of-workers-standards/a-49078052>

Tiemoko, R. (2004). Migration, return and socio-economic change in West Africa: The role of family. *Population, Space and Place*, 10(2), 155-174. <https://onlinelibrary.wiley.com/doi/pdf/10.1002/psp.320>

Transparency International (2018, July 11). How to win the fight against corruption in Africa [Press release]. Retrieved November 24, 2020, from https://www.transparency.org/news/feature/how_to_win_the_fight_against_corruption_in_africa

Transparency International (2019). Corruption Perceptions Index 2019. n.p. Retrieved May 27, 2020, from <https://www.transparency.org/en/cpi/2019>

UIS (2020). Education in Africa. Retrieved August 17, 2020, from <http://uis.unesco.org/en/topic/education-africa>

UN (2020a). Education during Covid-19 and beyond (Policy Brief). New York. Retrieved November 24, 2020, from https://www.un.org/development/desa/dspd/wp-content/uploads/sites/22/2020/08/sg_policy_brief_covid-19_and_education_august_2020.pdf

UN (2020b). Global Compact for Migration/Global Compact on Refugees. Retrieved April 11, 2020, from <https://refugeesmigrants.un.org/>

UN (2020c). Sustainable Development Goals: SDG 4: Ensure inclusive and equitable quality education and promote lifelong learning opportunities for all. New York. Retrieved August 14, 2020, from United Nations website: <https://sdgs.un.org/goals/goal4>

UNDESA (n. d.). Definition of regions. Retrieved May 9, 2020, from <https://population.un.org/wpp/DefinitionOfRegions/>

UNDESA (2005). World economic situation and prospects 2005. New York. Retrieved January 29, 2021, from <https://www.un.org/development/desa/dpad/wp-content/uploads/sites/45/PDFs/WESP/2005wesp.pdf>

UNDESA (2010). World economic situation and prospects 2010 (World Economic Situation and Prospects). Retrieved January 29, 2021, from https://www.un.org/en/development/desa/policy/wesp/wesp_archive/2010wesp.pdf

UNDESA (2019a). World Population Prospects 2019: Highlights. New York. Retrieved December 16, 2020, from https://population.un.org/wpp/Publications/Files/WPP2019_Highlights.pdf

UNDESA (2019b). International Migration 2019: Report. New York. Retrieved December 15, 2020, from https://www.un.org/en/development/desa/population/migration/publications/migrationreport/docs/InternationalMigration2019_Report.pdf

UNDP (2019a). Human Development Report 2019: Beyond income, beyond averages, beyond today: Inequalities in human development in the 21st century. New York. Retrieved November 11, 2020, from <http://hdr.undp.org/sites/default/files/hdr2019.pdf>

UNDP (2019b). Human development indicators. Retrieved January 29, 2021, from <http://hdr.undp.org/en/content/statistical-data-tables-7-15>

UNESCO (2019). Migration, displacement and education: Building bridges, not walls. Global Education Monitoring Report 2019. Paris. Retrieved December 16, 2020, from <https://unesdoc.unesco.org/ark:/48223/pf0000265866>

UNHCR (n. d.). Glossary. Retrieved August 11, 2020, from <http://www.issm.cnr.it/progetti/emigrazione/META-DATA%20E%20GLOSSARI/UNHCR/GLOSSARY%20UNHCR.pdf>

UNHCR (2020a). Climate change and disaster displacement. Retrieved December 16, 2020, from <https://www.unhcr.org/climate-change-and-disasters.html>

UNHCR (2020b). Global Trends: Forced displacement in 2019. Copenhagen. Retrieved December 16, 2020, from <https://www.unhcr.org/5ee200e37.pdf>

UNHCR (2020c). Resettlement. Retrieved October 10, 2020, from <https://www.unhcr.org/resettlement.html>

UNHCR (2020d). Who is an internally displaced person? Retrieved November 24, 2020, from <https://www.unhcr.org/teaching-about-refugees>

United Nations (n. d.). Sustainable Development Goals: SDG 10: Reduce inequality within and among countries. Retrieved from <https://indicators.report/goals/goal-10/>

UNODC (2018). Global report on trafficking in persons 2018. Retrieved May 20, 2021, from https://www.unodc.org/documents/data-and-analysis/glotip/2018/GLOTIP_2018_BOOK_web_small.pdf

Vlavanou, G. (2016). An uncertain transition: Security, violence, and neopatrimonialism in the Central African Republic. *Revue Tiers Monde*, 228(4), 121-142.

Vogler, M., & Rotte, R. (2000). The effects of development on migration: Theoretical issues and new empirical evidence. *Journal of Population Economics*, 13(3), 485-508. <https://doi.org/10.1007/s001480050148>

Wilhelm, J. P. (2020, March 19). Africa: More poverty despite economic growth: Fighting Poverty. Retrieved August 6, 2020, from <https://www.dw.com/en/africa-more-poverty-despite-economic-growth/a-52840817>

World Bank (2017). Africa's Pulse: Special section: The region's infrastructure performance across sectors (Africa's Pulse No. 15). Washington, D.C. Retrieved July 7, 2020, from <http://documents.worldbank.org/curated/en/348741492463112162/Africas-pulse>

World Bank (2018a). Groundswell: Preparing for internal climate migration: Internal climate migration in sub-Saharan Africa (Policy Note No. 1). Washington, D.C. Retrieved November 24, 2020, from <https://openknowledge.worldbank.org/bitstream/handle/10986/29461/GroundswellIPN1.pdf?sequence=6&isAllowed=y>

World Bank (2018b). Migration and remittances: Recent developments and outlook. Special topic: transit migration. Retrieved December 16, 2020, from <https://www.knomad.org/sites/default/files/2018-04/Migration%20and%20Development%20Brief%2029.pdf>

World Bank (2019). Leveraging economic migration for development: A briefing for the World Bank Board. Washington, D.C. Retrieved December 20, 2020, from https://www.knomad.org/sites/default/files/2019-08/World%20Bank%20Board%20Briefing%20Paper-LEVERAGING%20ECONOMIC%20MIGRATION%20FOR%20DEVELOPMENT_0.pdf

World Bank (2020a). Africa's pulse: The World Bank's bi-annual analysis of the state of African economies: Volume 1 to Volume 20. Retrieved August 6, 2020, from <https://www.worldbank.org/en/region/afr/publication/africas-pulse>

World Bank (2020b). Covid-19 crisis through a migration lens (Migration and Development Brief No. 32). Retrieved November 25, 2020, from <https://openknowledge.worldbank.org/handle/10986/33634>

World Bank (2020c). Personal remittances, received (% of GDP) – Low & middle income, Middle income, Low income countries: Data. Retrieved August 14, 2020, from <https://data.worldbank.org/indicator/BX.TRF.PWKR.DT.GD.ZS?locations=XO-XP-XM>

World Bank (2020d). Personal remittances, received (current US\$) – Low & middle income, Middle income, Low income countries: Data. Retrieved August 14, 2020, from <https://data.worldbank.org/indicator/BX.TRF.PWKR.CD.DT?locations=XO-XP-XM>

World Bank (2020e). Private capital flows: Data catalog. Retrieved October 11, 2020, from <https://datacatalog.worldbank.org/private-capital-flows-total-gdp>

World Bank (2020f). Migration and Remittances Data. Retrieved January 29, 2021, from <https://www.worldbank.org/en/topic/migrationremittancesdiasporaissues/brief/migration-remittances-data>

World Bank, & UIS (2011). School enrollment, tertiary (% gross) – Nigeria. Retrieved August 19, 2020, from <https://data.worldbank.org/indicator/SE.TER.ENRR?locations=NG>

World Bank, & UIS (2020a). School enrollment, primary (% gross) – Sub-Saharan Africa: Data. Retrieved August 19, 2020, from https://data.worldbank.org/indicator/SE.PRM.ENRR?locations=ZG&most_recent_value_desc=false

World Bank, & UIS (2020b). School enrollment, secondary (% gross) – Sub-Saharan Africa: Data. Retrieved August 19, 2020, from https://data.worldbank.org/indicator/SE.SEC.ENRR?locations=ZG&most_recent_value_desc=false

World Bank, & UIS (2020c). School enrollment, tertiary (% gross) – Sub-Saharan Africa: Data. Retrieved August 19, 2020, from https://data.worldbank.org/indicator/SE.TER.ENRR?locations=ZG&most_recent_value_desc=false

Yameogo & Tidey, 2019 (2019, August 22). School closures in West and Central Africa triple since 2017 [Press Release]. Dakar, Geneva, New York. Retrieved August 19, 2020, from <https://www.unicef.org/press-releases/school-closures-west-and-central-africa-triple-2017>

Zappe, A. C., Bastian, M., Leißner, L., Henke, J., & Fengler, S. (2019). Perspektivwechsel. Migrationsberichterstattung in ausgewählten afrikanischen Ländern und Deutschland aus Migrant*innensicht. In Gehrau, V., Waldherr, A. & Scholl, A. (Eds.), *Jahrbuch der Deutschen Gesellschaft für Publizistik- und Kommunikationswissenschaft 2019* (pp. 131-140). Münster: Deutsche Gesellschaft für Publizistik und Kommunikationswissenschaft.

Zeender, G. (2018). The Sustainable Development Goals and IDPs. *Forced Migration Review*, 59, 24-26. Retrieved December 15, 2020, from <https://www.fmreview.org/GuidingPrinciples20/zeender>

Zelinsky, W. (1971). The hypothesis of the mobility transition. *Geographical Review*, 61(2), 219-249. <https://doi.org/10.1177/030913259301700205>



MODULI 4

Vyombo vya habari na hadithi za uhamiaji – uchanganuzi wa nchi tofauti

na Susanne Fengler



MALENGO YA MODULI

- Kutoa maelezo ya jumla ya matokeo ya utafiti kuhusu utoaji wa habari za masuala ya uhamiaji na wakimbizi.
- Kuhimiza washiriki kuchanganua mitazamo tofauti ya ripoti zinazotolewa na vyombo vya habari.
- Kuwahamasisha washiriki kuhusu dhana potovu zisizo na uasili na mambo yasiyoleweka vyema katika ukusanyaji na utoaji wa habari za wahamiaji na wakimbizi.



MATOKEO YA MAFUNZO

Kufikia mwisho wa moduli hii, washiriki wanapaswa kuwa na uwezo wa:

- Kujadiliana athari zinazoweza kusababishwa na dosari za kueleza habari za wahamiaji na wakimbizi. → **Matokeo ya mafunzo kwa mitazamo ya kibinafsi na maadili: Kujibu**
- Kulinganisha jinsi vyombo vya habari vinavyotoa taarifa katika desturi tofauti za kisiasa na mifumo ya uanahabari. → **Matokeo ya mafunzo kwa stadi za utambuzi: Kuchanganua**
- Kutambulisha changamoto muhimu, hasa za kuripoti masuala yanayohusiana na uhamiaji katika mazingira yanayobadilika ya uanahabari. → **Matokeo ya mafunzo kwa stadi za utambuzi: Uchanganuzi**

Muhtasari

Vyombo vya habari vya kisasa huendesha shughuli zake katika ulimwengu unaokumbwa na mabadiliko makubwa ya kisiasa na kijamii; wakati ambapo utandawazi na udijitishaji zimeshika kasi. Uhamiaji tunaoushuhudia ni sehemu moja ya hali ya ulimwengu wetu unaobadilika kila kukicha. Wanahabari huumba mitazamo yao kuhusu wahamiaji na wakimbizi katika nchi asili na pia mwenyeji wao mpya kulingana na jinsi vyombo tofauti vya habari huripoti kuhusu masuala tofauti. Na hata iwapo vyombo vya habari hupuuza taarifa za wahamiaji na wakimbizi, au vinariipoti shingo upande, huenda jambo hili likaathiri hadhira na wenye mamlaka walio na majukumu ya kuchukua maamuzi. Huenda watu hawaelewi matokeo kamili ya masuala ya uhamiaji kwa jamii zao, wanachukua maamuzi ya kupotosha, wanashinikiza au wanakosa kushinikiza waandalizi wa sera kuchukua hatua, au kuhisi kana kwamba wamesalitiwa na vyombo vya habari. Wanazuoni wa uanahabari katika Ulaya hudai kwamba taarifa nyingi za habari kuhusu uliotajwa kuwa mzozo wa wakimbizi wa 2015 zimeimarisha shutuma za kisiasa kwa Muungano wa Ulaya miongoni mwa raia (Harteveld na wengine, 2018). Katika Afrika, Eric Chinje wa African Media Initiative anasema suala la uhamiaji lisipoangaziwa ipasavyo na vyombo vya habari vya nchi za Afrika, huenda kamwe pasiwe na watetezi wowote wenye msukumo, sauti na nguvu za kupigania sera za kuakisi kikamilifu masuala ya uhamiaji haramu. Mhamiaji kutoka Kenya aliyehojiwa kwa


mojawapo ya miradi yetu ya utafiti anasema kambi ya wakimbizi ya Kakuma ambayo ni makao ya wakimbizi na watafutaji hifadhi zaidi ya 180,000, ni hadithi iliyosahaulika kabisa na vyombo vya habari vya Kenya (Bastian na wengine, 2018).



ZOEZI LILILOPENDEKEZWA LA KUSHUGHULIKIA STADI ZA UTAMBUZI ZA UELEWA NA STADI MITAZAMO YA KIBINAFSI NA MAADILI ZA KUPOKEA:

Jadili ufahamu wako wa ripoti za vyombo vya habari kuhusu wahamiaji na wakimbizi. Unaweza pia kukagua matokeo ya utafiti uliofanyika Ulaya yaliyo hapa chini (tazama Kielelezo 14).

Kielelezo 14: Kiwango cha Wazungu kuridhishwa na taarifa zinazotolewa na vyombo vya habari kuhusu uhamiaji



“Kwa jumla, unafikiri unafahamu kwa kiwango gani kuhusu masuala ya uhamiaji na ushirikishwaji?” (% – EU)

Asili: European Commission (2018, uk. 4). Kielelezo chetu.

Ili kuwezesha vyombo vya habari kutoa ripoti huru, zisizopendelea na bora zaidi kuhusu wahamiaji na wakimbizi, kama yanavyohimiza Maafikiano ya Umoja wa Mataifa ya 2018, tunahitaji kuchunguza jinsi habari za uhamiaji zinaelezwa kwa sasa na kutambulisha mafanikio na pia dosari za jinsi vyombo vya habari hushughulikia suala hilo. Uchanganuzi linganishi wa vile taarifa za uhamiaji huelezwa utatuwezesha kufahamu vyema zaidi jinsi vyombo vya habari katika mataifa asili ya uhamiaji kwa upande mmoja, na kwa upande mwingine vyombo vya habari katika nchi wanazopitia na mataifa yanayowapatia hifadhi vinavyoakisi suala hilo. Hafez (2011, uk. 486) anahoji kwamba “mifumo ya habari hushughulikia matukio kulingana na umuhimu wake wa kitaifa. Matukio yanayoonekana kufanana huripotwa wakati huo huo kwa njia tofauti kote ulimwenguni.” Je, hivyo ndivyo ilivyo katika nyakati zetu, wakati wahamiaji na wakimbizi wame-

kuwa mojawapo ya masuala muhimu ya sera ya ulimwengu?¹ Kauli ya utoaji wa ripoti zisizopen-delea ni wazo la ukamilifu lililozusha ubishi mkubwa na ambalo maana yake hutofautiana katika mihadhara kuhusu uanahabari. Hata hivyo, linalobainika wazi ni kwamba ufasili na utekelezaji wa viwango vya kitaalamu vya uthibitishaji na maslahi ya umma hupambwa na masimulizi kuhusu masuala ya kiuchumi, kisiasa, taasisi, kidemografia, desturi na utambulisho.

Utafiti kuhusu kuripoti uhamiaji: mapitio ya maandishi

Awamu mbali mbali za uhamiaji zimechokonoa uchunguzi wa jinsi vyombo vya mawasiliano kwa umma hutoa habari kuhusu uhamiaji, ilhali habari kuhusu walio wachache (ambazo mara nyingine zinahusiana na masuala ya uhamiaji) zimekuwa ni mada ya uchanganuzi wa kila mara wa vyombo vya habari angalau tangu miaka ya 1980. Uchunguzi huo unaweka msingi wa kutathmini maendeleo na hali iliyopo ya utoaji wa habari za uhamiaji kutoka nchi moja hadi nyingine kwenye juhudi za kufahamu “vipengele vinavyounda jinsi habari kuhusu uhamiaji na walio wachache zinavyoripotiwa, pamoja na taathira za kuripoti habari hizo kwa mitazamo ya umma, sera zinazobuniwa au mahusiano ya jamii” (Bleich na wengine, 2015, uk. 857). Inafaa kufahamika kwamba asili ya idadi kubwa ya uchunguzi huo ni nchi za Kaskazini. Huku sababu na matokeo ya safari za wahamiaji na wakimbizi zikiendelea taratibu kutawala ushawishi wa vyombo vya habari kujenga hoja kwa jamii za Magharibi tangu 2015 (Fengler & Kreutler, 2020; Krüger & Zapf-Schramm, 2016), ni taarifa chache na vichwa vya habari kwenye vyombo Afrika huangazia watu wanaohama kutoka barani wakienda kaskazini, anahoji Eric Chinje wa African Media Initiative (Chinje, 2016). Utafiti kuhusu kuripoti kuhusu wahamiaji na wakimbizi katika nchi za Afrika umetilia mkazo Afrika Kusini ambapo kumekuwa na visa vya dhuluma kwa wahamiaji kutoka nchi nyingine za Afrika. Waandishi wanaochanganua magazeti katika Afrika Kusini ambao ni pamoja na Danso & McDonald (2001), McDonald & Jacobs (2005), na Fine & Bird (2002), wanahoji kwamba katika miaka ya karibuni, vyombo vya habari katika Afrika Kusini vimetoa sura isiyo kamili na pungufu ya mashambulizi ya chuki kwa wageni (Smith, 2009, uk. 11). Mbali na uchunguzi huo, Assopgoum (2011) ameangazia ripoti za habari kuhusu uhamiaji kutoka Senegal na Ujerumani, naye White (2015) ametoa maelezo ya jumla kuhusu miundo na hali ya utoaji wa habari za uhamiaji, ikiwa ni katika nchi kadhaa za Afrika. White (2015) anahoji kwenye “Moving Stories” kuwa wanahabari hukosa kusimulia kikamilifu na mara nyingi kunaswa na mitego ya propaganda inayowekwa na wanasiasa. Katika nchi asili za wahamiaji na wakimbizi, utoaji wa habari finyu mara nyingi hutokana na uhibitishi mkali wa wenye mamlaka au uhaba wa rasilimali ama mchanganyiko wa yote mawili. (tazama Moduli 5; tazama pia Al-Mazahara, 2016).

Kabla ya kutafakari kuhusu mtaala wa mawasiliano ya habari kwa umma katika nchi za Kaskazini, ni muhimu kufahamu kwamba historia ya uhamiaji katika nchi za Ulaya hutofautiana pakubwa: Uhamiaji uliodumu kwa muda mrefu kwenda Uingereza na Ufaransa kwa sababu ya uhusiano wa awali wa kikoloni, na uhamiaji wa ‘Gastarbeiter’ katika Ulaya Kusini na Watu-

1 Baadhi ya maandishi ya moduli hii yametolewa kutoka kwa machapisho ya awali ya mwandishi (Fengler na wengine (2020a)).

ruki ambao wamehamia Ujerumani tangu miaka ya 1960, ni tofauti na historia ya karibuni ya uhamiaji kwenda Uhispania, Italia na Ugiriki katika miaka ya 2010, nchi ambazo awali raia wake walikuwa wanahamia nchi za Ulaya Kaskazini. Matukio hayo yameathiri jinsi vyombo vya habari vya kitaifa hueleza masuala ya uhamiaji. Kadhalika, uchunguzi mwingi unachanganua habari kuhusu uhamiaji, wahamiaji na wakimbizi katika nchi moja, ingawa “uwanja huu wa sera umeendelea kubadilika na kuwa ushirikiano wa mataifa ya EU kuchukua uamuzi wa pamoja, kumaanisha kwamba inazidi kuwa muhimu kuchambua masuala ya uhamiaji yanayojadiliwa na umma kwa kuzingatia mtazamo wa Kizungu” (Horsti, 2008, uk. 42). Lakini katika muhtasari wa Meltzer na wengine (2018, uk. 1) wa uchambuzi wa wachanganuzi wa suala hilo “hapana utafiti linganishi mwingi kuhusu umuhimu wa masuala yanayohusiana na uhamiaji au wahusika katika vyombo vya habari kote katika nchi tofauti za Ulaya”.

Uchunguzi huo unaonyesha mabadiliko mengi kulingana na misimamo tofauti ya kisiasa kuhusu uhamiaji ndani ya nchi za Ulaya, lakini pia taratibu tofauti za uanahabari, desturi za vyombo vya habari na uwezo wa kufikia vyanzo vya utoaji wa habari za uhamiaji. Caviedes (2015, uk. 898) amelinganisha utoaji wa habari za uhamiaji katika Ufaransa, Uingereza na Italia, na kufuatia uchunguzi wake mwenyewe anahoji kuwa kiasi kikubwa cha habari za uhamiaji “zimeendelea kuhusishwa na masuala ya uhalifu na usalama”. Uhamiaji unaonekana pia kuwa “tishio la ustawi wa kiuchumi na utambulisho wa kitamaduni”. Mitazamo ya uchumi na usalama ilichukua nafasi kubwa ya habari kuhusu uhamiaji kati ya 2009 na 2012. “Mkazo na umuhimu wa masuala katika mijadala kuhusu uhamiaji hutofautiana kati ya nchi, kiasi kwamba kila nchi inaweza kudumisha masimulizi yake fulani yaliyo muhimu” (Caviedes, 2015, uk. 912). Kwa mujibu wa Esses na wengine (2013, uk. 520), mifumo hasi na migongano ya habari kuhusu wahamiaji na wakimbizi imeendelea kuwa ni kawaida katika Ulaya. Watu wanaohama kutoka nchi moja ya EU hadi nyingine mara nyingi huelezwa na vyombo vya habari kuwa “tisho kwa uchumi na mfumo wa jamii”, ilhali wahamiaji wasio raia wa EU huchukuliwa kuwa ni tishio kwa desturi za nchi wenyeji (Meltzer na wengine, 2018, uk. 6). Uchunguzi wa karibuni katika nchi saba za EU unathibitisha kwamba kuhamia EU kutoka nje ya eneo hilo hupewa sura mbaya zaidi na mara nyingi husisitiza masuala ya usalama (Eberl na wengine, 2019).

Horsti (2008) anatoa matokeo ya utafiti mojawapo ambao ni kati ya tafiti chache za uhamiaji wa Waafrika kuingia Ulaya, akiakisi taarifa za vyombo vya habari kuhusu wahamiaji 30,000 ambao hawakuwa na hati za usafiri walioingia katika visiwa vya Canary, Uhispania, mwaka 2006 (Fohrn, 2009). Uchunguzi wake wa gazeti moja la Finland na jingine la Sweden, ulibaini kwamba taarifa nyingi zilizochapishwa na magazeti hayo hazikuwaangazia Waafrika kama wahusika huru waliochukua maamuzi razini; kadhalika, tukio hilo lilipewa muhimu wa kinyumbani wa nchi hizo mbili kwa kusisitiza kuhusu wahusika wa Finland na Sweden na pia mitazamo yao katika tukio hilo la mbali katika Ulaya Kusini. Balabanova & Balch (2010) katika utafiti mwingine kuhusu uhamiaji wa wafanya kazi katika Uingereza na Bulgaria kufuatia kupanuliwa kwa EU mwaka 2007, na hivyo basi kulinganisha habari katika nchi zilizotoa wahamiaji na nchi mwenyeji wao, walitarajia habari tofauti kutoka nchi asili na mwenyeji kwa sababu ya faida na athari tofauti za uhamiaji. Hata hivyo, ajenda ya vyombo vya habari katika Bulgaria ilifanana pakubwa na ya Uingereza

kwa sababu vyombo vya habari vya Bulgaria vilinukuu habari zilizotolewa Uingereza kwa kukosa rasilimali katika vyombo vyake vya habari za kuwawezesha kujikusanyia wenyewe habari zao asili.

Wakiangazia uliotajwa kuwa mzozo wa wakimbizi Ulaya wa 2015, Berry na wengine (2015) waligundua kwamba utoaji wa habari kuhusu wahamiaji na wakimbizi uliotofautiana pakubwa miongoni mwa mataifa ya Ulaya; masuala ya ubinadamu yalipewa uzito zaidi katika Italia; magazeti na majarida ya Sweden yalitilia mkazo mambo ya kusaidia na kujenga; mengi ya Uingereza yaliendeleza msimamo hasi. Kwa mujibu wa uchanganuzi wa European Journalism Observatory (EJO), magazeti ya Magharibi mwa Ulaya yalionyesha huruma zaidi kwa hali mbaya ya wahamiaji na wakimbizi, yakilinganishwa na nchi za Ulaya ya Kati na Mashariki (EJO, 2015). Georgiou & Zaborowski (2017) walitafiti kuhusu utoaji habari katika nchi nane za Ulaya na kuhukumu kwamba vyombo vya habari hujali masuala ya wahamiaji na wakimbizi katika Ulaya kwa kiwango kidogo na kuyashugulikia hapa na pale, na ilikuwa nadra kwa taarifa zilizotolewa kuhusishwa na ripoti za vita au habari nyingine za kimataifa kutoka nchi asili za wahamiaji na wakimbizi. Fotopoulos & Kaimaklioti (2016) walilinganisha jinsi magazeti ya Ugiriki, Ujerumani na Uingereza yameshughulikia habari za mzozo wa wakimbizi wa 2015; kulingana nao, taswira ya wahamiaji na wakimbizi ni ya watu wasiojiweza na manusura wasio na matumaini wa vita vya wenyewe kwa wenyewe katika Syria, na magazeti yakaangazia pakubwa janga hilo. Kama anavyohoji Caviedes, taarifa za habari hutilia mkazo matokeo na athari za uhamiaji kwa mtazamo wa kiuchumi na masoko ya nguvukazi (Goedeke Tort na wengine, 2016). Isitoshe, uchunguzi umetambulisha uhaba wa ripoti za masimulizi ya wahamiaji binafsi (Georgiou & Zaborowski, 2017). Uchunguzi uliofanywa na ICMPD (2016) unadokeza kwamba pana uhaba wa maarifa miongoni mwa wana-habari katika Ulaya na nchi za MENA kuhusu suala tatanishi la mataifa wanakotoka wahamiaji. Kadhalika, vyumba vya habari vinayumbishwa kwa urahisi na shinikizo za watu wanaotafuta umaarufu katika umma na kupitia kwa mitandao ya jamii.



ZOEZI LILILOPENDEKEZWA LA KUSHUGHULIKIA STADI ZA UTAMBUZI ZA UELEWA NA STADI MITAZAMO YA KIBINAFSI NA MAADILI ZA KUPOKEA:

Mapitio ya maandishi yameangazia tofauti zinazobainika za jinsi uhamiaji unavyoripotiwa katika nchi mbali mbali. Pamoja na miktadha tofauti ya kisiasa, mifumo ya vyombo vya habari na mitazamo ya kitamaduni huenda ikawa na athari kubwa kwa kiasi na kiwango cha ripoti za vyombo vya habari za masuala ya uhamiaji na uhamishwaji wa kulazimishwa. Jadili taathira za masuala yafuatayo kwa kiasi na kiwango cha ripoti za habari za uhamiaji katika nchi za Afrika na Ulaya: Uhuru wa vyombo vya habari, mifumo mbali mbali ya vyombo vya habari, utaalamu na elimu ya uanahabari, rasilimali za vyumba vya habari, teknolojia, masoko ya matangazo ya biashara (unaweza kuongezea mada zingine).

Uchunguzi wa jinsi habari za uhamiaji huripotiwa katika nchi tofauti za Afrika na Ulaya

Ili kuchanganua habari kuhusu uhamiaji kote katika mifumo ya kisiasa na taratibu za uana-habari, shirika la Erich Brost Institute for International Journalism (EBI) limefanya tafiti mbili kulinganisha jinsi habari kuhusu wahamiaji na wakimbizi katika Afrika na Ulaya huripotiwa (utafiti wa 1) pamoja na kote katika Ulaya Magharibi na Mashariki, Marekani na Shirikisho la Urusi (utafiti wa 2). Mwongozo huu unawasilisha matokeo muhimu ya tafiti hizo mbili na kutoa vifaa ambatanishi katika tovuti ya mradi wetu, kwa matumaini ya kuhimiza watafiti wenzetu na wanafunzi wa ngazi za juu kufanya utafiti sawa katika Afrika na mabara mengine kwa lengo la kujenga msingi imara wa elimu na maarifa kuhusu kuripoti habari za uhamiaji.

Uchunguzi wa kwanza ulilinganisha yaliyochapishwa katika magazeti sita ya Ulaya na matano ya nchi za Afrika (Fengler na wengine, 2020a). Jopo lililoleta vyo vya Ulaya na Afrika pamoja lilichanganua makala kuhusu uhamiaji na uhamishwaji wa kulazimishwa zilizochapishwa katika matoleo ya mtandaoni ya magazeti mawili yanayotolewa kila siku yenye wasomaji wengi katika Ujerumani (Süddeutsche Zeitung, Frankfurter Allgemeine Zeitung), Uingereza (The Independent, The Telegraph), Ufaransa (Le Monde, Le Figaro), Italia (La Repubblica, Corriere della Sera), Ugiriki (Ta Nea; Kathimerini), Uhispania (El País, ABC) na Kenya (The Daily Nation, The Standard), Uganda (The New Vision, Monitor), Tanzania (Daily News, The Guardian), Ethiopia (The Ethiopian Herald, Addis Zemen) na Ghana (Ghanaian Times, Daily Graphic). Kwa kupekua mitandao, watafiti walipata makala 1,512 zilizochapishwa katika kipindi cha mwaka mmoja (Juni 1, 2015 hadi Mei 31, 2016) kuhusu uhamiaji kutoka Afrika kwenda Ulaya ambazo zilikaguliwa na kutathminiwa kwa kutumia uchanganuzi maudhui kitakwimu. Lengo lilikuwa ni kuuondoa mtazamo wa Kizungu (Waisbord & Mellado, 2014) kwenye utafiti, na kuchunguza tukio la uhamiaji kwa pande tofauti. Ndiposa watafiti Wazungu na Waafrika walishirikiana kwa karibu katika kila ngazi za uchunguzi — katika uandalizi wa mwongozo wa kanuni na taratibu, ukusanyaji wa data na utathmini wake pamoja na uchanganuzi wa mwisho.


Uchunguzi uligundua pengo kubwa kuhusiana na kiasi cha makala za uhamiaji kati vya vyombo vya habari vya Ulaya na Afrika. Zaidi ya asilimia 88 ya makala zilizopatikana wakati wa kipindi cha uchunguzi huo cha 2015/2016 zilikuwa zimechapishwa katika magazeti ya Ulaya, huku magazeti ya Afrika yakichangia asilimia 12 pekee. Tofauti hii ni kubwa, hata ikitiliwa maanani kwamba magazeti ya Afrika kwa jumla huwa na nafasi ndogo kwa taarifa za habari ikilinganishwa na yale ya Ulaya, na redio ndiyo inatawala kwa sababu ya pingamizi za kifedha na kiteknolojia pamoja na wengi kutojua kusoma na kuandika (African Media Barometer, 2018).

Habari za siasa za kila siku zilitwaa nafasi kubwa magazetini ya Ulaya na Afrika na ni taarifa ambazo hazikuwa na kina; chini ya asilimia tisa ya habari zote zilizochapishwa zilikuwa na usuli wa habari muhimu za kuwasaidia wasomaji kufahamu sababu hasa na athari za uhamiaji na watu kulazimishwa kuhama. Mada kuu za makala zilizochunguzwa zilikuwa ni siasa (43%) na uhamiaji kwa jumla (48%) — Mikasa na ajali za meli ikipewa umuhimu wa kipekee. Vyombo vya habari katika mabara yote mawili vilipuuzilia mbali pakubwa ripoti zenye mada nyingine kama

vile uchumi (2%), vyombo vya habari na uanahabari (1%), maisha ya kila siku (takribani 0%), historia, makala za masimulizi ya makabila na mila (1%) athari za kimkakati za uhamiaji (2%). Hivyo basi, vyombo vya habari katika Ulaya na Afrika vilipata kiwango kidogo cha usuli wa habari kuviwezesha kutathmini masuala ya wahamiaji na wakimbizi — au hata kuufahamu umuhimu wa mada hiyo.

Katika Ulaya, habari za uhamiaji kutoka Afrika ziliegemea pakubwa kauli za Wazungu kujipenda mno na zilihusu zaidi masuala ya usalama katika Ulaya. Ni robo (26%) pekee ya makala katika vyombo vya habari vya Ulaya ambazo ziliwaangazia Waafrika kama wahusika wakuu (tazama Kielelezo 15). Wakati huo huo, vyombo vya habari vya Ulaya vilipuuza nchi asili za wahamiaji za Afrika. Libya ikiwa njia muhimu ya kutoka Afrika kuingia Ulaya ilitajwa kwa kiasi kidogo tu (5%). Eritrea, ambayo ilikuwa na idadi kubwa zaidi ya wahamiaji katika Ulaya wakati wa utafiti, ilipewa nafasi ndogo kabisa ya chini ya asilimia moja. ‘Bara la Afrika’ ndilo lilikuwa ‘nchi kuu’ katika asilimia tatu za makala. Taarifa hizo zilikuwa na maelezo haba kuhusu wahamiaji na wakimbizi Waafrika ni nani na ni kwa nini huwa wanaamua kuhama.

Hata hivyo, vyombo vya habari vya Afrika havikuonekana kujali kamwe. Badala yake, vyombo hivyo vilitenga nafasi kubwa kwa ripoti za ajali na mikasa katika Bahari ya Mediterranean. Habari za uhamiaji katika nchi za Kiafrika ziliwapuuza kabisa watu: Raia walikuwa asilimia 13 pekee ya wahusika wakuu katika ripoti za vyombo vya habari — wakuu wa serikali na wanasiasa walipewa



nafasi kubwa katika taarifa za habari ambazo hazikuwa na sura yoyote ya ubinadamu; Magazeti ya Afrika yaliwataja kwa mara mbili zaidi wahusika wa kimataifa (mashirika ya kutoa misaada na wengineo) kama wahusika wakuu, nafasi iliyokuwa thuluthi mbili zaidi ya wahusika wote katika Afrika wakiwekwa pamoja. Wahusika wenye mamlaka na uwezo mkubwa kama vile wanasiasa (marais, wajumbe wa serikali au wanasiasa wa upinzani), maafisa wa serikali (mahakama, polisi, majeshi au mashirika ya ujasusi) na wahusika wa kimataifa wenye uwezo kama vile UNHCR ndio waliopewa nafasi kubwa zaidi. Pana haja ya kutaja kwamba utafiti ulithibitisha ni kwa nini habari za vyombo vya kigeni huwa na dosari nyingi, kama ilivyoielezwa na Hafez (2002). Mbali na mitazamo hasi, athari za kisiasa na kuwajali tu wenye mamlaka na wa tabaka za juu, ilikuwa dhahiri muktadha kamili ulipuuzwa. Vipengele vya kiuchumi na kimila nusura visionekane, sawa na matatizo ya kimuundo ya uhamiaji (tazama pia Moduli 3; Fengler na wengine, 2020a; Fengler na wengine, 2018).

Ili kuimarisha uaminika na uhalali wa uchanganuzi wa maudhui kuhusu ripoti za vyombo vya habari vya Ulaya na Afrika zinazoshughulikia wahamiaji na wakimbizi, kundi la watafiti wa EBI lilitumia mbinu ya ziada ya kujadiliana na jopo la wahamiaji katika Ujerumani (Zappe na wengine, 2020). Kwa mujibu wa uchunguzi huu, washirika walikubaliana kwamba ni nadra kwa masuala ya uhamiaji na watu kufurushwa makwao kupewa umuhimu ufaao katika vyombo vya habari vya nchi za nyumbani. Hasa habari mahsusi katika fani hii ilikuwa haba; kwa kiwango kikubwa, habari chache walizokuwa nazo kabla ya kuamua kuhama walijitafutia wenyewe kutoka kwa vyanzo binafsi. Kadhalika, walikariri kulikuwa na shaka kuhusu uaminika wa habari hizo za vyombo vya habari na kutoka kwa watu wengine, kama alivyosimulia mhamiaji mmoja kutoka Senegal: “Katika Senegal, huwezi kuupata ukweli. Hawakwambii ukweli. Unaupata ukweli ukifika hapa” (Zappe na wengine, 2020, uk. 136). Hata hivyo, ni muhimu kufahamu kwamba washirika walisema huenda hali hiyo imebadilika pole pole na kuwa bora zaidi katika miaka ya karibuni. Walieleza pia kuhusu picha iliyopotoshwa ya hali halisi ya maisha katika Ujerumani inayojitokeza katika vyombo vya habari vya Afrika na jamii, ambayo miongoni mwa mengine, hukariri wazo kwamba mhamiaji akiingia Ujerumani ana uhakika wa kupata pesa nyingi. Waliohojiwa walivitaka vyombo vya habari Afrika kueleza hali halisi iliyopo Ulaya: “Waandishi wetu wa habari katika Afrika, kwa sababu wanazozifahamu wenyewe, hukataa kuonyesha pia upande mbaya wa Ulaya, kama ambavyo nimekuwa nikiwaambia kila mara watu katika Afrika. Ndiposa ninafikiri uanahabari katika Afrika unatekeleza wajibu fulani katika uhamiaji wa watu” (akasema mhamiaji kutoka Ghana aliyenakiliwa na Zappe na wengine, 2020, uk. 136). Kwa mujibu wa washiriki katika majadiliano hayo, sio tu uhamiaji kutoka Afrika kwenda Ulaya lakini uhamiaji kutoka nchi moja ya Afrika hadi nyingine huangaziwa mara moja moja tu na vyombo vya habari. Hapa pia, mawasiliano kati ya watu wawili yanachukua nafasi kubwa katika kuwasilisha habari. Kwa maelezo zaidi, tazama makala amili iliyotolewa na Zappe na wengine (2020) inayoweza kupakuliwa kutoka kwa tovuti yetu ya mradi.



ZOEZI LILILOPENDEKEZWA LA KUSHUGHULIKIA STADI ZA UTAMBUZI ZA KUCHANGANUA NA STADI ZA MITAZAMO YA KIBINAFSI NA MAADILI ZA KU-POKEA:

Ni kwa nini vyombo katika nchi za Kaskazini huangazia zaidi kuripoti kuhusu wahamiaji? Linganisha athari za kisiasa na kijamii za uhamiaji na uhamaji wa kulazimishwa katika nchi asili na mwenyeji, pamoja na taratibu za desturi na maadili. Wapatie wahusika habari yote muhimu na kuwaacha waeleze athari zinazoweza kuletwa na ripoti za vyombo vya habari. Usisahau pia athari ziwezazo kuletwa na mifumo tofauti ya vyombo vya habari na masuala kuhusu uanahabari na pia pingamizi zinazoweza kuzuia habari za uhamiaji kuelezwa.

Uhamiaji na mtiririko wa habari za kimataifa

Uchanganuzi wa habari za kigeni kama mfumo wa uanahabari “ambao katika utekelezaji wake, habari huvuka mipaka ya nchi” una muundo na taratibu za kimsingi: Habari za kigeni mara nyingi huangazia siasa na wenye mamlaka ya kisiasa huwa kiini cha ripoti hizo (Hafez, 2002). Sifa nyingine za habari za kigeni ni kutilia mkazo ukabila (Meier, 1984), masuala ya kanda (Sreberny-Mohammadi na wengine, 1985) na mambo ya nyumbani (Kamps, 2008), sifa ambazo vyombo vya habari huzingatia zinaporipoti kuhusu matukio ya kimataifa katika ulimwengu unao-tawaliwa na mitazamo ya kitaifa. Sifa nyingine ya kimuundo ya ripoti za kigeni ni kwamba zime-tawaliwa na mtazamo hasi, na hasa katika masuala ya mizozo na mapambano.

Kutokana na uhaba katika mtiririko wa habari za kimataifa, utoaji wa ripoti kuhusu Afrika umebaki kuwa changamoto ya kipekee. Segev (2014, uk. 425) anasimulia “katika ngazi ya ulimwengu, mataifa mengi ya Afrika yana uwakilishi mdogo kabisa”. Uchunguzi kuhusu ripoti za habari za Afrika katika vyombo vya Ulaya huonyesha upungufu mwingi, hasa mkazo unaotiliwa kwa ripoti za mizozo katika Afrika, huku mitazamo ya Kimagharibi ikitawala habari zinazoripotiwa (Mükke, 2009). Mwelekeo wa chuki na ubaguzi kwenye vyombo vya habari vya Kimagharibi vinapoeleza habari za Afrika hujitokeza kwa kuangazia mada kama vita, mizozo, majanga, magonjwa, ufi-sadi na uhalifu (EL Zein & Cooper, 1992; Mengara, 2001). Huku uchunguzi uliopo ukihukumu kwamba bara la Afrika limeendelea kuwa ‘mahali pasipoonekana wala kueleweka vizuri’ katika ripoti za kigeni (Franks, 2010; Serwornoo, 2018), wachunguzi wengine wanadokeza kupunguka kwa ripoti kutoka Afrika zinazotilia mkazo mabaya na majanga tu katika magazeti ya Kimagharibi (kuhusu Australia: Obijiofor & Hanusch, 2011; Obijiofor & MacKinnon, 2016; kuhusu Marekani na Uingereza: Scott, 2015), na kuweka mtazamo ufaao kwa ukosoaji mkali wa ripoti za vyombo vya Magharibi kuhusu Afrika (Nothias, 2016).

Wasomi Waafrika pia wameng’ang’ana na suala la taswira ya Afrika katika vyombo vya habari vya Kimagharibi (na hasa Obijiofor & Hanusch, 2011; Serwornoo, 2018; Wa’Njogu, 2009). Oguh (2015) anahoji kwamba vyombo vingi vya habari hukosa kwenda sambamba na maendeleo halisi katika nchi za Afrika, kwa mfano kuongezeka kasi kwa maeneo ya miji ambayo ni kinyume kabisa

na taswira inayokaririwa kwamba Afrika ni bara la washamba. Kulingana na Wa’Njogu (2009), kiini cha tatizo hilo ni ukweli kwamba asili ya habari nyingi kuhusu Afrika zinazoripotiwa ulimwenguni si mashirika ya habari ya Afrika, lakini ya Wazungu. Mbali na masuala ya ndani, habari kuhusu Afrika husawiriwa na miundo ya vyombo vya habari. Uhaba wa mashirika ya ukusanyaji wa habari katika Afrika, kupunguka barani kwa idadi ya waandishi kutoka nje na maarifa finyu kuhusu Afrika miongoni mwa wahariri katika Ulaya mara nyingi husababisha uteuzi na utumiaji wa taarifa za habari zisizo na uasili (Hafez, 2005; Mükke, 2009; Stürmer, 2013). Kutilia mkazo mabaya na mizozo hutekeleza wajibu katika Afrika kwa sababu taswira hasi ya Afrika katika vyombo vya habari vya Magharibi huingiliana na mtazamo binafsi wa wahusika Waafrika (tazama Hall, 1997; Mengara, 2001).

Michael Yao Serwornoo PhD, ambaye ni profesa wa uanahabari katika Ghana, amefanya utafiti awali kuhusu sura ya Afrika katika magazeti ya Ghana (Serwornoo, 2018). Uchanganuzi wake unahukumu kwamba mara nyingi Afrika huwakilishwa na mifumo sawa na inayotumiwa na vyombo vya habari vya Magharibi, kwani vyombo vya habari Afrika hutegemea vyanzo vya nchi za Kaskazini hata kwa habari za mataifa jirani ya Kiafrika. Kwa kukosa wakusanyaji habari katika maeneo ya matukio, uhariri duni, uhaba wa nafasi kwa sababu ya sera ya matangazo ya biashara na dhana kuhusu maslahi ya umma katika mashauri ya siasa, kiwango cha habari za kigeni kingali chini sana. Isitoshe, ni nadra kwa vyombo vya Afrika kuzipatia nafasi ya haja habari za matatizo ya kisiasa na kiuchumi yanayosababisha tatizo la uhamiaji katika Afrika. Asante, Sun na Long (2013) wamefikia uamuzi kwamba “Afrika [...] hukabiliwa na maonevu kutokana na dosari asili za vyombo vyake vinavyotoa habari”. Kadhalika, utafiti mchache umefanywa kuhusu tatizo sugu kwamba vyombo vya habari vya Afrika vina mazoea ya kuzipatia kisogo nchi nyingine za Afrika, mara nyingi kutokana na uhaba wa rasilimali hitajika katika vyumba vya habari, hali iwezayo kuathiri pakubwa uwezekano wa nafasi za biashara kati ya nchi, kwa mfano (Turkson, 2012). Hatimaye, Ogunyemi (2011) anauliza iwapo intaneti inaweza kuwa kifaa cha thamani cha kusawiri picha ya kuaminika zaidi kuhusu Afrika katika mitandao ya jamii.

Utafiti wa jinsi habari za uhamiaji zinariptiwa katika nchi tofauti: Ulaya, USA, Urusi

Utafiti wa pili uliofanywa na EBI katika nchi tofauti unalinganisha uandalizi wa habari kuhusu wakimbizi katika nchi 17 za Ulaya Magharibi na Mashariki, Marekani na Urusi. Uchunguzi unachanganua ripoti za habari katika majuma sita teule kati ya Agosti 2015 na Machi 2018 (Fengler & Kreutler, 2020).²Tutaakisi hapa baadhi ya matokeo muhimu lakini ripoti kamili inaweza kupatikana katika tovuti ya mradi. Utafiti ulichokonoa jumla ya makala 2,417 katika majuma sita teule ya uchunguzi kati ya Agosti 2015 na Machi 2018 (tazama Kielelezo 16). Tofauti kuu kwa yaliyotiliwa mkazo katika ripoti kuhusu uhamiaji na kuhamishwa kwa lazima kote katika nchi hizo zote zilijitokeza katika majuma yote ya utafiti. Ripoti za habari katika Ujerumani na Hungary

2 Majuma ya uchunguzi yaliteuliwa kwa msingi wa uchunguzi wa mwanzo katika vyombo vinane vya habari ambapo majuma yaliyokuwa na ongezeko kubwa zaidi la makala ikilinganishwa na juma lililotangulia yalitambulishwa. Maelezo kuhusu mbinu za uchunguzi na maelezo ya jumla kuhusu makala zilizopatikana katika kila nchi yamo mtandaoni: Fengler and Kreutler (2020).



ZOEZI LILILOPENDEKEZWA LA KUSHUGHULIKIA STADI ZA UTAMBUZI WA KUCHANGANUA NA STADI ZA MITAZAMO YA KIBINAFSI NA MAADILI ZA KUPOKEA:

Wapatie washirika nafasi ya kuchanganua taarifa za kigeni katika nchi yako kwenye majadiliano kuhusu maswali yafuatayo:


1. Unachambujaje taarifa za habari za kigeni zinazotolewa katika nchi yako?
2. Nchi yako huripotiwaje ng'ambo?
3. Ni dhana gani zisizo na msingi kuhusu nchi yako hurudiwa kila mara? Una dhana gani zisizo na msingi kuhusu nchi za Kaskazini na za Kusini, na asili yake ni ipi?
4. Je, dosari za habari za kigeni zilizoelezwa hapo juu zinawezaje kuathiri utoaji wa habari za uhamiaji?
5. Unaweza kufanya nini kubadilisha hali hiyo ukiwa mwanahabari?

— mataifa mawili yaliyopata idadi kubwa zaidi ya maombi ya mara ya kwanza kutoka kwa wahamiaji — ni za kipekee tukiangalia idadi yake. Mada hiyo ilipata nafasi dogo zaidi katika magazeti mengine ya Ulaya. Makala nyingi pia zilipatikana katika magazeti makubwa ya kimataifa (The New York Times na The Guardian).

Isitoshe, magazeti mengi ya Ulaya huchukulia masuala ya uhamiaji na wakimbizi kuwa jambo la kigeni, linalotokea mbali na wasomaji katika nchi zao. Ni katika Italia, Ujerumani na Ugiriki pekee ambapo uhamiaji humulikwa kama suala la ndani. Magazeti ya Uingereza na Ufaransa huona kana kwamba mataifa yao yanahusika katika ngazi za kimataifa. Hali ni hiyo hiyo katika Hungary kutokana na jinsi serikali yake imemulikwa kisiasa kufuatia madai ya hatari zinazowakabili na mzigo unaosababishwa na wahamiaji. Katika magazeti ya Italia na kwa kiwango fulani ya Ufaransa, nafasi kubwa inachukuliwa na wahamiaji kutoka Afrika. Nchi nyingine katika Ulaya huwaangazia wahamiaji na wakimbizi kutoka Mashariki ya Karibu na ya Kati. Wahamiaji kutoka Ukraine wanaangaziwa katika Shirikisho la Urusi. Isitoshe, huwa inaonekana mara nyingi kana kwamba wanahabari hawawezi kutofautisha kati ya wakimbizi walio na haki chini ya Mkataba wa Geneva na wakimbizi wengine. Huenda wakati mwingine wanahabari wasiyafahamu maelezo ya mkataba huo kwani vifungu vyake vingi (asilimia 60) hutaja mchanganyiko wa makundi yaliyo katika hali tofauti, au swala la hali si bayana. Hata hivyo, tuligundua kwamba idadi ya makala ambazo zinazungumza wazi kuhusu wakimbizi na haki zinazowafaa ilipungua wakati wa utafiti.

Magazeti ya Ulaya Magharibi na ya mlengo wa kushoto au yaliyo huru huangazia zaidi hali ya wahamiaji na wakimbizi na misaada kwao, huku yale ya Katikati na Mashariki mwa Ulaya na ya mlengo wa kulia au yasiyopenda mabadiliko hutilia mkazo zadi matatizo na malalamiko. Bado katika karibu nchi zote wasomaji, wana fursa ya kuchagua kwani magazeti mawili makubwa yaliyochunguzwa yalitoa misimamo tofauti kuhusu mada hiyo. Uchanganuzi wa wahusika wakuu

Kielelezo cha 16: Idadi ya makala kuhusu uhamiaji zilizochapishwa katika majuma sita ya uchunguzi wa magazeti



Magazeti ambayo majina yake ni akronimu: FAZ – Frankfurter Allgemeine Zeitung; EFSYN – Efimerida ton Syntakton; NZZ – Neue Zürcher Zeitung. Kwa magazeti yaliyokuwa na makala zaidi ya 100, makala 100 zilichaguliwa bila utaratibu maalumu. Muda wa uchunguzi: ,15.10.17-.09.10 ,10.01.16-04.01 ,15.11.15-09.11 ,06.09.15-.31.08 25.02.18-.19.02 ,17.12.17-.11.12. Asili: Fengler and Kreutler (2020, uk. 20). Kielelezo chetu.

unasisitiza kwa mara nyingine umuhimu wa watu na mashirika yanayohusika na uandalizi wa sera katika utoaji wa ripoti kuhusu wahamiaji. Ni suala lifaalo kuangaziwa na serikali. Katika asilimia 37 ya makala, serikali au mwakilishi mmoja wa serikali au chama tawala ndiye mhusika mkuu; wapinzani wanatajwa kuwa wahusika wakuu katika asilimia mbili pekee ya makala. Wahamiaji huwakilisha asilimia 26.6 ya wahusika wakuu lakini mara nyingi wanawakilishwa na

makundi makubwa yasiyo na majina kuliko watu binafsi au makundi madogo kama vile familia ambazo huenda baadhi ya watu binafsi miongoni mwao wana ujuzi hitajika. Katika kila Makala 10, watu wengi wasio wahamaji wamenakiliwa moja kwa moja au kutajwa mara nyingi kuliko wahamiaji. Matokeo hayo yanasisitiza uchunguzi wa awali na yanahitaji kuangaziwa katika ripoti kuhusu uhamiaji. Kwa mfano, magazeti ya Marekani yaliyochunguzwa ni yale ambayo yaliwaan-gazia zaidi wahamiaji na wakimbizi binafsi, pengine kwa sababu ya itikeli za kitaalamu za uana-habari zinazolingana na lengo la kuwapatia sauti hata wale wasio nayo.



ZOEZI LILIOPENDEKEZWA LA KUSHUGHULIKIA STADI ZA UTAMBUZI ZA KUCHANGANUA NA STADI ZA MITAZAMO YA KIBINAFSI NA MAADILI ZA KUJIBU:

Yajadili matokea ya utafiti huu. Ni matatizo gani kati ya yaliyotambuliwa yawezayo kuonekana katika vyombo tofauti vya habari? Wanahabari na vyumba vya habari huenda wakakumbana na pingamizi na vikwazo gani? Hali hiyo inaweza kuathiri vipi shughuli za kuripoti kuhusu uhamiaji na uhamishwaji wa lazima?



KAZI YA ZIADA ILIYOPENDEKEZWA kushughulikia stadi za utambuzi za kuchanganua na stadi za mitazamo ya kibinafsi na maadili za kujibu (A), au kushughulikia stadi za utambuzi za kuchanganua na kubuni (B):

(A) Waruhusu washiriki kuchagua nchi moja ya kutafiti, kisha waombe watayarisha wasilisho/waandae podkasti/waunde posta kuhusu changamoto za kuripoti uhamiaji na uhamishwaji wa lazima katika mazingira yanayozidi kubadilika ya uanahabari.

(B) Pakua kitabu cha sheria bainifu za kuripoti kuhusu wahamiaji na wakimbizi kutoka kwa tovuti yetu ya mradi. Waombe wanafunzi waunde makundi na kufanya uchanganuzi kifani wa vyombo vya habari katika nchi yako, kwa kipindi teule (tuseme kwa mfano wiki nne) na matokeo yao yawasilishwe katika kikao cha mwisho. Waombe walinganisha ripoti za vyombo vya habari katika nchi yake na ripoti za vyombo vya habari katika nchi zilizoangaziwa katika utafiti wa Fengler na Kreutler (2020).



USOMAJI WA ZIADA:

Kiuanahabari:

Fengler, S., & Kreutler, M. (2020a). Migration coverage in Europe's media: A comparative analysis of coverage in 17 countries. Frankfurt/Main: OBS Working Paper 39.

Kiakademia:

Chinje, E. (2016). "Europe Has to Deal with the Causes of Migration from Africa." Retrieved December 20, 2020, from <http://www.theafricancourier.de/europe/europe-has-to-deal-with-the-causes-of-migration-from-africa-eric-chinje/> (accessed 22nd June 2018).

Kitaasisi:

White, A. (Ed.) (2015). Moving Stories. International Review of how Media Cover Migration. London: Ethical Journalism Network. Retrieved December 20, 2020, from <https://ethicaljournalismnetwork.org/assets/docs/054/198/8feb836-108e6c6.pdf> (accessed 26th June 2018)..

Marejeleo

African Media Barometer (2018). The african media barometer country report: Kenya 2012. Retrieved December 19, 2020, from <http://library.fes.de/pdf-files/bueros/africa-media/09404.pdf>

Al-Mazahara, M. (2016). The Jordanian media coverage of the Syrian refugee crisis in Jordan: Analytical study of daily newspapers. *Journal of Middle East Media*, 12, 1-20.

Asante, M. K., Sun, J., & Long, H. (2013). The western media and the falsification of Africa: Complications of Value and Evolution. *China Media Report Overseas*, 9(4), 64-70.

Assopgoum, F. T. (2011). Migration aus Afrika in die EU: Eine Analyse der Berichterstattung in deutschen und senegalesischen Zeitungen. Wiesbaden: VS Verlag für Sozialwissenschaften.

Balabanova, E., & Balch, A. (2010). Sending and receiving: The ethical framing of intra-EU migration in the European press. *European Journal of Communication*, 25(4), 382-397. <https://doi.org/10.1177/0267323110381005>

Bastian, M., Zappe, A.-C., Wüllner, G., Oppermann, L., Leißner, L., Henke, J., & Serwornoo, M. (2018). Abschluss-bericht Auswärtiges Amt: Evaluationsprojekt zur Qualität der aktuellen Berichterstattung in afrikanischen Schlüssel-ländern: EBI Working Paper 2018. Internal Document.

Berry, M., Garcia-Blanco, I., & Moore, K. (2015). Press coverage of the refugee and migrant crisis in the EU: A content analysis of five European countries: Report prepared for the United Nations High Commission for Refugees. Retrieved November 30, 2020, from <https://www.unhcr.org/protection/operations/56bb369c9/press-coverage-refugee-migrant-crisis-eu-content-analysis-five-european.html>

Bleich, E., Bloemraad, I., & Graauw, E. de (2015). Migrants, minorities and the media: Information, representations and participation in the public sphere. *Journal of Ethnic and Migration Studies*, 41(6), 857-873. <https://doi.org/10.1080/1369183X.2014.1002197>

Caviedes, A. (2015). An emerging 'European' news portrayal of immigration? *Journal of Ethnic and Migration Studies*, 41(6), 897-917. <https://doi.org/10.1080/1369183X.2014.1002199>

Chinje, E. (2016). Europe has to deal with the causes of migration from Africa. Retrieved June 22, 2018, from <https://www.theafricancourier.de/europe/europe-has-to-deal-with-the-causes-of-migration-from-africa-eric-chinje/>

Danso, R., & McDonald, D. A. (2001). Writing Xenophobia: Immigration and the print media in post-apartheid South Africa. *Africa Today*, 48(3), 115-137. <https://doi.org/10.1353/at.2001.0050>

Eberl, J.-M., Galyga, S., Lind, F., Heidenreich, T., Edie, R., Boomgaarden, H. G., Herrero, B, Gómez Montero, E. L., & Berganza, R. (2019). European media migration report: How media cover migration and intra-EU mobility in terms of salience, sentiment and framing. Report. Retrieved December 20, 2020, from <https://www.reminder-project.eu/wp-content/uploads/2019/08/REMINDER-D8.3.pdf>

EJO (2015). Wie Zeitungen aus West- und Osteuropa über die Flüchtlingskrise berichteten. Retrieved July 3, 2017, from <https://de.ejo-online.eu/forschung/wie-zeitungen-in-europa-ueber-die-fluechtlingskrise-berichteten>

EL Zein, H. M., & Cooper, A. (1992). New York Times coverage of Africa. In Hawk, B. G. (Ed.), *Africa's media image* (uk. 133-146). New York, London: Praeger.

Esses, V. M., Medianu, S., & Lawson, A. S. (2013). Uncertainty, threat, and the role of the media in promoting the dehumanization of immigrants and refugees. *Journal of Social Issues*, 69(3), 518-536. <https://doi.org/10.1111/josi.12027>

European Commission (2018). Special Eurobarometer 469: Integration of immigrants in the European Union. Summary. Retrieved November 24, 2020, from https://ec.europa.eu/home-affairs/news/results-special-eurobarometer-integration-immigrants-european-union_en

Fengler, S., Bastian, M., Brinkmann, J., & Zappe, A.-C. (2018). Die "Flüchtlingskrise": Ethische Herausforderungen für Medien in Europa und Afrika – Migrationsberichterstattung in 11 afrikanischen und europäischen Ländern. In Köberer, N., Prinzig, M., & Schröder, M. (Eds.), *Kommunikations- und Medienethik: Vol. 8. Migration, Integration, Inklusion: Medienethische Herausforderungen und Potenziale für die digitale Mediengesellschaft*. Baden-Baden: Nomos.

Fengler, S., Bastian, M., Brinkmann, J., Zappe, A. C., Tatab, V., Andindilile, M., Assefa, E., Chibita, M., Mbaine, A., Obonyo, L., Quashigah, T., Skleparis, D., Splendore, S., Tadesse, M. & Lengauer, M. (2020a). Covering Migration – in Africa and Europe: Results from a comparative analysis of 11 countries. *Journalism Practice*. <https://doi.org/10.1080/17512786.2020.1792333>

Fengler, S., & Kreutler, M. (2020). Migration coverage in Europe's media: A comparative analysis of coverage in 17 countries. Frankfurt/Main: OBS Working Paper 39. Retrieved December 20, 2020, from https://www.otto-brenner-stiftung.de/fileadmin/user_data/stiftung/02_Wissenschaftsportal/03_Publikationen/AP39_Migration_EN.pdf

Fine, J., & Bird, W. (2002). Shades of prejudice: An investigation into the South African media's coverage of racial violence and xenophobia: Research conducted by the media monitoring project. Retrieved December 15, 2020, from <https://www.google.com/url?sa=t&rct=j&q=&esrc=s&source=web&cd=&cad=rja&uact=8&ved=2ahUKEwiChZ-vDx8jsAhUKO8AKHaVBGsQFjAAegQIAhAC&url=https%3A%2F%2Fwww.csvr.org.za%2Fdocs%2Fforeigners%2F-shades.pdf&usg=AOvVaw03hc9KaYKk4DADaKoJnC9DT>

Fohrn, K. (2009). Nähe und Bedrohung: Medienberichterstattung über illegale Einwanderung aus Afrika. In Jäger, T. (Ed.), *Sicherheit und Medien* (pp. 93-108). Wiesbaden: VS Verlag für Sozialwissenschaften.

Fotopoulos, S., & Kaimaklioti, M. (2016). Media discourse on the refugee crisis: On what have the Greek, German and British Press focused? *European View*, 15(2), 265-279. <https://doi.org/10.1007/s12290-016-0407-5>

Franks, S. (2010). The neglect of Africa and the power of aid. *International Communication Gazette*, 72(1), 71-84. <https://doi.org/10.1177/1748048509350339>

Georgiou, M., & Zaborowski, R. (2017). Council of Europe report: Media coverage of the "refugee crisis": A cross-European perspective. Retrieved December 15, 2020, from <https://rm.coe.int/1680706b00>

- Goedeke Tort, M. N., Guenther, L., & Ruhrmann, G. (2016). Von kriminell bis willkommen. Wie die Herkunft über das mediale Framing von Einwanderern entscheidet. *Medien & Kommunikationswissenschaft*, 64(4), 497-517. <https://doi.org/10.5771/1615-634X-2016-4-497>
- Hafez, K. (2002). *Die politische Dimension der Auslandsberichterstattung. Theoretische Grundlagen: Vol. 1.* Baden-Baden: Nomos.
- Hafez, K. (2005). *Mythos Globalisierung: Warum die Medien nicht grenzenlos sind.* Wiesbaden: VS Verlag für Sozialwissenschaften.
- Hafez, K. (2011). Global journalism for global governance? Theoretical visions, practical constraints. *Journalism: Theory, Practice & Criticism*, 12(4), 483-496. <https://doi.org/10.1177/1464884911398325>
- Hall, S. (1997). *Representation – Cultural representations and Signifying Practices.* London: Sage.
- Harteveld, E., Schaper, J., Lange, S. L. de, & van der Brug, W. (2018). Blaming Brussels? The impact of (news about) the refugee crisis on attitudes towards the EU and national politics. *JCMS: Journal of Common Market Studies*, 56(1), 157-177. <https://doi.org/10.1111/jcms.12664>
- Horsti, K. (2008). Europeanisation of public debate. *Javnost – The Public*, 15(4), 41-53. <https://doi.org/10.1080/13183222.2008.11008981>
- ICMPD (2016). How does the media on both sides of the mediterranean report on migration? Preliminary findings, draft conclusions and draft recommendations. Retrieved December 15, 2020, from http://media-diversity.org/additional-files/Media_Migration_17_country_chapters.pdf
- Kamps, K. (2008). Nachrichtengeografie. In Hahn, O., Lönnendonker, J. & Schröder, R. (Eds.), *Deutsche Auslands-korrespondenten: Ein Handbuch* (pp. 80-98). Konstanz: UVK.
- Krüger, U. M., & Zapf-Schramm, T. (2016). Info-Monitor 2015: Europa und Deutschland rücken ins Zentrum globaler Krisen. *Media Perspektiven*. (2), 70-97.
- MacBride, S. (1980). *Many voices, one world: Communication and society, today and tomorrow.* Paris: Rowman & Littlefield.
- McDonald, D. A., & Jacobs, S. (2005). (Re)writing xenophobia: Understanding press coverage of cross-border migration in Southern Africa. *Journal of Contemporary African Studies*, 23(3), 295-325. <https://doi.org/10.1080/02589000500274050>
- Meier, W. A. (1984). *Ungleicher Nachrichtenaustausch und fragmentarische Weltbilder: Eine empirische Studie über Strukturmerkmale in der Auslandsberichterstattung.* Bern, New York: P. Lang.
- Meltzer, C. E., Eberl, J.-M., Theorin, N., Lind, F., Schemer, C., Boomgaarden, H. G., Strömbäck, J. & Heidenreich, T. (2018). Perceptions of the impact of immigration and attitudes towards free movement within the EU: A cross-national study: Working paper as part of the REMINDER project. Retrieved December 20, 2020, from https://www.reminder-project.eu/wp-content/uploads/2018/04/with-cover_D9.2.pdf
- Mengara, D. (2001). Introduction: White eyes, dark reflections. In Mengara, D. M. (Ed.), *Images of Africa: Stereotypes & realities* (pp. 1-20). Trenton, N.J.: Africa World Press.
- Mengara, D. M. (Ed.) (2001). *Images of Africa: Stereotypes & realities.* Trenton, N.J.: Africa World Press.
- Mükke, L. (2009). *Journalisten der Finsternis: Akteure, Strukturen und Potenziale deutscher Afrika-Berichterstattung.* Köln: Halem.
- Nothias, T. (2016). How western journalists actually write about Africa. *Journalism Studies*, 19(8), 1138-1159. <https://doi.org/10.1080/1461670X.2016.1262748>
- Obijiofor, L., & Hanusch, F. (2011). *Journalism across cultures: An introduction.* New York: Palgrave Macmillan.
- Obijiofor, L., & MacKinnon, M. (2016). Africa in the Australian press: Does distance matter? *African Journalism Studies*, 37(3), 41-60. <https://doi.org/10.1080/23743670.2016.1210017>

- Oguh, C. H. (2015). The representation of Africa in western media: Still a 21st century problem. Doctoral dissertation, Napier University, Edingurgh. Retrieved January 5, 2020, from https://www.researchgate.net/publication/292141961_The_Representation_of_Africa_in_Western_Media_still_a_21st_century_problem
- Ogunyemi, O. (2011). Representation of Africa online: Sourcing practice and frames of reference. *Journal of Black Studies*, 42(3), 457-478. <https://doi.org/10.1177/0021934710378747>
- Scott, M. (2015). The myth of representations of Africa: A comprehensive scoping review of the literature. *Journalism Studies*, 18(2), 191-210. <https://doi.org/10.1080/1461670X.2015.1044557>
- Segev, E. (2014). Visible and invisible countries: News flow theory revised. *Journalism: Theory, Practice & Criticism*, 16(3), 412- 428. <https://doi.org/10.1177/1464884914521579>
- Serwornoo, M. Y. W. (2018). Africa's image in the Ghanaian press: the influence of international news agencies (PhD Dissertation). Ruhr University Bochum. <https://hss-opus.ub.rub.de/opus4/frontdoor/index/index/docId/6140>
- Smith, M. J. (2009). The right to respond: A meta-review of the role of the South African media's coverage of xenophobia and the xenophobic violence prior to and including May 2008. Retrieved December 19, 2020, from http://www.atlanticphilanthropies.org/wp-content/uploads/2010/07/14_Media_c.pdf
- Sreberny-Mohammadi, A., Nordenstreng, K., Stevenson, R., & Ugboajah, F. O. (1985). Foreign news in the media: International reporting in 29 countries. Final report undertaken for UNESCO. Paris: United Nations Educational.
- Stürmer, M. (2013). Afrika! Ein Plädoyer für eine differenzierte Berichterstattung. Konstanz/München: UVK.
- Turkson, F. E. (2012). Trade agreements and bilateral trade in sub-Saharan Africa: Estimating the trade effects of the EU-ACP PTA and RTAs. *Research Papers 12/07*. Retrieved December 19, 2020, from [https://www.nottingham.ac.uk/credit/documents/papers/12-07.pdf](https://www.notttingham.ac.uk/credit/documents/papers/12-07.pdf)
- UN (2018). Global Compact for Safe, Orderly and Regular Migration: Intergovernmentally negotiated and agreed outcome. Retrieved December 20, 2020, from https://refugeesmigrants.un.org/sites/default/files/180713_agreed_outcome_global_compact_for_migration.pdf
- UNESCO (1954). Twisted images: How nations see each other. Paris: UNESCO Publications.
- Waisbord, S., & Mellado, C. (2014). De-westernizing Communication Studies: A reassessment. *Communication Theory*, 24(4), 361-372. <https://doi.org/10.1111/comt.12044>
- Wa’Njogu, J. K. (2009). Representation of Africa in the western media: Challenges and opportunities. In Njogu, K. & Middleton, K. (Eds.), *Media and identity in Africa* (pp. 76-83). London: Oxford University Press.
- White, A. (2015). Moving stories: International review of how media cover migration. Retrieved December 20, 2020, from <https://ethicaljournalismnetwork.org/assets/docs/054/198/8feb836-108e6c6.pdf>
- Zappe, A.-C., Bastian, M., Leißner, L., Henke, J., & Fengler, S. (2020). Perspektivwechsel. Migrationsberichterstattung in ausgewählten afrikanischen Ländern und Deutschland aus Migrant*innensicht. Retrieved December 18, 2020, from <https://www.ssoar.info/ssoar/handle/document/68126>



MODULI 5

Kuripoti kuhusu uhamiaji – Taathira za vyombo vya habari na changamoto za kitaalamu

na Anna-Carina Zappe



MALENGO YA MODULI

- Kuwafahamisha washiriki umuhimu wa athari za vyombo vya habari wanaporipoti kuhusu uhamiaji na wakimbizi.
- Kushughulikia athari za taarifa za vyombo vya habari kwa hadhira zake za kitaifa na kimataifa.
- Kuakisi changamoto za kitaalamu ambazo wanahabari hukumbana nazo wakitafuta na kueleza habari za wahamiaji na wakimbizi.



MATOKEO YA MAFUNZO

Kufikia mwisho wa moduli hii, washiriki wanapaswa kuwa na uwezo wa:

- Kujadili umuhimu wa taathira za modeli muhimu za vyombo vya habari katika kueleza kuhusu uhamiaji → **Matokeo ya mafunzo kwa stadi za mitazamo ya kibinafsi na maadili: Kujibu**
- Kuchunguza hali zinazotoa changamoto kwa ukusanyaji na utoaji habari za kitaalamu kuhusu wahamiaji na wakimbizi katika nchi tofauti. → **Matokeo ya mafunzo kwa stadi za utambuzi: Kuchanganua**
- Kukadiria kwa makini taathira za kiitikeli za habari kuhusu wahamiaji na wakimbizi → **Matokeo ya mafunzo kwa stadi za utambuzi: Kutathmini**

Muhtasari


Wanahabari ni kama “wanahistoria wa nyakati za sasa” (Feinstein na wengine, 2018, uk. 1), wanaorekodi matukio muhimu ya kitaifa na kimataifa. Uhamiaji na uhamaji wa kulazimishwa, kama ilivyoelezwa katika moduli zilizotangulia, kwa yakini ni masuala muhimu kwa ulimwengu na pia ndani ya kila nchi na yanahitaji kurekodiwa. Kukusanya na kueleza habari za uhamiaji kitaalamu na kwa umakinifu kunahitaji sio tu stadi za kitaalamu na maarifa ya kuutafuta ukweli lakini ufahamu kamili wa athari za ripoti za mwanahabari husika. Vyombo vya habari vinaweza kuwaathirisha wahamiaji na wakimbizi na pia watu walio katika nchi wanamopitia na kikomo cha safari zao; vyombo vya habari vinaweza pia kuathiri maamuzi ya kisiasa na taratibu za kuchukua maamuzi; vyombo vya habari vinaweza kushawishi mitazamo ya umma ya masuala na taswira za watu.¹Haya yote huwapa wanahabari changamoto mbali mbali za kitaalamu. Isitoshe, kukusanya na kutoa habari kuhusu uhamiaji na masuala kuhusu wakimbizi huathiriwa na mambo mengine

1 Utafiti mwingi umefanywa kuhusu athari za jumla za vyombo vya habari kwa maoni ya umma, kampeni za uchaguzi na siasa, na pia kuhusu ubaguzi, lugha baguzi ya vyombo vya habari dhidi ya wahamiaji au utofauti na uwingine wa wahamiaji, suala ambalo linaweza kuhakikiwa katika mjadala. Kadhalika, nadharia za vyombo vya habari, kama vile ‘nadharia ya matumizi na anisi’ au ‘masomo ya utamaduni’ huthibitisha kwa nguvu wajibu muhimu wa hadhira kwa mtiririko wa habari. Umuhimu wa hadhira umejadiliwa katika Moduli ya 13, hali ambayo inaweza kushawishi maudhui ya vyombo vya habari kutokana na jinsi hadhira inatumia vyombo hivyo. Kwa vile shabaha ya moduli hii ni kuwasilisha mada na kualika tafakari kuhusu taathira za vyombo vya habari na wahamiaji na wakimbizi katika hatua ya kwanza, ni masuala teule pekee yaliyotajwa ambayo yameshughulikiwa.

mengi.² Moduli hii inaangazia pingamizi ambazo wanahabari hukumbana nazo wanaporipoti kuhusu masuala ya wahamiaji na wakimbizi.

Maoni ya umma kuhusu uhamiaji

Uchunguzi uliofanywa na International Organisation for Migration (IOM), ulioshirikisha watu wazima 183,000 katika zaidi ya nchi 140 waliohojiwa kati ya 2012 na 2014, ulionyesha kwamba asilimia 34 ya wahojiwa kote duniani wangependa kuona uhamiaji ukipunguka, asilimia 21 wangetaka uongezeka, asilimia 22 wanataka ubaki katika kiwango cha sasa na asilimia 22 hawakukata kauli (Esipova na wengine, 2015). Utafiti huo ukifanyika, tatizo la uhamiaji halikuwa limefika Ulaya na nchi za Kaskazini (tazama Kielelezo 17).



Hata hivyo, kwa mujibu wa uchunguzi wa IOM, watu wa Ulaya walionekana kuwa na maoni mengi hasi kuhusu uhamiaji, huku wengi wao (52%) wakisema viwango vya uhamiaji vinapaswa kupunguzwa. Katika Afrika, asilimia 40 walitaka uhamiaji katika nchi zao upunguzwe (Esipova na wengine, 2015).

2 Inahusu pia suala la “siasa na uchumi” la utoaji habari za uhamiaji. Ndiposa miundo inayoweza au kutatiza ukusanyaji na utoaji wa habari hizo kama vile miundo ya kiuchumi, kisiasa, kitamaduni au kiteknolojia na itikadi nyingine zinazohusiana na miundo hiyo inaweza kushawishi vyombo ya habari kutimiza wajibu wake kuujenga vipendavyo mjadala kuhusu uhamiaji katika sehemu tofauti za dunia au hata ulimwengu.

Kufuatia kuongezeka kwa wahamiaji na wakimbizi walioingia Ulaya mwaka 2015, umuhimu wa mada hiyo ulibadilika pia. Uhamiaji ukawa mada ya kwanza — mada ambayo ilikosolewa na watu wengi. Kwa mujibu wa utafiti uliofanywa Novemba 2016 na Eurobarometer ukihusisha Wazungu zaidi ya 32,000, uhamiaji uliibuka kuwa suala muhimu namba moja, ukitangulia ugaidi na uchumi (European Commission, 2016). Katika Agosti 2015, wakati Chansela Angela Merkel wa Ujerumani aliposema: “Wir schaffen das” (“Tunaweza kufanya haya”), na mabadiliko ya mazingira ya kisiasa katika Uingereza na kote katika ulimwengu yakaanza, hisia tofauti zilijitokeza. (Thränhardt, 2019).

Ukadiriaji wa tishio la lililotajwa kuwa ‘mzozo wa wakimbizi’ wa 2015 ulikuwa wa viwango tofauti kote katika Ulaya (Poushter, 2016). Uchunguzi uliofanywa 2016 na Pew Research Center ulionyesha kuwa Wazungu wengi (kiwango cha wastani cha 59% kote katika nchi 10 za Ulaya) walihofia kwamba ongezeko kubwa la idadi ya wakimbizi lingezidisha uwezekano wa kuongezeka kwa ugaidi na nchi zao zibebeshwe mzigo. Hata hivyo, kauli hii inatofautiana kati ya nchi tofauti: 76% walikiri hayo katika Hungary na 71% katika Poland, lakini ni 46% pekee katika Ufaransa na 40% katika Uhispania (Poushter, 2016).


Tofauti za kimitazamo zilijitokeza kwenye uchunguzi uliofanywa 2018 na Pew Research Center uliohusisha nchi 27 katika mabara matano: Ulaya (11), Asia (6), Marekani (5), Afrika (4) na Oceania (1). Utafiti huo (tazama Kielelezo 18) unaonyesha kwamba watu katika nchi za Ulaya ambazo zimekuwa kiingilio cha idadi kubwa ya wahamiaji na wakimbizi, waliukosoa uhamiaji pakubwa. Hasa waliohojiwa katika Ugiriki (82%), Hungary (72%) na Italia (71%) walisema wangetaka wahamiaji wachache au asiingie mkimbizi hata mmoja katika nchi zao. Hata hivyo, washiriki katika nchi nne za Afrika zilizochunguzwa hawakuwa na shida wakimbizi wakiingia katika nchi zao — Nigeria (50%), Kenya (60%) na Afrika Kusini (65%) — ambazo zilikuwa mwenyeji wa makumi ya maelfu ya wahamiaji na wakimbizi katika miaka iliyopita. Katika Tunisia, nchi ya nne iliyochunguzwa barani, watu chini ya nusu (42%) walioshiriki kwenye uchunguzi walipinga uhamiaji. Isitoshe, fungu la idadi ya watu waliotaka uhamiaji zaidi lilikuwa kubwa pia katika nchi zote nne (Tunisia: 20%, Nigeria: 20%, Kenya: 15%, Afrika Kusini: 11%) kuliko kiwango cha wastani cha Ulaya (10%) (Connor & Krogstad, 2018; Migration Data Portal, 2020).³ Utafiti mwingine katika nchi saba za Ulaya (Uingereza, Uhispania, Ujerumani, Sweden, Poland, Hungary, Romania) unaonyesha kwamba uhamiaji ulichukuliwa kuwa ni tishio zaidi wala si tukio la faida kote katika Ulaya. Faida ya pekee ya kiuchumi na kitamaduni ilihusishwa tu na wahamiaji kutoka Ulaya, ilhali tishio za usalama zilihusishwa hasa na wahamiaji kutoka Afrika na Mashariki ya Kati. (Meltzer na wengine, 2018).

Matokeo ya siku za karibuni ya uchunguzi yanadokeza kwamba mitazamo kuhusu uhamiaji katika nchi za Kaskazini haijabadilika na kuwa chanya: Uchunguzi kuhusu simulizi za uhamiaji katika Ulaya kupitia kwa majadiliano kwenye mitandao ya jamii ya umma ulionyesha kuwa mija-

3 Wakati huo huo, watu zaidi ya asilimia 60 katika kila moja ya nchi nne za Afrika walihofu kuhusu watu walioondoka makwao kwenda kutafuta kazi katika nchi nyingine (Connor & Krogstad, 2018).

dala hiyo inatawaliwa na “msimamo unaoungwa mkono na wengi wa kupinga uhamiaji” (Rinke, 2019, uk. 5).⁴Mitazamo kama hiyo bila shaka haiwezi kubaki bila matokeo yake kuonekana na inaweza kujiakisi katika siasa na vyombo vya habari au kinyume chake.⁵

Kielelezo 18: Kundi la wahamiaji huathiri mitazamo katika Ulaya (matokeo kamili)



Asili: Meltzer na wengine (2018, uk. 14), N = 21,882. Mchoro wetu. Ukumbusho: Ili kuonekana vyema zaidi, kielelezo asili kilipangwa upya kuanzia -1 (kuonyesha faida za uhamiaji zinazofahamika) hadi +1 (kuonyesha vitisho vinavyofahamika vya uhamiaji).

4 Matokeo zaidi ya uchunguzi na takwimu za sasa za kauli ya umma kuhusu uhamiaji zinaweza kupatikana katika Migration Data Portal (2020).

5 Bila shaka, maoni katika jamii kuhusu masuala ya uhamiaji na watu kufukuzwa makwao hayaathiriwi na au kutegemea vyombo vya habari pekee. Miundo ya kiuchumi, kisiasa, kitamaduni au kiteknolojia na itikadi nyingine zinazohusiana na miundo hiyo, na matukio kama misukosuko ya kiuchumi hujenga ufahamu wa uhamiaji huo katika baadhi ya sehemu za dunia au hata ulimwengu wote.

Kampeni za uchaguzi na uhamiaji

Katika miaka ya karibuni, vyama vingi vya kisiasa vinavyofuata mfumo unaojali maoni na fikra za umma kote katika Ulaya vimejitafutia umaarufu kwa kutumia kwa manufaa yake hofu na wasiwasi zilizoenea kote kuhusu usalama katika jamii za Ulaya kutokana na athari za ongezeko la uhamiaji na watu kufukuzwa makwao. Mijadala kuhusu wahamiaji na wakimbizi huathiri paku-bwa kampeni za uchaguzi kote katika Ulaya. Mijadala hiyo imeathiri kampeni za uchaguzi katika Afrika pia. Hii hapa mifano ya siku za karibuni:⁶

- *Kenya 2017*: Kabla ya uchaguzi wa urais wa 2017 nchini Kenya, serikali ilitangaza mipango ya kufunga kambi za wahamiaji na wakimbizi kutoka Somalia. Ingawa Mahakama Kuu ilitibua mipango hiyo ilipoitaja kuwa kinyume cha Katiba, ilidokeza kuwa mpango huu wa kisiasa ulitokana na ongezeko la visa vya ugaidi (Warah, 2016; Whitaker, 2019). Rais Uhuru Muigai Kenyatta alihifadhi kiti chake alipochaguliwa tena baada ya kampeni kali.⁷
- *Afrika Kusini 2019*: Suala la chuki ya wageni lilishika nafasi kubwa katika kampeni za uchaguzi wa kitaifa na mikoa. Kwa mfano, bango la kampeni la chama cha Democratic Alliance lilikuwa na maandishi “linda mipaka yetu”. Chama hicho kiliibuka cha pili kikubwa baada ya kupata asilimia 20.77 ya kura zilizopigwa, kiasi ambacho kilishuka kidogo ikilinganishwa na uchaguzi uliotangulia. Hata hivyo, chama cha kisiasa cha mlengo wa kushoto kabisa cha Economic Freedom Fighters kiliibuka kwenye uchaguzi wa 2019 kuwa mojawapo ya vyama vilivyokua haraka kwa kuongeza kura zake kutoka asilimia sita hadi 10 (Tume ya Uchaguzi ya Afrika Kusini, 2019; Sguazzin, 2019).
- *Uingereza 2015*: Uchaguzi huu ulikuwa muhimu kwa EU yote kwani wapinzani wa EU kama vile UK Independence Party (UKIP) ambacho kilikuwa kinaisukuma Uingereza kujiondoa kutoka EU, kimepata ufuasi wa haja katika miaka ya karibuni. UKIP kiliibuka cha tatu kiku-bwa kwa kura kilizopata. Mada ya uhamiaji ilitumiwa pakubwa na UKIP kuonyesha hasara iliyodaiwa kuletwa na uanachama wa EU. (Evans & Mellon, 2019).
- *Austria 2017*: Freedom Party of Austria (FPÖ), chama cha kitaifa kinachofuata mfumo unaojali maoni na fikra za umma na kupinga mabadiliko kilipata asilimia 26 ya kura na hivyo basi kuibuka cha tatu miongoni mwa vyama vyenye uwezo mkubwa katika bunge. Vyombo vya habari vinakitaja chama hicho kuwa “mpinzani wa uhamiaji Freedom Party” (“Austria far right”, 2017).
- *Ujerumani 2017*: Chama cha Alternative for Germany (AfD) ambacho hapo awali hakikuwa na uwakilishi wowote katika bunge la Ujerumani, kiliibuka cha tatu chenye wabunge wengi

6 Katika yafuatayo, miktadha imewasilishwa lakini haelezwi bayana kwamba pana uwiano kasidi kuhusu matokeo ya uchaguzi na mitazamo ya watu kuhusu wahamiaji na/au wakimbizi.

7 Kwa mifano zaidi ya ufanisi wa uchaguzi na shughuli za vyama vya kisiasa vinavyopinga uhamiaji katika Afrika, tazama Whitaker (2019).

katika Bundestag, baada ya kupata asilimia karibu 13 ya kura za shirikisho zilizopigwa. Katika Jimbo la Saxony, kilipata ushindi mkubwa zaidi kwenye uchaguzi wa majimbo wa 2017. Unaotajwa kuwa “mzozo wa wakimbizi” wa 2015 ulibadilisha mandhari za kisiasa katika Ujerumani. AfD kililalamika — vikali wakati mwingine — kuhusu wasiwasi mkubwa wa sera ya Chansela Angela Merkel kutoa hifadhi kwa wahamiaji (Decker, 2020; Hanewinkel, 2017).

- *Italia 2018*: Chama cha Lega ambacho ni mpinzani mkubwa wa Jumuiya ya Ulaya na kinafuata pia mfumo unaojali maoni na fikra za umma, kilipata ufuasi mkubwa kwa kampeni zake za kuwakataa wakimbizi na kupinga utawala wa kisiasa uliokuwepo. Kilipata asilimia 18 ya kura (Dobbert, 2018; “Italian elections 2018”, 2018).
- *Bunge la Ulaya 2019*: Vyama vya mlengo wa kulia vilipata viti 73 kati ya 751 katika uchaguzi wa Bunge hilo, idadi ambayo ni karibu asilimia 10 (Europäisches Parlament, 2019). Magazeti yalianza kuandika kuhusu “ongezeko la ghafla la ufuasi wa wapigaji kura wanaounga mkono vyama vya mlengo wa kulia vinavyofuata mfumo unaojali maoni na fikra za umma (“Europe and right-wing”, 2019).

Kuripoti uhamiaji na watumiaji wa vyombo vya habari: taathira zinazoweza kujitokeza

Inaweza kuchukuliwa kwamba vyombo vya habari na wanahabari wanaweza kushawishi mitazamo ya umma kuhusu uhamiaji na uhamishwaji wa lazima (Entman, 1993; Iyengar na wengine, 1984; McCombs & Shaw, 1972; Weaver, 2007). Kipimo cha ushawishi kinategemea kwa kiwango fulani ni sura gani huonekana kwa umma wakati habari kuhusu wahamiaji na wakimbizi zinapoelezwa na ni zipi hazionekani.

BAADHI YA NADHARIA MUHIMU ZA TAATHIRA ZA VYOMBO VYA HABARI

Nadharia ya ushawishi wa hoja kwa umma: Vyombo vya habari “mara nyingi huenda visifanikiwe kuwaambia watu waangazie wapi fikira zao, lakini hupata ufanisi wa kushangaza katika kuwaambia wasomaji ni mambo gani wanapaswa kuyafikiria” (Cohen, 1963; McCombs & Shaw, 1972, uk. 177). Vyombo vya habari vinavyolenga umma hushawishi mtazamo wa umma kwa jinsi vinaripoti suala fulani, bila kujali vinafanya hivyo mara ngapi, na kwa kulipatia umuhimu suala ama kulipuuza kwenye ajenda yake ya habari, hivyo basi kuzipatia kipaumbele mada zake (Pürer, 2003).

Nadharia ya hali ya asili au kuerevusha: Nadharia hii haihusu athari za utambuzi kwa hadhara ya vyombo vya habari, lakini huathiri stadi za mitazamo ya kibinafsi. Ajenda inayosukumwa na vyombo vya habari inaweza kubadili mitazamo, dhana, mawazo na, hatimaye, uwezo wa kuamua, kwa mfano uamuzi wa mpigaji kura katika uchaguzi akizingatia kuvuta nadhari kwa baadhi ya masuala huku akipuuza mengine (Iyengar na wengine, 1984).

Nadharia ya stahabu: Nadharia hii hujulikana pia kama ngazi ya pili ya ushawishi wa hoja kwa umma, ingawa dhana hizi mbili ni tofauti (Weaver, 2007). Entman (1993, uk. 52) anaaridhia:

“Kustahabu ni kuchagua baadhi ya vipengele vya ukweli unaoonekana na kuvifanya kuwa muhimu na kujitokeza zaidi katika mawasiliano ya maandishi, kiasi cha kukuza uainishaji wa tatizo, ufasiri kasidi, utathmini wa maadili, na/au jinsi ya kuchukulia mapendekezo la kitu kinachoelezwa.”

Kuonyesha mfano: Taarifa hizi za vyombo vya habari zina matokeo tofauti zikilinganishwa na za maelezo dhahania (Fast na wengine, 2014). “Mifano dhahiri, ikilinganishwa na iliyosawijika huimarisha ufikiaji wa kiwango cha juu” (Zillmann & Brosius, 2010, uk. 48). Matokeo yake ni kwamba kuwainua watu kufikia kiwango cha kuwaonyesha kuwa mfano wa kuigwa huenda kukashawishi watumiaji wa vyombo vya habari (Brosius & Bathelt, 2016; Tversky & Kahneman, 1973). “Ukweli kwamba taarifa ya habari inaweza kubadilisha kauli kuhusu suala lenye uzushi kulingana na mifano dhahiri inayochaguliwa kueleza pointi za mjadala, na sio habari peke yake, ni muhimu” (Perry & Gonzenbach, 1997).⁸

Matokeo ya utafiti uliopo kuhusu nadharia hizi katika muktadha wa kuripoti kuhusu wahamiaji na wakimbizi kuzingatia mtazamo wa kutunga ushawishi wa kujenga hoja kwa umma, kuerevusha na kustahabu yanaonyesha kwamba vyombo vya habari vinaweza kushawishi hadhira (European Migration Network, 2018; IOM, 2019; UNHCR, n. d.):

- Katika uchunguzi wa nadharia za ushawishi wa hoja kwa umma na kuerevusha, Sogelola (2018) aligundua kwamba katika 2016, gazeti la Daily Mail la Uingereza — kabla ya kura ya maoni ya Brexit iliyohusu Uingereza kuitema EU — lilionyesha kuwa uhamiaji ni tukio mbaya.
- Goedeke Tort na wengine (2016) wameangazia suala la taswira ya vyombo vya habari ya wahamiaji katika Ujerumani mwaka 2014. Kati ya sura tano, ile ya “uhalifu” iliibuka kushika nafasi kubwa zaidi kwa wahamiaji kutoka Ulaya ya Kusini Mashariki (44%), na ilijitokeza pia kwa wahamiaji Waafrika (zaidi ya 20%). Kipimo cha upendelevu kilidhihirisha kiwango kikubwa cha mitazamo hasi kuliko jingine lolote (94%).
- Katika Uholanzi, watafiti waliangazia mitazamo kuhusu wakimbizi na kupata kwamba kua-kisi masuala yaliyoshirikisha tamaduni tofauti kulileta matokeo mazuri ya mitazamo kuhusu wahamiaji, ilhali taswira ya maonevu ilisababisha athari hasi (Bos na wengine, 2016).

8 Kuna nadharia nyingine nyingi fauka ya zilizotajwa. Isitoshe, mambo tofauti ya kinafsi na mishawasha mingine midogo ina nafasi yake pia. Hata neno moja moja linaweza kuwa na athari (tazama pia module 10). Kwa mfano, mara nyingine vyombo vya habari vikitumia kwa kubadilishana istilahi zenye maana tofauti au kuboronga maana za uhamiaji wa wahamiaji, wakimbizi, wahamiaji haramu, waliofurushwa makwao (IDPs), uhamiaji mchanganyiko na mengineyo vinaweza

- Lawlor (2015, uk. 351) alichunguza jinsi magazeti katika Canada na Uingereza kati ya 1999 na 2013 yalisawiri wahamiaji kwa kutumia uchanganuzi linganishi; matokeo yake yalikuwa kwamba “bado kuna hisia nzito za kichinichini za mjadala hasi zinazojitokeza katika taarifa za habari za magazeti yenye wasomaji wengi ambazo haziwezi kuchukuliwa kwa urahisi kuwa ni za wanaopinga uhamiaji pekee.”
- Medianu (2014) aligundua kwamba taswira ya wahamiaji katika vyombo vya habari vya Canada huenda bila kukusudia ikasababisha kudhalilishwa kwa wakimbizi — akirejelea athari za nadharia ya stahabu ya Arendt (2013).

Isitoshe, matokeo ya uhasama ya vyombo vya habari huenda yakajitokeza wakati watazamaji, wasikilizaji na wasomaji wa vyombo hivyo wanapohisi kwamba habari zinazoripotiwa kuhusu mizozo au masuala yenye ubishi mkubwa zinapendelea. (Vallone na wengine, 1985). Katika Ujerumani, Merten & Dohle (2019) walichunguza ung’amuzi kuhusu jinsi vyombo vya habari viliangazia lililotajwa kuwa “mzozo wa wakimbizi” wa 2015 miongoni mwa Wajerumani waliowakaribisha na waliowalaani wakimbizi.

“Matokeo ya uchunguzi yalionyesha kwamba mitazamo ya uhasama kwa ung’amuzi wa vyombo vya habari ilijitokeza katika makundi yote mawili, hasa miongoni mwa wapinzani wa kauli ya kirafiki ya kuwakaribisha wakimbizi. Mitazamo hiyo inalingana na kuongezeka kwa idadi ya wasio na imani na vyombo vya habari, utathmini mbaya zaidi wa kiwango cha ripoti kuhusu mada mahsusi, na ongezeko la hamaki” (Merten & Dohle, 2019, uk. 274).

Matokeo hayo yanaonyesha kwamba ripoti za magazeti kuhusu uhamiaji katika nchi za Kaskazini zinatawaliwa na mielekeo hasi, na huenda matokeo yake kwa kiwango fulani yakawa ushawishi hasi wa maoni ya umma kuhusu wahamiaji na wakimbizi katika nchi za Kaskazini. Kwa wanahabari ambao huangazia masuala ya wakimbizi na wahamiaji, ni muhimu kujifahamisha na mambo ya manufaa ya kujenga mawazo ya umma. Matokeo ya makala zinazosawiri utambulisho wa kundi (kwa kupinga dhana kwamba wahamiaji wakipata nafasi za kazi huwa wananyakua nafasi za wafanya kazi wa jamii mwenyeji wao) mara nyingi huwa kuibuka kwa mitazamo ya kusaidia wahamiaji.⁹ Isitoshe, kuhimiza muungano wa kitaifa unaoshirikisha wote, wenyeji kwa wahamiaji, huenda kukaibua mitazamo ya kufaa kwa wahamiaji (Esses na wengine, 2001; Esses na wengine, 2006; Meltzer na wengine, 2018). Uchunguzi uliofanywa 2006 katika Uswizi kuhusu ripoti za sheria za hifadhi za salama ulionyesha kwamba kueleza habari za kujenga za kampeni za walio wachache zina taathira

9 Katika muktadha huu, utazame mfano wa utafiti wa The Guardian. Kwa mujibu wa gazeti hilo, “wahamiaji wapya katika EU hawajaathiri pakubwa nafasi za kazi za vijana Waingereza wanaomaliza shule”, lakini “takribani nusu ya wapi-gaji kura wa Uingereza wanaamini kwamba athari za uhamiaji kwa ujiri ndio msingi wa mashaka yao kuhusu hali ya uchumi” (Howard, 2014).

za kufaa kwa mitazamo ya walio nje ya kundi hilo na pia umma (Schemer, 2014).¹⁰ Ingawa hakuna ripoti zozote za uchunguzi kutoka nchi za Afrika za uchanganuzi wa ripoti kuhusu uhamiaji kuzingatia dhana zilizoelzwa awali,¹¹ McDonald & Jacobs (2005) walitafiti ripoti kuhusu chuki kwa wageni katika nchi za kusini mwa Afrika, na kung'amua kuendelezwa kwa dhana potovu magazetini ya Afrika Kusini za mambo yasiyo na uasili, mgawanyiko mkubwa kati ya vyombo vya habari vinavyounga mkono na kupinga uhamiaji nchini Zimbabwe na kuchapishwa kwa ripoti za chuki kwa wageni katika Botswana.



ZOEZI LILILOPENDEKEZWA LA KUSHUGHULIKIA STADI ZA UTAMBUZI ZA KUCHANGANUA:

Andaa mjadala (A) au tumia mchezo fumbo wa kupanga vipande ili kupata picha kamili (B).

(A) Wanazuoni wa uanahabari wamebuni mitindo tofauti ya kueleza taathira za vyombo vya habari kwa watumiaji ambao ni hadhira yake. Nadharia hizo zinaweza kutekeleza wajibu mkubwa kwa kuripoti kuhusu wahamiaji na wakimbizi. Ingawa umuhimu wa mitandao ya jamii umeendelea kuongezeka miongoni mwa watumiaji kote ulimwenguni, taathira ya vyombo vikuu vya kiasili vya habari — hata kupitia kwa mitandao ya jamii — kuhusu ufahamu wa watu wa masuala ya uhamiaji ingalipo. Jadilieni tena mitindo na nadharia za mawasiliano wanazozifahamu washiriki kutoka kwa moduli za awali mkitilia maanani changamoto za kuripoti kuhusu wahamiaji na wakimbizi. Maelezo yaliyo kwenye kielelezo (“Baadhi ya nadharia kuu za taathira ya vyombo vya habari”) yanaweza kuwa kielekezi cha mjadala.

(B) Tayarisha shughuli tangamani kuhusu taathira za vyombo vya habari katika muktadha wa kukusanya na kutoa habari za wahamiaji na wakimbizi. Tumia mbinu ya mchezo fumbo ambayo inakuwezesha kuandaa shughuli ya darasa inayomfanya kila mwanafunzi kumtegemea mwenzake ili kufaulu. Gawa darasa katika makundi. Lazima kila kundi liakisi athari moja ya vyombo vya habari. Wanafunzi wajumuike kwa makundi kulingana na mada. Lazima kila mshiriki achangie mada na kundi litahitajika kuandaa bango kujibu swali hili: Vyombo vya habari huathiri kwa njia gani maoni na siasa katika muktadha wa masuala kuhusu wahamiaji na wakimbizi?”

PENDEKEZO BADILI KWA DARASA KUSHUGHULIKIA STADI ZA MITAZAMO YA KIBINAFSI NA MAADILI ZA KUJIBU:

Buni hali za kukusanya na kutoa habari ambazo zinahitaji uamuzi. Kwa mfano: Mhalifu alihusika katika kisa cha uhalifu na swali linaloibuka ni je, pana umuhimu wowote kutaja jina la mshukiwa na manusura pamoja na uraia wao unaporipoti kuhusu uhalifu uliofanyika? Waombe washiriki waeleze jinsi watashughulika. Hatimaye, shughulikia taathira inayojitokeza katika mfano huu: Stahabu).

10 Wojcieszak & Azrout (2016, uk. 1051) walidhihirisha kwamba “kuwaonyesha tu wahamiaji katika habari ni hatua tosha ya kuimarisha mitazamo”. Kiasi cha habari zilizotolewa kuhusu wahamiaji au kuongeza idadi ya taarifa za habari za kujenga kuliko za kukashifu wahamiaji, ziliisaidia hadhira kuanza kuwazoea, zikapunguza mashaka na kuimarisha uhusiano (Wojcieszak & Azrout, 2016). “Ndiposa, taswira ya kuwajenga wahamiaji na isiyowasawiri kama tishio” inaweza kuwa na matokeo hayo mema pia (Meltzer na wengine, 2018, uk. 16).

11 Onyebadi (2012) anaangazia ajenda za magazeti na maoni ya umma kuhusu uchaguzi wa urais wa Kenya uliofanyika 2007 na kuthibitisha kwamba nadharia ya ushawishi wa kujenga hoja kwa umma inaweza kujitokeza mbali na mipaka ya chimbuko lake katika Marekani na Ulaya, Asia na Amerika ya Kusini.

Taathira ya CNN na kisa cha “Alan Kurdi”

Taathira ya CNN hueleza matokeo ya habari zinazoenezwa na vyombo vya kimataifa kwa waandalizi wa sera kote ulimwenguni. Mtindo huu hudokeza kwamba athari za vyombo vya habari vyenye mitandao ya kimataifa, na ambavyo CNN ni mojawapo ya mifano ya vituo katika tasnia hii vilivyoanzishwa zamani, pamoja na mfululizo wa habari za 24/7, huwa ni kubwa kwa taratibu za maamuzi ya viongozi wa kisiasa kote duniani. Viongozi hao huenda wakajipata wakishinikizwa na umma kuingilia kati na kufadhili wenye shida na matatizo ya kisiasa ambayo pengine hata hayawahusu (Robinson, 2002). “Wengi huhoji kwamba walishawishiwa na taarifa za habari kuhusu watu waliokuwa wakiteseka katika kaskazini mwa Iraq (1991) na Somalia (1992) kuwasaidia waathiriwa wa vita” (Robinson, 2002, uk. 1).¹² Ndiposa katika muktadha unaoendelea wa sasa wa uhamiaji, ambao kwa kiwango fulani umesababishwa na migogoro na vita, athari za kisiasa zilizo sawa na taathira za CNN zimejidhihiri:

- Marais Donald Trump na Barack Obama wa Marekani walikabiliwa na picha za kutisha za mashambulizi ya gesi nchini Syria ambayo yaliripotiwa kote ulimwenguni (Doucet, 2018). Picha za wafu na watu waliokuwa wakifa kutokana na mashambulizi ya gesi katika Khan Sheikhoun, Syria, zilienea kwenye intaneti na mitandao ya jamii Aprili 2017. Kwa mujibu wa makala iliyochapishwa na gazeti la Washington Post, Rais Donald Trump alitangaza kwamba picha hizo zilimgusa sana (Bahador, 2017). Alichukua hatua kwa kutamka: “pana haja ya hatua kuchukuliwa” (Bash na wengine, 2017). Ilionekana kama kwamba sera ya Trump kuhusu Syria inabadilika (Bahador, 2017). “Uchunguzi wa serikali za Trump na Obama unasisitiza kwamba vyombo vya habari ni kiungo muhimu cha kudumisha shinikizo kwa wanaoandaa sera, wakiwemo wanasiasa, wambukuzi na wahusika mbali mbali wakuu katika mgogoro wa Syria” (Doucet, 2018, uk. 154).
- Ripoti moja ya CNN iliyotolewa 2017 ilifichua kwamba wakimbizi katika Libya walidhulumiwa na kuwekwa katika hali za kutisha zisizo za kibinadamu. Ripoti ilionyesha jinsi wahamiaji walikuwa wakiuzwa na walanguzi na kwamba palikuwa na soko la watumwa ndani ya Libya (“People for sale”, n. d.). Ripoti hiyo iliwagusa wengi ulimwenguni na kwa mara ya kwanza wanasiasa wa Afrika walichukua hatua; mathalani, Rwanda ilijitolea “kuwapatia makao wahamiaji Waafrika walioingizwa utumwani waliokwama Libya” (Said-Moorhouse, 2017). Isitoshe, viongozi wa kisiasa walijadili suala hilo katika kikao cha pamoja cha Muungano wa Afrika na Jumuiya ya Ulaya (Smith-Spark, 2017). La kushangaza ni kwamba IOM walikuwa wametahadharisha kuhusu kuwepo kwa wahamiaji waliokuwa wakinadiwa kama watumwa nchini Libya kabla ya ripoti hiyo ya CNN. Lakini ni ripoti ya kutia hofu ya CNN iliyosababisha kuchukuliwa kwa hatua kubwa ya kisiasa na wanasiasa wa Magharibi na Afrika (Völlinger, 2017).

¹² Ripoti za Al Jazeera kwa siasa, ambazo zimezaa kinachotajwa kuwa taathira ya Al Jazeera, kwa mfano katika Arab Spring ya Misri, zimetajwa kama mfano wa faida ya ziada na ambayo haikutarajiwa ya taathira ya CNN. Kwa habari zaidi, tazama Seib (2008), Zingarelli (2010), Ricchiardi (2011) miongoni mwa wengine.

Waandishi wa machapisho yaliyotolewa karibuni wanapendekeza ufasiri tofauti wa taathira ya vyombo vya habari ulimwenguni kwa siasa za kimataifa (Gilboa, 2005; Gilboa na wengine, 2016). Hata hivyo, vyombo vya habari vinaweza kuathiri watu kutokana na jinsi vinatoa habari za wahamiaji na wakimbizi. Kielelezo cha kuvutia ni picha ya Alan Shenu (ambaye mara nyingi huitwa na vyombo vya habari “Aylan Kurdi”¹³), mvulana kutoka Syria wa umri wa miaka mitatu ambaye alipatikana amekufa maji katika ufuo mmoja wa Uturuki wakati yeye na familia yake walikuwa wakijaribu kuingia Ulaya. Picha hiyo ilienea kama virusi na ikawa ishara ya hali ya wakimbizi ilivyo mbaya katika nchi za Magharibi na jinsi ulimwengu hukujali hadi kufikia wakati huo. Picha kubwa za maiti ya mvulana huyo zilichapishwa katika kurasa za mbele za magazeti na kuonyeshwa kwenye televisheni kote ulimwenguni. Data inaonyesha kwamba picha hiyo ilibadili kauli ya umma na kuufanya kuwa tayari zaidi kukaribisha wakimbizi (Sohlberg na wengine, 2018).¹⁴Uchunguzi katika nchi mbali mbali ulionyesha kwamba katika Ureno, Uingereza, Ujerumani na Italia, ripoti za kujenga za ubinadamu kuhusu wahamiaji na wakimbizi ziliongezeka mara tatu baada ya picha hiyo kuchapishwa (EJO, 2015). Slovic na wengine (2017) wanarejelea data inayoeleza “athari za wahanga mashuhuri”¹⁵. Kuhusu matokeo ya sera, Burns (2015) amepata matamshi ya viongozi wa kisiasa duniani inayoelezea masikitiko yao na akathibitisha uhusiano uliopo kati ya picha hiyo na majibu ya wanasiasa; matokeo yaliyothibitishwa pia na Vis & Goriunova (2015). Makamu wa rais wa Getty Images Hugh Pinney anaongezea pointi nyingine:

“Na madhumuni ya kuizungumzia baada ya kuchapishwa ni kwa sababu inavunja mwiko wa kijamii ambao umekuwepo katika desturi za magazeti kwa miongo mingi: picha ya mtoto mfu ni mojawapo ya kanuni msingi ya picha ambazo hufai kuchapishwa.” (Laurent, 2015)

Swali ni: Kwa nini wanahabari waliuvunja mwiko huu? Mojawapo ya maelezo huenda ikawa ni katika kujaribu kuhakikisha simulizi zao zinawashawishi wasomaji wao, watazamaji na wasikilizaji (tazama Moduli 13). Wakati ambapo hadhira inasukumiziwa picha nyingi kupindukia za merikebu zilizojaa watu kupindukia zikielekea Ulaya, au za halaiki za wahamiaji waliokwama katika nchi wanamopitia kama vile Libya, huwa wanazoea haraka picha hizo za kuogofya. Kadhalika, picha hueleza habari tofauti kabisa — si ya watu binafsi, lakini ya makundi makubwa ya wahamiaji, na hivyo kurahisisha usimulizi wa “mafuriko ya wahamiaji” Ni muhimu kutambua kwamba wahamiaji, hasa Waafrika, mara nyingi huwa hawaonyeshwi wakiwa watu binafsi (tazama Moduli4). Isitoshe, huwa huwa hawaonyeshwi wakihama kutoka eneo moja la bara hadi jingine, yaani wakati hawatoki nje ya Afrika (tazama Moduli 9). Ripoti hizo za habari zinazoonyesha upande mmoja tu wa tukio huenda zikaibua hofu katika nchi za Kaskazini dhidi ya “mafuriko

13 Inasemekana familia hiyo ilibadilisha jina ilipofika Uturuki (Elgot, 2015).

14 Ongezeko la wanaounga mkono sera huru kuhusu wakimbizi lilikuwa ni kwa muda tu na watu wakazidi kuiona picha hiyo kwa mtazamo wa kiitikadi mwezi mmoja baada ya kifo cha Alan (Sohlberg na wengine, 2018).

15 “Picha ya mtu binafsi mmoja anayetambulishwa iliwavuta watu wengi na kuwasukuma kuanza kujali na kutoa misaada kwa njia ambayo msukumo wake haukuwa takwimu za maafa ya mamia ya maelfu” (Slovic na wengine, 2017).

ya wahamiaji” kuingia Ulaya — kama takwimu zilizorejelewa katika mwanzo wa moduli zinavyoonyesha kwa kiasi fulani.



ZOEZI LILILOPENDEKEZWA LA KUSHUGHULIKIA STADI ZA UTAMBUZI ZA UTEKELEZAJI NA UCHANGANUZI:

Wasilisha taathira ya CNN, athari ya mtu binafsi na nafasi yake katika masuala kuhusu uhamiaji na wakimbizi na utumie mojawapo ya video kuanzisha mjadala:

- Filamu ya Vpro inayoonyesha hali halisi ya picha ya Alan Shenu: <https://www.youtube.com/watch?v=VcliHwsf8jl>
- Ripoti ya CNN kuhusu wakimbizi nchini Libya: <https://edition.cnn.com/2017/11/14/africa/libya-migrant-auctions/index.html>

Kuna mifano gani mingine ya taathira ya CNN au athari ya mtu binafsi kwa ripoti kuhusu wahamiaji na wakimbizi?

Kushughulikia stadi za utambuzi za kutathmini, wapatie washirika nafasi wajiamulie wenyewe kiwango na athari kwa maadili zinazoweza kusababishwa na ripoti zilizobuni taathira hii ya vyombo vya habari wakitegemea kiwango chao cha kutaalamika kuhusu taathira za vyombo vya habari.

Picha za merikebu zilizojaa wahamiaji au wakimbizi ama makundi makubwa ya watu wakiwasili katika fuo za Ulaya zimekuwa mashuhuri katika mjadala wa sasa kuhusu uhamiaji (McAuliffe & Kitimbo, 2018). Ndiposa picha moja ya maiti ya mtoto huenda ikahakikisha kushughulikiwa zaidi na kwa njia tofauti. Kwa jumla, ripoti za watu binafsi zinaweza kushawishi hadhira (Brosius & Bathelt, 1994; Fast na wengine, 2014; Zillmann & Brosius, 2010). Kuchapisha na kuonyesha picha ya Alan Shenu katika vyombo vya habari ni mfano wa kuvutia.

Mfano mwingine ni ripoti ya Óscar Alberto Martínez Ramírez, aliyekufa pamoja na bintiye wa umri wa miaka miwili, Valeria, wakijaribu kuvuka mpaka kutoka Mexico kuingia Marekani (tazama Moduli 11).

Changamoto za kitaalamu

Wanahabari wanaoripoti kuhusu wakimbizi na wahamiaji hawako peke yao miongoni mwa walio katika taaluma ya uanahabari wanaokabiliwa na changamoto nyingi za kitaalamu. Changamoto hizo ni pamoja na uhaba wa nyenzo (kwa mfano wasaa, fedha, wafanya kazi, maarifa na elimu), vyanzo vyenye ajenda iliyofichwa, mitandao ya jamii, udhibiti wa wenye mamlaka na kutokuwa na uhuru wa vyombo vya habari. Ni jambo la kawaida kupata changamoto kadha zinakusanyika kwa kisa kimoja. Bila shaka, hilo hubainika katika ripoti kuhusu masuala ya uhamiaji na wakimbizi

Dusan Mladjenovic, mwanahabari wa televisheni katika Serbia na mtangazaji wa habari za uhamiaji, anatoa mifano kutoka kusini mwa Ulaya:



Chanzo : Binafsi

“Kwa miaka mingi, wanahabari wamekumbana na matatizo mengi wakiripoti kuhusu suala la uhamiaji. Mara nyingi wanahabari huzuiliwa kuingia katika vituo ya uhamiaji na huruhusiwa kuingia tu katika vituo teule (vinavyowapatia wahamiaji maisha ya hali ya juu). Pana pia suala la maafisa katika kanda (Croatia, Hungary na Serbia) kutoa majibu finyu au kukataa kujibu baadhi ya maswali kuhusu hali na utendewaji wa wahamiaji. Mara nyingi wahamiaji hutumiwa kwa mada za kila siku za kisiasa. [...] Masuala huwa ni kwa manufaa ya uongozi wa wazalendo katika nchi zote mbili.”



ZOEZI LILIOPENDEKEZWA KWA DARASA LA KUSHUGHULIKIA STADI ZA UTAMBUZI ZA UCHANGANUZI:

Waombe washiriki kuwazia changamoto wanazokabiliana nazo wanahabari wakitafuta habari za wahamiaji na wakimbizi (1) na jinsi zinahusiana na hali katika nchi zao (2).

1. Endesha zoezi la kupanga mikakati. Mnapofanya hivyo, washiriki wanapaswa kuwazia changamoto ambazo wanahabari hukabiliana nazo wakitafuta habari za wahamiaji na wakimbizi. Kwa kuzingatia muktadha wa kitaifa (taratibu za vyombo vya habari, mifano ya uanahabari ya kuigwa, desturi na mengineyo) washiriki watambulishe changamoto za kitaalamu kwa muktadha wao mahsusi wa uanahabari.
2. Ikague hali iliyopo katika nchi utakayoichagua: Nyenzo za wanahabari zikoje? Hali ikoje kuhusiana na uhuru wa kutoa habari, uthibiti wa wenye mamlaka kwa utoaji habari, sheria za vyombo vya habari na ufiada? Kwa mfano, mitandao ya kijamii ina jukumu gani katika utoaji habari katika nchi hiyo?

Uhaba wa vitendea kazi

Vitendea kazi ni muhimu na vinahitaji kupewa kipaumbele. Tayari mwaka 2015 iliripotiwa kwamba:

“Vyumba vya habari havina wanahabari baada ya kushuhudia kufukuzwa kazi kwa wanahabari wengi katika hatua kubwa za kubana matumizi katika miaka ya karibuni, na magazeti hayawezi tena kuendesha shughuli za kila siku za kuripoti kama ilivyo-kuwa miaka kadhaa iliyopita. Pana wanahabari wachache wataalamu na bila shaka hakuna yeyote miongoni mwao aliyetaalamika kwa suala la uhamiaji, hata kama limekuwa suala kuu la kisiasa na kiuchumi.” (White, 2015, uk. 96)

Kote duniani, vyombo vya habari vinanywea na idadi inayozidi kupungua ya wanahabari inapambana na hali ngumu ya kazi katika mazingira ya uenezaji habari kidijitali yaliyo na ushindani

mkubwa (Cision, 2019; Hanitzsch na wengine, 2019). Kama gazeti la Uingereza la The Guardian lilivyochapisha kuhusu mazingira ya vyombo vya habari Afrika: “Uhaba wa fedha na stadi zimewaacha wanahabari barani waking’ang’ana na vyombo vikubwa vya habari vya Magharibi” (Allison, 2013). Mara nyingi, wanahabari Waafrika hukosa elimu na nyenzo za kuwawezesha kufanya utafiti wao. Mwandishi mmoja anakadiria kwamba kuna “ongezeko la idadi ya mafunzo ya uanahabari na mawasiliano yanayotolewa na vyuo vya umma na binafsi [...], lakini kiwango cha kazi yao bado ni pungufu” (Manda, 2018, uk. 35). Wanahabari wanakabiliwa pia na uhaba wa mashirika ya kitaalamu ya habari (ya Kiafrika) ya kuwawezesha kufikia kwa urahisi habari za kimataifa zenye mtazamo wa Kiafrika. Kutokana na udhaifu wake wa kiuchumi, ni nadra kwa vyumba vya habari Afrika kuwa na wanahabari katika nchi jirani na hivyo basi hutegemea ripoti za habari kutoka kwa mashirika ya dunia ya habari — ambayo pia yana wanahabari wachache sana katika Afrika (Mükke, 2009; Sturmer, 2013; Wittmann, 2006). Magazeti mengi barani Afrika hutegemea mashirika ya habari kama vile Reuters, the Associated Press (AP), Agence France Presse na BBC, pamoja na Al-Jazeera; utegemeaji wa mashirika ya kutoka China unazidi kuongezeka. Katika uwanda wa utoaji habari za uhamiaji, matokeo mbalimbali ya hali hiyo ni pamoja na kuenezwa kwa habari zisizo na uasili na kupuuzwa kwa mada nzima au vipengele (tazama Moduli 10).

Isitoshe, wanahabari na vyombo vya habari — karibu kote duniani — wanakumbwa na tatizo la fedha. Hali hiyo pia inaweza kuleta changamoto katika kuripoti kuhusu wahamiaji na wakimbizi. Kwa upande mmoja, ni nadra sana kwa wahamiaji kuwa sehemu ya hadhira inayoshughulikiwa (tazama Moduli 13), na kwa upande mwingine, huenda vyombo vya habari visipate haja ya kutenga pesa na rasilimali kuripoti kuwahuu. Moduli 4 imeshaonyesha ni mada fulani pekee kuhusu wahamiaji na wakimbizi zinazovuta macho ya vyombo vya habari. Kwa mfano, zikitokea fujo kutokana na chuki kwa wageni, vyombo vya habari hutoa ripoti nyingi na zinazoeleza kila kitu kwa ukamilifu; vinginevyo, wahamiaji huonekana katika ripoti za uhalifu, au hata hawaoonekani kamwe katika vyombo vya habari (White, 2015). Utafiti wa gharama ya juu wa suala — ambalo linaweza pitwa kwa urahisi na ripoti za gazeti kuhusu majanga yanayofuatiwa na mfululizo wa habari nyingi za kuripotiwa — ni wazo ambalo halifikiriwi katika bajeti za vyombo vingi vya habari. Hata hivyo, kuna hali maalumu, utafiti changamani na majukwaa ya kidijitali yanayofanikisha mfumo mtandao — baadhi ya mifano yake (taratibu bora) inapatikana katika Moduli 10-13. Hata hivyo, hali ya fedha ingali kishawishi muhimu na pia changamoto. Pana pia suala la umilikaji wa vyombo vya habari na mengine ambayo wenyewe wanamiliki.

Kwa jumla, uhaba wa nyenzo ni changamoto iliyo muhimu hasa katika masuala changamani kama vile uhamiaji na uhamishwaji wa lazima. Kadiri mada ilivyo tatanishi, ndivyo wanahabari wanahitajika kuleta maarifa na ndivyo wasaa, pesa, rasilimali, wafanyikazi na elimu zinahitajika. Rasilimali hizo zikikosekana, changamoto kubwa sana hutokea. Ina maana kwamba kuiangazia Afrika katika ukusanyaji na utoaji wa habari kuhusu wahamiaji na wakimbizi ni shughuli ambayo mara nyingi huwa haina kina (Allison, 2013). Lakini kwingineko duniani pia, ni nadra sana kupata makala kuhusu mada hiyo ambazo zina uasili kamili, zimefanyiwa utafiti wa kina na zinaangazia vipengele vyote (tazama Moduli 4).

Upendeleo na mawazo potovu yasiyo na uasili

Lidadi ndogo ya mashirika ya habari ya Kiafrika na wanahabari nyanjani walio nje ya nchi zao (kutoka mataifa ya Afrika na Ulaya wanaoripoti Afrika), na uhaba wa maarifa ya ukweli kuhusu nchi za Afrika ni mambo yawezayo kusababisha kuchaguliwa na kutumiwa kwa taarifa zenye mawazo potovu yasiyo na uasili (Hafez, 2005; Mücke, 2009; Sturmer, 2013). Na hasa zinapotolewa habari kuhusu wahamiaji na wakimbizi, ni muhimu kuepuka kuripoti dhana potovu zisizo na uasili (tazama Moduli 10). Wanahabari wanafaa kukumbuka kwamba wahamiaji kwa kawaida huwa ni kundi la watu tofauti, na wanaoainishwa katika makundi mengine madogo (wanawake, watoto na hasa wasioandamana na watu wazima, walemavu, LGBTI na wengineo). Ukweli kwamba huenda wanahabari katika vyumba vya habari wana asili mbali mbali za kitamaduni na wengine huenda hata wakawa wahamiaji ni mambo yawezayo kuhimiza kutolewa kwa ripoti tofauti tofauti zenye mawazo potovu machache.

Kadhalika, taarifa za habari kutoka nchi za Kaskazini huenda zikawa na upendeleo unaojitokeza kwa mbali au hata dhahiri (Bailey, 2018). Upendeleo huo huenda ukapashwa hadhira za Kiafrika bila kuchujwa. Kutegemea vyanzo vya habari kutoka miktadha mingine ya kisiasa na njia za mawasiliano huzidisha hatari ya vyumba vya habari vya Kiafrika kupuuza mitazamo yao, ya kanda, kitaifa na hata ya bara ambayo ni miundo muhimu ya kuwezesha ufahamu kamili wa umuhimu na taathira za uhamiaji kutoka nchi moja ya Afrika hadi nyingine (tazama Moduli 9).

Changamoto nyingine ya kitaalamu inayohusiana na hayo — mbali na uhaba wa stadi na maarifa, elimu na mafunzo kwa wanahabari — ni ukosefu wa mitandao ya ndani katika Afrika ya kuwaunganisha wanahabari na wenzao katika nchi majirani. (Zappe, 2015). Matokeo ya uhaba wa rasilimali si tatizo kwa Afrika pekee, jinsi wanahabari wake wanaripoti na hata ripoti wana-zotoa. Mambo yanaweza kuwa hayo hayo kwenye maeneo mengine ya ulimwengu yaliyo katika hali sawa.

Uhuru wa uanahabari na vyanzo vilivyo na ushawishi wa hoja kwa umma

Iwapo viwango vya kitaalamu na maadili vya uanahabari katika nchi vimeshuka, ama wanahabari hukosa nafasi ya kufanya kazi yao wakitegemea utafiti wa kina, vyombo vya habari huwa havistahili tena kuaminika. Miundo ya vyombo vya habari ndani ya nchi, mifumo ya vyombo vya habari na hali za kisiasa ni mambo yanayotekeleza wajibu mkubwa kwa kazi ya uanahabari katika muktadha huu. Kiwango cha uhuru wa vyombo vya habari katika nchi — ambacho kipimo chake ni “wingi, uhuru wa vyombo vya habari, aina na ubora wa miundo ya kisheria, na usalama wa wanahabari” (Reporters Without Borders, 2019) – huenda kikaathiri pakubwa uhuru wa wanahabari kufuatilia ripoti zinazoangazia wahamiaji na wakimbizi (Cottle na wengine, 2016). Mashirika na vyama kama vile Transparency International (Transparency International, n. d.), Reporters without Borders (Reporters Without Borders, n. d.), Freedom House (Freedom House, n. d.) na wengineo hutaarifu kuhusu hali ya uanahabari kote duniani.

Kadhalika, wanahabari wanapaswa kufahamu kwamba huenda wanaowapatia habari wakawa na njama fulani au wanatafuta kujinufaisha wenyewe. Kutokana na kuongezeka kwa utumiaji wa mitandao ya jamii, “mipaka bayana iliyokuwepo kati ya uanahabari huru, uhusiano mwema na matangazo ya biashara, na ukereketwa au propaganda imeingia ukungu huku washiriki wapya wa mashirika binafsi ya biashara na serikali wakijitosa katika ulingo ambao awali ulichukuliwa kuwa wa wanahabari” (Wahl- Jorgensen na wengine, 2016, uk. 810). Mazingira ya mbinu mpya za mawasiliano yanahatarisha jukumu la wanahabari kama “wanahistoria wa nyakati za sasa” (Feinstein na wengine, 2018, uk. 1).

Matukio hayo — mchanganyiko wa uhaba wa rasilimali, nguvu za mitandao ya jamii na ushawishi wa hoja kwa utoaji habari wa wahusika wa mashirika binafsi ya biashara na serikali — yanaweza kuwa hatari. Hili ni muhimu hasa kwa mada nyeti na zinazozua ubishani, kama zilivyoonyesha takwimu kuhusu mitazamo ya watu katika mwanzo wa moduli hii. Hii hapa mifano inayohusiana na utoaji wa habari kuhusu uhamiaji na ukimbizi:

- Gazeti la Uingereza la *The Guardian* liliwahoji waajiriwa kadhaa wa shirika la televisheni la serikali ya Hungary ambao wanaamini kwamba taarifa za kupinga wahamiaji katika ripoti za shirika hilo hutolewa moja kwa moja na maafisa wa serikali. (Noland & Walker, 2018).
- Kwenye utafiti katika mataifa ya Ulaya, wanahabari kadhaa Waitaliano ambao huandika habari za uhamiaji “walidhihirisha kwamba kuna kiwango kikubwa cha maagizo kutoka kwa wasimamizi wao — kiasi cha kuonekana kama kwamba kazi yao inaingiliwa kindani na mawakala (wa wamiliki wa vyombo vya habari) na kutoka nje (kama vile kutoka kwa vyama vya kisiasa, Kanisa Katoliki, mashirika ya biashara na vyama vya wafanya kazi). Hali hii huenda ikaathiri uhuru wao katika kuamua ni habari gani watatoa na zenye muundo gani” (Karstens na wengine, 2018, uk. 40).
- Watu kutoka The Gambia huvuka Jangwa la Sahara na kuingia Libya, kisha wanasafiri kwa merikebu hadi Ulaya. Wengi hupoteza maisha yao safarini. Lakini mnamo 2015, ripoti za habari za idadi kubwa ya wahamiaji zilikuwa chache na ilikuwa ni nadra kupata habari kuhusu dhiki na taabu wanazopata. “Kuthibitiwa kwa vyombo vya habari wa walio mamlakani au uhaba wa rasilimali — ama mchanganyiko wa yote mawili — ndizo sababu kuu za habari chache za uhamiaji. Pana pia tatizo la wanahabari kujihadhari na wanayoripoti wasije wakaudhi mwajiri wao au serikali” (White, 2015, uk. 6).
- Mnamo Februari 2019, Uganda ilikuwa imewahifadhi wakimbizi zaidi ya milioni 1.2, idadi ambayo wakati huo ilikuwa kubwa zaidi katika historia ya nchi hiyo (UNHCR, 2019). Ingawa Uganda ni mojawapo ya nchi mwenyeji wa wakimbizi wengi duniani, hili huwa halijitokezi kwenye taarifa za habari. Badala yake, “vyombo vya habari ulimwenguni havikuripoti vya kutosha hali iliyopo Uganda ikilinganishwa na ripoti za wahamiaji wakipitia Bahari ya Mediterranean” (Media Challenge Expo, 2018, uk. 8). Inachukuliwa kwamba sababu za ukosefu

wa ripoti za kutosha ni uhaba wa rasilimali za kuhakikisha habari za wakimbizi zinaripotiwa kutoka ndani ya Uganda na kuwekwa katika ajenda ya habari ulimwenguni, na mara nyingi wanahabari wenye mafunzo duni hulazimika kukabiliana na shinikizo za kisiasa uyumbishwaji (Media Challenge Expo, 2018).

- Katika Afrika, vyombo vya habari huakisi sana watu wanaong'ang'ana kuhama barani. Lakini kuna wengi wanaohamia Afrika Kusini, hali ambayo inakuwa ni changamoto kwa vyombo vya habari vya Afrika Kusini (tazama Moduli 9).

Ni muhimu kuzifahamu changamoto hizo na kujua jinsi ya kukabiliana nazo. Moduli 10 hadi 13 zinatoa mapendekezo kuhusu jinsi ya kukabiliana na changamoto hizo.



KAZI YA ZIADA ILIYOPENDEKEZWA YA KUSHUGHULIKIA STADI ZA UTAMBUZI ZA ZA KUCHANGANUA NA KUTATHMINI (A) PAMOJA NA STADI ZA MITAZAMO YA KIBINAFSI NA MAADILI ZA KUJIBU (B)

(A) Washiriki wachague nchi ya kigeni ama wapewe chombo cha habari wasichokijua katika nchi ya kigeni, waombwe wahusishe changamoto za wanahabari hapo na asili zake (uhuru wa vyombo vya habari, hali ya kifedha ya vyombo hivyo vya habari ...). Miundo yake ya kimsingi ina uhusiano gani na changamoto ambazo wanahabari hukabiliana nazo? Washiriki wapewe nafasi ya kutafuta ripoti katika vyombo vya habari kudhihirisha changamoto hizo. Waombwe kutafakari athari za kimaadili zinazoweza kuwepo.

(B) Wakubaliwe kushirikisha pia taathira za vyombo vya habari katika kuripoti kuhusu wahamiaji na wakimbizi kama changamoto ambazo wanahabari hukabiliana nazo. Waombe wjadili katika maandishi mafupi mahusiano ya taathira za “vyombo vya habari”, “changamoto za kitaalamu” na “kiini hasa” wakitumia mfano wa nchi waliyochagua.



USOMAJI WA ZIADA:

Kiakademia:

Hanitzsch, T., Hanusch, F., Ramaprasad, J., & de Beer, A. S. (2019). *Worlds of journalism*. New York: Columbia University Press.

Kiuanahabari:

Laurent, O. (2015, September 4). What the image of Aylan Kurdi says about the power of photography. *Time Magazine*. Retrieved March 29, 2019, from <https://time.com/4022765/aylan-kurdi-photo/>

Kitaasisi:

Esipova, N., Ray, J., Pugliese, A., & Tsabutashvili, D. (2015). How the world views migration? IOM. Retrieved November 30, 2020, from https://publications.iom.int/system/files/how_the_world_gallup.pdf

Marejeleo

Allison, S. (2013, March 1). African journalism is being stifled by a lack of resources: A shortage of money and skills leaves local reporters struggling to compete with big western media outlets. *The Guardian*. Retrieved March 27, 2019, from <https://www.theguardian.com/world/2013/mar/01/african-journalism-stifled-lack-resources>

Arendt, F. (2013). Dose-dependent media priming effects of stereotypic newspaper articles on implicit and explicit stereotypes. *Journal of Communication*, 63(5), 830-851. <https://doi.org/10.1111/jcom.12056>

Austria far right: Freedom party wins key posts in new government. (2017, December 16). *BBC*. Retrieved April 6, 2020, from <https://www.bbc.com/news/world-europe-42379985>

Bahador, B. (2017, April 10). Did pictures in the news media just change U.S. policy in Syria? *The Washington Post*. Retrieved March 28, 2019, from https://www.washingtonpost.com/gdpr-consent/?next_url=https%3a%2f%2fwww.washingtonpost.com%2fnews%2fmonkey-cage%2fwp%2f2017%2f04%2f10%2fdid-media-images-just-change-u-s-policy-in-syria-three-lessons-from-kosovo%2f%3fnoredirect%3don%26utm_term%3d.69c9a2166a38&noredirect=on

Bailey, I. J. (2018, November 13). How implicit bias works in journalism. *Nieman Reports*. Retrieved March 27, 2019, from <https://niemanreports.org/articles/how-implicit-bias-works-in-journalism/>

Bash, D., Herb, J., Starr, B., & Diamond, J. (2017, April 2017). Trump on Syria's Assad: "Something should happen". *CNN*. Retrieved March 20, 2019, from <https://edition.cnn.com/2017/04/06/politics/donald-trump-syria-options/index.html>

Bos, L., Lecheler, S., Mewafi, M., & Vliegenthart, R. (2016). It's the frame that matters: Immigrant integration and media framing effects in the Netherlands. *International Journal of Intercultural Relations*, 55, 97-108. <https://doi.org/10.1016/j.ijintrel.2016.10.002>

Brosius, H.-B., & Barthelt, A. (1994). The utility of exemplars in persuasive communications. *Communication Research*, 21(1), 48-78. <https://doi.org/10.1177/009365094021001004>

- Burns, A. (2015). Discussion and action: Political and personal responses to the Aylan Kurdi images. In Vis, F. & Goriunova, O. (Eds.). *The iconic image on social media: a rapid research response to the Death of Aylan Kurdi*. Sheffield: Visual Social Media Lab. Retrieved January 5, 2020, from [http://research.gold.ac.uk/14624/1/KURDI%20 REPORT.pdf](http://research.gold.ac.uk/14624/1/KURDI%20REPORT.pdf)
- Cision (2019). Cision's State of the Media report 2019. Retrieved November 29, 2019, from <https://www.cisionjobs.co.uk/article/cision-s-state-of-the-media-report-2019/>
- Cohen, B. C. (1963). *The Press and foreign policy*. Princeton, N.J.: Princeton University Press.
- Connor, P., & Krogstad, J. M. (2018). Many worldwide oppose more migration – both into and out of their countries. Retrieved November 19, 2019, from <https://www.pewresearch.org/fact-tank/2018/12/10/many-world-wide-oppose-more-migration-both-into-and-out-of-their-countries/>
- Cottle, S., Sambrook, R., & Mosdell, N. (2016). *Reporting dangerously: Journalist killings, intimidation and security*. New York, NY: Palgrave Macmillan.
- Decker, F. (2020, October 26). Wahlergebnisse und Wählerschaft der AfD. BpB. Retrieved March 20, 2019, from <http://www.bpb.de/politik/grundfragen/parteien-in-deutschland/afd/273131/wahlergebnisse-und-waehlerschaft>
- Dobbert, S. (2018, March 5). Sieg der Populisten. Zeit Online. Retrieved March 27, 2018, from <https://www.zeit.de/politik/ausland/2018-03/italien-wahl-fuenf-sterne-bewegung-populisten-wahlentscheidung>
- Doucet, L. (2018). Syria & the CNN effect: What role does the media play in policy-making? *Daedalus*, 147(1), 141-157. https://doi.org/10.1162/DAED_a_00480
- EJO (2015, November 9). Wie Zeitungen aus West- und Osteuropa über die Flüchtlingskrise berichteten. EJO. Retrieved July 3, 2017, from <https://de.ejo-online.eu/forschung/wie-zeitungen-in-europa-ueber-die-fluechtlingskrise-berichteten>
- Electoral Commission of South Africa (2019). 2019 National and provincial elections. Electoral Commission of South Africa. Retrieved November 23, 2019, from <https://www.elections.org.za/NPEDashboard/app/dashboard.html>
- Elgot, J. (2015). Father of drowned boy Aylan Kurdi plans to return to Syria. *The Guardian*. Retrieved April 9, 2020, from <https://www.theguardian.com/world/2015/sep/03/father-drowned-boy-aylan-kurdi-return-syria>
- Entman, R. M. (1993). Framing: Toward clarification of a fractured paradigm. *Journal of Communication*, 43(4), 51-58. <https://doi.org/10.1111/j.1460-2466.1993.tb01304.x>
- Esipova, N., Ray, J., Pugliese, A., & Tsubutashvili, D. (2015). How the world views migration? IOM. Retrieved November 30, 2020, from https://publications.iom.int/system/files/how_the_world_gallup.pdf
- Esses, V. M., Dovidio, J. F., Jackson, L. M., & Armstrong, T. L. (2001). The immigration dilemma: The role of perceived group competition, ethnic prejudice, and national identity. *Journal of Social Issues*, 57(3), 389-412. <https://doi.org/10.1111/0022-4537.00220>
- Esses, V. M., Wagner, U., Wolf, C., Preiser, M., & Wilbur, C. J. (2006). Perceptions of national identity and attitudes toward immigrants and immigration in Canada and Germany. *International Journal of Intercultural Relations*, 30(6), 653-669. <https://doi.org/10.1016/j.ijintrel.2006.07.002>
- Europäisches Parlament (2019, July 2). Ergebnisse der Europawahl 2019. Europäisches Parlament. Retrieved November 19, 2019, from <https://europawahlergebnis.eu/wahlergebnisse/2019-2024/>
- Europe and right-wing nationalism: A country-by-country guide. (2019, November 13). BBC. Retrieved November 19, 2019, from <https://www.bbc.com/news/world-europe-36130006>
- European Commission (2016, December 22). Autumn 2016 Standard Eurobarometer: Immigration and terrorism continue to be seen as the most important issues facing the EU. European Commission. Retrieved November 24, 2020, from http://europa.eu/rapid/press-release_IP-16-4493_en.htm

- European Migration Network. (2018). Asylum and migration. Glossary 6.0: A tool for better comparability produced by the European Migration Network. Retrieved December 15, 2020, from https://www.emn.at/wp-content/uploads/2018/06/emn-glossary-6-0_en.pdf
- Evans, G., & Mellon, J. (2019). Immigration, euroscepticism, and the rise and fall of UKIP. *Party Politics*, 25(1), 76-87. <https://doi.org/10.1177/1354068818816969>
- Fast, V., Müller, P., & Scherr, S. (2014). Der kombinierte Einsatz von Daten und Fallbeispielen in den Medien: Wirkung und Glaubwürdigkeit. In Loosen, W. & Dohle, M. (Eds.), *Journalismus und (sein) Publikum: Schnittstellen zwischen Journalismusforschung und Rezeptions- und Wirkungsforschung* (pp. 317-334). Wiesbaden: Springer VS.
- Feinstein, A., Pavisian, B., & Storm, H. (2018). Journalists covering the refugee and migration crisis are affected by moral injury not PTSD. *Journal of the Royal Society of Medicine Open*, 9(3), 1-7. <https://doi.org/10.1177/2054270418759010>
- Freedom House (n. d.). Publication Archives. Retrieved November 25, 2020, from <https://freedomhouse.org/reports/publication-archives>
- Gilboa, E. (2005). The CNN effect: The search for a communication theory of international relations. *Political Communication*, 22(1), 27-44. <https://doi.org/10.1080/10584600590908429>
- Gilboa, E., Jumbert, M. G., Miklian, J., & Robinson, P. (2016). Moving media and conflict studies beyond the CNN effect. *Review of International Studies*, 42(4), 654-672. <https://doi.org/10.1017/S026021051600005X>
- Goedeke Tort, M. N., Guenther, L., & Ruhrmann, G. (2016). Von kriminell bis willkommen. Wie die Herkunft über das mediale Framing von Einwanderern entscheidet. *Medien & Kommunikationswissenschaft*, 64(4), 497-517. <https://doi.org/10.5771/1615-634X-2016-4-497>
- Goriunova, O., & Vis, F. (2015). The iconic image on social media: a rapid research response to the death of Aylan Kurdi. Sheffield, United Kingdom: Visual Social Media Lab. Retrieved January 5, 2020, from <http://research.gold.ac.uk/14624/1/KURDI%20REPORT.pdf>
- Hafez, K. (2005). *Mythos Globalisierung: Warum die Medien nicht grenzenlos sind*. Wiesbaden: Springer VS.
- Hanewinkel, V. (2017, November 11). Wie stehen die deutschen Parteien zu den Themen Migration, Integration, Flucht und Asyl? Ein Blick in die Programme zur Bundestagswahl 2017. BpB. Retrieved March 27, 2019, from <http://www.bpb.de/gesellschaft/migration/laenderprofile/255670/parteien-zu-migration-integration-flucht-und-asyl>
- Hanitzsch, T., Hanusch, F., Ramaprasad, J., & de Beer, A. S. (2019). *Worlds of journalism*. New York: Columbia University Press.
- Howard, E. (2014, July 9). Six real life stories of migration. *The Guardian*. Retrieved December 17, 2019, from <https://www.theguardian.com/uk-news/2014/jul/09/six-real-life-stories-of-migration>
- IOM (2019). Glossary on Migration. International Organization for Migration Retrieved August 5, 2019 from https://publications.iom.int/system/files/pdf/iml_34_glossary.pdf
- Italian elections 2018 – full results. (2018, March 5). *The Guardian*. Retrieved November 19, 2019, from <https://www.theguardian.com/world/ng-interactive/2018/mar/05/italian-elections-2018-full-results-renzi-berlusconi>
- Iyengar, S., Kinder, D. R., Peters, M. D., & Krosnick, J. A. (1984). The evening news and presidential evaluations. *Journal of Personality and Social Psychology*, 46(4), 778-787. <https://doi.org/10.1037/0022-3514.46.4.778>
- Karstens, E., Kuznik, B., & McNeil, R. (2018). Media practices related to migration and intra-EU mobility in the EU-15 Member States: Working paper. Retrieved December 17, 2019, from https://www.reminder-project.eu/wp-content/uploads/2018/05/with-cover_D11.1.pdf

- Laurent, O. (2015, September 4). What the image of Aylan Kurdi says about the power of photography. *Time Magazine*. Retrieved March 29, 2019, from <https://time.com/4022765/aylan-kurdi-photo/>
- Lawlor, A. (2015). Framing immigration in the Canadian and British news media. *Canadian Journal of Political Science*, 48(2), 329–355. <https://doi.org/10.1017/S0008423915000499>
- Manda, L. Z. (2018). Journalism education and training in Malawi: A case for a national policy. *Journal of Development and Communication Studies*, 5(2), 35-53. <https://doi.org/10.4314/jdcs.v5i2.3>
- McAuliffe, M., & Kitimbo, A. (2018). Africa migration: What the numbers really tell us. *World Economic Forum*. Retrieved March 30, 2019, from <https://www.weforum.org/agenda/2018/06/heres-the-truth-about-african-migration/>
- McCombs, M. E., & Shaw, D. L. (1972). The Agenda-Setting function of mass media. *Public Opinion Quarterly*, 36(2), 176-187. <https://doi.org/10.1086/267990>
- McDonald, D. A., & Jacobs, S. (2005). (Re)writing xenophobia: Understanding press coverage of cross-border migration in Southern Africa. *Journal of Contemporary African Studies*, 23(3), 295-325. <https://doi.org/10.1080/02589000500274050>
- Media Challenge Expo 2018. (2018). Refugee Reporting Edition. Media Challenge Initiative. Retrieved November 25, 2020, from <https://mciug.org/media-challenge-expo2018/>
- Medianu, S. (2014). The role of the media in the automatic dehumanization of refugees. (Publication No. 2287) [Thesis, The University of Western Ontario, Canada]. Western Libraries.
- Meltzer, C. E., Eberl, J.-M., Theorin, N., Lind, F., Schemer, C., Boomgaarden, H. G., Strömbäck, J., & Heidenreich, T. (2018). Perceptions of the impact of immigration and attitudes towards free movement within the EU: A cross-national study (Rev. ed.). Role of European mobility and its impacts in narratives, debates and EU reforms. Retrieved November 30, 2020, from https://www.reminder-project.eu/wp-content/uploads/2018/04/with-cover_D9.2.pdf
- Merten, M., & Dohle, M. (2019). Wie beurteilen unterschiedliche Meinungslager die Medienberichterstattung zur „Flüchtlingskrise“? Ergebnisse einer Untersuchung zu Hostile-Media-Wahrnehmungen. *Studies in Communication and Media*, 8(2), 272-285. <https://doi.org/10.5771/2192-4007-2019-2-272>
- Migration Data Portal (2020). Migration. Data statistics. [Data set] Migration Data Portal. Retrieved November 30, 2020, from <https://migrationdataportal.org/data>
- Mükke, L. (2009). *Journalisten der Finsternis: Akteure, Strukturen und Potenziale deutscher Afrika-Berichterstattung*. Köln: Halem.
- Noland, D., & Walker, S. (2018, April 13). Hungarian journalists admit role in forging anti-migrant “atmosphere of fear”. *The Guardian*. Retrieved November 29, 2019, from <https://www.theguardian.com/world/2018/apr/13/hungary-journalists-state-tv-network-migrants-viktor-orban-government>
- Onyebadi, U. (2012). Newspaper agendas and public opinion in the 2007 Kenyan presidential election. *Ecquid Novi: African Journalism Studies*, 33(2), 36-53. <https://doi.org/10.1080/02560054.2012.711764>
- People for sale: Exposing migrant slave auctions in Libya. (n. d.). *CNN*. Retrieved March 29, 2019, from <https://edition.cnn.com/specials/africa/libya-slave-auctions>
- Perry, S. D., & Gonzenbach, W. J. (1997). Effects of news exemplification extended: Considerations of controversiality and perceived future opinion. *Journal of Broadcasting & Electronic Media*, 41(2), 229-244. <https://doi.org/10.1080/08838159709364403>
- Poushter, J. (2016, September 16). European opinions of the refugee crisis in 5 charts. *Pew Research Center*. Retrieved April 4, 2020, from <https://www.pewresearch.org/fact-tank/2016/09/16/european-opinions-of-the-refugee-crisis-in-5-charts/>

- Pürer, H. (2003). *Publizistik- und Kommunikationswissenschaft: Ein Handbuch*. Konstanz: UVK.
- Reporters Without Borders (n. d.). Reporters Without Borders. Retrieved November 25, 2020, from <https://rsf.org/en>
- Reporters Without Borders (2019). 2019 RSF Index: Big changes for press freedom in sub-Saharan Africa. Retrieved November 29, 2019, from <https://rsf.org/en/2019-rsf-index-big-changes-press-freedom-sub-saharan-africa>
- Ricchiardi, S. (2011). The Al Jazeera effect. Retrieved May 3, 2020, from <https://ajrarchive.org/article.asp?id=5077&id=5077>
- Rinke, T. (2019). Migration narratives in Europe: Through conversations on public social media. A Bakamo Public Project for the Friedrich Ebert Stiftung. Retrieved November 30, 2020, from <http://library.fes.de/pdf-files/bueros/budapest/15374-20190510.pdf>
- Robinson, P. (2002). *The CNN effect: The myth of news, foreign policy and intervention*. London, New York: Routledge.
- Said-Moorhouse, L. (2017, November 24). Rwanda offers refuge to “migrants held captive in Libya”. CNN. Retrieved March 29, 2019, from <https://edition.cnn.com/2017/11/24/africa/rwanda-reaction-libya/index.html>
- Schemer, C. (2014). Media effects on racial attitudes: Evidence from a three-wave panel survey in a political campaign. *International Journal of Public Opinion Research*, 26(4), 531-542. <https://doi.org/10.1093/ijpor/edt041>
- Seib, P. (2008). *The Al Jazeera effect: How the new global media are reshaping world politics*. Washington D.C.: Potomac Books.
- Sguazzin, A. (2019, April 24). Trump-like immigrant attacks adopted by S. Africa opposition. Bloomberg. Retrieved November 30, 2020, from <https://www.bloomberg.com/news/articles/2019-04-24/trump-style-immigrant-bashing-clouds-south-african-election>
- Slovic, P., Västfjäll, D., Eerlandsson, A., & Gregory, R. (2017). Iconic photographs and the ebb and flow of empathic response to humanitarian disasters. *Proceedings of the National Academy of Sciences of the United States of America*, 114(4), 640-644. <https://doi.org/10.1073/pnas.1613977114>
- Smith-Spark, L. (2017, November 29). Slavery, security on agenda as Merkel and Macron meet African leaders. CNN. Retrieved November 28, 2019, from <https://edition.cnn.com/2017/11/29/africa/au-eu-summit-ivory-coast/index.html>
- Sogelola, D. (2018). Brexit, agenda setting and framing of immigration in the media: the case of the Daily Mail. *LSE Undergraduate Political Review*, 1, pp. 128-142. doi: 10.21953/lse.btysqags6o6g
- Sohlberg, J., Esaiasson, P., & Martinsson, J. (2018). The changing political impact of compassion-evoking pictures: The case of the drowned toddler Alan Kurdi. *Journal of Ethnic and Migration Studies*, 45(13), 2275-2288. <https://doi.org/10.1080/1369183X.2018.1538773>
- Sturmer, M. (2013). *Afrika! Ein Plädoyer für eine differenzierte Berichterstattung*. Konstanz/München: UVK.
- Thränhardt, D. (2019). Welcoming citizens, divided government, simplifying media: Germany's refugee crisis, 2015-2017. In Dell'Orto, G., & Wetzstein, I. (Ed.), *Refugee news, refugee politics: Journalism, Public Opinion and Policy-making in Europe*. New York: Routledge (pp. 15-25).
- Transparency International (n. d.). Transparency International – The Global Anti-Corruption Coalition. Retrieved November 25, 2020, from <https://www.transparency.org/>
- Tversky, A., & Kahneman, D. (1973). Availability: A heuristic for judging frequency and probability. *Cognitive Psychology*, 5(2), 207-232. [https://doi.org/10.1016/0010-0285\(73\)90033-9](https://doi.org/10.1016/0010-0285(73)90033-9)

UNHCR (n. d.). Glossary. Retrieved November 25, 2020, from <http://www.issm.cnr.it/progetti/emigrazione/ME-TADATA%20E%20GLOSSARI/UNHCR/GLOSSARY%20UNHCR.pdf>

UNHCR (2019). Fact sheet: Uganda February 2019. Retrieved March 30, 2019, from <http://reporting.unhcr.org/sites/default/files/UNHCR%20Uganda%20Factsheet%20-%20February%202019.pdf>

Vallone, R. P., Ross, L., & Lepper, M. R. (1985). The hostile media phenomenon: Biased perception and perceptions of media bias in coverage of the Beirut massacre. *Journal of Personality and Social Psychology*, 49(3), 577-585. <https://doi.org/10.1037/0022-3514.49.3.577>

Völlinger, V. (2017, November 23). Ein Möglichkeitsfenster gegen Sklaverei. *Zeit Online*. Retrieved March 29, 2019, from <https://www.zeit.de/politik/ausland/2017-11/fluechtlinge-libyen-cnn-sklavenhandel-eu-frederica-mogherini-afrikanische-union-un-sicherheitsrat>

Wahl-Jorgensen, K., Williams, A., Sambrook, R., Harris, J., Garcia-Blanco, I., Dencik, L., Cushion, S., Carter, C., & Allan, S. (2016). The future of journalism: Risks, threats and opportunities. *Journalism Studies*, 17(7), 801-807. <https://doi.org/10.1080/1461670X.2016.1199486>

Warah, R. (2016, May 15). Somali refugees deserve better than being sent back to danger. *Nation*. Retrieved November 25, 2020, from <https://nation.africa/kenya/blogs-opinion/opinion/somali-refugees-deserve-better-than-being-sent-back-to-danger-1198970>

Weaver, D. H. (2007). Thoughts on agenda setting, framing, and priming. *Journal of Communication*, 57(1), 142-147. <https://doi.org/10.1111/j.1460-2466.2006.00333.x>

Whitaker, B. E. (2019, July 16). Migration and the politics of exclusion in Africa. *Italian Institute for International Political Studies*. Retrieved November 23, 2019, from <https://www.ispionline.it/en/publication/migration-and-politics-exclusion-africa-23513>

White, A. (2015). Moving stories: International review of how media cover migration. *Ethical Journalism Network*. Retrieved June 26, 2018, from <https://ethicaljournalismnetwork.org/assets/docs/054/198/8feb836-108e6c6.pdf>

Wittmann, F. (2006). Ungleichheiten im globalen Kommunikationsfluss: Interventionen zum Uno-Weltgipfel zur Informationsgesellschaft im Kontext Westafrikas. In Rehberg, K.-S. (Ed.), *Soziale Ungleichheit, kulturelle Unterschiede: Verhandlungen des 32. Kongresses der Deutschen Gesellschaft für Soziologie in München 2004* (pp. 4265-4271). Frankfurt am Main, New York: Campus.

Wojcieszak, M., & Azrout, R. (2016). I saw you in the news: Mediated and direct intergroup contact improve outgroup attitudes. *Journal of Communication*, 66(6), 1032-1060. <https://doi.org/10.1111/jcom.12266>

Zappe, A.-C. (2015, November 18). Medien und Flüchtlinge – Perspektiven aus Afrika. *EJO*. Retrieved February 19, 2019, from <http://de.ejo-online.eu/ausbildung/medien-und-fluechtlinge-perspektiven-aus-afrika>

Zillmann, D., & Brosius, H.-B. (2010). *Exemplification in communication: The influence of case reports on the perception of issues*. New York, Abingdon: Routledge.

Zingarelli, M. E. (2010). *The CNN effect and the Al Jazeera effect in global politics and society* (Master Thesis). Georgetown University, Washington, D.C. Retrieved November 25, 2020, from <https://repository.library.georgetown.edu/bitstream/handle/10822/553423/zingarelliMeganElizabeth.pdf>



MODULI 6

Uchanganuzi kifani wa Guinea-Bissau (Afrika Magharibi)

na Monika Lengauer



MALENGO YA MODULI

- Kuuelewa uchanguzi kifani huu wa nchi hii ya Afrika isiyoangaziwa sana na vyombo vya habari.
- Kuwasilisha vipengele teule kinzani kuhusu nchi hii yenye viwango vya chini vya ustawi wa kibinadamu.
- Kuhamasisha washiriki kuhusu simulizi za wanadamu zinazochangia idadi hii.



MATOKEO YA MAFUNZO

Kufikia mwisho wa moduli hii, sambamba na changanuzi kifani za awali, ili zote ziweze kulinganishwa katika ngazi za kimataifa, washiriki wanapaswa kuwa na uwezo wa:

- Kujadili uchanganu wa maamuzi yanayochukuliwa na wahamiaji na wakimbizi.
→ **Matokeo ya mafunzo kwa stadi za mitazamo ya kibinafsi na maadili: Kujibu**
- Kufafanua kile ambacho hadhira inahitaji kujua kuhusu uhamiaji ili iwezeshe kufanya maamuzi sahihi. → **Matokeo ya mafunzo kwa stadi za utambuzi: Kuelewa**
- Kutumia maarifa na marejeleo kuandaa wasifu mfupi wa nchi na wasifu mfupi kuhusu uhamiaji na uhamiaji wa kulazimishwa. → **Matokeo ya mafunzo kwa stadi za utambuzi: Kutumia maarifa**
- Kuchambua — kwa mtazamo wa kimataifa — uchanganuzi wa kifani wa Guinea-Bissau → **Matokeo ya mafunzo kwa stadi za utambuzi: Uchanganuzi**

Muhtasari

Guinea-Bissau inapatikana katika kundi la kipekee la mataifa yanayozungumza Kireno (Lusophone) barani Afrika kwenye ramani ya kufanyiwa utafiti wa masuala ya wahamiaji na wakimbizi Waafrika, mbali na tafiti zinazotumika sana za mataifa yanayozungumza Kiingereza (Anglophone) na Kifaransa (Francophone) barani Afrika.¹ Guinea Bissau ni nchi isiyofanyiwa utafiti wala kuangaziwa vya kutosha, si tu katika mawanda ya kiakademia na uanahabari, bali pia katika tafiti za kimataifa. Hata hivyo, Guinea-Bissau inadhihirisha baadhi ya sifa muhimu za muktadha wa uhamiaji na uhamiaji wa kulazimishwa, kama vile umaskini. Aidha, inatambuliwa kuwa na watu wasio na uraia. Nchi hiyo imetuama kwenye viwango vya chini kabisa vya ustawi wa binadamu tangu ilipopata uhuru wake 1974, na watu wake kunasika katika msururu wa migogoro ya kisiasa, ufasidi, umaskini na ukosefu wa fursa za kujiimarisha.

1 Nchi sita za Kiafrika za Lusophone yaani zinazungumza Kireno (Angola, Cape Verde, Equatorial Guinea, Guinea-Bissau, Msumbiji, São Tomé and Príncipe; CPLP, 2020).

Wasifu wa nchi

Guinea-Bissau ni nchi ndogo kwenye pwani ya Afrika Magharibi. Eneo lake la ardhi ni ndogo (36,000km²)² na idadi ya watu (milioni mbili), hasa ikilinganishwa na majirani zake wa karibu zaidi; Guinea (watu milioni 13 na eneo la 250,000km²) na Senegal (watu milioni 17 na eneo la 200,000km²). Barani Ulaya, Guinea-Bissau inalinganishwa kwa ukubwa wa eneo na Ubelgiji, na kwa idadi ya watu na Latvia, zote zikiwa nchi za pwani (UNdata, 2019)³.

Inakadiriwa kuwa idadi ya watu wa Guinea-Bissau itaongezeka kutoka milioni mbili hadi zaidi ya milioni 3.5 ifikapo 2050 (UNDESA, 2019b, uk. 24-25). Uwezo wa uzazi utapungua kutoka watoto 4.51 wanaozaliwa wakiwa hai kwa kila mwanamke (2015-2020) hadi watoto watatu wanaozaliwa (2045-2050; UNDESA, 2019b, uk. 138-139), na kiwango cha wastani cha ongezeko la idadi ya watu kwa mwaka kitapungua kutoka 2.5% (2015-2020) hadi 1.65% (2045-2050; UNDESA, 2019b, uk. 59).

Idadi ya watu wa Guinea-Bissau inajumuisha makabila mbalimbali.⁴ Uislamu ukiwa ndiyo dini kubwa, Ukristo nao ukiwa na watu wachache huku imani za kiasili zikiwa zimeenea sana. Watu huzungumza lugha nyingi tofauti ambazo kwa hakika huathiri utekelezaji wa uanahabari na taaluma ya uanahabari. Lugha rasmi ni Kireno lakini kwa kawaida watu huzungumza Krioli (Creole) au lugha mbalimbali za asili ya Kiafrika (Ocrisse-Aka & Bossard, 2006).

Ardhi ya Guinea-Bissau imekolea mazingira ya kijani kibichi na imejaa rotuba; upekee wa uanuwai wa viumbe-hai vyake unajumuisha mbuga za kitaifa, misitu mikubwa ya kitropiki, ardhi kubwa ya kilimo, mito, vinamasi vya mikoko na safu nyingi za visiwa. Eneo hili lenye uwezo mkubwa wa kiuchumi hata ingawa 'limelala', linahusisha shughuli za uzalishaji wa mbao, uchimbaji wa madini ya bauxite na fosfeti, na utalii wa kimataifa wenye thamani kubwa. Maeneo ya nchini humo yanafaa kwa uchukuzi na biashara za baharini na maziwa ya ndani ya nchi. Hata hivyo, ukwasi huu haujaanza kuguswa. Mazao ya kilimo, hasa korosho, huuzwa bila kutayarishwa na sehemu kubwa ya uchumi wake haijatumwa kuchuma pesa, badala yake biashara ni ya kubadilishana bidhaa kwa bidhaa. Usimamizi wa sekta ya umma unakumbwa na changamoto za kutumikia jamii zaidi hasa kwa wasomi kutumiwa kisiasa na kijeshi. Guinea-Bissau ina utendakazi duni ikilinganishwa na mataifa mengine mengi katika Afrika Magharibi;⁵ jinsi inavyoonekana katika Viwango vya Ustawi wa Kibinadamu – HDI (UNDP, 2019c, uk. 300-303). Kwa mtazamo wa kutia matumani, maendeleo kiasi fulani yametokea. Thamani ya jumla ya ustawi wa binadamu

2 Nambari na desimali zimefanywa herufi kamili katika maandishi haya katika juhudi za kuweka uwiano mzuri kati ya usahihi na usomaji.

3 Data inarejelea kipindi cha miaka mitano kinachotangulia mwaka uliorejelewa (UNdata, 2019).

4 Watu wa Fula (25 %), Balanta (25 %), Mandingo (14 %), Papel (9 %), Manjaca (9 %) na Mancanha kulingana na UNIOGBIS (2020).

5 Nchi zinazounda Jumuiya ya Kiuchumi ya Afrika Magharibi (ECOWAS) ni Benin, Burkina Faso, Cape Verde, Gambia, Ghana, Guinea, Guinea-Bissau, Ivory Coast, Liberia, Mali, Niger, Nigeria, Sierra Leone, Senegal na Togo (ECOWAS, 2016; ni Burkina Faso, Mali, Niger na Sierra Leone pekee zilizo na kiwango cha chini cha HDI kuliko Guinea-Bissau; UNDP, 2019c, uk. 300-303).

nchini iliimarika mfululizo tangu 2010 (UNDP, 2019a) licha ya kurudi nyuma hatua tatu kati ya 2013 na 2018 (UNDP, 2019c, uk. 306). Umri wa kuishi umeongezeka kwa takriban miaka minane kwa wanawake na tisa kwa wanaume tangu mwaka 2000 na sasa umefika miaka 61 kwa wanawake na miaka 57 kwa wanaume⁶ (UNDESA, 2019b, uk. 188-189). Umri wa kuishi katika changanuzi kifani nyingine mbili katika mwongozo huu ni miaka 62 kwa wanawake na miaka 59 kwa wanaume nchini Cameroon, miaka 84 kwa wanawake wa Ujerumani na miaka 80 kwa wanaume (UNDESA, 2019b, uk. 180-215). Watu wa Guinea Bissau wana umri wa kuishi wenye afya⁷ wa miaka 52 (WaCameroon: miaka 55; Wajerumani: miaka 70; UNDP, 2019b, uk. 6-9).

Guinea-Bissau inajitokeza kama “taifa la kwanza la Kusini ya Jangwa la Sahara [ambalo] lilitangaza uhuru wake kutoka kwa mkoloni wa Ulaya baada ya mapambano ya muda mrefu ya ukombozi. Baadhi ya mataifa mengine ya Kiafrika yalipata uhuru kutoka kwa tawala za kikoloni kwa mazungumzo na kisha kutwaa mamlaka kwa njia ya amani” (Lobban, 1974, uk. 15). Matumaini makubwa yaliyoibuliwa na uhuru huo yalififishwa na migogoro ya kutamausha iliyodumu kwa miongo kadhaa, ikiwemo ukosefu wa utulivu wa kisiasa na mapinduzi ya kijeshi na mauaji ya kisiasa. Mwaka 2019 uliashiria mabadiliko ya kihistoria: Kwa mara ya kwanza, rais alikamilisha hatamu yake ya miaka mitano mamlakani bila kukatizwa, uchaguzi wa kidemokrasia wa wabunge ukafanyika Machi, ukifuatiwa na kutangazwa kwa baraza la mawaziri lililozingatia usawa wa jinsia mnamo Julai na uchaguzi wa urais Novemba kisha awamu ya pili ya uchaguzi huo ikafanyika Desemba. Mwisho kabisa, maafisa wa polisi walinasa kiwango kikubwa zaidi cha kokeni (karibu kilo 800) mnamo Machi 9, 2019, usiku wa kuamkia uchaguzi wa wabunge, na miezi sita baadaye wakanasa kilo 1,800 zaidi. Hata hivyo, ripoti iliyofuata ya utathmini wa tukio hilo ilihoji “kurejea kwa genge la zamani la walanguzi wa kijeshi ambalo limekuwa likihusika na ulanguzi nchini Guinea-Bissau tangu 2007” (Shaw & Gomes, 2020, uk. 14). Mnamo Julai 2020, Marekani ilieleza wasiwasi wake “ikiwa kweli kulikuwa na nia njema ya kisiasa kukomesha ueneaji wa mihadarati katika nchi hiyo” (Idara ya Masuala ya Kigeni, 2020). Ukweli kwamba rais wa Guinea-Bissau aliwafuta kazi maafisa wawili wakuu katika vita dhidi ya ulanguzi wa dawa za kulevya — Waziri wa Sheria na Mkuu wa Polisi wa Mahakama — ulifasiriwa kuwa wa kutatani-sha. BBC iliripoti matukio hayo yenye kichwa cha habari cha kuvutia: “Jinsi ‘nchi ya mihadarati ya inavyojaribu kuachana na tabia yake (*“How Africa’s ‘narco-state’ is trying to kick its habit*)” (Shryock, 2020).

Sifa ya uhamiaji

Kama mojawapo ya nchi katika tapo la “ustawi wa chini wa kibinadamu” katika viwango vya HDI (UNDP, 2019a), raia wa Guinea-Bissau wanaonyesha kujinyanyua kwa njia nyingi, mbali na kuwa nchi hii ni makazi kwa watu kutoka maeneo mengine ya Afrika Magharibi.

6 Data inarejelea kipindi cha miaka mitano kinachotangulia mwaka unaorejelewa (UNdata, 2019).

7 Miaka ya kuishi kwa afya kuanzia wakati wa kuzaliwa hufafanuliwa kuwa wastani wa idadi ya miaka ambayo mtu anaweza kutarajia kuishi akiwa na afya nzuri na pia kujumuisha miaka aliyoishi akiwa na afya mbaya kwa sababu ya ugonjwa na majeraha (UNDP, 2019b, uk. 9, Maandishi).

Uhamiaji wa ndani kwa ndani

Hatua ya kwanza ya uhamiaji kwa kawaida huwa ni kutoka vijijini hadi mijini. Uhamiaji halisi katika maeneo ya nchi hii ni mkubwa kwa kiasi fulani. Takriban asilimia 44 ya watu wanaishi katika maeneo machache ya miji, na idadi hiyo inaendelea kuongezeka (UNdata, 2019). Hapa, watu hupata huduma nyingi na bora zaidi za taifa ambazo ni haba kwa jumla na ndipo penye umaskini mdogo ikilinganishwa na maeneo kama vile Oio, Bafata, Cacheu au Gabú. Hasa maeneo ya Bissau, Gabú na Oio yamekuwa mahali pa kuanzia kwa “uhamiaji usiokadirika [...] hali ambayo imeenea zaidi hivi majuzi” (IOM, 2018). Hatua hizi pia zimeonyeshwa katika utafiti wa waliohama kutoka Guinea-Bissau kupitia Bahari ya Mediteranean hadi Italia: 37% ya wote waliohojiwa kutoka Guinea-Bissau wanatoka mji mkuu wa Bissau, ikifuatiwa na 23% kutoka Gabú (eneo la mashariki linalopakana na Senegal na Guinea) na 18% kutoka Oio (eneo la Kaskazini linalopakana na Senegal; Scarabello, 2019, uk. 44). Katika tasnifu ya Abreu (201) kuhusu uhamiaji na kiustawi nchini Guinea-Bissau kupitia uchanganuzi kifani katika vijiji viwili, anafafanua uhamaji wenye sifa za kushangaza.

Wakimbizi wa ndani kwa ndani (IDPs)

Wingi wa wakimbizi wa ndani kwa ndani (IDPs) umeelezwa hapo awali katika mwongozo huu kama changamoto inayoongezeka barani Afrika. UNHCR inaripoti matukio ya 1998 nchini Guinea-Bissau, wakati wa vita vya wenyewe kwa wenyewe (vilivyoanzia Juni 7, 1998, hadi Mei 10, 1999) ambapo karibu watu 200,000 walijipata wakiwa wakimbizi wa ndani (UNHCR, 2020b); hii ni sawa na 17% ya jumla ya watu wapatao milioni 1.2 mwaka 1998 (UNDESA, 2019b, uk. 24). IDMC huchunguza na kuripoti ufurushwaji wa watu makwao unaotokana na migogoro, majanga na matukio mengine. Kuhusu Guinea-Bissau, ripoti ya IDMC inachunguza viwango vya chini vya visa hivi kwenye ulinganishaji wake. Takwimu za kila mwaka za migogoro na watu walio-toroka makwao kutokana na majanga hazionyeshi watu waliofurushwa kutokana na migogoro. Ufurushwaji mpya unaotokana na majanga ulirekodiwa katika 2008 (watu 500), 2010 (2,000), 2018 (3,700), na 2019 (410). Uhamaji uliorekodiwa unahusiana zaidi na hali ya hewa. Msimu wa mvua wa 2020 (Mei hadi Oktoba) uliharibu mamia ya nyumba, na kusababishia wananchi uhaba wa chakula na hali mbaya ya afya, hasa nyakati za janga la Uviko-19. Ingawa ni masikitiko makuu kushuhudia watu wakilazimika kuhama makwao, idadi hii inaweza kudhibitiwa kwa juhudi za watu waliopewa jukumu la kuwasaidia. Katika siku zijazo, IDMC inabashiri kuwa kwa wastani watu 770 watahama makazi yao kila mwaka kutokana na majanga (IDMC, 2020), ambayo yanatarajiwa kusababishwa na mabadiliko ya hali ya anga (tazama Moduli 3).

Uhamiaji wa ndani ya Afrika

ECOWAS inaruhusu utembeaji huru wa watu. Hapa ina maana zaidi ya, urahisi wa taratibu za usafiri na ukaribu wa kijiografia ambao huwafanya watu kuhama kieneo. Mataifa ya leo ya Guinea-Bissau na jirani zake Guinea na Senegal ni wenyeji wa makabila mengi yenye asili moja:

Wafulani, kwa mfano, wanaishi kwa wingi nchini Guinea-Bissau, Guinea na pia Gambia; Malinke wanaishi Guinea-Bissau, Guinea, Gambia na Senegal. “Dhana ya ukabila na sifa zake tatu za msingi za kitamaduni zinazokata katikati, ufahamu, na mipaka ya kitamaduni” (Young, 2017) inaonekana katika eneo hili la Afrika Magharibi. Sifa za kawaida ni pamoja na kizazi chenye asili moja, lugha, mienendo, kanuni za kuwapa watoto majina, matambiko na mengineyo. Hata hivyo, utambulisho wa makabila madogo ni kiungo muhimu katika mchakato wa kisiasa ambacho kinaonekana pia katika mashindano ya uchaguzi (Young, 2017). Temudo (2009) anaonyesha bayana jinsi watu wa Balanta nchini Guinea-Bissau walivyonyoosha tofauti zao, hali iliyokisaidia chama chao cha Party for Social Renovation (PRS) kushinda urais katika uchaguzi wa 2000, na kusababisha kukemewa kwa “ukabila” wa Balanta (Temudo, 2019, uk. 57) kwa kushindana kwa vyama vya kisiasa kama Chama cha Uhuru wa Guinea na Cape Verde yaani PAIGC.⁸ Uunganishaji wa ukabila na siasa, utamaduni na usasa, unafafanuliwa na Lundy (2018, uk. 13-14).

Uhamiaji wa muda na uhamiaji wa kudumu wa kimataifa

Idadi ya wahamiaji wa kimataifa⁹ nchini Guinea-Bissau (watu 27,000 mnamo 2019) inajumuisha zaidi raia kutoka Senegal (13,600), Guinea (5,400) na Gambia (1,600); kwa usawa, wengi wa raia wa Guinea-Bissau pia huhamia katika nchi hizi jirani: Senegal (30,600), Gambia (13,800) na Guinea (4,300). Nchi ya visiwa vya Afrika Magharibi ya Cape Verde¹⁰ ni kimbilio kubwa zaidi la watu wa Guinea-Bissau (5,300; 2019) huku idadi ya raia wa Cape Verde wanaohamia Guinea-Bissau ikiwa ndogo (606). Idadi ya wahamiaji kutoka Ulaya na Amerika Kaskazini ni ndogo zaidi huku kiwango cha uhamiaji kwenda Ulaya kikiwa kimeongezeka kutoka 29% ya wahamiaji wote wa kimataifa wanaotoka Guinea-Bissau katika mwaka 1990 hadi 42% mwaka 2019. Wakati huo huo, uhamiaji hadi katika nchi nyingine za Afrika umepungua kutoka 71% ya wahamiaji wote wa kimataifa wanaotoka Guinea-Bissau mnamo 1990 hadi 57% mnamo 2019 (UNDESA, 2019a). Mitindo hii ya Guinea-Bissau inalingana na ile ya bara la Afrika kwa jumla (tazama Moduli 9). Utafiti wa hivi majuzi unathibitisha mabadiliko hayo: Idadi ya raia wa Guinea-Bissau wanaoishi nchini Italia mara kwa mara iliongezeka mara tano tangu 2012 hadi 2018, mwanzoni ikiwa polepole (kwa takribani wananchi 100 kila mwaka), ikaruka baada ya 2015 (ambapo iliongezeka kwa zaidi ya watu 600 kutoka 2017 hadi 2018), na idadi ya maombi ya hifadhi katika nchi za kigeni iliongezeka mara nne kati ya 2012 na 2018 (Scarabello, 2019, uk. 39-40).

Kwa kawaida, uhamaji mara nyingi hufanyika ndani ya mipaka ya ardhi au utamaduni, kwa mfano watu wa Guinea-Bissau huchagua mataifa yanayozungumza Kireno (Lusophone) na Kifaransa

8 PAIGC, Chama cha African Party for the Independence of Guinea and Cape Verde (PAIGC), kilianzishwa na Amílcar Cabral. PAIGC iliongoza nchi hiyo, baada ya vita vya muda mrefu vya kupigania uhuru kutoka kwa wakoloni wa Ureno miaka ya 1960, hadi kupata uhuru mnamo 1974.

9 Takwimu zinarejelea idadi ya wahamiaji wa kimataifa. Idadi hii inajumuisha wakazi wote waliozaliwa nje ya nchi hiyo bila kujali ilikuwa lini walipoingia nchini humo. Kwa ufafanuzi wa idadi hii ya wahamaji, angalia faharasa/sherehe zinazopendekezwa katika Moduli ya 2 (EMN, 2018; IOM, 2019a).

10 Cape Verde ni mojawapo ya nchi zilizoendelea zaidi za Afrika Magharibi. Imeorodheshwa ya 126 kati ya nchi 189 katika kiwango cha ustawi wa binadamu kama inavyoonyeshwa katika HDI (UNDP, 2019c, uk. 300-303).

(Francophone)¹¹, ambazo ni Senegal (wahamiaji 30,600 kutoka Guinea-Bissau), Cape Verde (5,300) na Guinea (4,300) katika ngazi ya kanda, na Ureno (wahamiaji 29,000 kutoka Guinea-Bissau mnamo 2019), Ufaransa (3,400) na Brazili (1,300) katika mabara ya Ulaya na Marekani (data ya 2019; UNDESA, 2019a).

Uhamiaji rasmi wa kimataifa; 1: Hadi Ureno (Ulaya)

Uhamiaji hadi Ureno hutokana na uhusiano maalumu na taifa hilo lililoitawala kikoloni zamani, si tu kwa kushiriki lugha moja rasmi na uhusiano wa kitaasisi kupitia Jumuiya ya Nchi za Lugha za Kireno (CPLP) lakini pia kwa kufurahia sheria na kanuni maalumu za uhamiaji. Kila raia wa Guinea-Bissau anayetaka kusafiri hadi Ureno kwa njia rasmi (uhamiaji wa kawaida) anahitajika kutuma maombi ya viza (mchakato huo umekabidhiwa kampuni ya kibinafsi ya VFS Global). Viza hapa zinapatikana bila malipo (kwa watoto wa umri wa hadi miaka sita), ila kwa kawaida hugharimu €60 kama ada na hadi €75 kwa viza ya wanafunzi na kibali cha kikazi (Kituo cha Maombi ya Viza cha Ureno nchini Guinea-Bissau & VFS Global, 2020). Mwanahabari wa Guinea-Bissau hulipwa mshahara wa chini ya €100 kwa mwezi, ikiwa kweli atalipwa. Kwa hivyo, ada za viza hulingana na mshahara wa mwezi mmoja lakini matarajio ni kupata kazi Ureno na kufidia haraka gharama hizo za viza na usafiri. Hata hivyo, nafasi ya kufaulu kwa hilo ni ndogo. Capucha na wengine (2016, uk. 10) huripoti viwango vya ukosefu wa ajira Ureno miongoni mwa wahamiaji kutoka nchi za Kiafrika za Lusophone ambavyo ni vya juu zaidi kuliko vya wahamiaji kutoka nchi nyingine (40% kwa raia wa Guinea-Bissau ikilinganishwa na 15% kwa wa-Ukraine). Ajira ambazo Waafrika wa Lusophone hupata huhitaji ujuzi wa chini kuliko kazi ambazo watu wengine kwa jumla wanashikilia (37% ya wahamiaji wa Kiafrika wa nchi za Lusophone walifanya kazi katika taaluma za hadhi ya chini nchini Ureno ukilinganisha na 13% ya watu kwa jumla, data kutoka 2011). Mishahara ambayo wahamiaji kutoka Lusophone-Afrika wanapokea ni chini ya ile ya jumla (€500 dhidi ya €600). Abreu (2012, uk. 222) aligundua kuwa wahamiaji wengi wanaofanya kazi kutoka vijiji vilivyochunguzwa katika uchanganuzi huu walikuwa wakifanya kazi Ureno kama wajenzi au wengine hawakuwa na ajira kabisa. Scarrabello (2019, uk. 44-46) anaonyesha kuwa wahamiaji wengi wa Guinea-Bissau ni vijana wa kiume (wenye umri wa kati ya miaka 19 na 30) wasiokuwa na elimu ya kutosha (asilimia 30 hawajamaliza aina yoyote ya elimu rasmi); wengi walitangaza kuwa walikuwa wamejiajiri (54% ya waliohojiwa¹²) — wengi wao wakiwa kati ka sekta za ujenzi, uchukuzi, kilimo — au hawakuwa na ajira kabisa (37% ya washiriki) kabla ya kuondoka Guinea-Bissau. Kuhusu hali zilizowasukuma kuhama, wengi walitaja vita au migogoro (34%) na matatizo ya uchumi (32%), ikifuatiwa na dhuluma (21%) na ufikiaji wa huduma ndogo za kibinadamu (10%). Ni vyema kutambua kwamba wahamiaji si lazima waelekee Ulaya moja kwa moja kutoka Guinea-Bissau lakini mara nyingi ni baada ya kukaa Libya kwa muda mrefu (Scarabello, 2019, uk. 45-46).

11 Guinea-Bissau ni mwanachama wa jumuiya ya nchi zinazozungumza Kireno (Comunidade dos Países de Língua Portuguesa, CPLP) na jumuiya ya nchi zinazozungumza Kifaransa (Organization Internationale de la Francophonie (OIF), La Franco-phonie).

12 Mahojiano yalifanywa katika tafiti za IOM za DTM za vikundi vya kitaifa vinavyowasili kupitia njia ya Mediterania ya Kati kati ya 2016 na 2018, kulingana na Scarabello (2019, uk. 42).

Sheria ya Ureno inaruhusu aina mbalimbali za viza za ukaaji kwa raia wa Guinea-Bissau wanaotaka ajira, kujajiri, masomo na kuungana tena na familia zao. Chini ya makubaliano kati ya nchi hizo mbili, raia wa Guinea-Bissau wanaweza kusafiri na viza ya muda kwa sababu za matibabu hadi Ureno. Baadaye, baadhi ya wahamiaji hao hupewa kibali cha kuishi baada ya kupata kazi au kwa sababu hali zao za kiafya zinawazuia kurudi nyumbani. Vifaa vya matibabu nchini Guinea-Bissau havitoshi kutoa huduma hitajika kwa watu wote wa taifa hilo. Tathmini ya maendeleo katika kufanikisha Malengo ya Ustawi Endelevu — SDG 3 (“Kuhakikisha kuna maisha yenye afya na kukuza ustawi miongoni mwa watu wa umri wote”; UNDESA, n. d.) “kunadorora” na “changa-moto kuu zingalipo” (Sachs na wengine, 2020, uk. 45, Kielelezo 19; Figure 19; uk. 242-243).

Mnamo 2020, maendeleo makubwa yalisaidia wahamiaji na wakimbizi Ureno: Kutokana na athari za Uviko-19, serikali iliamua kuwapa kwa muda haki kamili za uraia. Hatua hiyo ilichukuliwa ili kuzidisha ufikiaji kamili wa huduma za afya na kupunguza hatari za afya ya umma (Schengen Visa News, 2020). Hatua ya pili inawawezesha watoto wa wahamiaji kuwa raia wa Ureno ikiwa wazazi wao wana vibali vya kuishi kwa mwaka mmoja (awali, sheria ya kitaifa ilikuwa imeweka sharti la kuishi kwa miaka miwili, kulingana na Muungano wa Ulaya; 2020).

Uhamaji usiokuwa rasmi kutoka Guinea-Bissau

Kulingana na IOM, uhamiaji usio rasmi, hasa kutoka maeneo ya Gabú, Oio na Bafata ya Guinea Bissau, “ulanguzi wa vijana katika siku za hivi karibuni umeenea huku idadi ya visa vya vijana kugeuka mawindo ya walanguzi hao ikiongezeka [...]” (IOM, 2018). Katika hali ya kusikitisha zaidi, vijana hawa hufa katika juhudi zao za kuvuka Jangwa la Sahara au Bahari ya Mediterranean. Kukosa kufahamu hatari ya uhamiaji usiokuwa rasmi mara nyingi huwachochea kuondoka nchini mwao. Wakiwa njiani, vijana wengi hujipata katika hali hatari, wakinyimwa haki zao. Njia moja ya kurejea nyumbani salama na kwa hiari ni kupitia mpango wa pamoja wa EU-IOM wa ulinzi wa uhamaji na ujumuishaji upya katika jamii. IOM huwasaidia wanaorejea kwa hiari kujikimu nyumbani, ama kwa kufadhili mipango yao ya biashara au kuwalipa pesa kwa kufanya kazi katika miradi ya malipo (tazama makala ya video ya Chantal Beil, maelezo katika mapendekezo ya darasani, ilivyotajwa hapo awali; EU na IOM, 2020; IOM, 2019b).

Wadau katika bodi nzima wanaripoti kwamba Guinea-Bissau imeathiriwa pakubwa na ulanguzi wa watu binafsi, ukijumuisha ulanguzi wa watoto kwa ajili ya kazi za kulazimishwa na dhuluma za kingono. Aina ya ushahidi thabiti ulioripotiwa ni ulanguzi wa watoto (unaojulikana kama tali-bés) nchini Senegal. Wazazi hukabidhi watoto wao kwa watu wazima wanaodai kuwa viongozi wa kidini wenye madhumuni ya kuwapa watoto hao elimu ya kidini. Watoto hawa mara nyingi huishia kufanya kazi za kulazimishwa au za ombaomba na hupitia dhuluma kali (Gama, 2020). Einarsdóttir na Boiro (2016, uk. 863) wanaelezea matarajio ya familia za watoto hao.



ZOEZI LILILOPENDEKEZWA LA KUSHUGHULIKIA STADI ZA UTAMBUZI ZA UELEWA NA KUTATHMINI, NA STADI ZA MITAZAMO YA KIBINAFSI NA MAADILI ZA KUJIBU:

Mwanafunzi mzoefu wa Taasisi ya Uanahabari, Chuo Kikuu cha TU Dortmund, ambaye pia ni mwanagenzi katika runinga ya Chantal Beil, ametayarisha makala kadhaa ya video kuhusu uhamiaji na uhamishwaji wa lazima kuhusiana na hali za kimuktadha kutoka/kwenda Guinea-Bissau. Aidha, Chantal Beil ametoa mafunzo kwa wanahabari wa Guinea-Bissau nchini humo chini ya Umoja wa Mataifa kuhusu jinsi ya kuwasilisha vyema hadithi ya uhamiaji kama mwanahabari wa TV.

Makala hayo yanapatikana kwenye tovuti ya mradi: www.mediaandmigration.com. Waonyeshe darasani.

Kila mshiriki aandike uhakiki wa ukurasa mmoja wa kazi ya uanahabari kwenye vyombo vya habari, akifuata maswali:

- Je, Beil anawasilisha ujumbe gani kuhusu masuala ya wahamiaji na wakimbizi?
- Je, anaisuka hadithi yake kwa mtindo upi?
- Je, anatumia mbinu gani za kusimulia hadithi za taaluma ya uanahabari?
- Je, mtazamo wake unaonyesha chuki kwa Muungano wa Ulaya au anasimulia moja ya hadithi za wahamiaji na wakimbizi wa Kiafrika au Guinea-Bissau?
- Je, kazi yake inaakisi ufahamu wa Guinea-Bissau?
- Je, vipengele ambavyo hadhira inahitaji kujua kuhusu uhamaji na uhamishwaji wa lazima vimeonyeshwa katika hadithi hiyo ili waweze kufanya maamuzi yao wenyewe?
- Je, ni kitu unadhani Beil angefanya vizuri zaidi kuliko alivyofanya?

Uhamiaji rasmi wa kimataifa 2: Kuelekea Brazil

Kama nchi chaguo la wahamiaji, Brazil ilipendwa na watu wa Guinea-Bissau katika enzi ya Rais Luiz Inácio Lula da Silva aliyeingia mamlakani 2003 na kuanzisha mabadiliko ya sera mba-limbali. Idadi ya wahamiaji kutoka Guinea-Bissau iliongezeka kutoka takwimu za chini (zisizo-julikana) mwaka wa 2000 hadi 1,270 mwaka wa 2019 (UNDESA, 2019a). Kwa Brazil, Afrika imepewa kipaumbele kikuu cha kigeni - mantiki hiyo imejumuisha mbinu za kimkakati za kui-marisha nafasi yake katika ushirikiano wa kitaalamu baina ya nchi zinazoendelea za kusini mwa

dunia na nchi za BRICS (Brazil, Urusi, India, China na Afrika Kusini.)¹³Afrika ilipewa umuhimu kama chimbuko la malighafi na soko la bidhaa za Brazil; historia inaziunganisha nchi hizi mbili kwani mamilioni ya Waafrika wa Magharibi walisafirishwa kimabavu kupitia bahari ya Atlantiki hadi Brazil wakati wa biashara ya utumwa. Ukaribu wa kijiografia na kitamaduni pia uliwezesha ushirikiano huo. Kireno ni lugha rasmi katika nchi hizo mbili wanachama wa CPLP. Guinea-Bissau ilijumuishwa baada ya Brazil kufuta madeni ya Kiafrika yanayokaribia dola milioni 900 (Abdenur & Neto, 2013). Historia ya Afrika imekuwa sehemu muhimu ya mitaala ya shule za nchi hiyo ya Amerika Kusini, na hata chuo kikuu kinachosajili sana wanafunzi wa Kiafrika, hasa kutoka nchi za Lusophone, kimeanzishwa (Abdenur & Neto, 2014, uk. 56). Hata hivyo, hali halisi iliyojitokeza 2020, inaashiria jambo tofauti. Antonio Brasil, ambaye ni mwanahabari wa TV na profesa wa taaluma ya uanahabari katika Chuo Kikuu cha Florianopolis, Brasil, anaeleza kuwa pamotokea mabadiliko kuhusu uhusiano wa kimataifa wa Brazili na mikakati ya kiuchumi (Brasil, 2020).

Hata hivyo, watu kutoka Guinea-Bissau na nchi nyinginezo za Afrika Magharibi bado wana matumaini ya kupata maisha bora nchini Brazili, kama vile kufanya kazi, na kutuma pesa nyumbani au kusoma bila malipo. Lakini wahamiaji hao wanaitaja safari ndefu ya kilomita 3,000 hadi Brazil kama changamoto kuu (Phillips, 2018).

Kutafuta hifadhi

Idadi ya wakimbizi, watafutaji hifadhi, wakimbizi waliorejeshwa, watu wasio na uraia na wengine waliotafuta makazi na ulinzi nchini Guinea-Bissau inaonyesha taswira ya kulazimisha uhamiaji unaosababishwa na migogoro katika eneo hilo. Kwa miaka mingi, wakimbizi wengi nchini Guinea-Bissau wametokana na mzozo wa muda mrefu wa Casamance nchini Senegal (Casamance ni eneo linalopakana na Guinea-Bissau). Wakimbizi kutoka Sierra Leone waliongezeka nyakati za vita vya wenyewe kwa wenyewe nchini humo (1991-2002; UNHCR, 2020a).

Idadi ya wanaotafuta hifadhi barani Ulaya kutoka Guinea-Bissau ni ndogo sana. Mnamo 2019, waombaji hifadhi 740 na waombaji wa mara ya kwanza walisajiliwa, idadi iliyo ndogo ikilinganishwa na nchi jirani za Guinea (13,590) na Senegal (6,695). Mnamo 2019, idadi hiyo ilikuwa ndogo hadi miaka ya katikati mwa 2010 na 2020 — lakini ikafikia kilele wakati wa mzozo huo ambapo wakimbizi 1,240 (2015) na 1,315 (2016) walitafuta hifadhi. Uwezekano wa waombaji hifadhi kufanya maamuzi bora ni mdogo. Mnamo 2019, watu 65 walioomba hifadhi kwa mara ya kwanza walifanya maamuzi mazuri, watu 30 kati yao wakinufaika kutokana na Mapatano ya Wakimbizi wa 1951 na Mkataba wake wa 1967 (tazama Moduli 2), 25 walichukuliwa kutokana na sababu za kibinadamu huku 770 wakikataliwa (Eurostat, 2020).

13 BRICS ni akronimu ya nchi tano zinazopiga hatua kubwa kiuchumi: Brazili, Urusi, India, China, Afrika Kusini.



ZOEZI LILIOPENDEKEZWA LA KUSHUGHULIKIA STADI ZA UTAMBUZI ZA KUTEKELEZA NA KUCHANGANUA, NA STADI ZA MITAZAMO YA KIBINAFSI NA MAADILI ZA KUJIBU:

Waruhusu wanafunzi kupata uelewa wa Guinea-Bissau kama nchi ya wahamiaji na wakimbizi kabla ya kujifunza mambo kinzani nchini humo.

Waalike washiriki kutayarisha wasifu mfupi wa nchi hiyo na mwingine mfupi kuhusu uhamiaji na uhamishwaji wa lazima nchini Guinea-Bissau.

- Ili kutunga wasifu hizi mbili, washiriki wachague data zao kutoka kwenye marejeleo yaliyoonyeshwa katika Moduli 2, hasa ukurasa wa nchi katika tovuti ya data ya uhamiaji Guinea-Bissau (Migration Data Portal, 2020).

Ili kuhuisha data, washiriki wachunguze ripoti za vyombo vya habari

- kutoka au kuhusu Guinea-Bissau ambazo wanaona kuwa zinaelimisha na kufahamisha.

Wawasilishe wasifu mbili katika mhadhara na wahitimishe kwa vipengele

- vitano muhimu ili kubainisha sifa kuu za Guinea-Bissau.

ZOEZI LILIOPENDEKEZWA LA KUSHUGHULIKIA STADI ZA UTAMBUZI ZA KUELEWA:

Wape washiriki jukumu la kueleza ni vipengee vipi vya wasifu wa nchi hiyo vinavyofaa kwa hadhira, hasa kuhusu mambo yanayowapa uwezo wa kufanya maamuzi sahihi kuhusu uhamiaji na uhamaji wa kulazimishwa.

Sababu teule za kimuktadha 1: Umaskini

Umaskini huathiri watu wengi Guinea-Bissau. Malengo ya Ustawi Endelevu (SDG 1) yanatoa wito wa kuangamizwa kwa umaskini katika hali zake zote ifikapo 2030, yaani miaka 10 tangu mwongozo huu uandikwe. HDR (UNDP, 2019c, uk. 67) inakiri kwamba “kupunguza umaskini uliokithiri ifikapo mwaka 2030 kunaweza kukosa kasi ya kutosha ifikapo [...] baada ya miongo kadhaa ya kupiga hatua, upunguzaji umaskini unapungua”. Hakika umaskini unaweza kutokomezwa kwani maendeleo ya kimataifa yameonyesha kuwa watu bilioni moja waliondolewa katika umaskini uliokithiri mwaka 2015 kuliko 1990. Katika 1990, asilimia 36 ya watu duniani waliishi katika umaskini uliokithiri kwa chini ya dola 1.90 kwa siku ikilinganishwa na asilimia 8.6 mnamo 2018. Hali ni kinyume katika ukanda wa Kusini mwa Jangwa la Sahara ambapo idadi ya watu wanaoishi katika umaskini uliokithiri imeongezeka kutoka wastani wa milioni 278 mwaka 1990 hadi milioni 413 mwaka 2015. Ikiwa mkondo wa sasa utaendelea, kufikia 2030, karibu 90% ya watu duniani wanaoishi katika umaskini uliokithiri watatoka nchi za Afrika za kusini ya Jangwa la Sahara. Huenda Guinea-Bissau ikawa miongoni mwao (UNDP, 2019c, uk. 67; Benki ya Dunia, 2018a, uk. 1-2).

Kuwa maskini kunafasiriwaje? Umaskini una ‘nyuso’ nyingi¹⁴, na umaskini wa kipato ni aina moja tu. *Multidimensional Poverty Index (MPI)*¹⁵ inashughulikia taswira tatu za umaskini (afya, elimu, viwango vya maisha) zenye viashirio kumi (lishe, vifo vya watoto; miaka ya kujipa elimu, shule; mafuta ya kupikia, usafi wa mazingira, maji ya kunywa, umeme, makazi na umiliki wa nyenzo/mali; OPHI, 2019, uk. 1; OPHI, & UNDP, 2018). Nchini Guinea-Bissau, zaidi ya 67%¹⁶ ya watu wanaishi katika umaskini wa kipato cha dola 1.90 kwa siku, idadi ambayo ni asilimia kubwa hata katika hali ya nchi za Afrika za kusini ya Jangwa la Sahara ambapo 45% ya watu wanaishi katika umaskini wa kipato. Ingawa umaskini mkubwa umekithiri katika jiji kuu la Bissau, ni mbaya zaidi katika maeneo ya mashambani (OPHI, 2019; UNDP, 2019c, kurasa za 67-70, uk. 320).

Huduma ni haba, iwapo hakika zipo zozote (IMF, & Serikali ya Guinea-Bissau, 2011, uk. 22-72). Ni asilimia 53 tu ya watu wa vijijini wanaopata maji safi ya kunywa, ikilinganishwa na 84% ya watu wa mijini. Ni asilimia tano tu ya watu wa vijijini wanaotumia vyoo bora ikilinganishwa na 35% katika maeneo ya mijini. Chini ya 10% ya wanawake katika maeneo ya vijijini wanajua kusoma na kuandika, tofauti na 40% katika ngazi ya kitaifa, na zaidi ya 50% katika jiji kuu la Bissau (data kutoka 2010). Umeme haupatikani kwa urahisi, na hasa kwa jamii za vijijini kwa kawaida, haupatikani kila mara. Mijini, umeme huzimwa mara kwa mara, na haupatikani kwa familia zote. Gharama za uendeshaji wa shughuli ni kubwa, sawa na wizi, pamoja na viwango vya chini vya ukusanyaji wa kodi. Tangu 2019, jiji la Bissau limekuwa likipokea umeme kutoka kwa meli iliyotia nanga katika bandari ya Bissau. Barabara za nchi hii ni za urefu wa kilomita 2,746 ambapo kati ya hizo ni kilomita 770 tu (asilimia 28) zilizowekwa lami. Usafiri wa barabarani, hata hivyo, ndiyo njia kuu ya kufikia miji mingi ya mashambani na jamii. Hali hiyo, kwa mfano, si tu hatari kwa watu kufikia vituo vya matibabu, lakini pia inatatiza usafirishaji wa bidhaa za kilimo kwa wateja katika maeneo ya mijini. Intaneti na laini za simu hazipatikani hasa katika sehemu za ndani ya nchi. Hata asilimia tatu ya watu Guinea-Bissau hawawezi kupata intaneti (Migration Data Portal, 2020).

“Kutia fora katika mazingira haya” ni kichwa chenye matamano cha ripoti iliyochapishwa mnamo 2018 (Benki ya Dunia, 2018b). Inaonyesha kuwa nchi ilikuwa na maafisa 4.7 wa usalama kwa kila wananchi 1,000 kulingana na orodha ya mishahara ikilinganishwa na chini ya moja kwa kila wananchi 1,000 kwa wahudumu wa afya (data ya 2017; Benki ya Dunia, 2018b, uk. 4; uk. 38, Kielelezo 2.2; uk. 40, Jedwali la 2.2). Upungufu wa uwekezaji katika sekta kuu za nchi hii umechapishwa katika muhtasari wa matumizi ya pesa za umma na sekta zilizo na data kutoka Wizara ya Uchumi na Fedha ya nchi hiyo (tazama Mchoro 19).

14 Mwongozo huu unazingatia mbinu mbili: ile inayochapishwa kila mwaka katika Ripoti ya Ustawi wa Kibinadamu (HDR) na ile inayochapishwa na Benki ya Dunia. Kila moja hutumia viashirio tofauti, lakini mbinu zote mbili zinaweza kulinganishwa kimataifa. Kipimo cha umaskini wa kimataifa cha Benki ya Dunia kinajumuisha umaskini wa fedha — unaopi-mwa kwa mtu kuwa na kipato cha chini ya dola 1.90 kwa siku — na kunyimwa elimu na miundombinu ya kimsingi kama vile maji, usafi wa mazingira na umeme (Benki ya Dunia, 2018c; Benki ya Dunia, 2020b; Benki ya Dunia, 2020a).

15 Mpango wa Oxford Poverty and Human Development Initiative (OPHI) hutayarisha MPI, na Ripoti za Ustawi wa Watu imekuwa ikichapisha MPI hiyo tangu 2010 (OPHI, & UNDP, 2018).

16 2007-2017. Data inarejelea mwaka wa hivi karibuni zaidi katika kipindi kilichobainishwa (UNDP, 2019c, uk. 320-321, tanbihi c).

Kielelezo 19: Guinea-Bissau : matumizi kwa sekta 2017 - 2015



Maendeleo ya Guinea-Bissau yanasalia kuwa changamoto, na rasilimali ni chache: “Matumizi ya umma katika sekta ya kijamii ni ya chini, ambayo, pamoja na ufanisi mdogo, huleta matokeo duni. Kwenye afya na elimu, nchi hiyo haitumii tu chini ya nchi nyingi za Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara, pia inafanya kazi vibaya kwa kila dola inayotumika. (Benki ya Dunia, 2018b, p. 1). *Data haipo kwenye hati chanzo.

Chanzo : Benki ya Dunia (2018b, p. 123, kielelezo 6.15). Mchoro ni wetu.

Umaskini ni ukosefu wa usawa na “haunyimi tu watu haki zao bali pia unakandamiza” (UNDP, 2019c, uk. 89). Katika Guinea-Bissau, asilimia 10 ya matajiri zaidi katika jamii wanamiliki 42% ya mapato, wakati 12.8% tu ya mapato yakishikiliwa na 40% ya watu maskini zaidi (2010-2017¹⁷) - hii ni sawa na ‘piramidi iliyogeuzwa chini juu’. Kiwango cha kutokuwa sawa kimapato, yaani *Gini coefficient*¹⁸ ni 50.7, ambacho ni cha juu sana ikilinganishwa na nchi jirani za Senegal (40.3) na Guinea (33.7), Guinea Bissau ikiwa miongoni mwa nchi zenye viwango vya juu zaidi vya kutokuwa sawa kimapato duniani. Watu wa Guinea-Bissau pia wanateseka kutokana na ukosefu mkubwa zaidi wa usawa kuliko jirani zao ijapo kwa ukosefu mkubwa wa usawa unaopimwa katika Viwango vya Ustawi wa Binadamu vilivyowianishwa na ukosefu wa usawa (UNDP, 2019c, uk. 308-311). Changanuzi kifani nyingine mbili katika mwongozo huu zinaonyesha kiwango cha Gini cha 46.8 (Cameroon) na 31.7 (Ujerumani). Taifa lililo lenye kiwango bora zaidi cha Gini duniani ni Ukraine cha 25.0, Slovakia ikiwa na 26.5 na Finland 27.1 huku Afrika Kusini ikiwa na kiwango cha juu zaidi cha Gini (63.0), ikifuatiwa na Namibia yenye 59.1 na Jamhuri ya Afrika ya Kati 56.2 (UNDP, 2019c, uk. 308- 311).

17 Data inarejelea mwaka wa hivi karibuni zaidi katika kipindi kilichobainishwa (UNDP, 2019c, uk. 311, Tanbihi e).

18 Kiwango cha kutokuwa sawa: Ni kipimo cha pengo la mgawanyo wa mapato kati ya watu binafsi au familia katika nchi dhidi ya mgawanyo bora zaidi wenye usawa. Tarakimu ya 0 inawakilisha usawa kamili, nayo tarakimu ya 100 inaashiria ukosefu kabisa wa usawa (UNDP, 2019c, uk. 311, Maandishi).

Sababu teule za kimuktadha 2: Ongezeko la watu na vijana

Kama ilivyoelezwa hapo awali (tazama Moduli 3), ongezeko la idadi ya watu ni mojawapo ya sababu kuu zinazoathiri uhamaji. “Kuongezeka kwa vijana” kunaweza kuwa kwa “manufaa” kama, kwa mfano, serikali zitawekeza katika afya, elimu na katika kuwawezesha wanawake; vinginevyo, ongezeko la watu linaweza kuongeza changamoto katika kufanikisha SDGs. Kwa kurejelea SDGs, ukuaji wa idadi ya watu “wakati mwingine huitwa kizingiti [...] ukichukuliwa sana kuwa mada nyeti ya kisiasa” isiyowekwa katika muktadha “bayana” (Abel na wengine., 2016, uk. 14298). SDGs zinazoshughulikia vifo vya watoto, vifo vya wanawake wajawazito, kinachosababisha vifo, afya ya uzazi na hasa elimu zinahusiana; jinsi wanawake wanavyoelimika zaidi, ndivyo wanavyopunguza kuzaa sawia na kupungua kwa vifo vya watoto (Abel na wengine, 2016, uk. 14298).

Ongezeko la idadi ya watu Guinea-Bissau limezidi kwa kasi kutoka 1950 (1.47% kila mwaka) hadi kiwango chake cha sasa cha 2.5% (2015-2020), na inabashiriwa kupungua hadi 1.65% kila mwaka ifikapo 2050 (UNDESA, 2019b, uk. 58- 59). Nguvu za uzazi ziliongezeka kutoka miaka ya 1950 hadi kiwango cha juu zaidi mwanzoni mwa miaka ya 1980 (1980-1985) ambapo wastani wa watoto 6.7 walizaliwa kwa kila mwanamke, na baada ya hapo idadi hiyo ilipungua sana hadi watoto 4.51 kwa kila mwanamke (kati ya 2015-2020) (UNDESA, 2019b, uk. 138-139). Kama hali ilivyo kote Afrika, idadi ya watu wa Guinea-Bissau ni ya watu wachanga: Umri wa wastani wa jumla ya watu ni miaka 18.8 (2020; nchi za Afrika za kusini ya Jangwa la Sahara: miaka 18.7¹⁹; UNDESA, 2020). Vijana hawa wanahitaji fursa za elimu na ustawi wa ajira, kitu ambacho nchi hii haifanikishi kwa urahisi.

UNESCO inatumia maneno mazito ya kutajia mfumo wa shule za taifa hili “unaohitaji mageuzi makubwa” (UNESCO, 2016, uk. 1). Ujuzi wa watu wengi “ni wa chini sana kiasi kwamba mata-rajio ya nchi hii kujiinua kiuchumi [na kupunguza umaskini] ni hafifu sana” (UNESCO, 2016, uk. 1). Familia zinazozongwa na maskini kama shirika la Viwango vya Umaskini (MPI) linavyozitaja (tazama hapo awali), hutatizika pakubwa na gharama ya juu ya elimu nchini humo. Hebu fikiria mama wa watoto watatu, akipata pesa kama mfanyakazi wa nyumbani, wakati mwingine akikosa kulipwa ujira wake, kumudu — au kudaiwa wakati hana uwezo wa kulipa — ada ya masomo, chakula cha shule na sare za watoto katika shule za kibinafsi (tazama video za makala ya Chantal Beil, Pendekezo la darasani, hapo awali). Guinea-Bissau, jinsi UNESCO inavyobainisha, ina “kiwango cha chini sana cha upataji elimu” (UNESCO, 2016, uk. 2).

Takriban nusu ya watoto wote wenye umri wa miaka sita na karibu theluthi moja ya watoto kati ya miaka sita na 11 “hawajawahi kuhudhuria shule” (Benki ya Dunia, 2018b, uk. 74; data kutoka 2014). Katika maeneo ya vijijini, na kwa familia maskini, hali ni mbaya hata zaidi: Miongoni mwa wale wanaoenda shule, viwango vya kuacha shule “vimeongezeka polepole kutoka asilimia tano hadi 44% kati ya umri wa miaka 12 na 24” (Benki ya Dunia, 2018b, uk. 74). Takriban

19 Kwa kulinganisha, umri wa jumla wa watu barani Ulaya ni miaka 42.5, nalo bara la Amerika ya Kusini na Caribbean ni miaka 31 (UNDESA, 2020).

40% ya wanafunzi wenye umri wa miaka sita hadi 11 katika maeneo ya mashambani hawajawahi kuhudhuria shule — ukilinganisha na 12% katika maeneo ya mijini (Benki ya Dunia, 2018b, uk. 74-75). Viwango vya jumla vya wanaohudhuria shule za sekondari ni chini ya 25% katika baadhi ya mikoa — ikilinganishwa na 115 %²⁰ jijini Bissau (Benki ya Dunia, 2018b, uk. 73). Makundi matatu yaliyo katika hali mbovu zaidi kielimu ni wasichana, watoto katika maeneo ya mashambani na tabaka la watu wenye kipato cha chini, ambapo matumizi ya serikali “huelekea kupendelea familia tajiri zaidi” (Benki ya Dunia, 2018b, uk. 76).

Walimu nao wananyimwa maarifa na malipo. Wafanyakazi wapya walioajiriwa na serikali 2013 walilipwa kwa miezi sita pekee, hali ambayo ni ya kawaida. Mara kwa mara, walimu hugoma wakidai malipo yao au wanafunzi kugoma wakilalamikia migomo ya walimu (AfricaNews, 2019). Matokeo ya ujifunzaji ni duni pia kutokana na tamrini duni ya walimu. Mpango wa Kikanda wa Uchambuzi wa Mifumo ya Elimu (PASEC) uligundua kuwa karibu 94% ya walimu wa darasa la tano hawawezi kujibu maswali yote katika lugha ya Kireno — lugha ya kufundishia — na 98% katika hisabati (Benki ya Dunia, 2018b, uk. 76).

Kutokana na ukosefu huu wa fursa, vijana huota kupata maisha mazuri mahali kwingine, kama Bordonaro (2009) anavyofichua. Anaeleza matumaini ya vijana kutoka visiwa vya Bijagó ambao wanataka kuwa wa kisasa, na usasa “Unapatikana kwingineko” (Ramsey-Kurz & Ganapathy-Doré, 2011; ona Moduli ya 7). Kwa vijana wa Bissau waliosawiriwa na Vigh (2006), “uhamiaji ni miongoni mwa ‘mbinu nyepesi zaidi’ za kuepuka kutengwa na jamii na kupuuzwa” (Bordonaro, 2009, uk. 135). Ulaya ndiyo mahali panapotamaniwa zaidi: “Njia pendwa za uhamaji zinaelekea Bissau, Dakar, Conakry, lakini ndoto kuu ya kila mtu bado ni Ulaya [...] pakitajwa kama chemchemi ya uwezo na utajiri” (Bordonaro, 2009, uk. 135). Maono yao yanaendelea kufasiri kuwa barani Ulaya kuna fursa za mapato ambazo nchi yao haitoi — kiwango chake cha ukosefu wa ajira cha asilimia sita kikizidi kuongezeka maradufu kwa vijana (12%; Data Migration Portal, 2020). Inatarajiwa kwamba “huko”, Ulaya, ni rahisi sana kupata pesa nzuri, na “chaguo pekee la kuwa mtu anayeweza kutambuliwa na jamii” (Bordonaro, 2009, uk. 135). Bordonaro (2009) na Lundy (2018) wanapendekeza kuwa kuna uwezekano mkubwa uhamiaji umekuwa sawa na tohara kwa wavulana. Vilevile, Schrover, & Moloney (2013, uk. 17), wanaitaja “tamaa ya kutalii” ambayo hujenga “desturi ya uhamiaji” kama hatua ya kawaida ya maisha ya watu wazima. Tohara ya kitamaduni ya Balanta, kwa mfano, inajumuisha desturi kadhaa kama vile mashindano kwenye ngoma za mavuno, mashindano ya mieleka, kuiba ng’ombe, kutahiri, na mengineyo, kabla ya wazee kuamua wakati umefika kwa kijana fulani kushiriki katika shughuli hatari ya ‘heshima’. Kijana huyo hukaa miezi miwili msituni, wakati huo akiwa katika hatari ya kiroho ya “kuathiriwa na mashambulizi ya uchawi” kutoka kwa maadui (Lundy, 2018, uk. 10). Uhamiaji wa kimataifa, Lundy (2018) anakisia, unaweza kuwa nafasi mpya ya kudhihirisha utu

20 Gross attendance ratio (GAR) yaani ngawira ya mahudhuro (shuleni) ya jumla «inaweza kuzidi 100% kutokana na kujumuishwa kwa wanafunzi waliozidi umri wa kawaida na wale walio na umri wa chini. Sababu zake — ni pamoja na kujiunga mapema au kuchelewa kujiunga shule, mbali na marudio ya darasa. Kuhusu elimu ya juu, GAR inaweza kuzidi 100% kutokana na kujumuishwa kwa wanafunzi wa nje ya rika la umri wa miaka 5, kuanzia umri rasmi wa kuhitimu shule ya sekondari» (UNESCO UIS, 2021).

uzima wa vijana hao wa kiume, hali inayolingana sana na mawazo ya kupata uraia wa kimataifa. Hata hivyo, uhamiaji ni ‘anasa’ ambayo ni wachache tu wanaoweza kumudu nchini Guinea-Bissau. Carling (2002) amebuni istilahi ya ‘ulemavu usio wa hiari’, ambayo bado haijaingia kwenye mabuku ya uhamiaji.

Sababu teule za kimuktadha 3: Kuvutwa hadi Bissau

Kwa kuzingatia “pengo la utekelezaji” wa sera na fasiri ijayo ya AU kuhusu wakimbizi (tazama Moduli 9), ni jambo la kupigiwa mifano kuwa Guinea-Bissau inaongoza barani Afrika katika kuwachukua watu wasio na uraia. Mjumbe wa UNHCR jijini Bissau aliusifu “uamuzi wa kipekee [...] ambao haujawahi kutokea katika ukanda wa Afrika Magharibi na ninaweza kusema hata ulimwenguni kote” (UNIOGBIS, 2018, uk. 1, 6). Suluhu ilipatikana kwa wakimbizi ambao walikuwa wakiishi nchini humo kwa takribani miaka 20. Ombi la UNHCR la kuwapa uraia wakimbizi wote wa Senegal lilikubaliwa 2018. Takriban wakimbizi 7,000 wa Senegal waliotoroka mgogoro wa Casamance walipewa hati za utambulisho halali; na wakimbizi kutoka Liberia na Sierra Leone pia wamejumuishwa katika makubaliano kati ya UNHCR na Serikali ya Guinea-Bissau. (UNIOGBIS, 2018, uk. 6).

Sababu kadhaa zinaifanya Guinea-Bissau kuwa nchi chaguo la kuishi au mahali pa kupitia wahamiaji hao, wakimbizi na wanaotafuta hifadhi kutoka eneo hilo; kwa mfano, kuwapo amani ya kuridhisha kutokana na kukosekana kwa migogoro mikubwa. Mlipuko mkubwa zaidi wa Ebola katika historia uliepuka jiji la Bissau huku ukivuruga eneo la Afrika Magharibi (Gamma na wengine, 2017) na hata Uviko-19 haikuathiri Guinea-Bissau kama ilivyoathiri nchi nyingine barani Afrika (WHO, 2020). Mwisho, uhuru wa kutembea bila ada ndani ya jumuiya ya ECOWAS huwezesha uhamiaji (Adepoju na wengine, 2010).



ZOEZI LILILOPENDEKEZWA LA KUSHUGHULIKIA STADI ZA UTAMBUZI ZA KUTEKELEZA, NA STADI ZA MITAZAMO YA KIBINAFSI NA MAADILI ZA KUJIBU:

Wape washiriki zoezi la kutambua na kutaja vipengele viwili vya muktadha vilivyochaguliwa — sababu mbili-mbili kinzani au mseto wa kila jozi moja kati ya mbili hizo — kwa Guinea-Bissau.

- Ili kubainisha sababu hizo mbili za muktadha, washiriki wanaweza kutumia Moduli 3 ya mwongozo huu. Bora zaidi, washiriki pia wabuni sababu mbili mpya za muktadha kwani uorodheshaji wa Moduli 3 si jumuishi.
- Wakizifafanua hali zinazowafanya watu wa Guinea-Bissau kuondoka makwao na watu wengine nao kuelekea Guinea-Bissau, washiriki watachunguza ripoti za vyombo vya habari au nakala za thibitisho.
- Wakiwasilisha sababu zao za kimuktadha zilizowasilishwa kwa wote katika hadhira, washiriki watajaribu kuleta uwiano kati ya nadharia na kipengele cha binadamu kinachoangaziwa.

Kwa hatua yake ya kuwapa uraia watu wasio na uraia, nchi hii imegeuka kuwa habari njema sana katika Ripoti ya Uhamiaji Duniani 2020 na vyombo vya habari (IOM, 2019c, uk. 41; Maclean, 2018).



KAZI YA ZIADA ILIYOPENDEKEZWA YA KUSHUGHULIKIA STADI ZA MITAZAMO YA KIBINAFSI NA MAADILI ZA KUJIBU, NA STADI ZA UTAMBUZI ZA KUTEKELEZA NA KUCHANGANUA:

Waombe washiriki wako wajenge hoja ya kuhamia au kutafuta hifadhi nchini Guinea-Bissau.

- Kuangalia marejeleo yaliyotangulizwa, kwa mfano, Tovuti ya Data ya Uhamiaji (Migration Data Portal, 2020), Viashiria vya Ustawi wa Watu (UNDP, 2020b) au ripoti za vyombo vya habari (The New Humanitarian, 2020).
- Zingatia hali ya watu wasio na uraia. Nchi walikotoka wahamiaji hao au watu waliohamishwa kwa lazima kwa muda mfupi, kwa kutumia marejeleo yaliyo hapo juu.
- Jenga hoja kuhusu kwa nini Bissau inavutia kama nchi chaguo la watu hao, tumia picha, video au vifaa vinginevyo.

Kwa mfano, labda mtu kutoka Cameroon anathamini amani hiyo ya kuridhisha? Je, mtu kutoka Mali anafurahia fursa ya kujipa riziki kwa kazi ya uvuvi? Mtu kutoka Ureno anaingiliana kwa urahisi na wenyeji kwa sababu lugha hiyo hiyo rasmi inazungumzwa nao pia? Onyesha kuwa nchi iliyotikiswa na misukosuko ya kisiasa na ustawi duni wa binadamu pamoja na huduma duni ina uwezo wa kuvutia watu kutoka nje ya mipaka yake.

ZOEZI LILILOPENDEKEZWA LA KUSHUGHULIKIA STADI ZA UTAMBUZI ZA KUELEWA NA KUTATHMINI:

Pata ripoti kuhusu Guinea-Bissau katika vyombo vya habari vya nchini au kimataifa na uwape wanafunzi wenzako ripoti moja. Kila mshiriki anapaswa kuandika tahakiki ya ukurasa mmoja ya kazi za uanahabari katika vyombo vya habari, akitathmini ubora.



USOMAJI WA ZIADA:

Kiakademia:

Abreu, A. J. (2012). *Migration and Development in contemporary Guinea-Bissau: A Political Economy Approach*. (PhD Thesis). London, UK: SOAS, University of London.

Kiuanahabari:

DW reports regularly on developments in Guinea-Bissau in English and the official language of Guinea-Bissau, Portuguese (DW, 2020).

Kitaasisi:

World Bank (2016). *Guinea-Bissau: Turning challenges into opportunities for poverty reduction and inclusive growth: Systematic country diagnostic (SCD)*. (Report No. 106725-GB). Washington, D.C. Retrieved November 18, 2020, from <https://openknowledge.worldbank.org/bitstream/handle/10986/24695/Guinea0Bissau00try0diagnostic00SCDO.pdf?sequence=1&isAllowed=y>

Marejeleo

Abdenur, A. E., & Neto, D. M. (2013). South-South cooperation and democracy in Africa: Brazil's role in Guinea-Bissau. *Africa Review*, 5(2), 104-117. <https://doi.org/10.1080/09744053.2013.855356>

Abdenur, A. E., & Neto, D. M. d. S. (2014). Brazil and African security. In Tjønneland, E. N. (Ed.), *Rising powers and the African security landscape* (pp. 49-77). Oslo: Chr. Michelsen Institute (CMI). Retrieved December 9, 2020, from <https://www.cmi.no/publications/file/5271-rising-powers-and-the-african-security-landscape.pdf>

Abel, G. J., Barakat, B., Kc, S., & Lutz, W. (2016). Meeting the Sustainable Development Goals leads to lower world population growth. *Proceedings of the National Academy of Sciences of the United States of America*, 113(50), 14294-14299. <https://doi.org/10.1073/pnas.1611386113>

Abreu, A. J. (2012). *Migration and Development in contemporary Guinea-Bissau: A Political Economy Approach*. (PhD Thesis). London, UK: SOAS, University of London.

Adepoju, A., Boulton, A., & Levin, M. (2010). Promoting integration through mobility: Free movement under ECOWAS. *Refugee Survey Quarterly*, 29(3), 120-144. <https://doi.org/10.1093/rsq/hdq032>

AfricaNews (September 2, 2019). *Guinea-Bissau: Students protest over threat by teachers to strike*. [Television broadcast]. Retrieved November 16, 2020, from <https://www.africanews.com/2019/02/09/guinea-bissau-students-protest-over-threat-by-teachers-to-strike/>

- Bordonaro, L. (2009). Sai fora: youth, disconnectedness and aspiration to mobility in the Bijagó Islands (Guinea-Bissau). *Etnografica*, 13, 125-141. <https://doi.org/10.4000/etnografica.1253>
- Brasil, A. (2020, January 25). Interview by M. Lengauer. Bissau, Guinea-Bissau, and Dortmund, Germany.
- Capucha, L., Calado, A., & Estêvão, P. (2016). Migration, ethnicity and resilience: Portuguese National Report. Instituto Universitário de Lisboa. Retrieved December 2, 2020, from https://repositorio.iscte-iul.pt/bitstream/10071/12303/1/other_WP10_Portuguese_National_Report.pdf
- Carling, J. (2002). Migration in the age of involuntary immobility: Theoretical reflections and Cape Verdean experiences. *Journal of Ethnic and Migration Studies*, 28(1), 5-42. <https://doi.org/10.1080/13691830120103912>
- CPLP (2020). Community of Portuguese Speaking Countries. Retrieved November 26, 2020, from <https://www.cplp.org/>
- DW (2020). Guiné-Bissau. Retrieved November 27, 2020, from <https://www.dw.com/pt-002/not%C3%ADcias/guin%C3%A9-bissau/s-30382>
- ECOWAS (2016). Basic information. Retrieved November 15, 2020, from <https://www.ecowas.int/about-ecowas/basic-information/>
- Einarsdóttir, J., & Boiro, H. (2016). Becoming somebody: Bissau-Guinean talibés in Senegal. *The International Journal of Human Rights*, 20(7), 857-874. <https://doi.org/10.1080/13642987.2016.1192532>
- EMN (2018). Asylum and migration: Glossary 6.0. Brussels. Retrieved November 27, 2020, from https://www.emn.at/wp-content/uploads/2018/06/emn-glossary-6-0_en.pdf
- EU, & IOM (2020). EU-IOM Joint Initiative: Guinea Bissau. Retrieved June 9, 2020, from <https://migrationjointinitiative.org/countries/sahel-and-lake-chad/guinea-bissau>
- European Union (2020). Portugal: Children of migrants now have easier access to citizenship. Retrieved November 15, 2020, from <https://ec.europa.eu/migrant-integration/news/portugal-children-of-migrants-now-have-easier-access-to-citizenship>
- Eurostat (2020). Statistics: Asylum applicants. Retrieved November 16, 2020, from https://ec.europa.eu/eurostat/databrowser/view/MIGR_ASYAPPCTZA__custom_215193/default/table?lang=en
- Gama, W. (2020). Bala Djamanca: The successful reintegration of a child in Guinea-Bissau. UNICEF. Retrieved November 20, 2020, from <https://www.unicef.org/guineabissau/stories/bala-djamanca>
- Gamma, A. E., Slekiene, J., Medeazza, G., Asplund, F., Cardoso, P., & Mosler, H.-J. (2017). Contextual and psycho-social factors predicting Ebola prevention behaviours using the RANAS approach to behaviour change in Guinea-Bissau. *BMC Public Health*, 17(1), 446. <https://doi.org/10.1186/s12889-017-4360-2>
- IDMC (2020). Country profile: Guinea-Bissau. Retrieved December 8, 2019, from <http://www.internal-displacement.org/countries/guinea-bissau>
- IMF, & Government of Guinea-Bissau (2011). Second National Poverty Reduction Strategy Paper. Retrieved November 27, 2020, from <https://www.imf.org/external/pubs/ft/scr/2011/cr11353.pdf>
- IOM (2018). Guinea-Bissau: Overview. Retrieved November 15, 2020, from <https://www.iom.int/countries/guinea-bissau>
- IOM (2019a). Glossary on Migration. Geneva. Retrieved August 5, 2019, from https://publications.iom.int/system/files/pdf/iml_34_glossary.pdf
- IOM (2019b). Towards the sustainable reintegration of returned migrants: Cash for work activities in Guinea Bissau. Retrieved June 3, 2020, from <https://www.iom.int/news/towards-sustainable-reintegration-returned-migrants-cash-work-activities-guinea-bissau>

- IOM (2019c). World Migration Report 2020. Retrieved November 30, 2019, from https://publications.iom.int/system/files/pdf/wmr_2020.pdf
- Lobban, R. (1974). Guinea-Bissau: 24 September 1973 and beyond. *Africa Today*, 21(1), 15-24.
- Lundy, B. D. (2018). Challenging adulthood: Changing initiation rites among the Balanta of Guinea-Bissau. *African Studies*, 77(4), 584-606. <https://doi.org/10.1080/00020184.2018.1496598>
- Maclean, R. (2018, October 10). "Complete equality": Refugees find a home – and citizenship in Guinea-Bissau. *The Guardian*. Retrieved November 27, 2020, from <https://www.theguardian.com/world/2018/oct/10/guinea-bissau-refugee-naturalisation-scheme>
- Migration Data Portal (2020). Guinea-Bissau. Retrieved July 31, 2020, from https://migrationdataportal.org/?i=stock_abs_&t=2019&cm49=624
- Ocrisse-Aka, F. & Bossard, L. (2006). Languages. ECOWAS, SWAC, & OECD (Eds.), *Atlas on Regional Integration in West Africa: Population series*. Retrieved November 27, 2020, from OECD website: <https://www.oecd.org/swac/publications/38409537.pdf>
- OPHI (2019). Country Briefing: Guinea-Bissau. Oxford. Retrieved November 16, 2020, from https://ophi.org.uk/wp-content/uploads/CB_GNB_2019_2.pdf
- OPHI, & UNDP (2018). *Global Multidimensional Poverty Index 2018: The most detailed picture to date of the world's poorest people*. Oxford. Received December 5, 2020, from https://ophi.org.uk/wp-content/uploads/G-MPI_2018_2ed_web.pdf
- Phillips, D. (2018, May 23). No food, no water: African migrants recount terrifying Atlantic crossing. *The Guardian*. Retrieved June 3, 2020, from <https://www.theguardian.com/world/2018/may/22/african-migrant-brazil-boat-rescue-atlantic-crossing>
- Portugal Visa Application Centre in Guinea-Bissau, & VFS Global (2020). Apply for visa to Portugal in Guinea-Bissau. Retrieved November 27, 2020, from <https://www.vfsglobal.com/portugal/guinea-bissau/English/Visa-Types.html>
- Ramsey-Kurz, H., & Ganapathy-Doré, G. (2011). *Projections of paradise in migrant writing*. Amsterdam: Rodopi.
- Sachs, J., Schmidt-Traub, G., Kroll, C., Lafortune, G., Fuller, G., & Woelm, F. (2020). *The Sustainable Development Report 2020: The Sustainable Development Goals and Covid-19*. Cambridge: Cambridge University Press. Retrieved December 2, 2020, from https://s3.amazonaws.com/sustainabledevelopmentreport/2020/2020_sustainable_development_report.pdf
- Scarabello, S. (2019). *Diaspora mapping: Profile of The Gambia, Guinea and Guinea-Bissau diasporas in Italy*. Rome: IOM. Retrieved December 1, 2020, from https://publications.iom.int/system/files/pdf/diaspora_mapping_italy_2019.pdf
- Schengen Visa Info (2020). Portugal grants migrants and asylum seekers full citizenship rights during Covid-19 outbreak. Retrieved November 15, 2020, from <https://www.schengenvisainfo.com/news/portugal-grants-migrants-and-asylum-seekers-full-citizenship-rights-during-covid-19/>
- Schrover, M., & Moloney, D. M. (2013). Introduction: Making a difference. In Schrover, M. & Moloney, D. M. (Eds.), *Gender, migration and categorisation: Making distinctions between migrants in Western countries, 1945-2010* (pp. 7-53). Amsterdam: Amsterdam University Press.
- Shaw, M., & Gomes, A. (2020). *Breaking the vicious cycle: Cocaine politics in Guinea-Bissau*. Geneva. Retrieved June 2, 2020, from https://globalinitiative.net/wp-content/uploads/2020/05/Guinea-Bissau_Policy-Brief_Final2.pdf
- Shryock, R. (2020, May 28). Cocaine and Guinea-Bissau: How Africa's 'narco-state' is trying to kick its habit. *BBC News*. Retrieved November 27, 2020, from <https://www.bbc.com/news/world-africa-52569130>
- Temudo, M. P. (2009). *From the margins of the state to the presidential palace: The Balanta case in Guinea-*

Bissau. *African Studies Review*, 52(2), 47-67. <https://doi.org/10.1353/arw.0.0203>

The New Humanitarian (2020). The global migrant & refugee crisis: Migration. An in-depth collection of global reporting on refugees, asylum seekers, migrants, and internally displaced people. Retrieved May 12, 2020, from <https://www.thenewhumanitarian.org/migration>

UNdata (2019). Country profile: Guinea-Bissau. Retrieved November 27, 2020, from <https://data.un.org/en/iso/gw.html>

UNDESA (n. d.). Sustainable Development Goal 3. Retrieved December 2, 2020, from <https://sdgs.un.org/goals/goal3>

UNDESA (2019a). Total migrant stock 2019: Migrant stock at mid-year by sex and by major area, region, country or area, 1990-2019. Retrieved December 5, 2020, from <https://www.un.org/en/development/desa/population/migration/data/estimates2/estimates19.asp>

UNDESA (2019b). World Population Prospects 2019, Volume I: Comprehensive Tables. New York. Retrieved July 30, 2020, from https://population.un.org/wpp/Publications/Files/WPP2019_Volume-I_Comprehensive-Tables.pdf

UNDESA (2020). World population prospects: Median age of the total population (years): Guinea-Bissau, sub-Saharan Africa, Europe, Latin America and the Caribbean. Retrieved November 16, 2020, from <https://population.un.org/wpp/DataQuery/>

UNDP (2019a). Country Profile Guinea-Bissau: Human Development Indicators. Retrieved June 4, 2020, from <http://hdr.undp.org/en/countries/profiles/GNB>

UNDP (2019b). Human development indicators. Retrieved June 1, 2020, from <http://hdr.undp.org/en/content/statistical-data-tables-7-15>

UNDP (2019c). Human Development Report 2019: Beyond income, beyond averages, beyond today: Inequalities in human development in the 21st century (Human Development Reports). New York. Retrieved March 10, 2020, from <http://hdr.undp.org/sites/default/files/hdr2019.pdf>

UNESCO (2016). A major overhaul of the Guinea-Bissau education system is well overdue (Country Note No. 26). Retrieved November 27, 2020, from <https://unesdoc.unesco.org/ark:/48223/pf0000247043>

UNESCO UIS (2021). Glossary: Gross Attendance Ratio. Retrieved January 5, 2021, from <http://uis.unesco.org/en/glossary-term/gross-attendance-ratio>

UNHCR (2020a). Refugee Data Finder: Asylum seekers in Guinea-Bissau from selected West African countries. Retrieved November 15, 2020, from <https://www.unhcr.org/refugee-statistics/download/?url=6q5M0I>

UNHCR (2020b). Refugee Data Finder: IDPs 1951-2020, country of origin Guinea-Bissau. Retrieved December 9, 2020, from <https://www.unhcr.org/refugee-statistics/download/?url=yvT8w4>

UNIOGBIS (2018). Our mandate includes helping those who have no country: The UNHCR Representative in Guinea-Bissau, Mamadou Diop, explained the mandate of this UN agency. Bissau, Guinea-Bissau. Retrieved November 14, 2020, from https://uniogbis.unmissions.org/sites/default/files/i_kuma_eng.pdf

UNIOGBIS (2020). Guinea-Bissau: Country profile. Retrieved November 14, 2020, from <https://uniogbis.unmissions.org/en/country-profile>

US Department of State (2020). Telephonic Press Briefing on drug trafficking in Africa: Heather Merritt, Deputy Assistant Secretary of State for the Bureau of International Narcotics and Law Enforcement Affairs. Retrieved November 15, 2020, from <https://2017-2021-translations.state.gov/2020/07/21/telephonic-press-briefing-on-drug-trafficking-in-africa/index.html>

Vigh, H. E. (2006). Navigating terrains of war: Youth and soldiering in Guinea-Bissau. New York: Berghahn.

WHO (2020). COVID-19 in the WHO African region. Retrieved November 14, 2020, from <https://who.maps>.

arcgis.com/apps/opstdashboard/index.html#/Oc9b3a8b68d0437a8cf28581e9c063a9

World Bank (2016). Guinea-Bissau: Turning challenges into opportunities for poverty reduction and inclusive growth: Systematic country diagnostic (SCD) (Report No. 106725-GB). Washington, D.C. Retrieved November 18, 2020, from https://openknowledge.worldbank.org/bitstream/handle/10986/24695/Guinea0Bissau00try0diagnostic_00SCD0.pdf?sequence=1&isAllowed=y

World Bank (2018a). Piecing together the poverty puzzle: Poverty and shared prosperity 2018. Washington, D.C. Retrieved June 4, 2020, from <https://openknowledge.worldbank.org/bitstream/handle/10986/30418/9781464813306.pdf>

World Bank (2018b). Seizing the moment: Managing public finance for development. Retrieved November 27, 2020, from <https://elibrary.worldbank.org/doi/pdf/10.1596/32004>

World Bank (2018c). Does monetary poverty capture all aspects of poverty? Retrieved June 4, 2020, from <https://blogs.worldbank.org/developmenttalk/does-monetary-poverty-capture-all-aspects-poverty>

World Bank (2020a). Poverty & Equity Data Portal. Retrieved November 27, 2020, from <http://povertydata.worldbank.org/poverty/country/GNB>

World Bank (2020b). Poverty: Overview. Retrieved November 27, 2020, from <https://www.worldbank.org/en/topic/poverty/overview>

Young, C. (2017, January 23). Ethnicity and politics. Oxford Bibliographies. DOI: 10.1093/OBO/9780199846733-0152



MODULI 7

Uchanganuzi wa kifani wa Cameroon (Afrika ya Kati)

na Monika Lengauer na Johanna Mack



MALENGO YA MODULI

- Kuuelewa uchanganuzi kifani wa taifa la Afrika linalotumia lugha mbili rasmi.
- Kuwasilisha masuala yaliyochaguliwa kimuktadha kuhusu nchi iliyoathirika na mizozano miwili mikali.
- Kuleta hisia za hadithi za ubinadamu zilizofichika nyuma ya takwimu.



MATOKEO YA MAFUNZO

Kufikia mwisho wa moduli hii, kuambatana na changanuzi kifani za awali ili zote zisawazishwe kimataifa, washiriki wanapaswa:

- Kujadili kwa kina chaguo za wahamiaji na mahitimisho ya wakimbizi. → **Matokeo ya mafunzo kwa stadi za mitazamo binafsi na maadili: Kujibu**
- Kuwasiliana vilivyo na washiriki juu ya haja ya wanachopaswa kujua kuhusu uhamiaji na uhamishwaji wa kulazimishwa ili wawe na uwezo wa kufanya maamuzi yenye ufahamu. → **Matokeo ya mafunzo kwa stadi za utambuzi: Kuelewa**
- Kuunda na kutekeleza maelezo mafupi ya nchi, vilevile maelezo mafupi kuhusu uhamiaji na uhamishwaji wa kulazimishwa, kwa kutumia ufahamu na hazinadata. → **Matokeo ya mafunzo kwa stadi za utambuzi: Utekelezaji**
- Kuchanganua – kwa mtazamo wa kimataifa – uchanganuzi wa kifani wa Cameroon. → **Matokeo ya mafunzo kwa stadi za utambuzi: Uchanganuzi**

Muhtasari

Cameroon ni nchi ya kipekee inayojumuisha historia ya mataifa ya Afrika yanayozungumza Kiingereza na Kifaransa. Kutokana na muundo wake unaotokana na historia ya ukoloni wa Uingereza na ukoloni wa Ufaransa, mbali na kuwa taifa linalotumia rasmi lugha mbili za kimataifa, hii leo Cameroon ina mifumo miwili ya kisheria, kielimu na fani za uanahabari. Kutokana na utofauti wake kikabila, kitamaduni na kijiografia — Cameroon ni nyumbani kwa zaidi ya makabila 200 tofauti — nchi hii mara nyingi hufahamika kama Africa in miniature kumaanisha Afrika kama sanamu au picha ndogo. Kinachofunika utofauti wa kikabila wa Cameroon, ni taifa lililogawanyika kutokana na historia yake ya kikoloni (MRGI, 2020) inayoiunganisha na visa vingi vya uhamiaji wa ndani kwa ndani. Nyamnjoh (2010) anaripoti kwamba vyombo vya habari vya Cameroon kila mara hukuza utambulisho wa kikabila, suala ambalo ni kizingiti katika ujenzi wa taifa. Cameroon ina historia ya uhamiaji huku ikiakisi masuala mbali mbali kama vile uthabiti na ufanisi wa kiu-chumi, angaa kulingana na miaka ya awali (mapema katika miaka ya 1950, mwisho wa miaka ya 1960, 1970) na kuhusiana na mataifa jirani (International Crisis Group, 2010). Masuala haya yalivutia wafanyakazi wahamiaji na wakimbizi hasa kutoka Afrika ya Kati na Magharibi. Katika miaka iliyopita, watu wamekuwa wakitoroka waasi wa Boko Haram nchini Nigeria, na kutokana na vita na migogoro katika mataifa ya Central African Republic, Chad na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, wamekuwa na wanaendelea kuishi hapa (Udelsmann Rodrigues & Tomàs, 2012).

Cameroon inaakisi masuala muhimu yanayowasukuma watu kuhama na/au kutafuta makazi kwingineko ikiwa ni pamoja na mizozo, ugaidi, siasa zinazopingwa na uhuru duni wa vyombo vya habari. Cameroon pia inakumbwa na tatizo la dhuluma za kijinsia, viwango vya juu vya ukosefu wa ajira, asilimia kubwa ya idadi ya vijana inayozidi kuongezeka huku fursa za kujipatia riziki na kujiendeleza zikiwa finyu, viwango vya juu vya umaskini na muunganisho muhimu wa raia wake sehemu nyingine (IOM, 2009, uk. 27-35; uk. 96). Mizozo miwili mikuu inachochea uhamiaji. Katika sehemu ya Kaskazini — eneo maskini zaidi nchini humo — waasi waliojihami wa Boko Haram wameenea kutoka Nigeria na wamekuwa wakiendeleza shughuli zao nchini Cameroon kutoka 2014. Migogoro katika maeneo ya Kaskazini Magharibi na Kusini Magharibi mwa nchi hii inawakilisha sababu ya pili ya uhamiaji. Migogoro hiyo ilianza 2016 serikali ilipowachukulia hatua kali waandamanaji katika eneo linalozungumza Kiingereza. Kufikia 2018, hali ilikuwa imezorota zaidi.

Maelezo mafupi kuhusu Cameroon

Cameroon iko eneo la katikati mwa Afrika,¹ Inapakana na Nigeria, Chad, Jamhuri ya Afrika ya Kati (Central African Republic), Congo, Gabon na Equatorial Guinea na inagawana mipaka ya pwani na Ghuba ya Guinea na Bahari ya Atlantic. Sehemu za nchi hii zilizokuwa chini ya mamla-ka ya kikoloni ya Ufaransa, zilipata uhuru 1960. Maeneo ambayo hii leo ni mikoa ya Magharibi (Kaskazini Magharibi na Kusini Magharibi) ilipiga kura za kujikomboa kutoka kwa utawala wa Uingereza mwaka mmoja baadaye na kuunda shirikisho na sehemu ya Cameroon inayozungu-mza Kifaransa. Cameroon ina watu milioni 26 na ndilo taifa la pili lenye idadi kubwa ya watu miongoni mwa majirani wake wa moja kwa moja (kati ya Nigeria iliyo na idadi ya watu milioni 206 na Chad iliyo na watu milioni 16; UNDESA 2019a, uk. 23-35). Sawa na mambo yalivyo katika mataifa mengine ya Afrika, idadi kubwa ya watu nchini Cameroon ni changa: Umri was-tani wa idadi jumla ya watu nchini humo ni miaka 19 (kuambatana na mataifa ya Afrika yaliyo kusini ya Jangwa la Sahara² UNDESA, 2020). Idadi ya watu huongezeka kwa 2.61% kila mwaka (2015-2020) pia inaambatana na wastani wa mataifa yaliyo kusini ya Jangwa la Sahara (pasipo kujumuisha nchi zenye mapato ya juu; World Bank, 2020 f; UNDESA 2019a, 57). Kiwango cha watoto 4.6 wanazaliwa wakiwa hai kwa kila mwanamke, chini kidogo ikilinganishwa na wastani wa mataifa ya kusini ya Jangwa la Saharan (pasipo kuhusisha mataifa yenye mapato ya juu) ya 4.72 na maradufu ikilinganishwa na viwango vya ulimwengu vya watoto 2.47 kwa kila mwa-namke (2015-2020). Viwango hivi vimepungua kutoka watoto 5.75 kwa kila mwanamke (1995-2000) (UNDESA 2019a, 137; World Bank, 2020b). Mwaka wa 2018, umri ambao wanawake walitarajiwa kuishi nchini humo ulikuwa miaka 60 (ikilinganishwa na miaka 63 katika mataifa Afrika yaliyo kusini ya Jangwa la Sahara, pasipo kuhusisha mataifa yenye mapato ya juu), kwa wanaume, ilikuwa miaka 58 (ikilinganishwa na miaka 59 katika mataifa yaliyo kusini ya Jangwa

1 Zingatia fasiri tofauti za Afrika ya Kati (wakati fulani imetajwa kama Afrika ya Katikati): Eneo hili linajumuisha Came-roon, Jamhuri ya Afrika ya Kati, Chad, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Jamhuri ya Kongo, Equatorial Guinea na Gabon katika AfDB, wakati Umoja wa Mataifa pia unajumuisha Angola na São Tomé & Príncipe.

2 Kwa kulinganisha, umri wa wastani wa jumla ya watu barani Ulaya ni miaka 42.5, na Marekani ya Kusini na Karibea ni miaka 31 (UNDESA, 2020).

la Sahara, pasipo kuhusisha mataifa yenye mapato ya juu), ongezeko kutoka miaka 53 (wanawake) na 50 (wanaume) mnamo 2000 (UNDESA, 2019a, uk. 186-187; World Bank, 2020c; World Bank, 2020d). Hii inaonyesha ufanisi muhimu japo changamoto zinasalia: Viwango vya kupunguza umaskini vinasalia nyuma ya ongezeko la watu [...] idadi jumla ya watu maskini iliongezeka kwa 12% hadi milioni 8.1 kati ya 2007 na 2014”, na umaskini ulikolea katika maeneo ya Kaskazini, huku 56% ya watu maskini wakiishi hapa (World Bank, 2019). Ongezeko la idadi ya watu, na hasa vijana, linapaswa kufasiriwa katika muktadha wa ustawi wa kiuchumi ambao umesababishwa na mabadiliko ya muundo wa idadi ya watu Cameroon (African Union, 2017) na vijana wana maoni yao kuhusu jinsi ya kukabiliana na haya (Nyingi, 2019). Mwaka 2015, mtangazaji Richard Onanena wa kituo cha redio cha Kalak FM jijini Yaoundé, aliambia Benki ya Dunia kwamba “kuna haja kuu ya serikali kubadilisha mfumo wa elimu ili kuangazia suala la ukosefu wa ajira miongoni mwa vijana” (World Bank, 2015). Mwito huu wa kuhusisha vijana katika mipango na uundaji wa sera unasalia kuwa tu ajenda.

Mara nyingi vijana huchukulia fursa zao maishani kuwa finyu. Wimbo White Collar ulioimbwa na bendi maarufu Cameroon, Prolific Dream Revolution, unaangazia viwango vya hali ngumu ya kiuchumi na ugumu wa kufikia nafasi za kazi, na hivyo kusababisha hali duni ya maisha na usalama duni wa kijamii: *Man get degree for law ooohh, but ei di push ei na truck! /Man get masters for medicine eh, but ei di sell na achombo!!*³(Prolific Dream Revolution 237, 2018). Takriban asilimia sita ya vijana wa Cameroon (miaka 15 hadi 24) wamekuwa bila ajira katika kipindi cha mwongo mmoja uliopita, kiwango ambacho hata hivyo ni bora zaidi ya muktadha wa kusini mwa jangwa la Sahara ambapo viwango vya ukosefu wa ajira miongoni mwa vijana ni 12% tangu mwaka wa 2010 (World Bank, 2020e).

Mfumo wa kisiasa Cameroon ni wa serikali moja kuu inayoongozwa na rais aliye na mamlaka, wadhifa ambao mara ya kwanza ulishikiliwa na Ahmadou Ahidjo kutoka 1960 hadi 1982, kisha Paul Biya ambaye amesalia mamlakani kwa kipindi cha miongo minne iliyopita. Morse (2018) anaeleza kwamba mfumo wa uongozi nchini Cameroon ni wa “rais mwenye mamlaka” kulingana na kitabu chenye anwani “Resilience of African electoral authoritarianism” (Morse, 2018, uk. 114-115). Cameroon ina viwango vya chini vya demokrasia kuambatana na mlingano ulimwengu (nafasi 142 ya mataifa 167), ambapo mwaka 2020 ilishikilia nafasi ya chini tangu 2006 (EIU, 2020, uk. 10-14, 21, 43; V-Dem Institute, 2020; Bertelsmann Stiftung, 2020, uk. 5).

Vyama vya kisiasa vilihalalishwa 1990 baada ya “shinikizo la walio wengi na jamii ya kimataifa” (Morse, 2018, uk. 122). Vikomo vya kipindi cha rais kuhudumu viliondolewa 2008 (Bertelsmann Stiftung, 2020, uk. 5) ambapo baadaye rais aliweza kuwania tena urais na akathibitishwa katika chaguzi mbili za urais zilizofuatia za 2011 na 2018. Matokeo ya uchaguzi wa urais wa 2018 yangali yanabishaniwa, sawa na uchaguzi wa bunge na udiwani wa 2020, uchaguzi ambao ni chanzo cha mzoano (International Crisis Group, 2020). Wanaharakati wa utengano wa sehemu

3 “Mtu anapata digrii ya sheria lakini anaishia kuendesha lori. Mtu mwingine anapata Shahada ya Uzamili katika utabibu, lakini anaishia kuuza achombo” (maandazi ambayo huliwa kwa maharagwe au mchuzi; tafsiri ya waandishi).

inayozungumza Kiingereza walitoa mwito wa kususia uchaguzi huu. The Bertelsmann Stiftung (2020, 3) anaandika kwamba viwango vya kujitokeza kupiga kura katika maeneo yanayozungumza Kiingereza ilikuwa 10%, wakaguzi wengine wanaandika ni asilimia tano (International Crisis Group, 2020, uk. 9-10).

Cameroon ina utajiri mkubwa wa maliasili ikiwa ni pamoja na gesi, mafuta, madini, ardhi yenye rutuba na desturi ya nchi inayoruhusu upanzi wa mimea tofauti. Hata hivyo, nchi hii inaorodheshwa nambari 153 miongoni mwa nchi 180 katika orodha ya ufidiaji ya shirika la Transparency International (2020). Inashikilia nafasi ya chini katika kikundi cha ustawi wastani wa kibinadamu, huku ikiorodheshwa nambari 150 miongoni mwa nchi 189 (UNDP, 2019, uk. 300-303). Kwenye nakala ya Migration-development nexus, uhamishaji wa rasilimali za fedha na mali uliongezeka katika kipindi cha miongo miwili iliyopita, kutoka dola milioni 15 mwaka 1999, dola milioni 185 mwaka 2009 hadi dola milioni 334 mwaka 2019. Lakini ulipungua na kufikia takriban dola milioni 319 mwaka 2020 (World Bank, 2020g), hali inayodhaniwa kusababishwa na maradhi ya Uviko-19 (World Bank, 2020a). Pesa zinazotumwa nyumbani na raia walio nje zinawakilisha chini ya asilimia moja ya jumla ya mapato ya nchi - GDP (katika muktadha wa Afrika, hii ni thamani ya chini; World Bank, 2020g) huku zaidi ya robo ya washiriki katika uchunguzi wakiripoti kutegemea pesa hizo kwa njia moja au nyingine (McMahon & Kalantaryan, 2020, 14). Cameroon ni taifa la mapato ya wastani wa chini huku linalokumbwa na migogoro mikali ya kimaeneo. Umaskini, kwa mfano, umepungua katika maeneo ya Kaskazini, Kaskazini Magharibi na Kusini Magharibi.

Maelezo mafupi kuhusu uhamiaji

ipoti ya kwanza ya uhamiaji barani Afrika iliyochapishwa na AU na IOM, haielezi kwa kina kuhusu uhamiaji kutoka au kuelekea Cameroon. Inaonyesha tu kwamba “duniani, zaidi ya theluthi mbili za nchi za Afrika zilikuwa miongoni mwa mataifa 10 ya juu katika uhamiaji wa ndani kwa sababu ya migogoro”, ikiwa ni pamoja na Cameroon (Adepoju na wengine, 2020, uk. 54-55). Katika uchanganuzi wa Afrobarometer, “Updating the narrative about African migration” (Appiah-Nyamekye Sanny & Rocca, 2018)⁴, anahitimisha kwamba kwa wastani zaidi ya theluthi moja ya Waafrika (37%) wamewahi angalau kuwazia suala la kuhamia nchi nyingine, ikiwa ni pamoja na mmoja kwa kila Waafrika watano (18%) ambao hawajawazia suala hilo sana (angalia Moduli 9; Appiah-Nyamekye Sanny & Rocca, 2018)⁴. Washiriki wachache kutoka Cameroon (14%) kuliko kutoka nchi za Afrika za kusini ya Jangwa la Sahara (37%) wamelifikiria suala la uhamiaji (namba 13 ya 34 kwa Cameroon), asilimia 26% waliwazia kuhama “kiasi/kidogo” na 59% “sio hata kidogo” (Appiah-Nyamekye Sanny & Rocca, 2018, uk. 3; Appiah-Nyamekye Sanny na wengine, 2019, uk. 5).

4 Uchanganuzi huo unatokana na takwimu rasmi na tafiti zilizofanywa kati ya 2016 na 2018, zikiwasaili zaidi ya Waafrika 45,000 katika nchi 34 jinsi wanavyoona na kufikiria kuhusu uhamiaji kwa mujibu wa Appiah-Nyamekye Sanny & Rocca (2018, uk. 2).

Mwaka 2019, Cameroon ilikuwa na wahamiaji⁵ ya 506,000, ikiwakilisha asilimia mbili ya idadi ya watu, kidogo chini ya 2017 (540,000). Jumla ya kiwango cha uhamiaji — wahamiaji walioingia Cameroon ukitoa walioondoka – tofauti ya 24,000 (Migration Data Portal, 2021).

Uhamiaji: Kipindi cha uthabiti wa kisiasa na ufanisi wa kiuchumi katika nusu ya pili ya karne ya 20 kilivutia wafanyakazi wahamiaji, wahamiaji wa muda mfupi wa kila mara ama mduara⁶ na wale wa kudumu. Hali ilididimia katika miaka ya 2010 mizozo (Boko Haram; migogoro katika maeneo yanayozungumza Kiingereza) ilipoanza kudhoofisha uthabiti. Hata hivyo, uchunguzi wa Gallup katika mataifa 146 mwaka 2011 ulionyesha kwamba 84% ya washiriki kutoka Cameroon wanaamini nchi yao ni kimbilio nzuri la wakimbizi. Kauli hiyo inazidi viwango vya mataifa ya Afrika yaliyo kusini ya Jangwa la Sahara (66%) lakini bado eneo hili limeorodheshwa la tatu baada ya nchi za Marekani na Ulaya (Wu & Ray, 2012). Katika kielelezo cha furaha ulimwengu, pia, raia wa Cameroon wana matumaini (namba 98 ya 153), na nchi hiyo imeorodheshwa ya pili pamoja na Ivory Coast, Benin, Congo na Ghana (Helliwell na wengine, uk. 20-22).

Wakimbizi na wanaotafuta hifadhi Cameroon: UNHCR (2020a) inaripoti kuwepo kwa takriban wakimbizi milioni mbili Cameroon kufikia Novemba 2020, ikiwa ni pamoja na wakimbizi 430,000 kutoka mataifa matatu ya asili ya Jamhuri ya Afrika ya Kati (310,000), Nigeria (117,000) na Chad (2,000). Hata hivyo, wakimbizi hawatafuti makao nchini Cameroon (tazama Moduli 3 na Moduli 9). Kuna tofauti kubwa baina ya idadi kubwa ya wakimbizi na idadi ndogo ya watu wanaotafuta hifadhi: Mwaka 2019, wakimbizi 7,400 walitoka Jamhuri ya Afrika ya Kati, ilhali wakimbizi 293,000 kutoka Jamhuri ya Afrika ya Kati walisajiliwa chini ya mamlaka ya UNHCR. Vile vile kutoka Nigeria ni wakimbizi 54 pekee waliosajiliwa ikilinganishwa na wakimbizi 111,000 (UNHCR, 2020c). Shirika lisilo la serikali la Human Rights Watch linalalama kwamba kutotekeleza Mapatano ya Muungano wa Afrika kuhusu wakimbizi kwa kurejesha kwa lazima wakimbizi wa Nigeria tangu 2015 (Human Rights Watch, 2019a, uk. 118).

Wakimbizi wa ndani kwa ndani (IDPs): Takriban watu 710,000 chini ya mamlaka ya UNHCR wamepoteza makao kutokana na migogoro na vurugu katika maeneo ya Kaskazini Magharibi/Kusini Magharibi na 320,000 katika eneo la Kaskazini (UNHCR, 2020a). Pia, IDMC (2020) inaripoti kwamba takriban wakimbizi milioni moja wa ndani kwa ndani (IDP) kutokana na migogoro na vurugu kufikia mwisho wa 2019 na wengine 80,000 wapya katika nusu ya kwanza ya 2020. Lakini takwimu hizi mara nyingi huwa 'makadirio' (angalia Moduli 2). Ukusanyaji na usambazaji wa data kuhusu wakimbizi wa ndani kwa ndani na uhamisho mipakani ni mchache, na data kidogo kuhusu athari za migogoro ndizo zinazopatikana. Septemba 2019, IDMC ilikuwa bado

5 Takwimu zinarejelea idadi ya wahamiaji wa kimataifa. Idadi hiyo ni pamoja na wakazi wote waliozaliwa nchini za kigeni walio nchini humo bila kujali waliingia lini nchini. Kwa nchi ambazo data kuhusu watu waliozaliwa katika nchi za kigeni haipatikani, UNDESA hutumia data ya raia wa kigeni. Kwa hivyo, idadi ya wahamiaji wa kimataifa inaweza kukosa kujumuisha wahamiaji wa kizazi cha pili ambao walizaliwa nchini lakini wana wazazi waliohamia humo. Data ya idadi hii pia haipaswi kuhusishwa kimakosa na data ya mtiririko wa wahamiaji wa kila mwaka (yaani, idadi ya wahamiaji walioingia au kuondoka nchini humo ndani ya mwaka mmoja). Kwa ufafanuzi, angalia faharasa/sherehe zinazopendekezwa katika Moduli 2 (IOM, 2019; EMN, 2018).

6 Kwa ufafanuzi wa uhamiaji wa 'mduara', angalia faharasa zinazopendekezwa katika Moduli 2 (EMN, 2018; IOM, 2019).

imeshindwa kusema kwa uhakika idadi ya watu waliopoteza makao yao, idadi ya watoto ambao hawakuwa wanaenda shule au idadi ya familia ambazo zilikuwa zimegawanyika 2019” (André na wengine.,uk. 50).

Wakimbizi kutoka Cameroon: Kutokana na sababu kuwa awali nchi hii ilitambulika kwa sababu ya uthabiti wake kisiasa, idadi ya wakimbizi kutoka Cameroon ilikuwa takriban 10,000 katika miaka ya awali ya 2010. Kufikia 2018 walikuwa wameongeza idadi ya wakimbizi kufikia 45,000 na 2019 waliongezeka hadi 66,000. Mataifa ambayo wakimbizi huelekea hasa huwa Nigeria (52,000), ikifuatiwa na Marekani (5,000) na Italia (2,200) ilhali mataifa wanayokimbilia ni ya Ulaya na Amerika Kaskazini (UNHCR, 2020b).

Uhamiaji: Afrobarometer inahitimisha katika utafiti wake kwamba “vijana Waafrika walioelimika wana uwezekano mkubwa wa kuwazia kuhama” (Appiah-Nyamekye Sanny na wengine, 2019,uk. 1). Takriban asilimia (18%) ya washiriki kutoka Cameroon kati ya miaka 18 na 25 wanawazia sana suala la kuhamia nchi nyingine”, wakilinganishwa na 14% katika vikundi vyote (Appiah-Nyamekye Sanny na wengine, 2019,uk. 5, Mchoro 2; uk. 7, Mchoro 5; uk. 27, Jedwali A.2). Mkusanyiko wa asilimia nne wa washiriki wote kutoka Cameroon wanajiandaa kuhamia nchi nyingine, 16% pia wanawazia kufanya hivyo katika kipindi cha mwaka mmoja au miwili ijayo, 20% hawana mipango ya sasa ya kuhama na 59% hawawazii kamwe kuhama (Appiah-Nyamekye Sanny na wengine, 2019,uk. 9, Kielelezo 6; uk. 10, Kielelezo 7). Endapo ingewabidi kuhamia nchi nyingine, 12% ya washiriki kutoka Cameroon wangepoteza kuhamia nchi ya eneo hilo, asilimia nane sehemu nyingine barani Afrika, 26% Ulaya, 33% Amerika Kaskazini (Appiah-Nyamekye Sanny na wengine, 2019,uk. 13, Kielelezo 11). Idadi kubwa ya washiriki kutoka Cameroon walitamani sana kupata ajira kama sababu yao kuu ya kuwazia kuhama (35%), waki-fuatiwa na wale waliotamani kufanya hivyo ili kuepuka umaskini/hali ngumu ya kiuchumi” (24%) na kutafuta elimu (10%). Asilimia ndogo ya washiriki wanasema kwamba wanatamani kutafuta demokrasia/uhuru (3%) au amani/usalama (6%; Appiah-Nyamekye Sanny na wengine, 2019,uk. 15, Kielelezo 13; uk. 16, Jedwali 1).

Huku washiriki wengi wakitamani kuhamia maeneo yanayokaribiana nyumbani na wanaonelea haja ya uhamiaji mipakani kuwa huru (56% ya washiriki kutoka Cameroon), wanaonelea ugumu kuvuka mipaka ya kimataifa (60%; Appiah-Nyamekye Sanny na wengine, 2019,uk. 20, Kielelezo 17; uk. 21, Kielelezo 18). Waandishi wa utafiti wa Afrobarometer wanahitimisha kwamba “wachache mno wanafanya mipango ya kuondoka, bila shaka” (Appiah-Nyamekye Sanny na wengine 2019, uk. 2) lakini walikuwa na tahadhari kwamba iwapo wanaowazia kuondoka wangefanya hivyo, nchi hiyo ingepoteza idadi kubwa ya vijana wake (angalia Moduli 9). Jobard (2019) anaonyesha ugumu anaokumbana nao mkimbizi asiyetambulika (“*wa siri*”)⁷katika picha ya makala.

7 Kwa ufafanuzi wa uhamiaji usio rasmi, haramu au wa kisiri, angalia faharasa zinazopendekezwa katika Moduli 2 (EMN, 2018; IOM, 2019).



ZOEZI LILILOPENDEKEZWA LA KUSHUGHULIKIA STADI ZA UTAMBUZI ZA KUTUMIA NA KUCHANGANUA, NA STADI ZA MITAZAMO YA KIBINAFSI NA MAADILI ZA MAJIBU:

Ruhusu darasa kupokea ufahamu kuhusu Cameroon kama nchi ya uhamiaji na uhamisho wa lazima kabla ya kujifunza kuhusu masuala yanayowalazimu watu kutoroka na yanayowavutia katika makazi mapya.

Wape fursa washiriki kuandaa maelezo mafupi ya Cameroon kuhusu uhamiaji na uhamisho wa lazima.

- Kuunda maelezo mawili mafupi, washiriki wanachagua data yao kutoka vyanzo vilivyoonyeshwa kwenye Moduli 2, hasa tovuti ya uhamiaji kwenye ukurasa wa Cameroon (Migration Data Portal, 2021).
- Ili kuchangamsha data, washiriki wanaleta uhai kwenye data, wanachunguza ripoti kutoka au kuhusu Cameroon, ambazo wanaonelea kuwa za kueleleza na kusimulia.
- Wasilisha maelezo mawili mafupi kamili na kuhitimisha kwa maangazio matano ili kutambua sifa kuu za Cameroon.

ZOEZI LILILOPENDEKEZWA KWA DARASA ILI KUANGAZIA STADI ZA UTAMBUZI ZA KUELEWA:

Wape washiriki jukumu la kueleza ni masuala yapi kuhusu maelezo ya nchi ni muhimu na ambayo hadhira, na hasa kuhusu masuala yanayowapa uweza wa kufanya maamuzi yenye ufahamu kuhusiana na uhamiaji na uhamisho wa lazima.

Masuala teule ya kimuktadha

Mizozano: Mizozano ni mojawapo ya masuala yanayowasukuma watu kuhama (angalia Moduli 3). Hasa wanawake ndio huwa hatarini katika masuala ya mapigano (angalia sehemu ya jinsia ya mwongozo huu, na sehemu ya jinsia kwenye moduli hii) kama Zenn & Pearson (2014) wanavyoonyesha katika mfumo wa Boko Haram wa dhuluma za kijinsia. Nchini Cameroon, kuna mizozano miwili mikuu inayochochea uhamisho, migogoro katika maeneo yanayozungumza Kiingereza na uasi wa wanamgambo wa Boko Haram. Ukiukaji wa haki za binadamu umeenea (Human Rights Watch, 2019a; Human Rights Watch, 2019b).

Uasi wa Boko Haram: Maneno “Boko Haram”, yakitafsiriwa kutoka lugha ya Hausa, yanamaanisha “Elimu ya Magharibi ni Dhambi” (Zenn & Pearson, 2014, 46). Kikundi kinachoitwa hivi kimetaja kuzindua sheria za Kiislamu (sharia) katika eneo hili kama mojawapo ya malengo yake ya kiitikadi. Kikundi hiki kilichojihami kina mizizi yake kaskazini mashariki mwa Nigeria na ki-meenea katika mataifa jirani ikiwa ni pamoja na Chad, Niger na Cameroon. Tangu 2014, kikundi hiki cha waasi kimetekeleza mashambulizi eneo la Kaskazini mwa Cameroon. Cameroon imeo-

rodheshwa ya pili miongoni mwa nchi zilizoathirika pakubwa na vurugu na ukosefu wa usalama unaohusishwa na Boko Haram, baada ya Nigeria. Takriban raia 17 waliuawa katika shambulio mjini Nguetechewe Agosti 2020 wakati kikundi hiki cha Kiislamu kilipotumia “watoto kama walipuaji wa kujitolea mhanga kushambulia wakimbizi [kosa ambalo] haliambatani na uhalifu wa kivita” (Human Rights Watch, 2020, uk. 175-176). Shambulio hili lilitokea kabla ya ongezeko la visa vya vurugu tangu mwanzo wa 2020, huku visa vya kila siku vya mauaji, utekaji nyara na uharibifu wa mali vikihusishwa na Boko Haram. Aidha, eneo hili limeathirika na uhaba wa chakula na ukosefu wa fursa za kiuchumi. Mizozano huchochea visa vya ukosefu wa usalama na ugumu wa kiuchumi, chakula, afya na elimu (Abel na wengine, 2019; Lundy & Adebayo, 2016). Japo mizozano na waasi wa Boko Haram “imepungua pakubwa”, kulingana na Bertelsmann Stiftung (2020, uk. 7), kikundi hiki cha Kiislamu kingali hai, na makundi tofauti ya kijamii [...] yalijitokeza kujilinda kutokana na Boko Haram, huku serikali ikielekeza upya majeshi katika maeneo yanayozungumza Kiingereza (Bertelsmann Stiftung, 2020, uk. 7-8).

Mzozo katika maeneo yanayozungumza Kiingereza: Hii ni “mojawapo ya mizozano iliyopuuzwa sana ulimwenguni” (André na wengine., 2019, 14) uliochochea uhamisho mara 20 zaidi ya uliosababishwa na uasi wa Boko Haram, yadai IDMC. Mzozano huu haujaripotiwa kwa kina, na hivyo uingiliaji kati wa kibinadamu na ustawi haujafadhiliwa vilivyo (André na wengine, 2019, 8; IDMC, 2019). Tamfu (2018) anaeleza baadhi ya masaibu.

Elimu ndio kiini cha mzozano huu huku Kifaransa ikiwa lugha ya mafunzo katika shule za watu wanaozungumza Kiingereza. Sondo (2020) anasimulia masaibu ya mwanafunzi anayezungumza Kiingereza na mwanahabari anayesomea na kutafiti katika taasisi zinazotumia Kifaransa. Idadi kubwa ya raia wa Cameroon wanaozungumza Kiingereza wanahisi kutowakilishwa vilivyo nchini, kupuuzwa kimfumo na serikali kuu, na kutokuwa na uweza wa kiuchumi (IDMC, 2019; Manih, 2018). Akiangazia vurugu “chini ya shinikizo la kimataifa” (International Crisis Group, 2020, uk. 6), serikali ilianzisha majadiliano ya kitaifa 2019 lakini ikafanya “mabadiliko madogo” ambapo baadaye wanaharakati wa utengano katika maeneo yanayozungumza Kiingereza walisusia hafla hiyo na badala yake “wakaongeza kasi katika kampeni yao ya vurugu” (International Crisis Group, 2020, uk. 7). Ufikiaji elimu na huduma za afya uko chini katika maeneo yanayozungumza Kiingereza ikilinganishwa na sehemu nyingine nchini humo. Kikundi cha Southern Cameroon Ambazonia Consortium United (SCACUF) kilitangaza kuwa jamhuri huru mwaka wa 2017, hatua iliyokabiliwa vikali na serikali (Human Rights Watch, 2019a).

Uhuru wa vyombo vya habari: Katiba inahakikishia uhuru wa vyombo vya habari, aeleza Ngangum (2020), lakini “kuna matumaini machache ya uhuru wa vyombo vya habari, na mchango wa vyombo vya habari katika demokrasia” (Ngangum, 2020, uk. 10). Nafasi ya nchi hii ulimwenguni katika viwango vya uhuru wa vyombo vya habari ilididimia hadi 134 miongoni mwa mataifa 180 mwaka 2020 kutoka 131 mwaka 2019 na 129 mwaka 2018 (Reporters Without Borders, 2020a; Reporters Without Borders, 2020b; CPJ, & ESCR-Net, n. d.).

Cameroon ina mashirika mawili ya ukusanyaji habari, shirika la ukusanyaji habari la lugha ya Kiingereza la Cameroon, na shirika la French Agence Cameroun Presse. Shirika la habari la BBC hushirikiana na baadhi ya mashirika ya habari yenye ushawishi kutokana na “mazingira ya shughuli nyingi”, kituo cha televisheni kinachosimamiwa na serikali cha CRTV, vituo vya radio, na “vituo kadhaa vya redio na televisheni na mamia ya vichwa vya habari” (The BBC, 2019). Tita & Wantchami (2016, uk. 3) wanataja kudidimia kwa viwango vya kitaalamu: “Viwango vya kawaida vya kanuni za utangazaji kama vile usahihi na haki, maadili, havizingatiwi [...] viwango vya uadilifu miongoni mwa wanahabari viko chini na ni wafisadi”. Mishahara ya chini na mazingira duni ya utendakazi yanatumika kama sababu. Vyombo vya habari vinachukuliwa kuwa chini ya udhibiti mkali wa serikali (vyombo vya habari vya serikali) au mara nyingi kutishwa (vyombo binafsi vya habari). Magazeti yamepigwa marufuku, wanahabari kuwekewa vikwazo, kushtakiwa kwa makosa ya kuharibifu jina na kwa “kutusi urais” (Bertelsmann Stiftung, 2020, uk. 11). Mswada wa 2014 wa sheria ya kukabiliana na ugaidi umetumika kupunguza uangazaji shughuli za serikali katika vita dhidi ya waasi wa Boko Haram na mgogoro wa maeneo yanayozungumza Kiingereza (Bertelsmann Stiftung, 2020). Huku uwezekano wa utangazaji huru ukiendelea kupungua, matumizi ya mitandao ya jamii yameongezeka — na serikali pamoja na wafuasi wake wakianzisha jitihada za kutumia majukwaa haya kueneza jumbe zao. Matumizi ya mitandao ya jamii yameongezeka: 23% ya raia wanatumia mtandao (2019; World Bank, 2020h), huku 59% wakitumia simu smati ili kufikia mtandao (International Crisis Group, 2020). Facebook ndilo jukwaa la mtandao wa jamii maarufu sana Cameroon (International Crisis Group, 2020, kurasa za ii-iii; uk. 23-26).

Mashambulio ya wanahabari yameongezeka, kulingana na the Committee to Protect Journalists (tazama Kielelezo 20). Mtangazaji Samuel Wazizi, aliyefungwa jela tangu Agosti 2, 2019, alishitakiwa kwa kushirikiana na wanaharakati wa utengano katika maeneo yanayozungumza Kiingereza na kueneza taarifa zao. Alifariki hospitalini ya kijeshi ya Yaoundé Juni 2020. UNESCO (2020) ilisihi upelelezi wa kifo chake na kutoa mwito kwa serikali kutoa mwangaza kuhusu matukio yaliyojiri kabla ya kifo hicho, na kuhakikisha ukiukaji wowote wa haki zake kama mwanahabari na kama mfunzwa vinakabiliwa kisheria.”

Mtandao katika maeneo yanayozungumza Kiingereza ulifungwa kwa siku 240 kati ya 2017 na 2018. Kila ilipowezekana, watu walitafuta mbinu za kukabiliana na marufuku hayo, kutumia mitandao ya kibinafsi ya Virtual Private Networks (VPNs; Kenmogne, n. d., uk. 2); waliandika barua pepe kwa kutumia simu smati na marafiki zao kuzibeba hadi maeneo ya nchi yanayozungumza Kifaransa ambapo barua pepe hizo zingetumwa (Kingsley, 2019); walianzisha “kambi ya wakimbizi wa mtandao” katika sehemu iliyokuwa na mtandao ambapo watu walipita kuunganishwa na mtandao (Kenmogne, n.d., uk. 3).

Serikali ilitetea hatua yake ya marufuku haya ikidai kukabiliana na “kuendeleza habari za uwongo kupitia mitandao ya jamii zenye uwezo wa kuchochea chuki na vurugu katika maeneo yaliyoathirika” (Muke redzi, 2017). Kutokana na hoja hiyo ya “kupotosha”, wanaharakati wa kutetea haki za kibinadamu Cameroon, walihoji kuwa maelezo ya serikali kuhusiana na kufungwa kwa mtandao limekuwa “tatizo halisi ambalo kila mmoja atalazimika kulikubali” (Marchant & Stremlau, 2020, uk. 4332).


Mbali na kunyamazisha mjadala wa umma, kufunga mtandao ni uamuzi ambao “unakiuka sheria za kimataifa”, [...] kunawanyima raia wa Cameroon uwezo wa kufikia huduma muhimu na rasilimali msingi”⁸, akasema mjumbe maalumu wa Umoja wa Mataifa kuhusu uhuru wa kujieleza, David Kaye, mwaka 2017 (CIPESA, 2017, uk. 6). Pia inaathiri pakubwa uchumi. Ushirikiano katika sera ya kimataifa ya teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA) eneo la Mashariki na Kusini mwa Afrika (CIPESA) unakokotoa kwamba Cameroon ilipoteza takriban dola milioni 40 katika kipindi cha siku 93 za marufuku hayo ya 2017 (CIPESA, 2017, uk. 21-22). Hasara hii hasa iliathiri Silicon Mountain, kituo cha kiteknolojia katika eneo linalozungumza Kiingereza la kusini magharibi mwa nchi (Kenmogne, n. d.). Ulimwenguni, biashara zilizokuwa zikiendeleza shughuli zilishindwa kufikia washiriki wao na kulalama kwamba pesa zilikuwa zikipotezwa” (Mukeredzi, 2017).

Kenmogne (n. d.) anasimulia siku 93 za giza za 2017, akieleza masaibu ya mwalimu wa TEHAMA ambaye alishindwa kusajili wanafunzi kwa sababu ya chagamoto za kiteknolojia; mama anayeishi ng’ambo aliyetenganishwa na watoto wake; mtafiti aliyekatiziwa mafunzo yake mtandaoni. Wanasema kwamba hatua hiyo iliwakasirisha watu na kuongeza wasiwasi. Mashirika yasiyo ya serikali ya kutetea haki za kidijitali — Intaneti Sans Frontières and Access Now — yaliishtaki serikali ya Cameroon kwa kuendeleza mfungo huo katika maeneo yanayozungumza Kiingereza (Access Now, 2018).

Mashirika yasiyo ya serikali ya vyombo vya habari yalitahadharisha ulimwengu kuhusu kisa cha mwanahabari wa redio Mancho Bibixy, aliyetiwa nguvuni 2017 kwa makosa ya ugaidi baada ya kutetea haki za raia wa maeneo yanayozungumza Kiingereza, na kuhukumiwa kifungo cha miaka 15 grezani (CPJ, 2020b).

8 Baraza la Haki za Kibinadamu la Umoja wa Mataifa, katika Azimio lililopitishwa tarehe 5 Julai 2018, «linalaani bila shaka» hatua zinazokiuka sheria za kimataifa za haki za binadamu ambazo zinazuia au kuvuruga uwezo wa mtu kutafuta, kupokea au kutoa taarifa mtandaoni, likitoa wito kwa mataifa yote kujiepusha na kusitisha hatua hizo” (UNGA, 2018, uk. 3; 5, aya ya 13). Azimio hilo linaisitiza intaneti inahitaji «kusalia ya kimataifa, wazi na inayoweza kushirikisha watumiaji wengi», na kwamba mataifa yanahitajika kujiepusha na «vikwazo visivyofaa dhidi ya uhuru wa kutoa maoni na kujieleza mtandaoni» yakiwemo mataifa ambayo «yamebana au kukandamiza uhuru wa kujieleza mtandaoni katika hali inayokiuka sheria za kimataifa”. Aya ya 12 ni ukumbusho wa kutoa «mazingira salama na wezeshi ya mtandaoni» ambayo yanaruhusu wanahabari «kufanya kazi zao kwa uhuru na bila kuingiliwa kusikofaa au kinyume cha sheria» (UNGA, 2018, uk. 4-5).

Kielelezo 20: Wanahabari hatarini nchini Cameroon tangu 1992



Mashirika yasiyo ya serikali ya vyombo vya habari kama vile Reporters Without Borders na Kamati ya Kulinda Wanahabari, vile vile UNESCO zinatahadharisha jamii ya kimataifa kuhusu wanahabari hatarini. Chanzo: CPJ (2020a). Kielelezo chetu

Mradi wa Wanahabari wa Kimataifa “Project Exile” unaonyesha masaibu ya wanahabari katika harakati za kujaribu kuishi katika nchi yao na pia walikotorokea, kwa mfano, mchoraji katuni raia wa Cameroon, Ako Eyong au Charles Atangana, mwanahabari wa upelelezi wa zamani (Beaton, 2018; Ethiemere, 2017). Mwanahabari mwanamke Mimi Mefo Takambou alipokea tuzo ya uhuru wa kujieleza katika kitengo cha uanahabari (Index on Censorship, 2019). Yeye ni mwanahabari na mwanamke wa kwanza kushikilia wadhifa wa mhariri mkuu katika kituo cha Kiingereza cha shirika la habari la kibinafsi nchini Cameroon, na alianzisha jukwaa lake la habari (Mimimefo, n. d.; English Pen, 2020).

Mimi Mefo, Paul Chouta na Boris Bertolt ni mabloga watatu wa kisiasa huku kila mmoja akiwa na zaidi ya wafuasi 100,000 kwenye majukwaa ya mitandao ya jamii (wawili wanaishi ng'ambo na mmoja yuko gerezani Cameroon; International Crisis Group, 2020, uk. 16).



ZOEZI LILILOPENDEKEZWA LA KUSHUGHULIKIA STADI ZA UTAMBUZI ZA KUTEKELEZA NA KUCHANGANUA, NA STADI ZA MITAZAMO YA KIBINAFSI NA MAADILI ZA KUPOKEA:

Wape washiriki jukumu la kutambua na kueleza masuala mawili ya kimuktadha yaliyochaguliwa – masuala mawili yanayowasukuma kutafuta kimbilio kwingine au mawili yanayowavutia kukimbilia kwingineko au mchanganyiko wa kila moja – kuhusu Cameroon.

- Ili kutambua masuala ya kimuktadha, washiriki watumie Moduli 3 ya mwongozo huu. Aidha, washiriki pia watatambulisha masuala mpya ya kimuktadha kwani orodha ya Moduli 3 haijajumuisha yote.
- Kufufua hali zinazowasukuma raia wa Cameroon kuhama makwao na wengine kukimbilia Cameroon, washiriki wachunguze ripoti za vyombo vya habari na ushahidi.
- Kuwasilisha masuala ya kimuktadha yaliyochaguliwa wakati wote, washiriki watajaribu kusawazisha baina ya nadharia na asili ya kibinadamu katika nadharia hiyo.

Jinsia

Jinsia ni mojawapo ya masuala muhimu ya kubainisha nia, matukio, aula na hali za uhamiaji na uhamishwaji wa lazima (angalia sehemu ya jinsia kwenye mwongozo huu). UNHCR inasema kwamba wakimbizi wanawake “ambao hawajaandamana na yeyote, wajawazito, wakuu wa nyumba zao, walemavu au wazee hasa ndio wamo hatarini” (UNHCR, 2020d). Wanawake wanaokimbia maeneo yanayozungumza Kiingereza Cameroon kuelekea Nigeria hukumbwa na changamoto ya ukosefu wa ajira katika vituo vinavyowapokea Nigeria na wanakumbwa na hatari kubwa ya dhuluma za kijinsia na kingono, vilevile dhuluma za kinyumbani, lakini visa vingi haviripotiwi (UNHCR, 2018).

Usawa wa kijinsia umeandikwa kwenye Katiba ya Cameroon (Nijkem, 2017), na kujumuishwa katika sera ya serikali, National Gender Policy (NGPC) kama “msingi wa kuongoza na stakabadhi ya marejeleo [...] [inayonuiwa] kuimarisha jamii yenye usawa” (Mefire na wengine, 2017, uk. 37). Uwakilishi wa wanawake katika bunge uliongezeka tangu 1997 (World Bank, 2021), lakini bado unasalia chini kwa ujumla huku tofauti kubwa ikiwa baina ya viwango vya kitaifa na kimaeneo” (UN Women, n.d.) na kazi ya wanawake wabunge imeathiriwa pakubwa na “nidhamu ya vyama na mfumo wa bunge” (Fokum & Fonjong, 2018, uk. 754). Ushiriki wa wanawake katika siasa ni muhimu kwa ustawi na juhudi za kuangamiza umaskini (Fokum & Fonjong, 2018, uk. 755; Mefire na wengine., 2017, uk. 37; tazama Moduli 3), hasa katika nchi ambapo 51% ya wanawake wanaishi chini ya viwango wastani vya umaskini ikilinganishwa na 39% ya idadi ya kitaifa; 53% pekee ya wasichana (65% ya wavulana) wanajiunga na shule ya upili; 43% ya wanawake katika mahusiano wanashuhudia dhuluma za kinyumbani (OCHA, 2019).

Ikilinganishwa na mataifa jirani katika kikundi sawa cha maendeleo⁹, Cameroon iko nafasi bora huku ikishikilia nafasi ya 140 katika viwango vya utovu wa usawa wa kijinsia, ikilinganishwa na Congo (145; hakuna data kuhusu Equatorial-Guinea; UNDP, 2019, uk. 318). Ikilinganishwa na majirani zake wawili katika kikundi cha maendeleo ya kati, Cameroon ina viwango vya chini vya visa vya mimba za utotoni, ina viwango vya juu vya wanawake bungeni, na ina viwango vya juu vya wanawake wafanyakazi. Kwa upande mwingine, Cameroon iko nyuma katika masuala ya wanawake na wanaume walio angalau na elimu ya sekondari. Ripoti ya viashiria ya Cameroon inaonyesha kwamba nchi hiyo hushuhudia takriban vifo 600 kwa kila watoto 100,000 wanaozaliwa wakiwa hai ikilinganishwa na 440 nchini Congo na 340 nchini Equatorial-Guinea (data kutoka 2015; UNDP, 2019, 318). Ukeketaji (FGM) umepigwa marufuku katika sheria (Thomson Reuters Foundation, 2018). Umri halali wa kuoa au kuolewa ni miaka 18 kwa wanawake na wanaume. Baadhi ya wakaguzi wanachukulia hatua za Cameroon kuwa muhimu “katika jitihada za kutimiza usawa wa kijinsia na kuwapa wanawake uweza wa kujitegemea” (Njikem, 2017). Wengine wanaangazia changamoto za kutekeleza sheria zilizopo zinazonuia kuafikia usawa wa kijinsia na kuzuia dhuluma dhidi ya wanawake na wasichana, wanaume na wavulana, kutoa usalama na haki kwa wahanga (UN Women, n. d.). Pia kiuchumi, usawa wa wanawake bado uko kwenye ajenda. Huku wanawake wakichukuliwa kuwa uti wa mgongo wa uchumi, bado wanatengwa na wanategemea zaidi wanaume kiuchumi ikilinganishwa na ilivyokuwa miaka michache baada ya uhuru na nyakati za awali” (Nana-Fabu, 2006, uk. 148).

Umoja wa Mataifa unaripoti kwamba takriban wanawake 194,000 na wanaume 189,000 waliokuwa wakihama kutoka Cameroon 2019 – wanawake wengi wakilinganishwa na wanaume walihama kutoka Cameroon (Migration Data Portal, 2021). Tangu 1990, vikundi vyote viwili vilichagua mataifa matajiri, mataifa yaliyostawi zaidi ya Ulaya ikilinganishwa na mataifa ya Afrika yaliyoko kusini ya Jangwa la Sahara. Idadi ya wanawake wakimbizi kutoka Cameroon imeongezeka kutoka 1990 hadi 2019 kwa takriban 250%, huku ongezeko kubwa likishuhudiwa 2000. Japo katika miaka ya 1990, wanawake wengi walihamia katika maeneo ambayo hayajastawi (54%) ikilinganishwa na waliohamia katika maeneo yaliyostawi (46%), hali hiyo kwa sasa imebadilika: 68% ya wakimbizi wanawake kutoka Cameroon walihamia maeneo yaliyostawi (wanaume: 60%). Katika kipindi cha miaka kadhaa, wameendelea kupendelea mataifa yenye mapato ya juu ikilinganishwa na yale ya mapato wastani, lakini kiwango hiki kimeongezeka: Mwaka 1990, asilimia 45 ya wanawake walihamia mataifa yenye mapato ya juu na 27% walihamia katika mataifa yenye mapato wastani na ya chini, ilhali 2019 asilimia 68 ya wanawake walihamia mataifa yenye mapato ya juu, 21% walihamia mataifa yenye mapato wastani na 11% pekee katika mataifa yenye mapato ya chini. Eneo lililopendelewa na wahamiaji ni Ulaya (50% ya wanawake wote waliohama kutoka Cameroon 2019; wanaume: 40%), ikifuatwa na Afrika (32%) na Amerika Kaskazini (18%), na mwelekeo huu wa kupendelea Ulaya ulionekana kushika kasi kati ya 1990 na 2019: Mwaka wa 1990, asilimia 43 ya wanawake walihamia Ulaya ikilinganishwa na 50% waliohama 2019 ilhali 1990 asilimia 54 ya wanawake walihamia katika mataifa ya Afrika ikilinganishwa na 32 mwaka 2019. Barani Afrika, wanawake wengi raia wa Cameroon walihamia

9 Mnamo 2019, Congo ilishika nafasi ya 138 kwenye HDI, Equatorial-Guinea ikachukua nafasi ya 144, na Cameroon nafasi ya 150 (UNDP, 2019, uk. 302).

Gabon (21,000 mwaka 2019), Chad (18,577 mwaka 2019), na Nigeria (12,717; UNDESA, 2019b, Jedwali 2, Jedwali 3).

Mataifa ya Baraza la Ushirikiano la Ghuba (GCC) ndio yalikuwa kikomo cha safari kwa wanawake wahamiaji kutoka Afrika ya Kati na Magharibi, ambao hasa huajiriwa kama wajakazi (IOM, 2018). Katika harakati za kusaka ajira na hivyo kuletea familia zao “fahari na heshima” (Malit & Oliver, 2020, 130) kupitia uhamiaji wa kimataifa wa kikazi, wahamiaji wanawake wanaoelekea mataifa ya GCC wameripoti visa vya dhuluma (Chimtom, 2015; Ebo’o & Oyono, 2019) suala ambalo lilichochea jitihada za kutaka kukomesha ulanguzi huu wa watu (Kindzeka, 2016). Kisa cha “Mirabel” kutoka eneo la Cameroon linalozungumza Kiingereza (alielekea Dubai kwa viza ya utalii kwa matumaini ya kufanya kazi kama mwalimu, ila kupata ajira kama mwalimu msaidizi) kinaambatana na kile cha “Susan” aliyetarajia kufanya kazi kama mhudumu wa afya nchini Kuwait ila kuishia kufanya kazi kama mjakazi (Chimtom, 2015; Malit & Oliver, 2020).

Bara Ulaya, wanawake raia wa Cameroon hasa huhamia mataifa yanayozungumza Kifaransa kama vile Ufaransa (57,000 mwaka wa 2019), Ubelgiji (10,000) na Uswizi (5,000), na Uingereza (5,000); Ujerumani (Wanawake wahamiaji 7,700 mwaka wa 2019; angalia Moduli 8) na Italia (wanawake wahamiaji 6,500 mwaka wa 2019) pia ni nchi zinazopendelewa (UNDESA, 2019b, Jedwali la 3). Nchini Ujerumani, idadi ya wanawake wahamiaji kutoka Cameroon imekuwa ikiongezeka katika kipindi cha miaka ya karibuni, na mchango mkuu wa wanaohamia kwingine katika ustawi wa Cameroon umetambulika (GTZ, 2007, uk. 8-9).

Kuingia Ulaya sio rahisi kama Frías (2019) anavyoonyesha. Anamtambulisha “Mireille” kutoka Cameroon, mwanamke wa kwanza wa Kiafrika kuvuka mpaka baina ya Melilla (Uhispania) na Morocco, aliyeleza kupitia vyombo vya habari kuhusu aliyokumbana nayo katika safari yake kutoka Cameroon kuelekea Uhispania. Hakuwa ametusiwa wala kudhulumiwa katika safari yake barani Afrika, na alikuwa ameamua kuelekea asikojua kwa sababu “[hata tukienda shuleni na kupata shahada hakuna cha kufanya]” (Frías, 2019, uk. 172). Mwanamke wa pili kuvuka mpaka eneo la Melilla alikuwa raia wa Cameroon kwa jina, “Astan”, akiwa na mimba ya wiki 12. Tatiana Kanga, pia kutoka Cameroon, alifanya safari ndefu barani Afrika na kuvuka bahari ya Mediteranean akiwa na mimba ya miezi tisa (Frías, 2019). Kwa wanawake wengi, uhamiaji ndio njia ya “kufikia rasilimali”, yaeleza IOM (2020). Kwa nini wao huondoka? Alpes (2017), kupitia utafiti wake wa kisayansi mashinani, anasisitiza kwamba “ndoto za kuhama [...] zinagusa vijana raia wa Cameroon kutoka familia tajiri na maskini, kutoka matabaka mbali mbali na viwango tofauti vya kielimu. Wanaume na wanawake wanafanikiwa kupata usaidizi wa kifedha kutoka kwa familia zao katika jitihada za kutaka kuhama” (Alpes, 2017, uk. 306), na aliye na nguvu zaidi mwi-showe huwa mhamiaji” (Alpes, 2017, 313), mwanamke au mwanamume. Sawa na jinsi vijana katika Guinea-Bissau ambao huhama wakiwa na matarajio ya kusaka maisha mema kwingineko” (Ramsey-Kurz & Ganapathy- Doré, 2011; angalia Moduli 6), hii inaakisiwa Kanga anaposema “Ni Ulaya!” (Frías, 2018, uk. 174). Lakini sio visa vyote vya uhamiaji huvuna matunda. Waliopo-

teza matumaini na wanaotamani kurejea nyumbani huenda wakanufaika na mipango ya kurejea nyumbani na kufungamanishwa iliyotekelezwa na IOM (2020). Wanawake wanaorejea nyumbani kama vile “Rafiatou” wanaeleza ushuhuda wao kwa wanaonua kuhamia nje kwa sababu “wanawake na wasichana wanapaswa kujua hatari zilizopo njiani” (IOM, 2020).

Kama ilivyo kawaida (angalia Moduli 3), wanawake raia wa Cameroon pia wanatarajiwa kutimiza matarajio ya wawekezaji nyumbani — familia na jamii — ambao “mara nyingi hufanya mipango ya awali na maajenti wa usafiri au walanguzi [na] [...] kuwalipa watu hawa” (Mixed Migration Center, 2018, uk. 36). Katika utafiti uwandani wa kiethnografia alioufanya kati ya 2007 na 2013, Alpes (2017) alifichua uhusiano baina ya wanawake wahamiaji, familia zao na walanguzi Cameroon, na ameweza kuonyesha jinsi ulivyo muunganisho wa uamuzi wa wahamiaji na utegemeaji.



KAZI YA ZIADA ILIYOPENDEKEZWA YA KUSHUGHULIKIA STADI ZA MIELEKEO YA KIBINAFSI NA MAADILI ZA KUPOKEA NA STADI ZA UTAMBUZI ZA KUTEKELEZA:

Waombe washiriki wako kutoa muhtasari kuhusu uhamisho wa ndani kwa ndani Cameroon.

- Tafuta ushauri kutoka kwa rasilimali zilizotambulishwa, kwa mfano, tovuti ya data ya uhamiaji (Migration Data Portal, 2021), viashiria vya ustawi wa kibinadamu (UNDP, 2019c) au ripoti za vyombo vya habari (The New Humanitarian, 2020).
- Wasilisha takwimu na sababu za uhamisho kwa kutumia rasilimali zilizo juu, ikiwa ni pamoja na hazinadata zilizotolewa na IDMC, UNHCR na IOM kuhusu idadi ya wahamiaji nchini Cameroon. Toa masuala yanayowasukuma watu kutoka makwao kuelekea maeneo salama Cameroon — na eleza kwa nini hawavuki mipaka ya kimataifa.
- Dhihirisha hali za uhamisho wa ndani kwa ndani — tumia picha, video au majukwaa mengine ya habari.

KAZI YA ZIADA ILIYOPENDEKEZWA YA KUSHUGHULIKIA STADI ZA UTAMBUZI ZA KUELEWA NA KUCHANGANUA:

Toa ripoti kuhusu Cameroon na wakimbizi wa ndani kwa ndani, wahamiaji au wakimbizi, ukitumia vyombo vya habari nchini mwako na kimataifa. Kila mshiriki anapaswa kueleza kwa kina masuala ya Cameroon na kutambua taarifa zinazozipa hadhira uwezo wa kufanya maamuzi yenye ufahamu kuhusu uhamiaji na uhamisho wa lazima.



USOMAJI WA ZIADA:

Kiakademia:

Global Journalist (2020). Project Exile. Retrieved January 22, 2020, from <https://globaljournalist.org/2018/01/8964/>

Kiuanahabari:

Jobard, O. (2019). From Cameroon to France: Travel Journal of a Clandestine Immigrant (Moving Walls). New York, Washington D.C., London: Open Society Foundation. Retrieved January 21, 2020, from <https://www.movingwalls.org/moving-walls/13/cameroon-france-travel-journal-clandestine-immigrant.html>

Kitaasisi:

Immigration and Refugee Board of Canada, & UNHCR (2012). Cameroon: Corruption of journalists. The falsification of newspaper articles for the purpose of refugee claims. Retrieved January 21, 2020, from <https://www.refworld.org/docid/4f9e37342.html>

Marejeleo

Abel, G. J., Brottrager, M., Crespo Cuaresma, J., & Muttarak, R. (2019). Climate, conflict and forced migration. *Global Environmental Change*, 54, 239-249. <https://doi.org/10.1016/j.gloenvcha.2018.12.003>

Access Now (2018). Access Now & ISF file legal intervention against Cameroon shutdown. Retrieved January 7, 2021, from <https://www.accessnow.org/access-now-isf-file-legal-intervention-cameroon-shutdown/>

Adepoju, A., Fumagalli, C., & Nyabola, N. (2020). Africa Migration Report: Challenging the narrative. Addis Ababa. Retrieved October 19, 2020, from <https://publications.iom.int/books/africa-migration-report-challenging-narrative>

African Union (2017). Harnessing the demographic dividend through investments in youth. Retrieved December 3, 2019, from <https://au.int/sites/default/files/documents/32665-doc-au-echo-magazine-2017-23june17-1.pdf>

Alpes, M. J. (2017). Why aspiring migrants trust migration brokers: The moral economy of departure in Anglophone Cameroon. *Africa* (87)2, 304-321. <https://doi.org/10.1017/S0001972016000978>

André, C., Anzellini, V., Hajžmanová, I., & Leduc, C. (2019). Africa Report on internal displacement. IDMC. Retrieved November 22, 2020, from <https://www.internal-displacement.org/publications/africa-report-on-internal-displacement>

Appiah-Nyamekye Sanny, J., & Rocca, C. (2018). "Updata-ing" the narrative about African migration. *AfroBarometer*. Retrieved October 22, 2020, from <https://afrobarometer.org/publications/updata-ing-narrative-about-african-migration>

Appiah-Nyamekye Sanny, J., Logan, C., & Gyimah-Boadi, E. (2019). In search of opportunity: Young and educated Africans most likely to consider moving abroad. *AfroBarometer*. (288). Retrieved December 1, 2019, from http://afrobarometer.org/sites/default/files/publications/Dispatches/ab_r7_dispatchno288_looking_for_opportunity_africans_views_on_emigration1.pdf

- Beaton, A. (2018, January 22). Tortured in Cameroon, a struggle for U.K. asylum [Charles Atangana]. *Global Journalist*. Retrieved November 27, 2020, from <https://globaljournalist.org/author/abeaton/>
- Bertelsmann Stiftung (2020). BTI 2020 Country Report – Cameroon. Gütersloh: Bertelsmann Stiftung, 2020. Retrieved January 7, 2021, from https://www.bti-project.org/content/en/downloads/reports/country_report_2020_CMR.pdf
- Chimtom, N. K. (2015, July 15). In search of jobs, Cameroonian women may end up as slaves in Middle East. *Inter Press Service*. Retrieved January 10, 2021, from <http://www.ipsnews.net/2015/07/in-search-of-jobs-cameroonian-women-may-end-up-as-slaves-in-middle-east/>
- CIPESA (2017). A Framework for calculating the economic impact of internet disruptions in sub-Saharan Africa. Collaboration on International ICT Policy in East and Southern Africa (CIPESA), Kampala. Retrieved January 7, 2021, from https://cipesa.org/?wpfb_dl=252
- CPJ (2020a). Journalists attacked in Cameroon since 1992. Retrieved May 18, 2020, from <https://cpj.org/africa/cameroon/>
- CPJ (2020b). Mancho Bibixy. Abakwa FM, Imprisoned in Cameroon, January 17, 2017. Retrieved January 7, 2021, from <https://cpj.org/data/people/mancho-bibixy/>
Ruhusu darasa kupata kiasi cha ufahamu kuhusu Ujerumani kama nchi ambayo ni chaguo kuu la wahamiaji na wakimbizi kwa sasa — na kama nchi asilia ya wakimbizi siku zilizopita.

Waalike watu ambao wanashiriki katika utayarishaji wa maelezo mafupi mawili: maelezo kuhusu nchi hii na maelezo kuhusu uhamiaji na kufurushwa kutoka kwenye makazi yao nchini Ujerumani.

- Ili kutunga maelezo haya mawili, wanaoshiriki huchagua data zao kutoka kwa vyanzo vilivyoonyeshwa katika Moduli 2, hasa ukurasa wa tovuti ya data ya uhamiaji kuhusu Ujerumani (2020c).
- Ili kuhuisha data, wanaoshiriki huchunguza ripoti za vyombo vya habari kuhusu Ujerumani, ambazo wanaona kuwa zinaelimisha na kutoa maelezo.
- Wasilisha maelezo haya mawili kikamilifu na uhitimisha kwa mambo matano muhimu ili kubainisha sifa kuu kwa Ujerumani.

ZOEZI LILILOPENDEKEZWA KWA DARASA KUSHUGHULIKIA STADI ZA UTAMBUZI ZA KUFAHAMU:

Wape wanaoshiriki jukumu la kueleza ni vipengele vipi vya maelezo ya nchi na sura ya uhamiaji na watu kufurushwa katika nchi hiyo ambavyo ni muhimu kwa hadhira yao ili ufahamu mpya wa hadhira uwawezeshe kuchukua maamuzi sahihi.

Watoto wasioandamana na watu mzima katika EU: Wasioonekana

Watoto mara nyingi ni kikundi cha umri wa chini ya miaka 18, kulingana na Mkataba wa Haki za Mtoto (CRC). Idadi ya watoto wahamiaji iliongezeka kwa wastani kutoka karibu milioni 24 mwaka 1990 hadi milioni 27 mwaka 2010 na kisha hadi milioni 33 kufikia 2019 (Migration Data Portal, 2020a). Ulimwenguni, kuna takriban watoto milioni 13 ambao ni wakimbizi na watoto 936,000 wanaotafuta hifadhi, na watoto milioni 17 ambao wamelazimishwa kuhama makazi yao ndani ya nchi zao (IOM, 2019b, uk. 238). Wengi wa watoto wasio na walezi na ambao wanatafuta hifadhi barani Ulaya mwaka 2018 walitoka Afghanistan (16%), Eritrea (10%), Syria, Pakistani (7%), Iraq, Guinea (6%) na Somalia (5%); UNHCR na wengine. , 2019, uk. 4). Asilimia 56 ya waliowasilisha maombi ya kutafuta hifadhi ya kisias mwaka 2018 walifaulu. Kati ya wale ambao maombi yao yalikubaliwa, asilimia kubwa ya watoto walipewa hadhi ya ukimbizi mwaka 2018 (63%) kuliko mwaka 2017 (50%). Wengi wa waombaji wa hifadhi ya watoto waliopata mahali ambapo hawakukusudia walitoka nchi za Afrika Kaskazini (UNHCR na wengine, 2019, uk. 4).

Watoto kwa kawaida hupata hadhi zao za uhamiaji kutoka kwa wazazi wao. Hata hivyo, watoto ambao hawajaandamana na walezi huhama kwa idadi kubwa kwenda Ulaya na kuendelea zaidi hadi Ujerumani. Mnamo 2015, kulikuwa na watoto mara tano zaidi waliokadiriwa kuhama peke yao kuliko mwaka wa 2010-2011. Kwa hivyo, idadi ya watoto ambao hawaandamani na walezi wanapomba hifadhi imeongezeka (Migration Data Portal, 2020a). Mnamo 2015, kulikuwa na watoto mara tano zaidi waliokadiriwa kuhama peke yao kuliko mwaka 2010-2011. Kwa hivyo, idadi ya watoto ambao hawaandamani na walezi imeongezeka (Migration Data Portal, 2020a). Mnamo 2018, karibu thuluthi moja ya watu wote wanaotafuta hifadhi barani Ulaya walikuwa watoto (191,000 kati ya 603,000) wakiwemo zaidi ya watoto 20,000 ambao hawakuandamana na walezi; wengi wao walihifadhiwa nchini Ujerumani (78,270 mwaka 2018; UNHCR na wengine, 2019, uk. 4).

Ferrara na wengine (2016) wanaandika kuhusu “watoto wasioonekana” ambao haki zao za kibinadamu zimeandikwa katika CRC. Roudik (2017) alichunguza sheria za maeneo 20 duniani kote ambazo zinahusiana na jinsi wahamiaji wasio na vibali waliofika wakiwa watoto wanavyoshughulikiwa, kustahiki kwao kupata hadhi ya kisheria na upataji manufaa ya kijamii, na uwezekano wao wa kuwa raia. Huku ikilenga watoto wa wahamiaji wasio na hati (uhamiaji usio halali)¹³, ripoti hiyo pia inaeleza sheria zinazohusiana na wahamiaji ambao ni watoto wasioandamana na walezi. Nchini Italia, kwa mfano, “Sheria namba 47 ya 2017 ilitungwa kulinda watoto wa kigeni wanaoingia Italia bila mtu mzima kwa kutambua haki zao ambazo watoto Waitaliano na wale wa EU wanafurahia [...]. Inawezekana watoto wa kigeni ambao hawajaandamana na walezi kutokataliwa mpakani, na kuwarudisha nyuma au kuwafukuza ni marufuku” (Roudik, 2017, uk. 46-47). Mnamo 2020, mzozo wa watoto wahamiaji wasio na walezi ulifikia kilele chake walipokuwa wakiishi katika vituo vya mapokezi vilivyojaa watu kwenye visiwa vya Ugiriki wakati wa janga la Uviko-19 (Psaropoulos, 2020; Schmitz, 2020; UNHCR, 2020b).

13 Kwa maana ya maneno, tazama faharasa zinazopendekezwa katika Moduli 2 (IOM, 2019a; EMN, 2018).

Kigezo cha mvuto: Sumaku ya ustawi

Manufaa ya wakimbizi nchini Ujerumani ni “ya juu kabisa,” na Ujerumani inatoa nafasi hiyo kuliko wanachama wengine wa EU, Waziri wa Mambo ya Ndani wa Ujerumani alisema alipotoa wito wa kuwepo kwa makubaliano ya EU kuhusu kiwango cha manufaa ambayo wakimbizi wanapokea (Staudenmaier, 2017). Euronews with Reuters (Trevelyan & Gareth, 2015) ilitayarisha muhtasari wa manufaa kwa wahamiaji katika nchi wanachama wa EU ambao ulikuwa tofauti wakati huo. Nchini Ujerumani, huduma hutofautiana kutoka jimbo hadi jimbo, na hata kutoka jiji moja hadi jingine. Ofisi ya Uhamiaji na Wakimbizi ya Jumuiya ya Ujerumani (BAMF; BAMF, 2020) inawafahamisha wahamiaji na wakimbizi nchini Ujerumani kuhusu masuala yanayohusu makazi, ushirikiano, ulinzi, kurudi kwa hiari, na mengineyo, tovuti ya uhamiaji ya EU inatoa taa-rifa za kina kuhusu taratibu katika nchi zote wanachama wa EU (Tume ya Ulaya, 2020a).

Sumaku ya ustawi mara nyingi huchukuliwa kuwa kigezo kikuu kutoka kwa nchi zilizo na mifumo duni ya ustawi hadi nchi zilizo na mifumo bora ya ustawi kama vile Ujerumani. Wasiwasi wa umma kuhusu uhamiaji wa kujistawisha unaondolewa, huku wahamiaji na wanaotafuta hifadhi wakidhaniwa kuwa wananufaika na huduma za kijamii kama vile afya, elimu, chakula (au pesa za matumizi), makazi, kupata wakalimani na wanasheria na mengineyo bila malipo. Jamii nyingine za Ujerumani zinahoji kuwa mchakato wa kupata hifadhi huwapatia waombaji nafasi za kutege-me manufaa ya jamii mwenyeji. Masuala haya yanashughulikiwa katika utafiti, ripoti za taasisi na mijadala ya umma. Mwanafalsafa wa Oxford David Miller – katika kitabu chake *Strangers in Our Midst* (2016) – anachanganua suala hili kwa mfumo wa kanuni unaolenga kubainisha suluhu za kisiasa; kwa muktadha wa Kijerumani wa falsafa ya Miller, tazama Bieber (2017). *The Economist* (2018) inaona “ubabedume wa ustawi” ukiongezeka.

Kiwango cha ujuzi kinachunguzwa kama kigezo muhimu cha kuamua kipimo kwa wahamiaji cha huduma za kijamii bila malipo na misaada ya fedha kwa wasiojiweza, huku utegemezi wa wahamiaji wenye ujuzi wa juu ukiwa mdogo kuliko wenzao walio na ujuzi wa chini (Giulietti & Wahba, 2012). Mfumo karimu wa ustawi wa jamii huvutia wahamiaji wenye ujuzi wa chini huku sera ya uhamiaji inayoendeshwa na mahitaji ya stadi na maarifa ikivutia wahamiaji wenye ujuzi zaidi kulingana na Razin & Wahba (2011). Ponce (2018) anatofautisha mvuto wa ustawi na dhana ya ujumuishaji na kugundua kuwa wahamiaji wanavutwa na ahadi ya ushirikishwaji wa kijamii na kisiasa, na mahali ambapo watu wa makabila yao wamekuwa raia kamili.

Kigezo cha mvuto: Kimbilio la salama

Ujerumani, miaka 75 baada ya kumalizika kwa dhuluma ya za utawala wa Nazi na miaka 30 baada ya kuungana tena, imekamilisha kikamilifu mpito wake kuelekea kwenye demokrasia (tazama hapo awali, Muhtasari). Utafiti wa 2019 ulionyesha kuwa 99% ya waliohojiwa waliridhishwa na mtindo wa kidemokrasia wa utawala badala ya udhalimu (Decker na wengine, 2020). Utafiti huo pia unaonyesha kuwa Wajerumani wengi hawajaridhishwa na jinsi ambavyo mfumo huo unaendelea, hasa kuhusiana na sera za kijamii na kiuchumi. Labda ni kwa mitazamo hii

ambapo Ujerumani inaorodheshwa ya 17 kati ya nchi 156 katika Kiwango cha Furaha Duniani (Helliwell na wengine, 2020). Nchi hii inaongoza katika viwango vyote vya uhuru duniani: Mbali na kuwa nambari nne kwenye HDI (tazama maelezo ya hapo awali), Ujerumani inashikilia nambari 13 kati ya nchi 167 katika kitengo cha “demokrasia kamili” ya Kiwango cha Demokrasia (EIU, 2020) ; uhuru wa vyombo vya habari huipa Ujerumani nafasi ya 11 kati ya 180 (Maripota Wasio na Mipaka, 2020); kukita kwa ufisadi ni haba kwani inachukua nafasi ya tisa kati ya 180 (Transparency International, 2020); usalama uko juu, ikizingatiwa kuwa ni taifa la 17 kati ya 163 kwenye Kiwango cha Amani Ulimwenguni (IEP, 2019), na hatari kwa ujumla ni ndogo, ikiwa katika nafasi ya 162 kati ya nchi 181 kulingana na Kiwango cha Hatari Duniani, ambacho kinazingatia athari za Uviko-19 (Bündnis Entwicklung hilft, & IFHV, 2020, uk. 6-7, uk. 25, uk. 59-60).

Hifadhi ya kisiasa ni mojawapo ya njia chache za kisheria za kufika Ulaya. Nchi wanachama wa EU zina desturi tofauti za kuruhusu na kuondoa hadhi ya ukimbizi. Tangu 1999, EU imekuwa ikishughulikia kuundwa kwa “Mfumo Jumla wa Hifadhi Ulaya” (CEAS) kwa lengo la kuoanisha viwango vya ulinzi na mapokezi. “Mkataba Mpya wa Uhamiaji na Ukimbizi” (Tume ya Ulaya, 2020b) unatoa hitimisho lake kuhusu mzozo wa wakimbizi wa 2015/2016, unaolenga “kuunda mfumo mpya ambao unadhibiti na kuhlalisha uhamiaji kwa muda mrefu na ambao umejikita kikamilifu kwenye maadili ya Ulaya na sheria za kimataifa” (Tume ya Ulaya, 2020b, uk. 1). Mbinu mpya inajumuisha sera za uhamiaji, hifadhi, ushirikiano na usimamizi wa mipaka. Inalenga “kupunguza njia zisizo salama wala halali na kukuza [...] njia salama za kisheria barani Ulaya kwa wale wanaohitaji ulinzi” (Tume ya Ulaya, 2020b, uk. 2). Mbinu mpya inakusudiwa kudhibiti kutegemeana kati ya sera na maamuzi mbalimbali ya nchi wanachama wa EU kwa nia ya “mshikamano na uwajibikaji wa pamoja” (Tume ya Ulaya, 2020b, uk. 5-6). Mahitaji ya watoto yame-tambuliwa na kupewa kipaumbele. Wahamiaji “wasio na haki ya kukaa” watarejeshwa “haraka” na “kwa ufanisi”, na kurejea kwa hiari kutahimizwa (tazama Moduli 6). Hivi sasa, ni theluthi moja tu ya watu walioamriwa kurudi kutoka kwa nchi wanachama wa EU wanaondoka, jambo ambalo “hudhoofisha imani ya raia katika mfumo mzima wa usimamizi wa hifadhi na uhamiaji” (Tume ya Ulaya, 2020b, uk. 7).

Nchini Ujerumani, kando na desturi ya ‘Kukaribisha Wakimbizi’ (tazama maelezo ya hapo awali katika Muhtasari), kuongezeka kwa ufuasi wa vyama vya mrenjo wa kulia na Wajerumani wanaopinga uhamiaji kumetawala vichwa vya habari za kimataifa (Al Jazeera, 2019; Bennhold & Eddy, 2020; Eddy, 2015; Ufaransa24, 2017). Utafiti wa uwakilishi unaopima ushirikishwaji wa tabianchi wa Ujerumani, hata hivyo, umeonyesha kuwa mitazamo ya raia wa Ujerumani kwa wakimbizi ni chanya kwa kiasi kikubwa (SVR, 2018). Wajerumani, walio na historia ya uhamiaji na wasio na historia ya uhamiaji, walichunguzwa, wakiwemo Wajerumani wahamiaji waliorudi Ujerumani baada ya kufurushwa (Aussiedler), watu wenye asili ya Kituruki, na wahamiaji kutoka EU na kwingineko duniani. Wengi wa waliohojiwa wanaamini kuwa wakimbizi hutajirisha nchi kiutamaduni na kiuchumi. Asilimia 60 ya wale wasio na historia ya uhamiaji wanaamini Ujerumani inapaswa kuendelea kupokea wakimbizi, hata kama ndiyo nchi pekee mwanachama wa EU kufanya hivyo. Matokeo hutofautiana katika makundi ya wahamiaji, na kiwango cha juu zaidi cha makubaliano kimesajiliwa kati ya watu wenye asili ya Kituruki; Wajerumani wahamiaji

waliorudi Ujerumani ni “waangalifu zaidi” (SVR, 2018, uk. 1). Sola (2017) anahitimisha kuwa, kutokana na uchunguzi wake uliofanywa wakati wa kilele cha mzozo wa wakimbizi, kuanzia Juni 2015 hadi mwisho wa mwaka huo: Wasiwasi miongoni mwa wakazi wa Ujerumani uliongezeka kwa 22% ikilinganishwa na kiwango cha mgogoro wa kabla ya wakimbizi ambacho anataja kuwa “kikubwa” (Sola, 2018, uk. 1). Kwa kuzingatia yote yaliyo hapo juu, Ujerumani ni mojawapo ya nchi zinazokubali wahamiaji zaidi, ikihifadhi nafasi ya 24 kati ya nchi 140 katika Orodha ya Kukubalika kwa Wahamiaji ya Gallup (Fleming na wengine, 2018). Waandishi wanahitimisha kwamba “cha kushangaza kwa kiasi fulani, nchi zilichaguliwa hivi majuzi zilikuwa na kauli-mbiu za kuwapinga wahamiaji — Marekani, Uingereza, Uholanzi, Ufaransa na Ujerumani — zote ni miongoni mwa nchi zinazokubali zaidi wahamiaji” (Fleming na wengine, 2018, uk. 116).



ZOEZI LILILOPENDEKEZWA LA KUSHUGHULIKIA STADI ZA UTAMBUZI ZA KUTEKELEZA NA KUCHANGANUA, NA STADI ZA MITAZAMO YA KIBINAFSI NA MAADILI ZA KUJIBU:

Waelekeze wanaoshiriki kutambua na kutaja vipengele viwili vya muktadha vilivyochaguliwa — vipengele viwili vya msukumo au vipengele viwili vya mvuto (vinavyokinzana) au kila mojawapo kwa pamoja — kwa Ujerumani.

- Ili kubainisha vipengele viwili vya muktadha, wanaoshiriki watumia Moduli 3 ya mwongozo huu, na pia kwa hakika wataanzisha vipengele vipya vya muktadha, kwa sababu Moduli 3 haijumuishi vipengele vyote.
- Wanaoshiriki watachunguza ripoti au ushahidi wa vyombo vya habari ili kuhuisha hali ambazo ziliwafanya Wajerumani kuondoka makwao siku zilizopita na hali zilizoenea katika maisha ya wahamiaji na wakimbizi nchini Ujerumani kwa sasa.
- Wanaoshiriki watajaribu, wakati wa kuwasilisha vipengele vyao vya muktadha vilivyoteuliwa kikamilifu, kuweka usawa kati ya nadharia na kipengee cha waasisi wa nadharia hiyo.



KAZI YA ZIADA ILIYOPENDEKEZWA YA KUSHUGHULIKIA STADI ZA MITAZAMO YA KIBINAFSI NA MAADILI ZA KUJIBU NA STADI ZA UTAMBUZI ZA KUTEKELEZA:

Waombe wanaoshiriki kutathmini Ujerumani kama nchi ambayo wahamiaji na wakimbizi wanaelekea.

- Rejelea nyenzo ambazo zimetangulizwa, kwa mfano, tovuti ya data ya uhamiaji (Portal ya Data ya Uhamiaji, 2020b), Viashiria vya Ustawi wa Watu (UNDP, 2019a) au ripoti za vyombo vya habari (The New Humanitarian, 2020).
- Wasilisha nchi asilia za wakimbizi na wahamiaji. Eleza mambo yanayowasukuma wakimbizi kutafuta hifadhi na wahamiaji kutafuta fursa bora za maisha nchini Ujerumani.
- Fanya hali za wakimbizi na wahamiaji nchini Ujerumani zieleweke kwa watu katika maeneo mengine ya ulimwengu — tumia picha, video au vyombo vingine vya habari.

KAZI YA ZIADA ILIYOPENDEKEZWA YA KUSHUGHULIKIA STADI ZA UTAMBUZI ZA KUFAHAMU NA KUCHANGANUA:

Toa ripoti kuhusu uhamiaji na uhamishwaji wa lazima katika Ujerumani, kwa kutumia vyombo vya habari vya nchini au vya kimataifa. Kila anayeshiriki anapaswa kufafanua vipengele muhimu katika ripoti hizi ambavyo ni muhimu kwa hadhira, vinavyowapa uwezo wa kufanya maamuzi sahihi kuhusu uhamiaji na kuhamishwa kwa lazima.



USOMAJI WA ZIADA:

Kiakademia:

Geddes, A., & Scholten, P. (2018). The politics of migration and immigration in Europe (2nd ed.) London: Sage.

Kiuanahabari:

Casey, R. (2019). The two contrasting sides of German refugee policy: 'They try to integrate some people while really try to get rid of others'. The New Humanitarian. Retrieved December 1, 2020, from <https://www.thenewhumanitarian.org/news-feature/2019/11/11/German-refugee-integration-policy>

Kitaasisi:

BAMF (2020). Putting people first: providing security, creating opportunities, embracing change. Retrieved December 2, 2020, from https://www.bamf.de/EN/Startseite/startseite_node.html

Marejeleo

- Al Jazeera (2019, September 30). German far-right group planned to carry out attacks. Retrieved May 28, 2020, from <https://www.aljazeera.com/news/2019/09/german-group-planned-carry-attacks-prosecutor-190930155253229.html>
- Amnesty International (2016a). 4 in 5 people worldwide say Yes, we welcome refugees! [Press release] Retrieved May 27, 2020, from <https://www.amnesty.org/en/latest/campaigns/2016/05/survey-4-in-5-worldwide-welcome-refugees/>
- Amnesty International (2016b). Refugees Welcome Survey 2016: The Results. Retrieved May 27, 2020, from <https://www.amnesty.org/en/latest/news/2016/05/refugees-welcome-survey-results-2016/>
- BAMF (2020). Putting people first: providing security, creating opportunities, embracing change. Retrieved December 2, 2020, from https://www.bamf.de/EN/Startseite/startseite_node.html
- Bauer, T., Dietz, B., Zimmermann, K. F., & Zwintz, E. (2005). German Migration: Development, assimilation, and labour market effects. In Zimmermann, K. F. (Ed.), *European Migration: What do we know?* (pp. 197-262). Oxford: Oxford University Press.
- Bennhold, K., & Eddy, M. (2020, February 21). 'Politics of Hate' takes a toll in Germany well beyond immigrants. *The New York Times*. Retrieved May 28, 2020, from <https://www.nytimes.com/2020/02/21/world/europe/germany-mayors-far-right.html>
- Bertelsmann Stiftung (2016). *Einwanderungsland Deutschland: Factsheet*. Gütersloh. Retrieved May 23, 2020, from https://www.bertelsmann-stiftung.de/fileadmin/files/Projekte/51_Religionsmonitor/BST_Factsheet_Einwanderungsland_Deutschland.pdf
- Bieber, F. (2017, December 4). Wo Einwanderung ihre legitimen Grenzen findet: Migrationskrise und Moral. *Frankfurter Allgemeine Zeitung (FAZ)*. Retrieved December 7, 2020, from <https://www.faz.net/aktuell/feuilleton/buecher/rezensionen/sachbuch/wo-einwanderung-ihre-legitimen-grenzen-findet-15306649.html>
- BMI (2020). Admission of ethnic German resettlers under the Federal Expellees Act. Berlin. Retrieved December 1, 2020, from <https://www.bmi.bund.de/EN/topics/community-and-integration/ethnic-german-resettlers/ethnic-german-resettlers-node.html>
- Bündnis Entwicklung hilft, & IFHV (2020). *World Risk Report 2019*. Berlin. Retrieved May 27, 2020, from <https://weltrisikobericht.de/wp-content/uploads/2020/09/WorldRiskReport-2020.pdf>
- Casey, R. (2019). The two contrasting sides of German refugee policy: 'They try to integrate some people while really try to get rid of others'. *The New Humanitarian*. Retrieved December 1, 2020, from <https://www.thenewhumanitarian.org/news-feature/2019/11/11/German-refugee-integration-policy>
- Ciobanu, R. O., Fokkema, T., & Nedelcu, M. (2016). Ageing as a migrant: Vulnerabilities, agency and policy implications. *Journal of Ethnic and Migration Studies*, 43(2), 164-181. <https://doi.org/10.1080/1369183X.2016.1238903>
- Connor, P. (2018, February 28). International migration from sub-Saharan Africa has grown dramatically since 2010. *Pew Research Center*. Washington, D.C. Retrieved March 3, 2021, from <https://www.pewresearch.org/fact-tank/2018/02/28/international-migration-from-sub-saharan-africa-has-grown-dramatically-since-2010/>
- Dagi, D. (2020). The EU-Turkey Migration Deal: Performance and prospects. *European Foreign Affairs Review*, 25(2), 197-216.
- Decker, F., Best, V., Fischer, S., & Küppers, A. (2020). *Vertrauen in Demokratie. Wie zufrieden sind die Menschen in Deutschland mit Regierung, Staat und Politik?* Bonn. Friedrich-Ebert-Stiftung. Retrieved May 27, 2020, from <http://library.fes.de/pdf-files/fes/15621-20190822.pdf>

- Der Bundespräsident (2020). Constitutional basis. Retrieved May 17, 2020, from <https://www.bundespraesident.de/EN/Role-and-Functions/ConstitutionalBasis/ConstitutionalBasis-node.html>
- Destatis (2016). Ältere Menschen in Deutschland und der EU. Wiesbaden. Retrieved December 1, 2020, from <https://www.bmfsfj.de/blob/93214/95d5fc19e3791f90f8d582d61b13a95e/aeltere-menschen-deutschland-eu-data.pdf>
- Destatis (2019). Ausländische Bevölkerung, Ergebnisse des Ausländerzentralregisters (Fachserie 1 Reihe 2). Wies-baden. Retrieved May 25, 2020, from https://www.destatis.de/DE/Themen/Gesellschaft-Umwelt/Bevoelkerung/Migration-Integration/Publikationen/Downloads-Migration/auslaend-bevoelkerung-2010200197004.pdf?__blob=publicationFile
- Destatis (2020a). Ausländerinnen und Ausländer. Retrieved May 23, 2020, from <https://www.destatis.de/DE/Themen/Arbeit/Arbeitsmarkt/Glossar/auslaenderinnen-auslaender.html>
- Destatis (2020b). Ausländerstatistik: 11,2 Millionen Ausländerinnen und Ausländer zum Jahresende 2019. Retrieved May 25, 2020, from <https://www.destatis.de/DE/Themen/Gesellschaft-Umwelt/Bevoelkerung/Migration-Integration/auslaenderstatistik-stichtag.html>
- Destatis (2020c). Population: Current population. Retrieved November 27, 2020 from https://www.destatis.de/EN/Themes/Society-Environment/Population/Current-Population/_node.html
- Destatis (2020d, January 17). Population growth in 2019 expected to be lowest since 2012 [Press release]. Wies-baden. Retrieved May 17, 2020 from https://www.destatis.de/EN/Press/2020/01/PE20_022_12411.html
- Destatis (2020e, October 26). United States' popularity as a destination for emigration has declined: Less Germans moving to the USA [Press release]. Wiesbaden. Retrieved November 29, 2020, from https://www.destatis.de/EN/Press/2020/10/PE20_N068_12411.html
- Dietz, B. (2000). German and Jewish migration from the former Soviet Union to Germany: Background, trends and implications. *Journal of Ethnic and Migration Studies*, 26(4), 635-652. DOI: 10.1080/713680499
- Eddy, M. (2015, August 13). Violent backlash against migrants in Germany asylum-seekers pour in. *The New York Times*. Retrieved May 28, 2020, from <https://www.nytimes.com/2015/08/14/world/europe/germany-migrants-attacks-asylum-seekers-backlash.html>
- EIU (2020, January 22). Global democracy has another bad year. *The Economist*. Retrieved May 27, 2020, from <https://www.economist.com/graphic-detail/2020/01/22/global-democracy-has-another-bad-year>
- EMN (2018). Asylum and migration: Glossary 6.0. European Migration Network. Brussels. Retrieved November 27, 2020, from https://www.emn.at/wp-content/uploads/2018/06/emn-glossary-6-0_en.pdf
- BMI (2020). Admission of ethnic German resettlers under the Federal Expellees Act. Berlin. Retrieved December 1, 2020, from <https://www.bmi.bund.de/EN/topics/community-and-integration/ethnic-german-resettlers/ethnic-german-resettlers-node.html>
- Bündnis Entwicklung hilft, & IFHV (2020). World Risk Report 2019. Berlin. Retrieved May 27, 2020, from <https://weltrisikobericht.de/wp-content/uploads/2020/09/WorldRiskReport-2020.pdf>
- Casey, R. (2019). The two contrasting sides of German refugee policy: 'They try to integrate some people while really try to get rid of others'. *The New Humanitarian*. Retrieved December 1, 2020, from <https://www.thenewhumanitarian.org/news-feature/2019/11/11/German-refugee-integration-policy>
- Ciobanu, R. O., Fokkema, T., & Nedelcu, M. (2016). Ageing as a migrant: Vulnerabilities, agency and policy implications. *Journal of Ethnic and Migration Studies*, 43(2), 164-181. <https://doi.org/10.1080/1369183X.2016.1238903>
- Connor, P. (2018, February 28). International migration from sub-Saharan Africa has grown dramatically since 2010. *Pew Research Center*. Washington, D.C. Retrieved March 3, 2021, from <https://www.pewresearch.org/fact-tank/2018/02/28/international-migration-from-sub-saharan-africa-has-grown-dramatically-since-2010/>

Dagi, D. (2020). The EU-Turkey Migration Deal: Performance and prospects. *European Foreign Affairs Review*, 25(2), 197-216.

Decker, F., Best, V., Fischer, S., & Küppers, A. (2020). Vertrauen in Demokratie. Wie zufrieden sind die Menschen in Deutschland mit Regierung, Staat und Politik? Bonn. Friedrich-Ebert-Stiftung. Retrieved May 27, 2020, from <http://library.fes.de/pdf-files/fes/15621-20190822.pdf>

Der Bundespräsident (2020). Constitutional basis. Retrieved May 17, 2020, from <https://www.bundespraesident.de/EN/Role-and-Functions/ConstitutionalBasis/ConstitutionalBasis-node.html>

Destatis (2016). Ältere Menschen in Deutschland und der EU. Wiesbaden. Retrieved December 1, 2020, from <https://www.bmfsfj.de/blob/93214/95d5fc19e3791f90f8d582d61b13a95e/aeltere-menschen-deutschland-eu-data.pdf>

Destatis (2019). Ausländische Bevölkerung, Ergebnisse des Ausländerzentralregisters (Fachserie 1 Reihe 2). Wies-baden. Retrieved May 25, 2020, from https://www.destatis.de/DE/Themen/Gesellschaft-Umwelt/Bevoelkerung/Migration-Integration/Publikationen/Downloads-Migration/auslaend-bevoelkerung-2010200197004.pdf?__blob=publicationFile

Destatis (2020a). Ausländerinnen und Ausländer. Retrieved May 23, 2020, from <https://www.destatis.de/DE/Themen/Arbeit/Arbeitsmarkt/Glossar/auslaenderinnen-auslaender.html>

Destatis (2020b). Ausländerstatistik: 11,2 Millionen Ausländerinnen und Ausländer zum Jahresende 2019. Retrieved May 25, 2020, from <https://www.destatis.de/DE/Themen/Gesellschaft-Umwelt/Bevoelkerung/Migration-Integration/auslaenderstatistik-stichtag.html>

Destatis (2020c). Population: Current population. Retrieved November 27, 2020 from https://www.destatis.de/EN/Themes/Society-Environment/Population/Current-Population/_node.html

Destatis (2020d, January 17). Population growth in 2019 expected to be lowest since 2012 [Press release]. Wies-baden. Retrieved May 17, 2020 from https://www.destatis.de/EN/Press/2020/01/PE20_022_12411.html

Destatis (2020e, October 26). United States' popularity as a destination for emigration has declined: Less Germans moving to the USA [Press release]. Wiesbaden. Retrieved November 29, 2020, from https://www.destatis.de/EN/Press/2020/10/PE20_N068_12411.html

Dietz, B. (2000). German and Jewish migration from the former Soviet Union to Germany: Background, trends and implications. *Journal of Ethnic and Migration Studies*, 26(4), 635-652. DOI: 10.1080/713680499

Eddy, M. (2015, August 13). Violent backlash against migrants in Germany as asylum-seekers pour in. *The New York Times*. Retrieved May 28, 2020, from <https://www.nytimes.com/2015/08/14/world/europe/germany-migrants-attacks-asylum-seekers-backlash.html>

EIU (2020, January 22). Global democracy has another bad year. *The Economist*. Retrieved May 27, 2020, from <https://www.economist.com/graphic-detail/2020/01/22/global-democracy-has-another-bad-year>

EMN (2018). Asylum and migration: Glossary 6.0. European Migration Network. Brussels. Retrieved November 27, 2020, from https://www.emn.at/wp-content/uploads/2018/06/emn-glossary-6-0_en.pdf

IOM (2019b). World Migration Report 2020. Retrieved December 1, 2020, from https://publications.iom.int/system/files/pdf/wmr_2020.pdf

Jopp, D. S., Wozniak, D., Damarin, A. K., Feo, M. de, Jung, S., & Jeswani, S. (2015). How could lay perspectives on successful aging complement scientific theory? Findings from a U.S. and a German life-span sample. *The Ger-ontologist*, 55(1), 91-106. <https://doi.org/10.1093/geront/gnu059>

Lüpke-Schwarz, M. (2014, February 5). The last victim of the Berlin Wall. *DW*. Retrieved May 24, 2020, from <https://www.dw.com/en/the-last-victim-of-the-berlin-wall/a-17408154>

- Mandiraci, B. (2020). Sharing the burden: Revisiting the EU-Turkey migration deal. Crisis Group. Retrieved November 22, 2020, from <https://www.crisisgroup.org/europe-central-asia/western-europemediterranean/turkey/sharing-burden-revisiting-eu-turkey-migration-deal>
- Marois, G., Bélanger, A., & Lutz, W. (2020). Population aging, migration, and productivity in Europe. *Proceedings of the National Academy of Sciences of the United States of America*, 117(14), 7690-7695. Retrieved December 2, 2020, from <https://doi.org/10.1073/pnas.1918988117>
- Migration Data Portal (2020a). Child and young migrants. Retrieved May 16, 2020, from <https://migrationdataportal.org/themes/child-and-young-migrants>
- Migration Data Portal (2020b). Germany. Retrieved August 14, 2020, from https://migrationdataportal.org/?i=stock_abs_&t=2019&cm49=276
- Miller, D. (2016). *Strangers in Our Midst: The Political Philosophy of Immigration*. Cambridge: Harvard University Press.
- Möhring, M. (2015). Mobilität und Migration in und zwischen Ost und West. In Bösch, F. (Ed.), *Geteilte Geschichte: Ost- und Westdeutschland 1970-2000* (369-410). Göttingen: Vandenhoeck & Ruprecht.
- Münz, R., & Weiner, M. (Eds.) (1997). *Migrants, refugees and foreign policy: U.S. and German policies toward countries of origin*. Providence, Oxford: Berghahn.
- Panagiotidis, J. (2015). What is the German's fatherland? The GDR and the resettlement of ethnic Germans from socialist countries (1949–1989). *East European Politics and Societies and Cultures*, 29(1), 120–146. <https://doi.org/10.1177/0888325414540934>
- Ponce, A. (2018). Is welfare a magnet for migration? Examining universal welfare institutions and migration flows. *Social Forces*, 11(5), 389. <https://doi.org/10.1093/sf/soy111>
- Psaropoulos, J. (2020, March 10). Turkey-Greece refugee crisis: Germany willing to take children in. Al Jazeera. Retrieved May 26, 2020, from <https://www.aljazeera.com/videos/2020/03/10/turkey-greece-refugee-crisis-germany-willing-to-take-children-in/>
- Razin, A., & Wahba, J. (2011). Migration policy and the generosity of the Welfare State in Europe. *CESifo*, 9(4), 28-31. Retrieved March 19, 2019, from <https://www.ifo.de/en/node/28288>
- Reporters Without Borders (2020). 2020 World Press Freedom Index. Retrieved May 27, 2020, from <https://rsf.org/en/ranking>
- Ritchie, H., & Roser, M. (2019). Age structure. *Our World in Data*. Retrieved May 20, 2020, from <https://ourworldindata.org/age-structure>
- Roudik, P. (2017). *Laws concerning children of undocumented migrants in selected countries*. Law Library of Congress. Washington, D.C. Retrieved November 23, 2020, from <https://www.loc.gov/law/help/undocumented-migrants/undocumented-migrant-children.pdf>
- Schmale, W. (2010). Europe as a cultural reference and value system. *European History Online (EGO)*. Retrieved October 17, 2018, from <https://d-nb.info/1031276416/34>
- Schmidt, C. M., & Zimmermann, K. F. (1992). Migration pressure in Germany: Past and future. In Zimmermann, K. F. (Ed.), *Population Economics. Migration and economic development*. Berlin, Heidelberg: Springer.
- Schmitz, F. (2020, April 18). Germany's evacuation of underage refugees from Greece seen as insufficient. DW. Retrieved May 26, 2020, from <https://www.dw.com/en/germanys-evacuation-of-underage-refugees-from-greece-seen-as-insufficient-aid-groups/a-53176001>
- Sola, A. (2018, February). The 2015 refugee crisis in Germany: Concerns about immigration and populism. SOEP-paper No. 966. Berlin. <http://dx.doi.org/10.2139/ssrn.3169243>

Staudenmaier, R. (2017, September 9). Refugee benefits in Germany are 'quite high,' Interior Minister de Maiziere says. DW. Retrieved December 1, 2020, from <https://www.dw.com/en/refugee-benefits-in-germany-are-quite-high- interior-minister-de-maiziere-says/a-40426704>

Steinmeier, W. (2019, September 1). Commemoration of Second World War at Warsaw, Warsaw. Retrieved May 17, 2020, from <https://www.bundespraesident.de/SharedDocs/Reden/EN/Frank-Walter-Steinmeier/Reden/2019/09/190901-Poland-Commemoration-Warsaw.html>

Süddeutsche Zeitung (2015, June 22). Denken wir heute nicht zu klein von uns? Gauck-Rede zu Flucht und Vertreibung. Retrieved May 21, 2020, from <https://www.sueddeutsche.de/politik/gauck-rede-zu-flucht-und-vertreibung-denken-wir-heute-nicht-zu-klein-von-uns-1.2530253>

SVR (2018). Integration Barometer 2018. Retrieved May 28, 2020, from https://www.svr-migration.de/wp-content/uploads/2018/09/SVR_Integration_Barometer_2018_Summary.pdf

The Economist (2018, July 12). Capitalism needs a welfare state to survive: But welfare must be reformed to cope with ageing and immigration. Retrieved December 1, 2020, from <https://www.economist.com/leaders/2018/07/12/capitalism-needs-a-welfare-state-to-survive>

Transparency International (2020). Corruption Perceptions Index: Germany. Retrieved December 1, 2020, from <https://www.transparency.org/en/countries>

Trevelyan, M., & Gareth, J. (2015, September 16). Which European countries offer the most social benefits to migrants? Euronews; Reuters. Retrieved December 1, 2020, from <https://www.euronews.com/2015/09/16/which-european-countries-offer-the-most-social-benefits-to-migrants>

Ulrich, R. (1990). Die Übersiedlerbewegung in die Bundesrepublik und das Ende der DDR. Forschungsgruppe Inter-nationale Beziehungen. Berlin. Retrieved December 12, 2020, from <https://bibliothek.wzb.eu/pdf/1990/p90-302.pdf>

UN News (2019). More than 90 per cent of African migrants would make perilous Europe journey again, despite the risks [Press release]. New York. Retrieved December 1, 2020, from <https://news.un.org/en/story/2019/10/1049641>

UNdata (2020). Country profile: Germany. Retrieved November 18, 2020, from <https://data.un.org/en/iso/de.html>

UNDESA (2001). Replacement migration: Is it a solution to declining and ageing populations? [Press release] New York. Retrieved November 18, 2020, from <https://www.un.org/en/development/desa/population/publications/ageing/replacement-migration.asp>

UNDESA (2017). International Migration Report 2017: Highlights. New York. Retrieved December 1, 2020, from http://www.un.org/en/development/desa/population/migration/publications/migrationreport/docs/MigrationReport2017_Highlights.pdf

UNDESA (2019a). Country profile: Germany: International migrant stock. Retrieved December 1, 2020, from <https://www.un.org/en/development/desa/population/migration/data/estimates2/countryprofiles.asp>

UNDESA (2019b). World Population Prospects 2019, Volume I: Comprehensive Tables. New York. Retrieved July 30, 2020, from https://population.un.org/wpp/Publications/Files/WPP2019_Volume-I_Comprehensive-Tables.pdf

UNDP (2019a). Human development indicators. Retrieved June 1, 2020, from <http://hdr.undp.org/en/content/statistical-data-tables-7-15>

UNDP (2019b). Human Development Report 2019: Beyond income, beyond averages, beyond today: Inequalities in human development in the 21st century. New York. Retrieved June 1, 2020, from <http://hdr.undp.org/sites/default/files/hdr2019.pdf>

UNDP (2019c). Scaling fences: Voices of irregular African migrants to Europe. New York. Retrieved November 13, 2019, from <https://www.africa.undp.org/content/rba/en/home/library/reports/ScalingFences.html>

UNHCR (2018). Global Trends: Forced displacement in 2017. Geneva. Retrieved August 25, 2018, from <http://www.unhcr.org/globaltrends2017/>

UNHCR (2019). Global Trends: Forced displacement in 2018. Geneva. Retrieved March 10, 2020, from <https://www.unhcr.org/5d08d7ee7.pdf>

Sola, A. (2018, February). The 2015 refugee crisis in Germany: Concerns about immigration and populism. SOEP-paper No. 966. Berlin. <http://dx.doi.org/10.2139/ssrn.3169243>

Staudenmaier, R. (2017, September 9). Refugee benefits in Germany are 'quite high,' Interior Minister de Maiziere says. DW. Retrieved December 1, 2020, from <https://www.dw.com/en/refugee-benefits-in-germany-are-quite-high-interior-minister-de-maiziere-says/a-40426704>

Steinmeier, W. (2019, September 1). Commemoration of Second World War at Warsaw, Warsaw. Retrieved May 17, 2020, from <https://www.bundespraesident.de/SharedDocs/Reden/EN/Frank-Walter-Steinmeier/Reden/2019/09/190901-Poland-Commemoration-Warsaw.html>

Süddeutsche Zeitung (2015, June 22). Denken wir heute nicht zu klein von uns? Gauck-Rede zu Flucht und Vertreibung. Retrieved May 21, 2020, from <https://www.sueddeutsche.de/politik/gauck-rede-zu-flucht-und-vertreibung-denken-wir-heute-nicht-zu-klein-von-uns-1.2530253>

SVR (2018). Integration Barometer 2018. Retrieved May 28, 2020, from https://www.svr-migration.de/wp-content/uploads/2018/09/SVR_Integration_Barometer_2018_Summary.pdf

The Economist (2018, July 12). Capitalism needs a welfare state to survive: But welfare must be reformed to cope with ageing and immigration. Retrieved December 1, 2020, from <https://www.economist.com/leaders/2018/07/12/capitalism-needs-a-welfare-state-to-survive>

Transparency International (2020). Corruption Perceptions Index: Germany. Retrieved December 1, 2020, from <https://www.transparency.org/en/countries>

Trevelyan, M., & Gareth, J. (2015, September 16). Which European countries offer the most social benefits to migrants? Euronews; Reuters. Retrieved December 1, 2020, from <https://www.euronews.com/2015/09/16/which-european-countries-offer-the-most-social-benefits-to-migrants>

Ulrich, R. (1990). Die Übersiedlerbewegung in die Bundesrepublik und das Ende der DDR. Forschungsgruppe Inter-nationale Beziehungen. Berlin. Retrieved December 12, 2020, from <https://bibliothek.wzb.eu/pdf/1990/p90-302.pdf>

UN News (2019). More than 90 per cent of African migrants would make perilous Europe journey again, despite the risks [Press release]. New York. Retrieved December 1, 2020, from <https://news.un.org/en/story/2019/10/1049641>

UNdata (2020). Country profile: Germany. Retrieved November 18, 2020, from <https://data.un.org/en/iso/de.html>

UNDESA (2001). Replacement migration: Is it a solution to declining and ageing populations? [Press release] New York. Retrieved November 18, 2020, from <https://www.un.org/en/development/desa/population/publications/ageing/replacement-migration.asp>

UNDESA (2017). International Migration Report 2017: Highlights. New York. Retrieved December 1, 2020, from http://www.un.org/en/development/desa/population/migration/publications/migrationreport/docs/MigrationReport2017_Highlights.pdf

UNDESA (2019a). Country profile: Germany: International migrant stock. Retrieved December 1, 2020, from <https://www.un.org/en/development/desa/population/migration/data/estimates2/countryprofiles.asp>

- UNDESA (2019b). World Population Prospects 2019, Volume I: Comprehensive Tables. New York. Retrieved July 30, 2020, from https://population.un.org/wpp/Publications/Files/WPP2019_Volume-I_Comprehensive-Tables.pdf
- UNDP (2019a). Human development indicators. Retrieved June 1, 2020, from <http://hdr.undp.org/en/content/statistical-data-tables-7-15>
- UNDP (2019b). Human Development Report 2019: Beyond income, beyond averages, beyond today: Inequalities in human development in the 21st century. New York. Retrieved June 1, 2020, from <http://hdr.undp.org/sites/default/files/hdr2019.pdf>
- UNDP (2019c). Scaling fences: Voices of irregular African migrants to Europe. New York. Retrieved November 13, 2019, from <https://www.africa.undp.org/content/rba/en/home/library/reports/ScalingFences.html>
- UNHCR (2018). Global Trends: Forced displacement in 2017. Geneva. Retrieved August 25, 2018, from <http://www.unhcr.org/globaltrends2017/>
- UNHCR (2019). Global Trends: Forced displacement in 2018. Geneva. Retrieved March 10, 2020, from <https://www.unhcr.org/5d08d7ee7.pdf>
- UNHCR (2020a). Global Trends: Forced displacement in 2019. Geneva. Retrieved August 20, 2020, from <https://www.unhcr.org/5ee200e37.pdf>
- UNHCR (2020b). UN agencies welcome first relocation of unaccompanied children from Greece. [Press release]. Retrieved May 26, 2020, from <https://www.unhcr.org/news/press/2020/4/5e9707ed4/un-agencies-welcome-first-relocation-unaccompanied-children-greece.html>
- UNHCR, UNICEF, & IOM (2019). Refugee and migrant children in Europe: Factsheet: Overview of trends, January- December 2018. Retrieved January 23, 2020, from <https://data2.unhcr.org/en/documents/download/69499>
- Von Weizsäcker, R. (1985, May 8). Speech during the Ceremony Commemorating the 40th Anniversary of the End of War in Europe and of National-Socialist Tyranny. Deutscher Bundestag, Bonn. Retrieved May 17, 2020, from https://www.bundespraesident.de/SharedDocs/Downloads/DE/Reden/2015/02/150202-RvW-Rede-8-Mai-1985-englisch.pdf?__blob=publicationFile
- Welcome Democracy (n. d.). Willkommenskultur und Demokratie in Deutschland: Flüchtlingspolitische Initiativen als Orte aktiver Bürgerschaft, kollektiver Konfliktaushandlung und demokratischen Lernens. Retrieved November 27, 2020, from <http://welcome-democracy.de/>
- Westwood, S. (Ed.) (2019). Ageing, diversity and equality. Abingdon: Routledge.
- World Bank (2020). Population ages 65 and above (% of total population). Retrieved December 1, 2020, from <https://data.worldbank.org/indicator/SP.POP.65UP.TO.ZS>
- Zick, A., Rees, J., Papendick, M., & Wäschle, F. (2020). MEMO: Multidimensional Remembrance Monitor: Study III. Institute for Interdisciplinary Research on Conflict and Violence at Bielefeld University. Retrieved December 1, 2020, from https://www.stiftung-evz.de/fileadmin/user_upload/EVZ_Uploads/Publikationen/Studien/EVZ_Studie_MEMO_2020_engl.pdf



MODULI 9

Uhamiaji na uhamaji katika Afrika: Kutoka barani, ndani ya bara, ndani ya nchi

na Monika Lengauer



MALENGO YA MODULI

- Kufahamu safari za Waafrika wahamiaji na wakimbizi kutoka Afrika (katika bara), ndani ya Afrika (kanda) na ndani ya nchi (ndani).
- Kuelewa utata wa uhamiaji wa Waafrika na uhamishwaji wa lazima katika miktadha ya nchi.
- Kusimulia “hadithi ya Kiafrika” ya wahamiaji na wakimbizi.



MATOKEO YA MAFUNZO

Kufikia mwisho wa moduli hii, washiriki wanapaswa kuwa na uwezo wa:

- Kuelezea hadithi zao za Kiafrika za wahamiaji na wakimbizi. → **Matokeo ya mafunzo kwa stadi za mitazamo binafsi na maadili: Kujibu**
- Kutumia maarifa na vyanzo kuandaa wasifu mfupi wa nchi na wasifu mfupi kuhusu uhamiaji na uhamaji wa kulazimishwa. → **Matokeo ya mafunzo kwa stadi za utambuzi: Kufahamu**
- Kuhusisha uhamiaji na uhamaji tofauti kutoka bara, ndani ya bara na ndani ya nchi. → **Matokeo ya mafunzo kwa stadi za utambuzi: Utekelezaji**
- Kuwa na ujuzi katika kuweka miktadha uhamiaji na uhamaji kutoka bara, ndani ya bara na ndani ya nchi kuzingatia mtazamo wa nchi ya kifani. → **Matokeo ya mafunzo kwa stadi za utambuzi: Kuchanganua**

Muhtasari

“Wakati mijadala mingi kuhusu uhamiaji wa Afrika¹ inalenga Bahari ya Mediteranean, ni muhimu kuisitiza kwamba uhamiaji na uhamaji wa jumla wa ndani ya Afrika unachangia 70% [ya uhamiaji wote wa Afrika]. Asilimia hii inapanda hadi 80% kwa nchi za Afrika Magharibi, Kati, Mashariki na Kusini”, alisema makamu mwandamizi wa Rais wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) Charles Boamah katika kikao cha Africa Resilience Forum (AfDB, 2019). Bw Boamah anakumbusha kwamba Waafrika walichangia karibu 10% ya uhamiaji wa kimataifa katika 2017 (AfDB, 2019). Kwa mwelekeo huu wa fikira, AU, katika ripoti yake ya kwanza kabisa ya uhamiaji wa Afrika, na wachapishaji wenza wake IOM wanataka kueleza “hadithi ya uhamiaji wa Waafrika kwa mtazamo wa Afrika” (Adepoju na wengine, 2020, uk. xiv.) Azma hii pia ni sehemu muhimu ya mwongozo huu (tazama Utangulizi na Moduli 1), tafiti zake (Moduli 6, 7) na Moduli hii ya 9. Inakusudia kuweka muktadha wa kauli mbili za kitaasisi za AfDB na AU/IOM, na imewaalika waandishi watatu mashuhuri — William Tayeebwa kutoka Uganda, Levi Manda kutoka Malawi na Levi Obonyo kutoka Kenya — kusimulia hadithi za Kiafrika za wahamiaji, wakimbizi na jamii zinazowapokea. Inatarajiwa kwamba waelimishaji wa uanahabari wanaotumia mwongozo huu watahimiza madarasa yao kuandika hadithi zao za Kiafrika za wahamiaji wa Kiafrika na wakimbizi

1 Kumbuka ufafanuzi wa uhamiaji na wahamiaji wa kimataifa kama ilivyobainishwa katika Moduli 2 na kufafanuliwa katika faharasa zinazopendekezwa katika Moduli 2 (EMN, 2018; IOM, 2019a; UNHCR, n. d.).

wa Kiafrika na pia jumuiya zinazowapokea kulingana na ujuzi, kitaaluma na uzoefu, na kuzipakia kwenye tovuti ya mradi www.mediaandmigration.com

Takwimu ambazo hutolewa na taasisi, jumuiya za washauri, vyombo vya habari na matumizi ya umma zinapaswa kushughulikiwa kwa tahadhari (angalia Moduli 2). Kupima uhamiaji na uhamaji wa kulazimishwa kutoka Afrika si rahisi, kwa sababu data bado ni chache. Ripoti ya Uhamiaji Afrika ya 2020 inaangazia ukweli kwamba bara halijasahihisha jumla ya idadi ya wahamiaji wa kimataifa tangu mwaka 2000 wa sensa ya watu (Adepoju na wengine, 2020, uk. 15-16). Nchi nyingi za za Kiafrika pia “hazina uwezo wa kukusanya data ya kiwango cha juu na kuiainisha kulingana na jinsia na umri” (Adepoju na wengine, 2020, uk. 15), na “takwimu rasmi zisizototisha hazisawiri picha kamili ya uhamiaji katika Afrika kwa sababu uhamiaji na uhamaji mwingi si wa kawaida” (Adepoju na wengine, 2020, uk. 20). Upungufu wa data kuhusu wahamiaji na wakimbizi umekuwa tatizo la mara kwa mara kama inavyojitokeza katika takriban moduli zote za mwongozo huu, suala ambalo limeshughulikiwa hasa katika Moduli 2 lakini pia katika sehemu za jinsia (tazama Moduli 3 na 7). Isitoshe, kama ilivyoonyeshwa hapo awali, suala la ufafanuzi ni muhimu — ni nani anayerejelewa wakati Bw Boamah anataja uhamiaji wa kimataifa? Wahamiaji? Wakimbizi? Kukumbusha kuhusu data na ufafanuzi kuhusiana na suala hili: Takwimu zifuatazo zinafaa kwa ufafanuzi wa takwimu wa Umoja wa Mataifa wa mhamiaji wa kimataifa wa muda mrefu kama “[mtu] anayehamia nchi nyingine mbali na ile ya makazi yake ya kawaida kwa muda wa angalau mwaka mmoja (miezi 12)” (UNDESA, 1998, uk. 10, Sanduku 10). Ufafanuzi huu haujumuishi harakati ambazo zinatokana na “burudani, likizo, kutembelea marafiki na jamaa, biashara, matibabu au safari za kidini” (UNDESA, 1998, uk. 10, aya 37) lakini unajumuishwa watu wengine wote wanaohama au kukimbia, na la muhimu hasa katika mwongozo huu ni kwamba, unajumuisha watu waliohamishwa kwa lazima kama vile wakimbizi (EMN, 2018; IOM, 2019a; UNHCR, n. d.).

Uhamiaji wa kimataifa wa Waafrika kutoka barani


Wahamiaji wengi wa kimataifa katika nchi za Afrika za kusini ya Jangwa la Sahara (89%; UNDESA, 2019) wanatoka nchi nyingine katika eneo hilo². Kuhamia nchi jirani ni hatua ya kawaida (ya kwanza) katika uhamiaji wa kimataifa. Kutembea ndani ya eneo la nyumbani ni rahisi kwa wahamiaji wengi na vile vile, mara nyingi, kwa jamii zinazowapokea. Barani Afrika, kuvuka mpaka wa kimataifa, kwa mfano kutoka Guinea-Bissau na kuingia Gambia, huwa ni kama kuhamia eneo asili la kabila lako (Knörr & Kohl, 2016). Kielelezo 26 kinaonyesha harakati hizi za kawaida za kimataifa. Hata hivyo mwelekeo wa Afrika umebadilika: Kwa wahamiaji waliozaliwa Afrika, “idadi ya wanaoishi katika nchi iliyo nje ya eneo lao la kuzaliwa iliongezeka” (UNDESA, 2017, uk. 12). Kwa kulinganisha, idadi ya wahamiaji wa kimataifa ambao walihamia ndani ya eneo lao la kuzaliwa imeongezeka katika Asia, Ulaya, Amerika ya Kusini na mahali pengine kati ya 2000 na 2017 (UNDESA, 2017, uk. 11-12, Kielelezo 5).

2 Nambari na desimali zimefanywa herufi kamili katika maandishi haya katika juhudi za kuweka uwiano mzuri kati ya usahihi na usomaji.

Connor (2018; Kielelezo 27) anaonyesha hivyo pia — kwa kulinganisha uhamiaji wa kimataifa usio wa kawaida — uhamiaji na uhamaji wa Afrika. Kwa kulinganisha takwimu za kuanzia 1990 hadi 2017, anafichua kuwa idadi ya wahamiaji wa ndani ya bara la Afrika imepungua kwa asilimia saba kati ya 1990 na 2017 (kutoka 75% hadi 68%), na idadi ya Waafrika walioondoka kutoka barani imeongezeka — uhamiaji kwenda Ulaya umeongezeka kwa pointi sita za asilimia kutoka 11% hadi 17%, na Marekani kutoka 2% hadi 6%.

Kwa idadi kamili — iliyochapishwa na UN na IOM — wahamiaji wa Kiafrika wanaoishi nje ya bara “wameongezeka zaidi ya mara mbili [tangu 1990] wengi wao zaidi wakielekea Ulaya” (IOM, 2019b, uk. 54). Mnamo 2019, wahamiaji wengi waliozaliwa Afrika wanaoishi nje ya eneo hilo


Kielelezo 26 : Idadi ya wahamiaji wa kimataifa walioainishwa kulingana na eneo wanakotoka na wanakoenda, 2017



Tanbihi: NA inarejelea Amerika Kaskazini, LAC inarejelea Amerika ya Kusini na Caribbean. Takwimu hii inaonyesha kwamba watu huhamia mara kwa mara ndani ya eneo lao la kuzaliwa — lakini mtiririko huu wa kawaida umebadilika kwa Afrika: Kwa wahamiaji waliozaliwa Afrika, idadi ya wale wanaoishi katika nchi nje ya eneo lao la kuzaliwa imeongezeka (UNDESA, 2017, 2017). uk. 12-11). Marejeleo: UNDESA (2017, uk. 11, Kielelezo 5).

walikuwa wakiishi Ulaya (milioni 11), Asia (milioni tano) na Amerika Kaskazini (milioni tatu; IOM, 2019b, uk. 54). Kielelezo 28 kinaonyesha jinsi harakati za uhamiaji na uhamaji wa kimataifa za raia wa Afrika zimekua kwa kasi kati ya 1990 na 2019, kutoka bara lao na ndani yake. Idadi ya Waafrika wanaoondoka kutoka nchi zao ni kubwa sana katika mitazamo yote — idadi


Kielelezo 27: Maeneo ya wahamiaji kutoka nchi za Afrika za kusini ya Jangwa la Sahara yanabadilika (watu waliozaliwa nchi za Afrika za kusini ya Jangwa la Sahara na wanaoishi katika nchi nyingine, kwa nchi/eneo la makazi, %)



Mwaka 1990, asilimia 75 ya wahamiaji kutoka nchi za Afrika za kusini ya Jangwa la Sahara waliishi katika nchi nyingine za eneo hilo, sehemu ambayo ilishuka hadi 68% kufika 2017. Katika kipindi hicho, sehemu ya watu kutoka nchi za Afrika za kusini ya Jangwa la Sahara wanaoishi Ulaya na Marekani imeongezeka (Connor, 2018). Marejeleo: Connor (2018). Kielelezo chetu

kubwa ya watu huhamia nchi za ndani ya Afrika, idadi kubwa zaidi ya watu huondoka kabisa kutoka bara la Afrika. Kinyume chake, idadi ya watu wanaohama kutoka mabara mengine hadi Afrika ni ndogo sana (IOM, 2019b, uk. 55, Kielelezo 1).

Kielelezo 28: Harakati za kuingia, ndani na kutoka Afrika, 1990-2019



Harakati za kimataifa ndani ya Afrika zimeongezeka sana baada ya 2010, kama inavyoonyeshwa kwenye safu ya katikati. Harakati za kimataifa kutoka Afrika hadi kanda nyingine za dunia zimeongezeka sana tangu miaka ya 2000 (safu ya kulia). Kinyume chake, uhamiaji kuelekea Afrika ni mdogo sana (safu ya kushoto). Kumbuka: "Wahamiaji wa Afrika" (safu ya kushoto) inarejelea wahamiaji wanaoishi Afrika ambao walizaliwa katika eneo lingine la ulimwengu (kwa mfano Ulaya). "Wahamiaji ndani ya Afrika" (safu ya kati) inahusu wahamiaji waliozaliwa katika eneo hilo (Afrika) na wanaoishi nje ya nchi yao ya kuzaliwa, lakini bado ndani ya eneo la Afrika. "Wahamiaji kutoka Afrika" (safu ya kulia) inarejelea watu waliozaliwa Afrika wanaoishi nje ya eneo hilo (k.m. huko Ulaya). Chanzo: IOM (2019b, uk. 55, Kielelezo 1). Kielelezo chetu



ZOEZI LILILOPENDEKEZWA LA KUSHUGHULIKIA STADI ZA UTAMBUZI ZA KUTEKELEZA NA KUCHANGANUA, NA STADI ZA MITAZAMO YA KIBINAFSI NA MAADILI ZA KUJIBU:

Ruhusu darasa kujipatia maarifa ya kiasi kuhusu Uganda, mojawapo ya nchi yenye wahamiaji wengi na wengine waliohamishwa kwa lazima kabla ya kusoma mtazamo wa nchi wa William Tayeebwa. Waalike washiriki kuandaa wasifu mfupi wa nchi na wasifu mfupi kuhusu uhamiaji na uhamishwaji wa lazima katika Uganda.

- Kutunga wasifu hizi mbili, washiriki wachague data zao kutoka kwa vyanzo vilivyoonyeshwa katika Moduli 2.
- Ili kuleta uhai katika data, washiriki wachunguze ripoti za vyombo vya habari kutoka au kuhusu Uganda ambazo zinazoelimisha na kufafanua.
- Wawasilishe maelezo mafupi haya mawili kwa washiriki wengine wote na uhitimisha kwa mambo matano muhimu ili kubainisha sifa kuu za Uganda.

Mitazamo kutoka Uganda

na William Tayeebwa, PhD, Mhadhiri Mkuu, Idara ya Uanahabari na Mawasiliano, Chuo Kikuu cha Makerere, Uganda:



Chanzo : Binafsi

Umuhimu wa kutumia dhana za wahamiaji, mkimbizi, mtafuta hifadhi ya kisiasa na masharti yanayohusiana nayo katika uandishi wa kitaaluma au uanahabari jinsi yanavyotofautishwa na UNHCR na IOM (EMN, 2018; IOM, 2019a; UNHCR, n. d., UNHCR, 2018) unafafanuliwa na White (2015, uk. 15). Kwa kweli, wahamiaji na wakimbizi mara nyingi hutumia njia na mbinu sawa za usafiri, na hutumia mitandao sawa. Harakati za kuvuka mpaka zinazohusisha wahamiaji na wakimbizi zinarejelewa kama uhamaji na uhamiaji mchanganyiko.³Waganda ambao wamefukuzwa kutoka katika maeneo yao ya nyumbani kwa sababu yoyote ile — ikiwa ni pamoja na waliokimbia makazi yao kwa sababu ya vita vya wenyewe kwa wenyewe vilivyoanza 1986 hadi 2006 kati ya vikosi vya serikali na Lord’s Resistance Army (LRA) — lakini kusalia ndani ya mipaka hakuzingatiwi kuwa sehemu ya masimulizi ya uhamiaji (Hovil & Okello, 2006). Isitoshe, vyombo vya habari vya Uganda vinaelewa wazi tofauti kati ya wahamaji wa ndani (IDPs) na wakimbizi. Jambo ambalo halibainiki kikamilifu katika ripoti za vyombo vya habari pamoja na ripoti zingine za sera ni tofauti kati ya mkimbizi na mhamiaji.

UNHCR na IOM zilibainisha kuwa Uganda — ikiwa na wakimbizi milioni 1.4 mwaka 2020 — bado inahifadhi idadi kubwa zaidi ya wakimbizi katika muktadha wa nchi nyingine

3 Kwa ufafanuzi wa uhamaji na uhamiaji mchanganyiko, angalia faharasa zinazopendekezwa katika Moduli 2 (IOM, 2019a; EMN, 2018).

za Kiafrika zinazohifadhi wakimbizi. Wakimbizi wengi wametoka DRC, Rwanda na Sudan Kusini (Migration Data Portal, 2020c). Kulingana na tovuti ya UNHCR ya Uganda Comprehensive Refugee Response Portal (UNHCR, 2020d), karibu wakimbizi 80,000 wanaishi katika jiji kuu la Kampala ambapo wengi wanajishughulisha na biashara za kibinafsi; wakimbizi wengine wote nchini wanahifadhiwa katika wilaya 12 za nchi (Coggio, 2018). UNHCR inaonyesha idadi kubwa inatoka Sudan Kusini ikiwa na asilimia 62 au watu 888,000 ikifuatiwa na DRC yenye asilimia 29 au watu 420,000. Nyingine zilizo- fuatana kulingana na idadi ni Burundi, Somalia, Rwanda, Eritrea, Sudan, Ethiopia na nyinginezo (UNHCR, 2020d).

Sambamba na hali iliyotangulia, Afrika Kusini ina idadi kubwa zaidi ya wahamiaji wa kiu- chumi barani, wengi wao wakiwa ni Waganda. Hii ilifanya nchi kukabiliwa na mashambu- lizi ya chuki kwa wageni huku wananchi wakiandamana dhidi ya wageni wanaowatuhumu kuwanyang'anya kazi zao (Bekker, 2015; Worby na wengine, 2008).

Wakati nchi nyingi zikikabiliana na suala nzito kama hilo la uhamishwaji wa lazima kwa kupitisha sera ngumu za kuingia na kupata makazi, Uganda kwa

“Wakati Ulaya na Marekani zinajaribu zaidi njia za ubunifu kuweka vikwazo kwa wakimbizi kufikia maeneo yao, mbinu ya wazi ya mipaka ya Uganda inatia mataifa mengine mengi aibu. Zaidi ya hayo, serikali imechukua hatua muhimu kuruhusu uhuru zaidi wa kutembea na kupata kazi kwa wakimbizi, tena kwenda kinyume na makubaliano ya kimataifa. Vipengele chanya vya mtazamo wa Uganda, kwa hivyo, vinapaswa kupongezwa bila shaka” (Hovil, 2018a, uk. 3).

Kuhusiana na sera ya kitaasisi, Hovil (2018a) anafuatilia maendeleo mbalimbali kuto- ka enzi za ukoloni kuanzia sheria iliyopitishwa 1955 kudhibiti wakimbizi kutoka Sudan, 1955 Control of Refugees from the Sudan Ordinance, hadi baada ya uhuru Control of Alien Refugees Act (CARA) ya 1960 ambayo ndiyo msingi wa sera ya 1999 “Mkakati wa Kujitegemea (SRS)” na 2003 “Msaada wa Maendeleo kwa Maeneo ya Kuhifadhi Wakim- bizi (DAR)” (Hovil, 2018a, uk. 6). Hovil anabainisha kuwa katika mifumo yote ya sera zilizopita na za sasa, hadhi ya kisheria ya wakimbizi hao ambao wamechagua kuishi mijini inabakia kuwa na utata kwa vile hawapati msaada wowote na “kwa kiasi kikubwa nje ya wigo wa sera rasmi za wakimbizi za Uganda” (Hovil, 2018a, uk. 7). Wakati mfumo wa sera wa kina uliwekwa katika Sheria ya Wakimbizi ya 2006 ambayo ilizingatia Mkataba wa Wakimbizi wa Umoja wa Mataifa wa 1951 (UNHCR, 2010) na Mkataba wa Wakimbizi wa OAU wa 1969 (OAU, 1969), wachanganuzi wamebaini kuwa utekelezaji ulikuwa wa polepole hadi wakati mzozo mpya ulipozuka Sudan Kusini mwaka 2013 na kulazimisha maelfu ya watu kukimbilia Uganda, ndiposa ukaleta nia mpya na nguvu katika kutekeleza Sheria (Bernstein na wengine, 2005; Hovil, 2018a; Watera na wengine, 2017).

Upungufu katika utekelezaji wa sera zilizowekwa za wakimbizi licha ya kuwa mvuto chanya wa modeli hiyo ya Uganda, ulitikiswa mwaka 2016 wakati vyombo vya habari vya ndani na kimataifa viliporipoti jinsi maafisa wa serikali ya Uganda ambao wanashtakiwa kwa usimamizi wa wakimbizi, wamehusika katika vitendo vya rushwa ambavyo ni pamoja na kuongeza idadi ya wakimbizi wanaotafuta hifadhi na wakimbizi katika baadhi ya kambi ili kufaidika na ufadhili wa kimataifa (Okiror, 2018; Patton, 2016). Kutokana na hali hiyo, nchi kadhaa wafadhili na mashirika yalisitisha ufadhili, hali iliyowaweka wakimbizi katika hali ngumu na kulazimisha serikali ya Uganda kuchukua hatua kupunguza kukaribisha

wakimbizi zaidi nchini (Green, 2018; Matengo, 2019). Wakati makadirio ya UNHCR na IOM yanaonyesha kuwa wakimbizi zaidi wataendelea kuja Uganda kutoka DRC na Sudan Kusini, ni uhakika kwamba modeli hiyo ya Uganda itaendelea kuchunguzwa zaidi kitaifa na kimataifa. Hata hivyo kwa maelezo zaidi, Lucy Hovil wa IRRI, mkosoaji mkubwa wa modeli hiyo ya Uganda, aliandika katika Refugees Deeply kwamba bila jumuiya ya kima-taifa kutekeleza ahadi yake ya misaada zaidi ya kifedha pamoja na makazi mapya katika nchi tajiri zaidi duniani, modeli hiyo ya Uganda “itaporomoka kama nyumba iliyojengwa kwa kadi” (Hovil, 2018b).

Kuripoti kuhusu uhamiaji na uhamaji wa ndani wa Waafrika katika vyombo vya habari vya Uganda kunafuata mkondo sawa na katika nchi zingine za Kiafrika kama ilivyoadiliwa kwa njia inayofaa na White (2015), Fengler na wengine (2020) na Pierigh (2017). Mjadala mahususi zaidi kuhusu suala hili umelezwa kwa kifupi na Nakitare (2018) ambaye ananasa matokeo ya mjadala kati ya wanahabari katika 2018 Media Challenge Expo jijini Kampala ambayo iliwaleta pamoja “wanafunzi 356 wa uanahabari kutoka vyuo vikuu mbalimbali nchini Uganda, vyombo vya habari 45, mashirika 22 ya wakimbizi, mashirika tisa ya maendeleo ya vyombo vya habari na wawakilishi kadhaa wa serikali” kujadili na kushiriki katika muda wa siku tatu juu ya mada ya “kuweka upya taarifa za vyombo vya habari kuhusu wakimbizi nchini Uganda”.

Nakitare (2018) anasimulia kuwa wakati wa hafla hiyo, shirika la Ethical Journalism Network (EJN) lilitumia warsha mbili zilizolenga kutoa ujuzi wa utendaji kwa wanahabari wachanga kwa kutumia miongozo waliyoiandaa kuhusu ‘kuripoti uhamiaji’ na pia kuepu-kana na ‘mazungumzo ya chuki’ (EJN, n. d.). Anaona kuwa katika mawasilisho na mjadala, watafiti na watendaji wa vyombo vya habari walibainisha jinsi usawiri wa wakimbizi kama “watu wanaotangatanga bila mwelekeo” unavyosaidia kushawishi mjadala ya umma kuhusu wakimbizi. Ilikuwa dhahiri kutokana na tukio hilo la siku tatu kwamba shauku ya jinsi vyombo vya habari vinavyoripoti (na vinapaswa kuripoti) kuhusu wakimbizi na wahamiaji inaongezeka nchini (Turpin, 2018).

Uhamiaji wa kimataifa wa Waafrika ndani ya bara

Kuhusiana na harakati za ndani ya bara, idadi kubwa zaidi ya wahamiaji na wakimbizi wa Kiafrika wako Afrika Kaskazini, kwa mfano katika nchi zinazozungumza Kiarabu zinazopakana na Bahari ya Mediteranean, hasa Morocco, Tunisia, Algeria na Libya (inayojulikana kama sehemu ya Maghreb) na Misri. Hatari za ulinzi katika baadhi ya nchi hizi ni kubwa (UNHCR, 2020c). Maghreb na Misri aidha zimekuwa nchi za hifadhi au za kupita hadi Ulaya kwa wahamiaji na wakimbizi kutoka bara hilo. Lakini Afrika Kaskazini haipokei tu wahamiaji na wakimbizi kutoka nchi za Afrika za kusini ya Jangwa la Sahara, watu wake pia wanahama na/au wanakimbia, hasa wakilenga Ulaya na mataifa ya Ghuba la Kiarabu — raia wa Afrika Kaskazini kwa kawaida hawahami au kukimbilia ndani ya Afrika (IOM) 2019b, ukurasa wa 66). Sifa za Afrika Kaskazini kama nchi asili, usafiri na hatima ya wahamiaji na wakimbizi kwa wakati mmoja zinaonyesha mifumo changamano katika sehemu hii ya dunia (IOM, 2019b, uk. 66-68; Migration Data Portal, 2020b). Knoll & Teevan (2020) wanachanganua mifumo hii kupitia lenzi ya Mkataba wa Ulaya

wa 2020 juu ya uhamiaji na hifadhi (European Commission, 2020) na pia wakitilia maanani janga la Uviko-19. Wanahitimisha: “Ni wazi kwamba Uviko-19, kwa kuisitiza matatizo ya kijamii na kiuchumi katika eneo lote, utatatiza zaidi mchakato wa kurekebisha mifumo ya hifadhi na uhamiaji” (Knoll & Teevan, 2020, uk. 2). Katika Afrika, Afrika Kusini inasalia kuwa kivutio kikubwa zaidi (Migration Data Portal, 2020a). Katika mashariki na kusini mwa Afrika, idadi kubwa ya wahamiaji wasio wa kawaida wanahama, mara nyingi katika mtiririko mchanganyiko⁴, na kufurushwa na sababu nyingi za muktadha. Usafirishaji wa wahamiaji haramu ni hatari sana (IOM, 2019b, uk. 61-64). Katika Afrika Magharibi, watu wengi wanahamia ndani ya kanda ndogo (IOM, 2019b, uk. 64), ambapo Afrobarometer iligundua kuwa watu kutoka Afrika ya Kati na Magharibi “wana uwezekano mkubwa wa kufikiria juu ya uhamiaji kuliko Waafrika wa Kusini na Mashariki” (Appiah -Nyamekye Sanny & Rocca, 2018, uk. 10). Uhamiaji wa kikanda katika Afrika Magharibi unawezeshwa na makabila mengi yaliyoenea katika mipaka ya kitaifa, mitandao yao ni imara, na safari hazina visa kama suala la sera kwa jumuiya ya kikanda kama vile ECO-WAS.⁵ Watu huhama hasa kama wafanyakazi wahamiaji katika sekta zenye ujuzi wa chini. ikiwa ni pamoja na biashara isiyo rasmi, kilimo na kazi za nyumbani. Katika Afrika ya Kati, uhamiaji wa wafanyakazi hupatikana mara kwa mara hadi Gabon, wakati migogoro na ukosefu wa utulivu huchangia pakubwa katika watu kuhama (IOM, 2019b, uk. 61-68).

Miongoni mwa nchi 20 bora za Afrika zinazopokea wahamiaji pia ni Afrika Kusini, Ivory Coast na Uganda (IOM, 2019b, uk. 57, Kielelezo 3). William Tayeebwa anafichua katika mtazamo wa nchi yake, Uganda (tazama usimulizi wa awali), jinsi nchi hiyo inavyosifiwa kimataifa kama nchi mfano wa jinsi wahamiaji na wakimbizi wanapokewa kutokana na sera yake ya milango wazi, na jinsi ambavyo imeshutumiwa pia kwa kuhusika kwake katika udanganyifu mkubwa wa kiasi cha fedha za msaada kwa sera yake.

Uhamiaji wa ndani ya bara ni suala la sera, linalowezeshwa na jumuiya za kanda kama vile Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na ECOWAS. Mnamo 2019, ECOWAS iliadhimisha miaka 40 ya Makubaliano ya Harakati Huru za Afrika Magharibi ya 1979 ambayo yanahusiana na haki ya ukaazi, na yanakusudia kuhimiza utangamano na maendeleo ya kanda (ECOWAS, 2019). AU, pia, yanahimiza sana uhamiaji wa ndani ya bara. AU katika mpango wake wa maendeleo, Agenda 2063, unaolenga kuipigisha Afrika hatua za maendeleo, mojawapo ya miradi 15 bora inayotarajia kutekeleza ni kuwapa Waafrika “Paspoti ya Afrika na Usafiri Huru wa Watu”⁶ (AU, 2013; AU, n. d.). AU, inasemekana, inakubali kwamba sera zake zimepitwa na wakati, jambo ambalo limeruhusu “ushawishi wa nje kupotosha masimulizi” (Chutel, 2019). Kwa hivyo, katika

4 Kwa ufafanuzi wa “mitiririko mchanganyiko”, angalia faharasa zinazopendekezwa katika Moduli 2 (EMN, 2018; IOM, 2019a).

5 Jumuiya ya Kiuchumi ya Afrika Magharibi (ECOWAS) na nchi wanachama wake ambazo ni Benin, Burkina Faso, Cape Verde, Gambia, Ghana, Guinea, Guinea-Bissau, Ivory Coast, Liberia, Mali, Niger, Nigeria, Sierra Leone, Senegal na Togo (ECOWAS, 2016).

6 Lengo kuu la nne la Agenda 2063 ni mradi unaojumuisha pasipoti ya Kiafrika na harakati za usafiri huru: “Ondoa vikwazo kwa uweza wa Waafrika kusafiri, kufanya kazi na kuishi ndani ya bara lao. Mpango huo unalenga kubadilisha sheria za Afrika, ambazo kwa ujumla zinaweka vikwazo kwa watu kusafiri licha ya dhamira za kisiasa za kupunguza mipaka kwa nia ya kukuza utoaji wa viza kwa nchi wanachama ili kuongeza uhuru wa raia wa Afrika katika nchi zote za Afrika uhuru wa kutembea popote.” (AU, 2013; AU, n. d.).

ripoti yake ya kwanza kabisa ya Uhamiaji barani Afrika (Adepoju na wengine, 2020), AU pamoja na IOM inakusudia “kupinga masimulizi”, kama kichwa kidogo cha arifa za ripoti hiyo. Wachapishaji wanatoa ikisiri yao iliyo na mada tatu za:

“upotoshaji unaodhihirisha masimulizi ya sasa kuhusu uhamiaji wa Waafrika: (a) Wahamiaji wengi wa Kiafrika hawavuki bahari, bali wanavuka mipaka ya nchi kavu ndani ya Afrika; (b) Asilimia 94 ya uhamiaji Waafrika kuvuka bahari ni kawaida; na (c) Wahamiaji wengi duniani si Waafrika. Afrika inachukua asilimia 14 ya idadi ya wahamiaji duniani, ikilinganishwa, kwa mfano, hadi asilimia 41 kutoka Asia na asilimia 24 kutoka Ulaya. Haya yanaimarisha hitaji la kusimulia tena hadithi ambayo kwa kiasi kikubwa inahusu uhamiaji wa ndani ya Waafrika, kinyume na habari zilizo-tiwa chumvi na za kutisha za uhamaji usio wa kawaida kutoka Afrika kupitia Bahari ya Mediteranean” (Adepoju na wengine, 2020, uk. 1).

Wachapishaji hutoa ufasiri tofauti wa data, kwa mfano utafiti uliosambazwa sana na Afrobarometer (Appiah-Nyamekye Sanny & Rocca, 2018; Appiah-Nyamekye Sanny na wengine, 2019). Utafiti huo ulifanyika katika nchi 34 za Afrika ambapo Waafrika 45,000 wa Kiafrika walihojiwa kuhusu uhamiaji. Waandishi wanahitimisha:

“Kwa wastani, zaidi ya Mwafrika mmoja kati ya watatu (37%) wamefikiria kuhama, ikiwa ni pamoja na karibu mmoja kati ya watano (18%) ambao wamelifikiria suala hilo mara ‘nyingi’. Ni wachache sana wanaofanya mipango ya kuondoka, bila shaka. Lakini hata katika asilimia tatu tu ya watu, idadi ya Waafrika ambao wanasema wanajishughulisha sana na kupanga na kufanya maandalizi ya kuondoka, kama vile kupata viza, ni kubwa sana. Asilimia nyingine 11 ya watu wanasema wanapanga kuhama katika mwaka mmoja au miwili ijayo, ingawa kwa sasa hawafanyi maandalizi.” (Appiah-Nyamekye Sanny & Rocca, 2018, uk. 2)

Katika “kupinga simulizi”, wachapishaji wa ripoti ya kwanza ya AU ya Uhamiaji Afrika wanatoa tafsiri yao mbadala ya idadi, kwa kuwa “asilimia ndogo tu ya watu wanapanga na kujiandaa kwa bidii kuhama [...]. Katika Afrika Magharibi, watu milioni 10.3 waliripoti mwaka 2015 kwamba walikuwa wakifanya mipango ya kuhama katika kipindi cha miezi 12 ijayo lakini ni milioni 2.7 tu ndio walikuwa wamefanya maandalizi yoyote kwa ajili ya hatua hiyo” (Adepoju na wengine, 2020, uk. 19-20).

Afrobarometer pia inaripoti kwamba wengi wa waliojibu kwa kweli wangependelea kukaa karibu na nyumbani: 29% wanapendelea nchi nyingine ndani ya eneo lao na 7% nchi nyingine katika bara, ikilinganishwa na 27% ya wahojiwa ambao walionyesha upendeleo wao kwa Ulaya na 22% kwa Amerika Kaskazini. Ipasavyo, wengi wa wahamiaji wa nchi za Afrika za kusini ya Jangwa la Sahara walihamia katika nchi katika bara — ambayo waliona “ngumu” au “ngumu sana” wakati mwingine, wakilalamikia mahitaji ya viza, ukosefu wa kutambuliwa, na ulinganifu wa ujuzi na

uhitimu wakivuka kutoka nchi moja hadi nyingine. Sababu kuu za Waafrika kuondoka katika nchi zao zilikuwa kutafuta kazi (44%) na kuepuka umaskini (29%), kulingana na Afrobarometer ambao walipata majibu hayo mara kwa mara katika nchi zote zilizofanyiwa utafiti. Ni 6% tu ya waliohojiwa wanatafuta elimu nje ya nchi. “Kwa maneno mengine”, waandishi wanamaliza, watu wanatafuta “fursa ambayo hawawezi kuipata nyumbani” (Appiah- Nyamekye Sanny & Rocca, 2018, uk. 7).

UNDP katika ripoti yake *Scaling Fences* (2019b) waligundua kuwa thuluthi mbili ya washiriki waliohojiwa, kufanya kazi na kupata mishahara ya ushindani katika nchi zao hakujawazuia kuhama. Ilibainika kuwa zaidi ya 90% ya wahamiaji wa Kiafrika walikuwa tayari kufanya safari hatari ya Ulaya tena na tena.



ZOEZI LILILOPENDEKEZWA LA KUSHUGHULIKIA STADI ZA UTAMBUZI ZA KUTEKELEZA NA KUCHANGANUA, NA STADI ZA MITAZAMO YA KIBINAFSI NA MAADILI ZA KUJIBU:

Ruhusu washiriki kutafuta maelezo wawezayo kuhusu Malawi kama nchi mwenyeji wa wahamiaji na uhamishwaji wa kulazimishwa kabla ya kusoma mtazamo wa nchi uliotolewa na Prof. Levi Manda.

Waalike washiriki kuandaa wasifu mfupi wa nchi na wasifu mfupi kuhusu uhamiaji na kulazimishwa kuhama Malawi.

- Kutunga wasifu hizi mbili, washiriki wachague data kutoka kwa vyanzo vilivyoonyeshwa katika Moduli 2.
- Ili kuleta uhai wa data, washiriki wachunguze ripoti za vyombo vya habari kutoka au kuhusu Malawi ambazo zinaelimisha na kufafanua.
- Wawasilishe maelezo mafupi haya mawili kwa washiriki wengine wote na uhitimisha kwa mambo matano muhimu ili kubainisha sifa kuu za Malawi.

Mitazamo kutoka Malawi

na Levi Manda, PhD, Mlezi wa Taaaluma katika Shule ya Wahitimu ya Vyombo vya Habari na Mawasiliano, Chuo Kikuu cha Aga Khan, Malawi:

Malawi ni nchi ndogo kijiografia lakini yenye watu wengi Kusini-Mashariki mwa Afrika. Ina wakazi milioni 18 na eneo la kilomita 118,000 mraba. Malawi ni miongoni mwa nchi 10 zenye msongamano mkubwa wa watu barani Afrika. Asilimia 30 ya eneo hilo linachukuliwa na Ziwa Malawi, milima, vinamasi na mito (Migration Data Portal, 2019; UNdata, 2019).



Chanzo : Binafsi

Nchini Malawi, watu hujitambulisha kwa wilaya/maeneo na asili ya makabila. Kwa kawaida, Wamalawi watajitambulisha kama: Chewa/Nyanja ambao wanamiliki zaidi eneo la kati na sehemu za eneo la kusini mwa Malawi; kama Watumbuka ambao wengi wanapatikana katika maeneo ya magharibi ya eneo la kaskazini, kama Watonga ambao wanamiliki zaidi sehemu ya mashariki ya kaskazini na kati mwa Malawi; Yao walio wengi kwenye ufukwe wa ziwa kati na kusini mwa Malawi. Nchini Malawi, watu hujitambulisha kwa wilaya/maeneo na asili ya makabila. Kwa kawaida, Wamalawi watajitambulisha kama: Chewa/Nyanja ambao wanamiliki zaidi eneo la kati na sehemu za eneo la kusini mwa Malawi; kama Watumbuka ambao wengi wanapatikana katika maeneo ya magharibi ya eneo la kaskazini, kama Watonga ambao wanamiliki zaidi sehemu ya mashariki ya kaskazini na kati mwa Malawi; Yao walio wengi kwenye ufukwe wa ziwa kati na kusini mwa Malawi. Makabila mengine makubwa ni pamoja na Wangonde ambao wanaishi Kaskazini Mashariki mwa Malawi, na Lhomwe ambao wanamiliki kusini-mashariki mwa nchi (kwa muundo wa makabila tazama Ingham na wengine, 2020). Katika wilaya ya Chitipa, kuna zaidi ya makabila matano, kila moja ikiwa na lugha, desturi na utamaduni wake (Centre for Language Studies [CLS], 2006). Uhusiano wa kikabila hudhihirishwa wakati wa mazishi mtu anapozikwa nyumbani kwao ingawa huenda alizaliwa, akakua na kufanya kazi maisha yake yote katika jiji kuu lililo mbali na makazi yake ya kikabila. Ukabila unaonyeshwa hata kwenye nambari za usajili wa magari. Hivi sasa, sera ya kitamaduni ya Malawi inahimiza uundaji wa vyama vya kitamaduni na sherehe za utamaduni na mila (Serikali ya Malawi, 2011). Ukabila haupingani na ukweli kwamba jamii ya Malawi daima huwa safarini za kuhama. Uhamiaji mwingi wa ndani hufanyika. Hii inaweza kuwa ndani ya wilaya, ndani ya eneo, lakini pia kati ya kanda na kimataifa. Sababu kuu za uhamiaji wa ndani ni pamoja na kutafuta kazi, kambi za uvuvi (ugowi), na uhamisho kwa sababu ya ndoa, yaani, wakati mwanamume au mwanamke anapotoka katika kabila lake na kuanza maisha mapya na mwenzake. (Beegle & Poulin, 2013). Kwa kuwa jamii ya Malawi hufuata nasaba kukeni au kuumeni, hali ni hiyo hiyo katika ndoa ambapo maarusi hufuata mila ya kuhamia kukeni au kuumeni (Anglewicz, 2012).

Uhamiaji kwa sababu za kiuchumi pia unabainika kwa idadi kubwa ya Wamalawi katika nchi jirani za Tanzania, Msumbiji, Zambia, Zimbabwe na Afrika Kusini. IOM inakadiri kuwa takriban 79% ya wahamiaji wote wa kiuchumi wa Malawi wanahamia Afrika Kusini (IOM, 2015, uk. 1).

Benki ya Dunia inakadiri kuwa Wamalawi walioko ughaibuni hutuma kiasi kikubwa cha fedha kwa familia zao nchini Malawi, ambayo, mwaka 2020 (takwimu za Oktoba 2020), zilifikia dola milioni 189 au sehemu ya 2.3% ya pato la taifa — ongezeko kubwa ikilinganishwa na 2010 (dola milioni 22; Benki ya Dunia, 2020b). Kwa sababu ya uchache wa data ya kuaminika na ya sasa, wahamiaji wa kiuchumi katika nchi za kigeni mara nyingi hawaripotiwi kama IOM (2015) inavyokubali.

Callamard (1994) na Makhema (2009) wanaona kwamba wakati Malawi ilianza kuwakaribisha wakimbizi na wanaotafuta hifadhi katika miaka ya 1970, mtihani wake mkubwa kama nchi inayohifadhi wakimbizi ulikuwa kati ya 1986 na 1993 wakati Wamsumbiji milioni 1.2 walimiminika Malawi. Idadi hiyo ilikuwa kubwa sana hivi kwamba serikali ililazimika kuwahifadhi bila kufuata taratibu za kuwachunguza ipasavyo na hata wapiganaji walishukiwa kuhifadhiwa katika kambi 12 za wakimbizi (Callamard, 1994). Kabla ya kipindi hiki, wananchi wa Msumbiji walikuja kama familia ndogo zinazotafuta hifadhi na mahusiano nchini Malawi au kama watu binafsi wanaotafuta ulinzi.

Kwa kuzidiwa na wimbi la wakimbizi, Malawi ilibidi iombe usaidizi wa UNHCR na kambi zikaanzishwa katika wilaya zote 12 zinazopakana na Msumbiji (Dzimbiri, 1993). Akianadika kuhusu athari za kijamii na kiuchumi za wakimbizi wa Msumbiji, Dzimbiri (1993) alibainisha kuwa ingawa wakazi wa Malawi walinufaika kutokana na kuwahifadhi wakimbizi hao katika masuala ya ajira na biashara, wakimbizi hao waliilazimu Malawi kutumia fedha nyingi kwao na wakaathiri vibaya hali ya asili ya mazingira. Gomez & Christensen (2010), akitoa mfano wa ripoti ya pamoja ya Serikali ya Malawi, Benki ya Dunia, UNDP na UNHCR ya 1990, alibainisha kuwa kutokana na wimbi la wakimbizi wa Msumbiji, Malawi ilielekeza fedha kutoka kwa bajeti ya miundombinu, maendeleo na huduma za kijamii ya dola milioni 9.4 mwaka 1988 na dola milioni \$ 8.4 mwaka uliofuata kwa misaada ya wakimbizi. Dzimbiri (1993, uk. 6) ananukuu tathmini ya Serikali ya Malawi ya 1992 ambayo ilionyesha kwamba “ingawa ilifadhiliwa kwa kiasi na UNHCR, hati za matumizi ya sekta ya watu waliohamishwa makazi pekee ilionyesha jumla ya gharama ya ziada kwa Serikali ya Malawi ya dola milioni 25.1.” Ongezeko hili kubwa la matumizi ni dalili ya idadi ya wakimbizi katika Malawi wakati huo na kujitolea kwa Serikali ya Malawi. Nyaraka zinaonyesha kwamba wakati wa mzozo wa wakimbizi wa Msumbiji, umakini mkubwa ulikuwa kwenye hifadhi, riziki na afya badala ya utoaji bora wa elimu kwa wakimbizi. Muda mfupi baada ya wakimbizi wa Msumbiji kurejeshwa makwao kwa mafanikio kufuatia kumalizika kwa vita vya wenyewe kwa wenyewe 1993 (Callamard, 1994), kambi za wakimbizi zilifungwa. Baadaye, Malawi ilianza kupokea waomba hifadhi kutoka Kanda ya Maziwa Makuu ya Afrika wa Burundi, Rwanda na DRC. Baadhi ya wakimbizi hao wameishi, kupata watoto na hata wajukuu, walikufa na kuzikwa Malawi.

Ikilinganishwa na mzozo wa wakimbizi wa Msumbiji, hali ya wakimbizi baada ya 1993 nchini Malawi imebadilika kabisa. Wakimbizi wa sasa wako katika kambi moja ambapo wakati mmoja wakimbizi wa Msumbiji 2,852 walihifadhiwa lakini sasa wamerudishwa nyumbani kwa hiari (Chitsulo, 2018).

UNHCR inaendelea kusahihisha idadi na taarifa nyingine kuhusu wakimbizi na wanaotafuta hifadhi nchini Malawi, ikitoa data nyingi kupitia tovuti ya Operational Portal (UNHCR, 2020b): Kufikia Desemba 2020, kulikuwa na takriban wakimbizi 77,000 na wanaotafuta hifadhi nchini Malawi, karibu 30,000 kutoka DRC; 11,000 kutoka Burundi; 7,000 kutoka Rwanda; na 29,000 kutoka nchi nyingine (UNHCR, 2020b). Kwa sababu kuwarejesha nyumbani ni kwa hiari, Malawi haiwarudishi wakimbizi hao katika nchi zao za asili, hasa DRC, Rwanda na Burundi ambako kuna amani kiasi kwa sasa. Kwa hiyo, idadi ya wanao-wasili na wanaozaliwa inaongezeka. Kuanzia 2010 hadi 2014, idadi ya waliozaliwa kwa wakimbizi katika kambi ya Dzaleka iliongezeka kutoka 341 hadi 623 (WFP, UNHCR, & Serikali ya Malawi, 2014). Watoto hawa waliozaliwa katika ardhi ya Malawi wanastahili usajili wa kuzaliwa ili kuepuka kuwabaki bila utaiifa. Kimataifa, ni kinyume cha haki za binadamu kumfanya mtu yeyote, hasa watoto, kutokuwa na uraia (OHCHR, 1990).

Wanahabari wanahitaji kuelewa kwamba uhamiaji na uhamishwaji wa lazima na mambo kama vile mateso, migogoro, misingi ya kidini, uchumi, mabadiliko ya hali ya hewa, utawala na mambo mengine (tazama Moduli 3).

Uelewa wa kina wa vipengele hivi na vingine utasaidia wanafunzi wa uanahabari kuelewa kikamilifu mambo yanayosababisha uhamiaji na uhamishwaji wa kulazimishwa. Hadithi nzuri ni ya msingi wa ushahidi, ina muktadha wazi na uchambuzi ili kufichua hali ya kibinadamu ya wakimbizi, wanaotafuta hifadhi na wahamiaji wa kiuchumi.

Labda kutokana na kutoelewa uhamiaji na uhamishwaji wa lazima, uhamiaji na uhamaji wa watu wengi haziripotiwa mara kwa mara na vyombo vya habari nchini Malawi, isipokuwa tu wakati jambo kubwa au janga limetokea, kama vile kuhama kutokana na vimbunga na mafuriko au kufukuzwa au kuhamishwa kutoka nchi ya kigeni kwa sababu tofauti ikiwa ni pamoja na chuki ya wageni. Wahamiaji, wakimbizi na wanaotafuta hifadhi kwa hakika hawapo kwenye vyombo vya habari vya Malawi isipokuwa tu kunapokuwa na tukio kubwa sana, kama vile mpango wa kuwahamisha hadi eneo tofauti, mkoa au wilaya, kama vile Karonga, kwenye mpaka na Tanzania, na mpango ambao ulipingwa vikali na wenyeji (Kumwenda & Phimbi, 2016). Inaweza kuonekana kuwa kuangazia uhamiaji na uhamishwaji wa lazima sio kipaumbele cha vyumba vya habari nchini Malawi kwani hadithi nyingi kuhusu wahamiaji na wakimbizi zimeandikwa kwa mtazamo wa mashirika ya kimataifa ya misaada na ufadhili, kwa namna moja au nyingine.

Ili hadithi kuhusu uhamiaji na uhamishwaji wa lazima kupata kuangaziwa inavyostahili, wanahabari hawafai kuogopa kushirikisha watazamaji wao kwa mambo yanayowasukuma watu kuhama na kutoa changamoto kwa maadili ambayo yanaonekana kuwawekea mipaka watangazaji wa habari kwa kuwasisitizia kufuata '5Ws na H' za habari na piramidi iliyo-geuzwa ya uanahabari.

Uhamishwaji wa lazima kutokana na migogoro: wakimbizi na wahamiaji wa ndani (IDPs)

“Ingawa kulazimishwa kuhama ni jambo la kimataifa, linajulikana zaidi barani Afrika”, aliandika kamishna wa AU wa masuala ya kisiasa katika ripoti ya Afrika ya kituo cha ufuatiliaji wa wahamiaji wa ndani — Africa Report of the Internal Displacement Monitoring Centre (IDMC) (André na wengine, 2019, uk. 7), na kusisitiza kuwa “Afrika inakaribisha zaidi ya thuluthi moja ya watu waliolazimika kuhama duniani kote”. Hadi kufikia mwisho wa 2018, baadhi ya Waafrika milioni 17 walikuwa wakimbizi wa ndani (IDPs), milioni 7.4 walikuwa wakimbizi na 712,000 walikuwa watu wasio na utaiifa.⁷ Idadi inazidi kuongezeka, hata baada ya AU kutangaza 2019 kuwa “Mwaka wa wakimbizi, wanaorudi nyumbani na IDPs: Kuelekea suluhu za kudumu za kulazimishwa kuhamishwa” huku Uganda ikiwa bingwa (AU, 2019). Uhamishaji uliotokea 2019 kutokana na migogoro na maafa⁸ “una uwezekano wa kuendelea kuongezeka”, inatabiri IDMC katika ripoti yake ya Afrika (André na wengine, 2019, uk. 8). Afrika ndilo eneo lenye matatizo makubwa zaidi duniani kutokana na vita na migogoro (tazama pendekezo la darasani, Moduli 1). SIPRI, taasisi huru ya kimataifa inayojishughulisha na utafiti kuhusu migogoro, silaha, uhibitaji wa silaha na upokonyaji silaha, iliyoko Stockholm, Uswizi, iliripoti katika Kitabu chake cha Mwaka 2019:

“Nchi 11 zilikuwa na migogoro ya silaha katika eneo la Afrika la kusini ya Jangwa la Sahara mwaka 2018: Burkina Faso, Cameroon, CAR, DRC, Ethiopia, Mali, Niger, Nigeria, Somalia, Sudan Kusini na Sudan. Mingi ya migogoro hii inaingiliana katika majimbo na kanda, haswa katika Bonde la Ziwa Chad na Sahel, kama matokeo ya shughuli za kimataifa za vikundi vya Kiislamu vyenye vurugu, vikundi vingine vyenye silaha na mitandao ya uhalifu. Pia zinahusishwa na umaskini uliokithiri, utawala duni, udhaifu wa kiuchumi na viwango vya chini vya ustahimilivu. Masuala mtambuka matatu pia yalichagiza eneo hili mwaka wa 2018: (a) kuendelea kwa shughuli za kimataifa za kukabiliana na ugaidi barani Afrika; (b) mabadiliko katika kiwango na kujirudia kwa ghasia zinazohusiana na uchaguzi; na (c) uhaba wa maji na kuongezeka kwa athari za mabadiliko ya hali ya hewa” (SIPRI, 2019, uk. 3).

Mwaka mmoja baadaye, idadi ya nchi zilizo na mizozo ya kijeshi iliongezeka kutoka 11 hadi angalau 15 (SIPRI, 2020, uk. 8).

Wakati Ajenda 2063 ya AU inalenga “Kunyamazisha bunduki ifikapo 2020” (AU, 2013; AU, n. d.), UNHCR ilihitimisha katika ikisiri yake ya Afrika ya Ripoti ya Kimataifa ya 2017 kwa tathmini kwamba: “suluhu mpya za kisiasa zinaonekana” (UNHCR, 2017, Dibaji). Bunduki hazijanyamizishwa kufikia 2021. Utafiti ulionukuliwa sana unahitimisha kuwa vita vya wenyewe kwa wen-

7 Dokezo kuhusu data ambayo haiwezi kulinganishwa mara kwa mara katika vyanzo vyote: UNHCR inanukuu data ya IDMC kwa idadi ya IDPs (UNHCR, 2020a, uk. 3, Tanbihichini 1).

8 IDMC inagawanya maafa kama ya kijiografia (mitetemko ya ardhi, milipuko ya volkeno) na yanayohusiana na hali ya hewa (dhoruba; tufani, vimbunga; mafuriko; joto kali; maporomoko ya ardhi; ukame; moto wa nyika) (IDMC, 2020, uk. 33-33, uk. Kielelezo A.8).

yewe barani Afrika vinatokana na viwango vya juu vya umaskini,⁹ taasisi za kisiasa zilizoshindwa kufanya kazi zake ipasavyo na utegemezi wa kiuchumi kwa rasilimali asilia ambayo mkakati bora ungekuwa mageuzi ya kidemokrasia, utawala bora (Elbadawi & Sambanis, 2000). SIPRI, pia, inaamini kwamba migogoro katika Afrika inahusishwa na umaskini uliokithiri (tazama nukuu la awali). Zaidi ya 40% ya “maskini duniani wanaishi katika uchumi ulioathiriwa na hali tete, mizozo na vurugu, na idadi hiyo inatarajiwa kuongezeka hadi 67% katika muongo ujao” (Benki ya Dunia, 2020a). Idadi ya watu maskini inakadiriwa kuongezeka zaidi katika muunganiko wa migogoro, maafa na janga la Uviko-19 (Benki ya Dunia, 2020a).

Umaskini umeenea miongoni mwa wakimbizi na IDPs, ikiwa ni pamoja na umaskini uliokithiri. Utafiti wa Benki ya Dunia (2019) kuhusu wakimbizi wa ndani umefichua kuwa migogoro ya silaha, ghasia na ukosefu wa usalama ndizo sababu kuu za watu kuhama katika Nigeria, Somalia, Sudan Kusini na Sudan; utafiti unajumuisha wakimbizi, IDPs na jumuiya zinazowahifadhi. Inaonyesha kuwa karibu jamii tisa kati ya 10 zilizohamishwa nchini Sudan ziliondolewa kwa sababu ya migogoro (Benki ya Dunia, 2019, uk. 12). Wakimbizi na IDPs wako katika hatari zaidi na maskini zaidi kuliko wakazi ambao tayari ni maskini sana, hasa katika wakazi wa vijijini. Zaidi ya wahamiaji wanane kati ya 10 katika nchi hizo nne wanaishi katika umaskini uliokithiri. Wakimbizi ni maskini zaidi kwa pointi 38 za asilimia kuliko jumuiya zinazowapokea, wakati IDPs na jumuiya zinazowapokea wanakaribiana katika kiwango cha umaskini, hasa katika maeneo ya vijijini (Benki ya Dunia, 2019, uk. vii). Nchini Sudan Kusini, wakimbizi na IDPs wengi ni wanawake. Wanakabiliwa na hatari fulani: Hawawezi kujitosheleza kwa chakula wakilinganishwa na wanaume waliohamishwa, wana mwelekeo wa kuwa na matokeo mabaya zaidi ya elimu na kazi kuliko wanaume (Benki ya Dunia, 2019, uk. vii). Watoto walio na umri wa chini ya miaka 15 wanawakilisha idadi kubwa ya wakimbizi (zaidi ya 50%) na pia IDPs (karibu 50%), ambayo inaonyesha idadi kubwa katika familia (Benki ya Dunia, 2019, uk. vi). Kwa ujumla, “idadi ya watu maskini sana inaendelea kuongezeka katika nchi za Afrika za kusini ya Jangwa la Sahara, huku ikishuka kwa kasi katika maeneo mengine yote” (Wadhwa, 2018; tazama Kielelezo 29).

Wakimbizi wa ndani (IDPs)

Uhamiaji wa ndani katika nchi za Kiafrika kijadi umetafitiwa kama harakati kutoka maeneo ya vijijini hadi mijini na changamoto kubwa zinazohusiana na ukuaji wa miji na ujenzi wa miji mikubwa (Awumbila, 2014; Migration Data Portal, 2020d). Uhamishwaji wa lazima unazidisha changamoto za maeneo ya mijini kwani IDPs wanaishi katika vitongoji vilivyotengwa na bila huduma au makazi rasmi, miongoni mwa watu maskini wa mijini, ambapo pana uhaba wa maji safi, vyoo, elimu, nafasi za kazi na mengineyo, na kuwaacha kivyao na hatarini. IDPs wanazidi kuhamia mijini, ambayo mara nyingi inawapa kambi lakini “ukuaji haraka wa miji, usiopangwa katika maeneo mwenyeji unasababisha matatizo ya ajira, miundombinu, na ufikiaji wa huduma” kwa watu wote (tazama makala ya awali ya Levi Manda kuhusu Malawi; Benki ya Dunia, 2019, uk. 9). “Maskini wapya” labda wataishi hapa, katika vituo vya mijini, wakijishughulisha na

9 Mwongozo huu unaangazia aina mbili za umaskini; kwa maelezo, angalia Moduli 2.

huduma zisizo rasmi na sekta zile zilizoathiriwa zaidi na kufuli na vizuizi vya uhamiaji kutokana na Uviko-19 (Benki ya Dunia, 2020a).

AU imesifiwa kwa Mkataba wake wa “Ulinzi na Usaidizi wa Wakimbizi wa Ndani katika Afrika” — maarufu kama Makubaliano ya Kampala — kama chombo cha kwanza cha kisheria cha kanda kuhusu IDPs kinachopaswa kuzingatiwa na wote waliotia sahihi mkataba huo. Inawakilisha juhudi muhimu za kukuza uwajibikaji wa serikali kwa ulinzi na usaidizi wa IDPs. Muongo mmoja baada ya kuanza kutumika, hata hivyo, chini ya nusu ya wanachama 55 wa AU wameidhinisha makubaliano hayo, na matukio ya migogoro na maafa ya 2019 yanapendekeza kwamba idadi ya watu waliokimbia makazi yao huenda ikaendelea kuongezeka (André na wengine, 2019; Dieng, 2017).

Takriban Waafrika milioni 17 walikuwa wakimbizi wa ndani¹⁰ kutokana na migogoro kufikia mwisho wa 2018, idadi kubwa zaidi kuwahi kurekodiwa katika bara hili na karibu 40% ya jumla ya kimataifa, inaripoti IDMC (André na wengine, 2019, uk. 11). Majanga, hasa yale yanayohusiana na hatari za hali ya hewa kama vile mafuriko, dhoruba na ukame, yalisababisha watu wapya milioni 2.6 kuyahama makazi yao 2018.¹¹


Ingawa ulimwenguni kote, uhamiaji wa ndani unaosababishwa na mabadiliko ya hali ya hewa, kwa mfano huko Asia-Pasifiki, umeangaziwa kwa makini zaidi katika nchi za Afrika za kusini ya Jangwa la Sahara, uhamishwaji mpya ulifanyika hasa kutokana na vita 2018, isipokuwa Msumbiji (vimbunga Idai na Kenneth, 2019) au ukame wa Somalia¹². Kwa ujumla, mafuriko yanachangia 83% ya watu waliohama kutokana na maafa barani Afrika kati ya 2009 na 2018 (André na wengine, 2019, uk. 19).

10 UNHCR inaeleza kuwa IDPs walio chini ya ulinzi au usaidizi wa UNHCR ni “watu au vikundi vya watu ambao wame-lazimishwa kuacha nyumba zao au maeneo ya makazi yao ya kawaida, haswa kwa sababu ya, au ili kuepuka athari za migogoro ya kivita, hali za vurugu za jumla, ukiukwaji wa haki za binadamu au majanga ya asili au ya kibinadamu, na ambao hawajavuka mpaka wa kimataifa” (UNHCR, n. d.). Nambari zilizoshirikiwa hapa chini ni za IDMC.

11 Haijabainika ni watu wangapi ambao wamehamishwa na maafa kwa jumla kufikia mwisho wa 2018, hivyo basi kulinganisha uhamiaji kutokana na migogoro na kuhamishwa kwa maafa kwa mwaka huo ni vigumu sana. Jumla ya watu milioni 21.2 walihamishwa na maafa kati ya 2009 na 2018. Ukosefu wa data ya mwaka baada ya mwaka unaweza kuhusishwa na ukweli kwamba IDMC inadhibitiwa na “makadirio bora zaidi ya kiwango cha watu waliohamishwa barani Afrika, mapengo ya data yamesalia” (André na wengine, 2019, uk. 12, uk. 19).

12 Ukame ni kichocheo cha uhamiaji ambacho hakiripotiwa sana: IDMC ilirekodi watu milioni 1.6 waliohama makazi yao kutokana na ukame kati ya 2009 na 2018, lakini data hizi zilizoainisha na ukame zimepatikana tu tangu 2017 na kwa majaribio machache ya nchi (André na wengine, 2019, uk. 19).

Kielelezo 29: Idadi ya watu maskini sana inaendelea kuongezeka katika nchi za Afrika za kusini ya Jangwa la Sahara, huku ikishuka kwa kasi katika maeneo mengine yote (watu walio katika umaskini uliokithiri; mamilioni)



Makadirio yanaonyesha kuwa "fungu la maskini barani Afrika lilishuka kutoka 56% mwaka 1990 hadi 43% mwaka 2012 lakini kwa sababu ya ongezeko la watu, kwa idadi kamili, watu wengi zaidi ni maskini" (Benki ya Dunia, 2016), na hali hiyo inaendelea — lakini kwa Afrika pekee: Ulimwenguni kote, umaskini uliokithiri – watu wanaoishi kwa dola 1.90 kwa siku au chini ya hapo – umepungua. "Utabiri unaonyesha kuwa kufikia 2030, karibu watu tisa kati ya kila 10 maskini sana wataishi katika nchi za Afrika za kusini ya Jangwa la Sahara" (Wadhwa, 2018). Chanzo: Wadhwa (2018). Kielelezo chetu.

Maoni kutoka Kenya

na Prof. Levi Obonyo, Mkuu wa Shule ya Mawasiliano, Chuo Kikuu cha Daystar, Nairobi, Kenya:

Kenya imekuwa na historia ndefu ya kuwahifadhi wakimbizi. Majirani wengi wa Kenya wamekuwa na historia yenye misukosuko ya vita, majanga ya asili, na ukosefu wa utulivu wa kisiasa na kuwalazimisha raia kutafuta hifadhi kwingine. Katika siku za hivi karibuni, hata hivyo, wakimbizi wengi nchini Kenya wanatoka Sudan Kusini na Somalia. Wakimbizi hao kutoka Sudan Kusini kwa jadi wamehifadhiwa Kaskazini Magharibi mwa Kenya katika Kakuma, kaunti ya Turkana. Wakimbizi kutoka Somalia wamekuwa mpaka siku za karibuni waki-hifadhiwa katikati mwa mashariki mwa nchi kwa mfululizo wa kambi ambazo zimekuja kujulikana kama Daadab. Maeneo haya yako mbali sana na jiji la Nairobi na kwa kawaida ni maeneo yenye hali ngumu ya maisha. Wakimbizi wengi wamekaa katika kambi hizi kwa muda mrefu na kulea familia huko.



Chanzo : Binafsi

Habari kuhusu wakimbizi katika vyombo vya habari nchini zinafuata mielekeo ya kitamaduni, ikiwa ni pamoja na mitazamo ya kikabila. Kenya inajumuisha jamii nne kubwa: Wabantu waliofika katika eneo ambalo leo ni Kenya kutoka kusini, wa-Nilo Hamites walio-pitia sehemu ya magharibi, na watu wa asili ya Somalia na Ethiopia ambao hasa wanakaa sehemu ya kaskazini mwa nchi. Mojawapo ya mambo yanayotofautisha na wakati huo huo kuunganisha makundi haya ya watu wa nchi hiyo ya Afrika Mashariki ni lugha yao, kando na mazoea mengine ya kitamaduni. Wabantu — hata kama ni wa makabila tofauti — wanaweza kuelewana. Vikundi hivi vidogo vya makabila tofauti vina baadhi ya mambo yanayofanana. Kwa mfano, Wabantu wanaelekea kufanana, nao wa-Nilo Hamites wengi wana ngozi nyeusi sana. Lakini mazoea miongoni mwa makundi haya mapana yanatofautiana sana. Ingawa lugha inaunganisha, pia ni chombo cha kutenganisha. Kwa maana hii basi, Wasomali kwa ujumla wanaonekana kuwa tofauti na wengine nchini, jambo ambalo kwa mfano linaweza kuathiri utangazaji wa vyombo vya habari kuhusu wakimbizi katika Daadab.

Kwamba uanahabari wa Kenya unaathiriwa na — miongoni mwa sababu nyingine — usuli wa kitamaduni ni suala ambalo halihitaji kusesitizwa. Ingawa nchi ina baadhi ya wataalamu wasifika wa uanahabari, uchunguzi wa awali pia umeonyesha kuwa wanahabari wa Kenya wakati huo huo wanaeleza habari kwa mtazamo wa kikabila. Vyanzo vya habari kutoka jamii mahususi vinapendelea kutoa habari kwa wanahabari kutoka makabila yao, huku vyombo vya habari vikiwa na wakuu wa ofisi za nyanjani kutoka jamii za wenyeji isipokuwa miji mikuu ya Mombasa na Nairobi.

Hakika, ni sifa ya kutatanisha ya uanahabari wa Kenya kwamba wakati vyombo vya habari

vya kitaifa hutumia wanahabari kutoka jamii za mashinani ili kuangazia jumuiya hizo, utendaji kazi wa vyombo vya habari vya kimataifa ni tofauti. Kwa mantiki hii basi, wakimbizi katika Daadab wanaweza kuwa na fursa ya kutangazwa kwani vyombo vya habari vina zidi kuwaajiri wanahabari kutoka jamii hizi ambao wana uwezekano wa kujitambulisha na wakimbizi kwani wana mwelekeo mmoja wa kitamaduni.

Kuna maeneo matatu makuu ya wakimbizi nchini. Kambi za wakimbizi na wanaotafuta hifadhi karibu na mji wa Daadab zimekuwa mojawapo ya maeneo makubwa zaidi duniani, zikihifadhi zaidi ya wakimbizi nusu milioni hadi serikali ilipoamuru kufungwa majuzi. Kambi ya pili kwa ukubwa ya wakimbizi nchini Kenya ni ya Kakuma kaskazini magharibi mwa nchi. Inakaribisha karibu watu 200,000 (UNHCR, 2020e). Kakuma iko karibu na Sudan Kusini, lakini ni mbali kutoka Nairobi na inaleta changamoto za kufika huko kwa urahisi. Ingawa hali huko ni ngumu, si tofauti sana na walikotoka wakimbizi wenyewe na kuna uhusiano wa karibu kati ya wakimbizi na jamii mwenyeji. Hata hivyo, umbali wa kambi hizo kutoka katika miji ni changamoto kwa wanahabari wa Kenya hata wakitaka kuripoti kuhusu wakimbizi hao. Shughuli nyingi za vyombo vya habari vya Kenya hufanyika katika maeneo ya mijini, au maeneo ambayo yana watu wengi, wengi wao wakiwa kwenye njia ya reli ya jadi ya Kenya. Kakuma na Daadab zote ziko nje ya kile kinachoweza kuchukuliwa kama ukanda wa habari wa Kenya. Kwa kuanzia, iwe hadithi ya wakimbizi au la, matukio katika maeneo haya mara nyingi hayaripotiwi na vyombo vya habari kwa kawaida, na yanaporipotiwa, ripoti hutilia mkazo majanga kama vile njaa na maafa. Kwa sababu ya ufinyu wa bajeti, vyumba vya habari havichapishi ripoti za wanahabari katika sehemu hizi za nchi, na kwa vyovyote vile nafasi ya habari iliyotengwa kwa ajili ya habari kutoka sehemu hizi za nchi ni ndogo sana. Uchakataji wa habari wa Kenya umejikita kwenye ukanda mkuu wa habari. Kwa hivyo, haijasaidia kwamba — iwe Kakuma au Daadab — maeneo haya ya mbali na magumu kufikiwa hukumbwa na tatizo la kuzorota kwa usalama. Isitoshe, ukweli kwamba kambi hizo zimekuwepo kwa muda mrefu na hivyo basi kuondoa thamani yoyote ya habari za kuvuta hisia za wanahabari. Kambi hizi za wakimbizi zinahifadhi familia ambazo zimekuwa huko kwa muda mrefu au kweli zimelelewa huko.

Lakini sababu nyingine ya kutoangaziwa ipasavyo kwa hadithi za wakimbizi ni mtazamo wa kidesturi wa wanahabari wa kuwaona walio wachache kama “wengine wasio muhimu”. Walio wachache nchini huchukuliwa kuwa watu wawezao kupuuzwa, ikitiliwa maanani kwamba wanaishi mbali na maeneo makuu ya biashara, huduma muhimu na uongozi badala ya kupewa fursa kuwakilishi mtazamo mbadala wa maisha. Katika suala hili, wakimbizi ni wachache. Kwa ujumla, huduma ya wakimbizi nchini Kenya ni ya matukio. Huongezeka wakati kuna wimbi la wakimbizi kufuatia kuongezeka kwa migogoro katika nchi zao asili, au maafa ya asili yanayotokea nyumbani kama vile njaa kutokana na ukame.

Vyombo vya habari vya Kenya huangazia kambi hizo pakitokea fujo. Kwa vile utangazaji huu ni wa matukio, wanahabari husafirishwa huko kukusanya habari hitajika, kisha kurudi Nairobi. Kwa kiasi kikubwa maudhui ya vyombo vya habari kuhusiana na wakimbizi yana

mwelekeo wa mambo matatu: maoni ndiyo yanayoongoza yakifuatiwa na habari na tahariri nyingine. Ukiangazia kwa juu juu habari katika magazeti mawili yenye wasomaji wengi Kenya, The Daily Nation na Standard, hakuna tofauti yoyote katika jinsi zinawaangazia wakimbizi.

Kambi ya Daadab iliangaziwa zaidi na vyombo vya habari kufuatia agizo la serikali kwamba ifungwe. Kwa upande wa msisitizo wa habari, vyombo vya habari vinakatalia sifa kuu ya mtazamo wa ufadhili na masuala ya kibinadamu, ikifuatiwa na kuchunguza sera ya serikali na kiwango ambacho inazingatia sera na kanuni za kimataifa kuhusiana na jinsi inawashughulikia wakimbizi. Hali hii imezoroteshwa na kupunguzwa kwa bajeti za vyombo vya habari na kusababisha kuongezeka kwa uanahabari wa afisini ambapo wanahabari hawaendi nyanjani kukusanya habari, ila wanapambanya kutoka kwa mtandao. Isitoshe, vyombo vya habari hupatia hadithi za wakimbizi nafasi ndogo sana na idadi ya juu zaidi kuchapishwa magazetini kwa mwezi ilikuwa taarifa nane pekee za jumla ya nusu ukurasa. Mengine yanayochapishwa huwa ni maoni tu ya wadadisi kuhusu suala hilo, wala si habari kamili zinazotolewa na wakimbizi.

Kufuatia kufungwa kwa Daadab, hakujakuwa na hadithi za wakimbizi kwenye vyombo vya habari. Lakini kwa upande wa uwasilishaji chanya wa vyombo vya habari vya Kenya kuhusu wakimbizi, kambi ya Kakuma imeangaziwa kwa kiasi kikubwa kama sehemu jumuishi ya uchumi wa ndani. Mnamo 2020, kulikuwa na vituo vya redio vinavyotangaza katika eneo hilo, na huduma za kijamii zilitolewa kwa jamii. Wakazi wa kambi ya Kakuma waliunganishwa katika uchumi wa eneo hilo. Wakimbizi ambao wamehusishwa na kambi ya Kakuma lakini ambao wameingia katika jiji la Nairobi wana uwezo wa kupata uwakilishi mkubwa katika vyombo vya habari kuliko wale waliosalia Kakuma. Hii ni kwa sababu wanaanza kushindania rasilimali na wasomi wa Nairobi. Habari hasi za hivi majuzi zilikuwa za tajiri wa Sudan Kusini anayeishi Nairobi akijinaki na kuonyesha hadharani utajiri wake.

Huu ni muhtasari. Ripoti kamili inapatikana kwenye tovuti ya mradi www.mediaandmigration.com



USOMAJI WA ZIADA:

Kiakademia:

Elbadawi, I., & Sambanis, N. (2000). Why are there so many civil wars in Africa? Understanding and preventing violent conflict. *Journal of African Economies*, 9(3), 244-269. <https://doi.org/10.1093/jae/9.3.244>

Kiuanahabari:

Gardner, T. (2019, February 28). Ethiopia's neglected crisis: No easy way home for doubly displaced Gedeos. *The New Humanitarian*. Retrieved December 1, 2020, from <https://www.thenewhumanitarian.org/news-feature/2019/02/28/ethiopia-s-neglected-crisis-no-easy-way-home-doubly-displaced-gedeos>

Kitaasisi:

AU (2013). *Agenda 2063: The Africa We Want: A long-term 50-year development trajectory for Africa*. Retrieved December 2, 2020, from <https://au.int/en/agenda2063/overview>

Marejeleo

Adepoju, A., Fumagalli, C., & Nyabola, N. (2020). *Africa Migration Report: Challenging the narrative*. Addis Ababa. Retrieved October 19, 2020, from <https://publications.iom.int/system/files/pdf/africa-migration-report.pdf>

AfDB (2019). Migration takes centre stage at the third edition of the Africa Resilience Forum. Retrieved December 2, 2020, from <https://www.afdb.org/en/news-and-events/the-african-development-bank-calls-for-strong-responses-to-migration-at-the-3rd-africa-resilience-forum-19057>

André, C., Anzellini, V., Hajžmanová, I., & Leduc, C. (2019). *Africa Report on internal displacement*. IDMC. Retrieved December 7, 2019, from <https://www.internal-displacement.org/publications/africa-report-on-internal-displacement>

Anglewicz, P. (2012). Migration, marital change, and HIV infection in Malawi. *Demography*, 49(1), 239–265. <https://doi.org/10.1007/s13524-011-0072-x>

Appiah-Nyamekye Sanny, J., & Rocca, C. (2018). "Updata-ing" the narrative about African migration. Retrieved December 8, 2020, from <https://afrobarometer.org/sites/default/files/publications/Publications%20conjointes/par-te-naires/afrobarometer-moibrahim-updata-ing-the-narrative-about-african-migration.pdf>

Appiah-Nyamekye Sanny, J., Logan, C., & Gyimah-Boadi, E. (2019). In search of opportunity: Young and educated Africans most likely to consider moving abroad. Retrieved October 22, 2020, from http://afrobarometer.org/sites/default/files/publications/Dispatches/ab_r7_dispatchno288_looking_for_opportunity_africans_views_on_emigration1.pdf

AU (n. d.). *Flagship projects of Agenda 2063s*. Retrieved December 1, 2020, from <https://au.int/agenda2063/flagship-projects>

AU (2013). *Agenda 2063: The Africa we want: A long-term 50 year development trajectory for Africa*. Retrieved December 2, 2020, from <https://au.int/en/agenda2063/overview>

AU (2019). *Visit of the champion of the theme of the year 2019 to the Republic of Uganda*. Retrieved December 2, 2020, <https://au.int/en/newsevents/20191214/visit-champion-theme-year-2019-republic-uganda>

- Awumbila, M., Owusu, G., & Teye, J. K. (2014). Can rural-urban migration into slums reduce poverty? Evidence from Ghana. University of Sussex. Brighton. Retrieved December 8, 2020, from <http://www.migratingoutof-poverty.org/files/file.php?name=wp-13---awumbila-owusu-teye-2014-can-rural-urban-migration-into-slums-reduce-poverty-final.pdf&site=354>
- Beegle, K., & Poulin, M. (2013). Migration and the transition to adulthood in contemporary Malawi. *The Annals of the American Academy of Political and Social Science*, 648 (July: Youth Migration and Transitions to Adulthood in Developing Countries), 38-51. doi:10.1177/0002716213481329.
- Bekker, S. (2015). Violent xenophobic episodes in South Africa, 2008 and 2015. *African Human Mobility Review*, 229-252. Retrieved December 1, 2020, from <https://www.sihma.org.za/journals/1.Simon-Bekker1.pdf>
- Bernstein, J., Clark, C., Johnston, K. J., & Razia, S. (2005). "A drop in the ocean": Assistance and protection for forced migrants in Kampala. Refugee Law Project. Kampala. Retrieved March 6, 2020, from https://www.refugeelawproject.org/files/working_papers/RLP.WP16.pdf
- Callamard, A. (1994). Malawian refugee policy, international politics and the one-party regime. *Journal of International Affairs*, 47(2), 525-556. Retrieved December 2, 2020, from <https://www.jstor.org/stable/24357294>
- Centre for Language Studies (CLS) (2006). Language mapping survey for Northern Malawi. Zomba: University of Malawi. Retrieved March 9, 2020, from <http://unima-cls.org/Docs/MappingNorthernMalawi/Im-northernmalawi.pdf>
- Chitsulo, L. (2018, December 3). UNHCR to handover Luwani refugee camp to govt. *The Nation Online*. Retrieved March 3, 2020, from <https://www.mwnation.com/unhcr-to-handover-luwani-refugee-camp-to-govt/>
- Chutel, L. (2019, February 15). At least 80 % of African migrants never leave the continent, but the focus is on Europe. *Quartz Africa*. Retrieved December 2, 2020, from <https://qz.com/africa/1550885/at-least-80-of-african-migrants-never-leave-the-continent-but-the-focus-is-on-europe/>
- Coggio, T. (2018). Can Uganda's breakthrough refugee-hosting model be sustained? Migration Policy Institute. Retrieved March 6, 2020, from <https://www.migrationpolicy.org/article/can-ugandas-breakthrough-refugee-hosting-model-be-sustained>
- Connor, P. (2018). International migration from sub-Saharan Africa has grown dramatically since 2010. Pew Research Center. Retrieved December 1, 2019, from <https://www.pewresearch.org/fact-tank/2018/02/28/international-migration-from-sub-saharan-africa-has-grown-dramatically-since-2010/>
- Dieng, A. (2017). Protecting internally displaced persons: The value of the Kampala Convention as a regional example. *International Review of the Red Cross*, 99(1), 263-282. Retrieved July 10, 2018, from <https://international-review.icrc.org/articles/protecting-internally-displaced-persons-value-kampala-convention-regional-example>
- Dzimhiri, L. B. (1993). Political and Economic Impacts of Refugees: Some Observations on Mozambican Refugees in Malawi. *Refuge*, 13(6), 4-6. Retrieved December 2, 2020, from <https://refuge.journals.yorku.ca/index.php/refuge/article/view/21752/20422>
- ECOWAS (2016). Basic information. Retrieved November 15, 2020, from <https://www.ecowas.int/about-ecowas/basic-information/>
- ECOWAS (2019). 40 Years of free movement in ECOWAS. Retrieved September 23, 2020, from <https://www.ecowas.int/40-years-of-free-movement-in-ecowas/>
- EJN (n.d.). Ethical Guidelines for Migration Reporting: Five Point Guide for Migration Reporting. Ethical Journalism Network. Retrieved June 30, 2020, from https://cdn.ethicaljournalismnetwork.org/wp-content/uploads/2016/11/Migration-infographic_update-1.pdf
- Elbadawi, I., & Sambanis, N. (2000). Why are there so many civil wars in Africa? Understanding and preventing violent conflict. *Journal of African Economies*, 9(3), 244-269. <https://doi.org/10.1093/jae/9.3.244>

EMN (2018). Asylum and migration. Glossary 6.0. European Migration Network. Brussels. Retrieved November 27, 2020, from https://www.emn.at/wp-content/uploads/2018/06/emn-glossary-6-0_en.pdf

European Commission (2020). Communication from the Commission to the European Parliament, the Council, the European Economic and Social Committee and the Committee of the Regions on a New Pact on Migration and Asylum. Brussels. Retrieved December 2, 2020, from https://ec.europa.eu/info/sites/info/files/1_en_act_part1_v7_1.pdf

Fengler, S., Bastian, M., Brinkmann, J., Zappe, A. C., Tatah, V., Andindilile, M., Assefa, E., Chibita, M., Mbaine, A., Obonyo, L., Quashigah, T., Skleparis, D., Splendore, S., Tadesse, M. & Lengauer, M. (2020a). Covering Migration – in Africa and Europe: Results from a comparative analysis of 11 countries. *Journalism Practice*. <https://doi.org/10.1080/17512786.2020.1792333>

Gardner, T. (2019, February 28). Ethiopia's neglected crisis: No easy way home for doubly displaced Gedeos. *The New Humanitarian*. Retrieved December 1, 2020, from <https://www.thenewhumanitarian.org/news-feature/2019/02/28/ethiopia-s-neglected-crisis-no-easy-way-home-doubly-displaced-gedeos>

Goldstein, J. (2018, October 18). As rich nations close the door on refugees, Uganda welcomes them. *The New York Times*. Retrieved March 6, 2020 from <https://www.nytimes.com/2018/10/28/world/africa/uganda-refugees.html>

Gomez, P. M., & Christensen, A. (2010). The impacts of refugees on neighboring countries: A development challenge. World Bank. Retrieved March 9, 2020, from <http://documents.worldbank.org/curated/en/459601468337158089/pdf/620580WP0The0I0BOX0361475B00PUBLIC0.pdf>

Government of Malawi (2011). Malawi: National cultural policy. n. p. Retrieved March 9, 2020, from https://en.unesco.org/creativity/sites/creativity/files/activities/conv2005_eu_docs_malawi_policy.pdf

Green, A. (2018). Uganda went from being a model of refugee response to a cautionary tale. *World Politics Review*. Retrieved December 2, 2020, from <https://www.worldpoliticsreview.com/insights/26946/with-its-open-door-policy-toward-refugees-uganda-has-gone-from-model-to-cautionary-tale>

Hovil, L., & Okello, M. (2006). Only peace can restore the confidence of the displaced. IDMC. Retrieved March 6, 2020, from <https://www.internal-displacement.org/publications/only-peace-can-restore-the-confidence-of-the-displaced>

Hovil, L. (2018a). Uganda's refugee policies: The history, the politics, the way forward. IIRRI. Kampala. Retrieved March 6, 2020, from <http://refugee-rights.org/uganda-refugee-policies-the-history-the-politics-the-way-forward/>

Hovil, L. (2018b). We need a more honest discussion of Uganda's 'model' refugee policies: The idealization of Uganda's refugee model is unhelpful for Ugandans and refugees. *News Deeply*. Retrieved December 20, 2020, from <https://www.newsdeeply.com/refugees/community/2018/10/22/we-need-a-more-honest-discussion-of-ugandas-model-refugee-policies>

IDMC (2020). Methodological annex: Global report on internal displacement. Retrieved October 10, 2020, from <https://www.internal-displacement.org/global-report/grid2020/downloads/2020-IDMC-GRID-methodology.pdf>

Ingham, K., Phiri, K. M. G. P., Kadzamira, Z. D., Kalinga, O. J., & Mitchell, J. C. (2020). Malawi. *Britannica*. Retrieved December 2, 2020, from <https://www.britannica.com/place/Malawi/Malawi-since-1994>

IOM (2015). Migration in Malawi. Geneva. Retrieved August 5, 2019, from https://publications.iom.int/system/files/pdf/mp_malawi.pdf

IOM (2019a). Glossary on Migration. Geneva. Retrieved August 5, 2019, from https://publications.iom.int/system/files/pdf/iml_34_glossary.pdf

IOM (2019b). World Migration Report 2020. Geneva. Retrieved November 30, 2019, from https://publications.iom.int/system/files/pdf/wmr_2020.pdf

Knoll, A., & Teevan, C. (2020). Protecting migrants and refugees in North Africa: Challenges and opportunities for reform. ECPDM. Retrieved October 21, 2020, from <https://ecdpm.org/wp-content/uploads/Protecting-Migrants-Refugees-North-Africa-Challenges-Opportunities-Reform-Discussion-Paper-281-October-2020-ECDPM.pdf>

Knörr, J., & Kohl, C. (Eds.) (2016). The upper Guinea Coast in global perspective. *Integration and Conflict Studies: Vol. 12*. New York, Oxford: Berghahn.

Kumwenda, T., & Phimbi, E. (2016, October 31). Malawi govt decision to relocate Dzaleka refugee to Karonga angers residents. *Nyuasa Times*. Retrieved December 2, 2020, from <https://www.nyasatimes.com/malawi-govt-decision-relocate-dzaleka-refugee-karonga-angers-residents/>

Makhema, M. (2009). Social protection for refugees and asylum seekers in the Southern Africa Development Community (SADC). World Bank. Retrieved December 2, 2020, from <http://documents1.worldbank.org/curated/en/799011468104641822/pdf/491680NWPOAsyl10Box338943B01PUBLIC1.pdf>

Matengo, D. (2019, March 29). Uganda asks Rwandan, Burundian refugees to return home. *China General Television Network*. Retrieved March 7, 2019, from <https://africa.cgtn.com/2019/03/29/uganda-asks-rwandan-burundian-refugees-to-return-home/>

Migration Data Portal (2019). Malawi. Retrieved October 22, 2020, from https://migrationdataportal.org/?i=stock_abs_&t=2019&cm49=454

Migration Data Portal (2020a). Data: South Africa. Retrieved October 22, 2020, from https://migrationdataportal.org/?i=stock_abs_&t=2019&cm49=710

Migration Data Portal (2020b). Northern Africa Region. Retrieved October 21, 2020, from <https://migrationdataportal.org/regional-data-overview/northern-africa>

Migration Data Portal (2020c). Uganda. Retrieved October 21, 2020, from <https://migrationdataportal.org/?i=groups&t=2019&cm49=800>

Migration Data Portal (2020d). Urbanization and migration. Retrieved December 8, 2020, from <https://migrationdataportal.org/themes/urbanisation-et-migration>

Nakitare, R. (2018). Reframing media coverage of refugees and migrants in Uganda. *Ethical Journalism Network*. Retrieved March 7, 2020, from <https://ethicaljournalismnetwork.org/reframing-media-coverage-refugees-uganda>

OUA (1969). Convention governing the specific aspects of refugee problems in Africa: Adopted on 10 September 1969 by the Assembly of Heads of State and Government CAB/LEG/24.3. It entered into force on 20 June 1974. Addis Ababa. Retrieved December 1, 2020, from <https://www.unhcr.org/about-us/background/45dc1a682/oua-convention-governing-specific-aspects-refugee-problems-africa-adopted.html>

OHCHR (1990). Convention on the rights of the child. Retrieved March 22, 2020, from <https://www.ohchr.org/en/professionalinterest/pages/crc.aspx>

Okiror, S. (2018, October 30). Inquiry finds refugee numbers were exaggerated by 300,000 in Uganda. *The Guardian*. Retrieved March 6, 2020, from <https://www.theguardian.com/global-development/2018/oct/30/inquiry-finds-refugee-numbers-exaggerated-in-uganda>

Patton, A. (2016, August 20). Is Uganda the best place to be a refugee? *The Guardian*. Retrieved March 6, 2020, from <https://www.theguardian.com/global-development-professionals-network/2016/aug/20/is-uganda-the-best-place-to-be-a-refugee>

Pierigh, F. (2017). Changing the narrative: Media representation of refugees and migrants in Europe. *World Association for Christian Communication*. Retrieved March 7, 2020, from https://www.refugeesreporting.eu/wp-content/uploads/2017/10/Changing_the_Narrative_Media_Representation_of_Refugees_and_Migrants_in_Europe.pdf

SIPRI (2019). SIPRI Yearbook 2019: Summary. Retrieved December 4, 2020, from https://www.sipri.org/sites/default/files/2019-08/yb19_summary_eng_1.pdf

SIPRI (2020). SIPRI Yearbook 2020. Summary. Retrieved December 4, 2020, from https://www.sipri.org/sites/default/files/2020-06/yb20_summary_en_v2.pdf

Strochlic, N., & Lorec, N. (2019, April). In Uganda, a unique urban experiment is under way: The world's second largest refugee camp is slowly but surely transforming into a permanent city. National Geographic. Retrieved March 6, 2020, from <https://www.nationalgeographic.com/magazine/2019/04/how-bidibidi-uganda-refugee-camp-became-city/>

Turpin, S. (2018). Media coverage on migration: A practical guide for journalists. Retrieved March 7, 2020, from <https://rodakar.iom.int/sites/default/files/document/publications/Media%20Toolkit%202018%20-%20EN%20RO%20Dakar%20%281%29.pdf>

UNdata (2019). Country profile: Malawi. Retrieved October 22, 2020, from <http://data.un.org/en/iso/mw.html>

UNDESA (1998). Recommendations on statistics of international migration. Revision 1. New York. Retrieved December 8, 2020, from https://unstats.un.org/unsd/publication/seriesm/seriesm_58rev1e.pdf

UNDESA (2017). International Migration Report 2017: Highlights. New York. Retrieved December 1, 2020, from http://www.un.org/en/development/desa/population/migration/publications/migrationreport/docs/MigrationReport2017_Highlights.pdf

UNDESA (2019). International Migration 2019. Retrieved December 1, 2020, from https://www.un.org/en/development/desa/population/migration/publications/wallchart/docs/MigrationStock2019_Wallchart.pdf

UNDP (2019a). Human Development Report 2019: Beyond income, beyond averages, beyond today: Inequalities in human development in the 21st century. New York. Retrieved December 2, 2020, from <http://hdr.undp.org/sites/default/files/hdr2019.pdf>

UNDP (2019b). Scaling fences. New York. Retrieved November 13, 2020, from <https://www.africa.undp.org/content/rba/en/home/library/reports/ScalingFences.html>

UNGA (2018). Global Compact for Safe, Orderly and Regular Migration: Resolution adopted by the General Assembly on 19 December 2018. Retrieved September 22, 2020, from https://www.un.org/en/ga/search/view_doc.asp?symbol=A/RES/73/195

UNHCR (n. d.). Glossary. Retrieved December 7, 2020, from <http://www.issm.cnr.it/progetti/emigrazione/METADATA%20E%20GLOSSARI/UNHCR/GLOSSARY%20UNHCR.pdf>

UNHCR (2010). Convention and protocol relating to the status of refugees. Geneva. Retrieved July 1, 2018, from <https://www.unhcr.org/protection/basic/3b66c2aa10/convention-protocol-relating-status-refugees.html>

UNHCR (2017). Africa: Global Report 2017: Regional Summary Africa. Retrieved December 2, 2020, from <https://www.unhcr.org/publications/fundraising/5b30b9d07/unhcr-global-report-2017-africa-regional-summary.html>

UNHCR (2018). Migrant definition: Emergency handbook. Retrieved March 6, 2020, from <https://emergency.unhcr.org/entry/250459/migrant-definition>

UNHCR (2020a). Global Trends: Forced displacement in 2019. Copenhagen. Retrieved August 20, 2020, from <https://www.unhcr.org/5ee200e37.pdf>

UNHCR (2020b). Operational Portal: Malawi. Retrieved December 4, 2020, from <https://data2.unhcr.org/en/country/mwi>

UNHCR (2020c). Subregion: North Africa: 2019 End-year-report (Global Focus). Retrieved October 21, 2020, from <https://reporting.unhcr.org/sites/default/files/pdfsummaries/GR2019-NorthAfrica-eng.pdf>

UNHCR (2020d). Uganda comprehensive refugee response portal. Retrieved from December 4, 2020, from <https://data2.unhcr.org/en/country/uga>

UNHCR (2020e). Kakuma camp and Kalobeyi settlement. Operational Update 1-30 September 2020. Retrieved December 4, 2020, from <https://www.unhcr.org/ke/monthly-kenya-operation-updates>

Wadhwa, D. (2018). The number of extremely poor people continues to rise in Sub-Saharan Africa. World Bank. Retrieved December 8, 2020, from <http://blogs.worldbank.org/opendata/number-extremely-poor-people-continues-rise-sub-saharan-africa>

Watera, W., Seremba, C., Otim, I., Ojok, D., & Mukhone, B. (2017). Uganda's refugee management approach within the EAC policy framework: A study by youth4policy, a youth think-tank initiative of the Konrad-Adenauer-Stiftung, Uganda and South Sudan programme. Kampala. Retrieved March 3, 2020, from https://www.kas.de/c/document_library/get_file?uuid=72aba01c-362f-bb7d-9285-2be31890913f&groupId=280229

WFP, UNHCR, & Government of Malawi (2014). Joint assessment mission report: Dzaleka refugee camp, Malawi. Lilongwe, Malawi. Retrieved March 22, 2020, from <https://www.unhcr.org/5680f7d09.pdf>

White, A. (2015). Moving Stories: International Review of How Media Cover Migration. Ethical Journalism Network. London. Retrieved December 7, 2020, from <https://ethicaljournalismnetwork.org/assets/docs/054/198/8feb836-108e6c6.pdf>

Worby, E., Hassim, S., & Kupe, T. (2008). Go home or die here: Violence, xenophobia and the reinvention of difference in South Africa. Johannesburg: Wits University Press.

World Bank (2016). While poverty in Africa has declined, number of poor has increased. Retrieved December 2, 2020, from <http://www.worldbank.org/en/region/afr/publication/poverty-rising-africa-poverty-report>

World Bank (2019). Informing durable solutions for internal displacement in Nigeria, Somalia, South Sudan, and Sudan: Volume A: Overview. Washington, D.C. Retrieved October 27, 2020, from <http://documents1.worldbank.org/curated/en/761091557465113541/pdf/Volume-A-Executive-Summary.pdf>

World Bank (2020a). Poverty: Overview. Retrieved October 28, 2020, from <https://www.worldbank.org/en/topic/poverty/overview>

World Bank (2020b). Migration and remittances data: Annual remittances data as of October 2020. Retrieved December 7, 2020, from <https://www.worldbank.org/en/topic/migrationremittancesdiasporaisues/brief/migration-remittances-data>



MODULI 10

Kuripoti kuhusu uhamiaji kitaalamu: Utendaji kazi bora na mkabala wa kiitikeli

na Anna-Carina Zappe



MALENGO YA MODULI

- Kuwatahadharisha washirika kuhusu haja ya umakinifu kufikia na kukadiria vyanzo vya kuelezea habari za uhamiaji.
- Kuwahamasisha washiriki kuhusu maneno muafaka na mtazamo ufaao.
- Kutoa ushauri wa kuripoti kitaalamu kuhusu wahamiaji na wakimbizi kwa kuwasilisha mifano ya utendaji kazi bora na kupata ushauri wa wanahabari wazoefu.



MATOKEO YA MAFUNZO

Kufikia mwisho wa moduli hii, washiriki wanapaswa kuwa na uwezo wa:

- Kutambua vipengele tofauti (kwa mfano viwango vya ubora wa habari, uhusiano na chaguo la vyanzo) katika utaratibu wa kuripoti kuhusu wahamiaji na wakimbizi.
→ **Matokeo ya mafunzo kwa stadi za mitazamo ya kibinafsi na maadili: Kujibu**
- Kutumia kanuni za vielekezi vya kuripoti kiitikeli kuhusu uhamiaji. → **Matokeo ya mafunzo kwa stadi za mitazamo kibinafsi na maadili: Kupokea**
- Kuchagua vyanzo vya kuaminika na kushughulika kuunda mtazamo wa kiitikeli katika kueleza habari za uhamiaji. → **Matokeo ya mafunzo kwa stadi za utambuzi: Kutathmini na kubuni**

Muhtasari

“Wasomi wa uanahabari wa uhamiaji wamehoji kwamba uhamiaji ni suala ngumu kufuatilia na kuripoti kwa sababu ni simulizi linalochirizika, wala si la muda si punde — ndiposa taarifa za punde za kuzama kwa meli ya kusafirisha wahamiaji kimagendo ni rahisi kuripoti kwa sababu ya changamoto za kijamii na kisiasa, kide-mografia na kiuchumi za tukio hilo lote.” (Dell’Orto, n. d.)

Huenda pia ikawa ni rahisi kwa hadhira kupokea habari za muda si punde za uhamiaji, na za kuvutia zaidi kwa wahariri kuchapisha. Hata hivyo, shabaha ya moduli hii ni kuwahimiza washiriki kutoa habari za wahamiaji na wakimbizi kwa mtazamo changamani na tofauti katika maneno na fikira — kwa sababu mengi yanahitajika kulifahamu kikamilifu tukio hilo.

Kuripoti kuhusu wahamiaji na wakimbizi ni shughuli inayohitaji stadi maalumu. Wanahabari wanahitaji mbinu kamili za utafiti, na pia ustadi wa kukadiria vyanzo vya habari za kutegemewa. Wanafaa kuzingatia busara na hekima katika uteuzi wa wahusika wakuu, fokasi, hali ya akili na mitazamo, habari wanayokusanya, na pia mbinu za uwasilishaji kwa jumla. Ufahamu wa kanu-

ni za itikeli zilizotayarishwa hususan kwa kuripoti kuhusu wahamiaji na wakimbizi¹ unaweza kuwasaidia wanahabari ambao mara nyingi hukabiliwa na mtanziko wa itikeli wanapokusanya na kutoa habari za masuala hayo.

Ndiposa moduli hii ina taarifa za wanahabari wanaoshughulikia masuala ya uhamiaji kote dunia-ni na wanarejelea uzoefu wao wa kikazi, huku wakiorodhesha yaliyo muhimu katika kukusanyaji na kueleza habari unaozingatia uwajibikaji.

Uhamiaji kama habari

Utafiti wa kina huanza na uteuzi wa kitaalamu wa kipengee cha habari kinachohitaji kuchunguzwa. Kwa sababu ya kutingwa na muda na uhaba wa nafasi, wahariri hulazimika kuamua ni taarifa gani za habari na hadithi za kuwavutia wasomaji, wasikilizaji na watazamaji wao. “Mvuto mkuu wa utumiaji wa ripoti za habari ni mafao yake kwa hadhira” (Schröder, 2019). Watu huthamini habari zinazowafaa zaidi na zenye mvuto na ushawishi katika maisha yao binafsi katika ngazi za mashinani, kitaifa na kimataifa; na mara nyingi thamani ya habari hutokana pia na jinsi zinavyoweza kusambaziwa wengine. Chaguo la habari kwa hadhira limejadiliwa kwenye maada ya “kuuza habari” katika moduli 13. Hata hivyo, inafaa kukumbukwa kwamba huenda pakawa na tofauti ya thamani ya habari kwa wanahabari na kwa umma (Boczkowski & Mitchelstein, 2015; Chakraborty na wengine, 2019). Lakini matokeo ya utafiti “yanaonyesha kwamba wanaopokea habari mara nyingi huwa hawatumii yanayowavutia na huwa pia hawavutiwi na wanayopokea” (Swart na wengine, 2017, uk. 1343). Ndiposa chaguo la habari za kuelezea ni uamuzi thabiti ambao huchukuliwa katika utaratibu wa kuchagua kwamba baadhi ya simulizi kuhusu uhamiaji na wakimbizi kamwe hazitaifikia hadhira². Uteuzi huo, ukichanganuliwa, unaweza kufungamishwa na baadhi ya kanuni za thamani ya habari³. Thamani ya habari ni kigezo cha kupimia habari zinazochaguliwa na wanahabari kwa thamani yake na ambazo pia hutumiwa kwa uhakiki wa vyombo vya habari.

Mwaka 1965, Galtung & Ruge (2016) waliandaa mfumo msingi wenye vipengee 12 wa viwango vya thamani ya habari, ambao umeimarishwa zaidi na wanazuoni wengine⁴. Harcup & O’Neill

-
- 1 Kwa maelezo, tafadhali angalia faharasa zilizopendekezwa katika Moduli 2 (European Migration Network, 2018; IOM, 2019a; UNHCR, n. d.).
 - 2 Ripoti *Moving Stories. International Review of How Media Cover Migration*, iliyotayarishwa na Ethical Journalism Network (EJN) imeorodhesha simulizi kuhusu uhamiaji ambazo mara nyingi haziripotwi (White, 2015).
 - 3 Bednarek & Caple (2017, uk. 438) wanafasili ubora wa habari kuwa sifa stahiki za habari za wahusika, matukio na masuala kuambatana na muundo unaotambuliwa, viwango vya ubora kama vile mitazamo hasi, matukio kuwa karibu na hadhira lengwa na mengineyo” na kuhusisha istilahi hiyo na malengo ya uandishi wa habari na vipengele vya kuchagua habari.
 - 4 Hata hivyo, utafiti na mjadala kuhusu vigezo vya ubora wa habari hubadilika kila mara na kuleta mambo mapya. Baadhi ya watafiti wamekuwa wakiwazia upya dhana hiyo kama Donsbach (2004) anayeeleza vigezo vya ubora wa habari huhusisha maamuzi ya dhahania. Wengine kama Harcup & O’Neill (2017, uk. 1482) wanapendekeza kwamba vigezo vya ubora wa habari vinahitaji kutoa fursa ya kusambaziana, kipengee chenye maana kwamba “habari zinazokisiwa kuwa zinaweza kusambaziwa wengine katika Facebook, Twitter na mitandao mingine ya jamii, na kuchochea maoni”. Isitoshe, wanazuoni wengine huangazia mitazamo tofauti kama Bednarek & Caple (2017) ambaye hupendekeza uchanganuzi wa taswira ya vigezo vya ubora wa habari katika picha za habari za magazeti, televisheni na mtandaoni.

(2017) wameongezea kaida zaidi za thamani za habari zinazofaa nyakati zilizopo za kidijitali, kama vile upekee, habari mbaya, ugomvi, mastaajabu, vielekezo vya kusikia na kuona, kusambazika kwa wengine, burudani, vituko, kufuatilia, wahusika wenye mamlaka, mafao, ukubwa au ukuu, umaarufu, habari njema na ajenda ya shirika la habari. Galtung & Ruge (2016) wanahoji kuwa viwango vya thamani ya habari si vya wote na maeneo yote ulimwenguni, na havifanani kutoka utamaduni mmoja hadi mwingine. Kwa Conley & Lamble (2006, uk. 56), thamani “sio imara na hubadilishwa na taratibu za kijamii, kiuchumi na kitamaduni” pia. Kwa upande mwingine, Lee (2010, uk. 377) anahoji kwamba “wanahabari wengi wanaofanya kazi katika magazeti ya Kiingereza katika Asia ni Wazungu na/au wamesomea Uzunguni na wakilinganishwa na wenzao wenyeji, mara nyingi huwa wanazingatia viwango na kanuni za habari vya Uzunguni, ikiwa ni pamoja na kanuni za uandishi wa habari”. Kwa upande mwingi, Masterton (2005, uk. 42) alitafiti kaida za uanahabari za nchi za Uzunguni na Asia na kuhukumu kwamba “wanahabari kote duniani wanakiri kuwa kuna vipengele vitatu vya kimsingi vya habari zinazostahili ambavyo visipokuwepo hakuna taarifa yoyote inaweza kuwa habari. Vipengee hivyo ni shauku, wakati wa kufaa na udhahiri”.

Kielelezo 30: Vipengele vya thamani ya habari

<i>Upekee</i>	<i>Habari za kuvunja moyo</i>	<i>Ugomvi</i>	<i>Mastaajabu</i>	<i>Vielekezo vya kusikia na kuona</i>
<i>Kusambazika kwa wengine</i>	<i>Burudani</i>	<i>Vituko</i>	<i>Ufuatiliaji</i>	<i>Wahusika wenye mamlaka na uwezo</i>
<i>Mafao/umuhimu</i>	<i>Ukuu</i>	<i>Umaarufu</i>	<i>Habari njema</i>	<i>Ajenda ya shirika la habari</i>

Asili: Mchoro wetu kuambatana na Harcup & O'Neill (2017).

Kauli hii inalingana na mapitio ya maandishi ambayo yanabaini kiasi kikubwa cha mwambatano na ulinganifu kuhusu vipengele vya thamani ya habari (Caple & Bednarek, 2013). Agunda (n. d., uk. 4) anahoji kwamba vipengele vya thamani ya habari katika uanahabari wa Kiafrika vinaweza kufanana na vipengele vya thamani ya habari vya “Uzunguni”, kwa sababu “ni maenezi tu ya uanahabari wa kimagharibi”. Uchunguzi wake katika nchi za Afrika Mashariki unaonyesha kwamba wanahabari wanawaenzi sana wenye mamlaka ya kisiasa, ambao ni waamuzi wakuu. Isitoshe, taratibu za uanahabari zinaweza kuwa na taathira kubwa kwa vipengele vya thamani katika utamaduni mahsusi wa wanahabari. Agunda (n. d., uk. 4) anatoa mfano wa Tanzania:

“Tanzania ambayo ina kiasi cha utamaduni mpya wa vyombo vya habari vya kibinafsi kufuatia mabadiliko ya mfumo wa kiuchumi tangu miaka ya 1990, imefanya mazoea ya kuwapuuza watu mashuhuri wanaoibuka na walio na mshawasha mku-bwa miongoni mwa vijana, na hivyo basi kuendeleza mazoea ya zamani ya vyombo vya habari vya Serikali kuripoti tu kuhusu viongozi wa chama tawala na wa ngazi nyingine pekee.”

Je, ukweli kwamba vipengele vya thamani ya habari ni muhimu kwa uchaguzi na hivyo basi kuripoti, unatwambia nini kuhusu hali iliyopo ya ukusanyaji na utoaji wa habari za wahamiaji na wakimbizi? Katika Moduli 4, tunajifunza kwamba vyombo vya habari vya Ulaya vikiripoti kuhusu masuala hayo mara nyingi huyahusisha na ugomvi na migogoro. Kadhalika, ripoti hizo kwa jumla hupewa nafasi ndogo sana na vyombo vya habari. Wanazuoni kadhaa wameangazia thamani ya habari za wahamiaji na watu kufukuzwa makwao. Maelezo ya jumla ya Eberl na wengine (2018, uk. 210) yanabaini: “Matukio halisi ulimwenguni, kama vile chaguzi au mashambulizi ya kigaidi, yanaweza kuinua umuhimu wa masuala yanayohusiana na uhamiaji katika vyombo vya habari.” Hili linaashiria baadhi ya vipengele muhimu vya thamani ya habari: habari za kuvunja moyo, hasa za majanga na matukio mabaya kama vile meli kuzama. Mfumo ulioundwa na Harcup & O’Neill (2017) unatupatia uwanda mpana wa vipengele vya thamani ya habari (tazama Kielelezo 30), ambavyo huenda zikapatiakana katika habari za uhamiaji.



MJADALA WA DARASANI ULIOPENDEKEZWA KUSHUGHULIKIA STADI ZA UTAMBUZI ZA UCHAMBUZI NA STADI ZA MITAZAMO YA KIBINAFSI NA MAADILI ZA KUPOKEA AU KUJIBU:

Linganisha habari kuhusu wahamiaji na wakimbizi kutoka nchi tofauti, kwa mfano kutoka nchi yako asili na kutoka nchi jirani. Tazama pia mifano kutoka kwa vitengo mbalimbali vya habari (mtandaoni, redio na televisheni, magazeti na vinginevyo) kwa kila taifa. Ni vipengele vipi vya thamani ya habari vya Harcup & O’Neill (2017) umetambua katika kitengo kipi? Yajadili matokeo yako.

MJADALA WA DARASANI ULIOPENDEKEZWA KUSHUGHULIKIA STADI ZA UTAMBUZI ZA MATUMIZI NA STADI ZA MITAZAMO YA KIBINAFSI NA MAADILI ZA KUPOKEA:

Wanafunzi wanapaswa kutayarisha taarifa fupi za habari na kwa njia ambayo zina vipengele vingi vya thamani ya habari iwezekanavyo. Ikumbukwe kwamba vipengele mahususi vinavyopatia habari thamani vinachaguliwa na kiongozi wa darasa au kutokana na majadiliano darasani. Hatimaye matokeo yanapaswa kujadiliwa darasani washiriki wakiangazia vipengele mbali mbali.

Ni muhimu kuvifahamu vipengele muhimu vya thamani ya habari. Itakuwa ni muhimu kwa wana-habari kujiuliza ni vipengele gani vya thamani ya habari wanavyovingatia wanapochagua habari

za kutoa kwa hadhira zao. Bila shaka, uchaguzi wa habari ni zaidi ya kuangazia vipengele hivyo tu. Ni muhimu pia kufahamu “ni nani anachagua habari, anamchagua nani, katika chombo gani na kwa mbinu ipi (na nyenzo zilizopo), [...] kwani huenda vipengele vya ubora wa habari viwemo au visiwemo katika taarifa yoyote iwezayo kupatikana” (Harcup & O’Neill, 2017, uk. 1483). Fauka ya uamuzi binafsi (unaoweza kumwelekeza makusudi au bila kujua kwa vipengele asili vya thamani ya habari katika tukio au suala lolote), chombo cha mawasiliano, mifumo ya vyumba vya habari, desturi za uanahabari na mengineyo huenda yakateleleza wajibu fulani katika kuamua iwapo simulizi linaweza kuwa habari au la.

Kuripoti kitaalamu: vigezo vya utendaji kazi bora

Shapiro na wengine (2006, uk. 431) walichunguza maana ya ubora katika uanahabari. Matokeo kufuatia uchanganuzi wao wa asili na vyanzo vingi yalikuwa ni kuratibu vigezo vifuatavyo:

- “faidi jamii kupitia kwa taathira kwa umma, mafao au huduma inayotolewa na simulizi”,
- “chambua kwa uangalifu na mantiki ya habari zilizoripotiwa kwa lengo la kuleta uwazi katika mada tatanishi na kuuweka ukweli uwezao kuthibitishwa katika muktadha wa usuli wake na kutafuta jinsi maswali kuhusu vipi na kwa nini yamejibiwa kwenye taarifa ya habari”,
- dhihirisha uadilifu (“yaani kutenda mambo kuzingatia haki na uhuru wa vyanzo vyao”), “zingatia uwazi katika mbinu unazotumia — yaani hadhira inafaa kufahamu habari inatoka wapi”,
- “dhihirisha sifa za kipekee za usimulizi”.

Kama ilivyo katika mada yoyote, kigezo hicho cha ubora kinafaa pia kuzingatiwa na wahabari wanaoripoti kuhusu wahamiaji na wakimbizi — mafao kwa jamii ambayo ripoti hizo zinahusu ni dhahiri, hasa ukizingatia yanayoshughulikiwa katika Moduli 5. Moduli 1 hadi 3 zinathibitisha kwamba mada hii ni changamani na inahitaji kushughulikiwa kwa uangalifu na makini kabisa. Ni muhimu pia kuiangazia mada hii pana kuzingatia uhuru na uwazi, kama changanuzi za kifani za Moduli 6 hadi 9 zinavyobaini tofauti kati ya nchi.

Wanahabari wanaporipoti kuhusu masuala ya uhamiaji na wakimbizi, wanapaswa kuhakikisha usahihi wa kiufundi, watayarisha habari zenye muundo mzuri na umbo la kuvutia, zinazostaajabisha hadhira na kuonyesha ubunifu wa chaguo la mada na uwasilishaji. Bila shaka, kanuni za msingi za itikeli za uanahabari — haki, utu na uwajibikaji — zinafaa kutiliwa maanani (Ethical Journalism Network, n. d.c).

Wanahabari na mashirika ya habari wanapaswa kushauriwa kuheshimu mfumo wa sheria za taaluma ya uanahabari ambazo huorodhesha kanuni za utendaji kazi bora katika kuripoti kuhusu wahamiaji na wakimbizi. Kuna hati nyingi rasmi zinazoelezea kanuni za taaluma kama vile Chata ya Idomeni (“Charter of Idomeni,” n. d.) ya Ugiriki au Chata ya Roma (“Charter of Rome,” n. d.), pamoja na miongozo ya kimataifa ya itikeli ya EJA kuhusu kuripoti masuala ya wahamiaji na wakimbizi (Ethical Journalism Network, n. d.a), ada za uanahabari mtandaoni za Shirika la Haki za Msingi la Jumuiya ya Ulaya (European Union Agency for Fundamental Rights, 2020) na

nyinginezo zinazolenga kuimarisha stadi za wanahabari za kuripoti kuhusu uhamiaji (European Federation of Journalists, 2016). Kufanya kazi kuzingatia hati mbali mbali za ada za kitaalamu huwapa wanahabari kanuni za thamani kubwa za kuripoti.



ZOEZI LILILOPENDEKEZWA LA KUSHUGHULIKIA STADI ZA UTAMBUZI ZA MAARIFA:

Ili kuwafahamisha wanafunzi kuhusu mada, wanapaswa kukusanya na kujadili vigezo muhimu vya ubora katika kuripoti kitaalamu. Shabaha za majaribio za kuongoza mjadala huo zimo kwenye aya iliyotangulia.

Chaguo la vyanzo na wahojiwa wanaofaa

Kukusanya na kutoa habari za wahamiaji na wakimbizi kitaalamu na kwa hekima kunahitaji stadi za ziada. Wanahabari na watafiti wanakubaliana kwa kauli moja kwamba wanahabari wanapaswa kujitayarisha vyema kwa kazi kama hizo. Wanapaswa kuanza kwa kufanya maandalizi makubwa ya utafiti maalumu wa habari wanayofuatilia. Wanahabari wanapaswa kuanza kwa kupitia ripoti za awali za vyombo mbali mbali vya habari ili kupata maelezo ya jumla ya muktadha wa kisiasa, kitamaduni na kijamii wa nchi husika. Ili kufanya hivyo kwa ustadi, wanahabari wanapaswa kutambulisha na kusoma ripoti na kupata data inayofaa kutoka kwa mashirika ya kimataifa, kitaifa na mengine ndani ya nchi, taasisi na mashirika yasiyo ya serikali yanayohusika na suala hilo. Wachunguze pia mitandao ya jamii, wanasisa na maafisa, na wazungumze na wataalamu wa masuala ya uhamiaji (miongoni mwao ni: Abu-Fadil, n. d.; Terceros, 2018).


Kuna mbinu tofauti za kuufanya utafiti huu: Wanahabari wanaweza kupata habari hitajika kwa utendaji na pia kimyakimya. Vyumba vingi vya habari hutumia zaidi ripoti za intaneti kuripoti kuhusu masuala ya uhamiaji. Taasisi ya Erich Brost Institute for International Journalism (EBI) katika Chuo Kikuu TU Dortmund iliandaa semina za mafunzo ya kuripoti kuhusu uhamiaji katika Afrika na Ulaya (tazama Utangulizi). Kwenye kikao cha mafunzo kilichofanyika 2018 jijini Dakar, Senegal, washiriki walidokeza kuwa asili za habari za mtandaoni ndizo hutumika sana. Kadhalika, taarifa kwa wanahabari, mahojiano (ya ana kwa ana au kwa simu) na vyombo vingine vya habari, na habari zozote kutoka kwa serikali na wakuu wengine hutumiwa mara nyingi. Hata hivyo, ni nadra sana kwa wanahabari kutumia blogu au kuwahoji wenzao. Mikutano na wanahabari, na mitandao ya jamii haitumiki sana. Matokeo hayo yanalingana na uchunguzi wa wanazuoni kwamba vyombo vya habari hupokea habari kimyakimya — hutegemea taarifa za habari kutoka kwa wanaotafuta kuripotiwa au habari za mashirika ya habari (miongoni mwa wengine: Machill & Beiler, 2009; Neuberger na wengine, 2009). Sehemu kubwa ya “uanahabari huangazia tu ripoti chache zinazopatikana kwenye intaneti” (Machill & Beiler, 2009, uk.178). “Injini za kusachia, na hasa Google, zinashika nafasi kubwa ya utaratibu wa kuamua kuhusu vyanzo vya habari na hivyo basi zina ushawishi mkubwa kwa uamuzi kuhusu mkondo wote wa utafiti wa wanahabari” (Machill & Beiler, 2009, uk. 178).

Aina nyingi ya vyanzo – simu, mitandao ya jamii, mikutano ya ana kwa ana na ya kidijitali (kongandau), njia nyingine za kutoa habari, kuchunguza kwa makini data (kubwa), utafiti wa kichunguzi na nyinginezo – mara nyingi huwa havitumiki ipasavyo. Mashirika yasiyo ya serikali pamoja na chimbuko nyingine thabiti kama vile serikali, vyama vya kisiasa, majaji na mahakimu, idara za polisi, serikali za maeneo, mashirika ya biashara, vyama vya wafanya kazi, makanisa, wahusika wa kimataifa, na wengineo wawezao kushauriwa. Lakini wanahabari wanaoripoti kuhusu uhamiaji na uhamaji wa kulazimishwa hawafai kutegemea tu vyanzo rasmi na vya wenye mamlaka tu na badala yake wanapaswa kutumia asili mbali mbali za habari — kipengee ambacho mara nyingi hakipatikani kwenye vyombo vya habari vya Ulaya na Afrika Kaskazini (International Centre for Migration Policy Development, 2016).

Asili kubwa ya habari za kuripoti kuhusu wahamiaji na wakimbizi ni waathiriwa wenyewe. Ukweli ni kwamba habari zinazowapatia wahamiaji na wakimbizi na jamii zao nafasi ya kueleza kuhusu hali yao ni miongoni mwa chaguo lifaalo zaidi kwa wanahabari. (European Federation of Journalists, 2016). Kuna sauti nyingi muhimu nje ya uwanda wa siasa kwa sababu wanasiasa hupewa nafasi kubwa kuliko wanavyostahili katika ripoti kuhusu suala hili. (tazama Moduli 4). Mwongozo wa Shirika la habari la Ethiopian Africa News Channel “Sera ya Uhariri Kuhusu Kuripoti Uhamiaji”, ulioandikwa kwa Ki-Amharic, unawashauri wanahabari kutaaradhi kwa kina masuala muhimu: Watu walio mashinani wanaathiriwaje? Jaribu kutafuta mbinu za kuripoti kuhusu athari ambazo hazijitokezi bayana, kama vile matokeo ya majeraha ya akili na kiwewe miongoni mwa wahamiaji na wakimbizi, taathira ambazo huenda zikaongeza uwezekano wa waathiriwa kuhatarisha hali ya wengine siku zijazo, iwe ni kuhatarisha hali ya jamii zao au wakiwa kundi, kuhatarisha makundi mengine au nchi nyingine (Africa News Channel, 2019). Hili ni muhimu kwa sababu wahamiaji na wakimbizi si wahusika pekee lakini wana nafasi kubwa zaidi katika masimulizi. Wote ni binadamu na kila mmoja ana masimulizi binafsi na pia hisia, kama ilivyojadiliwa katika Moduli 11.

Ulriikka Myöhänen, mwanahabari wa majukwaa tofauti ya habari wa Finland


“Enenda nyanjani ukiwa tayari kusikiliza na kupokea mawazo ya wengine, zungumza na watu tofauti, zisikilize kauli nyingi kadiri iwezekanavyo na utafute ukweli thabiti ili uwe nanga ya usimulizi wako. Kadhalika, eleza bayana kutoka mwanzo wa habari yako, kwa nini ni muhimu kuyazungumzia masuala hayo. Na la muhimu zaidi: jiepuche kabisa na mtego wa dhana potovu na dunifu zisizo na uasili na ukumbuke kuhakikisha usawa wa jinsia!”



Chanzo : Binafsi

Gloria Laker Adiiki Aciro, mwanahabari kutoka Uganda ambaye ni mratibu wa Uganda Refugee Online News Network


“Wakimbizi kuripoti kuhusu wakimbizi na kwa manufaa ya wakimbizi wenyewe: Ajiri, funza na shirikisha wakimbizi vijana na wahamiaji ambao ni wanahabari watoe simulizi zao wenyewe. [...] Pana haja kubwa ya kushirikisha uanahabari wa amani katika kuripoti kuhusu wakimbizi na wahamiaji, ikitiliwa maanani utata wa migogoro na hali mbaya ya kiuchumi inayowasukuma Waafrika kutoka makwao. Kwa kuhimiza kutolewa kwa ripoti kuhusu amani katika nchi za nyumbani, mashauriano na juhudi za mapatano miongoni mwa wakimbizi walio kambini zitasaidia pakubwa kuhimiza wakimbizi kuchangia katika juhudi za amani nyumbani walikotoka.”



Chanzo : Binafsi

Jelena Prtoric, mwanahabari huria wa Croatia

“Ifikapo ni kuripoti, kutumia wasaa zaidi na wahamiaji, kuwa nao mahali pao, ni muhimu sasa, sawa na vile imekuwa awali. Tunahitaji kutumia muda wa kutosha nyanjani ili kufahamu utata wa hali yao, simulizi zao binafsi, hali katika nchi wanazopitia na mambo yalivyo katika nchi zao za nyumbani, ili kuweza kutoa simulizi kamili.”



Chanzo : Binafsi



ZOEZI LILILOPENDEKEZWA LA KUSHUGHULIKIA STADI ZA UTAMBUZI ZA UTATHMINI NA STADI ZA MITAZAMO YA KIBINAFSI NA MAADILI ZA KUPOKEA:

Tafadhali itazame na uijadili video *Choosing Credible Resources for Research* (Osinski, 2016). Sifa kadhaa muhimu za data na vyanzo muafaka zimetajwa katika moduli hii na pia kwenye video.

Washiriki wapewe fursa ya kuratibu sifa hizo na kujadiliana iwapo wangetaka kupunguza zingine katika orodha yao au kuacha nje zingine, kulingana na uzoefu wao na desturi. Unaweza pia kuwatahini ukitumia mfano wa uanahabari. Mifano imo katika moduli hii kwenye sehemu iliyo na anwani “Kuripoti kuhusu wahamiaji na wakimbizi: Mifano ya kiutendaji”.

Habari za kuaminika na utafiti wa kutegemewa

Ni dhahiri, ubora wa data iliyokusanywa ni muhimu pia: Wanahabari wanahitaji kutafiti data maasumu na kwa ukamilifu (tazama Moduli 2), ili waweze kujaza pengo la habari bora wakianadika taarifa kuhusu binadamu (European Federation of Journalists, 2016). Ni muhimu kukagua habari hizo kwa jumla.

Bila shaka, wanahabari hawawezi kuhakikisha ukweli katika kila jambo, lakini kupata ukweli na hakika ni “kiini cha kanuni za uanahabari” (Ethical Journalism Network, n. d.c). Kwa upande mmoja, hali inaendelea kuchafuka na kubishaniwa kuhusu taswira ya kuripoti masuala ya wahamiaji na wakimbizi katika baadhi ya sehemu za dunia ambapo wanahabari wanahitaji kufahamu kwamba baadhi ya asili zao huenda zina ajenda ya binafsi (tazama changamoto za kitaalamu katika Moduli 5 kwa mifano ya kuripoti kuhusu uhamiaji). Kwa upande mwingine, “vyombo vya habari kushambuliwa kwa madai ya kuendeleza” upendeleo, taarifa ya uongo kwa makusudi au habari za uongo, hii inapaswa kuwa hoja ya kutosha kuwasukuma wanahabari kuhakikisha kwamba wanachunguza kwa makini asili zao za habari (Abu-Fadil, n. d., uk. 34). Na sio tu vyanzo rasmi, kama vile serikali na ajenda yake fiche ya kisiasa, kampuni binafsi ambazo huenda zinatafuta manufaa ya kiuchumi zinapotoa habari au mashirika na taasisi zinazojali tu maslahi yao. Hali ni hiyo hiyo kwa mashirika ya utetezi wa haki za raia na wahamiaji na wakimbizi kwani wote ni sehemu ya jamii na wanaweza hata nao kusukuma ajenda yao kupitia kwa habari wanazotoa.

Wanahabari wanahitaji kuchagua asili zao za habari kwa uangalifu wakifahamu kuwa hata nao wana dhana wanazozishikilia bila upendeleo na kwa uaminifu. “Uanahabari unahitaji [...] hatua thabiti kupeleleza na kufichua visa vipya na aina za taarifa za uongo zinazotolewa kwa makusudi” (Berger, 2018, uk. 11). Utafiti katika intaneti unaweza kutoa kurasa za tovuti zenye habari finyu, iliyopitwa na wakati au isiyo sahihi. Ndiposa “ni muhimu kuwa waangalifu tunapotumia habari za mitandao, hasa wakati huu ambapo hatua za kihisibati na kimantiki zinazotumika kutafutia ufumbuzi wa matatizo fulani (algorithimu) zimeendelea kutawala ueneaji kasi wa habari katika mtandao kwa kusambaziana na ‘liking’ habari inayopatikana katika kurasa za habari na mitandao ya jamii” (Vergeer, 2018, uk. 49). Ni lazima mwanahabari ahakikishe kuwa tovuti anayoitumia ni ya kuaminika, inazingatia uwajibikaji kuhusu asili ya habari iliyomo na iwapo asili ya habari imeonyeshwa, habari hiyo ni ya lini na iwapo inaweza kuaminika.

Ukamilifu huu haufai kuthibitishwa tu kwa asili za intaneti. Wanahabari kwa jumla wanapaswa kuchunguza mafao, uhalali, manufaa mantiki ya habari — iwe ni mitandaoni au nje ya mitandao. Wanahabari wanapaswa kufahamu kila mara kwamba wao ni wanahabari wachunguzi ambao hawana budi kutaaradhi asili zao zote na pia masuala ili hatimaye kutoa “uchanganuzi kamili wa muktadha wa habari wanazotoa kadiri ya uwezo wao na katika muda wanaopewa wa kuwasilisha habari” (Quinn, 2018, uk. 6). Kuna tovuti za kuchunguza ukweli, vielekezi na miongozo kuhusu habari za uongo zinazotolewa makusudi, kwa mfano *Journalism, ‘Fake News’ and Disinformation. Handbook for journalism education and training* (Ireton & Posetti, 2018) au *Factfulness* (Rosling, 2018). Mbinu nyingine muhimu za kuimarisha uchunguzi wa ukweli ni pamoja na ushirikiano na kubadilishana mawazo na wanahabari wengine (tazama Moduli 13), na asili za kuaminika (tazama Moduli 2).

Mbali na uaminika wa asili za habari, ni muhimu kwa wanahabari na hadhira yao kuzielewa waziwazi asili hizo. Mwanzo, kuna suala la uelewa wa wanahabari: Kwa mfano takwimu zinaweza kutatanisha wanahabari. Data na takwimu kutoka kwa serikali, mashirika yasiyo ya serikali, mashirika ya kimataifa na mashirika ya utetezi wa haki za jamii zinaweza kutoa habari zisizo-

fikiana. Ni muhimu kueleza muktadha kamili na asili (tazama Moduli 2 na 3) katika kuripoti (Abu-Fadil, n. d.).

Mfano wa Sofia Papadopoulou, mwanahabari wa shirika Athens News Agency-Macedonian Press Agency (ANA-MPA), ambaye aliripoti kutoka kwa kambi ya wakimbizi ya Idomeni, Ugiriki, ambaye aliainisha kwamba ni muhimu kwa wanahabari kufahamu wahojiwa wao, sawa na uelewa wa wanahabari wa data na takwimu:

“Siku moja, kijana mwanamume alifika akiwa amebeba mikononi mtoto mchanga aliyezaliwa karibuni, akaketi katikati ya njia na akisaidiwa na kijana mwingine aliye-kuwa akizungumza Kiingereza kiasi, akaanza kulalamika kuhusu hali ya maisha kambini. Ni hakika mtoto aliyembeba alikuwa na umri wa siku chache na mwanahabari mmoja wa televisheni akarusha swali: Je, mtoto huyu alizaliwa kambini? ‘Ndiyo,’ mkalimani akajibu. Baba mtoto alipomwambia kwa Kiarabu kwamba mtoto alizaliwa hospitalini na akaletwa kambini siku chache baadaye, alisema ‘*ma’leesh*’ (ni sawa/usijali).” (Fronista & Papadopoulou, 2018, uk. 138)

Aida Alami na Salaheddine Lemaizi, wanahabari wa kimataifa kutoka Morocco

“Ukweli mbele: **Kuwa sahihi, bila kupendelea, fanya kazi kwa kujitegemea, kwa haki na uwajibikaji. Jiepushe kuandika mambo ambayo huwezi kuyathibitisha. Usiwaruhusu walio mamlakani au mashirika kuathiri ripoti unazotoa.** Safiri kadiri uwezavyo mpa-ka mahali penye tukio la kukusanyia habari. Jaribu kujithibitishia mambo wewe mwenyewe. [...]



Chanzo : Binafsi

Uanahabari kuhusu uhamiaji ni fursa ya pekee kwa sababu ni muhimu kwa wanahabari kurudi uwanjani. Uandalizi wa ripoti za vyombo vya habari kuhusu uhamiaji unaweza tu kufanikishwa na kufikia kiwango cha utaalumu wanahabari wakifanikiwa kwenda nyanjani kufanya uchunguzi, kuripoti na kuhoji watu. Ripoti na vipindi vya vyombo vya habari vinaweza tu kufanikiwa na kufikia kiwango cha kitaalamu iwapo wanahabari watafanikiwa kufanya kazi yao kwa uchunguzi, kuripoti na mahojiano, mahojiano mengi. [...] Ukiwa mwanahabari, unapaswa kutenganisha hisia zao na tukio husika na kuangazia masuala muhimu na mambo yanayotendeka yawezayo kuthibitishwa. Hata hivyo, kuwa mpole kwa unaowaangazia na uzingatie maadili yafaayo, huku ukitilia maanani muktadha mpana na utoe nafasi kamili ya simulizi zao kusikika. Jenga uhusiano na wahamiaji unaowahoji, andika kuhusu mambo ya ndani na ya binafsi yanayoeleza masuala makuu. [...] Jihadhari na matamshi ya kukashifu ya ubaguzi wa rangi au jamii na hakikisha unahimiza utoaji wa ripoti zenye ushahidi kamili. Pinga matamshi ya chuki kwa kueleza ukweli kamili wazi wazi na unafaa kujiepusha na dhana potovu zisizo na uasili, na mchuuko. Jithibitishie mwenyewe mambo ya uhakika na ushahidi uliowasilishiwa. Jaribu kuhakikisha kwamba wanaokupatia habari wanatoa ithibati kadiri wawezavyo. [...] Dhuluma za kijinsia na ubaguzi ni sehemu ya habari za uhamiaji. Kuakisi masuala hayo kwa mtazamo wa kijinsia ni jambo liwezalo kuimarisha ripoti zinazotolewa na kupanua simulizi zilizopo.”

Makosa au kutoelewana katika tafsiri na fasiri ya taarifa za lugha ya kigeni, kukanganya asili au habari za kupotosha ni mambo yawezayo kusababisha makosa au kutolewa kwa ripoti zisizo sahihi. Ndiposa kwa vile wahojiwa wanaweza kutoeleweka kwa sababu mbali mbali (kwa mfano tazama Moduli 11), ni muhimu habari hiyo ichunguzwe kwa makini sana. Ni muhimu pia kwamba isishughulikiwe kwa njia sawa na kisa kilichotajwa na mwanahabari wa shirika la ANA-MPA la Ugiriki, aliyewaonyesha baadhi ya wenzake kosa katika tafsiri na mmoja wao akasema: “Bora tu alisema hivyo na nilimnasa kwa kamera, sitakubali ukweli wako uharibu taarifa nzuri!” (Fronista & Papadopoulou, 2018, uk. 138).

Pili, ufahamu mwema wa vyanzo ni muhimu pia kwa hadhira. Wanahabari wanaweza kuzisaidia hadhira zao kulifahamu vyema zaidi suala tatanishi la uhamiaji. Kufanya hivyo kunaimarisha uwazi kwa vyanzo na kuwawezesha kukabiliana na habari za uongo au propaganda (European Federation of Journalists, 2016). Ina maana ni wajibu wa yaliyomo katika habari kusahihisha makosa (White, 2015). Isitoshe, kuzingatia uwazi kwa asili zako na mbinu za utafiti ni muhimu, sawa na kuwasilisha muktadha na usuli wa maelezo husika ya matukio ya habari (Abu-Fadil, n. d.). Kuishughulikia habari yako kwa mapana yote muhimu husaidia kuepuka maonevu, urahishaji na mawazo finyu ya kueleza habari za uanahuruma (Ethical Journalism Network, n. d.b).



PENDEKEZO LA KIKAO CHA KUTANGAMANA DARASANI KUANGAZIA STADI ZA UTAMBUZI ZA KUFAHAMU NA STADI ZA MITAZAMO YA KIBINAFSI NA MAADILI ZA KUJIBU:

Baada ya kutambulisha vyanzo mbali mbali na thamani ya habari katika kuripoti kuhusu wahamiaji na wakimbizi, tafadhali fanya zoezi lifuatalo, liitwalo “Mizani ya ustadi”.

1. Unda taarifa na ueleze kwa utaratibu “Taarifa kwa wanahabari ni asili muhimu kwa habari za kuripoti kuhusu uhamiaji” au “Katika kuripoti kuhusu uhamiaji, mara nyingi huwa ninatumia taarifa kwa wanahabari.”
2. Bandika posta mbili darasani. Moja iwe na maneno “Ninakubali kabisa” na nyingine “Sikubaliani kwa vyovyote vile”.
3. Waombe washiriki kujipanga kulingana na taarifa waliyochagua, kisha wjadili misimamo yao. Wape nafasi kuhoji ni kwa nini wanatumia asili mahsusi.
4. Iweke mitazamo hiyo katika muktadha pamoja na vidokezi kuhusu kipengele gani cha kila asili kinachopaswa kuangaziwa.

Kwa njia hii, washirika wanajifunza kuhoji na kutafakari kuhusu jinsi wanatumia asili, na mitazamo yao kwa vyanzo hivyo.

Maneno sahihi na mitazamo

Bila shaka, si kila taarifa ya mwanasiasa kuhusu wahamiaji na wakimbizi inapaswa kuaminiwa, na sio kila habari katika intaneti kuhusu uhamiaji ni ya kweli; kuripoti kuhusu masuala hayo kunatoa nafasi ya kupinga visasili (European Federation of Journalists, 2016) na dhana potovu zisizo na uasili. Kumbuka kwamba utumiaji wa maneno na istilahi sahihi ni mbinu moja ya kufanya kazi iwezayo kutumiwa na wanahabari ili kuepuka visasili na dhana potovu zisizo na uasili. Kwa “mfano, badala ya kuandika ‘tatizo la uhamiaji na ukimbizi’ na hivyo huwafanya watu kuonekana kuwa ndio tatizo, ni bora kuandika ‘tatizo la sera ya uhamiaji’; badala ya kuzungumzia ‘maadili ya EU/kitaifa’ au ‘itikeli za uadilifu’, ni bora kuzungumzia ‘maadili yanayokubalika na wote ambayo Ulaya inathamini’” (European Federation of Journalists, 2016). Kwenye mahojiano ya kitaalamu kuhusu ukusanyaji na utoaji habari za wahamiaji na uhamiaji, wanahabari wanashauriwa kuepuka kutumia majina ya kupachikwa kama “haramu” au “wasio na hati”. Badala yake, wanahabari wanapaswa kueleza hali iliyopo au hali ya mtu kwa usahihi kadiri iwezekanavyo na kutoa muktadha. Kwa mfano, hakuna mtu yeyote ambaye ni haramu ila yeye kwa sasa anaishi kiharamu katika nchi. Hali ni hiyo hiyo kuhusu maonevu: Wahamiaji na wakimbizi sio “waathiriwa”, na hivyo wanapaswa tu kuitwa hivyo iwapo wenyewe wamejiita hivyo (Carcamo na wengine, 2014). Kadhalika, lugha ya “maonevu” kama vile “fukara”, “bananga”, “asiye na ulinzi wala utetezi”, “kusikitisha” na “janga”, inafaa kuepukwa. Maneno hayo huwanyima wahamiaji na wakimbizi mamlaka na kuwapunguzia nafasi za mabadiliko (Africa News Channel, 2019). Lakini kwa upande mwingine, haifai kutumia vibaya neno liwezalo kuamsha hisia kusimulia yaliyowakumba watu. Wahamiaji hawafai kuripotiwa kuwa ni mashujaa. Kwa mujibu wa mwongozo wa Ethiopian African News Channel (Africa News Channel, 2019) taarifa za habari hazifai kuakisi safari za ufanisi za baadhi ya wahamiaji. Kanuni tano elekezi za mwongozo huo zinawataka wanahabari kuufahamu mfumo wa kisheria ili kuepuka maneno ya kupotosha wanapozungumza kuhusu wahamiaji na wakimbizi (Ethical Journalism Network, n. d.c). Kwa kutumia maneno, wanahabari wanaweza pia kusahihisha taswira za kupotosha. Wanahabari wakitilia maanani taswira ambazo watu wengi wamesheheni mawazoni mwao za wakimbizi na wahamiaji, na hofu inayohusishwa na taswira hizo, wanaweza kuonyesha kwamba “wakimbizi na wahamiaji sio vijana barubaru wanaotumia simu smati au familia za watalii wanaosafiri wakiwa wamebeba mizigo ghali [japo kwa makosa]” (European Federation of Journalists, 2016). Wengi wao huwa ni watoto wasioandamana na mtu yeyote mzima⁵.

Kwa hivyo, wanahabari katika simulizi zao ama uchaguzi wa maneno wanapaswa kushikilia mambo muhimu na dhahiri ya kweli, badala ya kuleta mwelekeo uliotiwa chumvi kuibua hisia. Kanuni hizo za itikeli ni muhimu, hasa kwa mada nyeti kama vile uhamiaji na masuala yanayowahusu wakimbizi. Vyombo vya habari mara nyingi huangazia tu matukio mahususi, vinatia chumvi matukio hayo na kuzingatia zaidi mikasa (tazama Moduli 4). Mbinu mbadala inaweza pia kuipatia habari mandhari pana kwa kiwango fulani ambayo ni tofauti kabisa na msisitizo wa kawaida wa

5 “Watoto wasioandamana na watu wazima ni sehemu kubwa ya mtiririko wa uhamiaji usio wa kawaida” (IOM, 2019b, uk. 105). Idadi ya watoto miongoni mwa wakimbizi ni “kubwa sana, hubadilikabadilika” kati ya asilimia 41 na 52 katika miaka iliyopita (IOM, 2019b, uk. 39).

ugomvi na matatizo. Uanahabari unaolenga kusaidia⁶ unahusu kuangazia siku zijazo. Wanahabari wanaweza kuakisi ufumbuzi badala ya kusimulia tu kuhusu matatizo na vituko. Kwa mfano, usimulizi huo mbadala ni pamoja na kusisitiza kuhusu wepesi wa watu waliokuwa manusura wa ulanguzi katika muktadha wa uhamiaji na kufukuzwa makwao, kujirekebisha na kuanza maisha upya. Pana haja pia ya kuchunguza jinsi masuala ya sera yanaweza kuimarishwa (White, 2015).

Ni muhimu, kwa hivyo, kutafakari kuhusu wajibu wako ukiwa mwanahabari. Mwanahabari anapaswa kuitalii habari “kwa uangalifu, makini na heshima” sawa na vile wangetaka ifanyike “endapo wangebamilishana nafasi” (Nobel, 2018). Hiyo ina maana pia kwamba pana mengi zaidi ya mtazamo wa kitaifa. Na kama ilivyoelezwa awali, inahusu mada zaidi ya moja: Fauka ya meli kuzama na masuala ya mipaka, mada kama vile makao, dini, ajira, wasanii, wataalamu na wajasiriamali waliofanikiwa pamoja na maelezo ya msingi ni vipengele na masuala yawezayo kushughulikiwa (Triandafyllidou, 2017).

Dkt Lydia Ouma Radoli, Mtangazaji Mkenya na mtafiti wa vyombo vya habari

“Mfumo wa uanahabari unaosaidia utachangia katika kuleta mtazamo mzuri kuhusu uhamiaji. Uhamiaji ni tukio lenye nguvu mwendo na huenda tukashuhudia safari zisizo na kikomo za uhamiaji, pengine kuakisia jinsi uhamiaji unaweza kutumiwa kuleta utangamano wa kimataifa na kanda, badala ya kuwa tukio la kuleta migawanyiko ya jamii na watu kupoteza utambulisho. Wahariri na waandishi wa habari wanaweza kuwekeza zaidi ili kupata elimu na maarifa kuhusu uhamiaji, hasa kulinganisha uhamiaji na mada nyingine kama vile maendeleo, kuunganisha na kutalii tamaduni badala ya msisitizo wa sasa wa vitishio vya usalama, siasa za kujitafutia sifa na umaarufu ulimwenguni, na maafa. Sisemi kwamba habari hizo hazifai kuripotiwa lakini pana haja ya kuangalia pande zote katika ukusanyaji na utoaji habari ili kuonyesha kwamba simulizi za uhamiaji haziegemei upande mmoja ila inafichua tukio halisi linalokumba wanadamu.”



Chanzo : Binafsi

Cécile Debarge, mwanahabari huria aliye Italia

“Simulizi nyingi za uhamiaji zinahusu uvukaji; kuvuka mpaka, kuvuka mto, kuvuka mlima, jangwa, kuvuka Bahari ya Mediterranean, kuvuka kila kitu lakini hadithi inakwamia mpakani. Hilo ni kosa kubwa kwa sababu uhamiaji ni utaratibu, ni safari ndefu ya maisha. Mitazamo inayoonyesha ubunifu mkubwa ni ile inayotaribu kutafuta usimulizi wa kina kabla ama baada ya wahamiaji kuvuka mpaka; habari ambazo lengo lake sio kutambulisha watu kulingana na safari zao. Hapo ndipo pana nafasi ya kusisitiza ubinadamu kwenye simulizi lako kwa wote. Mwelekeo huo huimarisha simulizi wezeshi, simulizi linalowaakisi wahamiaji sio tu kama watu wanaoteseka au wanaohitaji misaada lakini wahusika katika kujiletea mabadiliko. Mara nyingi mambo hayo hayaripotiwi kikamilifu.”




Chanzo : Binafsi

6 Kwa habari zaidi kuhusu uanahabari wa kujenga na kuboresha kwa jumla tazama Constructive Institute (2020), McIntyre & Gyldensted (2018), Mast na wengine (2019), miongoni mwa wengine.

Dennis Kwadwo Peprah, mwanahabari wa shirika moja la habari la Ghana

“Ni lazima maneno na matamshi ya kudunisha watu yaepukwe. [...] Ni lazima habari za uhamiaji ziwe zikiwekwa katika muktadha wa kimataifa kila mara na ihakikishwe zinashughulikia pande zote. Kadhalika, ni lazima zishirikishe vyanzo mbali mbali — wahamiaji, makundi ya wakimbizi, mashirika ya utetezi wa haki za raia, mashirika yasiyo ya serikali, mashirika husika ya umma na watetezi wa haki za binadamu. Baadhi ya habari nzuri ambazo wanahabari wanaweza kuangazia na kuziweka katika ulingo wa kimataifa ni pamoja na athari za kiuchumi za nchi wanakotoka wakimbizi na nchi mwenyeji, uhamiaji na teknolojia (utumizi wa Teknohama [ICT] kufanikisha uhamiaji, sana sana uhamiaji haramu na usio wa kawaida unaowahusisha walanguzi), na masuala ya ubaguzi wa kijinsia na katika sehemu za kazi.”



Chanzo : Binafsi

Tersoo Peter Zamber, mwanahabari wa redio Nigeria

1. Wanahabari wanafaa kupatia habari za uhamiaji sura ya kiutu.
2. Waeleze mambo kama yalivyo, wakieleza kuhusu pande zote, mabaya na mazuri ya uhamiaji.
3. Waeleze manufaa ya uhamiaji kwa watu binafsi, nchi ya asili, wanakopitia na nchi mwenyeji.”



Chanzo : Binafsi



ZOEZI LILILOPENDEKEZWA LA KUSHUGHULIKIA STADI ZA UTAMBUZI ZA KUBUNI NA STADI ZA MITAZAMO YA KIBINAFSI NA MAADILI ZA KUPOKEA:

Moduli hii inatoa mifano mingi ya utendaji kazi bora katika kuripoti kuhusu wahamiaji na wakimbizi ikiwa ni msingi wa kuwasaidia washirika kujenga vigezo bora vya uanahabari. Malengo yawezayo kuigwa yametajwa katika vidokezi vilivyotangulia. Washiriki wanaweza pia kujadiliana kuhusu tathmini tofauti za umuhimu wa vigezo hivyo kama alama teule ya uanahabari.

Kuripoti kuhusu wahamiaji na wakimbizi: mifano ya utendaji

Kote duniani kuna mifano ya kiwango cha juu ya utendaji kazi bora wa ukusanyaji na utoaji wa habari za uhamiaji. Mifano ifuatayo imependekezwa kuwezesha kuchunguza mbinu nyeti na bunifu za kushughulikia suala hilo.

- Filamu *“The War on my Phone”* inatoa picha ya ndani ya maisha katika nchi iliyokumbwa na mapigano ya Syria, na wakimbizi wanne ambao wamepata shida ya kuchagua kati ya kubaki Syria au kwenda Ulaya. Haiangazii siasa pekee lakini inasimulia pia kuhusu wakimbizi binafsi. Inashughulikia mada ya kiutu na kuzuia michomo ya moyo ya waandalizi wake kujitokeza (*“The war on my phone”*, 2018)⁷.
- Ripoti *“Workers in Spain’s Strawberry Fields Speak Out on Abuse”* ni kuhusu kipengele cha uhamiaji ambacho mara nyingi hupuuza kwa kiwango fulani: Je, wahamiaji huishi katika hali gani katika nchi mwenyeji wao? Inaangazia muktadha wa kisiasa, kitamaduni na kibinafsi wa matukio. Ripoti inaeleza kuhusu mambo yaliyotendeka na masimulizi ya watu binafsi, huku ikijaribu kutoa kauli yenye mitazamo mingi. Isitoshe, inawafichulia watazamaji asili zake zote na kueleza ni kwa nini majina na sura za baadhi ya watu zimebanwa. La muhimu zaidi ni kwamba imejaribu kutoa tunu ya maelezo ya kimuktadha (Alami, 2019a, 2019b).
- Makala yenye anwani *“Assad’s Victory. What Comes after War in Syria?”* ilichapishwa na jarida *Der Spiegel* la Ujerumani na inahusu hali inayokumba Syria baada ya utawala kuwashinda pakubwa waasi. Makala imeshughulikia uhamiaji. Imeeleza kwa mapana misimamo ya kisiasa, matukio na mambo halisi yaliyotendeka, ikitilia maanani muktadha wa kihistoria, kimataifa na kitamaduni. Wahusika wakuu wanafuatwa, wanawasilishwa na kunukuliwa. Mwandishi wake anafuata mbinu ya mitazamo mingi (Koelbl, 2017; Koelbl, 2018).
- Filamu moja ya shirika la Deutsche Welle (DW) ionyeshayo maisha halisi *“The gatekeepers of Europe. Outsourcing border controls to Africa”* inaangazia suala la Ulaya “kulipa nchi za Kiafrika mabilioni ya euro ili kuwa askari wake wapya wa kulinda mipaka”, na kutumia misaada ya maendeleo “kama zawadi kwa kukabiliana na uhamiaji” (Schäfer & Schlindwein, 2019). Filamu hiyo ya DW inaonyesha mambo halisi yaliyotendeka na yaliyotafitiwa na kuwekewa msingi wa kutosha unaoshirikisha pia waathiriwa. Inaangazia mambo wanayokumbana nayo wahamiaji na wakimbizi wanaohatarisha maisha yao katika Jangwa la Sahara lakini hupuuza na vyombo vya habari (Schäfer & Schlindwein, 2019).

⁷ Nakala za Kiingereza, Kijerumani na Kihispania zinapatikana katika mtandao wa Deutsche Welle (DW). Kiingereza: <https://www.dw.com/en/the-war-on-my-phone-lifeline-to-syria-1/av-46642884>, Kijerumani: <https://www.dw.com/de/the-war-on-my-phone-1/av-46642882>, Kihispania: <https://www.dw.com/es/la-guerra-en-mi-celular-noticias-de-siria-1/av-46642906>.

- Kutoka Morocco, makala “*Émigration irrégulière. À bord des zodiacs de la mort*” iliyo kwenye tovuti ya habari ya shajara Les Inspirations éco inatoa mfano bora zaidi wa kuripoti kuhusu suala hilo kwa njia ya kuvutia na inayoelevesha kikamilifu. Makala inaangazia mkasa wa meli iliyozama na kuangamiza abiria 45 kati ya abiria 56. Ina maana wahamiaji 11 pekee ndio walinusurika. Kwa kuwahoji manusura na jamaa za waliokufa, mwanahabari amefichua mbinu za wanaowasafirisha wahamiaji na wakimbizi kimagendo. Kadhalika, wahamiaji hao waliingia mtegoni wa wanamagendo hao kwa ahadi za uongo na zilizoleta maafa kutokana na uhaba wa habari na maarifa. Vyanzo vya ziada vimeipatia makala hiyo taswira kamili na kudhihirisha umuhimu wake. Makala imenukuu takwimu rasmi, maafisa wakuu wa serikali pamoja na shirika moja la kitaifa lisilo la serikali, na kutaja hatua zilizochukuliwa na Umoja wa Mataifa, Jumuiya ya Ulaya na wengineo (Les Inspirations éco, 2019).



KAZI YA ZIADA ILIYOPENDEKEZWA YA KUSHUGHULIKIA STADI ZA UTAMBUZI ZA KUUMBA NA KUTATHMINI, NA STADI ZA MITAZAMO YA KIBINAFSI NA MAADILI ZA KUPOKEA NA KUJIBU:

(A) Wapatie washirika nafasi ya kutoa ripoti ya tukio la wakati uliopo kuhusu mada ya wahamiaji na wakimbizi, wakitumia vigezo vyote adilifu vya ubora wa habari vilivyojadiliwa katika moduli hii.

(B) Washirika wapewe nafasi ya kutayarisha makala kutafakari kuhusu vipengele tofauti katika taratibu zao za kutayarisha taarifa za habari kuhusu uhamiaji (kwa mfano vipengele vya thamani ya habari au itikeli kutoka kwa vielekezi vya kuripoti kwa uadilifu).

(C) Waruhusu washiriki kubadilishana ripoti zao za habari na kutambulisha asili zilizochaguliwa. Waamue iwapo asili hizo zinaaminika na utafiti uliofanywa unategemewa.



USOMAJI WA ZIADA:

Kiakademia:

Harcup, T. & O’Neill, D. (2017). ‘What is news? News values revisited (again)’, *Journalism Studies* 18(12). 1470-1488. <https://doi.org/10.1080/1461670X.2016.1150193>

Kiuanahabari:

Ruz, Camila (2015). The battle over the words used to describe migrants. Retrieved November 25, 2020, from <https://www.bbc.com/news/magazine-34061097>

Kitaasisi:

Ethical Journalism Network. (n. d.) Media and Migration. Retrieved November 25, 2020, from <https://ethicaljournalismnetwork.org/what-we-do/media-and-migration>

Marejeleo

Abu-Fadil, M. (n. d.). Migration and Media: A Journalist's Handbook. Open Media Hub; EuroMed Migration; Inter-national Centre for Migration Policy Development. Retrieved March 25, 2020, from <https://openmediahub.com/wp-content/uploads/2019/06/Migration-and-Media-A-Journalists-Handbook.pdf>

Agunda, J. (n. d.). News values in east Africa. Retrieved January 26, 2019, from http://archives.aefjn.org/index.php/africa/articles/journalists-news-values-in-east-africa.html?file=tl_files/aejfn-files/Africa/Africa%20news%20eng/Journalists%20news%20values%20in%20east%20africa.pdf

Alami, A. (2019a, July 20). Workers in Spain's Strawberry Fields Speak Out on Abuse. The New York Times. Retrieved September 22, 2020, from <https://www.nytimes.com/2019/07/20/world/europe/spain-strawberry-fields-abuse.html>

Alami, A. (2019b, July 22). Trabajadoras de los campos de fresas de España denuncian abusos. The New York Times. Retrieved September 22, 2020, from <https://www.nytimes.com/es/2019/07/22/espanol/temporeras-fresas-espana-marruecos.html>

Africa News Channel. (2019). Editorial policy on migration reporting. [Internal document]

Bednarek, M., & Caple, H. (2017). The discourse of news values: How news organizations create newsworthiness. New York: Oxford University Press.

Berger, G. (2018). Foreword. In Ireton, C. & Posetti, J. (Eds.), Journalism, "fake news" & disinformation: Handbook for journalism education and training. UNESCO Series on Journalism Education. Paris: United Nations Educational Scientific and Cultural Organization.

Boczkowski, P. J., & Mitchelstein, E. (2015). The news gap: When the information preferences of the media and the public diverge. Cambridge, Massachusetts: The MIT Press.

Caple, H., & Bednarek, M. (2013). Delving into the discourse: Approaches to news values in journalism studies and beyond. Oxford: Reuters Institute for the Study of Journalism Retrieved December 7, 2020, from <https://reutersinstitute.politics.ox.ac.uk/our-research/delving-discourse-approaches-news-values-journalism-studies-and-beyond>

Carcamo, C., Matza, M., Pierre-Pierre, G., Sacchetti, M., & Ritchin, A. (2014, January 6). Covering immigrants & immigration: Tips from experts. Dart Center. Retrieved January 16, 2019, from <http://dartcenter.org/content/covering-immigrants-immigration-tips-from-experts>

Chakraborty, A., Ghosh, S., Ganguly, N., & Gummadi, K. P. (2019). Editorial versus audience gatekeeping: Analyzing news selection and consumption dynamics in online news media. IEEE Transactions on Computational Social Systems, 6(4), 680-691. <https://doi.org/10.1109/TCSS.2019.2920000>

Charter of Idomeni (n. d.). Retrieved November 25, 2020, from <http://europeanjournalists.org/wp-content/uploads/2017/05/Charter-of-Idomeni-%CE%95%CE%9D.pdf>

Charter of Rome (n. d.). Code of conduct regarding asylum seekers, refugees, victims of trafficking and migrants. Federazione Nazionale del la Stampa Italiana. Retrieved November 25, 2020, from <http://www.cartadiroma.org/wp-content/uploads/2014/10/CODE-AND-GLOSSARY-ENGLISH.pdf>

Conley, D., & Lambie, S. (2006). The daily miracle: An introduction to journalism (3. ed.). Melbourne: Oxford University Press.

Constructive Institute (2020). Retrieved December 7, 2020, from <https://constructiveinstitute.org/>

Dell'Orto, G. (n. d.). The visible & invisible borders of migration: Journalism challenged. [Blog post]. Media Governance & Industries Lab blog at the University of Vienna. Retrieved December 23, 2019, from <https://uni-viennamedialab.wordpress.com/2017/01/11/the-visible-invisible-borders-of-migration-journalism-challenged/>

Donsbach, W. (2004). Psychology of news decisions: Factors behind journalists' professional behavior. *Journalism: Theory, Practice & Criticism*, 5(2), 131-157. <https://doi.org/10.1177/146488490452002>

Eberl, J. M., Meltzer, C. E., Heidenreich, T., Herrero, B., Theorin, N., Lind, F., Berganza, R., Boomgaarden, H.G., Schemer, C., & Strömbäck, J. (2018). The European media discourse on immigration and its effects: a literature review. *Annals of the International Communication Association*, 42(3), 207-223. <https://doi.org/10.1080/23808985.2018.1497452>

European Federation of Journalists. (2016, November 28). 8 tips for migration coverage. [Blog post]. European Federation of Journalists. Retrieved December 3, 2019, from <https://europeanjournalists.org/blog/2016/11/28/8-practical-tips-for-migration-coverage/>

Ethical Journalism Network. (n. d.a). Ethical Guidelines for Migration Reporting: Five Point Guide for Migration Reporting. Ethical Journalism Network. Retrieved June 30, 2018, from <https://ethicaljournalismnetwork.org/resources/infographics/ethical-guidelines-on-migration-reporting>

Ethical Journalism Network. (n. d.b). Ethical guidelines on migration reporting. Ethical Journalism Network. Retrieved November 25, 2020, from <https://ethicaljournalismnetwork.org/ethical-guidelines-on-migration-reporting>

Ethical Journalism Network. (n. d.c). The 5 principles of ethical journalism. Ethical Journalism Network. Retrieved December 2, 2019, from <https://ethicaljournalismnetwork.org/who-we-are>

European Migration Network. (2018). EMN Information leaflet. Asylum and migration. Glossary 6.0: A tool for better comparability produced by the European Migration Network. European Migration Network. Retrieved December 2, 2019, from https://www.emn.at/wp-content/uploads/2018/06/emn-glossary-6-0_en.pdf

European Union Agency for Fundamental Rights. (2020). E-media toolkit on migration: Trainer's manual. European Union Agency for Fundamental Rights. Retrieved November 25, 2020, from <https://fra.europa.eu/en/publication/2020/e-media-toolkit-migration-trainers-manual>

Fronista, P., & Papadopoulou, S. (2018). Down and out and wet and bedraggled: Navigating the emotional and ethical maelstrom of reporting from the crisis flashpoint of Idomeni. In Dell'Orto, G. & Wetzstein, I. (Eds.), *Refugee news, refugee politics: Journalism, public opinion and policymaking in Europe* (pp. 127-140). New York: Routledge.

Galtung, J., & Ruge, M. H. (2016). The Structure of Foreign News: The presentation of the Congo, Cuba and Cyprus crises in four Norwegian newspapers. *Journal of International Peace Research*, 2(1), 64-90. <https://doi.org/10.1177/002234336500200104>

Harcup, T., & O'Neill, D. (2017). What is news? News values revisited (again). *Journalism Studies*, 18(12), 1470-1488. <https://doi.org/10.1080/1461670X.2016.1150193>

International Centre for Migration Policy Development. (2016). How does the media on both sides of the Mediterranean report on migration? Preliminary findings, draft conclusions and draft recommendations. Ethical Journalism Network. Retrieved June 26, 2018, from https://cdn.ethicaljournalismnetwork.org/wp-content/uploads/2017/03/Draft_Migration_and_Media_Report.pdf

IOM (2019a). Glossary on Migration. International Organization for Migration. Geneva. Retrieved August 5, 2019, from https://publications.iom.int/system/files/pdf/iml_34_glossary.pdf

IOM. (2019b). World migration report 2020. International Organization for Migration Geneva. Retrieved November 25, 2020, from https://publications.iom.int/system/files/pdf/wmr_2020.pdf

Ireton, C. & Posetti, J. (2018). Journalism, "fake news" & disinformation: Handbook for journalism education and training. UNESCO Series on Journalism Education. Paris: United Nations Educational Scientific and Cultural Organization.

Koelbl, S. (2018, January 21). What comes after war in Syria? Der Spiegel. Retrieved November 25, 2020, from <https://www.spiegel.de/international/world/assad-s-victory-what-comes-after-war-in-syria-a-1188244.html>

- Koelbl, S. (2017, December 28). Assad hat den Krieg gewonnen – und jetzt? Der Spiegel. Retrieved November 25, 2020, from <https://www.spiegel.de/spiegel/syrien-das-assad-regime-hat-den-krieg-gewonnen-bis-zum-frieden-ist-es-noch-weit-a-1185131.html>
- Lee, S. T. (2010). Peace journalism: Principles and structural limitations in the news coverage of three conflicts. *Mass Communication and Society*, 13(4), 361-384. <https://doi.org/10.1080/15205430903348829>
- Les Inspirations éco. (2019, November 4). Émigration irrégulière: Á bord des zodiacs de la mort. LesEco. Retrieved December 7, 2020, from <https://leseco.ma/decryptages/347-enquete/81936-emigration-irreguliere%3E%20-a-bor%3E%20d-des-zodiacs-de-la-mort.html>
- Machill, M., & Beiler, M. (2009). The importance of the internet for journalistic research. *Journalism Studies*, 10(2), 178-203. <https://doi.org/10.1080/14616700802337768>
- Mast, J., Coesemans, R., & Temmerman, M. (2019). Constructive journalism: Concepts, practices, and discourses. *Journalism*, 20(4), 492-503. <https://doi.org/10.1177/1464884918770885>
- Masterton, M. (2005). Asian journalists seek values worth preserving. *Asia Pacific Media Educator*, 16, 41-48. Retrieved November 25, 2020, from <https://ro.uow.edu.au/apme/vol1/iss16/6>
- McIntyre, K., & Gyldensted, C. (2018). Positive Psychology as a Theoretical Foundation for Constructive Journalism. *Journalism Practice*, 12(6), 662-678. <https://doi.org/10.1080/17512786.2018.1472527>
- Neuberger, C., Nuernbergk, C., & Rischke, M. (2009). "Googleisierung" oder neue Quellen im Netz? In Neuberger, C., Nuernbergk, C. & Rischke, M. (Eds.), *Journalismus im Internet: Profession, Partizipation, Technisierung* (pp. 295-334). Wiesbaden: Springer VS.
- Nobel, C. (2018, August 9). 10 rules for reporting on war trauma survivors. *Journalist's Resource*. Retrieved November 25, 2020, from <https://journalistsresource.org/tip-sheets/reporting/10-rules-interviewing-trauma-survivors/>
- Osinski, J. [osinskije]. (2016, August 9). Choosing credible resources for research [Video]. YouTube. Retrieved November 25, 2020, from <https://www.youtube.com/watch?v=VXHQ2y8FIUQ&t=308s>
- Quinn, A. (2018). *Virtue ethics and professional journalism*. Cham: Springer.
- Rosling, H. (2018). *Factfulness: Ten reasons we're wrong about the world and why things are better than you think*. London: Sceptre.
- Schäfer, J.M. & Schlindwein, S. (2019, March 3). Outsourcing border controls to Africa. [Video]. DW. Retrieved November 25, 2020, from <https://www.dw.com/en/outsourcing-border-controls-to-africa/av-45599271>
- Schrøder, K. C. (2019). What do news readers really want to read about? How relevance works for news audiences. Oxford: Reuters Institute for the Study of Journalism. Retrieved November 25, 2020, from <http://www.digitalnewsreport.org/publications/2019/news-readers-really-want-read-relevance-works-news-audiences/>
- Shapiro, I., Albanese, P., & Doyle, L. (2006). What makes journalism "excellent"? Criteria identified by judges in two leading awards programs. *Canadian Journal of Communication*, 31(2), 425-44. <https://doi.org/10.22230/cjc.2006v31n2a1743>
- Swart, J., Peters, C., & Broersma, M. (2017). Navigating cross-media news use: Media repertoires and the value of news in everyday life. *Journalism Studies*, 18(11), 1343-1362. <https://doi.org/10.1080/1461670X.2015.1129285>
- Terceros, B. A. (2018, November 6). How can we tell migrants' stories better? Here are 10 ways. *Bright Magazine*. Retrieved December 7, 2020, from <https://brightthemag.com/ways-to-tell-migrant-stories-better-journalism-caravan-refugees-immigration-journalism-c0d006dcaacd>
- The war on my phone (2018). *The war on my phone*. Retrieved November 25, 2020, from <https://www.thewaronyourphone.com/>

Triandafyllidou, A. (2017). *Media Coverage on Migration: Promoting a Balanced Reporting*. IOM: Geneva. Retrieved November 12, 2019, from https://publications.iom.int/system/files/pdf/media_coverage_on_migration.pdf

UNHCR. (n. d.). *Glossary*. Retrieved November 25, 2020, from <http://www.issm.cnr.it/progetti/emigrazione/META-DATA%20E%20GLOSSARI/UNHCR/GLOSSARY%20UNHCR.pdf>

Vergeer, M. (2018). Incorrect, fake, and false. Journalists' perceived online source credibility and verification behavior. *Observatorio Journal*, 12(1), 37-52. <https://doi.org/10.15847/obsOBS12120181126>

White, A. (2015). *Moving stories: International review of how media cover migration*. Ethical Journalism Network. Retrieved June 26, 2018, from <https://ethicaljournalismnetwork.org/assets/docs/054/198/8feb836-108e6c6.pdf>



MODULI 11

Kuripoti kuhusu wahamiaji na wakimbizi: Kukabiliana na majeraha ya mawazo

na Anna-Carina Zappe



MALENGO YA MODULI

- Kufahamu hali tofauti za majeraha ya mawazo.
- Kuwahimiza washiriki kufanya kazi ya uanahabari kwa kuwahurumia waathiriwa wa majeraha ya mawazo.
- Kuwasaidia washiriki kutafakari kuhusu mchango wao na afya yao ya akili.



MATOKEO YA MAFUNZO

Kufikia mwisho wa moduli hii, washiriki wanapaswa kuwa na uwezo wa:

- Kutambua jinsi majeraha ya mawazo yanavyoweza kuathiri wahamiaji na wakimbizi.
→ **Matokeo ya mafunzo kwa stadi za utambuzi: Kupokea**
- Kutambua kwamba wanahabari wanaweza kuathirika kupitia uhusika binafsi.
→ **Matokeo ya mafunzo kwa stadi za utambuzi: Kupokea**
- Kuwaeleza jinsi hali za kutetereka kwa akili kutokana na uhusika binafsi zinaweza kuathiri uanahabari hasa wanahabari wanaporipoti kuhusu wahamiaji na wakimbizi, sanasana wakirejelea hali iliyosabababisha kutetereka. → **Matokeo ya mafunzo kwa stadi za mitazamo na maadili: Kufahamu**
- Kufanya kazi na kuandika habari kuhusu wahamiaji na wakimbizi, kiutu, kulingana na modeli ya TTIIM na hatua za kujikinga. → **Matokeo ya mafunzo kwa stadi za mitazamo ya kibinafsi na maadili: Kubuni**

Muhtasari

Changamoto na mbinu za kuangazia masuala ya wahamiaji na wakimbizi yaliyojadiliwa katika moduli iliyotangulia sasa zimepanuliwa na kujumuisha mitazamo ya kiitikeli, kisaikolojia na kibinafsi. Wanahabari wanaoripoti kuhusu watu wanaotoroka na wahamiaji¹, waliokumbana na hali ngumu ama kuripoti kuhusu watu wanaoishi kambini, mara nyingi katika hali ya kusikitisha wakikabiliana na upungufu wa chakula, hali duni ya vifaa vya usafi ama matibabu, hukabiliana na changamoto mpya. Wanapowahoji na kuripoti kuhusu wahamiaji ama wakimbizi, ama kutangamana na waathiriwa hawa, wanahabari wanakumbana na changamoto za kiakili. Hali hizi zote zinahitaji wanahabari kujitathmini. Watu wanaweza kupata majeraha ya mawazo, suala ambalo linaweza kutatiza mahojiano na hoja hii inastahili kutiliwa maanani hasa katika kuripoti habari zinazoweza kusababisha majeraha ya mawazo. Isitoshe, wanahabari hawana budi kufikiria jinsi wanavyohusika kibinafsi na afya yao ya akili. Kufahamu kwa kina changamoto zinazowakumba wanahabari katika muktadha wa kuripoti vyema masuala ya kutetereka kwa akili, istilahi ‘majeraha ya akili’ au ‘kiwewe’ itatambuliwa na kufafanuliwa kwanza. Tena, ni muhimu kukumbuka hatua mbalimbali ambazo zimependekezwa wakati wa kuripoti taarifa za uhamiaji na watu kula-zimika kutoroka kwao kwa sababu ya athari za majeraha ya mawazo. Kadhalika, mwongozo wa

1 Kwa ufafanuzi, tafadhali tazama maelezo yaliyopendekezwa katika Moduli 2 (European Migration Network, 2018; UNHCR, n. d.; IOM, 2019).

uhusika binafsi na masuala ya afya ya akili unaweza kuwasaidia wanahabari kujikinga wakiwa kazini.



ZOEZI LILILOPENDEKEZWA LA KUSHUGHULIKIA STADI ZA UTAMBUZI ZA KUKUMBUKA NA STADI ZA MITAZAMO YA KIBINAFSI NA MAADILI ZA KUPOKEA

Tumia picha za gazeti la *The Guardian* (Tondo 2019) kwa majadiliano darasani.

Waelekeze washiriki wajadili changamoto zinazowakumba wanahabari wanaporipoti kuhusu wahamiaji na wakimbizi, kama iliyoelezwa awali. Kusanya changamoto na kuzijadili wakati wa kikao kikuu.

Majeraha ya mawazo

Vichwa vya taarifa za habari vinavyolenga wahamiaji na wakimbizi vimejaa istilahi ‘kutetereka akili’; kama vile wahamiaji waliotetereka akili, yaliyowafuma wakimbizi, waathiriwa wa majeraha ya mawazo. Lakini kutetereka akili kutokana na matukio kama vile ajali au vita kuna maana maalumu na wanahabari hawana budi kuyatumia maneno kutetereka kwa uangalifu na ipasavyo. (European Union Agency for Fundamental Rights, 2020). Wanahabari wanaofahamu istilahi hii na maana yake hung’amua umuhimu wake katika kuripoti masuala ya wahamiaji na wakimbizi. Asili ya neno la Kiingereza la kutetereka akili, kiwewe au majeraha ya mawazo ni neno linalomaanisha jeraha kwa Kigiriki. Dass-Brailsford (2007, uk. 2-3) anasema neno hilo “linaashiria jeraha la mwili na linaenda sambamba na donda la mawazo linaloweza kufuata baada ya tukio la kutia kiwewe.” Jeraha la kimwili linamaanisha maradhi ama jeraha la kimwili ilhali jeraha la mawazo linarejelea “matukio yanayohatarisha maisha ama mwili wa mtu” (Ford, 2009 uk 6).

Mara nyingi, istilahi majeraha ya mawazo hutumika sawa na maneno mengine na hatimaye maana halisi kufifia. Ingawa istilahi hiyo inaweza kueleza tukio, kwa mfano, tukio la kujeruhi, inaweza kumaanisha matokeo ya matukio hayo. Hii ni kwa maana, kulingana na tukio, ni pamoja na “yanayompata mtu anapopatwa na tukio la kufadhaisha” (Ford & Courtois, 2009, uk. 15). Neno kiwewe likifahamika kuwa jeraha la mawazo, linatokana na tukio moja ama mengi yanayosababisha hali ya kutetereka kwa akili, na huzua hofu kuu ama kufanya hisia za mtu kushindwa kujisaidia.(Seidler, 2013).

Majeraha ya kibinafsi yanatofautiana kutoka mtu mmoja hadi mwingine ingawa “matokeo ya majeraha ya mawazo hayajabadilika pakubwa kuambatana na wakati wala utamaduni.” (Dass-Brailsford, 2007, uk. 3). Watu hukabiliana na matukio ya kufadhaisha kwa njia tofauti pamoja na kuonyesha dalili mbalimbali. (Storr na wengine, 2007). Baadhi ya watu wanaweza kuhimili majeraha kutokana na mbinu zao za kinga. Wengine wanashindwa kutokana na sababu za

hatari zinazowakabili. (Ford, 2009). Kadhalika, matukio mengi yanaweza kuchochea majeraha ya mawazo. Baadhi ya matukio hayo ni vita, mizozo, majeraha ya mwili, dhuluma za kingono (ubakaji, dhuluma kwa watoto/kuwachafua watoto), ajali, moto ama majanga ya kawaida. (Perkonigg na wengine, 2001). Wanasaikolojia wanatofautisha aina za majeraha ya mawazo kutokana na tukio moja (Type 1) na matukio mengi ambayo yanarudiwarudiwa ama yasiyoeleweka (Type 2). Kwa mfano, aina ya kwanza huenda ikawa tukio la kujeruhi, janga la kawaida ama shambulio la kigaidi. Aina ya pili ya tukio (Type 2) huenda ikawa dhuluma zinazoendelea, dhuluma za nyumbani, vita ama uchinjaji wa watu kutoka kundi ama jamii maalumu (Terr, 1995). Zaidi ya hayo, suala la mfuatano wa majeraha ya mawazo huenda likahusiana na marudio ya matukio ya kufadhaisha. Hali hii ya majeraha ya mawazo imejadiliwa kwa kina hasa katika muktadha wa uhamiaji na uhamishwaji wa kulazimishwa. Wengine wanaoathiriwa, ingawa si moja kwa moja², na majeraha ya mawazo ni pamoja na wasaidizi ama wanahabari (Palm na wengine, 2004). Aina hii ya waathiriwa imejadiliwa kwa kina hasa jinsi wanavyohusika na afya yao ya akili baadaye katika moduli hii.



ZOEZI LILILOPENDEKEZWA LA KUSHUGHULIKIA STADI ZA UTAMBUZI ZA KUKUMBUKA NA STADI ZA MITAZAMO YA KIBINAFSI NA MAADILI ZA KUPOKEA

Tumia maelezo yaliyotangulia kubuni mafunzo ya dakika 10. Mafunzo hayo yalenge mada ya majeraha ya mawazo na maana ya istilahi hiyo na matukio ya kusababisha majeraha ya mawazo, kulingana na muktadha wa desturi na nchi yenu. La muhimu ni kuelewa saikolojia ya majeraha ya mawazo kwa kuyatofautisha na athari kali.

Andaa mtihani mfupi ukiwauliza washiriki kuhusu vipengee vya majeraha ya mawazo. Unaweza kujumuisha maswali ya kuchagua jibu, yanayohitaji kujibu ukweli/uwongo ama maswali yanayohitaji ufafanuzi wa istilahi.

Majeraha ya mawazo, wahamiaji na wakimbizi

Uhamiaji na kulazimishwa kuhama ni mambo yawezayo kuumiza akili na hivyo basi kusababisha majeraha makali ya mawazo. Kuna ushahidi kwamba wahamiaji na wakimbizi wanakumbwa na ongezeko la matatizo ya akili; miongoni mwa wakimbizi na wanaotafuta hifadhi za salama, ongezeko la dalili za kutetereka akili baada ya kukumbana na matukio ya kutisha, kufadhaisha au kuhofisha (PTSD) lilihusishwa na idadi kubwa ya mikasa na mikosi inayosababisha kiwewe. (Carswell na wengine, 2011; Ford, 2009; Steel na wengine, 2009).

2 Kuna istilahi zaidi ya 20 za Kiingereza zinazoeleza sababu za hali ya akili kutetereka, kwa mfano jeraha la mawazo linalotokana na usimulizi uliofuatia tukio la kuteterekesha akili kwa mfano vita au ajali (Lemke, 2013).

Ifuatayo ni mifano mifupi ya takwimu zinazothibitisha kuenea kwa majeraha ya mawazo:


- Katika uchunguzi kuhusu magonjwa ya akili yanayoandamana na kudumu kwa muda mrefu, na pia hali ya afya miongoni mwa wakimbizi wa Bosnia waliohamia Croatia baada ya kutoroka vita nchini Bosnia na Herzegovina, walioripoti dalili zinazoashiria depresheni (39%) na PTSD (26%), asilimia 21 ya waliohojiwa walithibitisha kuwa na dalili za magonjwa yote mawili kwa muda mrefu (Mollica na wengine, 1999).
- Utafiti kuhusu hali ya matukio ya kuogofya na afya ya akili miongoni mwa wakimbizi kutoka Jamhuri ya Demokrasia ya Korea (“Wakimbizi wa chakula”) walio China, unaonyesha wenye PTSD (56%) na wasiwasi (90%) na depresheni (81%). Wahamiaji waliripoti matukio takribani 12 ya kujeruhi mawazo (Lee na wengine, 2001).
- Utathmini wa jumla wa matokeo ya uchunguzi miongoni mwa wakimbizi katika mataifa ya Magharibi unaonyesha kiwango cha PTSD (9%), depresheni kubwa (5%) na kiwango kikubwa cha matatizo yasababishwayo na hali hizo mbili (Fazel na wengine, 2005).
- Kutokana na ripoti za majibu ya ukaguzi binafsi, wahamiaji kutoka Amerika ya Kati, hasa Honduras, El Salvador na Guatemala waliohojiwa kwenye mpaka wa Marekani na Texas, walipatikana wakiwa na viwango vya PTSD vya 32%, depresheni (24%), na PTSD na depresheni (17%). Matokeo yanaashiria kuwa hali ya kutetereka kwa akili kwa wahamiaji hao imetokana na ghasia na mauaji (Keller na wengine, 2017).

Hivyo, huku asilimia ya wahamiaji na wakimbizi wanaokumbwa na PTSD ikitofautiana, wote huenda wakapatwa na matatizo ya majeraha ya mawazo. Utafiti unaolinganisha afya ya akili ya makundi mbalimbali ya wahamiaji na wakazi asili wa Uswizi unaonyesha kwamba kila kundi lililohojiwa lilithibitisha sababu za kuugua PTSD, (viwango vya mara ambazo hali hizo kutokea) kwa mfano, waliotafuta hifadhi (54%); wakimbizi (41%); “wahamiaji haramu” (6%), wahamaji waliotafuta ajira (17%); wazaliwa wa Uswizi (8%). Huenda idadi hizi zitafanya watu kufikia uamuzi kwamba hali ya uraia/na/ama sababu ya kuhama nchi ya kuzaliwa tayari ni ishara ya kukumbwa na PTSD (Heeren na wengine, 2014). Kundi la watafiti wa Brazil limeonyesha kuwa “PTSD imeenea sana (47%), hasa miongoni mwa wakimbizi, ambao wanatatizika mara mbili zaidi kuliko wahamiaji wafanyakazi. (Bustamante, na wengine, 2018). Tatizo la PTSD miongoni mwa waathiriwa wa mateso ya kimwili ni kati ya asilimia 50 na 70 (van Velsen na wengine, 1996).

La muhimu kufahamu ni kwamba matukio mengi yanayofuatana, siyo tukio moja, yanachangia katika kujeruhi mawazo ya wakimbizi. Matukio mbalimbali yanayofuatana na kusababisha matatizo ya akili hufuata mkondo maalumu, (Becker, 2014; Keilson, 1979; Zimmermann, 2012). Utafiti (Marshall, 2005; Mollica na wengine, 1998; Mollica na wengine, 1999) “umeonyesha kuwa wakimbizi na watu binafsi wanaoathiriwa na vita na kunyimwa haki za binadamu hufumwa

na visa vingi vya kutetereka akili.” (Carswell na wengine, 2011, uk. 107). Wahamiaji na wakimbizi hupatwa na mfululizo wa majeraha ya akili.

Kielelezo 31 kinachorejelea Zimmermann (2012) kinaweza kulinganishwa na matukio ya sasa. Kufikia wakati wa kuhariri Moduli hii (2020); watu wakitoroka vita nchini Iraq, Syria, Sudan Kusini ama Jamhuri ya Demokrasia ya Congo, huenda walikumbana na matukio ya kutisha, mbali na wale waliokuwa wakitoroka hali ya kuogofya kama vile watu wa Nigeria walioteswa na kundi la Boko Haram, ama wale waliotoroka mauaji ama ukosefu wa haki za binadamu kama kuteswa (tazama Moduli 3). Lililo wazi miongoni mwa waathiriwa wote ni kwamba tukio la kutisha, kufadhaisha na kuleta dhiki huzuka kabla ya wao kutoroka. Kabla ya kulazimishwa kutoroka, huenda watu wakapoteza marafiki na/ama jamaa, wakaingiwa na wahaka wa kuzingirwa na vifo, wakafungwa jela, wakateswa, wakapoteza mali, wakakosa chakula na lishe bora, wakajeruhiwa kimwili, wakakumbwa na hofu kuu, ubakaji na kupoteza riziki.



Katika utafiti uliotajwa hapo awali ambao unachunguza masaiibu yanayofuma familia na watu binafsi kabla ya kuhama, wakitoka Amerika ya Kati, kwenye mpaka wa Marekani, 83% walisema walihama kwa sababu ya ghasia nchini mwao (Keller na wengine, 2017). Hilo si tukio geni. Kwa mfano, mnamo 1998, kulingana na utafiti wa Australia, waliotafuta hifadhi, wakimbizi na wahamiaji wenye asili ya Kitamil waliripoti walihama kwao baada ya “kukabiliana na matatizo ya kiafya bila matibabu, ukosefu wa makao, kulazimishwa kutengana na wanafamilia wao, mauaji ama vifo visivyo vya kawaida vya wenzao” (Silove na wengine, 1998, uk.179).

Tukio jingine la kuhofisha ni wakati wa kutoroka, ambalo linaweza kuchukua siku, miezi au hata miaka na huenda likawajeruhi akili wakimbizi na pia wahamiaji, na wanaosafiri kwa sababu nyingine zaidi. Wakati huo, watu hutengana na marafiki ama wanafamilia, wananyang'anywa mali, wanalazimishwa kujijeruhi ama kujiua, wanashuhudia mateso ama mauaji, na/ama wanapoteza wanafamilia na marafiki waliosafiri nao. Isitoshe, huenda wasijue waliko kwa muda, wapotee ama wakabiliane na hali ngumu ya mazingira. Kwa mfano, ripoti ya shirika la UNHCR na Mixed Migration Center cha Danish Refugee Council, inaonyesha kuwa maelfu ya wakimbizi na wahamiaji hufa na kuteseka kutokana na kunyimwa haki za kibinadamu wanaposafiri wakielekea pwani ya Mediterranean upande wa Afrika na pia kutoka Magharibi na Mashariki mwa Afrika.

Wakiwa safarini na wakifika mwisho wa safari, ambao huenda uwe nchi ambayo wakimbizi ama wahamaji hawakuchagua, watu hawa hukumbwa na tukio jingine. Hawana budi kukubali mas-kani mapya, lugha geni na mazingira mapya. Mara nyingi, uraia wao huwa kitendawili, hivyo huwa hawana uhakika wa kukubaliwa kuishi nchini humo. Wakati huo, hali yao ya uraia isiyoju-likana huwapa hofu ya kudumu. Mfano mmoja wakati wa kuhariri moduli hii ni Kambi ya Wakim-bizi ya Moria, Ugiriki, ambapo wakazi wamekuwa wakingoja kwa miaka, tena katika mazingira duni, uraia wao kubadilishwa. Utafiti kutoka miongo iliyopita unaonyesha athari za kungoja uraia kubadilishwa unaweza kuumiza akili. Watafiti nchini Ujerumani waliwahoji vijana katika makao ya hifadhi na kugundua kwamba mazingira ya wakimbizi hao wachanga (hata ya zamani) yalisi-kitisha mno. Kwa vijana, changamoto zilikuwa pamoja na mabadiliko katika muundo wa familia pamoja na mabadiliko ya majukumu ya wanafamilia, kwa mfano, mwanafamilia yupi anashughu-likia mawasiliano rasmi (Gavranidou na wengine, 2008).

Tena, baadhi ya wahamiaji na wakimbizi wanapatwa na matatizo ya akili wakirudi nchi zao asili. Kulingana na shirika la EUROSTAT (2019), kuanzia 2015 hadi 2019, maombi yapatao milioni mbili watu waliotaka hifadhi yalikataliwa na mataifa wanachama wa EU. Huenda wakaathiriwa zaidi kimawazo wakirejea katika nchi zao asili. Kuna sababu mbalimbali za kuwaongezea maje- raha ya mawazo, ikiwa ni pamoja na kufungwa jela na kutenganishwa na marafiki wapya ama wanafamilia katika nchi geni, mbali na kuhofia maisha katika nchi asili.

Hatimaye, wahamiaji na wakimbizi tena huogopa kurejelea maisha ya kusikitisha na hivyo wa-naanza tena mipango ya kutoroka. Wahamiaji na wakimbizi wanaorejea nyumbani hukabiliwa na hatari ya umaskini kwani waliacha mali walipotoka. Wanaporudi, huenda wasiwe na sababu ya kuishi na huenda wakatengwa na wanafamilia na jamii (Zimmermann, 2012). Watu wanaorejea nyumbani mikono mitupu huenda wakaonekana walifeli machoni pa waliobaki nyumbani (Pujol-Mazzini, 2019). Hofu hii huenda ikasukuma watu kuanza tena mipango ya kuhama.



ZOEZI LILILOPENDEKEZWA LA KUSHUGHULIKIA STADI ZA UTAMBUZI ZA KUCHANGANUA NA STADI ZA MITAZAMO YA KIBINAFSI NA MAADILI ZA KUPOKEA:

Waonyeshe washiriki sehemu za filamu zilizopendekezwa zinazoonyesha wahamiaji ama wakimbizi wanaokabiliwa na matatizo ya majeraha ya mawazo na sababu mbalimbali za majeraha hayo. Kabla ya kuwasilisha filamu, waelekeze washiriki kusikiliza kwa makini kile wahamiaji na wakimbizi wanasema na wanachoambiwa kuhusu uhamiaji, kutoroshwa na majeraha ya mawazo yanayosababishwa. Washiriki watafakari na kulinganisha maana ya tukio linalosababisha akili kutetereka, ambalo huenda likawaogofya na kuwalemea waathiriwa. Wape washiriki muda wa kutafakari jinsi kiwango cha tukio hilo kinaeleza maana ya matukio ya kusababisha majeraha ya mawazo ambayo huenda mbinu za kukabiliana nalo zikakosekana na hivyo kuwa tatizo la kudumu kwa waathiriwa.

Video zilizopendekezwa (zimetayarishwa kwa Kiingereza):

1. *Kuyapatia sura mpya majeraha ya mawazo ya watoto wakimbizi katika Lesbos - Reshaping the Trauma of Refugee Children in Lesbos* (National Geographic, 2018) Muda: 00:00-00:15
2. *Wakimbizi katika Lesbos - Refugees on Lesbos* (Sallet, 2017) Muda: 02:16-02:26
3. *Kuipatia Afrika jukumu la kulinda mipaka - Outsourcing border controls to Africa* (Schäfer & Schlindwein, 2019) Muda: 20:10-21:20

Rejelea filamu kwa majadiliano. Jadili matokeo na maoni yenu. Katika muktadha huu, ingiza istilahi “mfululizo wa majeraha ya mawazo”.

Kuwahoji wahamiaji na wakimbizi na kuchunga usiwajeruhi mawazo

Kama ilivyojadiliwa katika moduli zilizotangulia, ni muhimu kuzungumzia suala la wahamiaji na wakimbizi, mbali na kuzungumza na wao wenyewe. Wakati mwingine, mahojiano na wahamiaji na wakimbizi yanachapishwa ama kuripotiwa kikamilifu, wakati mwingine ni kifungu tu ndicho kinachapishwa katika muktadha wa ripoti. Hata hivyo, kila mara, wanahabari hawana budi kukutana na wahamiaji na wakimbizi na kuzungumza nao, kuwauliza maswali. Taarifa za habari za Ulaya tangu 2015 zinaonyesha jinsi ripoti hizi na mawasiliano zinavyoshughulikiwa (tazama Moduli 4). Tutazame kisa kingine. Unakumbuka picha ya Óscar Alberto Martínez Ramírez na binti yake, Valeria, aliyekuwa na umri wa karibu miaka miwili. Wawili hao walikufa maji kwenye mpaka wa Marekani na Mexico, kama ilivyoelezwa katika Moduli 5. Vyombo vingi vya habari vilionyesha picha za mama yake Óscar, Rosa Ramirez, akilia na kusimulia mazungumzo ya mwisho na mwanawe, huku akionyeshana doli za mjukuu wake na kamera zikimulika mfululizo. Rosa, akifurikwa na machozi, alisimulia jinsi alivyohisi na mwanawe na mjukuu wake mdogo, walivyofunga safari na vile alivyohisi nyumbani bila wao. Wanahabari walimwuliza Rosa maswali

kadhaa — mengine ya kumwumiza moyo (miongoni mwa wengine: Renteria, 2019; Thebault na wengine, 2019; BBC News, 2019). Ni wazi kwamba maswali yanaweza kufufua kumbukumbu za majonzi. Hali hii inaathiri si tu mama wa mhasiriwa aliyefariki na mwanawe, bali wahamiaji na wakimbizi wote, na ndiposa ni muhimu kutafakari maswali yepi ya kuuliza wahamiaji na wakimbizi walioathiriwa kiakili pamoja na familia zao (Hanaford na wengine, 2016; McMahon na wengine, 2014).

Kituo cha The Dart Center for Journalism and Trauma (Dart Center) kinachowafunza wanahabari wanaoripoti kuhusu matukio ya kusikitisha na kufadhaisha yawezayo kujeruhi mawazo kote duniani, kimechapisha DVD/filamu mtandaoni kuwasaidia wanahabari na wanafunzi kujifunza mbinu za maadili ya kuandaa ripoti sahihi kuhusu waathiriwa wanaokumbana na majanga. Katika video hiyo, familia saba zinazokumbwa na janga, zinaeleza njia bora za kushirikiana na watu, ambao wanalengwa na wanahabari. Video hiyo inapatikana kwa Kiingereza na Kihispania (Dart Center, 2014).³

Wanahabari wanapaswa kutilia maanani mtazamo wao na tabia, mbali na maswali ya kuuliza. Jukumu kuu la mwanahabari linahusu mahitaji ya mhamiaji na mkimbizi na mhojaji ambaye ni mhusika mkuu katika taarifa ya mwanahabari. Hata hivyo, baadhi ya wanahabari hujifanya kuwa, “wanahabari watalii kuliko wanahabari wa wahamiaji,” mhariri wa gazeti la Italia la kila siku La Stampa, Anna Masera, alinukuliwa akisema mnamo 2016 (Albeanu, 2016). Kuangazia tu masaibu ya wahamiaji na wakimbizi na kuwahoji huku maoni, na afya yao ya akili zikipuuzwa kunawafanya wanahabari kuwa sawa na tai wanaofurahia majanga kuliko wanahabari wanaohe-shimiwa. Ili kuepuka kuwa “watalii wa majanga” wanahabari wanapaswa kutathmini mitazamo yao katika kila muktadha; mhojiwa ni “mwathiriwa”, ameshindwa kubadili hali yake ama ni “manusura” ambaye anajua kuhimili hali ngumu. Majibu kwa haya maswali yana maana kwa mahojiano (Nobel, 2018). Lakini huenda yakahitaji wanahabari kubadili tabia, pamoja na sauti zao, mbinu za mahojiano na mwelekeo wa taarifa.

Pia, wanahabari wanastahili kuwazia swali kwa kina, ili kuepuka kuwajeruhi tena waathiriwa wanaouguza majeraha. Kwa mfano, wakati wa mahojiano, neno ama maelezo mafupi yanaweza kufufua visa ama kumbukumbu za majonzi na wanahabari wanapaswa kuwapa wahojiwa muda wa kutulia. (Hanaford na wengine, 2016). “Mwanahabari afanye kila awezalo kumdhiti mtu anayehojiwa — wahojiwa wafahamu kuwa hawapaswi kujibu maswali yote na wanaweza kutamatisha mahojiano wakati wowote. Ni muhimu kusesitiza hoja hii kwani inaweza kuwa vigumu waathiriwa kuwaamini watu wengine.”

Hivyo ndivyo alivyosema Katy Robjant, mtaalamu wa saikolojia kwenye mahojiano na Dart Centre, kuhusu wanahabari wanaoandaa habari zinazohusiana na wahamiaji na wakimbizi (Hanaford na

3 Maelezo zaidi kuhusu kuripoti mada ya majeraha ya mawazo yanapatikana kwa mfano katika Healey (2019), ambaye ni mwanahabari maarufu wa shirika la BBC ama Simpson na wengine (2006). Roger Simpson alikuwa mwanahabari wa mashirika ya *The Wall Street Journal* na *Detroit Free Press* na alikuwa mkurugenzi mwanzilishi wa kituo cha Dart Center.

wengine, 2016). Inapendekezwa wanahabari wauliza maswali maalumu badala ya maswali ya jumla. Hivyo, wahamiaji ama wakimbizi wanaweza kupokezana taarifa hizo, bila kuhisi wanalazimishwa kufafanua visa ambavyo wahojiwa hawataki kukumbuka (Hanaford na wengine, 2016). Mwongozo ambao wanahabari wanapaswa kufuata wakiwahoji manusura (Journalist's Resource⁴) unasisitiza kuwa “wanahabari wana jukumu la kufanya kila wawezalo kuepuka kuwasukumia waathiriwa mateso zaidi na kuepuka kudunisha heshima yao katika jamii.” (Nobel, 2018).

Hivyo, wanahabari wanastahili kutambua kuwa wahamiaji na wakimbizi wanaweza kutoa maoni yao (ikiwezekana) kabla ya habari kutangazwa kwani hatua hii inaweza kupunguza athari na makali wakiangaziwa hadharani (Nobel, 2018).

Kanuni na machapisho⁵ kadhaa zinazogusia mahojiano bora zinaelekeza wanahabari la kufanya wakati wa mahojiano. Tumekusanya kanuni zifuatazo (TIIM – Trauma Informed Interviews with Migrants) kwa wanahabari wanapowahoji wahamiaji na wakimbizi. (Tazama Kielelezo 32, Dart Center, 2011; Hanaford na wengine, 2016; Hight & Smyth, 2009; Nobel, 2018). Kanuni hizi zinaimarisha ufahamu kwamba huenda mhamiaji ama mkimbizi anayehojiwa amejeruhiwa mawazo ama ana magonjwa ya akili.

Mahojiano bora na wahamiaji yanayojali majeraha ya mawazo (TIIM)

1. Maandalizi: Jitayarisha vyema kwa mahojiano – Mbali na stadi maalumu (kwa mfano stadi za mahojiano) na kufahamu sheria za uhamiaji, takwimu kuhusu wahamiaji na wakimbizi na historia ya wahamiaji, wanahabari wanapaswa kufahamu suala la athari za akili na kimwili. Wakifahamu vyema uwezekano wa kuwepo kwa majeraha ya mawazo wanahabari watakuwa wamechukua hatua muafaka ya maandalizi. Wanahabari wafahamu hoja za jinsia, lugha, tabaka, utamaduni ama uraia, ambazo zanaweza kuathiri mahojiano pande zote.

2. Kujitambulisha – Onyesha uaminifu na uwazi tangu mwanzoni. Kabla ya kuuliza maswali, wanahabari wanapaswa kujitambulisha na kueleza wajibu wao: “Jina langu ni John Doe, nafanya kazi na gazeti la Daily Magazine. Ningependa kuripoti kuhusu uhamiaji.” Huenda wahojiwa wasikubali ombi hilo mara moja. Wanahabari wadhibiti hisia zao wakikumbuka huenda wahojiwa wakakataa kutokana na machungu yaliyowapata. Ikiwa mwathiriwa atakataa kuhojiwa, mwanahabari anaweza kuacha kadi inayoeleza jinsi ya kumfikia na kupendekeza kufanya mahojiano baadaye.

3. Kumbuka kwamba, ni nadra wahojiwa kuwa watalaamu wa uanahabari – Wanahabari wafahamu huenda wahamiaji ama wakimbizi wanatoka maeneo ambapo desturi za vyombo vya habari ni

4 Kituo cha Journalist's Resource katika Shorenstein Center on Media, Politics and Public Policy, Harvard, kilihariri kanuni za viwango vya kuzingatia kwa wanahabari wanaoripoti manusura wa majanga. Kanuni hizo zililolewa kwanza na The War Horse ambalo huripoti habari za vita, majeraha ya mawazo na maswala ya askari na wanajeshi wastaafu (Nobel, 2018)

5 Kanuni za kituo cha Journalist's Resource (tazama tanbihichini 4) ni za kwanza, zingine ni kanuni za wanahabari wakihoji manusura wa majanga za Data Centre (Hight & Smyth, 2009). Kadhalika, mahojiano ya Data Centre ya “Kuripoti kuhusu Wakimbizi: Vidokezo kuhusu kuripoti katika hali tata (Hanaford na wengine, 2016) na taarifa “Kufanya Kazi na Manusura na waathiriwa” (Dart Center, 2011) pia yanatoa kanuni zaidi kwa wanahabari.

tofauti na za wanahabari. Wanapaswa kueleza utaratibu wa uanahabari eneo hilo na vile taarifa, picha na/ama huenda zikatumiwa. Kadhalika, wanahabari waeleze kwamba habari wanazokusanya zitahaririwa kabla au baada ya kuchapishwa, huenda zikatumiwa mara kadhaa au zisitumiwe kabisa. Kadhalika, wanahabari wasiwape waathiriwa mzigo zaidi wa makubaliano maalumu ya kutotoa usimulizi wao kwa wanahabari wengine. Watu wengi hawaelewi kuhusu makubaliano maalumu na vyombo vya habari na kujadili mipango ya aina hii na mwathiriwa huenda ikawa ukawa mzigo usiofaa.

4. Heshima – Wakati wote waheshimu wahojiwa. Wanahabari wanastahili kuheshimu haki za wahamiaji na wakimbizi wanaokataa kuhojiwa, kupigwa picha za filamu ama picha nyingine; Hili lina maana kwamba ni lazima watoe kibali kwanza. Wahamiaji na wakimbizi wanaoguzi majeraha ya kimwili na kimawazo na huenda wasiweze kuhojiwa, kuchukuliwa filamu ama kupigwa picha; na kushindwa kutoa idhini muafaka kuhusiana na mahojiano. Wanahabari hawana budi kutilia hili maanani. Watu waliokumbana na matukio ya kuteterekesha akili kutokana na vita, ajali, maafa na mengineyo huenda wasitake kukumbuka matukio hayo lakini wawe tayari kuzungumzia maswala mengine. Wanahabari wasiwasukume kuhojiwa, kwa kudai mahojiano hayo yatasaidia watu wengine.

5. Mandhari – Beba jukumu la kuandaa mahala salama pa mahojiano – Waathiriwa huwa hawataki kuzungumzia machungu yaliyowapata mbele ya wasikilizaji wasiowataka ama mahala penye mambo mengine ya kuteka akili. Isitoshe, wanahabari wajitahidi kuwadhibiti wahojiwa kwa kiwango fulani. Tafuta mazingira ambapo wahamiaji ama wakimbizi wanaelewa kwamba siyo lazima wajibu maswali yote ama kueleza (kwa kina), masaiibu yao na kwamba mahojiano yanaweza kutamatishwa wakati wowote, endapo hawataka kuendelea kuzungumza.

6: Maneno: Teua maneno yako kwa makini – Wanahabari wasivae uso wa huruma bandia lakini watumie maneno ya kuhimiza. Kwa mfano waseme, “Nasikitika kwa yaliyokupata” wala siyo, “Unahisi vipi?”. Wanahabari waepuke kusema, “Naelewa unavyohisi.” Haijalishi vile wanahabari wamejiandaa kwani hawawezi “kuelewa” yale waathiriwa wamepitia. Wanahabari watumie neno “manusura” badala ya “mwathirika.” Wahamiaji na wakimbizi siyo “waathiriwa” kama hawajiti hivyo. Tena, wanahabari waepuke lugha ya kulaumu na kuwa makini wakiuliza maswali ya “Kwa nini”, “maswali yenye dhana kwamba huenda mhojiwa angefanya jambo tofauti, kwa kuwa wahamiaji ama wakimbizi huenda wakajilaumu, wakahisi walikosa ama waone aibu.

7. Muda: Chukua muda unaofaa katika mahojiano – Wahamiaji na wakimbizi wamepitia hali ngumu na ya kibinafsi, hivyo wanahabari wachukue tu muda waliokubaliana na wahojiwa. Wahamiaji na wakimbizi wanaweza kuwaamini wanahabari. Hili lina maana kwamba wanahabari pia wanahitaji kutega masikio na kutowahukumu waowahoji. Baada ya muda, wahojiwa huenda watoe taarifa ambazo huenda wanahabari hawangeuliza.

8. Mjibizo: Kuwa tayari kukabiliana na mabadiliko ya ghafla ya fikra na hisia – Wakati wa mahojiano, wanahabari huenda, bila kutarajia, wakataja kisa ambacho kinafufua kumbukumbu za matukio ya kuumiza yaliyosahaulika. Huenda mhojiwa akaanza kuhangaika, akalemewa na hisia ama kunyamaza. Wakionyesha kana kwamba wanaumia au kukerwa, wanahabari wawape wahamiaji muda wa kutulia. Ushauri ni kuwa “Jaribu kutulia, na uhakikishe wahojiwa wanaweza kutabiri vitendo vyako.” (Hannaford na wengine, 2016). Wanahabari wajitolee kuwasaidia,

wahakikishie wahamiaji kuwa wako mahala salama na kuwakumbusha wao ni wanahabari. Mhojiwa anapotulia, wanahabari wanaweza kuuliza: “Uko tayari kuendelea na mahojiano?” Unaweza kufutulia mbali mahojiano mhojiwa anapolemewa na hisia.

Kielelezo 32 : Mfumo wa TIIM - mambo muhimu ya kukumbuka



Chanzo: Mkusanyiko wa mapendekezo kutoka Kituo cha Dart (2011), Hanaford et al. (2016), Hight and Smyth (2009) na Nobel (2018). Kielelezo asilia.

Baada ya mahojiano na wahamiaji ama wakimbizi, wanahabari wanastahili kutathmini ikiwa jambo lolote limewabadilikia wakimbizi kutokana na mahojiano hayo. Wanahabari hawana budi kujiuliza nani atawatunza wahojiwa. Ikiwa mahojiano yalizua hisia kali, ni vyema kutowaacha wahojiwa pekee yao. Wakati huo huo swali kuu linajitokeza; Utakabiliana vipi na haja ya kuwasiliana kibinafsi na wahojiwa? Utakabiliana vipi na hisia za kutaka kuwasaidia wahojiwa kibinafsi? Tena, utakabiliana vipi na nia ya wahamiaji na wakimbizi kusaidiwa? Wahojaji wanapaswa kusaidiwa ndipo wapate majibu kwa maswali haya. Baadhi ya hoja hizi zinaegemea hoja za kuhusika na afya ya mwanahabari. Kadhalika, ni muhimu kuwajulisha wahojiwa — haswa wakiwa nchini kiharamu — kutojitambulisha, yaani wajiamulie wenyewe iwapo hawataki majina yao kutokea katika taarifa za vyombo vya habari. Wanapoandika taarifa ama makala, wanahabari wanapaswa kusalimu matakwa ya wahojiwa. Kipengee hiki kizingatiwe, ikiwa kabla ya uchapishaji habari, wahamiaji ama wakimbizi wataamua hawataki kutambuliwa ama hawangependenda ripoti ya mahojiano yao kuchapishwa (Carcamo na wengine, 2014).

Isitoshe, uanahabari unaozingatia itikeli na kuwajali walio na majeraha ya mawazo, unaheshimu kanuni zilizojadiliwa katika Moduli 10; Chanzo na kukagua uhalisia wa habari, maneno yaliyotumika na mtazamo havina budi kuwa na usawa kwenye ripoti zinazowahusu wahamiaji na wakimbizi ili taarifa hizo zisiwaathiri vibaya wahamiaji ama wakimbizi ambao tayari wanauguza maje-

raha ya akili. Wanahabari wakumbuke kwamba wanapozungumza na mhamiaji ama mkimbizi, mhojiwa anaweza kuwa amechanganyikiwa ama mawazo kuwa mbali. Ni vyema kusoma tena ripoti uliyokusanya kuhakikisha iko sawa. (Hight & Smyth, 2009). Watu ambao wamepatwa na makuu na habari zao kueleza kwenye vyombo vya habari, baadaye, wamelalamika kuwa ripoti hizo zilivurugwa, kwa mfano, majina yaliandikwa vibaya, miaka haikuwa sahihi ama matukio na tarehe hazikuwa sahihi. (Simpson na wengine, 2006).



ZOEZI LILILOPENDEKEZWA LA KUTANGAMANA LA KUSHUGHULIKIA STADI ZA UTAMBUZI ZA KUBUNI NA STADI ZA MITAZAMO YA KIBINAFSI NA MAADILI ZA KUPOKEA:

Tumia kanuni zilizotolewa hapo chini kuwafunza washiriki kukutana na kuwahoji wahamiaji. Baadaye, waelekeze wanafunzi wazungumzie walichohisi wakati wakati wa uigizaji. Wape maelekezo ya kuwahoji wahamiaji na wakimbizi (TIIM) na wayajadili. Kushughulikia stadi za mitazamo binafsi na maadili za kujibu: Waambie washiriki warudie mahojiano — wakati huu wakizingatia kanuni mpya.

Maelekezo ya uigizaji

Maelekezo: Buni makundi ya washiriki wanne hadi sita katika kila kundi. Mshiriki mmoja aigize mkimbizi na wengine, wanahabari. Wagawie nafasi na kuwapa washiriki muda mfupi wa kusoma nafasi zao. Waeleze kwamba watakuwa na dakika 15 za uigizaji.

Jukumu la mwanahabari: Wajibu wako ni kuripoti hali ya mkimbizi binafsi katika kambi ya wakimbizi. Kwa nini alihama nchi yake asili? Alikumbwa na matukio yepi? Tukio lipi lilikuwa baya zaidi? Matokeo ya mahojiano yajumlishe nukuu za moja kwa moja pamoja na picha za wahojiwa.

Jukumu la mkimbizi: Tazama tena Moduli 2 na uelekezwe na masimulizi ya kibinafsi ya wahamiaji na wakimbizi. (Infomigrants, 2020; IOM, 2017; Médecins Sans Frontières, 2019).

Wapendekezee waigizaji kubuni hadithi ya wahusika wao.



MBINU MBADALA YA KUSHUGHULIKIA STADI ZA UTAMBUZI ZA UCHANGANUZI NA STADI ZA MITAZAMO YA KIBINAFSI NA MAADILI ZA KUPOKEA:

Waonyeshe washiriki video zilizopendekezwa kutoka Dart Center *Trauma-Informed Interviewing: Techniques from a Clinician’s Toolkit* (Porterfield, 2019) na wajadili maelekezo kwa watu binafsi ya mahojiano bora ya watu waliotetereka akili.

Afya ya akili ya wanahabari wanaoripoti kuhusu wahamiaji na wakimbizi

Wanahabari wanaweza kutetereka akili kutokana na wanachoripoti (Feinstein & Storm, 2017). Athari zisizo za moja kwa moja zinaweza kumpata mwanahabari anapoelezwa kwa kina, matukio ya kuhofisha — hata kwa mbali na hata bila kushuhudia tukio lenyewe (American Psychiatric Association, 2013). Hivyo, athari zilizojitokeza wakati wa mazungumzo zinaweza kufufua kumbukumbu za wasikilizaji ambao wamewahi kukumbana na tukio la kuogofya lililowaathiri akili. (Krans na wengine, 2010). Hatimaye, dalili za majereha ya mawazo zinaweza kuhamishiwa wanaowatunza wahasika, jamaa ama wanahabari. Wanahabari wanaweza kujeruhiwa wanapozungumza na wahamiaji ama wakimbizi waliotetereka akili. Uchanganuzi wa tafiti kadhaa kuhusu wanahabari na PTSD zinaonyesha kwamba kuna hatari zinazowakumba wanahabari wakiwa kazini, kwa mfano, matukio ya kutisha katika historia yao ya kibinafsi, kiwango cha kushuhudia matukio ya kuogofya, msaada duni kutoka jamii na wataalamu, mbali na ukosefu wa tajriba⁶. Uchanganuzi huo pia unaonyesha kwamba kuna mbinu za kukabiliana na hali hiyo, kwa mfano msaada wa kijamii na kujiondoa kitaalamu kwenye tukio lililosababisha hali ya kutetereka kwa akili — hatua ambayo huenda ikadhihirisha dalili za kujitenga na jambo (Weidmann, 2008). Mfano wa jinsi wanahabari wanaoripoti kuhusu wahamiaji na wakimbizi wanavyobeba mzigo wa matukio unaelezwa na Simon Shuster, mwanahabari wa Time Magazine, New York, aliyesimulia aliyoshuhudia katika kambi ya wakimbizi ya Idomeni, kaskazini mwa Ugiriki. “Niligutuka nilipowasili kambini humo na kujionea hali — nilishuhudia visa vingi vya kusikitisha” (Scott, 2016).

Will Vassilopoulos, mwanahabari Mgiriki anayefanya kazi na shirika la habari la Agence France-Presse, alieleza hali katika eneo la Lesbos, Ugiriki, mnamo 2016 kuwa ya “kuogofya” na “mbovu” (Feinstein & Storm, 2017, uk. 21). Hali hii bila shaka ina matokeo mabaya yawezayo kusababisha madhara. Mbali na PTSD na depresheni, wanahabari wanaoripoti maswala ya wahamiaji na wakimbizi huenda wakaathiriwa na “majeraha ya maadili” (Feinstein na wengine, 2018), yanayofafanuliwa kuwa uvunjaji wa viwango vya itikeli binafsi. Mtu anaweza kujeruhiwa kimaadili kwa kushuhudia (siyo moja kwa moja) tukio mbaya. (Stein na wengine, 2012).

“Majeraha ya kiitikeli kwa wanahabari wanaoripoti matatizo ya wakimbizi yanahusiana na kuwa mzazi, kufanya kazi peke yako, kushuhudia vita kwa mara ya kwanza, ongezeko la kazi karibu, imani kwamba hakuna msaada kutoka kwa mwajiri na ukosefu wa vifaa hitajika unaporipoti” (Feinstein na wengine, 2018, uk. 4).

Kadhalika, kuna uhusiano mkuu kati ya kuhisi kuwa na hatia na majeraha yaletwayo na kukiuka maadili. Wanahabari walioripoti taarifa za wahamiaji na wakimbizi karibu na nyumbani ama walioamua kuwasaidia wahamiaji — badala ya kuripoti kuwahusu — wakati huo huo wakitekeleza jukumu la mwanahabari — huhisi zaidi kuwa na hatia (Feinstein na wengine, 2018). Kuna ripoti nyingi zinazokinzana kuhusu itikeli ambazo huwafanya wanahabari kujitwika majukumu ya kujali maslahi ya wahojiwa ama mada wanayoshughulikia na zinaweza kuwaweka katika hali tatanishi,

6 Pia, kazi ya kitaalamu kwa muda mrefu humfanya mtu kujirundikia majeraha ya akili. (Weidmann, 2008).

kama ile iliyotajwa na Simon Shuster, aliyesema kwamba alivishwa vazi la uraia na kuwasaidia watu. Aliliita, “kujitathmini kila mara ambapo mtu hana budi kusitisha na kutafakari ” kuhusu jukumu kuu — kuripoti ama kujihusisha na matendo ya ufadhili (Scott, 2016). Kisa kingine ni cha mkimbizi kutoka Syria, aliyemsihi mwanahabari Jess Hurd kumsaidia akisema: “Nipige risasi ama uniweke sandukuni mwako” (Hurd, 2015). Kadhalika, kuna mkimbizi aliyemwendea mwanahabari Mjerumani Raniah Salloum, na kuanza kumlaumu kwa “kushindwa kuzuia polisi kutumia nguvu kupindukia dhidi ya wakimbizi.” (Hanaford na wengine, 2016).

Hili linamaanisha kwamba wanahabari hawana budi kutambua mchango wao wakati wa matukio; Mimi ni nani, msaidizi ama mwanahabari? Ni majukumu yepi yanaoambatana na kila nafsi? Mamlaka ya mwanahabari yanafikia wapi? Hatua na msaada wa kibinadamu unahitajika wapi? “Data inatoa ushahidi kwamba majeraha ya itikeli huenda yasijitokeze miongoni mwa wanahabari wanaofahamu jukumu lao rasmi wanalotarajiwa kutekeleza (Feinstein & Storm, 2017).

Kisa cha mwanahabari Fredrik Örnevall kinaonyesha jinsi mwanahabari anavyoweza kujikutaka kwenye njiapanda. Örnevall, mpiga picha wake na mkalimani waliingiza Sweden, kimagendo, mtoto mkimbizi kutoka Ugiriki walipokuwa wakiandaa makala ya televisheni nchini Ugiriki, mnamo 2015. Örnevall alienda mahakamani na kutoa ushahidi kuwa angekosha amani milele kama hangemsaidia mvulana huyo (Crouch, 2017).⁷ Kisa kingine ni cha mwanahabari Alice Petréni wa shirika la Swedish Radio. Aliporipoti kuhusu familia kutoka Afghanistan ikiwa Ulaya Kusini, aliwapa pesa zake binafsi. Hata hivyo, baadaye alibadili kauli. Alieleza: “Amekuwa akiniandikia akitaka pesa zaidi na nikamjibu, ‘Mimi ni mwanahabari siyo mwanaharakati. Siwezi kurudi huko mpakani. Nilifanya hivyo kwa sababu nilionea familia hiyo huruma ingawa nilitambua baadaye ulikuwa uamuzi mbaya kwani unainua matarajio na siwezi kutimiza hayo matarajio kwa hivyo, sina budi kukomesha tabia hiyo.” (Feinstein & Storm, 2017, uk. 27)

Mwanahabari Sofia Papadopoulou alijitolea kusaidia wenzi wawili katika kambi ya Idomeni, Ugiriki. Anasema: “Hapo ndipo nilitambua ni vigumu kuzingatia sheria kali za uanahabari nilizofunzwa shuleni, na kwamba hakuna tajriba ya kazini inayoweza kulinganishwa na mafunzo ya darasani” (Fronista & Papadopoulou, 2018). Wanahabari wanashauriwa kutathmini mchango wao wanapokusanya taarifa zinazohusiana na wahamiaji na wakimbizi na huenda wakahitajika kurejelea mchango huo mara kwa mara.

Kwa jumla, wanahabari wanastahili kufahamu wanaweza kushiriki katika njia bora mbalimbali. Wanapaswa kufikiria jinsi ya kukabiliana na hali na jinsi ya kujikinga, kabla ya kuanza kuripoti. Wanapaswa kutambua hali halisi ni tofauti na chochote walichofunzwa. Katika mwongozo wa Columbia Journalism School, mbinu za usalama na ujitunzaji kwa wanahabari zimetolewa kwa muhtasari. Mbinu hizi zinawahimiza wanahabari kujitunza wakiwa nje kazini na kuwa tayari, kujali na makini (Hylton, 2015).

7 Vidokezo zaidi kuhusu afya ya akili kwa wanahabari vinapatikana katika Karki (2017) au Hylton (2015).



KAZI YA ZIADA ILIYOPENDEKEZWA YA KUSHUGHULIKIA STADI ZA UTAMBUZI ZA UFAHAMU NA UBUNIFU NA STADI ZA MITAZAMO YA KIBINAFSI NA MAADILI ZA KUPOKEA:

(A) Waelekeze wanafunzi watazame ripoti ya video ya Simon Shuster kutoka Kambi ya Idomeni (Shuster, 2016). Waambie waandike jinsi majeraha ya mawazo na uhusika binafsi zinaweza kuathiri maandalizi ya habari kuhusu wahamiaji na wakimbizi na kwa kiwango kipi mizozo inaweza kusababishia mwanahabari hali ya kutetereka kwa akili.

(B) Kukiwa na nafasi ya kuwapa wanafunzi fursa ya kutangamana na wahamiaji ama wakimbizi (kupitia mashirika ama halmashauri), wahimize wanafunzi wako kuandaa mahojiano na mhamiaji ama mkimbizi. Upande mwingine, wahimize wanafunzi kutayarisha mahojiano na kila mmoja kubuni utaratibu wa mahojiano hayo. Watilie maanani hali tatanishi inayoweza kuibuka kutokana na majeraha ya akili na afya yako binafsi ya akili.



USOMAJI WA ZIADA:

Kiakademia:

Fronista, P., & Papadopoulou, S. (2018). Down and out and wet and bedraggled: Navigating the emotional and ethical maelstrom of reporting from the crisis flash-point of Idomeni. In Dell'Orto, G. & Wetzstein, I. (Eds.), *Refugee news, refugee poli-tics: Journalism, public opinion and policymaking in Europe* (127-140). New York: Routledge.

Kiuanahabari:

Shuster, S. (2016, March 24). This 13-Year-Old Girl Stranded in a Refugee Camp Is Praying to Get Out. [Video]. *Time Magazine*. Retrieved May 11, 2020, from <https://time.com/4269714/syrian-refugee-girl/>

Kitaasisi:

Hanaford, A., Hurd, J., Parkinson, J., Robjant, K., Salloum, R., & Gering, J. (2016, February 26). Reporting on refugees: Tips on covering the crisis. Dart Center. Retrieved December 18, 2018, from <https://dartcenter.org/resources/reporting-refugees-tips-covering-crisis>

Marejeleo

Albeanu, C. (2016, April 21). Journalists should not act like “disaster tourists” when covering the refugee crisis. *Journalism*. Retrieved November 25, 2020, from <https://www.journalism.co.uk/news/journalists-should-not-act-like-disaster-tourists-when-covering-the-refugee-crisis/s2/a630816/>

American Psychiatric Association. (2013). *Diagnostic and statistical manual of mental disorders* (5th ed.). Washington, DC: American Psychiatric Association.

BBC News (2019, June 27). Rio Grande drowning: “I knew it was the last time I would see my son” – BBC News. [Video]. YouTube. Retrieved November 25, 2020, from <https://www.youtube.com/watch?v=osMi-Kx1Lg>

Becker, D. (2014). *Die Erfindung des Traumas: Verflochtene Geschichten*. Gießen: Psychosozial-Verlag.

Breen, D. (2019). “On this journey, no one cares if you live or die”. Abuse, protection, and justice along routes between East and West Africa and Africa’s Mediterranean coast. UNHCR. Retrieved November 25, 2020, from <https://www.unhcr.org/protection/operations/5f2129fb4/journey-cares-live-die-abuse-protection-justice-along-routes-east-west.html>

Bustamante, L. H. U., Cerqueira, R. O., Leclerc, E., & Brietzke, E. (2018). Stress, trauma, and posttraumatic stress disorder in migrants: a comprehensive review. *Brazilian Journal of Psychiatry*, 40(2), 220-225. <https://doi.org/10.1590/1516-4446-2017-2290>

Carcamo, C., Matza, M., Pierre-Pierre, G., Sacchetti, M., & Ritchin, A. (2014, January 6). Covering immigrants & immigration: Tips from experts. Dart Center. Retrieved January 16, 2019, from <http://dartcenter.org/content/covering-immigrants-immigration-tips-from-experts>

Carswell, K., Blackburn, P., & Barker, C. (2011). The relationship between trauma, post-migration problems and the psychological well-being of refugees and asylum seekers. *The International Journal of Social Psychiatry*, 57(2), 107-119. <https://doi.org/10.1177/0020764009105699>

Crouch, D. (2017). “Do I regret it? Not for a second”: Swedish journalist goes on trial for helping refugees. *The Guardian*. Retrieved March 13, 2019, from <https://www.theguardian.com/world/2017/jan/25/swedish-journalist-on-trial-people-smuggling-refugees-fredrik-onnevall>

Dart Center (2011, February 22). Working with victims and survivors. Dart Center. Retrieved November 25, 2020, from <http://dartcenter.org/content/working-with-victims-and-survivors#.VUYw-kJhP39>

Dart Center (2014, March 24). Ethical reporting on people affected by trauma. [Video]. Dart Center. Retrieved November 25, 2020, from <https://dartcenter.org/media/ethical-reporting-people-affected-trauma>

Dass-Brailsford, P. (2007). *A practical approach to trauma: Empowering interventions*. Thousand Oaks, CA: Sage Publications.

European Union Agency for Fundamental Rights. (2020, February 2). E-media toolkit on migration: Trainer’s manual. European Union Agency for Fundamental Rights. Retrieved November 25, 2020, from <https://fra.europa.eu/en/publication/2020/e-media-toolkit-migration-trainers-manual>

European Migration Network. (2018). EMN Information leaflet. Asylum and migration. Glossary 6.0: A tool for better comparability produced by the European Migration Network. European Migration Network. Retrieved November 25, 2020, from https://www.emn.at/wp-content/uploads/2018/06/emn-glossary-6-0_en.pdf

EUROSTAT (2019). First instance decisions on applications by citizenship, age and sex: Annual aggregated data (rounded). [Data set]. Statistical Office of the European Union (EUROSTAT). Retrieved September 21, 2020, from https://appsso.eurostat.ec.europa.eu/nui/show.do?dataset=migr_asydcfsta&lang=en

Fazel, M., Wheeler, J., & Danesh, J. (2005). Prevalence of serious mental disorder in 7000 refugees resettled in western countries: A systematic review. *The Lancet*, 365(9467), 1309-1314. [https://doi.org/10.1016/S0140-6736\(05\)61027-6](https://doi.org/10.1016/S0140-6736(05)61027-6)

- Feinstein, A., Pavisian, B., & Storm, H. (2018). Journalists covering the refugee and migration crisis are affected by moral injury not PTSD. *Journal of the Royal Society of Medicine Open*, 9(3), 1-7. <https://doi.org/10.1177/2054270418759010>
- Feinstein, A., & Storm, H. (2017). *The emotional toll on journalists covering the refugee crisis*. Oxford: Reuters Institute for the Study of Journalism. Retrieved November 25, 2020, from <https://reutersinstitute.politics.ox.ac.uk/sites/default/files/2017-07/Storm%20and%20Feinstein%20-%20Emotional%20Toll.pdf>
- Ford, J. D., & Courtois, C. A. (2009). Defining and understanding complex trauma and complex traumatic stress disorders. In Courtois, C. A. & Ford, J. D. (Eds.), *Treating complex traumatic stress disorders: An evidence-based guide* (pp. 13-30). New York: The Guilford Press.
- Ford, J. D. (2009). *Posttraumatic stress disorder: Scientific and professional dimensions*. Burlington, San Diego, London, New York: Academic Press.
- Fronista, P., & Papadopoulou, S. (2018). Down and out and wet and bedraggled: Navigating the emotional and ethical maelstrom of reporting from the crisis flashpoint of Idomeni. In Dell'Orto, G. & Wetzstein, I. (Eds.), *Refugee news, refugee politics: Journalism, public opinion and policymaking in Europe* (127-140). New York: Routledge.
- Gavranidou, M., Niemiec, B., Magg, B., & Rosner, R. (2008). Traumatische Erfahrungen, aktuelle Lebensbedingungen im Exil und psychische Belastung junger Flüchtlinge. *Kindheit und Entwicklung*, 17, 224-231. <https://doi.org/10.1026/0942-5403.17.4.224>
- Hanaford, A., Hurd, J., Parkinson, J., Robjant, K., Salloum, R., & Gering, J. (2016, February 26). Reporting on refugees: Tips on covering the crisis. Dart Center. Retrieved December 18, 2018, from <https://dartcenter.org/resources/reporting-refugees-tips-covering-crisis>
- Healey, J. (2019). *Trauma reporting. A journalist's guide to covering sensitive stories*. London: Routledge.
- Heeren, M., Wittmann, L., Ehlert, U., Schnyder, U., Maier, T., & Müller, J. (2014). Psychopathology and resident status – comparing asylum seekers, refugees, illegal migrants, labor migrants, and residents. *Comprehensive Psychiatry*, 55(4), 818-825. <https://doi.org/10.1016/j.comppsy.2014.02.003>
- Hight, J., & Smyth, F. (2009). *Tragedies & Journalists*. Dart Center. Retrieved December 18, 2018, from <https://dartcenter.org/content/tragedies-journalists-6?section=all>
- Hurd, J. (2015, August 24). Calais: "Shoot me or put me in your trunk". [Blog post]. Jess Hurd. Retrieved January 4, 2020, from <http://jesshurd.com/2015/08/24/calais-shoot-me-or-put-me-in-your-trunk/>
- Hylton, A. (2015). Safety & self-care strategies for every beat. Dart Center. Retrieved January 16, 2019, from <http://dartcenter.org/resources/panel-offers-strategies-on-safety-security-and-self-care>
- Infomigrants (2020). Stories about migrants. Retrieved October 10, 2020, from <https://www.infomigrants.net/en/>
- IOM (2019). Glossary on Migration. International Organization for Migration. Geneva. Retrieved August 5, 2019, from https://publications.iom.int/system/files/pdf/iml_34_glossary.pdf
- IOM (2017). I am a migrant. Retrieved October 10, 2020, from <https://iamamigrant.org/stories>
- Karki, A. (2017, November 1). 6 tips for protecting your mental health when reporting on trauma. [Blog post]. International Journalists Network. Retrieved May 10, 2020, from <https://ijnet.org/en/story/6-tips-protecting-your-mental-health-when-reporting-trauma>
- Keilson, H. (1979). *Sequentielle Traumatisierung bei Kindern: Deskriptiv-klinische und quantifizierend-statische follow-up Untersuchung zum Schicksal der jüdischen Kriegswaisen in den Niederlanden*. Stuttgart: Enke.
- Keller, A., Joscelyne, A., Granski, M., & Rosenfeld, B. (2017). Pre-migration trauma exposure and mental health functioning among Central American migrants arriving at the US border. *PLoS One*, 12(1). <https://doi.org/10.1371/journal.pone.0168692>

- Krans, J., Näring, G., Holmes, E. A., & Becker, E. S. (2010). "I see what you're saying": Intrusive images from listening to a traumatic verbal report. *Journal of Anxiety Disorders*, 24(1), 134-140. <https://doi.org/10.1016/j.janxdis.2009.09.009>
- Lee, Y., Lee, M. K., Chun, K. H., Lee, Y. K., & Yoon, S. J. (2001). Trauma experience of North Korean refugees in China. *American Journal of Preventive Medicine*, 20(3), 225-229. [https://doi.org/10.1016/S0749-3797\(00\)00282-8](https://doi.org/10.1016/S0749-3797(00)00282-8)
- Lemke, J. (2013). *Sekundäre Traumatisierung: Klärung von Begriffen und Konzepten der Mittraumatisierung* (3rd ed.). Kröning: Asanger Verlag.
- Marshall, G. N. (2005). Mental health of Cambodian refugees two decades after resettlement in the United States. *JAMA: Journal of the American Medical Association*, 294(5), 571-579. <https://doi.org/10.1001/jama.294.5.571>
- McMahon, C., Ricketson, M., & Tippet, G. (2014, March 25). Ethical reporting on traumatised people. Dart Center. Retrieved November 25, 2020, from <https://dartcenter.org/content/dvd-launched-ethical-reporting-people-affected-by-trauma>
- Médecins Sans Frontières (2019). Refugees around the world: Stories of survival. Retrieved October, 10, 2020, from <https://www.msf.org/refugees-around-world-stories-survival-world-refugee-day>
- Mollica, R. F., McInnes K., Sarajlic, N., Lavelle, J., Sarajlic I., & Massagli, M. P. (1999). Disability associated with psychiatric comorbidity and health status in Bosnian refugees living in Croatia. *JAMA: Journal of the American Medical Association*. (282), 433-439. <http://doi.org/10.1001/jama.282.5.433>
- Mollica, R. F., McInnes, K., Pool, C., & Tor, S. (1998). Dose-effect relationships of trauma to symptoms of depression and post-traumatic stress disorder among Cambodian survivors of mass violence. *British Journal of Psychiatry*, 173(6), 482-488. <https://doi.org/10.1192/bjp.173.6.482>
- National Geographic. (2018, June 24). Reshaping the Trauma of Refugee Children in Lesbos. National Geographic [Video]. YouTube. Retrieved December 18, 2018, from <https://www.youtube.com/watch?v=V6lVZ569wsk>
- Nobel, C. (2018, August 9). 10 rules for reporting on war trauma survivors. *Journalist's Resource*. Retrieved December 7, 2020, from <https://journalistsresource.org/tip-sheets/reporting/10-rules-interviewing-trauma-survivors/>
- Palm, K. M., Polusny, M. A., & Follette, V. M. (2004). Vicarious traumatization: Potential hazards and interventions for disaster and trauma workers. *Prehospital and Disaster Medicine*, 19(1), 73-78. <https://doi.org/10.1017/S1049023X00001503>
- Perkonig, A., Kessler, R. C., Storz, S., & Wittchen, H. U. (2001). Traumatic events and post-traumatic stress disorder in the community: Prevalence, risk factors and comorbidity. *Acta Psychiatrica Scandinavica*, 101(1), 46-59. <https://doi.org/10.1034/j.1600-0447.2000.101001046.x>
- Porterfield, K. (2019, November 12). Trauma-informed interviewing: Techniques from a clinician's toolkit. [Video]. Dart Center. Retrieved May 10, 2020, from <https://dartcenter.org/resources/trauma-informed-interviewing-techniques-clinician%E2%80%99s-toolkit>
- Pujol-Mazzini, A. (2019). When Returning Home is a Deadly Journey, "Shame is the Returnee's Worst Enemy". IOM. Retrieved October 12, 2020, from <https://www.iom.int/news/when-returning-home-deadly-journey-shame-returnees-worst-enemy>
- Renteria, N. (2019, June 26). "I told him not to go", mother of drowned Salvadoran migrant laments. Reuters. Retrieved June 26, 2019, from <https://www.reuters.com/article/us-usa-immigration-mexico-mother/i-told-him-not-to-go-mother-of-drowned-salvadoran-migrant-laments-idUSKCN1TR2PJ>
- Sallet, O. (2017, December 16). Refugees on Lesbos. [Video] DW. Retrieved December 18, 2018, from <https://www.dw.com/en/refugees-on-lesbos/av-41822207>

- Schäfer, J.M. & Schlindwein, S. (2019, March 3). Outsourcing border controls to Africa. [Video]. DW. Retrieved December 18, 2018, from <https://www.dw.com/en/outsourcing-border-controls-to-africa/av-45599271>
- Scott, C. (2016, April 5). A reporter's ethical dilemma while covering the refugee crisis. Journalism. Retrieved May 11, 2020, from <https://www.journalism.co.uk/news/a-reporter-s-ethical-dilemma-while-covering-the-refugee-crisis/s2/a625814/>
- Seidler, G. H. (2013). *Psychotraumatologie: Das Lehrbuch*. Stuttgart: Kohlhammer.
- Shuster, S. (2016, March 24). This 13-Year-Old Girl Stranded in a Refugee Camp Is Praying to Get Out. [Video]. Time Magazine. Retrieved May 11, 2020, from <https://time.com/4269714/syrian-refugee-girl/>
- Silove, D., Steel, Z., McGorry, P., & Mohan, P. (1998). Trauma exposure, postmigration stressors, and symptoms of anxiety, depression and post-traumatic stress in Tamil asylum-seekers: comparison with refugees and immigrants. *Acta Psychiatrica Scandinavica*, 97(3), 175-181. <https://doi.org/10.1111/j.1600-0447.1998.tb09984.x>
- Simpson, R., Coté, W., & Scherer, M. (2006). *Covering violence. A guide to ethical reporting about victims & trauma*. New York: Columbia University Press.
- Steel, Z., Chey, T., Silove, D., Marnane, C., Bryant, R. A., & van Ommeren, M. (2009). Association of torture and their potentially traumatic events with mental health outcomes among populations exposed to mass conflict and displacement. *JAMA: Journal of the American Medical Association*, 302(5), 537-549. <https://doi.org/10.1001/jama.2009.1132>
- Stein, N. R., Mills, M. A., Arditte, K., Mendoza, C., Borah, A. M., Resick, P. A., & Litz, B. T. (2012). A scheme for categorizing traumatic military events. *Behavior Modification*, 36(6), 787-807. <https://doi.org/10.1177/0145445512446945>
- Storr, C. L., Ialongo, N.S., Anthony, J. C., & Breslau, N. (2007). Childhood antecedents of exposure to traumatic events and posttraumatic stress disorder. *American Journal of Psychiatry*, 164(1), 119-125. <https://doi.org/10.1176/appi.ajp.164.1.119>
- Terr, L. (1995). *Schreckliches Vergessen, heilsames Erinnern: Traumatische Erfahrungen drängen ans Licht*. München: Kindler.
- Thebault, R., Velarde, L., & Hauslohner, A. (2019, June 26). The father and daughter who drowned at the border were desperate for a better life, family says. *The Washington Post*. Retrieved November 25, 2020, from <https://www.washingtonpost.com/world/2019/06/26/father-daughter-who-drowned-border-dove-into-river-desperation/>
- Tondo, L. (2019, September 2). I'm like a mouse in a trap': trauma of Europe's refugees – in pictures. *The Guardian*. Retrieved December 5, 2018, from <https://www.theguardian.com/global-development/gallery/2019/sep/02/im-like-a-mouse-in-a-trap-trauma-of-europes-refugees-in-pictures>
- UNHCR (n. d.). Glossary. Retrieved November 25, 2020, from <http://www.issm.cnr.it/progetti/emigrazione/ME-TA-DATA%20E%20GLOSSARI/UNHCR/GLOSSARY%20UNHCR.pdf>
- Van Velsen, C., Gorst-Unsworth, C., & Turner, S. (1996). Survivors of torture and organized violence: Demography and diagnosis. *Journal of Traumatic Stress*, 9(2), 181-193. <https://doi.org/10.1007/BF02110654>
- Weidmann, A. (2008). Primäre und sekundäre Traumatisierung: Ein Berufsrisiko für Journalisten? *Trauma & Gewalt*, 2(3), 234-245. Retrieved January 12, 2020, from <https://elibrary.klett-cotta.de/article/99.120130/tg-2-3-234>
- Zimmermann, D. (2012). *Migration und Trauma: Pädagogisches Verstehen und Handeln in der Arbeit mit jungen Flüchtlingen*. Gießen: Psychosozial-Verlag.



MODULI 12

Mipango ya ushirikiano katika kuripoti kuhusu uhamiaji

na Tina Bettels-Schwabbauer
na Nadia Leihs



MALENGO YA MODULI

- Kuonyesha mbinu tofauti za ushirikiano wa uanahabari pamoja na mifano ya utendaji kazi bora.
- Kuwapatia washiriki maarifa kuhusu kazi ya pamoja na mawasiliano kuhusu tamaduni mbalimbali.
- Kuangazia faida za ushirikiano katika uanahabari, hasa katika kuripoti kuhusu uhamiaji.



MATOKEO YA MAFUNZO

Kufikia mwisho wa moduli hii, washiriki wanapaswa kuwa na uwezo wa:

- Kutambua umuhimu wa kushirikisha mitazamo tofauti katika ripoti zao za habari
→ **Matokeo ya mafunzo kwa stadi za utambuzi: Kuchanganua**
- Kushirikiana na wanahabari kutoka maeneo tofauti ya kijiografia pamoja na umma katika kuandaa makala kuhusu wahamiaji na wakimbizi. → **Matokeo ya mafunzo kwa stadi za mitazamo ya kibinafsi na maadili: Kujibu**
- Kufahamu kinachohitajika ili kuweza kushirikiana na makundi kutoka tamaduni tofauti → **Matokeo ya mafunzo kwa stadi za utambuzi: Kuchanganua**

Muhtasari

Moduli zinazotangulia zimeonyesha kiasi cha data iliyopo kuhusu uhamiaji na uhamishwaji wa kulazimishwa — katika tovuti ya International Organisation of Migration (IOM) — Shirika la Umoja wa Mataifa la Wakimbizi (UNHCR) na Idara ya Shirika la Umoja wa Mataifa la Masuala ya Uchumi na Jamii (UNDESA), miongoni mwa mashirika mengine. Mashirika haya yana data murua inayohusiana na wahamiaji na wakimbizi baina ya nchi na mabara. Data kutoka Benki ya Dunia, Afisi ya Takwimu ya Jamii za Ulaya (EUROSTAT) ama Mixed Migration Monitoring Mechanism Initiative (4Mi), inaweza kusaidia wanahabari kutayarisha taarifa zinazotaja hali ilivyo nje ya nchi na kulinganisha hali katika nchi walikotoka wahamiaji na wakimbizi na wanakoenda. Ni nini hali halisi ya wahamiaji na wakimbizi wanakotoka, wanakopitia na takwimu za kutegemea nchini wanakoenda? Ingawa moduli zinazotangulia zimegusia jinsi data iliyopo inaweza kutumiwa kikamilifu, moduli hii inalenga njia muafaka ya kuwasilisha masimulizi ya kufafanua takwimu hizo. Uanahabari wa ushirikiano huenda ukaimarisha masimulizi yanayohusiana na uhamiaji na uhamishwaji wa lazima, kwa kuunganisha jitihada za wanahabari, kuanzia mwanzo, safarini na nchi wanakoenda wahamiaji na wakimbizi. Katika juhudi za kushirikiana, wanahabari watapata habari zaidi kuliko anavyoweza mwanahabari mmoja. Bila shaka, miradi ya ushirikiano katika uanahabari inahitaji muda na juhudi na hivyo huenda ikatekelezwa, endapo mada inahitaji jitihada hizo. Hata hivyo, makala kuhusiana na taarifa za uhamiaji na uhamishwaji wa lazima inaweza kusimuliwa kutoka pande nyingi.

Huku idadi ya wanahabari wanaoripotia katika nchi za kigeni ikizidi kupungua hata katika vyombo vya habari vya ‘Magharibi’, nazo rasilimali katika vyumba vya habari zikiendelea kunywea,

kiasi kwamba hata haviwezi kuripoti kutoka nchi jirani, miradi ya ushirikiano wa wanahabari huenda ikawa suluhu kwa kuripoti na kuweka taarifa zao katika muktadha unaofaa. Wanahabari kutoka nchi ama mabara huenda wakaungana kuchanganua data kuhusu uhamiaji na kuandaa taarifa. Isitoshe, miradi ya ushirikiano huenda ikajumuisha wahamiaji na wakimbizi na hatimaye, kuhakikisha vyombo vya habari vinawaangazia zaidi.

Ushirikiano wa wanahabari wataalamu

Ushirikiano wa wanahabari na mashirika ya uanahabari umepata umuhimu mkubwa, hasa miongoni mwa vyombo vya habari vinavyojihusisha zaidi na upelelezi. Ushirikiano unawapa fursa ya kuunganisha rasilimali na ujuzi wa kupeleleza masuala muhimu kwa umma, kwa mfano, katika nyanja za siasa, biashara na uhalifu; kwenye ngazi za kitaifa na kimataifa (Alfter, 2016; Sambrook, 2018). Ushirikiano wa uanahabari unahitajika zaidi katika masuala ya mfumo ya hali ya juu wa teknolojia ya fedha ama uhalifu unaofanyika kupitia kwa mtandao (Sambrook, 2018, uk. 95). Pakiwa na data chungu nzima inayohitaji kuchanganuliwa, inabidi wanahabari zaidi washirikiane na kusaidiana (Sambrook, 2018, uk. 94). Mtindo wa uanahabari unaotegemea data unawalazimisha wanahabari kuungana na wastawishaji wa programu za kompiuta, wabunifu na wasomi ili kuchanganua data ipasavyo na kuiwasilisha kwa njia rahisi kwa hadhira zao.

Mtindo huu mpya wa uanahabari umefanikishwa na harakati za kidijitali. Ingawa umewawezesha wanahabari kuwasiliana na kwa urahisi wakiwa afisini na nchi tofauti, na hata kufikia maeneo ya mbali, na kwa gharama ya chini, umesababisha kudidimia kwa hadhira na mapato ya matangazo ya biashara katika vyombo vya habari vya zamani (Pew Research Center, 2014, uk. 2). Hivyo, ushirikiano unakuwa mbinu ya “kutumia vilivyo rasilimali zilizoko” wakati ilikuwa lazima kupunguza mahitaji, wafanyakazi na hadhira wakajifunza kujitafutia habari katika mtandao mara nyingi iwezekanavyo badala kulipia taarifa na burudani. (Stonbely, 2017, uk. 9).

Ijapokuwa mashirika makubwa ya habari huenda yakawa bado na “uzito kirasilimali, maarufu na yana hadhira pana ambazo vyombo vipya vya habari havina”, yameamua kuungana na mashirika mapya, makundi ya wanahabari kwenye mtandao kwa kuibua hoja mpya ambazo huenda zikavutia hadhira changa yenye stadi za kiufundi (Sambrook, 2017). Katika mifano mingine, mashirika makuu ya vyombo vya habari yanashirikiana na washindani wa zamani kubuni teknolojia ya pamoja kama vile mifumo ya kusimamia taarifa, kutathmini hadhira, katika harakati za kukabiliana na hali ngumu ya uchumi. (Collaborative Journalism, 2020a).

Mfano bora wa ushirikiano wa uanahabari baina ya nchi ni mradi wa Panama Papers ulioasisiwa 2016. Ukiongozwa na kundi la wanahabari wapelelezi la International Consortium of Investigative Journalists (ICIJ) na gazeti la Ujerumani la Süd-deutsche Zeitung (SZ), umetokea kuwa mradi mkubwa wa ushirikiano wa wanahabari katika historia. Wanahabari zaidi ya 400 — wakiwemo maripota, wahariri, wastawishaji wa programu za kompiuta na wachunguzi wa usahihi wa taarifa — kutoka nchi takriban 80, wenye ujuzi wa lugha 25 walishiriki katika mradi huo wa Panama

Papers. Walifichua kampuni za kigeni zilizohusishwa na wanasiasa 140 katika nchi zaidi ya 50 (ICIJ, 2017; ICIJ, 2018).

Katika uanahabari wa kushirikiana, wanahabari na vyumba vya habari huupuza ushindani na badala yake, huungana kwa “faida ya mashirika yao, huduma zao na hadhira yao” (Stonbely, 2017, uk. 17). Pia katika Howe na wengine (2017, uk. 2), “kuna mwanzo wa mabadiliko, kutoka kwa sekta ya habari yenye ushindani mkubwa na kuzaa sekta moja inayoelekezwa kutumia kwa pamoja, kushirikiana na uwazi.” Howe na wengine (2017, uk. 3) wanasema kuwa katika mashirika bunifu “ugawaji wa vyumba vya habari vya zamani katika idara kama vile ubunifu, upigaji picha, utafiti, michezo na madarasa” utatwaliwa na hali ya ushirikiano ambao “utakubali makundi yenye vipawa tofauti kujiunda.”

Waanzilishi wa uanahabari wa ushirikiano ni wale waliojijhusisha na wastawishaji wa programu za kompiuta na kanuni za wazi za kufanya kazi pamoja (Howe na wengine, 2017, uk. 2). Hata hivyo, wanahabari bado wanashindana katika uzalishaji wa mawazo bora zaidi na kupata taarifa na huenda wakajipata wamebanwa na waajiri wao siku za usoni.



ZOEZI LILILOPENDEKEZWA LA KUSHUGHULIKIA STADI ZA UTAMBUZI ZA UFAHAMU NA STADI ZA MITAZAMO YA KIBINAFSI NA MAADILI ZA KUJIBU:

Jadili faida na changamoto za miradi ya ushirikiano katika uanahabari. Tumia utaratibu unaofuata kuandaa matokeo ya mjadala

Faida	Vizuizi
Makundi yenye utaalamu mbalimbali hubuni kwa urahisi mipango ya uanahabari.	Mashirika ya vyombo vya habari hayana budi kubuni mazingira ya ushirikiano ili kuwezesha makundi kufanya kazi pamoja.
Kubuni mbinu mpya za kuripoti, kwa mfano, uanahabari wa data, uanahabari simulizi kupitia vyombo vya uanahabari.	Ushirikiano wa nchi na mabara unahitaji kukubaliana kuhusu lugha ya kutumia na kutilia maanani kanda za kijiografia zinazotumia majira yanayofanana.
Kubuniwa kwa mifumo mipya ya biashara.	Makundi yenye ujuzi tofauti yanaweza kutatizwa na filiosofia tofauti za utendaji.
Ushirikiano wa kimataifa unaweza kukinga mradi dhidi ya kuingiliwa na asasi za kitaifa.	Washirika wanaweza kupuuza mikataba, kwa mfano kuchapisha taarifa kabla ya wakati uliokubaliwa, wasilete matokeo, wapuuzwa wakati wa kuwasilisha kazi, waibe taarifa na mengineyo.

Kuimarisha nafasi ya wanahabari binafsi wanapojadiliana na wahariri na mameneja wa vyumba vya habari.	Washirika wote hawawezi kufikia vyanzo vya habari, kwa mfano taarifa rasmi.
Muungano wa wanahabari wenye ujuzi mbalimbali kwa mfano, kuchanganua data nyingi.	Washirika wanaweza kutatizwa na mifumo ya miundo ama uhaba wa fedha.
Kuimarisha hali ya kufikia na kupata habari muafaka.	Mawasiliano ya kidijitali yanaweza kupelelezw.

Kulingana na Koch (2018, uk. 64-77) mashirika yasiyo ya serikali (NGOs) kama vile Transparency International huwa washirika muhimu. Alfter (2018, uk. 42) anasema “makundi yenye ujuzi tofauti kama vile wanahabari na wasomi” yanaweza kuungana katika ushirikiano wa uanahabari. Kulingana na Alfter (2016, uk. 300),

“Wanahabari kutoka **nchi tofauti**....

.... wanashirikiana kutafiti **makala ama mada**.

Wanaweka pamoja, wanakagua tena na kujumuisha matokeo yao ili....

... **kukagua tena na kueleza matokeo hayo kwa hadhira** katika ngazi za kanda, kitaifa ama mashinani.”

Ijapokuwa kuna makubaliano ya jumla kwamba ushindani kimawazo unalemaza ushirikiano wa uanahabari, matokeo yawezayo kuletwa na ushirikiano yanatofautiana pakubwa. Stonbely (2017, uk. 14) anaona wanahabari kufanya kazi pamoja ni “mpango (rasmi au usio rasmi) wa ushirikiano kati ya mashirika mawili au zaidi unaoweza kuwa wa muda, ama uwezao kuendelea, hasa katika kuandaa kazi miongoni mwa washirika walioungana wakiwa katika makundi tofauti, kufanya kazi pamoja ama kwa makundi yaliyochanganyana (Collaborative Journalism, 2020a; Stonbely, 2017, uk. 20-50).¹

1 Tazama pia hati yake ya mashauri mtandaoni (Collaborative Journalism, 2020b).



ZOEZI LILIOPENDEKEZWA LA KUSHUGHULIKIA STADI ZA UTAMBUZI ZA UFAHAMU NA STADI ZA MITAZAMO YA KIBINAFSI NA MAADILI ZA KUKABILI:

Waelekeze washirika kusoma mahojiano ya Tabea Grzeszyk, mwanahabari Mjerumani na mwanzilishi wa shirika la Hostwriter, ambalo linalenga kuwaunganisha wanahabari ili kuwawezesha kubadilishana mada za makala mbali na kuwatafutia washirika kutoka nchi mbalimbali wanahabari wa kushirikiana nao katika uanahabari peleezi. (Hostwriter, 2020).

Waelekeze wanafunzi wako kujadili katika makundi, iwapo Hostwriter ni shirika linalofaa kuwaunganisha wanahabari kutoka kote ulimwenguni na nafasi gani nyingine zilizoko za kuwawezesha kuwasiliana na kuwaunganisha na wanahabari kutoka nchi zingine.

Uanahabari baina ya nchi na kuripoti kuhusu uhamiaji

Maswali matatu kwa Tabea Grzeszyk, mwanahabari mwanzilishi wa Hostwriter

Uanahabari usiojali mipaka una faida gani?

Tabea Grzeszyk : Naamini kwamba wakati fulani siku za usoni, hili swali halitaibuka tena, kwani ni wazi kwamba hatuna budi kushirikiana ili kudadisi mada hizi. Mwanahabari mmoja anawezaje kuripoti mada ya uhamiaji, uhalifu baina ya nchi ama mabadiliko ya anga akiwa pekee yake? Ili kuthibitisha kuwa sisi ni walinzi wa jamii zetu na kujitahidi kufikia kiwango cha uanahabari bora, naamini wanahabari hawana hiari ila kushirikiana na wenzao nje ya nchi. Ukweli ni kuwa tunaishi katika ulimwengu tandazi na mada nyingi za karne ya 21 mara nyingi hazijali mipaka. Sisemi kwamba hakuna mada muhimu za mashinani bali ninamaanisha kuwa hakuna haja ya kuripoti mada zinazohusu nchi nyingine ambazo hazina umuhimu mashinani. Lakini ikiwa mwanahabari anahitaji ujuzi kutoka nchi nyingine, katika lugha ya kigeni, hana budi kutegemea wanahabari wenzake katika nchi nyingine ambao wanaweza kufikia taarifa hizo za mashinani.

Utawashuri nini wanahabari ambao hawajawahi kufanya kazi katika nchi nyingine?

Kwa kawaida mimi hupendekeza kuwa wazungumze na watu ambao wamewahi kufanya kazi ugenini. Kuna wachache ambao wanapatikana kupitia mashirika, kwa mfano, Investigate Europe (Investigate Europe, 2020), Organized Crime and Corruption Reporting Project (2020) ama International Consortium of Investigative Journalists (ICIJ, 2020). Wanachama wa makundi haya ni wastaarabu na hupatikana katika kongamano na huwa tayari kuzungumzia upelelezi wa kimataifa.

Tumebuni Hostwriter kutokana na dhana kwamba uanahabari baina ya nchi usitengewe wanahabari bora zaidi duniani ila ikumbukwe kwamba kila mwanahabari atauhitaji siku za usoni. Kwa hivyo tunajiona kama shirika thabiti na jumuishi ambapo wanahabari wanaweza kuchukua hatua za kwanza. Wanafunzi wa uanahabari pia wanakubaliwa, kwa hivyo, ukiwa hata mwanafunzi, unaweza kujisajili, kutafuta wanahabari wengine na kushiriki katika majadiliano. Tunataka kuhakikisha uanahabari usiojali mipaka ya nchi unapanuka na kushika mizizi, na zaidi, unapatikana na kufikiwa kuwa urahisi — hata kwa watu kutoka maeneo ambayo hayafikiki kwa urahisi, hayana pesa na hayana watu wa kuwasiliana nao. Lengo letu katika Hostwriter ni kuwa na wanachama katika kila nchi duniani. Tayari tuna wanachama katika nchi 150 na tunaamini kuwa, hatimaye tutaunganisha wanahabari kote duniani.

Uaminifu ni hoja muhimu katika ushirikiano wa wanahabari wa nchi tofauti. Uaminifu huchukua muda kujengeka — na ndiposa siwezi kuwahiza kuanza utafiti mkuu wa upelelezi mara moja. Wanaoanza wabuni kundi dogo la kushughulikia mradi usiohitaji viwango vikuu vya uaminifu na usalama — huenda watu kutoka kundi hilo wawaite wenzao watakaojiunga na kundi hilo. Kwanza, wanahabari wajumuishwe katika harakati za muda ambazo zitajenga imani kabla ya kufikiria kuchapisha kazi kubwa. Wajaribu kukutana ana kwa ana wakikumbuka huenda wanahabari wa kimataifa wakakumbana na pingamizi viza, wanapochagua mahala muafaka pa kukutana.

Kwa nini suala la uhamiaji liripotiwe baina ya nchi?

Watu hulazimika kuvuka mipaka ya nchi wakitoroka. Hoja hii pekee yake tayari ni mada ya makala inayohusu 'kuvuka mipaka ya nchi'. Ni muhimu kuripoti kuwa wakimbizi wamewasili, kwa mfano, Ujerumani, lakini kila nchi wanakopitia, kuna matukio ya kuripoti ili hatimaye kupata taswira pana. Ni muhimu kushirikiana na wanahabari kutoka nchi ya asili ya wahamiaji, nchi wanazopitia na nchi ambapo wanahitimishia safari zao. Wananchi wa mashinani wanaelewa kikamilifu hali halisi ya tukio na wanaweza kufukua habari zaidi. Isitoshe, wanahabari katika nchi ambako wahamiaji wanapitia wanaweza kurahisisha taarifa — kwa mfano, kwa kufafanua jinsi mikataba ya biashara ya EU imesukuma watu kuhama nchi zao. Hivyo, Ulaya siyo tu mahala wakimbizi wanaenda bali pia imechangia kwa shida zinazosababisha uhamiaji.

Kushirikiana na umma

Ingawa kufikia sasa hakuna makubaliano katika taaluma ama watafiti wa sayansi ya jamii kuhusu kushirikisha umma katika uanahabari, yaani uanahabari wa umma, baadhi ya wasomi wanashikilia kuwa ushirikiano wa umma ni hatua inayowezekana, na huenda ikawa sehemu ya ushirikiano

wa uanahabari. Kwa mfano, Stonbely (2017, uk. 4) anaona hatua hiyo kuwa “kitengo cha ushirikiano”. Bradshaw (2013, uk. 4) anapendekeza ushirikiano wa uanahabari ni “aina ya mbinu ya kufuatilia habari ambazo zinahusu watu walio nje ya vyumba vya habari” kwa mfano, kutafuta ripoti za habari kwa ushirikiano na umma kupitia kwa mashirika ya kijamii pamoja na jamii za mitandao.

Mipaka ya dhana ya uanahabari wa raia si wazi. Istilahi “uanahabari shirikishi” na “uanahabari wa raia” mara nyingi hutumika kama visawe kueleza taarifa zinazoandaliwa na watu wasio wataalamu wa uanahabari na shughuli za vyombo vya habari. Istilahi nyingine zinazoeleza kuhusu taarifa zinazoandaliwa na umma ni pamoja na raia wanahabari, uanahabari wa makubaliano, vyombo vya habari vya kiraia, uanahabari wa mitandao ya umma, uanahabari wa pamoja na uanahabari wa jamii. Uanahabari shirikishi unarejelea maandalizi ya kitaalamu ya taarifa za habari unaoshirikisha hadhira lengwa. Hili linamaanisha mfumo wa kubuni pamoja taarifa na wahusika wote (raia na wanahabari wataalamu) wakichangia, kwa mfano, taarifa asili ama wakitoa maoni.

Kiasi cha uhusika wa raia katika uanahabari kimeanza kuongezeka, kwa mfano, huenda, kisadfa, wakashuhudia tukio ama kujitwika jukumu la kuandaa taarifa, kupiga picha ama video ili kutangaza tukio hilo. Hata hivyo, taarifa zinazotolewa na wanahabari raia zinafikia umma wakati vyombo vya habari vyenye hadhira kubwa vinapoamua kuzisambaza (Usher, 2016, uk. 248), ingawa hali hii inaonekana kubadilika kwani baadhi ya taarifa zimekuwa zikionekana kwenye mitandao ya jamii. Wanapokumbana na hali tatanishi kama vile shambulio la kigaidi katika maeneo ya miji, majanga ya kawaida ama vita vya wenyewe kwa wenyewe, vyombo vya kawaida vya habari hukazimika kutegemea taarifa zinazotolewa na watu wasio wataalamu. Katika misimu ya siasa za kumalizana, ni muhimu kuchunguza tena taarifa zozote zinazojitokeza mitandaoni ya jamii (Stearns, 2016; Wardle, 2016). Kadhalika, unapotumia taarifa zinazotolewa na wasio wataalamu, kumbuka kuomba idhini, kuwahamasisha raia waliochangia kuhusu viwango vya uanahabari na kuhakikisha usalama wao wa kibinafsi, kisaiokolojia na kidijitali.

Aina ya ushirikiano maalumu na raia unaojumuisha “raia” na “kutafuta” ulipigiwa debe na Howe (2006). Hatua ya kuwagawia raia majukumu madogo inaweza kutumiwa kutekeleza majukumu kadhaa yakiwemo kutambua taarifa na picha ili kuzithibitisha, kuchanganua na kuweka katika vitengo, aina tofauti ya taarifa, video, ama makala yaliyorekodiwa ama kutumia simulizi nafsi na kukusanya data (Aitamurto, 2015; Onuoha na wengine, 2015). Mifano bora kutoka ulimwengu wa uanahabari ni mwito wa gazeti la *The Guardian* kuchunguza stakabadhi zilizogusia matumizi ya pesa za bunge la Uingereza (Rogers, 2009) na pia uchunguzi wa CrowdNewsroom uliotekelezwa na kituo cha uchunguzi cha Correctiv (Correctiv, 2020).

Ushirikiano na wahamiaji na wakimbizi katika kuripoti

Ushirikiano wa uanahabari huweza kusaidia vyumba vya habari kujumuisha masuala pana ya uhamiaji na uhamishwaji wa lazima katika ripoti zao kwa kuungana na makundi ya wanahabari walio ugenini, hadhira ama wahusika wakuu katika habari zinazokusanywa — wahamiaji na

wakimbizi. Mradi wa The Refugee Journalism Project jijini London unahoji kuwa wanahabari wanaporipoti, wanapaswa kufikiria tena kuhusu ripoti wanazotoa kwani “wakimbizi [...] wamekuwa tu watusika baridi wakati masimulizi yanayowahusu yanapoandaliwa” (Abidi, 2018). Mradi huo unawasaidia wakimbizi na wanahabari wakimbizi kuanza upya kazi zao katika Uingereza. Washiriki huandaliwa warsha mbalimbali, wanapewa watu wa kuwashika mikono kitaalamu na kupewa nafasi za uanagenzi. Lengo la mradi ni kuwasaidia wakimbizi wanahabari kufanya kazi ya uanahabari Uingereza, mbali na kuwapa nafasi ya kuchapisha kazi zao na kuwaimarishia ushirikiano. Mfano ni uchunguzi wa makala ya tukio la ongezeko la watu kuhamia tena Syria yaani “Road back to Damascus”, yaliyochapishwa kwa mara ya kwanza kwa Kiarabu na katika the Irish Times (Hayden & Ghandour, 2017). Makala hayo yalitayarishiwa Uingereza na mwanahabari na mpiga picha Mwingereza Sally Hayden ambaye ameshinda tuzo kadhaa za uanahabari anayeangazia uhamiaji, mizozo na matatizo ya kibinadamu. Alishirikiana na Ziad Ghandour, mwanahabari na mtafiti wa shirika la British Broadcasting Cooperation (BBC) mwenye asili ya Kiarabu aliyetoroka Syria 2015 (The Refugee Journalism Project, 2020).

Federico Tarditi, mtaalamu wa kubuni na kushirikisha hadhira katika shirika la habari la Fusion na mmoja wa waandalizi wa mradi wa “19 Million Project” (2015a), anataja uhamiaji kuwa “suala gumu ambalo haliwezi kuandikwa kwa mtazamo mmoja” (amenakiliwa na Gupta, 2017, uk. 6). Washiriki wa miradi hii wanafanya kampeni za kuwapa wahamiaji na wakimbizi sauti wanapoandika taarifa za uhamiaji na uhamishwaji wa lazima. Wanahabari wapatao 150, watawajaji programu za kompiuta, wabunifu na raia kutoka kote duniani walibuni makundi, waka-jadili, wakazungumza na kuwahudumia wahamiaji na wakimbizi na kutayarisha miradi ya ushirikiano wa uanahabari na teknolojia, wakiangazia tatizo lilotajwa kuwa “mzozo wa wakimbizi” wa 2015. Kulingana na taarifa ya azma yao, wanahabari hao wamejitolea kutafuta mbinu muafaka za kuimarisha taarifa zinazogusia tatizo la wakimbizi na kuchunguza jinsi teknolojia za kisasa na mitindo ya kusimulia hadithi kidijitali itaboresha kuripoti na kuchochea dunia kuchukua hatua. Mradi mmoja ambao umeibuka ni “Moving Voices” ambao uliwaunganisha wanahabari na wasimulizi pamoja na wahamiaji na wakimbizi, kuwasaidia kubadilishana mawazo halisi yasiyohaririwa. “Mpango huu umetokana na dhana kwamba huruma huchipuka kutoka kwa hadithi zinazosimuliwa na waliohusika.” (19 Million Project, 2015b).

Kwa mwaka mmoja na nusu, magazeti ya El País (Uhispania), The Guardian (Uingereza), Le Monde (Ufaransa) and Der Spiegel (Ujerumani) yalifuatilia kwa makini jamii za wahamiaji na wakimbizi zilizowasili Ulaya yakijaribu kujua changamoto zao ugenini, hali yao ya kibinadamu, ndoto za kitaalamu na athari zao kwa nchi wenyeji na nchi asili zao. Kulingana na taarifa za vyombo vya habari, mradi huo unafuatilia kwa karibu wahamiaji na wakimbizi, ili kuandika taarifa halisi. (The New Arrivals, 2020).

Katika kilele cha kile kilichodaiwa kuwa “mzozo wa wakimbizi” wa 2015, shirika la uanahabari lisilo la serikali, Internews, lilishirikiana na shirika la kujitolea la Standby Task Force (SBTF) kukusanya na kuchapisha taarifa ambazo lilidhamiria kuwapa sauti wasafiri waliokuwa kwenye eneo Balkan. Internews lilikuwa limegundua kwamba wakimbizi wengi kutoka Uturuki walikosa taarifa muhimu kama vile viwango vya msaada kwa wakimbizi walio Ulaya na mahali pa kupata

misaada hiyo. (Norris, 2016, p. 229). Kwa kuwa SBTF tayari lilikuwa na shirika la wataalamu waliojitolea kukusanya na kuthibitisha data, Internews lilishirikiana na SBTF kukusanya taarifa kutoka kwa umma, ripoti za vyombo vya habari na zilizotayarishwa na raia, intaneti na mitandao ya jamii, katika wiki moja Septemba 2015 (SBTF, 2015). Internews lilichapisha taarifa hizo katika majukwaa tofauti mtandaoni zikiwemo blogu, spreadsheets, ramani na video. Mwezi uliofuata, likitegemea ujuzi lililopata kwa kushirikiana na SBTF, Internews lilianza kuchapisha “News on the Move” ili kutoa taarifa za kuwafaa wahamiaji ama waliotorokea kupitia Ulaya.²



ZOEZI LILIOPENDEKEZWA LA KUSHUGHULIKIA STADI ZA UTAMBUZI ZA UFAHAMU NA STADI ZA MITAZAMO YA KIBINAFSI NA MAADILI ZA KUKUBALI

Chagua mradi mmoja ulioelezwa awali na mkiwa na washiriki wako mchunguze simulizi hizo. Jadili matokeo na faida za mbinu za ushirikiano. Jadili, iwapo miradi ya aina hii inaweza kutekelezwa katika vyumba vya habari katika nchi yako.

Ushirikiano baina ya nchi

Katika miaka ya karibuni, miradi ya ushirikiano wa uanahabari unaovuka mipaka umevutia watu kutokana na wanahabari kupeleleza kwa pamoja taarifa muafaka kati ya nchi mbalimbali, bila kujali tofauti za lugha, mbinu za uanahabari na nia ya kulenga hadhira za kanda, kitaifa na kimataifa (Alfter, 2018). Faida kuu ya wanahabari wa nchini kuungana na wale wa ugenini ni kuwa taarifa hizo zinaweza kufikia hadhira na vyombo tofauti vya habari. Isitoshe, ushirikiano na jamii ya uanahabari wa kimataifa huenda ukawapa wanahabari wanaofanya kazi katika mazingira magumu usalama kiasi. Ili kuweza kushiriki katika makundi ya kimataifa ya uanahabari, stadi za kutangamana baina ya tamaduni tofauti pamoja na uaminifu ni muhimu. (Alfter, 2019, uk. 64-78).

Mfumo wa kutuma na kupokea ujumbe hufanikiwa kiasi katika mawasiliano kati ya jamii mbalimbali, ikiwa pande zote mbili zinaelewa ipasavyo ujumbe [...]. Mara nyingi, mawasiliano bora baina ya tamaduni tofauti yanaweza tu kufanikishwa na utaratibu. Mawasiliano baina ya tamaduni tofauti yanaweza kufanyika ikiwa mmoja yuko tayari kushirikiana na tamaduni geni, yaani kukubali utamaduni huo ni mgeni. Ni muhimu kupata maarifa, ikiwa ni pamoja na lugha, ishara muhimu za kuwasiliana kwa viungo tofauti vya mwili, vipengee vya kipekee vya tamaduni mbali na uwezo wa kuwa na subira ya kuchunguza mbinu mbalimbali za mawasiliano (Broszinsky-Schwabe, 2011, uk. 40)

2 Ukurasa huo umeondolewa mtandaoni lakini kwenye jukwaa la Twitter channel ambapo ukurasa ulipakiwa Oktoba 2015 na kubaki hadi Mei 2017, linatoa mwelekeo kuhusu habari iliyochapishwa: <https://twitter.com/newsthatmoves>.

Kwa jumla, inakubalika kuwa misingi ya mawasiliano baina ya tamaduni ni heshima na subira. Pakiwa na tofauti na kuelewana vibaya, subira ya wahusika itaondoa tofauti hizo. Kadhalika, ni bora kujadili kanuni za masuala kama vile kuhudhuria mikutano bila kuchelewa, mawasiliano, kutokubaliana na mengineyo. Ni vyema kuuliza swali kuhusu mambo usiyoyaelewa badala ya kudhani unaelewa. Pia ni bora kutathmini kwamba wahusika wote “wanakubaliana na sheria” ili kuondoa tofauti. (Commisceo Global, 2016).

Alfter (2019, uk. 49-54) anafafanua viwango vitatu vya ushirikiano kati ya nchi kuwa: ushirikiano wa kiwango cha chini, ushirikiano wenye mipaka na ushirikiano wa karibu.

- Katika ushirikiano wa kiwango cha chini, kuna wanaoshughulikia mada sawia ambao wanahudumia mashirika makuu ya kimataifa ama wanatumia mbinu sawa. Ushirikiano huu unaweza kuonekana kama hauna kanuni na masharti, hali inayorahisisha mambo. Unaweza kuelekeza mtu kwa wanachama zaidi, taarifa ama mada za wanachama, hivyo, huenda ukawa mwanzo wa kubuni kundi la upelelezi baina ya nchi. Washiriki zaidi hupatikana kupitia mikutano ya uanahabari, warsha ama kongamano.
- Katika ushirikiano wenye mipaka, wanachama wa mashirika wanabadilishana taarifa maalumu kuhusiana na mashirika yaliyo ugenini ama ombi, kwa mfano, wakizingatia sheria kuhusu uhuru wa habari za nchi zao. Hawana budi kukumbuka kwamba ushirikiano huu ni wa manufaa kwa pande zote. Mbali na kuwa tayari kutoa habari, ni muhimu kwa wahusika wa pande zote mbili kuhojiana kuhusu tajriba na ujuzi wa mambo wa kila upande. Ushirikiano huu wenye mipaka unaweza kuvunjwa punde tu ubadilishanaji habari ukikamilika.
- Ushirikiano huu wa karibu unajumuisha makundi ya upelelezi yaliyo katika nchi mbalimbali. Muungano huu hurahisisha kazi ambazo mwanahabari mmoja hawezi kutelekeza kibinafsi. Wanachama wote wanaweza kupata taarifa hizo na kuzitumia zinazofaa hadhira zao zilizo nchini ama eneo lao. Katika muktadha huu, uaminifu ni sifa kuu na muhimu. Ni muhimu pia kuzungumza wazi wazi kuhusu mbinu za kufanya kazi na tofauti za kitamaduni. Uaminifu ukiendelea kujengwa, wanahabari wanaoshirikiana kwa karibu wanafahamiana kwa miezi ama miaka. Mara nyingi wanafanya kazi kwa uchunguzi wa miradi midogo na miepesi kwanza kabla ya kuzamia miradi migumu.



KAZI YA ZIADA ILIYOPENDEKEZWA YA KUSHUGHULIKIA STADI ZA UTAMBUZI ZA KUCHANGANUA NA STADI ZA MITAZAMO YA KIBINAFSI NA MAADILI ZA KUKUBALI:

- 1) Waelekeze washiriki kutumia kipindi cha “mafunzo kwenye mtandao” kuhusu “utekelezaji wa mradi wa ushirikiano — mawasiliano baina ya tamaduni tofauti” uliobuniwa na EU chini ya mradi wa stadi mpya kwa kizazi kijacho cha wanahabari (NEWSREEL), ili kujiandaa kwa majadiliano yanayohusu stadi za tamaduni tofauti.

2) Waelekeze washiriki kutumia kipindi cha mafunzo kwenye mtandao kuhusu “Kuandaa Mradi wa Ushirikiano” uliobuniwa na mradi wa EU (NEWSREEL) kutayarisha mradi kwa mhariri ama kwa shirika la kutoa misaada na uwelekeze kuuwasilisha darasani na kupata majibu ya wenzao.

Unaweza kupata vipindi hivyo viwili hapa: https://newsreel.pt.e.hu/e_learning/collaborative_journalism



USOMAJI WA ZIADA:

Kiakademia:

Heft, A. (2020). Conditions to strengthen future cross-border journalism. Weizenbaum Series #5 Short Paper. Berlin: Weizenbaum Institute for the Networked Society – The German Internet Institute. Retrieved December 11, 2020, from https://www.weizenbaum-institut.de/media/Publikationen/Weizenbaum_Series/Weizenbaum_Series_5_Heft_080420.pdf

Kiuanahabari:

Alfter, B. (2019). Cross-border collaborative journalism: a step-by-step guide. London: Routledge. Retrieved December 11, 2020, from <https://lostineurope.org/>

Kitaasisi:

Hostwriter. (2018). Cross-border journalism as a mindset. Retrieved December 11, 2020, from <https://blog.hostwriter.org/wp-content/uploads/2018/12/crossborder-journalism-mindset-final.pdf>

n-ost. (2020). Cross-border playbook. A compilation of projects, tips and experiences. Retrieved December 11, 2020, from <https://playbook.n-ost.org/>

Marejeleo

- Abidi, A. (2018). Rethinking our reporting of the refugee crisis: How collaborative journalism can improve how we cover migration. Retrieved November 26, 2020, from <https://magazine.journalismfestival.com/rethinking-our-reporting-of-the-refugee-crisis-how-collaborative-journalism-can-improve-how-we-cover-migration/>
- Aitamurto, T. (2015). Crowdsourcing as a knowledge-search method in digital journalism. *Digital Journalism*, 4(2), 280-297. <https://doi.org/10.1080/21670811.2015.1034807>
- Alfter, B. (2016). Cross-border collaborative journalism: Why journalists and scholars should talk about an emerging method. *Journal of Applied Journalism & Media Studies*, 5(2), 297-311. https://doi.org/10.1386/ajms.5.2.297_1
- Alfter, B. (2018). New method, new skill, new position? Editorial coordinators in cross-border collaborative teams. In Sambrook, R. (Ed.), *Global teamwork: The rise of collaboration in investigative journalism* (pp. 41-58). Oxford: Reuters Institute. Retrieved November 26, 2020, from https://reutersinstitute.politics.ox.ac.uk/sites/default/files/2018-03/sambrook_e-ISBN_1802.pdf
- Alfter, B. (2019). *Cross-border collaborative journalism: A step-by-step guide*. London: Routledge.
- Bradshaw, P. (2013). Stories and streams: Teaching collaborative journalism with peer to peer learning. Retrieved November 26, 2020, from <https://onlinejournalismblog.com/2013/01/15/free-ebook-on-teaching-collaborative-journalism-and-peer-to-peer-learning/>
- Broszinsky-Schwabe, E. (2011). *Interkulturelle Kommunikation: Missverständnisse – Verständigung*. Wiesbaden: VS Verlag für Sozialwissenschaften.
- Collaborative Journalism. (2020a). What is collaborative journalism? Retrieved November 26, 2020, from <https://collaborativejournalism.org/what-is-collaborative-journalism/>
- Collaborative Journalism. (2020b). Best practices and guides. Retrieved November 26, 2020, from <https://collaborativejournalism.org/guides/>
- Commisceo Global. (2016). Intercultural communication tips. Retrieved November 26, 2020, from <https://www.commisceo-global.com/blog/intercultural-communication-tips>
- Correctiv. (2020). CrowdNewsroom. Retrieved November 26, 2020, from <https://correctiv.org/en/crowdnewsroom/>
- Gupta, A. (2017). Bringing collaborative journalism to the issue of international migration: An interview about the 19 million hackathon. *Media Fields Journal* 12/2007, 1-19. Retrieved November 26, 2020, from <http://static1.1.sqspcdn.com/static/f/707453/27402858/1483737599450/Gupta.pdf?token=dz6Kwt8D0ahp%2Fc1XHwJ%2BPpR9TKw%3D>
- Hayden, S., & Ghandour, Z. (2017). Road to Damascus: the Syrian refugees who want to go home. Retrieved November 26, 2020, from <https://www.irishtimes.com/news/world/middle-east/road-to-damascus-the-syrian-refugees-who-want-to-go-home-1.3309941>
- Hostwriter. (2020). About Hostwriter. Retrieved November 26, 2020, from <https://hostwriter.org/about>
- Howe, J. (2006). *Crowdsourcing: The book*. Retrieved November 26, 2020, from: https://crowdsourcing.typepad.com/cs/2007/01/crowdsourcing_t.html
- Howe, J., Bajak, A., Kraft, D., & Wihbey, J. (2017). Collaborative, open, mobile: A thematic exploration of best practices at the forefront of digital journalism. Northeastern University School of Journalism Working Paper. Retrieved November 26, 2020, from <http://www.storybench.org/docs/collaborative-open-mobile-whitepaper.pdf>
- ICIJ. (2017). Panama Papers wins Pulitzer Prize. Retrieved November 26, 2020, from <https://www.icij.org/blog/2017/04/panama-papers-wins-pulitzer-prize/>

ICIJ. (2018). The Panama Papers: Exposing the rogue offshore finance. Retrieved November 26, 2020, from <https://www.icij.org/investigations/panama-papers/>

ICIJ. (2020). About. Retrieved November 26, 2020, from <https://www.icij.org/about/>

Investigate Europe. (2020). Europäische Recherchen. Retrieved November 26, 2020, from <https://www.investigate-europe.eu/en>

Koch, A. (2018): Investigative journalism and advocacy: Natural allies? In Sambrook, R. (Ed.), *Global teamwork: The rise of collaboration in investigative journalism* (pp. 64-77). Oxford: Reuters Institute. Retrieved November 26, 2020, from https://reutersinstitute.politics.ox.ac.uk/sites/default/files/2018-03/sambrook_e-ISBN_1802.pdf

Norris, W. (2016). Digital humanitarians. *Journalism Practice*, 11(2-3), 213-228. <https://doi.org/10.1080/17512786.2016.1228471>

Onuoha, M., Pinder, J., & Schaffer, J. (2015). Guide to crowdsourcing. Retrieved November 26, 2020, from https://www.cjr.org/tow_center_reports/guide_to_crowdsourcing.php#crowdsourcing-in-newsrooms

Pew Research Center. (2014). Journalism partnerships: A new era of interest. Pew Research Center Report. Retrieved November 26, 2020, from https://www.pewresearch.org/wp-content/uploads/sites/8/2014/12/PJ_Journalism_Partnerships_120414.pdf

Rogers, S. (2009). How to crowdsource MPs' expenses. Retrieved November 26, 2020, from <https://www.theguardian.com/news/datablog/2009/jun/18/mps-expenses-houseofcommons>

Sambrook, R. (2017). Paradise papers yet another example of the power of collaboration in investigative journalism. *The Conversation*. Retrieved November 26, 2020, from <http://theconversation.com/paradise-papers-yet-another-example-of-the-power-of-collaboration-in-investigative-journalism-87376>

Sambrook, R. (Ed.) (2018). *Global teamwork: The rise of collaboration in investigative journalism*, Oxford: Reuters Institute. Retrieved November 26, 2020, from https://reutersinstitute.politics.ox.ac.uk/sites/default/files/2018-03/sambrook_e-ISBN_1802.pdf

SBTF. (2015). Online European refugee response assessment – Humanitarian data exchange. Retrieved November 26, 2020, from <https://data.humdata.org/dataset/european-mediterranean-refugee-response>

Stearns, J. (2016). Lessons from the New York Times super tuesday hoax: Five ways to spot fake news. Retrieved November 26, 2020, from <https://firstdraftnews.org/latest/lessons-from-the-new-york-times-super-tuesday-hoax-five-ways-to-spot-fake-news-bernie-sanders-elizabeth-warren/>

Stonbely, S. (2017). Comparing models of collaborative journalism. Montclair State University Working Paper. Retrieved November 26, 2020, from <https://collaborativejournalism.org/wp-content/uploads/sites/8/2017/09/Models-for-Collaborative-Journalism-research-paper.pdf>

The New Arrivals. (2020). About. Retrieved November 26, 2020, from <https://thenewarrivals.eu/index.html>

Organized Crime and Corruption Reporting Project. (2020). About. Retrieved November 26, 2020, from <https://www.occrp.org/en/about-us>

The Refugee Journalism Project. (2020). About us. Retrieved November 26, 2020, from <https://www.refugee-journalismproject.org/about-us-2/>

Usher, N. (2016). The appropriation/amplification model of citizen journalism: An account of structural limitations and the political economy of participatory content creation. *Journalism Practice*, 11(2-3), 247-265. <https://doi.org/10.1080/17512786.2016.1223552>

Wardle, C. (2016). 6 types of misinformation circulated this election season. Columbia Journalism Review Website. Retrieved November 26, 2020, from https://www.cjr.org/tow_center/6_types_election_fake_news.php

19 Million Project. (2015a). About. Retrieved November 26, 2020, from <http://the19millionproject.com/>

19 Million Project. (2015b). Check out the final projects. Retrieved November 26, 2020, from <http://the19millionproject.com/2015/12/18/check-out-the-final-projects-19-million-project-hackathon-launches-13-innovative-storytelling-and-technology-projects-to-address-the-european-migration-crisis/>



MODULI 13

Kuboresha taathira: Mikakati ya uanahabari na masoko ya habari

na Anna-Carina Zappe
na Gordon Wüllner-Adomako



MALENGO YA MODULI

- Kuthibitisha hadhira ya habari kuhusu uhamiaji na uhamishwaji wa kulazimishwa ni nani.
- Kuwahami washiriki na mikakati ya uhamasishaji wa mada za masuala yanayohusiana na uhamiaji.
- Kuwahimiza washiriki kufikiri kivumbuzi wakiripoti kuhusu uhamiaji na ukimbizi.



MATOKEO YA MAFUNZO

Kufikia mwisho wa moduli hii, washiriki wanapaswa kuwa na uwezo wa:

- Kueleza jinsi wanahabari wanaweza kuimarisha taathira ya habari za wahamiaji na wakimbizi. → **Matokeo ya mafunzo kwa stadi za mitazamo ya kibinafsi na maadili: Kujibu**
- Kukumbuka mikondo ya utumizi wa vyombo vya habari. → **Matokeo ya mafunzo kwa stadi za utambuzi: Kukumbuka**
- Kutumia mikakati (kwa mfano modeli ya SOI) kwa lengo la kuhakikisha habari za uhamiaji zinaifaa hadhira. → **Matokeo ya mafunzo kwa stadi za utambuzi: Kutumia**
- Kudhihirisha stadi za 'kuuza' habari kuhusu uhamiaji. → **Matokeo ya mafunzo kwa stadi za utambuzi: Kutumia**

Muhtasari

Akiwazungumzia mamilioni ya watu wanaotoroka vita vya wenyewe kwa wenyewe katika Syria, mwanadiplomasia Jan Egeland kutoka Norway ambaye pia ni mtaalamu wa masuala ya siasa, kiongozi wa shughuli za ufadhili na mwanasiasa wa zamani, aliaridhia kwamba: “vyombo vya habari, isipokuwa vichache tambulika, vimelipatia kisogo suala hili na imedhihirika wazi vituo vingi vya redio na televisheni na magazeti yenye wasomaji wengi havina haja” (Egeland, 2015, uk. 1).

Yasikitisha kupata kwamba ripoti za uchunguzi wa kina (tazama Moduli 10) na zinazoakisi kiiitikeli (tazama Moduli 11) wakimbizi na wahamiaji¹, mara nyingia hazifikii hadhira kubwa. Ukiangalia kinyume chake, ripoti zinazokwepa kashfa, urahihisaji na changamano mara nyingi hupeuzwa kabisa na hadhira. Ukweli ni kwamba sehemu kubwa ya matukio ya habari wahamiaji na wakimbizi hutokea mbali na maeneo yanayofikiwa na vyombo vya habari. Aidan White katika ripoti yake Moving Stories. International Review of How Media Cover Migration, iliyochapishwa na Ethical Journalism Network, ameorodhesha baadhi ya hizo simulizi ambazo mara nyingi hupeua kisogo na vyombo vya habari (White, 2015). Egeland anahoji kwamba mara nyingi habari hizo hukosa nafasi inayostahili kwa sababu “hakuna mpiga picha au mwanahabari karibuni

1 Kwa maelezo kuhusu mhamiaji, mkimbizi na istalahi nyingine muhimu, kagua faharasa iliyopendekezwa katika Moduli 2 (European Migration Network, 2018; IOM, 2019; UNHCR, n. d.).


zinapotokea nyanjani kusimulia habari hizo” (Egeland, 2015, uk. 1); sababu za kutokuwepo kwa wanahabari zimeakisiwa katika Moduli 5. Hata hivyo, kuna sababu nyingine nyingi mbali na wanahabari kutokuwepo katika maeneo ya matukio, ambazo zitajadiliwa katika moduli hii. Wanahabari wanafahamu jinsi hadhira zao hutumia habari za vyombo vya, kiasi kwamba wanafahamu kundi lengwa wawezalo kulifikia au makundi lengwa hayo hupatikana wapi. Isitoshe, wanahabari hulazimika kujaribu kushawishi vyombo vya kutoa habari na wahariri ambao huenda wasiamini simulizi za maandishi hao, ilhali kila habari inahitaji hadhira. Changanuzi za kifani katika vyumba vya habari vya mtandao vya Ugiriki ulionyesha kwamba hadhira haikujali habari kuhusu wakimbizi zilizochapishwa 2015, navyo vyombo vya habari pia havikutumia mbinu mpya za kuvutia hadhira (Panagopoulos, 2019). Wasomaji, watazamaji na wasikilizaji wakipuuza habari zinazotolewa na vyombo vya habari, ni wasaa muafaka wa kufikiria mikakati mipya na kutafuta mbinu za kiuvumbuzi.

“Uanahabari unaotia fora haufai tu kuwa asilia [kuisitiza uasilia] kimaudhui (habari za hivi punde ama kutoa vipengele vya kipekee vya habari) lakini unapaswa kuwa vumbuzi na kuvutia kwa tekniki zilizotumika kwa usimulizi huo” (Shapiro na wengine, 2006, uk. 431).

Kwa kweli wanahabari wanahitaji kuwa wavumbuzi wanapotoa habari kuhusu uhamiaji na uhamishwaji wa lazima, na pia ‘wanapoziua’. Mbali na kutoa habari muhimu kuhusu hadhira na jinsi ya kueleza habari za uhamiaji kuwa muhimu kwa hadhira na wahariri, moduli hii inatoa ripoti zilizofana na za kivumbuzi kuhusu wahamiaji na wakimbizi za kuwatia moyo washiriki katika kozi hii.

Aida Alami na Salaheddine Lemaizi, wanahabari wanaoripotia Morocco

“Uanahabari kuhusu uhamiaji ni fursa inayomhitaji mtu kuwa mvumbuzi, sio tu kati-ka maudhui lakini pia muundo. Hatuwezi tena kuendelea kusimulia habari za uhamiaji kama tulivyozoea miaka nenda miaka rudi. Umma umechoshwa na masimulizi ya dhiki na mateso ya wahamiaji. Wahamiaji nao pia wanataka habari. Kutimiza hilo, tunahitaji mtindo mpya wa uanahabari, uanahabari wa data, na uthibitishaji wa habari, ziwe makala ndefu au fupi, zote zitaongezwa.”



Chanzo : Binafsi

Matumizi ya vyombo vya habari katika Afrika na Ulaya

Kabla ya kuipatia hadhira habari za wahamiaji na wakimbizi, wanahabari wanapaswa kujibu bayana maswali yafuatayo: Hadhira yao ni gani? Hadhira kwa jumla ni watu mbali mbali katika nchi asili na nchi wenyeji. Hawa ni pamoja na watu binafsi wanaonua kuihama nchi yao, watu binafsi ambao familia zao zimetoroka ama kuhama, na pia wakazi wa mataifa wenyeji ambapo wahamiaji na wakimbizi wameingia. Uchunguzi wa matumizi ya vyombo vya habari unaonyesha jinsi baadhi ya vyombo vya habari ni muhimu kwa baadhi ya makundi na kwa nini ni muhimu kwa wanahabari kufikia watu kupitia kwa vyombo hivyo. La muhimu pia ni hadhira zinazoshawishi ama kujibu maoni ya umma na sera za umma. Ndiposa habari hazifai tu kulenga umma kwa jumla lakini pia viongozi wenye ushawishi mkubwa kwa umma na wanaotunga sera katika bunge na serikalini.

Ingawa Afrika ina mazingira pana yaliyo na vyombo vingi tofauti vya habari (Paterson, 2013, uk. 80), watumiaji wa vyombo hivyo katika bara hilo kwa jumla wamegawanyika kati ya “walio navyo” na “wasio navyo”: wakazi wa maeneo ya miji wanafikia vyombo mbali mbali wawezavyo kuchagua kutumia vya kianalogi na kidijitali (walio navyo) ilhali wenzao mashambani hawana vyombo vya habari vya kidijitali na hata vya kianalogi kama vile redio na televisheni ni vichache (Balancing Act, 2014, uk. 5). Afrika inatajwa kuwa bara la redio (Bergstresser, 2009, uk. 4), kwani kati ya asilimia 70 na 80 ya watu wake wana redio. Tangu milenia mpya ilipoanza, idadi ya vituo binafsi vya redio na pia vya mashirika yasiyo ya biashara na pia redio za jamii imeongezeka kwa kiasi kikubwa, kwa kiwango fulani kwa sababau ya “kiu ya vyombo vya habari mbadala wa vinavyo-milikiwa na serikali” (Myers, 2008, uk. 12). Redio za jamii ni muhimu kwa “wasio navyo” kwa kufikia na kutangaza katika sehemu za mashambani (Paterson, 2013, uk. 81). Ingawa hali hii ya kutokuwa sawa katika kufikia habari ni dhahiri, Wangari (2017) anahoji kuwa kwa kizazi cha milenia katika Afrika “zaidi ya asilimia 60 kati yao hutumia mitandao ya jamii kama asilia ya msingi ya habari”. Facebook hasa “imekua kiasi cha kuwa jukwaa la mtandao wa jamii linalotumiwa zaidi na watu karibu milioni 20 katika Nigeria na Kenya pekee” (The Nielsen Company, 2015, uk. 22). Kadhalika, mara nyingi maafisa wa AU hutumia mitandao ya jamii na intaneti kama asilia zao za msingi za kupata habari (Bronsther na wengine, 2016, uk. 15).

Vivyo hivyo katika Ulaya, “Intaneti na mitandao ya jamii ndivyo vyombo vya habari vinavyotumiwa na raia wengi wa Ulaya” (European Commission, 2017). Ripoti nyingine ya Tume ya EU iliyotolewa 2019 inathibitisha kwamba utumiaji wa vyombo vya kidijitali unazidi kuongezeka: asilimia 80 hutumia intaneti angalau mara moja kwa wiki, ongezeko la pointi mbili za asilimia tangu majira ya kupatikana majani ya 2018 (European Commission, 2019). Lakini katika nchi nyingi za Ulaya: “ukuaji wa matumizi ya mitandao ya jamii kupata habari [...] umekoma au kuanza kupungua” (Newman na wengine, 2018a, uk. 10). Tukichukua kwa mfano Uingereza, utumiaji uliongezeka kutoka asilimia 20 (2013) hadi 41 (2017) kabla ya kushuka hadi asilimia 39 mnamo 2018. Kama ilivyoelezwa katika Reuters Institute Digital News Report 2018, ambayo inaonyesha data kutoka nchi 24 za Ulaya, mabadiliko ya alogarithimu kuzipatia kipaumbele habari za binafsi kuliko taarifa za habari zilizokuwa zikitolewa na Facebook mnamo 2018 yame-

sababisha hali hiyo mpya (Newman na wengine, 2018a, uk. 11). Hata hivyo, bado pana nafasi nzuri ya usambazaji kupitia mitandao ya jamii – hali ambayo imechangia pakubwa kuibuka kwa tovuti badili zinazojali fikra za umma au hata kuegemea upande mmoja (Newman na wengine, 2018a, uk. 20). Sifa nyingine za utumiaji wa habari za mitandao ya kidijitali katika Ulaya ni pamoja na idadi kubwa ya vijana walio na umri wa chini ya miaka 25 wanaotumia mitandao ya jamii kama lango la kupata habari (Newman na wengine, 2018a, uk. 15), umuhimu wa simu smati kama chombo cha matumizi ya mitandao ya jamii na umaarufu wa maudhui za video za mtandaoni (Newman na wengine, 2018a, uk. 27). Katika Uingereza, yaonekana usomaji wa magazeti ulioanza kupunguka muda mrefu uliopita umekwamia asilimia 26 ya wanaodai kusoma magazeti kila siku au karibu kila siku. Hata hivyo, kiwango cha umuhimu wake kiko chini kikilinganishwa na asilimia 80 wanaotazama televisheni (televisheni zinazopokea ishara za matangazo kwa transmita na za kidijitali) na asilimia 47 wanaosikiliza redio (European Commission, 2019). “Usikilizaji [...] umeanza kupata mvuto mpya kutoka kwa wachapishaji kufuatia ongezeko la idadi ya watu wanaotumia simu zao kwa jambo hilo na pia kutokana na mahitaji ya teknolojia inayotumika kwenye magari ya vielekezo vya kusikizia ambavyo vimevuruga usikilizaji wa redio” (Newman na wengine, 2018b, uk. 54). Matokeo yake yamekuwa ni soko jipya la podcasti, ambazo zimeendelea kupata umaarufu katika nchi nyingi za Ulaya (Newman na wengine, 2018b, uk. 54). Bila shaka, tukiangalia idadi ya watumiaji, hatufai kusahau kwamba magazeti hata mitandaoni yanatekeleza wajibu muhimu wa ushawishi wa kujenga hoja kwa, hasa kwa raia, viongozi wenye ushawishi na watungaji sera.

Jinsi wahamiaji na wakimbizi hutumia vyombo vya habari

Kwa mujibu wa mwauo wa wahamiaji na wakimbizi Waafrika katika Ujerumani kwenye mjadala wa jopo, (Zappe na wengine, 2020), washiriki walisema walipata kiasi kidogo tu cha habari kuhusu uhamiaji na uhamishwaji wa lazima katika vyombo vya habari vya nyumbani. Walipata habari zilizowahimiza kuamua kuhama kutokana na mazungumzo ya moja kwa moja na watu wengine, habari ambazo mara nyingi zilitiliwa nguvu na taswira chanya kutoka Ulaya walizopata katika mitandao ya jamii. Kulingana na uchunguzi huo, habari kutoka kwa tovuti za umma — zikilinganishwa na mawasiliano ya kiasili — hazikuteteleza wajibu mkubwa kwa wahamiaji katika nchi zao za asili. Mawasiliano ya moja kwa moja — kama vile mawasiliano kupitia kwa mitandao ya jamii ni muhimu kwa wahamiaji Waafrika (Fiedler, 2017). Tafiti nyingine zimedhihirisha umuhimu wa mawasiliano ya simu na mitandao ya jamii kwa wakimbizi. Wakimbizi tisa kati ya 10 katika utafiti mmoja walitumia Facebook (UNHCR, 2016, uk. 17), na kwa wengi wao kuweza kuwasiliana kwa simu za mkono ni muhimu hata kuliko elimu, mavazi na huduma za afya (UNHCR, 2016, uk. 19). Utafiti uliofanyika kambini mbili za Uganda (Nakivale na Kakuma) ulionyesha kuwa ni asilimia ndogo tu ya wakimbizi (chini ya asilimia 20) ambao hawana simu za mkono.

Kwa mujibu wa uchunguzi mwingine: “Facebook, WhatsApp na Google hutoa majukwaa mengi zaidi ya mawasiliano yanayotumiwa na wakimbizi na mara nyingi yalitajwa kuwa njia za mawasiliano za kuaminika, huku yakichangia kiasi cha karibu asilimia 40 ya shughuli za intaneti”

(Hounsell & Owuor, 2018, uk. 31). Kadhalika, WhatsApp, Facebook, Viber au Telegram — utafiti uliofanyika Ujerumani — ni muhimu kwa wakimbizi kutoka Syria, Iraq na Asia ya Kati. Upen-deleo wa mtandao wowote wa jamii unategemea taifa asili. Utafiti unadokeza kwamba habari za televisheni na intaneti haziaminiki (Emmer na wengine, 2016, uk. 9). Hilo ni dhihirisho kwamba mitandao ya jamii “ni asili ya lazima ya habari kwa wakimbizi wa siku hizi” (Dekker na wengine, 2018, uk. 9), ingawa habari nyingi ambazo hazijathibitishwa na hata uvumi huenezwa kwa mi-tandao kuu ya jamii. Wanahabari wanaweza kutimiza jukumu muhimu kwa kukabiliana na habari za uongo na za kupotosha zinazotolewa makusudi. Majukwaa kama Infomigrants.net, ambalo ni ushirikiano wa shirika la kimataifa la utangazaji la Ujerumani DW, EU na vyombo vingine vya habari vya Ulaya, yanaweza kuwa mfano mwema.



ZOEZI LILILOPENDEKEZWA LA KUSHUGHULIKIA STADI ZA UTAMBUZI ZA KUKUMBUKA:

Tekeleza kipengele cha habari darasani kwa kutumia maandiko na vyanzo vilivyotajwa hapo awali na uandae mhadhara mfupi wa dakika 10 kuhusu hadhira na matumizi yao ya vyombo vya habari. Unaweza kutilia mkazo nchi yako au vyombo teule vya habari, uupanue uwasilishaji wako kwa kuzingatia vipengele vinavyalifaa eneo lako na uwape wanafunzi jaribio la maswali ya kuchemsha bongo.

Wapatie washiriki vifaa vya ziada na nafasi ya kuigiza watumiaji tofauti wa vyombo vya habari wakijadiliana kuhusu vyombo vya habari wapendavyo kuvitumia.

Hadhira na maslahi ya vyombo vya habari

Kama ilivyotajwa katika Moduli 10, hadhira husoma, husikiliza na hutazama habari muhimu kwao katika maeneo yao na ngazi za kitaifa na kimataifa (Schrøder, 2019). Umuhimu hulingana na hadhira kama anavyosisitiza Lee (2010) katika utafiti wake: Upokeaji wa habari unaweza kushawishiwa na habari, burudani, mawazo au jamii. Watu wa aina zote wana sababu zina-zowasukuma kutafuta habari (Lee, 2010)². Isitoshe, la muhimu zaidi kwa hadhira si lazima liwe muhimu pia kwa wahariri. Kwa mfano uchanganuzi mmoja wa chaguo la habari la waha-riri wakilinganishwa na hadhira na utumiaji wa habari mtandaoni ulibainisha kwamba ingawa vyombo vya habari hupenda kuchagua kutoa habari nzito (kwa mfano mada za siasa, hazina na biashara), hadhira zao hupendelea habari zisizo nzito (kwa mfano hadithi za maisha na burudani na zinazoangazia ubinadamu) (Chakraborty na wengine, 2019). Utafiti mwingine uliolinganisha

2 Pana aina nyingi za uainishi, utofautishaji na matokeo ya utafiti wa yanayovutia hadhira na pia matakwa yao, ambayo huenda washiriki wanaifahamu kutokana na kozi nyingine walizosomea. Mifano miwili ni: The Digital News Report from Newman na wengine, (2019) na uainishi wa Schrøder & Kobbernagel (2010).

chaguo la mada kati ya watumiaji na wanahabari ulionyesha kuwa wanahabari wanapendelea zaidi masuala ya kisiasa kuliko hadhira yao pana. Ingawa hadhira ya intaneti kwa jumla haivutiwi sana na siasa na hupendelea mada za huduma, wanahabari huyapatia kisogo masuala ya huduma (Wendelin na wengine, 2017). Lakini uchanganuzi wa kuripoti kuhusu wahamiaji na wakimbizi umebaini kwamba wanahabari huangazia zaidi siasa (tazama Moduli 4). Ndiposa, imedhihirika wazi kwamba ni nadra kwa ripoti kuhusu wahamiaji kuwa za kuvutia kila mara na kuwa na manufaa kwa mtazamo mpana wa umma (Panagopoulos, 2018). Taarifa za wanahabari Lydia Ouma Radoli, Ulriikka Myöhänen na Cécile Debarge, ambao wameripoti kwa muda mrefu kuhusu masuala ya wahamiaji na wakimbizi, zinaonyesha wanapendekeza habari za ubinadamu zipewe nafasi zaidi kuliko kutilia mkazo habari za siasa. Wakati huo huo, pana haja ya kuepuka mtazamo wa jumla kuhusu nyakati na mahali kwa sababu mitazamo ya kisiasa inayohusu uhamiaji inaweza kuvutia hadhira tofauti na kubwa.

Bila shaka, haina maana kwamba masuala yote kuhusu wahamiaji na wakimbizi si ya kuvutia hadhira kubwa mno: Kwa mfano, ripoti kuhusu janga la Alan Shenu (ambaye mara nyingi huitwa “Aylan Kurdi” kwenye ripoti za vyombo vya habari), iliyojadiliwa katika Moduli 5, imegusa hisia za vyombo vya habari na hadhira. Watu walivutiwa na mada hiyo ambayo awali haikuwa tukio la kisiasa. Masuala ya uhamiaji yanaweza kuvutia hadhira kubwa wakati vyombo vya habari vinasimulia habari kuhusu meli za magendo kutoka Libya na kupitia Mediterranean, kuhusu hali katika Calais, ambapo polisi wa Ufaransa na Uingereza walikumbana na wahamiaji wasio wa kawaida wakijaribu kuvuka The Channel, kuhusu meli zikivuka kutoka Uturuki hadi Ugiriki au “matukio ya watu wakipitia katika nchi za Balkan” (Trilling, 2019).

Hata hivyo, mifano kutoka Ulaya iliyotajwa hapa inaangazia zaidi upeo wa majanga na misimu ya kampeni za uchaguzi. Uhamiaji ulipewa nafasi kubwa katika habari za siasa za shirika la utangazaji la umma la Ujerumani wakati wa kampeni za uchaguzi wa 2017 (Liesching & Hooffacker, 2019). Hata hivyo msisitizo huo wa siasa huenda usivutie hadhira kubwa (mtandaoni) kila mara. Kwa hivyo, wanahabari wanakabiliwa na kibarua tatanishi: Ulimwenguni, wanalazimika kufanya kazi na wahariri wasio tayari kutoa habari za uhamiaji zisizo na mtazamo wa kisiasa — hasa katika nchi za Afrika ambapo mada hiyo haijashamiri katika ajenda ya vyombo vikuu vya habari, kama ilivyoonyeshwa katika Moduli 4. Kashfa na habari ziliorahisishwa huenda zikapata mauzo mengi na wasomaji, wasikilizaji na watazamaji wengi kuliko habari zinazosisitiza taarifa za kweli na ripoti zenye usuli changamani ambazo ni ghali kutoa kwa kampuni za habari. Hali hii inatoa changamoto kubwa kwa wanahabari wakitafuta njia za kufikia hadhira yao pana.

Chaguo moja ni kusimulia vipengele vya misiba katika simulizi kwa kupanua mada za kutilia mkazo. Jukumu la ripoti za habari za kujenga na zinazohimiza maoni ya kusaidia tayari limeshughulikiwa katika Moduli 10 na, kulingana na mwanahabari Will Vassilopoulos wa AFP, linavutia hadhira.

Dkt Lydia Ouma Radoli, Mtangazaji Mkenya na mtafiti wa vyombo vya habari




Chanzo : Binafsi

“Ningependekeza kwamba msisitizo wa suala la wahamiaji uwe kwa watu kwa kuangazia zaidi wanayokumbana nayo katika maisha, mata-tizo, mafanikio. Mambo hayo yanafaa kutiliwa mkazo na wanahabari wanapotaribu ‘kuzuza’ habari zao ili uhamiaji usiwe tu ni takwimu au vidokezi vya dhiki kwa nchi za Kaskazini. Wanahabari waonyeshe **sura za wanaohusishwa na tarakimu hizo**. Kadhalika, wanahabari wanahitaji kusaili mawazo yaliyopo ambayo hayajahakikishwa, na dhana potovu zisizo na uasilia zilizo katika muundo-jamii kuhusu uhamiaji.”

Ulriikka Myöhänen, mwanahabari wa Finland anayechangia majukwaa tofauti ya habari

“Ushauri wangu bora zaidi kwa wanahabari wenzangu ni kwamba wa-tafute **mhusika mkuu thabiti** wa kila habari. Hiyo ina maana kwamba unahitaji kufahamu wale unaoripoti kuwahuu na ujaribu kutafuta jambo linalorahishia jamii **kujihusisha** na mhusika huyo.”



Chanzo : Binafsi

Cécile Debarge, journaliste indépendante basée en Italie.



Chanzo : Binafsi

“Si rahisi kamwe kuzuza **habari za wahamiaji na wakimbizi kwa mtindo usio wa kawaida**, nje ya muktadha wa migogoro na matatizo mengine kwa sababu mara nyingi inachukuliwa kwamba hali hiyo ni matokeo ya mgogoro au upeo wa matatizo. Uhamiaji unaweza kuwa ni zaidi ya kawaida hiyo. Kwa mfano, habari nyingi hutilia mkazo nchi zinazo-walazimisha wakimbizi kurudi nchi zao za asili lakini ni ripoti chache sana husimulia mahojiano ya waliorudi nyumbani. Vyombo vya habari vilitoa ripoti nyingi kupindukia za safari za wahamiaji katika Marekani ya Kati na sera ya Marekani wakati wa utawala wa Donald Trump, lakini nilipozuru Guatemala na kukutana na baadhi ya waliorudishwa kwao, niligundua kwamba kwenye utafiti hakuna yeyote alikuwa amewahi kusimulia hadithi zao. Kuna baadhi yao ambao hawakuwa wamekulia Guatemala, lakini walilazimishwa kwenda Jiji la Guatemala na hawangetamka hata neno moja la Kihispania. Katika hali kama hii, kukusanya na kutoa habari za wahamiaji ni sawa na kujaribu kufanya marekebisho baada ya madhara makubwa kutokea.”

Will Vassilopoulos, mwanahabari Mgiriki wa AFP:

“Habari za uhamiaji na ukimbizi huhusishwa na dhiki na lazima zisi-muliwe. Lakini pia kuna zingine kuhusu masuala hayo za kutia moyo na ni muhimu pia. Habari hizo ni za ushujaa, hadhi, upendo na uvumilivu wa moyo wa binadamu katika hali mbaya na ya kutisha zaidi. Hizo ndizo habari hunivutia mimi kusoma.”



Chanzo : Binafsi

Asili: Angelos Tzortzinis.



ZOEZI LILILOPENDEKEZWA LA KUSHUGHULIKIA STADI ZA UTAMBUZI ZA KUFHAMU NA STADI ZA MITAZAMO YA KIBINAFSI NA MAADILI ZA KUPOKEA:

Anzisha mjadala na washiriki wako wakitumia mojawapo ya nukuu za Lydia Ouma Radoli, Ulriikka Myöhänen, Cécile Debarge au Will Vassilopoulos, zilizotajwa hapo awali. Wape fursa ya kutafakari ni habari zipi kuhusu uhamiaji na uhamishwaji wa lazima wangependa kuona, kusoma au kusikiliza na ni zipi hawangependa kamwe.

Hitimisha mjadala kwa mwauo wa matokeo ya hoja walizotoa hapo juu. Waweza pia kuongeza data kutoka nchi yako au bara.

Habari za kuvutia

Wanahabari wanaweza kufikiria na kuakisi hoja zinazofanya habari kuhusu wahamiaji na wakimbizi kuwa za kuvutia. Ifuatayo ni mifano ya hoja zilizotolewa na Modeli ya habari za kuvutia (SOI; tazama Kielelezo 33):

1. Ni habari zinazohusu ulimwengu na zina kundi kubwa lengwa.

Mfano: Wahamiaji kutoka Eritrea wanapaswa kulipa kodi ya mapato ya asilimi mbili iwapo wanahitaji huduma za wenye mamlaka Eritrea. Wakishindwa kutekeleza hilo, huenda waka-kumbwa na tatizo la kupata ajira katika nchi wanayonua kuhamia³ — hali ambayo ghafla inapatia sheria za Eritrea umuhimu katika vyombo vya habari vya Ujerumani, Italia na Sweden.

3 Kwa mfano, raia wa Eritrea katika ripoti ya Wüllner na wengine (2016) hakupata cheti chake cha diploma ya chuo kikuu. Vyeti vya kuthibitisha uzao wa mtu na vinginevyo ninavyoweza kutumiwa kuthibitisha uhitimu wa kazi havipo na hili linaweza kusababisha matatizo.

Kielelezo 33: Modeli ya Habari za Kuvutia



1. Habari zinazohusu ulimwengu na zina kundi kubwa lengwa.

2. Habari nyeti pakubwa.



3. Habari zilizo na vipengee vingi.

4. Habari ambazo bado hazijasimuliwa



5. Habari zinazosimuliwa kwa mtindo badili.

6. Habari zenye taathira kwa watu.



Asili: Mchoro wetu

2. Ni hadithi nyeti pakubwa.

Mfano: Hali ya misiba na maafa inayokumba wakimbizi katika vituo vya kuwazuilia nchini Libya inawavunja pakubwa hadhi zao kama binadamu kiasi kwamba inaamsha huruma miongoni mwa watu wa mataifa tofauti.

3. Ni habari zilizo na vipengee vingi.

Mfano: Masomo ya uhamiaji ambayo yana fani nyingi za elimu yanahusiana pia na tasnia ya wanahabari kuripoti kuhusu uhamiaji. Huenda matokeo ya utafiti kuhusu sababu za raia wa Cameroon kuhama kutoka nchi yao yakawa ni kupatikana kwa habari kuhusu ugomvi baina ya nchi zinazotumia Kiingereza na zinazotumia Kifaransa, kiwango cha uwezo wa kuzaa, uhaba wa nafasi za kazi, kuhimizwa na raia wa Cameroon waliotawanyika nje ya nchi hiyo, taswira ya umma ya nchi ambazo wengi hupenda kuhamia au athari za mabadiliko ya hali ya anga kwenye Ghuba la Guinea, miongoni mwa mada zingine.

4. Ni habari ambazo bado hazijasimuliwa.

Mfano: Badala ya kutafuta habari za kawaida zinazofanana, tafuta habari mpya au zinazoleta mwelekeop mpya. Ripoti "Upeo wa tatizo la wahamiaji waliopuuzwa zaidi ulimwenguni" iliyo-

chapishwa 2019 inatoa wazo kuhusu habari mpya na vipengee vipya katika ripoti hii kuhusu watu wanaohama kutoka DRC kwa sababu “kwa mwaka wote huo, vyombo vya habari vya kimataifa vilitilia mkazo tu matokeo yaliyocheleweshwa ya uchaguzi wa urais na mlipuko wa Ebola” (Skarstein, 2019).

5. Ni habari zinazosimuliwa kwa mtindo badili.

Mfano: Iwapo kila siku watu wanapata dazani za habari kutoka Mediterranean za misiba na meli kuzama na wanaonyeshwa kila mara picha za mamia ya wakimbizi wakiwa na wahaka wa maisha yao au hata wakifa, watashangazwa na mtazamo tofauti, kama ilivyofanyika walipoona picha Alan Shenu — anayeripotiwa mara nyingi kama “Aylan Kurdi”.

6. Ni habari zenye taathira kwa watu.

Mfano: Iwapo watu wanahitaji habari za kuwafaa, hilo linapaswa kutiliwa maanani katika kuripoti kuhusu uhamiaji na uhamishwaji wa kulazimishwa. Ni jambo liwezalo kusaidia kutoa vyanzo vya habari zaidi na hatua zifaazo kuchukuliwa, kwa mfano.

Bila shaka, ushirikiano na wanahabari wengine unaweza kusaidia kutimiza baadhi ya malengo ya kuwasilisha habari kwa njia itakayovutia hadhira (Egwu, 2020). Moduli 12 inatoa vidokezi vingi tofauti vya jinsi ya kushirikiana kuripoti kuhusu wahamiaji na wakimbizi.



ZOEZI LILILOPENDEKEZWA LA KUSHUGHULIKIA STADI ZA UTAMBUZI ZA KUTEKELEZA NA STADI ZA MITAZAMO YA KIBINAFSI NA MAADILI ZA KUPOKEA:

Kabla ya kuwasilisha modeli ya SOI, wape washiriki zoezi la kuchemsha bongo kwa kuwauliza kuhusu hoja mbali mbali zinazoweza kuleta mabadiliko mahususi katika masuala ya uhamiaji na kuwezesha kutolewa kwa habari ya kuvutia (mawazo yamo kwenye maandishi yaliyotangulia). Baada ya kuwasilisha modeli ya SOI, wape washiriki zoezi jingine la kuchemsha bongo kwa kuwauliza wafikirie kuhusu mawazo thabiti ya habari wanazoweza kutekeleza.

Hadithi za mfano za uhamaji na uhamishaji wa kulazimishwa: muhtasari wa mazoea mazuri

Hadithi zinapaswa kujitokeza kutoka kwa umati na kuvunja msingi mpya. Hadithi zinapaswa kushughulikia masilahi ya watu wa asili na vilevile katika nchi wanakokwenda. Wanapaswa kukata rufaa kwa wanachama

wa jumuiya za wageni na wenyeji. Hakika, mfano wa SOI unaweza kusaidia kubadilisha mwelekeo wa hadithi ili kuifanya kuvutia. Waandishi wa habari wanaweza kutengeneza hadithi kuhusu masuala ya wahamiaji na wakimbizi zaidi mashuhuri na kuyawasilisha kwa njia ya kipekee - wakati bado yanatimiza vigezo vya ubora, kama ilivyojadiliwa katika Moduli ya 10 na Moduli ya 11. Kesi zifuatazo za utendaji mzuri zinaweza kuwa msukumo kwa wanahabari kutafuta mitazamo mipya juu ya mada:

- Mtu hujisikiaje akiwa mkimbizi au mhamiaji, akizingwa na mchanganyiko na wahaka kuhusu maisha akiwa safarini ya meli? BBC Media Action (shirika la ufadhili la kimataifa la BBC) lilitunga filamu ya kuvutia (Your phone is now a refugee's phone), inayoweza kutazamwa kwa simu.
- Utunzi bunifu wa habari na ufumbuzi wa kitaalamu wa matatizo hutoa uwezekano wa nafasi mpya za kukumbana na wanayoyapitia wakimbizi. Watumiaji huona jumbe fupi za majonzi zikiwasili kwa simu na mitandao ya jamii, isipokuwa simu ambazo hazishiki vizuri ishara hitajika za mawasiliano na zinazokaribia kuisha moto ... Ni mbinu ya uwasilishi inayofanya habari hizo kuvutia zaidi hadhira kubwa. Kutokana na utafiti uliofanywa na BBC Media Action, filamu hiyo husambazwa pia kwa mitandao ya jamii kama Facebook. Mtindo sawa umetumiwa kwa video Jafor is calling..., Aisha is calling... na Nani is calling... Kila mojawapo ya hizo filamu, mhusika anaigiza upigaji simu na zinasimulia habari kutoka kambini kubwa ya wakimbizi ulimwenguni ya Cox's Bazar, Bangladesh (BBC Media Action, 2016).⁴
- Migration Trail Project hutumia ramani, data na vielekezo vya kusikia. Filamu ya mtandaoni ya mambo yasiyo ya kubuni ambayo Alison Killing alitayarisha kwa kujitosa ndani ya tukio analoliakisi, inampa mtazamaji nafasi ya kuwafuata katika muda halisi wahusika wawili waigizaji kwenye safari hatari ya siku 10 ya kwenda Ulaya. Shabaha yake ni kusimulia kwa kina na kwa njia ya kushangaza zaidi suala ambalo wengi hufikiria kuwa tayari wanalifahamu kikamilifu kupitia kwa ripoti za vyombo vya habari. Watazamaji watasoma jumbe za simu za wakimbizi, watawafuata kwenye ramani na kusikiliza matamshi yao na sauti zingine; dhana potovu zisiso na uasili zinayoyoma, na wahamiaji na wakimbizi hujitokeza wakiwa watu binafsi. Mbinu hiyo ya kuonyesha matukio halisi wakati yakitokea inawezesha hadhira kufahamu vyema takwimu na mambo ya kweli yatendekayo. Ingawa wahusika ni waigizaji, wanayotenda yanalingana na matukio ya kweli. Isitoshe, pana podkasti iliyo na simulizi la ukweli (Migration Trail, 2017).
- Video ya Time Magazine, Stories of Migrants Risking Everything for a Better Life ni mchanganyiko wa picha za wahamiaji na zinazoonyesha michoro ya wahamiaji na wakimbizi za nyumbani walikotoka na safari yao, maoni na simulizi la kina la usuli wa kisiasa na taswira kamili ya hali yao. Ni ripoti ya wanahabari kuhusu matukio katika nchi tofauti, na wahusika wake mbali mbali na masuala inayoakisi yanatoa vipengele vingi (Edwards, 2019). #FindA-

4 Kiungo cha habari na filamu: Hannides na wengine (2016). Kiungo cha filamu za Facebook: BBC Media Action (2019b), BBC Media Action (2019c), BBC Media Action (2019a).

zam imeangaziwa kimataifa katika majukwaa tofauti ya mitandao ya jamii. Mwanahabari John Sweeney anakutana kwa muda mfupi na mvulana mkimbizi “Azam katika Serbia mnamo Septemba wakati akitayarisha filamu isiyo ya kubuni ya kipindi cha yaliyomo cha BBC, Panorama, kuhusu safari ya wakimbizi katika Ulaya”. Filamu hiyo ilichochea kuanzishwa kwa kampeni ya mitandao ya jamii #FindAzam. Ndiposa mnamo 2015 Sweeney akaamua kumtafuta na “akafuata nyayo za safari ya ukimbizi aliyoichukua Azam” (Sweeney, 2015). Aliirekodi safari hiyo katika mitandao ya jamii akitumia Twitter, Facebook, YouTube and Snapchat na kuandika kuihusu kwenye blogu. Simulizi hilo lilitafsiriwa kwa Kiarabu na Kituruki. Shughuli ya kumtafuta Azam imebinafsisha safari ya wahamiaji na wakimbizi wengi na kurahisisha uelewa wa mada tatanishi iliyofikia hadhira pana ya kimataifa. (Sweeney, 2015).

- Filamu Refugee Bedtime Stories ilichagua tukio la kila siku maishani kuwa chanzo cha kuripoti kuhusu hali ya wakimbizi ambayo wengi wanaielewa vyema ya kusimulia watoto wakimbizi hadithi kitandani (Epp na wengine, 2018; Nastasa na wengine, 2016).
- Makala A Refugee’s Christmas Carol ilichapishwa na gazeti la The Telegraph la Uingereza. Kabla ya Krismasi ya 2015, mwanahabari alitembelea kituo cha wakimbizi jijini Roma na kuzungumza na watoto wawili kuhusu walivyozoea kusherehekea nyumbani, yale wangepanya siku hiyo na matumaini yao ya siku zijazo. Isitoshe, simulizi hizo mbili zimeonyeshwa kwa michoro isiyo ya rangi (Rowley, 2015).
- Ripoti ya tovuti The Smuggling Game kutoka kwa Thomson Reuters Foundation News inasimuliwa kwa picha tagusani. Video, kifaa cha kusikizia, picha na maandishi na nakshi hai zinachochea kwa njia tofauti na kumwezesha mtu kupata taswira kamili ya mada tatanishi kwa njia inayoeleweka kwa urahisi; habari za watu binafsi zinachanganywa na tarakimu na namba (Taylor & Cardi, 2017).
- CBC imetayarisha makala yenye anwani I Am A Refugee ambapo kwa maneno na lugha yao ‘Wacanada sita wapya’ wanasimulia habari zao. Hadhira inaweza kusoma taarifa za kuanjikwa, kutazama video katika lugha tofauti zenye tafsiri za Kiingereza za mazungumzo pamoja na picha na nakshi zenye namba na maandishi. Ni ripoti kutoka nchi tofauti iliyotayarishwa na wanahabari kutoka nchi mbali mbali (Haleem, n. d.).
- Huenda likawa pia ni jambo la manufaa kuhimizwa na kazi za mashirika husika yasiyo ya serikali. Amnesty International wameanzisha mradi “Upworthy”, kuunganisha wakimbizi na watu wa nchi mwenyeji wao za Ulaya. Hisia kubwa zinazoamshwa na habari hizo zinahimiza uelewa bora (Amnesty International Vlaanderen, 2018; Upworthy, 2016). Mradi wa kampeni wa Migrants as Messengers ulioanzishwa Afrika Magharibi na IOM hutumia teknolojia ya simu smati kusambaziana habari halisi za matukio ya uhamiaji waliyokumbana nayo, na kuzisambaza pia kupitia kwa majukwaa tofauti ya mitandao ya jamii kama vile Facebook. Wahamiaji wanasimulia waliyokumbana nayo na kuzungumzia kundi lengwa moja kwa moja (Migrants as Messengers, n. d.).



ZOEZI LILILOPENDEKEZWA LA KUSHUGHULIKIA STADI ZA UTAMBUZI ZA KUCHANGANUA NA STADI ZA MITAZAMO YA KIBINAFSI NA MAADILI ZA KUPOKEA:

Onyesha baadhi ya mifano ya utendaji kazi bora kisha muijadili na washiriki. Ni vipengele gani vya maudhui za habari nzuri na ya kuvutia ambavyo vinapatikana katika mifano hiyo?

Kuuza’ habari kuhusu uhamiaji na uhamishwaji wa kulazimishwa

Hata kama wanahabari wanafahamu hadhira zao na mbinu za mawasiliano na uwasilishaji wa mada za kuwafikia, ni muhimu pia kwao kuweza kushawishi wahariri wao wakuu kukubali habari zao zinazoifaa hadhira mahsusi.

Nukuu la ripota mzoefu wa masuala ya uhamiaji Anthony Akaeze linaonyesha kwamba ni muhimu kuwa na wazo komavu la habari badala ya kutapatapa ukijaribu kushawishi wahariri kuhusu habari unazonuia kuelezea za masuala ya wahamiaji na wakimbizi. Lakini pana ushauri wa kimsingi ambao huenda ukasaidia pakubwa katika kuuza habari kuhusu wakimbizi na wahamiaji. Wanahabari wanaweza kufuata mapendekezo yaliyotolewa kwa wanahabari huria, kama vile ushauri wa Kira Cochrane (2016) uliowalenga wasomaji wa The Guardian Opinion, Abigail Edge (2016), anayetoa muhtasari wa ushauri wa wanahabari wengine huria, na Mattia Peretti (2015), ambaye aliwataka wanahabari kadhaa kueleza kuhusu mbinu muafaka zaidi ya kuuza habari.⁵ Vidokezi hivi vinaweza pia kuwasaidia wanahabari waajiriwa kuimarisha uandalizi wa mawazo yao kuhusu makala zao kabla ya kushawishi wakuu wao kuyakubali: Waandishi huria wanapaswa kufikiria kuhusu mtazamo wa habari ambazo mashirika yao huangazia na kulenga jukwaa lifaalo. Hamna haja ya kuandaa makala ndefu iliyotafitiwa kikamilifu na kutayarisha ripoti yenye usuli kamili wa uhamiaji, kisha kuiwasilisha kwa jarida la makala za kubuni na burudani.

Inapendekezwa kwamba huenda likawa wazo nzuri kujaribu kushawishi wahariri kuhusu makala kamili ya uhamiaji kwa kuandika sentensi kadhaa kueleza wazo lako. Kadiria umuhimu wa ripoti yako. Wanahabari wanapaswa kuwa sahihi na dhahiri, wajibu maswali muhimu zaidi (kwa nini habari ni muhimu, kwa nini inafaa kwa wakati huo, unanuia kufuata kipengele kipi na unanuia kuwahoji nani?) na waeleze kwa nini ripoti yao inahitaji kutolewa hivi punde. Maarifa ya fani ya kuripoti kuhusu uhamiaji na uhamishwaji wa lazima ni muhimu na ni shughuli inayohitaji maandalizi makubwa ya takwimu, misingi muhimu ya kisheria, siasa na historia pamoja na utafiti wa wahusika (tazama Moduli 10) ili kuweza kuhimili uhakiki mkali wa mhariri. Mbali na maudhui, huenda ikawa muhimu ukiwa hakika na muundo utakaotumia. Kama ilivyotajwa awali katika

5 Huenda ikafaa kuangalia pia AJ Labs (2016) “How to pitch to Al Jazeera.com”.

moduli hii, sio kila muundo huvutia. Isitoshe, mbinu moja ya kuwashawishi wahariri huenda ikawa ni kusesitiza utaalumu wa pekee au uwezo maalumu katika uwanda wa kuripoti kuhusu wahamiaji, wakimbizi na jamii mwenyeji wao kuthibitisha uwezo wa mwanahabari kutayarisha ripoti husika. Mwanahabari asipopata jibu la pendekezo lake, asisite kumkumbusha mhariri na hata ampigie simu ama kuomba kukutana naye ana kwa ana.

Kukumbuka kuhusu umuhimu unaozidi kuongezeka wa mitandao ya jamii kama asilia msingi ya habari, wanahabari wanaweza kutenga nafasi maalumu ya kuuza mawazo na makala zao katika majukwaa hayo. Mitandao ya jamii huwapatia wanahabari fursa ya kuthibitisha utaalumu wao katika uwanda wa uhamiaji na uhamishwaji wa kulazimishwa.

Anthony Akaeze, mwanahabari Mnigeria

“Wanahabari wanahitaji uwezo wa kuwasilisha na kutetea mawazo ya habari zao kwa nguvu, wakianza na **kichwa cha habari** na kuonyesha ni kwa nini makala inayopendekezwa ni muhimu. Kwa kufanya hivyo, inakuwa ni rahisi kwa mhariri kushawishika.”



Chanzo : Binafsi



ZOEZI LILIOPENDEKEZWA LA KUSHUGHULIKIA STADI ZA UTAMBUZI ZA KUCHANGANUA NA STADI ZA MITAZAMO YA KIBINAFSI NA MAADILI ZA KUJIBU (A) NA STADI ZA UTAMBUZI ZA KUTEKELEZA NA STADI ZA MITAZAMO YA KIBINAFSI NA MAADILI ZA KUJIBU (B):

(A) Washirika wachague mfano mojawapo wa utendaji bora wa kazi kati ya iliyotolewa hapo awali, kisha wajitwike jukumu la waandishi wake. Wapewe fursa kubuni mkakati wa uvumishi. ‘Walitumia mbinu gani ‘kuwauzia’ wahariri simulizi zao? Simulizi hizo ziliihusuje hadhira?

(B) Washirika wachague mfano mojawapo wa utendaji bora wa kazi kati ya iliyotolewa hapo awali, kisha wajitwike jukumu la waandishi wake. Wapewe fursa kubuni mkakati wa uvumishi. ‘Walitumia mbinu gani ‘kuwauzia’ wahariri simulizi zao? Simulizi hizo ziliihusuje hadhira?



KAZI YA ZIADA ILIYOPENDEKEZWA YA KUSHUGHULIKIA STADI ZA UTAMBUZI ZA KUCHAMBUA NA STADI ZA MITAZAMO YA KIBINAFSI NA MAADILI ZA KUJIBU:

Andaa kipindi cha kuigiza mbinu za kuvumisha habari. Wape washiriki fursa ya kutunga barua pepe kwa mhariri wanayetaka 'kumwuzia' makala kuhusu uhamiaji na uhamishwaji wa kulazimishwa. Washiriki wanapaswa kueleza katika barua hiyo kwa nini habari wanayopendekeza ni ya kuvutia kwa hadhira mahsusi ya chombo hicho cha habari na/ama jukwaa la habari. Kadhalika, wanapaswa kuakisi katika barua hiyo hatua za kuimarisha taathira ya habari hizo kuhusu wahamiaji na wakimbizi.



